# MASWALI NA MAJIBU

## Sheria za Tanzania

FAyaz A. Bhojani
Gaudiosus Ishengoma

Toleo la 1



FB ATTORNEYS

fbattorneys.co.tz

# MASWALI NA MAJIBU

## Sheria za Tanzania

Toleo la 1

FAyaz A. Bhojani (Wakili)
BCom (McGill), LLB (London), LLM (Berkeley)

Gaudiosus Ishengoma (Wakili)
LLB (UDSM)

Toleo la 1 liliandaliwa na kuchapishwa katika lugha ya Kiingereza ('Q&A with FB Attorneys') mnamo mwaka 2017. Chapisho hili la Kiswahili linatokana na tafsiri ya Toleo hilo la Kiingereza iliyofanywa na Bw. Jaba Tumaini Shadrack (UDSM), na kuhaririwa na Dkt. Laurean Mussa (UDSM) akisaidiana na Bw. Rwekamwa Andrea Rweikiza (Wakili).

Dar es Salaam • Tanzania

Q&A with FB ATTORNEYS

Hairuhusiwi kunakili, kuhifadhi, kuchapisha kwa njia ya kielektroniki au mekaniki, kutoa vivuli (kudurufu), kurekodi au kubadili sehemu yeyote ya kitabu hiki kwa njia, namna au mfumo wowote bila idhini ya maandishi kutoka FB Attorneys. Maswali yoyote juu ya kitabu hiki yatumwe FB Attorneys kwenye barua pepe: info@fbattorneys.co.tz

**Angalizo:** Maelezo yaliyomo katika kitabu hiki yanalenga kutoa mtazamo wa jumla wa sheria. Sio mbadala wa mshauri wako wa masuala ya kisheria. Ikiwa una changamoto za kisheria, tunakusihi sana uwasiliane na mwanasheria wako. Tafadhali kumbuka na zingatia kuwa, sheria ambazo ndio msingi wa majibu na hoja zetu hapa zinaweza kuwa zimebadilika kitambo.

Toleo la 1
Kimechapishwa na Kusanifiwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
ISBN 978-9976-5241-0-9

FB

Kwa mke wangu Shemina, na binti zangu Alisa na Riana.
*FAyaz A. Bhojani*

Kwa familia yangu.
*Gaudiosus Ishengoma*

# Dibaji

Karibu kwenye toleo la kwanza la 'Maswali na Majibu na FB Attorneys'.

Safu ya Maswali & Majibu na FB Attorneys ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 2009 katika gazeti la Daily News, na kuifanya kuwa safu ya kwanza ya maswali na majibu ya kisheria katika ukanda wa Afrika Mashariki. Baada ya kuendesha safu hii kwa zaidi ya miaka minane, na kutambua kiu ya uelewa wa masuala ya kisheria katika jamii, waandishi waliamua kukusanya makala zote toka kuanza kwa safu husika na kuandaa kitabu hiki.

Kitabu hiki, ambacho kinajumuisha maswali na majibu kutoka mwaka 2009 hadi 2011 juu ya Sheria za Tanzania na Kimataifa, ni mwongozo muhimu kwa wasomaji wa kawaida, wanafunzi, walimu, wanasheria na umma kwa ujumla. Kitabu hiki kina sura sita zenye mada kama vile: mahusiano, wosia, migogoro ya ajira, haki za walaji/wateja, migogoro ya kibiashara, masuala ya mahakama na uhalifu.

Kitabu kina lengo la kuwafikia wasomaji kutoka katika kila nyanja ya maisha na kuelimisha umma juu ya sheria na madhara ya kuvunja sheria. Sheria inaweza kuchanganya, kukatisha tamaa na wakati mwingine inaweza hata isiwe upande wako, lakini utaratibu ni kwamba inapaswa kufuatwa. Kitabu hiki kitakuelimisha juu ya sheria, haki zako na mambo yote unayopaswa kufanya au kutokufanya.

Pamoja na kujibu maswali mazito juu ya sheria, kitabu hiki kina ucheshi ndani yake na hivyo kufanya safu/makala hizi zinazochapishwa kila wiki kuwa ni somo zuri la Jumatatu asubuhi huku ukiwa na kikombe cha kahawa pembeni.

Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Daily News, gazeti la Kiingereza linaloongoza nchini Tanzania, ambalo linachapisha safu ya Maswali & Majibu kila Jumatatu (www.dailynews.co.tz). Kumekuwa na ushirikiano bora kati ya Daily News na FB Attorneys.

Tunatumaini utafurahia kusoma kitabu hiki.

# FB Attorneys

FB Attorneys ni kampuni ya kisheria iliyopo jijini Dar es Salaam na yenye uzoefu limbikizi wa zaidi ya miaka kumi na saba katika ukanda wa Afrika Mashariki. Tunashughulikia masuala yote ya kisheria na tumebobea zaidi katika Mambo ya Mashirika na Biashara ikiwa ni pamoja na Madini, Mafuta na Gesi, Kodi, Kesi za Madai, Mabenki, Ushindani, Mali zisizohamishika, Sheria ya Hati Miliki, na Sheria ya Ardhi, miongoni mwa mambo mengine mengi.

Tunaheshimiwa sana kwenye ukanda wetu na kimataifa. Sifa yetu imejengwa na umahiri wetu katika kushughulikia kwa mafanikio changamoto ngumu za kibiashara ambazo zinahitaji mbinu na ufanisi wa hali ya juu. Hutegemewa mara nyingi na wateja kama chaguo namba moja miongoni mwa makampuni ya kisheria katika kesi za madai. FB Attorneys hutoa ushauri wa kisheria wa kipekee katika masuala mbalimbali ya makampuni na ya kibiashara.

FB Attorneys tuna mahusiano ya muda mrefu na baadhi ya taasisi mashuhuri za kifedha, mashirika ya Serikali, asasi za kiraia, na sekta nyingine maarufu za umma na binafsi katika ukanda wa Afrika Mashariki.

# Kuhusu Waandishi

## FAyaz A. Bhojani (Wakili)
BCom (McGill), LLB (London), LLM (Berkeley)

FAyaz Bhojani ana miaka kumi na saba ya ujuzi katika masuala ya kibiashara na ni mkuu wa Idara ya Sheria za Biashara. Yeye ni mhitimu wa Shule maarufu ya Sheria ya Berkeley, katika Chuo Kikuu cha California, inayoheshimika sana duniani. Baada ya kuwa mshauri katika baadhi ya benki zinazoongoza, na kampuni za madini, bima, mafuta na gesi, FAyaz hutumia uzoefu huo wa kibiashara katika shughuli zake za kisheria. Utaalamu wake unajumuisha maeneo muhimu kama vile Sheria ya Mashirika na Biashara hasa Sheria ya Madini, Mafuta na Gesi, Sheria ya Kodi, Mabenki na Uunganishaji na Ununuzi Mashirika. Katika Shahada ya kwanza, FAyaz alisomea Sayansi ya Takwimu-Bima chini ya Taasisi ya Wataalam wa Takwimu-Bima (Society of Actuaries - SOA), na hivyo kumjengea ujuzi thabiti wa hisabati.

## Gaudiosus Ishengoma (Wakili)
LLB (UDSM)

Baada ya kufanya kazi kama Mwanasheria wa Serikali kwa miaka minane, Ishengoma ana uzoefu mkubwa katika kusimamia kesi nyeti na ngumu. Katika kazi yake ya kisheria kwa muda wa miaka ishirini na miwili, amebobea katika Sheria ya Ardhi, Sheria ya Madini, na Sheria ya Mikataba. Amehusika katika kesi kubwa zilizofunguliwa Mahakama Kuu ya Tanzania (Kitengo cha Ardhi na Kitengo cha Biashara), na Mahakama ya Rufaa. Ishengoma amekuwa na rekodi nzuri katika ufuatiliaji wa madeni ya benki; alifundishwa mbinu za uendeshaji mashtaka na Baraza la Uingereza (British Council) chini ya timu ya wataalamu kutoka Bunge la Mabwanyenye (House of Lords).

# Yaliyomo

Familia, Mahusiano, Wosia na Mirathi ........ 1

Migogoro ya Kazi ........ 31

Haki za Mteja na Mdai ........ 43

Migogoro ya Biashara na Malalamiko ........ 83

Mambo Yahusuyo Wanasheria, Taratibu za Mahakama na Maadili ........ 135

Jinai/Uhalifu ........ 193

# Familia, Mahusiano, Wosia na Mirathi

**Kadiri unavyotumia muda mwingi ukiwa mbali na nyumbani huku ukifurahia kitendo hicho, ndivyo unavyoongeza uwezekano wa siku moja kuhitaji mwanasheria.**

... kwenye raha, umaskini, ugonjwa na afya, mpaka kifo kitakapotutenganisha ni sehemu ya ahadi tunayofanya kwa wapendwa wetu tunapooana. Tunaahidi kupendana na kuwa waaminifu, hatulazimishwi katika hili – tunachagua kufanya hivyo. Kuahidi ni rahisi! Kutunza ahadi ni jambo lingine. Sura hii inagusia maswali ya kuvutia juu ya mahusiano ya kifamilia na kutoa mifano mbalimbali ya kesi zilizokwisha tatuliwa katika kujibu maswali haya. Sura hii pia inajibu maswali juu ya wosia, mirathi na urithi. Kwa wengi wetu, kuandika wosia ni ukumbusho pekee wa uhakika tulionao maishani - kifo hakizuiliki, kwa nini usijitayarishe!

## Kutiwa Nguvuni kwa Kumtongoza Mwanamke

**Kwa muda mrefu jirani yangu amekuwa akinituhumu kuwa nina uhusiano wa kimapenzi na mke wake. Mnamo Januari 2010 kulikuwa na sherehe ya ubatizo katika nyumba ya jirani yetu mwingine ambako familia yangu na ile ya jirani yangu anayenituhumu tulialikwa. Jirani yangu alinikuta nimesimama nje ya nyumba pamoja na mkewe, alikasirika sana, akaondoka naye kwenda nyumbani baada ya kunifokea mbele ya watu. Muda mfupi baada ya kuondoka, polisi walifika na kunikamata. Kwenye kituo cha polisi nilihojiwa juu ya tukio hilo na kuachiwa kesho yake. Siyo kweli kuwa nina uhusiano wa kimapenzi na mke wa jirani yangu. Je, ninaweza kukamatwa?**

*18 Aprili 2011*

Nguli wa filamu James Bond angekuwa katika shida kubwa ikiwa kumtongoza mke wa mtu ni kosa la jinai. Lakini siyo, na hivyo huwezi kukamatwa kwa hili. Kwa jibu hili, hatulengi kutoa ushauri wa mahusiano - kuna magazeti mengine mengi yenye safu za namna hiyo – tunatoa ushauri katika mtazamo wa kisheria. Ni vibaya kimaadili kumshawishi mke wa mtu - ni kosa, ambalo ni kosa la madai, si jinai. Polisi hawana haki ya kumkamata mtu ambaye anatuhumiwa kwa vitendo hivyo. Kwa upande wako, unaweza kuwashtaki polisi waliokukamata na jirani yako na kudai fidia kwa kukuweka kizuizini kimakosa. Kwa upande mwingine, kwa kuwa ushawishi huo ni kosa la madai, mumewe anaweza kukushtaki na kudai fidia ikiwa anaweza kuwa na ushahidi.

## Mahusiano ya Ngono na Mwanafunzi

**Mimi ni mfanyabiashara na nimekuwa na mahusiano ya kingono na mwanafunzi wa shule fulani ya sekondari. Desemba iliyopita, baba yake aligundua uhusiano wetu na msichana huyo alikiri kuwa tuna mahusiano ya miaka miwili na kwamba ananipenda. Cha kushangaza, nilikamatwa na polisi na nimeshtakiwa kwa kosa la ubakaji. Sijawahi kumbaka binti huyo - na msichana amekiri kuwa tumekuwa tukifanya ngono kwa ridhaa yake. Ninahisi kuwa polisi na Hakimu watakuwa wamehongwa. Nifanye nini?**

*28 Machi 2011*

Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wa kike wanaoacha shule kutokana na ujauzito na tabia ya watu wazima kuwarubuni wasichana wadogo, sheria iko wazi kwamba hairuhusiwi kuwa na mahusiano ya kingono na msichana aliye katika shule ya msingi au ya sekondari, au msichana yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18. Mtu yeyote anayejamiiana na mtoto chini ya miaka 18 atakuwa na hatia ya ubakaji bila kujali ridhaa ya mtoto husika. Msingi wa sheria hii ni kuwa msichana wa umri huo ana upeo mdogo na hivyo hawezi kuridhia mahusiano ya kingono. Kwa hiyo, tunakubaliana na msimamo wa polisi na Hakimu. Kama utakutwa na hatia, jiandae kutumikia kifungo cha miaka thelathini jela.

## Mali yenye Thamani Kubwa, haijakatiwa Bima

**Baba yangu ana mtazamo hasi kuhusu makampuni ya bima. Amekuwa akiamini kuwa ni wahalifu wakubwa duniani. Kwa sababu ya imani yake hii, mali yote anayomiliki iko hatarini. Sisi ni familia ya watoto wanane, wavulana watano na wasichana watatu. Baba yangu ameandaa wosia na kunitaja kama mrithi wa baadaye wa mali hii yenye thamani kubwa. Mali hiyo kwa sasa imekodishwa kwa kampuni inayojihusisha na uchanganyaji na usambazaji kemikali. Mpangaji huyo anahatarisha mali hii - lakini baba hataki kuiwekea bima mali husika. Kwa kuwa**

**mimi hatimaye nitakuwa mmiliki wake, je ninaweza kuiwekea bima mali hii ili kulinda maslahi yangu?**

*21 Machi 2011*

Lazima ukumbuke kuwa hii bado siyo mali yako. Una matarajio tu ya kuirithi. Jambo hilo linaweza kuwa kweli lakini huna uhakika kamili, wosia hubadilika na unaweza kufa kabla ya baba yako. Kwa bahati mbaya, kwa kuwa si mmiliki wa hii mali huwezi kudai kuwa na maslahi au kustahili kuiwekea bima, na hivyo huwezi kuikatia bima kwa jina lako. Hata kama kungekuwa na bima ya namna hiyo, ingekuwa ni vigumu kuweka mipaka juu ya nani anayeweza kukata bima - kwa mfano, mke wako na watoto wanaweza pia kuanza kuiwekea bima, wakitarajia kuwa watarithi mali hiyo baada ya kifo chako.

## Kugawanya Haki na kuongeza Majukumu

**Nilikuwa mwanamume mwenye furaha sana kabla ya ndoa hadi nilipolazimishwa kuoa miaka mitano iliyopita. Baada ya kuwa na mke, haki zangu zimegawanywa na majukumu yameongezeka mara dufu. Hakuna amani nyumbani. Mke wangu analalamika juu yangu muda wote kila anaponiona. Nimekosa njia sahihi ya kuifanya familia yangu kuwa na furaha. Nifanyeje?**

*14 Machi 2011*

Kuna mambo mengi katika swali lako ambayo ni nje ya upeo wetu wa ushauri. Hakuna muujiza tunaoweza kufikiria ili kumridhisha mkeo. Matatizo kati ya mume na mke yamekuwepo tangu wakati wa Adamu na Hawa, na yataendelea kuwepo. Ikiwa umepoteza tumaini katika ndoa, una machaguo mawili; kutengana na kuruhusu muda wa upatanisho, au kuomba talaka. Maisha yanaendelea hata baada ya talaka, hivyo unapaswa kufikiria hilo pia. Hata hivyo, unaweza kumshirikisha mshauri wa ndoa kabla ya kuchukua hatua zaidi.

## Simpendi tena

**Nilichumbiwa na mtu niliyempenda. Miezi michache baada ya kuchumbiwa nilibadilisha mawazo yangu na sitaki kuendelea na mchakato wa harusi. Je, ninaweza kufanya hivyo? Marafiki zangu wananiambia kuwa siwezi kufanya hivyo, kwa kuwa kisheria ninapaswa kuolewa na mwanamume huyu. Nifanyeje?**

*21 Februari 2011*

Tuanze kwa kusema kuwa, wewe au marafiki zako mnaonekana kufikiri kuwa umeshaolewa. Bado hujaolewa. Maana ya uchumba katika sheria ni ahadi ya kuoana, ambayo kwa kawaida huwa kwa njia ya pete ya uchumba. Sheria haikulazimishi kuolewa na uchumba unaweza kuvunjwa, kinyume na kile marafiki zako wanakuambia. Ingependeza sana kujua hao unaowaita marafiki zako wana mtazamo gani kuhusu talaka. Kwa vile wana mtazamo mkali juu ya kuvunja uchumba, ni rahisi kuwashauri wengine kwamba talaka ni batili!

Baada ya kusema haya, ikiwa una nia ya kusitisha uchumba na hatimaye ndoa, unaweza kushtakiwa kwa hasara yoyote ambayo upande mwingine umepata wakati wa maandalizi ya ndoa. Pia, upande ulioathirika na kitendo hicho unaweza kushtaki na kudai kurudishiwa zawadi zilizotolewa kwa matumaini kuwa ndoa ingefungwa.

## Kulazimishwa na Mume

**Mume wangu ni mtu mwenye kuniendesha na mwenye jeuri. Anatuongoza kwa mkono wa chuma, kosa dogo tu linaweza kusababisha mtu yeyote kuadhibiwa vikali, ikiwa ni pamoja na mimi. Sina elimu rasmi na ninamtegemea mume wangu kwa kila kitu, na hivyo siwezi kufikiria**

**kuomba talaka. Katika tukio la hivi karibuni, msichana wetu wa kazi aliacha nyama kwenye jiko na kuisahau. Nyama iliungua, jiko likaharibika na kuwa katika hali mbaya. Mume wangu alipofika nyumbani na kugundua kilichotokea, alikasirika sana. Aliniamuru nimpige msichana wa kazi. Nilikataa na alianza kunipiga na kuniambia ataacha kunipiga ikiwa tu nitampiga msichana wa kazi. Nilimpiga msichana huyo kwa ufagio kichwani mara kadhaa na sasa nimeshtakiwa kwa shambulio kubwa la kudhuru mwili. Baada ya kukamatwa, mume wangu aliamua kunitelekeza na niliwekewa dhamana na jirani yangu. Nifanyeje?**

*7 Februari 2011*

Ukatili huo siyo wa kawaida, na sheria itakulinda. Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, kuna kifungu kinachosema kwamba ikiwa mwanamke atafanya kosa (isipokuwa mauaji au uasi) mbele ya, na kulazimishwa na mumewe, utetezi wa wazi ni kuthibitisha pasi na shaka kwamba alitenda kosa hilo kwa kulazimishwa na mumewe. Unapaswa kuelekeza utetezi wako katika mwelekeo huo. Kama yote uliyotuambia ni kweli na inaweza kuthibitishwa hivyo mahakamani, unaweza kuachiwa huru.

Hata hivyo, tunapaswa kukuonya kwamba shambulio kubwa la kudhuru mwili ni kosa kubwa sana ukilinganisha na shambulio la kawaida. Shambulio kubwa la kudhuru mwili inamaanisha madhara makubwa kwenye mwili. Kwa upande wako, inategemea na ukubwa na uzito wa ufagio uliotumia, ni sehemu gani ya mwili uliyompiga, silaha husika ilikuwa na ncha kiasi gani, na kwa nini uliamua kumpiga msichana wa kazi kichwani na si sehemu nyingine za mwili. Shambulio kubwa la kudhuru mwili uhusisha pia kuumizwa kisaikolojia lakini haijumuishi hisia kama vile huzuni au hofu.

## Makubaliano kabla ya Ndoa nchini Tanzania

**Mimi ni raia wa Afrika Kusini na nimeishi Tanzania kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita. Kwa miaka mingi nimekuwa katika mahusiano na msichana mrembo wa kitanzania, ambaye ninamuamini sana. Hivi karibuni baadhi ya wanasheria kutoka ng'ambo walitembelea ofisi zetu nchini Tanzania, na baada ya kuwaambia kuhusu mipango yangu ya ndoa, walinishauri tuandikishane mkataba kuhusu mali kabla ya ndoa kwa tahadhari ya talaka. Je, hii inawezekana chini ya sheria za Tanzania na mikataba ya namna hiyo inaweza kuwa na nguvu za kisheria? Nini ninapaswa kuzingatia katika mkataba huo? Nini maana ya mkataba baada ya kufunga ndoa?**

*31 Januari 2011*

Makubaliano kabla ya ndoa, pia huitwa mkataba unaotangulia mkataba wa ndoa ni mkataba ulioingiwa na pande mbili kabla ya ndoa. Maudhui ya mikataba hiyo hutofautiana sana, lakini kwa kawaida inajumuisha masharti ya mgawanyo wa mali na kumtunza mwenza baada ya talaka au kuvunjika ndoa. Mkataba huo unaweza pia kujumuisha masuala ya unyang'anywaji mali kutokana na talaka iliyosababishwa na uzinzi.

Masharti mengine kuhusu malezi ya watoto yanaweza kuingizwa pia. Pindi watu mwenye mali nyingi wanapoingia katika makubaliano haya, moja ya masharti muhimu zaidi ni kuhusu mali iliyopatikana kabla ya ndoa kubakia kwenye miliki ya mwanandoa aliyeitafuta kama wataamua kupeana talaka. Hii inahakikisha 'usalama wa mali' kwa upande ambao vinginevyo ungeishia kulipa fidia ya mabilioni ya pesa juu ya mali wakati wa kupeana talaka.

Katika nchi nyingine, hususani za Ulaya, watu hupendelea mikataba hii, kwa vile ni mtihani tosha wa upendo - njia pekee ya

kujua kwamba mtu anapendwa kweli, na sio kupendwa tu kwa sababu ya utajiri alionao. Hata hivyo, mikataba hii imekumbana na upinzani mkali; viongozi wengi wa dini wanaona kuwa inahatarisha taasisi ya ndoa kwa sababu haifuati kanuni ya 'mpaka kifo kitutenganishe'. Kwa Tanzania, sheria ya ndoa iko kimya juu ya suala hili. Mahakama pia haijawahi kusikiliza kesi ya namna hii. Kwa hiyo, jibu letu linajikita katika ujuzi binafsi kuhusu suala hili, pamoja na mfumo wa kisheria kwa ujumla nchini Tanzania.

Uhalali wa makubaliano ya namna hii nchini Tanzania hutegemea kwa kiasi kikubwa, maneno yaliyotumika katika mkataba ulioingiwa kabla ya ndoa. Ikiwa mkataba utadhoofisha maadili au ni kinyume na sera za nchi, makubaliano hayo yatakosa nguvu ya kisheria. Swali linalofuatia ni mambo gani tunaweza kusema yanakiuka maadili au sera za nchi. Hii inategemea mtazamo binafsi, historia ya wahusika, dini, na utamaduni wao katika kutolea maamuzi.

Sheria inaangalia ndoa kama pingu za maisha. Yawezekana dhana hii ilikuwa chachu wakati sheria ilipoanza kutumika mwanzoni mwa miaka ya 1970, lakini kupungua uvumilivu kati ya wanandoa, kuongezeka kwa uwazi na ufahamu wa sheria kumechangia ongezeko la talaka. Hii si Tanzania tu, bali duniani kote. Ikiwa mahakama itaangalia sera za nchi kwa mtazamo mpana zaidi, na kuzingatia nyakati husika (hatuna uhakika kama wataweza), hatuoni kwa nini makubaliano ya namna hii yasiwe na nguvu kisheria. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa hapo awali, Mahakama haijawahi kupokea kesi ya namna hii, na hivyo hatuwezi kukupa jibu la moja kwa moja.

Hata hivyo, hakuna madhara yatokanayo na aina hii ya makubaliano, na tunapendekeza sana ufanye hivyo. Si tu kwamba itaokoa muda mwingi, pesa na nguvu kwa wanaoshtakiana lakini pia itapunguza mzigo kwa mahakama.

Ikiwa mkataba huo hautakubalika mahakamani, unaweza kusaidia kuonesha madhumuni ya pande zote. Kifungu cha mkataba kinachoondoa kipengele kilichokataliwa na mahakama kuwa sehemu ya mkataba kinapaswa kuingizwa ili masharti au vifungu vingine vya mkataba viendelee kuwa na nguvu ya kishera.

Jibu la sehemu ya mwisho ya swali ni kuwa makubaliano baada ya ndoa yanafanana na makubaliano kabla ya ndoa, isipokuwa haya yanafanyika baada ya wanandoa kuoana. Mara nyingi ni vigumu sana kuafikiana baada ya ndoa kufungwa, hivyo hatukushauri kusubiria ndoa ili kuingia mkataba wa namna hii.

## Amri ya Matunzo dhidi ya Baba

**Nimekuwa katika uhusiano na mwanamume kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita na nimejifungua mtoto wa kiume. Kama ilivyo kawaida ya wanaume, amenitelekeza na nimebaki namtunza mtoto peke yangu. Nashindwa kujitimizia mahitaji. Je, baba (mzazi mwenzangu au baba mtoto) anapaswa kuchangia matunzo ya mtoto? Je haki zangu ni zipi?**

*17 Januari 2011*

Chini ya Sheria ya Watoto ya mwaka 2009, maombi ya amri ya matunzo yanaweza kufanywa mahakamani na mama mtarajiwa dhidi ya baba wa mtoto, wakati wowote kabla mtoto hajazaliwa; wakati wowote ndani ya miezi ishirini na nne tangu kuzaliwa kwa mtoto; wakati wowote baada ya kuzaliwa kwa mtoto na kuwepo ushahidi kuwa mtu anayedaiwa kuwa baba wa mtoto ndani ya miezi ishirini na nne baada ya kuzaliwa kwa mtoto amelipa fedha kwa ajili ya matunzo yake; au wakati wowote ndani ya miezi ishirini na nne baada ya kurudi Tanzania Bara mtu huyo anayedaiwa kuwa baba wa mtoto, kwa kuthibitisha kwamba aliacha kuishi Tanzania kabla au baada ya kuzaliwa kwa mtoto.

Sheria hiyo inaitaka mahakama kukataa kutoa amri ya matunzo mpaka iwe imeridhika kuwa kuna sababu nzuri ya kuamini kwamba mtu huyo anayedaiwa kuwa baba wa mtoto ni kweli ni baba halisi na kwamba maombi ya matunzo yamefanywa kwa nia njema na si kwa lengo la kutisha na ulaghai; na mtu huyo anayedaiwa kuwa baba wa mtoto ameombwa na mlalamikaji au na mtu mwingine kwa niaba ya mlalamikaji, atoe matunzo ya mtoto na amekataa au ameghaili kutoa matunzo, au ametoa matunzo yasiyokidhi.

Kwa maelezo hapo juu, una kesi nzuri na endelea na maombi husika.

## Ndoa ya Watu wa Jinsia Moja

**Je, sheria nchini Tanzania inaruhusu ndoa ya watu wa jinsia moja, na kama ndivyo, wapenzi hawa wanaweza kuasili mtoto? Nimeambiwa kuwa sheria za ndoa zimebadilishwa na mahusiano hayo sasa yanatambulika. Ikiwa ndivyo, ni kwa utaratibu gani? Vipi kuhusu ndoa za mkataba/muda mfupi? Je mwanamume anaweza kuwa na mke zaidi ya mmoja nchini Tanzania?**

*3 Januari 2011*

Sheria ya Ndoa haijafanyiwa marekebisho, na ndoa za jinsia moja, kama ilivyo katika nchi nyingine nyingi, ni batili. Sheria nchini Tanzania imeelezea ndoa kama muungano wa hiari kati ya mwanamume na mwanamke wanaotaka kuishi kwa pamoja maisha yao yote. Kwa ufafanuzi huu, ndoa za mkataba/muda mfupi, au vyovyote unavyomaanisha haziruhusiwi.

Ndoa ya mke mmoja ni muungano kati ya mwanamume mmoja na mwanamke mmoja tu.

Ndoa ya mitala ni muungano ambao mume anaweza kuoa mwanamke au wanawake wengine.

Kwa mujibu wa sheria, kuna aina mbili za ndoa: zile ambazo ni za mke mmoja au inatarajiwa kuwa ya mke mmoja, na zile ambazo ni mitala au zinatarajiwa kuwa za mitala. Kwa mujibu wa sheria, ndoa zilizofungwa katika mfumo wa Kiislam au kwa mujibu wa sheria za kimila Tanzania Bara (Tanganyika), labda kama kutakuwa na ushahidi tofauti, zinatambulika kuwa ni mitala au zinatarajia kuwa za mitala. Katika hali nyingine yoyote, ndoa ni mume na mke mmoja, isipokuwa tu kama kutakuwa na ushahidi tofauti. Kwa hivyo tunajibu sehemu ya mwisho ya swali lako kwa kukubali kuwa, nchini Tanzania mwanamume anaweza kuwa na mke zaidi ya mmoja.

## Wosia wangu Umehifadhiwa Nje ya Nchi

**Niliandaa wosia nchini Tanzania miaka mitatu iliyopita na kuutunza benki huko London kwa ajili ya usalama wake. Karibia natimiza miaka 80 na sitarajii kuishi muda mrefu sana. Ningependa kubadili wosia wangu na kuiandikia barua benki yangu huko London. Lakini benki inataka niwepo mwenyewe kupokea bahasha yenye nakala ya wosia. Nimedhoofika sana na siwezi kusafiri umbali huo tena. Benki inaonekana kabisa haitaki kunielewa juu ya hili. Nifanye nini, kwani nina shauku kubwa ya kubadilisha wosia wangu? Nini kitatokea ikiwa kuna wosia mbili?**

*13 Desemba 2010*

Kabla ya kujibu swali lako tunashangaa ni kwa nini benki nchini Uingereza haitaki kutoa wosia. Labda hawajui kwamba bahasha hiyo ina wosia. Tunastaajabu nini kingetokea kwa bahasha hiyo ikiwa ungekuwa umefariki. Kama benki ingefanya hivyo ikiwa ungekuwa umefariki, ingekuwa haina maana kwako kuandika wosia, kwa kuwa hakuna mtu angeweza kuupata. Tunashauri kuweka wosia katika sehemu maalum ya kuhifadhia wosia

na kumjulisha msimamizi wa mirathi.

Swali lako ni rahisi sana - ili uandike wosia mpya, huhitaji kuwa na wosia wa zamani. Wosia mpya hufuta wosia wa zamani mara moja. Kwa hiyo, labda kama kuna maelezo mengine ambayo hujaweka wazi, hakuna haja ya kuomba benki ikutumie wosia wa sasa. Endelea kuandaa wosia mpya, na uhakikishe kuwa utautunza mahali ambapo msimamizi wa mirathi anaweza kuupata.

Ikitokea kuwa kuna wosia mbili tofauti na zote ni halali, wosia wa mwisho kuandaliwa huwa na nguvu zaidi ya kisheria, kwani kuna dhana kwamba wosia mpya hufuta wa awali.

## Kulazimisha Wanandoa kukaa pamoja

**Niliolewa mwaka 1990 na ndoa yetu imebarikiwa kupata watoto watatu. Katika miezi kadhaa iliyopita mke wangu na mimi tumekuwa na migogoro ya mara kwa mara katika ndoa yetu, mke wangu hakubaliani na baadhi ya tabia zangu. Kwa sasa amerudi kwa wazazi wake, na anakataa kurudi kwenye nyumba yetu ya ndoa. Je, mahakama inaweza kunisaidia kwa kutoa amri ya kumwamuru kurudi?**

*6 Desemba 2010*

Ndoa ni muungano wa hiari kati ya mwanamume na mwanamke iliyoridhiwa na pande zote mbili. Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inaweka wazi kuwa hakuna mashtaka ambayo yanaweza kufunguliwa mahakamani kulazimisha mke kuishi na mumewe au mume kuishi na mkewe. Kwa hiyo, mahakama haiwezi kuwalazimisha kuishi pamoja. Msaada pekee kwako ni kupeleka suala hilo kwenye Bodi ya Upatanishi wa Ndoa. Vinginevyo, ili kuokoa ndoa yako, unapaswa kwa vyovyote vile kubadili tabia zako.

## Mama amefariki, Baba ametajirika

**Mama yangu ambaye amefariki dunia hivi karibuni alikuwa mfanyabiashara tajiri na maarufu huko Mwanza. Baba yangu, ambaye hakuwa na uhusiano mzuri sana naye, ametoa wosia ambao ni ajabu kabisa kwamba amemrithisha mali zaidi ya tulivyotarajia - sasa baba ni tajiri. Je, tunaweza kufanya nini kuupinga wosia huo? Mwishoni mwa wosia, mama yangu amesaini kama mtoa wosia kiume. Je! Hilo siyo kosa la msingi?**

*15 Novemba 2010*

Hukutaja kama kuna wosia mwingine ambao mama aliandika; swali lako limejikita katika fununu tu. Ili kuthibitisha kama wosia huo ni wa kweli, ni vizuri kuwauliza mashahidi walio saini wosia husika. Unaweza pia kupata ushauri kutoka kwa mtaalamu wa maandishi ili kuthibitisha kama sahihi iliyoko kwenye wosia inaendana na sahihi ya mama yako. Maelezo yako kuwa mama yako alisaini kama mtoa wosia kwa nafsi ya kiume na si ya kike yanavutia. Hata hivyo, katika Kiingereza cha kisasa, neno mtoa wosia linaweza kutumiwa na jinsia zote mbili bila tatizo, ni kama maneno mwigizaji, mzee wa baraza, mwendesha mashtaka na msimamizi wa mirathi. Hatujashawishika kwamba mahakama inaweza kupotoka na hivyo kubatilisha wosia husika kwa misingi kuwa mwanamke amesaini wosia wake kama mwanamume, hasa katika zama hizi ambazo sheria imeweka wazi kuwa maneno yanayomaanisha jinsia ya kiume yanajumuisha pia jinsia ya kike na kinyume chake. Unaweza kuhitaji ushauri wa kisheria na tunapendekeza umuone mwanasheria wako.

## Nani anaweza kushuhudia Wosia wangu?

**Nimeandaa wosia na nitahitaji shahidi kuusaini. Nani anaweza kuwa shahidi? Je, ni lazima awe Hakimu au mwanasheria au anaweza kuwa mtu yoyote? Nisingependa wosia wangu upingwe mahakamani.**

*1 Novemba 2010*

Kwanza kabisa, unahitaji mashahidi wawili kushuhudia wosia wako na siyo mmoja. Si lazima shahidi awe Hakimu au mwanasheria. Kiujumla inashauriwa kuwa wosia ushuhudiwe na watu unaowajua na waaminifu, na ikiwa wataitwa, waweze kushuhudia kwamba wosia ulitiwa saini na wewe mbele yao.

Mwenzi/mwanandoa, mnufaika (wasii), mwenzi wa mnufaika, kipofu, mtoto na mtu asiye na akili timamu hawawezi kushuhudia wosia. Mashahidi wanapaswa kuwa na uelewa juu ya wanachofanya na athari zake.

Lazima uzingatie kwamba mashahidi wote lazima wawe katika sehemu moja, kwa wakati mmoja na pamoja nawe wanapokuwa wanasaini. Ikiwa, mmoja wa mashahidi wako atafariki kabla yako, tunapendekeza kuwa uandae wosia mwingine mara moja na kupata shahidi mwingine. Sheria inahitaji uthibitisho wa mashahidi wakati wa kufungua mirathi na shahidi aliyekufa anawezakusababisha usumbufu na kucheleweshamchakato mzima wa mirathi.

## Kudai Urithi kutoka kwa Baba yangu

**Baba yangu ni mtu tajiri sana – ni miongoni wa watu tajiri zaidi nchini. Ananihudumia vizuri sana na ninapata fedha ya matumizi, gari na kazi. Hata hivyo, baba yangu hataki kunipa mtaji ili nifungue biashara ambayo ninaweza kusimamia mwenyewe. Anadai kuwa akifariki nitapata 50% ya utajiri wake. Ninakaribia miaka 30 na ningependa kupewa urithi na baba yangu na kuanza kujitegemea. Ninaogopa kwamba anaweza kubadilisha mawazo yake na wosia kwani kuna uvumi kuwa ana kimada na amezaa naye watoto. Ningependa kumuuliza juu ya uhusiano huo wa nje ya ndoa. Tafadhali naomba ushauri.**

*4 Oktoba 2010*

Tunadhani unataka kushauriwa kama unaweza kudai urithi wako kwenye wosia na si juu ya wewe kumuuliza baba kuhusu kimada wake. Kwa bahati mbaya, kuhusu swali la pili, hatuwezi kukujibu.

Kwa kuanzia, wewe ni mtu mzima na siyo mtoto mdogo. Hakuna nchi yoyote duniani yenye sheria ambayo inaruhusu mnufaika wa wosia kudai sehemu ya mali kabla ya kufariki kwa mwandaa wosia. Wosia huwa na nguvu za kisheria baada ya kifo cha mwandaa wosia. Kwa bahati nzuri (au mbaya), baba yako bado yu hai hivyo huwezi kudai urithi chini ya wosia. Haina tofauti kabisa kama baba yako ni mtu tajiri zaidi nchini Tanzania au hata akiwa tajiri zaidi katika Afrika - kiasi cha utajiri wake hakibadili sheria.

Pia fahamu kuwa wosia si jiwe, hubadilika. Mwandaaji wa wosia anaweza kuubadilisha wakati wowote kabla ya kufariki. Kumsumbua baba yako kwa njia yoyote ile kunaweza kumfanya abadili mawazo yake juu yako – ni vyema kukumbuka hili wakati unafikiria mpango wa kumuuliza kuhusu kimada wake.

## Kumpa Talaka Mke aliyerukwa na Akili

**Miaka mitano iliyopita nilifunga ndoa ya Kikristo na msichana mmoja hivi. Ndoa yetu imebarikiwa kupata mtoto wa kiume anayekaribia kufikisha miaka mitatu. Mnamo Januari 2008, mke wangu aliugua malaria na kupimwa na kutibiwa na dawa isiyofaa. Kisha akapoteza fahamu na alikaa hospitali kwa miezi mitatu kabla ya kuruhusiwa. Toka aruhusiwe amekumbwa na changamoto ya kiakili na hawezi kula, kuoga au kutembea mwenyewe. Nimejitahidi sana kumvumilia, lakini nimeshindwa. Natamani kumtunza maisha yake yote, lakini ningependa kumpa talaka. Je, hii inaweza kuwa sababu tosha ya kumpa talaka? Ni sababu zipi nzuri za kutoa talaka naweza kuja nazo na hivyo kufanikiwa? Tafadhali zingatia kuwa ndugu wawili wa mke wangu ni wanasheria.**

*27 Septemba 2010*

Tunaingiwa na huruma kusikia masahibu ya mkeo. Tunapenda kukukumbusha viapo mlivyopeana mlipofunga ndoa na kufanya harusi na kuahidi kuishi na mkeo katika hali yoyote ile, iwe ni wakati wa furaha au huzuni, ugonjwa au afya njema. Vivyo hivyo katika sheria, ugonjwa sio msingi wa talaka, kutengana au kubatilishwa kwa ndoa. Ingekuwa tofauti ikiwa mkeo alikuwa na tatizo hili kabla ya kufunga ndoa na ukawa umefichwa ukweli huo. Kama ingelikuwa hivyo, ndoa yako ingeweza kuzuilika na tungekushauri kwenda mahakamani ili ifutwe.

Kwa kuwa umefichua ukweli, sisi kama maafisa wa mahakama ni wajibu wetu kutoipotosha mahakama yoyote na hivyo hakuna haja ya kujadili sababu nyingine ambazo unataka kutengeneza. Kama ulivyotujulisha ndugu wawili wa mkeo ni wanasheria – hii ni taarifa muhimu kwani ni wazi kuwa watamwongoza vizuri juu ya suala hili na unapaswa uelewe hivyo.

## Kupewa Barua ya kusimamia Mirathi kwa uharaka

**Baba yangu alikufa wiki chache zilizopita bila kuacha wosia. Kwa kuwa mimi ni mzaliwa wa kwanza na mama yetu alifariki kabla ya baba, nilikubaliana na wadogo zangu kuwa niombe barua za usimamizi wa mirathi ya mali zake. Kabla ya barua ya usimamizi kutolewa, mwanamke mmoja alijitokeza hadharani, na kupinga maombi yangu, akidai kuwa ni mjane wa marehemu baba yangu. Sijawahi kumwona mwanamke huyu katika maisha yangu na jambo hili sasa liko mbele ya mahakama. Kwa kutokuwepo kwake, tumegundua kuwa mali kadhaa za baba yetu zinatumiwa vibaya. Mali nyingine, ikiwa ni pamoja na gari lake, liko chini ya umiliki wa dereva wake ambaye hana nia njema. Washirika wa baba wa kibiashara pia wananipa wasiwasi kwani hawataki kuweka wazi baadhi ya taarifa za kibiashara. Kesi mahakamani itachukua muda mrefu. Tunaweza kufanya nini katika hatua hii ili kukomesha wizi huu?**

*27 Septemba 2010*

Hautapewa barua ya usimamizi wa mirathi uliyoomba mpaka maombi yaliyofanywa na anayedai kuwa ni mjane wa marehemu baba yako yapatiwe ufumbuzi na mahakama. Umeeleza kwa usahihi kabisa kuwa hii inaweza kuchukua muda mrefu, na kwa kuwa muda ni mali, unahitaji kukomesha wizi huu na matumizi mabaya ya mali ya marehemu.

Sheria zetu zinaruhusu kutolewa kwa barua ya usimamizi mirathi kwa muda yenye mipaka katika utendaji. Barua ya muda mfupi ya usimamizi mirathi itampa msimamizi wa muda haki na mamlaka yote ya msimamizi mkuu, isipokuwa mamlaka ya kugawa mali tu. Katika sheria, hii inajulikana kama kutolewa kwa barua ya usimamizi wa mirathi wa muda kabla ya kuteuliwa msimamizi rasmi (pendente lite). Tunapendekeza kuwa uombe mara moja barua ya usimamizi mirathi ili kulinda mali ya marehemu baba yako kabla ya uamuzi wa mahakama kwenye kesi ya msingi.

Maombi haya yanapaswa kufunguliwa chini ya 'hati ya dharura' ili kupangiwa tarehe ya kusikilizwa haraka.

## Mume wangu ana 'Nyumba Ndogo'

**Tumefunga ndoa ya Kikristo yapata miaka kumi na tano sasa na kubarikiwa kupata watoto watano. Nina ushahidi kuwa mume wangu ana kimada na nyumba nyingine (nyumba ndogo). Je, hili si kosa la jinai? Nichukue hatua zipi?**

*20 Septemba 2010*

Kwa kuwa na nyumba ndogo, mumeo anafanya uzinzi. Tafsiri ya uzinzi ni kufanya mapenzi kati ya mtu aliyeolewa/kuoa na mtu ambaye si mwenzi wake halali wa ndoa.

Kwa bahati mbaya, hili si kosa la jinai nchini

Tanzania, hivyo mtu hawezi kukamatwa kwa kuwa katika aina hii ya uhusiano.

Ikiwa tabia hii haitabadilika au uhusiano wenu hauwezi kurudi kama mwanzo, hii ni sababu tosha ya kuomba talaka. Pia una haki ya kumshtaki kimada wake (nyumba ndogo) na kudai fidia, lakini madai hayo yanaweza kukataliwa na mahakama ikiwa itathibitika kuwa kwa mwenendo wako, matendo yako au kushindwa kwako kumtendea mumeo kumechangia au kumlazimisha mumeo kuwa na tabia hiyo.

## Umuhimu wa Mahari

**Nilifunga ndoa ya Kikristo na mwanamke mmoja hivi. Cha kushangaza, baba yake alikuja na kumchukua kinyume na matakwa yake, akidai kwamba sijamtolea mahari. Sipingi kutoa mahari, lakini kiasi kinachohitajika ni kikubwa. Je, baba ana haki ya kunitenga naye kisa sijalipa mahari? Je, mahari ni jambo la lazima chini ya sheria? Tafadhali nishauri.**

*16 Agosti 2010*

Chini ya Sheria ya Ndoa si lazima kutoa mahari. Kwa maneno mengine, kunaweza kuwa na ndoa halali kati ya mwanamume na mwanamke, bila kujali kwamba mahari imelipwa au la. Kitendo cha baba mkwe wako kumchukua mke wako na kumtenga mbali nawe ni kinyume cha sheria na si halali.

Ikiwa mkeo hawezi kurudi, unaweza kuiomba mahakama kumlazimisha baba mkwe wako kumrudisha mkeo.

## Ndoa za Kidini dhidi ya Ndoa za Kimila

**Niliolewa mwaka 1989 chini ya sheria ya ndoa za kimila na kubarikiwa kupata watoto watatu. Mwaka 2004, mume wangu alitaka kuoa mke wa pili akiwa bado amenioa mimi, sikuweka pingamizi. Alifunga ndoa ya Kikristo na mwanamke huyo mpya na walizaa watoto wengine wawili. Tuliishi kwa amani, kwani mume wetu alitutunza vizuri. Mwaka 2008, mume wangu alifariki bila kuacha wosia, na shemeji yangu alichaguliwa kuwa msimamizi wa mirathi. Cha kushangaza, baada ya matanga, msimamizi wa mirathi aliniondoa mimi na wanangu katika orodha ya warithi. Mali yote ya mume wangu alipewa mke mwenza na watoto wake. Baada ya matanga niliambiwa kwamba ndoa yangu na marehemu haitambuliki kisheria, na kuwa ndoa ya Kikristo na mke wa pili ilikuwa bora kuliko ndoa ya kimila. Je, hii ni kweli? Ninawezaje kupigania haki yangu? Je, mimi si mke halali wa marehemu ambaye nimekuwa naye katika ndoa kwa muda mrefu zaidi kuliko mke wa pili? Tafadhali nishauri.**

*2 Agosti 2010*

Sheria ya Ndoa inatambua aina mbili za ndoa - mitala na mke mmoja. Aina nyingine zote za ndoa huangukia katika makundi haya mawili. Sheria inatambua ndoa za Kikristo, za Kiislam, za kimila au za Serikali kwa kiwango sawa, na hakuna iliyo bora kuliko nyingine. Ndoa za kimila, Serikali na Kiislam zinachukuliwa kama ndoa za mitala, maana yake ni kwamba mtu anaweza kuwa na mke zaidi ya mmoja. Ndoa ya Kikristo ni ya mke mmoja tu.

Zaidi ya hayo, Sheria ya Ndoa inamzuia hasa mtu aliye katika ndoa ya mitala au ndoa yake inaruhusu kuwa na wake wengi kufunga ndoa ya mke mmoja na kuwatenga wake zake wengine.

Katika kesi yako, ndoa ya pili ya mumeo, kama ilifungwa kama ndoa ya mke mmoja, kamwe haikuwa halali na kwa hiyo haina nguvu kisheria, kwa sababu kisheria alikuwa tayari katika ndoa inayomruhusu kuwa na wake wengi, na hivyo asingeweza kufunga ndoa ya mke mmoja wakati bado akiwa amekuoa. Unachoweza kufanya ni kupinga mgawanyo huo wa mali za marehemu anaopendekeza msimamizi wa mirathi.

## Matunzo ya Mimba

**Mimi ni mwanamke mwenye umri wa miaka 20 ambaye nimekuwa na uhusiano wa kimapenzi kwa miezi sita na mwanamume. Miezi miwili baada ya kutengana niligundua kuwa nilikuwa na ujauzito. Nilipomwambia kuwa nina mimba na nahitaji matunzo ya mtoto alikataa, na kusema kuwa mtoto sio wake. Pia nilifukuzwa kazi yangu kama mfanyakazi wa nyumbani baada ya mwajiri wangu kujua kwamba nina ujauzito. Je, nina haki yoyote kisheria dhidi ya mwanamume huyu, kwa kuzingatia kwamba si mume wangu kisheria na mtoto hajazaliwa?**

*2 Agosti 2010*

Kwa bahati mbaya, na kwa sababu ya mrundikano wa maswali, jibu la swali hili linaweza kuwa limepitwa na wakati, yaani, unaweza kuwa umeshajifungua.

Hujathibitisha kama unaamini kuwa mtoto ni wa huyo mwanamume uliyekuwa nae katika mahusiano. Tuchukulie kuwa yeye ndiye baba, kutokuwa mume wa ndoa haizuii kisheria mama mtarajiwa kudai matunzo kwa baba anayesadikiwa kuwa ni baba mzazi. Sheria inampa wajibu mtu huyo kumtunza mama wa mwanae mtarajiwa. Kama inaweza kuthibitishwa, kitu ambacho teknolojia inaweza kufanya, kuwa ujauzito ni wake, unaweza kuwasilisha maombi mahakamani kudai matunzo. Hakika unapaswa kutunzwa.

Jambo lingine ni juu ya kuachishwa kazi na mwajiri wako. Maoni yetu ni kwamba kufukuzwa kazi kwa sababu ya mimba ni kinyume cha sheria, na una kesi nzuri dhidi ya mwajiri wako.

Hakuna sheria nchini Tanzania ambayo inakataza mwanamke kupata mimba, sembuse kutoruhusiwa kufanya kazi wakati ni mjamzito.

## Kumsaidia Mke wa Jirani yangu

**Jirani na kwangu kuna mwanamke asiye na ajira ambaye ametengana na mumewe miaka michache iliyopita. Watoto wake wana umri chini ya miaka 7. Kwa wema wangu, nimekuwa nikiisaidia familia hii kwa chakula na ada za shule. Hivi karibuni nimebaini kuwa mumewe ni tajiri sana. Baada ya kuwa nimetumia mamilioni ya pesa kumsaidia mwanamke huyo, niliamua kumfuata mumewe na kumdai pesa zote nilizotumia. Mwanamume huyo amekataa kunirudishia, akisema kwamba nilikuwa natoa msaada kwa sababu nilikua nampenda mwanamke huyo. Je kuna njia yoyote ambayo ninaweza kurudisha pesa zangu kutoka kwa mtu huyu? Je sheria inanilinda? Yeye ni wakili – je hiyo inaweza kuathiri maoni yenu?**

*19 Julai 2010*

Kutokana na maelezo uliyotupa, tumeshindwa kubaini kama walikuwa wameoana kisheria au la, na kama ndivyo, ndoa hiyo ipo. Hata hivyo, kwa kuzingatia umri wa watoto na hali ya kifedha ya familia, ulikuwa sahihi kutimiza wajibu wako wa kuwatunza. Ulibeba kwa pamoja jukumu la kisheria na kimaadili la mume wakati ambapo hakuwepo, hata kama hakukuwa na mkataba katika hilo.

Kitendo cha kuisaidia familia ya mwanamume huyo kinajulikana kisheria kama "agency of necessity", hivyo basi unayo sababu ya kuchukua hatua dhidi yake.

Wakili wako anaweza kukuelekeza jinsi ya kumshitaki mtu huyu. Sheria haitofautishi mwanasheria na asiye mwanasheria, hivyo basi ushauri wetu ni uleule hata kama madai ni dhidi ya mwanasheria mwenzetu.

## Utata katika Wosia

**Baba yangu aliacha wosia ambao una utata. Wawili kati yetu tuna majina sawa ya kwanza na la ukoo isipokuwa majina ya kati ni tofauti. Kuna mali ambayo baba yetu amerithisha mmoja wetu, lakini hakutaja jina la kati, hivyo haifahamiki nani anastahili**

**kuirithi. Hii imesababisha utata fulani katika familia yetu. Je, tunapaswa kufanya nini?**

*5 Julai 2010*

Hatuelewi ni kwa nini mna majina sawa ya kwanza na mwisho, lakini mnatofautiana majina ya kati. Hata hivyo tutajibu swali lako kama ulivyouliza.

Ni muhimu wosia kuwa wazi na usio na utata wowote. Ikitokea kwamba kuna utata, wosia unaweza kutafsiriwa kwa kutumia kanuni za tafsiri, mojawapo ya kanuni inayoendana na kesi hii ni 'kukalia kiti cha mwandaa-wosia', hii ni kanuni ambayo ilianzishwa na Jaji wa Mahakama ya Rufaa nchini Uingereza miaka ya 1800. Kanuni hii inaruhusu uingizwaji wa ushahidi kutoka nje ya wosia ili kufafanua maneno na kuelezea wosia. Mahakama inaweza, kwa mfano, kupokea ushahidi wa tabia za mtoa wosia anapozungumzia familia yake, mali, marafiki na watu wa karibu ili kupata tafsiri sahihi ikiwa imejivisha wasifu au kukalia kiti cha mtu aliyeandika wosia.

Katika kesi hii, tunapendekeza kuwa usome wosia wote, uelewe na kuona kama kanuni hii inaweza kutumika. Jaribu kupata ufumbuzi kwa kurejea matendo ya marehemu alikuwa akimaanisha nani katika kipindi cha uhai wake.

Hatutaki kuongeza utata, lakini labda marehemu alimaanisha wote wawili mnapaswa kurithi mali hiyo. Wakili wenu anatakiwa kuchukua nafasi ya mtoa wosia ili awaongoze vyema.

## Jinsi ya kuthibitisha Mtoto siyo wangu

**Nilikuwa na mahusiano na mwanamke kwa miaka kadhaa na kutengana mwaka uliopita. Miezi michache iliyopita aliwasiliana nami na kunieleza kwamba, alijifungua mtoto na kudai kuwa mimi ni baba wa mtoto huyo. Nilimtazama mtoto lakini hakuna namna yoyote nimefanana nae. Mama wa mtoto anasisitiza kuwa, nitoe matunzo ya mtoto, na ameniletea notisi (hati ya madai) kutoka ofisi ya wanasheria akidai pesa kwa ajili ya matunzo yake na mtoto. Kimsingi, kama mtoto angekuwa wangu nisingesumbuka kuwaandikia. Tafadhali nishauri.**

*28 Juni 2010*

Ni vizuri umetuandikia, hatukubaliani moja kwa moja na maelezo yako. Kwa kuanzia, kipimo cha uhakika kama mtoto ni wako au la, sio kwa kuangalia mtoto na kuona kama mnafanana. Hiki ni kipimo ambacho kilitumika katika zama za kale, na hakina ushahidi wa kisayansi katika zama hizi.

Njia sahihi zaidi ni kufanya kipimo cha vinasaba (DNA). Kwa sasa, Tanzania kuna vifaa na sheria inayounga mkono vipimo hivyo. Kwa mujibu wa Sheria ya Vinasaba, kuna watu na taasisi chache tu ambazo zinaweza kuomba kufanyika vipimo vya vinasaba, ikiwa ni pamoja na polisi kwa madhumuni ya uchunguzi, mahakama, daktari mwenye leseni husika au wakili.

Katika shauri lako, ikiwa mama wa mtoto hajapinga kufanya vipimo vya vinasaba, basi unaweza kumuomba daktari au wakili wako kuandika kwa Mkemia Mkuu wa Serikali na kuomba vipimo vya vinasaba. Ikiwa mama wa mtoto atapinga kupima, unaweza kupeleka ombi mahakamani.

Kutegemea na uzito wa hoja za maombi yako, mahakama inaweza kutoa au kutokutoa amri ya kufanya vipimo hivyo. Lakini kwa sasa usipofushwe na kutofanana kwako na mtoto - hilo halina uhakika.

## Msimamizi wa Mirathi anadai Gharama za Mazishi

**Mdogo wangu alifariki mwaka jana na kuacha mali kadhaa. Hakuwa ameoa ila alikuwa akiishi na mwanae wa miaka 12. Kabla ya mazishi nilipokea kiasi cha pesa kutoka kwa mmoja wa wadeni wake.**

**Nilitumia fedha hizo kwa ajili ya mazishi. Hatukujua kama marehemu aliacha wosia mpaka hivi karibuni tulipogundua kuwa alikuwa amemteua mmoja wa marafiki zake kuwa msimamizi wa mirathi. Msimamizi wa mirathi amenifuata na kudai nirudishe pesa nilizotumia kwa ajili ya mazishi la sivyo atachukua hatua za kisheria dhidi yangu. Je hii ni haki? Tafadhali nishauri.**

*24 Mei 2010*

Kwa ujumla Sheria inasema kwamba mtu yeyote ambaye anaingilia mali za marehemu au atatenda kitendo chochote ambacho kinahusiana na ofisi ya msimamizi wa mirathi na hakuwa msimamizi mwenye haki, atakuwa anakosea na kwa hiyo, atawajibika kwa msimamizi halali, mrithi au wadai wa marehemu.

Hata hivyo, tukizingatia maelezo uliyotupatia, tumegundua kwamba kutumia pesa za mdogo wako kwa ajili ya mazishi ilikuwa sahihi.

Tunakushauri umueleze vizuri msimamizi wa mirathi na umuoneshe stakabadhi za matumizi yote yaliyofanyika. Kama fedha zilitumika kihalali kwa ajili ya mazishi hatuoni kwa nini unapata wasiwasi. Inaonekana msimamizi amehisi matumizi mabaya ya fedha hizo.

## Msimamizi ameshindwa Kuchukua Hatua

**Baba yetu alifariki miaka miwili iliyopita na kwa bahati aliacha wosia ambao ulimteua rafiki yake kipenzi kuwa msimamizi wa mirathi. Kwa bahati mbaya, msimamizi ameshindwa kufungua mirathi kwa miaka miwili sasa. Badala yake amekuwa akitupatia mirathi yetu kupitia malipo ya akaunti na kutufanya tuendelee kuwa chini yake. Je, kuna namna yoyote tunaweza kumuondoa kuwa msimamizi wa mirathi na kumteua mtu mwingine badala yake? Tafadhali shauri.**

*17 Mei 2010*

Ni jambo la kuvutia sana unapozungumzia kuhusu malipo ya kupitia akaunti. Inashangaza kuona mnakubali malipo ya akaunti bila kumshinikiza msimamizi wa mirathi kwenda kufungua mirathi na kugawa mali kwa mujibu wa wosia.

Sheria ya Urithi na Usimamizi wa Mirathi inatamka kuwa ikiwa msimamizi wa mirathi anashindwa kutimiza majukumu yake anaweza kuondolewa na kuteuliwa mtu mwingine badala yake. Mrithi au mdai wa mali za marehemu anaweza kupeleka maombi mahakamani na kuiomba mahakama imuite msimamizi huyo ajivue madaraka ya usimamizi wa mirathi au afungue mirathi. Ikiwa msimaizi wa mirathi atashindwa kufungua mirathi kwa muda uliowekwa na mahakama basi muombaji anaweza kuiomba mahakama itangaze kuwa msimamizi wa mirathi amejivua nafasi yake. Ikiwa amri ya kujivua usimamizi wa mirathi itaidhinishwa na mahakama, familia ya marehemu inaweza kumteua mtu mwingine kuwa msimamizi wa mirathi.

## Makubaliano na Talaka

**Mke wangu amerejea kutoka masomoni nchini Marekani. Tangu arejee hapendi kuendelea na uhusiano wetu na hana tena upendo na mimi. Hivi karibuni nimegundua ana uhusiano wa kimapenzi na mwanamume mwingine. Je, tunaweza kupeana talaka kwa ridhaa au kupeana talaka kwa makubaliano na tukaachana kama inavyofanyika katika nchi nyingine? Je, ni hatua gani zingine tunaweza kuzifuata kupata talaka?**

*10 Mei 2010*

Kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa, walio katika ndoa hawawezi kuachana kwa kukubaliana. Taasisi pekee ambayo inaweza kutoa talaka kwa ndoa ya aina yoyote ni mahakama. Mahakama inaweza tu kutoa talaka pale ambapo ndoa imevunjika kiasi cha kushindwa

kusuluhishika, kwani serikali inapenda zaidi ustawi wa familia kuliko mifarakano. Kwa kujibu swali lako, hamuwezi kuandika talaka ya makubaliano na kuachana kwa kuwa ni mahakama pekee ndiyo yenye mamlaka ya kuachanisha wanandoa.

Hatua ya kwanza ya kupata talaka ni kuanzia kwenye. Baraza la Upatanishi wa Migogoro ya Ndoa. Baraza hili kwa kawaida lipo kwenye nyumba za ibada. Baraza litajaribu kuwapatanisha na kuwapa muda ili muweze kuondoa tofauti zenu. Ikiwa baraza litaona kwamba limeshindwa kuwasuluhisha na kujiridhisha kuwa ndoa yenu imevunjika kabisa, litawapa cheti kuonesha kwamba ndoa yenu imevunjika kabisa.

Baada ya kutolewa cheti hicho, unaweza kupeleka kesi mahakamani ambako utatakiwa kuiridhisha mahakama kwamba ndoa yenu imevunjika kabisa. Kutegemea mwenendo wa kesi yenyewe, mahakama inaweza ikatoa maamuzi stahiki juu ya haki za watoto, haki za kutembeleana, kugawana mali zilizopatikana ndani ya ndoa na kadhalika.

## Ufafanuzi wa Kisheria juu ya Kutengana

**Mimi ni msichana. Naogopa kufunga ndoa kutokana na ongezeko la talaka na visa vya kutengana kuwa juu duniani. Naelewa maana ya talaka, lakini nahitaji ufafanuzi wa kisheria kuhusu kutengana. Je, wakati ambao wanandoa wametengana wanaweza kushiriki tendo la ndoa?**

*10 Mei 2010*

Kisheria, kutengana ni amri inayotolewa na mahakama ambayo inawazuia wanadoa kushiriki tendo la ndoa na pia kuwatenganisha wasiishi pamoja. Amri hii haivunji ndoa bali inawapa wanandoa uhuru wa kutokuendelea na majukumu ya ndoa. Kama wanaweza kufanya tendo la ndoa, jibu ni ndio wanaweza lakini hawalazimishwi.

Kama kuna amri ya mahakama ya kuwatenganisha, wanandoa hawawezi kuoa wala kuolewa na hawaruhusiwi kufanya uzinzi kwa kuwa makubalino ya ndoa yanaendelea mpaka pale watakapopeana talaka. Unaweza kuchukulia kutengana kama hatua ya mwanzo wakati mkifikiria talaka.

## Ndoa na Wosia

**Nilirithi mali za baba yangu miaka ishirini iliyopita ambayo ilijumuisha mali na uwekezaji mwingine. Wakati nilipofikisha miaka 18, nilishauriwa na rafiki wa karibu wa baba yangu kuandika wosia. Mwanasheria Mwingereza aliniandikia wosia lakini iliniwia vigumu kuusaini kwa kuwa sikujua ni nani nitamwachia mali ikiwa nitafariki. Sasa nimeoa na nimeambiwa na mwanasheria yule yule kwamba wosia wangu wa awali utakuwa umepitwa na wakati. Tafadhali nishauri.**

*26 Aprili 2010*

Mapendekezo yetu ni kwamba mtu yeyote mwenye umri wa kuanzia miaka 18 anaweza kuandika wosia. Katika hali yako, kutokujua nani wa kumwachia urithi inamaanisha kwamba ni muhimu sana kuandika wosia. Ni lazima ujue kuwa wosia hauandikwi wakati una familia tu. Kuna watu wengi ambao walikuwa hawajaoa na waliacha mali zao nyingi kwenye taasisi za misaada ambazo zinaendelea kunufaika na mali hizo.

Kwa kujibu swali lako, mwanasheria wako yuko sahihi. Ukioa, moja kwa moja utakuwa umefuta wosia wako. Hivyo, unapaswa kuandika wosia mwingine. Hatuelewi kwa nini unasita kwani kuandika wosia hakusababishi wewe kufa mapema.

## Hatujafunga Ndoa lakini Tunaishi pamoja

**Nimekuwa nikiishi na mwanamke kinyumba kwa miaka kadhaa mpaka mpenzi wake wa zamani aliporudi kutoka nje ya nchi na**

**sasa ananitishia kunichukulia hatua. Sina hakika nifanye nini. Je, ninafanya makosa? Ni aina gani ya hatua zinaweza kuchukuliwa pale ambapo mwanamume na mwanamke kwa hiari yao wenyewe wameamua kuishi pamoja? Je, tunatakiwa kufunga ndoa ili kuishi pamoja na kuwa na mahusiano? Je, waliooana tu ndio wanaweza kuishi pamoja? Nifanye nini?**

*19 Aprili 2010*

Tumesoma swali lako ambalo ni la kuvutia sana. Kwa kuwa hatukujui na wala hatuna namba yako ya simu ili tukupigie utufafanulie, tunatafsiri maneno yako 'kutishia kuchukua hatua' kuwa na maana ya kutishia kufungua shauri mahakamani dhidi yako. Lakini kama alimaanisha kukuchukulia hatua kwa maana ya kukutishia kukudhuru mwili basi tunakushauri kutoa taarifa polisi kwa kuwa hiyo itakuwa ni kesi ya jinai.

Je, kuna sheria ambayo inazuia watu wawili ambao hawajaoana kuishi pamoja? Jibu letu ni hapana, sheria haikatazi uhusiano huo. Kuna mifano ya sheria kutoka nchi nyingine ikiwa ni pamoja na Uingereza ambayo inakubaliana na kile tunachokisema.

Mojawapo ya kesi za hivi karibuni tunayoifahamu, ambayo inafanana na mazingira yako kwako ni ya kutoka India ambapo Mahakama ya Juu ilijiuliza kama kuishi pamoja na kushiriki mapenzi kabla ya ndoa lilikuwa kosa kisheria. Mahakama ikaamua kuwa hakuna kosa kisheria kwa kuishi pamoja na kushiriki mapenzi kabla ya ndoa. Mahakama ikahitimisha kuwa kimsingi kuishi pamoja ni haki ya maisha.

Inawezekana unachanganya kati ya maadili na sheria. Kuishi pamoja na kushiriki tendo la ndoa kabla ya ndoa ni suala la kimaadili na sio la kisheria. Kwa upande wetu hatuwezi kuzungumzia suala la maadili.

## Hatuna Watoto wa Kiume kwenye Ndoa

**Mimi na mume wangu tuna watoto watatu wa kike. Mume wangu anataka mtoto wa kiume. Baada ya kupata mimba nyingine tulienda kwa daktari ili kujua jinsia ya mtoto aliyeko tumboni. Baada ya vipimo tukaambiwa ni wa kike tena. Mume wangu anataka nitoe mimba. Je, hiyo ni sawa kisheria? Je, sababu hii inatosha kwa mume wangu kutaka kunipa talaka? Amenitishia zaidi ya mara moja kama sitamzalia mtoto wa kiume, ataniacha. Niko kwenye shinikizo kubwa/njia panda. Tafadhali nisaidie.**

*12 Aprili 2010*

Utoaji mimba kwa kuzingatia maelezo yako hapo juu ni kinyume cha sheria na ni kosa la jinai. Shida ya mume wako ya kuwa na mtoto wa kiume haiwezi kusababisha wewe kutoa mimba ya mtoto wenu wa nne. Mtoto huyu ni wenu. Kama sababu za kutoa mimba ingekuwa ni kulinda afya ya mama, ingekuwa sawa kisheria. Na si vinginevyo.

Sababu hiyo pia si ya msingi kwa kutoa talaka. Unaweza kumuelimisha mumeo kwamba jinsia ya mtoto inategemeana na mbegu za kiume na si yai la kike.

## Mama ana Mahusiano ya kimapenzi na Kijana mdogo

**Wazazi wangu walipeana talaka miaka miwili iliyopita na nimekuwa nikiishi na mama yangu tangu wakati huo. Hivi karibuni mama yangu ameanza "kutoka" na mmoja wa rafiki zangu ambaye pia amepevuka na nasikia kwamba wanaweza kufunga ndoa. Hii imesababisha matatizo katika uhusiano na rafiki yangu. Je, kuna sheria ambayo hairuhusu mahusiano ya namna hiyo? Je, ninaweza kupata zuio la mahakama?**

*12 Aprili 2010*

Hatuna uhakika unamaanisha nini unaposema "kutoka". Kama "kutoka" ulimaanisha ni uhusiano wa kimapenzi, hakuna kibaya chochote katika uhusiano

huo kwa kuwa mama yako tayari ana talaka na mtu anayetoka naye kimapenzi ni mtu mzima. Hakuna sheria yoyote ambayo inazuia uhusiano huo.

Hata hivyo, Sheria ya Ndoa imeweka mipaka ya ndoa. Sheria iko wazi kwamba mtu hapaswi kuoa au kuolewa kabla hajafikisha umri fulani ambao kwa mvulana ni miaka 18 na msichana ni miaka 15. Sheria pia inaweka marufuku kwa mtu kuoa au kuolewa na bibi au babu yake, mzazi, mtoto au mjukuu, dada au kaka, mama mkubwa au baba mkubwa, shangazi au mjomba, binamu au mpwa. Sheria inasema zaidi kwamba ni marufuku kwa mtu kuoa au kuolewa na bibi au babu yake, mtoto au mjukuu wa mwenzi wake au mwenzi wake wa zamani na ni marufuku kwa mtu kuoa au kuolewa na mtu ambaye umemuasili au mtu ambaye ameasiliwa.

Kesi yako haiangukii katika kundi lolote hapo juu. Kwa bahati mbaya huwezi kuomba amri yoyote ya mahakama.

## Kuasili kwa Mgeni

**Mimi ni Mkenya ninapenda kuasili mtoto nchini Tanzania. Je, kuna masharti yoyote? Kwa nini kuasili hapa nchini ni vigumu kuliko katika nchi nyingine?**

*5 Aprili 2010*

Kuasili kunasimamiwa na Sheria mpya ya Mtoto ya mwaka 2009.

Sheria hii inaainisha masharti kadhaa kwa mtu yeyote anayetaka kuasili mtoto nchini Tanzania.

Kwa mgeni, unatakiwa kuiridhisha mahakama kwamba mtoto atatunzwa kwa kuzingatia maslahi mapana ya mtoto, uwe umekaa Tanzania angalau kwa muda wa miaka mitatu mfululizo, mtoto amekuwa chini ya uangalizi wako kwa angalau miezi mitatu chini ya usimamizi wa Idara ya Ustawi wa Jamii, huna kumbukumbu yoyote ya uhalifu katika nchi yako ya asili au nchi nyingine yoyote, kuwe na mapendekezo juu ya uwezo wako wa kuasili mtoto kutoka kwa afisa ustawi wa jamii wa nchi yako au mamlaka yoyote husika ya nchi ambayo una makazi ya kudumu, na mwisho, umeiridhisha mahakama kwamba nchi yako ya asili inaheshimu na inatambua amri za kuasili.

Kama umetimiza vigezo hivyo hapo juu basi unaweza kuomba amri ya mahakama. Kwa ujumla, wajibu wa mahakama ni kuhakikisha kuwa maslahi mapana ya mtoto yanalindwa.

Juu ya masharti kuwa magumu hapa Tanzania kuliko sehemu nyingine, hatuna uhakika sehemu gani ya dunia unaiongelea. Lazima utambue kwamba maslahi mapana ya mtoto ni muhimu katika uamuzi wowote kutoka katika mahakama yoyote. Maslahi mapana ya mtoto ni kanuni ulimwenguni kote ambayo mahakama zote huzingatia.

## Mama amepata Mtoto baada ya Baba kufariki

**Baba yetu alifariki mwaka 2007 na akabaki mama na kaka zangu wawili. Miaka michache baadaye, mama yangu alijifungua mtoto wa kike. Mama yangu aliteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu baba yetu na amemuorodhesha mtoto wake huyo kama mmoja wa warithi wa mali za baba yetu japokuwa mtoto huyu sio mtoto halali wa marehemu baba yetu. Hakimu anayesikiliza shauri hili anaonesha kuunga mkono jambo hili. Je, sheria inasemaje?**

*29 Machi 2010*

Kwa kuwa shauri lipo mahakamani na linasubiri uamuzi huwezi kutoa uamuzi wa mapema juu ya suala hilo. Hata hivyo, kwa namna tunavyosoma swali lako, ni kwamba katika maoni yako binafsi inaonekana kama Hakimu ameegemea upande wa mama yako.

Kwa kuwa baba wa mtoto hajulikani, sheria inatamka kwamba kama mjane amepata

mimba, mtoto wa mjane huyo ana haki ya kurithi mali ya marehemu hata kama mtoto sio damu ya marehemu. Hivyo dada yako anaweza kurithi. Hata hivyo, hii pia hutegemea mila ambazo mnafuata. Kwa kuwa hatuna uhakika na mila zako, tunakushauri kutafuta ushauri mwingine.

## Mwanamke kuzaa Watoto wengi

**Je, kuna sheria ambayo inamzuia mtu kuendelea kuzaa? Mimi ni mhudumu wa afya katika moja ya hospitali za vijiji hapa Tanzania. Mama wa rafiki yangu anao watoto kumi na mbili na tayari ni mjamzito. Sitashangaa ikiwa baada ya mimba hii atabeba mimba nyingine. Ninawezaje kupata amri ya mahakama ya kuzuia jambo hili kutokea? Je, kuna mtu anaweza kuja kumwokoa mwanamke huyu?**

*8 Machi 2010*

Hatujui kama tusikitike na wewe au la, kwa kuwa hatuna uhakika mwanamke huyo anachukuliaje hali hiyo. Kwenye baadhi ya jamii wanawake wanazaa watoto wengi. Wakati zipo sheria kwenye baadhi ya nchi kama China ambazo zinaweka kiwango cha watoto ambacho familia inaweza kuwa nao, nchini Tanzania kwa bahati nzuri au mbaya, hakuna sheria kama hiyo.

Nchini Tanzania, baadhi ya familia zimeendelea kuwa na watoto wengi. Ongezeko la Idadi ya watu ni kikwazo katika maendeleo ya nchi maskini; kwa bahati mbaya mila hizo bado zinaendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Kutokana na kukosekana kwa sheria, tunapendekeza kwamba uwaombe wanandoa hao wawasiliane na mshauri wa uzazi wa mpango kwa msaada zaidi, kwa kuwa huwezi kushinda kesi ya namna hii mahakamani.

## Ridhaa ya kuweka Mali Rehani katika Ndoa ya Mitala

**Nina wake wawili. Nina nyumba moja ambayo wake zangu hukaa kwa zamu ya mwezi mmoja mmoja. Ninakusudia kukopa fedha benki na kuanzisha biashara na kuiweka nyumba rehani. Benki inataka mke wangu asaini kwenye hati ya mkopo. Mke wangu wa pili ni muelewa na ndiye ninataka atie saini. Je, hiyo inatosha? Kutatokea nini nikishindwa kurejesha mkopo na mke mwingine (ambaye hakukubaliana) akipinga mauzo ya nyumba? Je, nitafunguliwa mashtaka yoyote ya jinai?**

*15 Februari 2010*

Una utaratibu wa kusisimua sana jinsi unavyoishi na wenzi wako. Unapokusudia kuweka rehani nyumba yako ili upate mkopo, wake zako kuridhia ni suala muhimu sana kwa sababu ya unyeti wa suala lenyewe. Sheria ya Ndoa inatamka wazi kuwa kama mume ana mke zaidi ya mmoja, wake wote watakuwa na hadhi na nafasi sawa katika ndoa. Sheria iko wazi pia kwamba kama mwanandoa anataka kuweka rehani nyumba ya familia ni lazima apate ridhaa ya mwenzi wake. Nyumba ya familia imeelezwa kama ni nyumba ambayo mke na mume kwa kawaida huwa wanaishi.

Kwa kuwa wanawake wote wanaishi kwenye hiyo nyumba ingawa kila mmoja kwa wakati wake, hiyo ni nyumba ya wote na hivyo unahitaji kupata ridhaa ya wake wote wawili. Jibu lingekuwa tofauti kama kila mwanamke angekuwa na nyumba yake.

Hatukushauri kuidaganya benki kuhusu idadi ya wanawake ulio nao, kwa mujibu wa sheria ya mwaka 2008 ya kuweka rehani, ni wajibu wa anayeomba kuweka rehani kutaja kama ana mwenzi au wenzi na kama ukisaini kiapo au kutoa maelezo kwa benki kuhusiana na jambo la mwenzi au wenzi na ikajulikana kuwa ni uongo unaweza kufunguliwa kesi ya jinai.

Ukishindwa kulipa mkopo, ambayo tunaamini si nia yako, na mke wako mwingine hakusaini hati ya kuridhia, benki inaweza

kushindwa kutekeleza mauzo ya nyumba iliyowekwa rehani ijapokuwa bado benki inaweza kuendelea kukufuatilia uilipe.

## Mume kuoa mara Mbili

**Nimekuwa nikiishi na mwanamume tangu 1989 na kubahatika kuzaa nae watoto sita. Miaka sita baadaye, mpenzi wangu alifunga ndoa ya kikiristo na mwanamke mwingine. Tuliendelea kuishi pamoja na mke mwenzangu mpaka mume wetu alipougua na kufariki. Kipindi anaugua alikwenda kanisani na akaomba atakapofariki azikwe kwa imani ya Kikristo. Hata hivyo, aliwekewa vikwazo vya kumuacha mke mmoja kabla ya ombi lake kukubaliwa. Alimchagua mke wa pili ambaye alifunga nae ndoa ya Kikristo. Alifariki miezi michache baadaye na hakuacha wosia. Mke aliyefunga naye ndoa alichukua mali zote za marehemu na kujimilikisha na watoto wake bila ya kunigawia chochote mimi na wanangu. Alidai mbele ya viongozi kwamba sikuwa mke halali wa marehemu na kwa hiyo watoto wangu hawawezi kurithi mali za marehemu. Haki zangu ni zipi ikiwa nimeishi na mwanamume huyo kwa zaidi ya miongo miwili?**

*8 Februari 2010*

Sheria ya Ndoa inatambua aina mbili za ndoa. Ndoa za mitala na za mke mmoja. Ndoa hizi zinaweza kufungwa kikristo, kiisilamu, kimila au kiserikali. Bila kujali aina, ndoa hizi zote zina hadhi sawa kisheria. Hata hivyo, wakati ndoa za kimila, kama zilivyo ndoa za Kiislamu, zinaweza kuwa za wake wengi, ndoa za kikiristo ni za mke mmoja tu, ikiwa na maana kwamba hakuna ndoa nyingine inaweza kufungwa.

Hata kama hukuwa na cheti rasmi cha ndoa, wewe umekuwa ukiishi na mtu huyo kwa miaka mingi na kwenye macho ya sheria, mnatumbulika kama mume na mke.

Ikiwa huo ndio ukweli, ndoa ya kikristo iliyofungwa ni kinyume cha sheria na ni batili. Hii ni kwa sababu ndoa yako na marehemu ilikuwa ya kwanza na bado iliendelea kuwepo wakati anafunga ndoa inayodaiwa kuwa ya kikristo. Pili, ndoa ya baadaye ikiwa ya kikiristo, isingeweza kufungwa ya mke mmoja.

Je, hiyo inamaanisha kuwa sasa mke wa pili hana haki? Kwa kuwa mke wa pili pia aliishi na alikuwa na watoto na mume wako, yeye pia anatambuliwa kama mke wa marehemu chini ya sheria ya kimila na hivyo wewe, yeye na watoto wenu mna haki ya kunufaika na mali za marehemu. Wala hakuna hata mmoja wenu anayeweza kutengwa.

## Mtoto sio wangu.

**Nina miaka 24 na nipo kwenye mahusiano tangu mwaka 2007. Nilisitisha mahusiano na mpenzi wangu mwezi Januari mwaka 2009 kutokana na kutokuwa na maelewano. Mwezi Machi 2009 msichana huyo alijifungua mtoto wa kiume. Moja ya sababu iliyopelekea kuachana ni kutokuwa na uhakika kama nilikuwa ndiye baba wa mtoto kwa kuwa mpenzi wangu alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na rafiki yangu wa karibu. Kwa sasa msichana huyu ananilazimisha kuweka jina langu kama baba kwenye cheti cha kuzaliwa. Je sheria inasemaje kwenye hali kama hii? Ninawezaje kuthibitisha kuwa mimi si baba wa mtoto?**

*1 Februari 2010*

Sheria inasema kwamba ni lazima kwa kila mtoto aliyezaliwa akiwa hai kusajiliwa, na jukumu hilo limewekwa kwa wazazi. Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo inatamka kuwa hakuna mtu atasajiliwa kama baba wa mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa isipokuwa tu kama baba huyo ataomba kusajiliwa na kujitambulisha kuwa ndiye baba wa mtoto na kusaini au kuweka alama ya vidole katika fomu za usajili.

Kwa kifupi, sheria haikulazimishi kuweka

jina lako kwenye cheti cha kuzaliwa kama baba wa mtoto huyo.

Swali lako la mwisho ni vigumu sana kulijibu. Sayansi imepiga hatua kubwa na enzi za kale za baba kukataa mtoto kuwa sio wake zimepitwa na wakati. Katika zama za leo, kipimo tu cha kawaida cha vinasaba (DNA) kitaonyesha ni nani baba halisi wa mtoto. Hakuna namna ya kuhakikisha kuwa wewe siye baba wa mtoto. Huu sio mchezo wa kompyuta kwamba unaweza kubadilisha chaguo.

## Kubadili Wosia wangu

**Nimeoa hivi karibuni na nafikiria kuandika wosia. Hata hivyo, kuna baadhi ya mali nimezipata na ninataka kuziingiza kwenye wosia. Je, nisubiri mpaka manunuzi yote yakamilike? Ni mara ngapi ninaweza kubadilisha wosia wangu?**

*8 Februari 2010*

Kuna msemo maarufu sana wa Waingereza ambao unasema: kuna vitu viwili visivyoepukika maishani; kifo na kodi! Ni lazima kila mtu atakufa na ndiyo maana tunashauri kila mtu awe na wosia. Ni moja ya nyenzo muhimu sana ambazo utazitengeneza na hazitakusaidia wewe, bali zitawasaidia wale unaowapenda na warithi wako. Watu wengi hawaupi uzito ukweli huu.

Tumetilia maanani biashara unayotaka kufanya. Tunapendekeza uandike wosia na utaje vitu unavyotarajia kuvimiliki. Mara tu biashara husika itakapokamilika, tunapendekeza uandae wosia mwingine ambao utahusisha mali mpya na uhakikishe unazitaja kwa uwazi.

Unaweza kubadilisha wosia wako mara nyingi kadiri upendavyo. Ukiandika wosia mpya, wosia huo mpya unafuta wosia uliotangulia mara moja.

## Kujua Wosia

**Nimeandika wosia na ninataka kujua iwapo kuna njia ya moja kwa moja itakayowafanya wanufaika kujulishwa kuwa ni wanufaika baada ya kifo changu. Pia ninapenda kujua msimamizi wa mirathi yangu atajuaje kwamba nimemchagua yeye. Nisingependa kilichomo kwenye wosia wangu kijulikane kwa mtu yeyote ikiwa ni pamoja na mke wangu na wanufaika wengine. Je, kuna sehemu yoyote maalum ninaweza kuitumia kutunza wosia wangu?**

*11 Januari 2010*

Hakuna wanufaika wala msimimizi au wasimamizi watajua kama wametajwa kwenye wosia wako kama hutawapa taarifa. Ni hivyo tu. Hakuna mamlaka ambayo itawapa taarifa.

Pendekezo letu la kwanza, hakikisha unamshirikisha mtu unayetaka awe msimamizi wa mirathi ili kujua anakubali au la. Ni busara pia kumteua msimamizi mbadala ikiwa msimamizi wa kwanza atashindwa kusimamia kwa sababu fulani. Hakikisha pia unamjulisha msimamizi wako mbadala. Watu wengi wanasahu kuteua msimamizi mbadala.

Pili, unapaswa kuhakikisha kwamba mtu mmoja unayemuamini sana, awe msimamizi, mnufaika au mtu mwingine yeyote, anajua mahali ambapo unatunza wosia wako. Hakikisha sehemu unayotunzia wosia isifahamike mpaka pale utakopafariki.

Usalama wa wosia pia ni muhimu. Unaweza kuufanyia mabadiliko wosia wako, kwa mfano kumuongeza mtoto aliyezaliwa au mjukuu katika wosia wako. Vyovyote itakavyokuwa, ni wazo zuri kuupitia wosia wako mara moja kila baada ya kipindi fulani.

Baadhi ya watu wanahifadhi wosia wao nyumbani. Wengine wanahifadhi katika kasiki za mabenki na kutoa maelekezo kwa benki hizo kutotoa wosia huo kwa watu husika mpaka pale watakapofariki.

Wengine hutumia sehemu maalum za kuhifadhia wosia. Hatuna ufahamu wa

sehemu husika za kuhifadhia wosia nchini, lakini kuna sehemu nyingi kama hizo nje ya nchi.

Sehemu hizi hutoa hakikisho kwamba wosia hautafunguliwa na kupatikana kwa urahisi. Hizi ni sehemu ambazo zinazuia moto na zinatunza kumbukumbu kwa zaidi ya miaka mia mbili.

## Kuamua mapema juu ya Matibabu

**Mimi ni tajiri. Ninataka kuhakikisha kuwa kama itatokea hali ambayo itanifanya nisiwe na uwezo wa kufanya maamuzi yoyote juu ya hali yangu ya kiafya, ambayo inaweza kunikumba, mtu nitakayemchangua atafanya maamuzi husika kwa kuzingatia maelekezo yangu ya maandishi. Je, ninawezaje kulifanya hili?**

*21 Desemba 2009*

Ni swali zuri. Kwa kuanzia, huhitaji kuwa mtu mwenye utajiri mkubwa kufanya hivyo. Wengi tu hufanya maamuzi kama hayo kwa kuzingatia sababu za kidini na sababu nyingine za familia.

Hicho unachotaka kukifanya kinajulikana kama 'uamuzi wa mapema.' Ni uamuzi unaoufanya kwa ajili ya baadaye, ambao utafanya kazi katika mazingira ambayo hautaweza kukubali au kukataa matibabu unayoweza kupatiwa. Uamuzi huo utasaidia kuzuia kufanyiwa matibabu ambayo wewe mwenyewe hukuyapenda.

Kwa maneno mengine, hii ni njia ya kuweka wazi mapema matakwa yako ya kukataa aina fulani ya matibabu ambayo unaweza kupewa. Inaweza kutumika kukataa matibabu yoyote katika misingi ya kidini au vinginevyo.

Ni muhimu kuwa wazi sana na kwa usahihi ni matibabu gani unayabainisha na katika hali gani unakusudia kukataa. Ni vyema kumwona daktari kwa ajili ya maelezo sahihi ya matibabu unayokusudia kuyakataa.

Uamuzi huu wa mapema hautafuatwa kama kuna sababu za msingi za kuamini kwamba kuna mazingira ambayo hukuyategemea wakati ulipofanya uamuzi huo wa mapema na ambao ungeweza kuathiri uamuzi ambao ulikusudia.

Tafadhali kumbuka kuwa uamuzi wa mapema unaweza tu kutumika pale ambapo mtu anayeiangalia afya yako anafahamu. Itabidi ufikirie kwa makini ni wapi na namna gani utawasilisha uamuzi wako kwa wahusika. Ni muhimu kuwa na nakala ya kumbukumbu ya uamuzi wa mapema kwenye faili lako la hospitali. Pia unapaswa kuijulisha familia na marafiki zako juu ya uwepo wa uamuzi wa mapema. Tunapendekeza kwamba uamuzi huu wa mapema ufanywe kwa maandishi na kwa hati ya uwakilishi.

Pia hatuna uhakika kwa nini unafikiri kufanya hivyo. Je, una ugonjwa wowote mkubwa unakusumbua? Kama ndivyo, tunapendekeza pia uandike wosia.

## Utoaji Mimba zisizotarajiwa

**Nilipewa mimba na mwanamume ambaye sikutarajia kuzaa naye. Ninajua kutoa mimba ni kinyume cha sheria lakini baadhi ya marafiki zangu wamekuwa wakiniambia kwamba ninaweza kutoa mimba ya mtoto ambaye hajazaliwa kama ninazo sababu za msingi kufanya hivyo. Je, hii ni kweli?**

*26 Octoba 2009*

Jibu letu linaweza lisikufurahishe. Kutokana na swali lako, tunashukuru umeweka wazi kwamba sababu yako ya kutoa mimba ni kuwa hukufikiria kuzaa na mwanamume ambaye amekupa ujauzito. Umesema kwa usahihi kabisa kuwa utoaji mimba ni kosa kisheria, vinginevyo kuwe na sababu ya msingi ya kufanya hivyo. Sababu yako haikubaliki katika sheria zetu na hivyo huwezi kutoa mimba.

Utoaji mimba umekuwa jambo lenye utata katika jamii duniani kote kwa sababu za kimaadili. Pamoja na kwamba utoaji mimba

umekuwa ukizuiliwa mara kwa mara lakini bado limeendelea kuwa jambo la kawaida katika maeneo mengi ambako umezuiliwa. Nchini Tanzania chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu, utoaji mimba kiujumla umezuiliwa. Mtu yeyote, ambaye ana nia ya kumsaidia mtu kutoa mimba anaweza kukabiliwa na kifungo cha miaka kumi na nne. Mwanamke mjamzito anayefanya kitendo kama hicho kuhusiana na ujauzito wake au kuruhusu tendo la utoaji mimba kufanyika anakabiliwa na kifungo cha miaka saba. Unaweza kuona kwamba kama utatoa mimba unaweza kuishia gerezani.

Hata hivyo zuio hili lina mipaka yake hasa pale ambapo utoaji mimba utafanyika ili kuokoa maisha ya mama mjamzito. Kifungu cha 230 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu kinasema kwamba mtu hawajibiki kisheria kama, kwa nia njema na chini ya uangalizi wa juu na ustadi wa dakatari, atatoa mimba ili kuokoa maisha ya mama, na kwa kuzingatia hali ya mgonjwa kwa muda huo. Aidha kifungu cha 219 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu kinasema kuwa hakuna mtu atakayekuwa na hatia ya kusababisha kwa makusudi kifo cha mtoto aliyeko tumboni kama jambo hilo lilifanyika kwa nia njema na kwa lengo la kuokoa maisha/uhai wa mama.

## Mke wangu anakataa Kuzaa na Mimi

**Tumefunga ndoa tangu mwaka 2006. Kabla ya ndoa yetu mke wangu hakuwahi kupinga kuwa na watoto ukizingatia kwamba binafsi ninapenda watoto. Kinyume na matarajio yangu, baada ya ndoa, mke wangu alianza kusisitiza matumizi ya kinga kuzuia mimba kitu ambacho mwanzoni sikukataa kwa kudhani kuwa hakutaka kuwa na watoto mapema baada ya ndoa. Sasa ni zaidi ya miaka mitatu na hataki kutoa vipandikizi vya kuzuia mimba. Pia hapendi kujadili jambo hilo na hataki kushiriki tendo la ndoa bila kinga kitu ambacho kinaleta mvutano kwenye uhusiano wetu. Hili linaathiri afya yangu. Je, ninaweza kufanya nini?**

*21 Septemba 2009*

Watanzania wengi wanaamini kwamba watoto huleta bahati kwenye familia, japo sheria haisemi hivyo. Sheria ya Ndoa haiwalazimishi wanandoa kuwa na watoto. Watoto ni matokeo tu ya ndoa.

Unayo machaguo machache. Mnaweza kwenda kumwona mshauri wa masuala ya ndoa. Hata hivyo, huo sio ushauri wa kisheria. Uamuzi wa pili ni kuomba talaka. Moja wapo ya sababu ya kuomba talaka unayoweza kuitumia ni kufanyiwa ukatili. Kitendo cha mke wako kuendelea kusisitiza juu ya matumizi ya vipandikizi vya kuzuia mimba na kukataa kuzaa mtoto inakusababishia mfadhaiko wa akili. Unaweza kushinda kulingana na utakavyoweza kuishawishi mahakama. Mke wako kuendelea kukataa kuwa na watoto inaweza kutafsiriwa kuwa ni ukatili.

Kama ushauri nasaha haufanyi kazi, na hamu yako ya kuwa na watoto inazidi umuhimu wa kuwa katika ndoa na mwanamke huyo, basi wasilisha maombi yako ya talaka katika sehemu husika.

## Marekebisho ya Wosia

**Niliandika wosia miaka kumi iliyopita na ninafikiria kuubadilisha. Mjomba wangu ambaye pia atakuwa msimamizi wa mirathi yangu ananishauri kwamba sina haja ya kuandika upya wosia wangu; ninaweza kufanya marekebisho na kuyaunganisha na ule wosia wa awali. Je, mnapendekeza nini?**

*18 Augusti 2009*

Wosia wa nyongeza (codicil) ni marekebisho ya kimaandishi yaliyofanywa kwenye wosia wa awali wa mtu, ambayo ni lazima yawe na tarehe, yasainiwe na yashuhudiwe kama ambavyo hufanyika kwa wosia wa awali. Wosia wa nyongeza ni lazima ufanye marejeo au utaje wosia wa

awali unaofanyiwa marekebisho. Wosia wa nyongeza unaweza kuongeza, kupunguza au kuboresha masharti ya wosia wa awali. Wakati mtu atakapofariki, wosia wa awali na wosia wa nyongeza huwasilishwa mahakamani kwa ajili ya kuidhinisha mirathi na ni sehemu ya msingi ya usimamizi wa mali husika.

Ni jambo jema kufanya marekebisho kwenye wosia wako. Hata hivyo, inaonesha hujapitia wosia wako kwa muda mrefu. Kwa kawaida huwa tunawashauri wateja wetu kuhuisha wosia wao kila baada ya miaka miwili kama si kila mwaka, hasa kulingana na mabadiliko ya mali.

Ijapokuwa wosia nyongeza unafaa, tunapendekeza uandike wosia mpya ambao utazingatia mabadiliko katika wigo wako wa mali ndani ya miaka 10. Kuandaa wosia mpya haichukui muda na unapaswa sana kutilia maanani.

Kama bado unafikiri kuandika wosia wa nyongeza hakikisha kwamba wosia huo uko wazi na hauna utata.

## Hakuna Tendo la Ndoa baada ya Kuoana

**Miezi miwili iliyopita nilimuoa msichana kutoka India ambaye amekataa kufanya tendo la ndoa na mimi. Hatoi sababu yoyote. Alisisitiza nipime virusi vya UKIMWI na nilipima. Majibu yalionesha sina virusi lakini bado hatoi ushirikiano. Je, nifanyeje? Hii ilikuwa ndoa ya kupangwa na wazazi - mke wangu anaonekana kama nyota wa filamu na marafiki zangu wananiambia siendani nae.**

*10 Agosti 2009*

Upo katika wakati mgumu sana. Sisi ni wanasheria na si washauri wa ndoa. Hata hivyo tungependa kukushauri kutafuta kwanza msaada kwa mshauri wa ndoa ambaye anaweza kukusaidia.

Sheria iko wazi sana. Kufanya tendo la ndoa ni kukamilisha ndoa kwa kuingiliana kimwili, yaani kuingiza uume ukeni bila au kwa kutumia kondom. Ikiwa mwenzi wako hawezi kushiriki au amekataa bila sababu za msingi kushiriki tendo la ndoa, inaweza kuwa ni sababu ya msingi ya kubatilisha ndoa. Mahakama inaweza kubatilisha ndoa kwa kutoa amri ya kwamba ndoa baina yenu si halali kisheria, yaani hamkuwahi kufunga ndoa.

Ukweli kwamba mkeo anaonekana kama nyota wa filamu na kwamba wewe huendani nae haijalishi. Kuna kesi moja maarufu sana iliyoamuliwa nchini Uingereza inayofanana na ya kwako. Kusudio lako la kuvunja ndoa litafanikiwa bila kujali mwonekano wako.

## Sina Mawasiliano na Mume wangu

**Mimi na mume wangu tulikuwa tunaishi Dar es Salaam kwa miaka mingi kabla ya yeye kuhamishiwa Kongo (DRC). Tangu aondoke mwaka 2002, niliwasiliana naye mara moja mwaka alioondoka, na hatujawahi kuwasiliana tena toka kipindi hicho. Familia yake pia haijui alipo, kifupi hana mawasiliano na yeyote. Hivi karibuni nimempata mwanamume mwingine na ningependa kuolewa tena. Tafadhali naomba mwongozo.**

*3 Agosti 2009*

Katika mazingira ya kwako, Sheria ya Ndoa inasema kuwa ikiwa hakuna habari/taarifa kuhusiana na mtu fulani kwa muda wa miaka mitano au zaidi, kwa watu ambao walipaswa kuwa na taarifa kuwa yu hai, basi kutakuwa na dhana inayopingika kuwa mtu huyo amefariki. Hivyo kisheria, inaweza kudhaniwa kwamba mume wako hayupo tena duniani.

Sheria yetu inasema kwamba katika hali kama hiyo huwezi kufunga ndoa nyingine bila kupata amri ya mahakama ya kuvunja ndoa hiyo kwa sababu ya kutelekezwa. Utahitaji kufanya maombi rasmi mahakamani ili

kupata amri hiyo, na mpaka amri hiyo itolewe, hutakiwi kufunga ndoa na mwanamume mwingine kamwe.

## Tofauti ya Uzinzi kati ya Mke na Mume

**Niliolewa miaka saba iliyopita na nimeishi na mume wangu kwa furaha mpaka mwaka jana alipoanza mahusiano ya nje ya ndoa na aliyewahi kuwa mfanyakazi wetu wa ndani. Kwa hasira na ili kulipiza kisasi, nilianza mahusiano ya kimapenzi na mwanamume fulani. Wiki chache baadaye, mume wangu alinifuma nikimbusu mwanamume huyo. Alianza kunituhumu kwa uzinzi. Nilimkumbusha mahusiano yake na mfanyakazi wetu. Aliniamuru kunyamaza akidai kuwa yeye ni kichwa cha familia. Je, hii ni haki?**

*13 Julai 2009*

Maana ya uzinzi haijafafanuliwa kwenye sheria yetu ya ndoa. Hata hivyo, uzinzi unaweza kufafanuliwa kama kitendo au vitendo vyenye athari ya kuharibu kiapo cha ndoa ambacho kimefanywa na mwanandoa yoyote, kwa kujamiiana na mtu mwingine. Uzinzi pia unaweza kufanywa kwa vitendo zaidi ya kujamiiana ambavyo pia hujumuisha kuvunja kiapo cha uaminifu, kama vile mihemko ya kingono na kupandikiza mimba. Kwa hiyo kufanya uzinzi haimaanishi tu kukiuka maadili ya ndoa lakini pia matendo ya kawaida yaliyozuiliwa yanayofanywa na mke au mume, na mtu mwingine ambaye si mumewe au mkewe inatosha kuwa uzinzi.

Tukirudi tena kwenye swali lako, ulisema kuwa ulianza kuwa katika 'mahusiano ya ghafla ' (bila kujali unachomaanisha) na mtu na hivyo hakuna shaka kuwa kitendo chako cha kumbusu mwanamume huyo ni uzinzi.

Hakuna tofauti kati ya uzinzi uliofanywa na mwanamke na mwanamume. Ndoa kati ya wenzi inasimamiwa kwa usawa wa maadili na sheria na mipaka iliyowekwa na sheria ili kulinda umoja wa familia. Hata hivyo, tunakataa kukubali kwamba mume ana haki zaidi ya mke kuhusu kuvunja uaminifu katika ndoa. Kwa kuzingatia hali ya mambo kwa sasa, inaonekana kama ndoa yako inavunjika na hatua za haraka kwa wote zinahitajika ili kunusuru ndoa yako. Kabla ya kumwona mwanasheria tunapendekeza kumwona mshauri wa masuala ya ndoa kwa mwongozo.

## Hakulipa Mahari kwa ajili ya Ndoa

**Nilizaliwa miaka thelathini na sita iliyopita Wilayani Serengeti, Mkoani Mara. Mwaka 2000, nilimpa binti wa jirani yangu mimba na baadaye tuliishi kama mume na mke. Pia tumebarikiwa watoto watatu. Mwezi uliopita, mke wangu alifariki katika ajali ya basi na wazazi wake walichukua mwili wa marehemu na kunikatalia kuuzika kwa madai kuwa sikuwa nimelipa mahari. Ili kuepusha fujo zozote nilikubaliana na matakwa yao. Je, ilikuwa ni sawa kwa wao kufanya hivyo?**

*8 Juni 2009*

Tangu tarehe moja, Mei 1971, masuala yote ya ndoa nchini Tanzania yanasimamiwa na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971. Sheria hii inaeleza wazi kwamba ndoa yoyote itakuwa halali kama ilifungwa kwa kuzingatia masharti yaliyomo kwenye sheria hiyo, bila kujali desturi za ulipaji wa mahari au zawadi kabla au baada ya ndoa. Kwa maneno mengine tangu kuanza kwa Sheria ya Ndoa, kulipa mahari si jambo la lazima katika kutambua uhalali wa ndoa. Ulipaji wa mahari ni hitaji la kimila ambalo halina nguvu ya kisheria kwa ajili ya ndoa.

Kitendo cha wewe na mkeo kuishi pamoja katika hali ambayo ilipelekea watu wa nje kuamini kwamba mlikuwa mume na mke kilitosha kuwa ndoa halali katika mtazamo wa kisheria. Hivyo, hoja ya kwamba ulikuwa si mume ilikuwa si sahihi na wazazi wa marehemu hawakukutendea haki.

## Je, ninaweza kubadilisha Wosia wangu?

**Ninamiliki majengo matano jijini Dar es Salaam na niliandika wosia ambapo nilitoa majengo mawili kati ya hayo matano na kumpa mke wangu, na matatu yaliyobakia kwa kila mmoja wa watoto wangu watatu. Hata hivyo, kutokana na hali ya sasa ya soko, ninapaswa kuuza majengo manne na kubakiza moja tu. Je, niufanyeje wosia wangu? Je, ninaweza kuuza majengo niliyoandika kwenye wosia?**

*15 Juni 2009*

Mara nyingi watu hudhani kuwa wakishagawa mali zao kwenye wosia basi wanakosa haki ya kuuza au kufanya chochote juu ya mali hizo wakiwa hai. Dhana hii sio ya kweli. Unabaki na haki ya kufanya chochote unachoamua juu ya mali yako, bila ya kujali kutajwa kwake kwenye wosia.

Huwezi kugawa usichokuwa nacho. Hivyo majengo hayo manne hayawezi kurithiwa na mkeo au watoto. Mali imebadilishwa umiliki. Tunapendekeza uandike wosia mpya.

## Kurithi Mali Watoto wanaozaliwa Nje ya Ndoa

**Baba yangu alifariki miaka miwili iliyopita na kuacha wosia ambapo theluthi mbili ya mali yake amewarithisha watoto wawili ambao baba yangu aliwazaa nje ya ndoa. Sijaridhika jinsi baba yangu alivyogawanya mali zake. Je, ninaweza kufanya nini?**

*1 Juni 2009*

Kila mtu anayemiliki mali ana haki ya kufurahia na kuzitumia mali zake jinsi atakavyo. Mtu aliyekufa anaweza kushughulikia mali zake kupitia wosia.

Wosia ni kauli ya maandishi iliyosainiwa kwa mujibu wa taratibu fulani ambapo mtu hugawanya mali zake na huanza kufanya kazi baada ya kufa kwake.

Kama mtu anataka kuacha mali zake kwa watu fulani au taasisi, anapaswa kuacha wosia halali. Wosia utakuwa halali kama upo katika maandishi, umesainiwa, umeshuhudiwa na haujaacha utata wowote kuhusu ugawaji wa mali za mtu baada ya kifo. Mtu akifa akiwa na wosia halali, anahesabika kuwa amegawanya mali zake. Na ikiwa mtu atakufa bila kuacha wosia atahesabika kuwa hakuacha mgawanyo wa mali zake. Uhalali wa wosia kwa kawaida hutolewa na mahakama.

Mchakato wa kuthibitisha wosia huitwa mirathi. Wakati wa mchakato wa mirathi, mahakama hupitisha na kutoa mamlaka kwa msimamizi wa mirathi, ambaye ni mtu aliyeteuliwa kutekeleza masharti ya wosia. Baada ya mirathi kukamilika, msimamizi atatekeleza matakwa ya wosia. Hata hivyo, msimamizi wa mirathi hana nguvu kisheria wala mamlaka ya kubadilisha au kugawanya mali za marehemu kinyume na matakwa ya wosia.

Tukija kwenye swali lako, japo tunasikitika na wewe, labda kama wosia ulioachwa na baba yako si halali, hakuna kitu chochote unachoweza kufanya. Matakwa ya baba yako yanapaswa kuheshimiwa na mali za baba yako ni lazima zigawanywe kwa mujibu wa wosia. Hata hivyo, unaweza kuchukua nakala ya wosia na ukutane na wakili wako kwa ushauri zaidi.

## Mama Mkwe ni Jinamizi

**Mimi na mume wangu tunaishi na mama mkwe. Zaidi ya miezi sita sasa nimekuwa na matatizo makubwa na mama mkwe wangu. Sikubaliani na namna anavyonitendea. Kila ninachokifanya ni tatizo kwake. Ananiuliza maswali binafsi na siishi kwa amani. Ninataka talaka. Je, ninaweza kufanya nini juu ya hili?**

*11 Mei 2009*

Mkataba wa ndoa ni kama mkataba mwingine wowote - umejengwa kwa misingi

ya makubaliano na maelewano baina ya pande mbili. Umefunga ndoa na mume wako na si mama mkwe wako. Mkataba ni kati yako na mume wako na si mama mkwe wako.

Mama mkwe wako kukutendea vibaya haimaanishi kwamba umpe talaka mumeo. Swali lako halisemi kwamba mume wako anakutendea visivyo. Umemtaja mama mkwe wako peke yake. Kwa kujibu swali lako, sababu uliyotaja hapo juu si msingi wa wewe kumpa talaka mumeo.

Hata hivyo, kama mume wako anafungamana na mama yake, na huna utulivu wa nafsi au unatendewa ukatili na mume wako, unaweza kuomba talaka. Hata hivyo kabla ya kufungua maombi, sheria inakutaka kupeleka jambo hilo kwenye Baraza la Usuluhisi wa Ndoa ambalo litawaita na kujaribu kutatua mzozo husika. Kama Baraza la Usuluhishi wa Ndoa likishindwa kutatua mzozo huo, litatoa hati itakayoweka bayana maoni yake na hivyo unaweza kuendelea mahakamani.

Ili mahakama ipitishe amri ya talaka, ni lazima iridhike kwamba kuna sababu za msingi ambazo zinaonesha kwamba ndoa imevunjika na wahusika hawawezi kupatanishwa tena. Baadhi ya sababu hizo ni uzinzi, kunyimwa tendo la ndoa, ukatili, kutelekeza/kutelekezwa kwa makusudi, kufungwa maisha au kwa kipindi kisichopungua miaka mitano, ugonjwa wa akili uliothibitishwa angalau na madaktari wawili au mmoja wa wanandoa amebadili dini.

Katika ombi lako, unaweza pia kuomba mambo mengine kama vile uangalizi wa watoto, kama wapo, na matunzo yako na ya mtoto/watoto.

## Kuvunja ahadi ya Kuoa

**Mimi ni msichana mwenye umri wa miaka 26 na nilikuwa kwenye mahusiano na mume wa mtu ambaye nimezaa nae mtoto mwenye umri wa miaka 5. Mwanamume huyo aliniahidi kunioa lakini sasa amebadili mawazo. Hataki tena kuniona wala kumtunza mtoto wetu. Je, nifanye nini?**

*20 Aprili 2009*

Kwa kuwa mwanamume ana ndoa halali hawezi kukuoa. Kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa mwanamume aliyeoa hawezi kuingia makubaliano ya kumuoa mtu mwingine labda ndoa halali iwe ni ya wake wengi. Hujatuambia aina ya ndoa aliyonayo mwanamume huyo kama ni ya mke mmoja au mitala. Hujatuambia pia sababu ya kukukwepa au kukataa kumtunza mtoto. Hata hivyo, ukichukulia ukweli jinsi ulivyo, inaonekana kwamba mwanamume huyo amekudanganya na hivyo amevunja ahadi ya kuoa.

Chini ya sheria, anaweza kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kukiuka ahadi ya kuoa. Hata hivyo, huwezi kumshitaki atekeleze ahadi, yaani ili kushinikizwa akuoe, ila inaruhusiwa kushitaki kudai fidia ya kukusababishia madhara yanayotokana na kuvunja ahadi ya ndoa ndani ya mwaka mmoja toka siku ya kuvunja ahadi hiyo. Kushtaki ili kudai fidia inayotokana na kukusababishia madhara yanayotokana na kuvunja ndoa ndio njia pekee kwa kuwa mahakama haiwezi kumlazimisha mtu kuoa.

Kwa upande wa suala la matunzo ya mtoto, unapaswa kuzingatia kuwa mtoto huyo amezaliwa nje ya ndoa kwa hiyo chini ya Sheria ya Ndoa, hana haki ya moja kwa moja ya matunzo kutoka kwa mwanamume huyo. Hata hivyo, hili lisikukatishe tamaa. Unaweza kuendelea kuwasilisha ombi mahakamani na kupata amri dhidi ya mwanamume huyo kumtunza mtoto.

Kwa Sheria ya Kuhalalisha Mtoto (Sura ya 278) unaruhusiwa kumshtaki mahakamani ili kupata amri ya matunzo ya mtoto kama unaweza kuthibitisha kuwa mtu huyo ndiye baba mzazi wa mtoto na kama mwanamume huyo amewahi kulipa baadhi ya matunzo ya

mtoto ndani ya miezi kumi na mbili baada ya kuzaliwa kwa mtoto.

## Usimamizi wa Mali za Baba ambaye ni Mzee na amepoteza Kumbukumbu

**Baba yetu ana umri wa miaka 92 na amekuwa hawezi kusimamia mambo yake. Mama yetu wa kambo anatumia mwanya huo kuhamisha umiliki wa mali za baba kwa majina yake na kutumia baadhi ya mali bila ridhaa ya wanafamilia wengine. Tufanyeje?**

*28 Aprili 2009*

Hata kama baba yako amekuwa hawezi kusimamia mambo yake mwenyewe ikiwa ni pamoja na mali, haimaniishi kuwa hazitaki na amepoteza haki zake. Mama yenu wa kambo hawezi kutumia mali za baba yenu kama anavyopenda kwani hana mamlaka ya kufanya hivyo. Sheria ya Magonjwa ya Akili imeweka utaratibu wa kusimamia mambo ya mtu aliye na matatizo kama hayo ya baba yenu. Sheria inamruhusu ndugu yoyote kuwasilisha maombi Mahakama Kuu ili kupata amri ya kuweza kusimamia mali za mtu kama huyo. Maombi hayo yafanywe kwa kutumia maombi maalum.

Hati ya kiapo lazima ieleze kwa undani misingi ya kutengenezwa kwake na iambatane na maelezo ya mali na uhusiano wake na mwombaji. Kwa hiyo tunakushauri kuandaa kikao cha familia au ukoo ambacho kitateua mtu anayefaa. Mtu aliyeteuliwa na mahakama chini ya sheria hii atatekeleza majukumu yake kwa maelekezo ya mahakama.

## Afumaniwa Akizini

**Kwa muda mrefu nimekuwa nikimhisi jirani yangu kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mke wangu. Niliandaa mtego ambao uliniwezesha kuwafumania wakifanya mapenzi. Tukio hilo lilishuhudiwa na polisi wawili pamoja na watu wengine. Cha kushangaza askari polisi wamekataa kumpeleka mtuhumiwa mahakamani wakidai kwamba tumalize jambo hilo nyumbani. Je, hili ni sawa?**

*20 Aprili 2009*

Polisi hawafungui jalada la kesi kwa kila lalamiko lililofikishwa kwao isipokuwa yale ambayo yana ushahidi wa jinai. Kwa sheria zetu, uzinzi si kosa la jinai. Ni kosa la madai lililofanywa na mzinzi. Kwa kuwa ni kosa la madai, polisi hawawezi kushughulikia kosa/ tukio la uzinzi. Kazi ya polisi ni kuwafanya watu watii sheria, kuzuia na kushughulikia uhalifu. Kwa kuwa uzinzi ni kosa la madai na sio jinai, polisi hawana cha kufanya juu ya hilo labda kama siku ya tukio kulikuwa na vurugu zilizosababisha majeraha ya mwili, haikuwa hivyo. Kwa hiyo tunakubaliana na polisi. Kama tulivyosema hapo juu, unaweza kumshitaki mgoni wako kwa kumlaghai/kumtongoza mkeo.

## Mume ana Uhusiano wa Kimapenzi Nje ya Ndoa

**Ni wazi kuwa mume wangu ana mahusiano ya kimapenzi nje ya ndoa. Kiukweli siwezi kuthibitisha lakini nimekuta ujumbe wa kimapenzi kwenye simu yake. Je, ninaweza kupata talaka? Nifanyeje?**

*13 Aprili 2009*

Kuwa na mahusiano ya kimapenzi nje ya ndoa ni moja ya sababu ambazo mahakama inaweza kuzitumia/kuzitegemea kuvunja ndoa. Tatizo lipo katika kuthibitisha uzinzi. Hii ni kwa sababu wale wanaofanya zinaa hufanya hivyo kwa siri. Hata hivyo, hii isikukatishe tamaa kuwasilisha maombi ya talaka kama unapenda kwa sababu mahakama inaweza kutoa amri ya talaka baada ya kuzingatia ushahidi wote muhimu kuhusu mwenendo na mazingira yote yanayowazunguka watu wanaosadikika wana mahusiano ya kizinzi.

Katika kesi yako, umesema kwamba

huwezi kuthibitisha kuwa anazini. Hata hivyo umedai kwamba umeona baadhi ya ushahidi ambao unakufanya uamini kuwa ana ukaribu na mtu mwingine.

Ushahidi kama huo na mwingine wa kujitegemea unaweza kutumika mahakamani. Bado hujatuambia ni lini ulifunga ndoa na mume wako. Kama miaka miwili imepita tangu mfunge ndoa, utaratibu wa kufuata ni kupeleka mgogoro wa ndoa kwenye Baraza la Upatanishi wa Ndoa kwa ajili ya maridhiano. Kama maridhiano yatashindikana, Baraza litakupa cheti ambacho unaweza kukitumia kupeleka maombi yako ya talaka mahakamani. Katika maombi yako ya talaka unaweza pia kuambatanisha na; maombi ya uangalizi wa watoto wa ndoa, kama kuna matunzo ya watoto na wewe mwenyewe, na mgawanyo wa mali zilizochumwa kwa pamoja kipindi cha ndoa. Swali lako la mwisho, 'je, nifanye nini?' hatuwezi kulijibu. Ni uamuzi wako na jinsi gani utapenda kulitatua suala hili.

## Talaka ya Nje ya Nchi

**Nilipata talaka yangu nchini Uingereza miezi michache iliyopita. Mimi ni Mtanzania na ningependa kufahamu kama ninatakiwa kuisajili hapa. Ndoa yangu ya kwanza ilifungiwa jijini Dar es Salaam miaka sita iliyopita.**

*6 Aprili 2009*

Sheria yetu za Ndoa iinatambua uamuzi uliopitishwa na mahakama yoyote ya kigeni yenye uwezo kisheria. Talaka iliyotolewa nje ya nchi inakubalika na inaweza kusajiliwa nchini Tanzania bila kujali ni wapi ndoa ilifungwa.

Kuna utaratibu wa msingi unaopasa kufuatwa ili kufanya usajili huo. Maombi kwa ajili ya usajili wa talaka iliyotolewa nje ya nchi unafanyika ofisi ya Msajili Mkuu wa Vizazi na Vifo (RITA). Inashauriwa usajili amri ya talaka mapema iwezekanavyo.

## Nitakufa Mapema ikiwa nitaandaa Wosia

**Familia yetu inaamini kwamba ikiwa utaandika wosia utakufa mapema. Rafiki yangu wa karibu ananishauri kwamba ni muhimu kuwa na wosia. Mnapendekezaje?**

*30 Machi 2009*

Hatuwezi kusema chochote kuhusu imani kuwa mtu atakufa mapema ikiwa ataandika wosia. Tunachoweza kukuambia ni kwamba kuandika wosia ni muhimu. Bila wosia huwezi kudhibiti/kuamua ni nani atarithi mali zako ukifariki. Ikiwa utafariki bila kuandika wosia basi umefariki bila kugawanya mali, na uangalizi wa mali zako utawekwa chini ya msimamizi aliyeteuliwa na mahakama. Tumebaini kwamba hii husababisha migogoro mikubwa, ambayo huweza kuigawa familia.

Rafiki yako amekushauri vyema. Katika dunia ya leo inayobadilika kwa haraka, ni muhimu kwa yeyote aliye juu ya miaka 18 kuandika wosia. Kama umeoa, wote wewe na mkeo mnapaswa kuandika wosia hata kama mali zilizochumwa kwenye ndoa zipo kwa jina la mwenzi mmoja.

Kwa kawaida ungependa kumfanya mwenzi wako kuwa mfaidikaji mkuu kwa kuambatanisha zawadi mbadala ambayo itamnufaisha ikiwa atafariki baada yako.

Kabla ya kuandaa wosia wako, hakikisha kwamba una orodha ya mali zako na jinsi gani unataka mali zako zigawanywe. Utapaswa pia kumteua msimamizi kwenye wosia, ambaye atakuwa na jukumu la kusimamia mali utakapofariki na kugawanya mali kutokana na masharti ya wosia. Mara tu wosia utakapotayarishwa, unabaki kuwa halali hadi utakapofutwa. Tunakushauri kuwa ufanye mapitio ya wosia wako angalau mara moja kila mwaka.

Tumebaini kuwa watu wengi hawaandiki wosia kwa kuwa ni masikini au wana kipato

kidogo. Hata uwe masikini vipi, ni lazima uandae wosia. Kuandaa wosia si ghali na ni rahisi/haraka.

## Msimamizi mpya wa Mirathi anakataa Mauzo ya Zamani

**Mwaka 2004, nilinunua nyumba kutoka kwa msimamizi wa mirathi katika mji mdogo wa Turiani. Mauzo yalifanyika katika ofisi ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, na mmoja wa mashahidi alikuwa Hakimu. Miezi mitatu baadaye, mmoja wa wanafamilia alipinga mchakato uliopelekea uteuzi wake. Msimamizi wa mirathi aliondolewa baada ya kesi. Nilikuwa tayari nimebomoa nyumba ya zamani na kujenga nyumba mpya katika kiwanja hicho. Msimamizi mpya wa mirathi anawatisha mafundi wangu kwamba mimi si mmiliki halali wa mali hiyo, na kwamba kwa kuteuliwa kwake kuwa msimamizi ana haki juu ya mali zote, ikiwa ni pamoja na zilizouzwa. Nifanyeje?**

*9 Machi 2009*

Msimamizi ni mtu aliyeteuliwa na mahakama kusimamia mali za marehemu, majukumu yake makuu kati ya mengine mengi ni kukusanya mali za marehemu, kulipa madeni kama yapo na ugawaji wa mali za marehemu kwa walengwa.

Katika usimamizi wa mali za marehemu, mabadiliko au kuondolewa kwa msimamizi ni jambo la kawaida. Mabadiliko ya msimamizi yanaweza kutokea kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kifo cha msimamizi, kushindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na sababu za kiafya, uzembe au ulaghai au vitendo visivyo vya uaminifu. Ikiwa mojawapo ya haya yatathibitika, mahakama inaweza kuamuru kuondolewa kwa msimamizi.

Hata hivyo, jambo muhimu hapa ni hatma au haki ya mtu baki ambaye anaweza kuwa amefanya jambo/shughuli fulani na msimamizi aliyeondolewa. Kwa maneno mengine, nini nafasi ya masuala/mambo yaliyofanyika kati ya upande wa tatu na msimamizi aliyeondolewa? Je, kuondolewa kwa msimamizi kunaweza kuathiri mambo aliyoyafanya na mtu baki pindi akiwa katika nafasi hiyo? Majibu ya swali hapo juu lazima yawe kinyume/hapana. Kuondolewa kwa msimamizi hakuwezi kubatilisha vitendo au shughuli zilizofanywa naye wakati akiwa katika nafasi ya msimamizi wa mirathi ya marehemu. Hii ni kwa sababu katika kufanya kazi na msimamizi, mtu baki aliamini katika kila hali, alikuwa anafanya kazi na mtu sahihi.

Hata hivyo kuna mazingira fulani adimu ambapo kuondolewa kwa msimamizi kunaweza kukaathiri mambo aliyoyafanya. Moja ya mambo hayo ni pamoja na; baada ya kushika wadhifa huo, msimamizi alijihusisha na vitendo visivyo vya uaminifu au ulaghai na kusababisha hasara kwa walengwa/ wafaidikaji na mali za marehemu. Kwa mfano, msimamizi anapotoa mali za marehemu kwa ndugu zake au yeye mwenyewe kuchukua mapato ya mali za marehemu kwa ajili ya matumizi yake binafsi. Katika hali hiyo, mabadiliko ya msimamizi ni dhahiri kwamba yataathiri pia mambo aliyoyafanya, na kama itabainika kuwa mtu baki ulihusika katika ubadhirifu uliopelekea kuondolewa kwa msimamizi. Katika kesi yako, wewe ni mnunuzi halali kwa kuwa hukushiriki katika ubadhirifu wowote. Ikiwa msimamizi mpya anakutishia wewe au wafanyakazi wako, unaweza kuchukua hatua za kisheria dhidi yake ikiwa ni pamoja na kufungua shauri ili kupata amri ya kudumu ya mahakama ya kuzuia msimamizi mpya kutokuingilia furaha yako ya kumiliki nyumba.

## Wazazi walifariki, Msimamizi anatudaganya

**Mimi ni mtoto mkubwa katika familia yetu. Wazazi wetu walifariki mwaka jana na mjomba wetu aliteuliwa na Mahakama**

**Kuu kuwa msimamizi wa mirathi ya wazazi wetu. Hatunufaiki na mali za wazazi wetu. Tunataka kumwondoa msimamizi wa mirathi kwa udanganyifu. Je, tunaweza kufanya nini juu ya hili?**

*16 Februari 2009*

Hii imetokea kwa watu wengi katika maeneo mengi duniani. Baadhi ya wasimamizi walioteuliwa huangalia maslahi yao binafsi na si waaminifu na hawako wazi katika kutekeleza majukumu yao kama wasimamizi au watekelezaji.

Ili kuondoa au kubatilisha barua ya usimamizi kwa msimamizi (mjomba wako), utapaswa kuthibitisha kwamba si mwaminifu katika shughuli zinazohusu mali/mirathi husika. Utapaswa kuwasilisha maombi kwenye Mahakama Kuu, Mahakama ile ile iliyomteua mjomba wako, ili kusitisha barua ya usimamizi wa mirathi na utatakiwa kuthibitisha tuhuma zilizotolewa. Maombi lazima yawasilishwe kwa njia ya maombi maalum na hati ya kiapo. Kama suala ni la haraka, basi unaweza pia kuambatanisha hati ya dharura ili kuharakisha kusikilizwa kwa maombi yako. Hakikisha kuwa umejiandaa vizuri kuthibitisha madai yako.

## Mama hafahamu Ndoa ya Binti yake wa miaka 16

**Mume wangu aliridhia ombi la ndoa ya binti yetu mwenye umri wa miaka 16 wakati nikiwa kwenye safari ya kibiashara. Nilishtuka niliporejea baada ya kugundua kuwa binti yangu ameolewa. Je, hii ni sawa kisheria?**

*23 Februari 2009*

Ndoa ni muungano wa hiari kati ya mwanamume na mwanamke kwa lengo la kuwa pamoja kwa maisha yao yote. Ndoa hufungwa kwa ridhaa ya pande mbili zinazokusudia kuoana. Kwa sheria zetu, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, mtu haruhusiwi kuoa msichana ambaye hajatimiza umri wa miaka 15 labda kuwe na sababu maalum. Hata hivyo, binti yako ana miaka 16 ambayo kisheria anaruhusiwa kuolewa. Hata hivyo, kuoa msichana ambaye ametimiza umri wa miaka 16 au zaidi lakini ikiwa hajatimiza umri wa miaka 18, Sheria inasema kwamba anapaswa pia kupata ridhaa ya baba yake. Kama baba amefariki apate ridhaa ya mama, na kama mama pia amefariki unaweza kupata ridhaa ya mlezi wake.

Ikiwa binti yako aliridhia ndoa kwa hiari na uhuru, na kwa kuwa baba pia alikubali, makubaliano hayo ya ndoa hayawezi kupingwa.

Ikiwa binti yako alilazimishwa kuolewa na hivyo ridhaa ilipatikana kwa njia ya udaganyifu au kwa kutumia nguvu, makubaliano hayo ya ndoa yanaweza kupingwa.

Unahitaji kuzungumza na binti yako mara moja na kujua kama alikubali kuolewa. Kama alilazimishwa kuolewa, unaweza kuwasilisha maombi ya kubatilisha ndoa.

## Mume anampiga Mkewe

**Nimeolewa na ninaishi na mume wangu hapa Kigoma. Tangu tufunge ndoa yetu mwezi wa sita mwaka 2007, mume wangu amekuwa akinipiga sana na ninahisi kwamba siwezi kuendelea kuishi naye tena. Je, ninaweza kumpa talaka?**

*19 Januari 2009*

Kisheria, kumpiga mkeo ni ukatili na ni sababu nzuri ya kuomba talaka. Hata hivyo, Sheria ya Ndoa hairuhusu wanandoa kupeana talaka kama ndoa haikudumu angalau kwa miaka miwili. Chaguo ulilonalo ni kuomba mahakama ikupe kibali cha kufungua kesi ya kuomba talaka kabla ya miaka miwili iliyoainishwa kisheria. Hata hivyo, kabla ya kwenda mahakamani kwa ajili ya kuwasilisha maombi ya kuruhusiwa kufungua kesi ya kuomba talaka, sheria inakutaka kupeleka

mgogoro huo kwenye Baraza la Usuluhishi wa Ndoa ambalo litakuita wewe na mumeo na kujaribu kuwapatanisha. Kama Baraza litashindwa litatoa hati yenye kutoa mapendekezo.

Wakati kibali kimetolewa utatakiwa kuwasilisha maombi ya talaka mahakamani ukiambatanisha na hati kutoka Baraza la Usuluhishi. Ombi linaweza kuwasilishwa katika mahakama yoyote kama vile Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama Kuu.

Ili mahakama ipitishe amri ya talaka ni lazima kuridhika kwamba ndoa imevunjika na haiwezi kusuluhishika. Baadhi ya sababu zinazoonesha hivyo ni kuwepo kwa uzinzi, hamu ya kufanya ngono iliyokubuhu, ukatili, kutelekeza, kifungo cha maisha au kwa muda wa zaidi ya miaka mitano, ugonjwa wa akili ulio thibitishwa angalau na madaktari wawili au kubadilisha dini kwa upande wowote.

Katika ombi lako, unaweza pia kuomba mambo mengine kama vile uangalizi wa watoto, kama wapo, na matunzo kwa ajili yako mwenyewe na watoto.

## Mvutano wa Uangalizi wa Mtoto

**Ni vigezo gani mahakama huzingatia kabla ya kuamua mtoto mchanga awekwe chini ya uangalizi wa nani? Kijana wangu ana umri wa miezi 12.**

*26 Januari 2009*

Kanuni ya msingi ni ustawi wa mtoto. Kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa, kabla ya kuamua juu ya uangalizi wa mtoto, mahakama huzingatia sababu kadhaa ambazo baadhi yake ni: umri wa mtoto, tabia ya wazazi (mfano, ukahaba au ulevi), matakwa ya mtoto ikiwa ana umri ambao unamruhusu kuweza kutoa maoni yake binafsi, kipato na matakwa ya wazazi. Kama una akili timamu, tabia nzuri, na kipato cha kuweza kumtunza mtoto, na kwa vile mtoto yupo chini ya umri wa miaka saba, kuna uwezekano mkubwa kwamba mahakama itakupa uangalizi wa mtoto kama Sheria ya Ndoa inavyotamka wazi kuwa ni vizuri kwa mtoto mdogo chini ya umri wa miaka saba kuwa chini ya uangalizi wa mama yake.

# Migogoro ya Kazi

> **Vile unavyowafanyia wafanyakazi wako ndivyo watakavyokufanyia.**

Mara nyingi uelewa wa sheria ya ajira ni changamoto kubwa. Dhana potofu, tafsiri potofu na utata kwa kawaida hutufanya kutafuta ushauri na ufafanuzi kutoka kwa mwajiri na mwajiriwa. Sura hii inatoa ufafanuzi juu ya baadhi ya masuala ya ajira na sheria za kazi. Sheria hizo zinaweza kutekelezwa au zisitekelezwe katika maeneo ya kazi, hata hivyo kama kuna mgogoro wa kazi, sheria ya kazi itatumika na mara nyingi sheria humpendelea mfanyakazi. Kutokujua sheria si utetezi. Fahamu haki zako za kisheria; fahamu haki za mfanyakazi na za mwajiri. Itakusaidia kuokoa muda na pesa za kampuni/taasisi yako.

## Kulipwa kama Mtaalamu wa Kigeni

**Nilizaliwa nchini Tanzania lakini nimeishi nchini Norway kwa kipindi cha miaka kumi na tano. Nilikuja kutembelea Tanzania baada ya miaka kumi na kupapenda. Niliamua kufanya maombi tena ya hati yangu ya kusafiria (pasipoti) ya Tanzania ambayo niliipata ndani ya siku saba. Kwa sasa nimepata kazi kwenye kampuni ya ushauri na ninataka kuomba kibali cha kufanya kazi ili nilipwe kama mtaalamu wa kigeni. Je nifanye nini?**

*7 Aprili 2011*

Kwa sheria zetu kitendo chako cha kuomba hati ya pili ya kusafiria ni kinyume cha sheria na unaweza kushtakiwa. Kwa sasa, Tanzania hairuhusu raia wake kuwa na uraia wa nchi mbili. Kuomba kibali cha kufanya kazi ilihali ukiwa raia wa Tanzania ni kinyume cha sheria pia. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kusamehewa kuchangia NSSF

**Mimi ni mfanyakazi niliyeajiriwa na kampuni tanzu nchini Uingereza. Kwa sasa ninafanya kazi na kulipwa Tanzania. Ninachangia kwenye mfuko wa pensheni wa nchini kwangu lakini Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) unaitaka kampuni yangu kulipa michango ya pensheni kwa mujibu wa sheria. Nifanye nini?**

*7 Mei 2011*

NSSF inasimamiwa na Sheria ya NSSF. Katika Sheria hii, mfanyakazi anafafanuliwa kama mtu ambaye ana mkataba wa ajira na ameajiriwa Tanzania bara.

Kanuni ya kawaida ya pensheni ni kuwa 'mtu, yaani mstaafu, hatanufaika mara mbili na pensheni' inahusika hapa. Lazima ukumbuke kwamba pensheni ni fedha yako inayowasilishwa NSSF kwa mujibu wa sheria ili wewe unufaike wakati wa kustaafu. Kwa kuwa wewe tayari umejiunga katika mpango wa pensheni wa nchi yako, unaweza kutuma maombi NSSF ili uondolewe/usamehewe kwenye mpango wao. Kama mpango wa pensheni wa nchini kwako ni sawa na mpango wa NSSF, unaweza kuondolewa kwenye mfuko wa pensheni nchini. Vinginevyo utatakiwa kuchangia NSSF, na kampuni yako ikishindwa kufanya hivyo inaweza kufunguliwa kesi ya jinai.

## Kufukuzwa Kazi kwa sababu ya Facebook

**Niliajiriwa kama karani katika moja ya benki jijini Dar es Salaam. Miezi michache iliyopita kulikuwa na ujumbe mfupi uliotumwa na uongozi kwamba haturuhusiwi kutembelea mitandao yoyote ya kijamii kama vile Facebook na Twitter. Baada ya wiki kadhaa, nilionekana nimetembelea mtandao wa Facebook, bosi wangu alinionya kwa maneno. Wiki chache baadaye mkuu wangu wa idara pia aliniona nimetembelea mojawapo ya mitandao hii, na alitoa taarifa kwa Meneja Rasilimali Watu. Meneja wa Rasilimali Watu aliitisha kikao cha nidhamu na siku tatu baadaye nilifukuzwa kazi. Mojawapo ya sababu ilikuwa ni maoni yangu niliyoyatuma kwenye mtandao kuhusiana na mwajiri wangu na sehemu yangu ya kazi. Je, hii ilikuwa sawa kisheria? Ninafikiri hii haikuwa sawa kwa sababu niliingia tu kidogo kwenye mtandao wa Facebook na utendaji wangu wa kazi haukuwa mbaya kabisa.**

*21 Februari 2011*

Tunasikitika na wewe kwa kupoteza kazi yako. Ingawa hatusikitishwi na sababu zilizopelekea kufukuzwa kazi.

Sheria ya ajira ya Tanzania inasema kuwa kusitishwa kwa ajira ya mfanyakazi kutaamuliwa kama ni sawa au la baada ya kupima sababu na taratibu zilizotumika kusitisha ajira husika. Kipimo hiki mara nyingi

hutegemea hali au mazingira husika.

Inaonekana kwamba uliwahi kupewa onyo kuhusu kutembelea mtandao wa Facebook wakati wa kazi. Zaidi ya hayo, mwajiri wako alitoa nafasi ya kukusikiliza kabla ya kukufukuza, hivyo alifuata utaratibu sahihi.

Hata kama mitandao ya kijamii kama vile Facebook ni mipya nchini Tanzania, wakati wowote inapokuwa inaingilia kazi unayofanya, unaweza kuachishwa kazi. Kitendo chako cha kuweka maoni yako kwenye ukurasa wako wa Facebook kuhusu sehemu yako ya kazi na mwajiri kinaweza kuwa sababu ya kuachishwa kazi pia.

Waajiri wengi hawaruhusu matumizi ya mtandao wa Facebook mahali pa kazi, kwani matumizi ya Facebook ni uraibu na huathiri umakini wa mfanyakazi husika, na kusababisha utendaji mbovu kazini. Kwa mtazamo wa kawaida, sisi binafsi tunafikiri kuwa mwajiri alikuwa sahihi kusitisha ajira yako. Hata hivyo, unapaswa kuwasiliana na wanasheria wako, ambao wanaweza kukusikiliza na kutoa ushauri na mwongozo zaidi.

## Aina ya Vibali vya Kazi

**Nina nia ya kuwekeza nchini Tanzania, hivyo napenda kujuzwa ugumu uliopo katika kupata kibali cha uhamiaji. Je, kuna aina ngapi za vibali hivyo, na nitaanzia wapi kufuatilia? Ikiwa nataka kuajiriwa kama mtaalamu wa kigeni, nifanyeje?**

*7 Februari 2011*

Kuna aina tatu za vibali vya ukaazi. Kwa sasa vibali hivi hushughulikiwa chini ya sheria mbili tofauti. Hata hivyo, jibu la swali inabidi liwe chini ya sheria iliyokuwepo mwaka 2011, ambavyo hutolewa kwa mtu yeyote anayetaka kufanya biashara, kazi, au lengo lolote linalokubalika kisheria nchini Tanzania. Navyo ni Daraja A, kwa wageni waliojiajiri (wawekezaji), Daraja B, kwa wageni waliopata ajira nchini Tanzania, na Daraja C, kwa makundi mengine ya wageni kama vile waeneza-dini/wamisionari, wanafunzi au wafanyakazi wanaojitolea.

Mkurugenzi wa Idara ya Uhamiaji ndiye mwenye mamlaka ya kutoa kibali cha ukaazi. Waombaji ambao hawataridhishwa na uamuzi wa Mkurugenzi wanaweza kukata rufaa kwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

Kama mwekezaji mtarajiwa, lazima uombe kibali Daraja A, na utapaswa kuwa na cheti kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), barua ya utambulisho, wasifu binafsi, vyeti vya elimu (kama vinahitajika), Hati ya usajili wa kampuni, Kanuni na Mwongozo wa Kampuni, uthibitisho wa ofisi/makazi ya kampuni, kibali (idhini) cha kisekta kutoka wizara yoyote husika (ikiwa kinahitajika), cheti cha hisa, na nakala ya hati ya kusafiria (pasipoti) kuthibitisha utaifa na uhalali wa pasipoti.

## Mkurugenzi wa Kampuni

**Niliajiriwa katika nafasi ya ukurugenzi wa kampuni inayojihusisha na kilimo. Kwa miaka kumi iliyopita, faida yote iliyopatikana ilibakizwa na kuwekezwa tena katika biashara. Mnamo Januari 2010, kampuni ilitangaza gawio kutokana na faida, lakini sikupewa gawio kama mkurugenzi wa kampuni. Nifanyeje?**

*10 Januari 2011*

Kama mkurugenzi una haki ya kulipwa mshahara/ujira wa ukurugenzi kama ilivyokubaliwa. Wewe si mbia/mwanahisa wa kampuni, hivyo hauna haki ya kupata gawio. Tuna wasiwasi kuwa unachanganya kuwa mkurugenzi wa kampuni na kuwa mwanahisa. Hata hivyo, kuna baadhi ya makampuni ambayo wakurugenzi ni wanahisa pia.

Kwa upande wako, labda kwa sababu ya sifa zako za kitaaluma au mahusiano yako na wajumbe wengine au wakurugenzi wa kampuni hiyo, umechaguliwa kuwa

mkurugenzi wa kampuni na haumiliki hisa zozote. Hatuoni chochote kibaya kuhusu msimamo wa kampuni dhidi yako.

## Kipengele cha Mkataba kinachomkataza Mfanyakazi Kuajiriwa 'kwingine'

**Nilimwajiri, kumfundisha kazi na kumpandisha cheo rubani wa ndege kwa maelewano/masharti kuwa hawezi kufanya kazi na kampuni nyingine yoyote ya usafiri wa anga (ndege) kwa kipindi cha miaka mitano. Hivi karibuni amenipa notisi/barua ya kuacha kazi ndani ya miezi mitatu. Nimeshindwa kumshawishi asiondoke. Je, naweza kumzuia kufanyakazi katika kampuni nyingine za ndege?**

*30 Novemba 2010*

Hii inategemea na maneno halisi yaliyotumiwa kwenye mkataba/kifungu husika. Hata hivyo, kifungu cha mkataba kinachomzuia mwajiriwa 'kutokufanya kazi na mashirika mengine ya ndege' kwa miaka mitano si cha kiungwana. Kama suala hili litafika mahakamani, hoja ya mfanyakazi wako itakuwa 'unatarajia atapata wapi ujira/mapato katika kipindi chote cha miaka mitano ambayo hatokuwa na ajira?' Jiweke katika nafsi yake – hudhani kuwa kifungu hiki cha mkataba ni kikwazo/tata na si cha kiungwana? Huwezi kutarajia rubani aache kurusha ndege na aanze kuendesha daladala kwa sababu tu aliingia kipumbavu katika mkataba wa ajabu na wewe, labda kwa kutokuelewa, kujua na pengine kwa sababu ya mfadhaiko/kukata tamaa.

Kama una makubaliano naye ya mkopo wa elimu na anatakiwa arejeshe kwa kukatwa mshahara, unaweza kumshitaki kupitia mkataba wa mkopo na kudai kiasi ulichomkopesha. Huwezi kumzuia kufanya kazi mahali pengine. Kipengele hicho kinazuia kufanyika biashara/kazi, kwa maoni yetu, hakuna mahakama inayoweza kukubaliana na hilo.

## Sheria za Kazi hazitendi Haki kabisa

**Mimi ni mwekezaji wa kigeni, niko hatua za mwisho kufungua kiwanda Magharibi mwa Tanzania. Nimefahamishwa na wanasheria wangu kwamba Tanzania huwezi tu kumwachisha kazi mwajiriwa. Je, hii inamaanisha kuwa wafanyakazi wangu wana mikataba ya kazi ya maisha? Je, ni kweli pia kuwa kuna mlolongo mrefu na mgumu katika kutatua kesi katika Mahakama ya Kazi?**

*15 Novemba 2010*

Si kweli kwamba wafanyakazi wana mikataba ya kazi ya maisha nchini Tanzania. Baada ya uwepo wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, kumewekwa utaratibu maalum wa kusitisha ajira za wafanyakazi wako.

Huwezi tu kuamka siku moja bila sababu ya msingi au vigezo, ukasitisha ajira za wafanyakazi wako.

Ni bora kuwa na mkataba wa kipindi maalum wenye kipengele cha kusitisha ajira mara tu baada ya muda huo kufikia kikomo. Unaweza, kwa kuamua mwenyewe, kuwapa tena mikataba na kwa jinsi hii utaweza kulinda maslahi yako.

Kuna miongozo ya wazi ambayo inaonesha ni kwa jinsi gani mfanyakazi anaweza kuacha au kuachishwa kazi. Kama mfanyakazi amefanya kosa kubwa la utovu wa nidhamu, hii ni sababu tosha ya kusitisha ajira, lakini unapaswa kufuata taratibu zilizowekwa ikiwa ni pamoja na kumpa mwajiriwa nafasi ya kujitetea/kusikilizwa. Kama utaratibu haukufuatwa, inaweza kuwa ni sababu kwa mfanyakazi kudai kuwa ameachishwa kazi kimakosa katika ngazi inayofuata.

Inaonekana kama ukiajiri watanzania unakuwa mtumwa. Hivyo sivyo – ingawa

wengi wanadai kuwa sheria inapendelea wafanyakazi, lakini ni kweli pia kuwa kuna ulinzi wa kutosha kwa waajiri. Suala la msingi ni kuhakikisha kuwa unafuata utaratibu sahihi unapositisha ajira.

Kuhusu kesi mahakamani, ni kweli kwamba kuna kesi nyingi katika Mahakama ya Kazi ikiwa ni pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi. Wafanyakazi wametambua haki zao, cha kusikitisha, waajiri wameendelea kukiuka sheria na kusitisha ajira bila kuzingatia taratibu. Wakati mwingine tunahisi kuwa waajiri ama hawaelewi sheria au hawajazisoma tu.

## Athari za Kisheria za kuondoa Sehemu ya Madai

**Mwaka 2008 niliachishwa kazi na mwajiri wangu kinyume cha sheria na nilifungua kesi. Baada ya kusikilizwa kwa muda mrefu, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ilinitendea haki na kutoa malipo ya kutokupewa notisi, malipo ya likizo, mkono wa kwaheri/kiinua mgongo, n.k. Kiasi chote ni shilingi milioni 3.5. Mwajiri alitekeleza amri na nililipwa ipasavyo. Hivi karibuni niligundua kwamba sikudai malipo ya muda wa ziada, ambayo ni shilingi 800,000. Ni utaratibu gani ninaweza kufuata kupata malipo yangu ya muda wa ziada? Tafadhali nishauri ipasavyo.**

*8 Novemba 2010*

Ni kwa faida ya utoaji haki kuwa mgogoro siku moja ufike mwisho. Wadai ni lazima wadai stahiki zao zote, labda wawe wamesamehe/wameacha kwa hiari kuzidai. Katika kesi yako, ulipaswa kudai malipo ya ziada katika madai ya awali kwa sababu kwa sehemu kubwa ni jambo hilo hilo. Sheria ipo wazi, kama mtu anachagua kudai sehemu ya madai na wakati huo huo sehemu nyingine ya madai inayotokana na madai hayo hayo ya msingi ikaondolewa au kuachwa, sehemu iliyoondolewa au kuachwa kwa hiari, kwa kawaida, haiwezi kudaiwa baadaye. Kuna uwezekano kwamba, sehemu ya madai iliyobaki hairuhusiwi tena kisheria chini ya kanuni 'inayokataza kufunguliwa upya kwa shauri ambalo limeshasikilizwa na kutolewa uamuzi na mahakama'(res judicata).

## Bosi wangu analipwa mara Kumi ya Mshahara wangu

**Nilirudi kutoka Ulaya miaka miwili iliyopita na nimekuwa nikifanya kazi kama Katibu Muhtasi kwenye kampuni ya madini Mwanza. Wiki chache zilizopita niliweza kuangalia orodha ya malipo ya kampuni na kugundua kwamba bosi wangu, ambaye si mwerevu kama anavyodhani, hulipwa mara kumi ya mshahara wangu. Je, huo si ubaguzi? Inawezekanaje mtu mmoja kulipwa kiasi kikubwa kama hicho? Je, ni jinsi gani ninaweza kufungua shauri dhidi ya kampuni?**

*4 Oktoba 2010*

Hakuna sheria nchini Tanzania ambayo inaweka kiwango cha juu cha malipo ya bosi/mtendaji katika sekta binafsi. Umedai kuwa umewahi kuishi Ulaya, basi ulipaswa kujua hilo. Haijalishi kuwa bosi wako ni mwerevu au la, kama anavyofikiri au kuonekana. Kama unalipwa juu ya kima cha chini cha mshahara, kampuni ya madini haivunji sheria yoyote.

Ni muhimu tukaongeza jambo moja zaidi – kitendo chako cha kuangalia kinyemela orodha ya malipo ya mishahara kinaweza kusababisha kufukuzwa kazi. Tafadhali zingatia hilo.

## Ajira kwa Mtu mwenye Ulemavu

**Nimekuwa mlemavu tangu utotoni kutokana na kuathiriwa na ugonjwa wa polio/kupooza. Nimekulia Kigoma, alafu nikahamia Moshi na baadaye Dar. Katika kipindi chote cha maisha yangu, kumekuwa hakuna vifaa/sehemu maalum kwa ajili ya walemavu. Kigoma na Moshi, nilikuwa**

**nabebwa kupelekwa shule na ofisini kwa kuwa majengo hayo hayakuwa na sehemu maalum za kupitia walemavu. Dar es Salaam, ijapokuwa kuna majengo mapya, bado hakuna tofauti. Je, hakuna sheria ambayo inailazimisha tasnia ya ujenzi kuzingatia uwepo wa miundombinu kwa ajili ya walemavu? Swali langu la pili linahusu ubaguzi wa kazi kwa watu wa aina yangu. Tunalipwa kidogo, tunanyanyaswa na mara nyingi hatuajiriwi. Je, ni nani anatulinda?**

*30 Agosti 2010*

Umeuliza maswali muhimu sana. Kwa bahati mbaya, majengo ya zamani bado hayana sehemu maalum ambazo zinapitika kirahisi na watu wenye walemavu.

Sheria mpya imepitishwa na bunge – Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya 2010. Sheria hii imetatua baadhi ya dukuduku zako.

Sheria iko wazi kwamba watu wote wenye ulemavu wanastahili mazingira rafiki yenye nyenzo rafiki ili kuwawezesha kufika sehemu za umma kwa ajili ya huduma za jamii, barabara na mawasiliano. Sheria inaeleza zaidi kwamba wasanifu majengo, wakandarasi na watu wengine wote wnaohusika katika usanifu na ujenzi wa majengo wanapaswa kuzingatia suala la ufikikaji ili kuhakikisha kwamba majengo yote mapya, barabara, viwanja vya michezo, miundombinu ya usafiri na uboreshaji wa majengo ya zamani, yanasanifiwa kwa lengo la kuwa na sehemu maalum za kupitia walemavu. Chini ya sheria hii, ni kosa kwa mtu mwenye ulemavu kunyimwa haki ya kufika/kutumia kwa urahisi majengo ya umma.

Kuhusu suala la ubaguzi kwenye ajira kwa mtu mwenye ulemavu, sheria inasema kwamba hili ni kinyume cha sheria na ni kosa na linaadhibiwa kwa faini, kufungwa jela au vyote kwa pamoja. Kwa ufupi, mwajiri au mwajiri mtarajiwa yoyote ambaye anambagua mtu kwa sababu ya ulemavu anaweza kuishia jela.

## Kazi bila Mkataba

**Nimekuwa nikifanya kazi kwenye kampuni iliyosajiliwa hapa nchini kwenye sekta ya kilimo. Tangu nilipoanza kufanya kazi, sijawahi kusaini mkataba wa ajira. Huu ni mwaka wangu wa saba katika kampuni, na hivi karibuni nilipokwenda kuomba mkataba wangu walinitilia mashaka sana. Tafadhali naomba ushauri.**

*24 Mei 2010*

Swali lako linavutia sana – je, umeajiriwa na kampuni ambayo umekuwa ukifanyia kazi? Jibu ni ndiyo. Kutokuwa na mkataba haina maana kwamba hufanyi kazi kwenye kampuni hiyo au hauna haki dhidi ya mwajiri wako. Sheria inakutizama kama mfanyakazi, na unapaswa kupata haki sawa na mwenzako aliye na mkataba. Ikiwa utafukuzwa kazi utapewa stahiki zako zote kwa mujibu wa sheria.

## Uhamisho wa Mwajiriwa

**Nimeajiriwa kwenye kampuni binafsi yenye matawi mikoa mbalimbali Tanzania. Wakubwa wangu wa kazi wamenihamishia Kusini mwa Tanzania. Sijapinga, lakini nataka mke wangu na watoto niondoke nao. Tatizo linalonikabili ni kwamba, kama mke wangu ataungana nami, atapoteza kazi yake. Je, mwajiri wangu pia anapaswa kumtafutia kazi mke wangu?**

*3 Mei 2010*

Ingawa tunasikitishwa pia na athari ulizozipata baada ya kuhamishiwa kituo kipya cha kazi, tuna maoni thabiti kuwa mwajiri hana jukumu lolote kisheria kumtafutia kazi mkeo. Haitakuwa na maana/tija kibiashara kama sheria itamtaka mwajiri kufanya hivyo.

Kwa kuzingatia wewe kukubaliana na uhamisho huo, mkeo kupoteza ajira ni suala la kifamilia ambalo mnahitaji kulitatua kifamilia. Hata hivyo, mwajiri anapaswa kulipia gharama

za uhamisho wako kwenda kituo kipya cha kazi.

## Kuchelewa Kazini

**Kampuni yangu ni mojawapo ya washiriki/wadau wakubwa katika sekta ya kilimo nchini Tanzania. Nimebaini wafanyakazi wangu wengi hawafiki kazini kwa muda uliopangwa au kwa kudai kuwa wanaumwa. Wafanyakazi wanaochelewa, wanadai kuwa wanategemea huduma ya usafiri ambayo si ya uhakika, hivyo huchelewa kazini. Nimefukuza baadhi ya wafanyakazi na sasa wamenipeleka mahakamani. Je, hii inaruhusiwa? Je, sheria haininiruhusu kuwafukuza kazi wanaochelewa au watoro kazini?**

*15 Machi 2010*

Haijalishi kama wewe ni mshiriki/mdau mkubwa au mdogo. Sheria inafanya kazi kwa wote na huwezi kumzuia mtu kwenda mahakamani. Tunaungana na wewe kusikitika juu ya utoro - ijapokuwa ili ufukuze mfanyakazi kuna taratibu ambazo sheria imeeleza na zinapaswa kufuatwa.

Kwa wale wafanyakazi wanaochelewa, ni lazima waonywe kwa tabia zao na kama tabia hizi hazikomi, unapaswa kuwapa barua ya onyo ikielezea malalamiko yako. Kama tabia hii haibadiliki, unapaswa kuitisha kikao cha kamati ya nidhamu na kuwapa angalau masaa 48 kujiandaa kwa ajili ya kikao hicho. Katika kikao hicho, mwajiriwa anaweza kuja na mwakilishi kutoka chama cha wafanyakazi au mwajiriwa mwenzake. Kumbukumbu za kikao hicho lazima ziandikwe, kutokana na mwajiriwa kupewa nafasi ya kusikilizwa na akatoa sababu ambazo hazikuridhishi unaweza kumfukuza kazi. Tafadhali kumbuka kwamba huwezi kumfukuza kazi mfanyakzi bila kufanya kikao hiki na kufuata taratibu zilizoainishwa hapo juu.

Kuhusu likizo ya ugonjwa, tafadhali tambua kwamba mfanyakazi anapodai likizo ya ugonjwa lazima aonyeshe cheti/hati ya matibabu kutoka kwa daktari ambaye unaweza kumteua au unamkubali. Bila hati ya matibabu, mfanyakazi hawezi kudai likizo ya ugonjwa na unaweza kuendelea kufuata taratibu kumuachisha kazi kama ilivyobainishwa hapo juu.

## Mfanyakazi Mgonjwa

**Nilikuwa na majeraha ya mgongo na sikuwa kazini kwa muda wa miezi mitatu. Niliambiwa nipumzike na kuondoa msongo wa mawazo. Mwajiri wangu alisisitiza kwamba kwa kuwa mimi ni mtaalamu wa programu za kompyuta, naweza kufanya kazi nikiwa kitandani ili kuondoa msongamano wa majukumu. Nilikataa kutokana na ushauri wa daktari. Baada ya kuruhusiwa kutoka hospitali, niliporejea kazini nilikuta taarifa za kuachishwa kazi. Dawati langu limeondolewa vitu na mhudumu wa mapokezi ameelekezwa kunizuia nisiingie. Niliaibika sana. Je, nifanye nini?**

*22 Februari 2010*

Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004 iko wazi sana juu ya likizo ya ugonjwa - mfanyakazi ambaye atatoa cheti/hati ya matibabu kutoka kwa daktari ambaye amesajiliwa na anayekubaliwa na mwajiri, ana haki ya likizo ya ugonjwa, na mgonjwa ana haki ya kulipwa mshahara wake kamili kwa siku sitini na tatu za kwanza na nusu mshahara baada ya siku sitini na tatu za pili. Katika tukio lako, ulikuwa na haki ya kupata mshahara kamili wakati ulipokuwa hospitali - huhitaji kufanya kazi ili ulipwe kwani una likizo ya ugonjwa, isipokuwa kama mwajiri wako hakupewa taarifa. Kuhusu kuachishwa kazi, ikiwa mwajiri wako alijua juu ya ugonjwa wako, huwezi kufukuzwa kazi kwa sababu zilizotajwa katika swali lako na unaweza kuendelea kulifuatilia suala hilo.

## Kukosana na Bosi wangu

**Nimekuwa nikifanya kazi kwenye kampuni kwa miaka mingi. Hivi karibuni, nimekosana na bosi wangu na anaendelea kunipa kazi ngumu. Kwa mazingira hayo, utendaji wangu wa kazi umeshuka na nimelazimishwa kujiuzulu. Je, haki zangu ni zipi? Miezi michache iliyopita kampuni hiyo pia iliendesha zoezi la kupima afya ambapo wafanyakazi walipimwa VVU/UKIMWI pia. Mmoja wao alionekana kuwa na virusi na aliondolewa kimya kimya. Sheria inamlindaje mtu huyu?**

*15 Februari 2010*

Kanuni za Ajira na Mahusiano Kazini (Kanuni za Utendaji Bora) TSN 42 zinasema wazi kuwa pale ambapo mwajiri anatengeneza mazingira ya kufanya kazi yasivumilike, na hivyo kusababisha mfanyakazi kujiuzulu, kujiuzulu huko ni sawa na kulazimishwa kuacha kazi. Labda kama kuna kitu hukutueleza, kesi yako ni ya aina hii na una sababu za msingi kupeleka malalamiko yako kwenye Tume ya Usuluhishi na Uamuzi. Una nafasi nzuri ya kufanikiwa.

Kanuni hizo pia hutumika kumlinda mtu ambaye ana virusi vya UKIMWI kwa kutamka kuwa hakuna ajira ambayo itasitishwa kwa misingi ya mtu kuwa na virusi vya UKIMWI. Na inaenda mbali zaidi na kusema kwamba wafanyakazi walioathirika na virusi vya UKIMWI wataendelea kufanya kazi chini ya taratibu za kawaida za ajira zao ikiwa wako sawa kiafya kufanya hivyo. Mwajiri amemwachisha kazi mfanyakazi aliyeathirika na UKIMWI kinyume cha sheria, na anaweza kuchukuliwa hatua za kisheria tulizopendekeza kwako.

## Kuachishwa Kazi sababu ya VVU

**Ninafanya kazi kwenye kampuni ambayo inatengeneza viatu. Hivi karibuni, kampuni hiyo imeanza kuwapima wafanyakazi wake VVU/UKIMWI na kisha kuwaachisha kazi baadhi ya wafanyakazi kimya kimya. Ninaamini ni kwa sababu ya kupatikana na mambukizi ya virusi vya UKIMWI. Je, ufukuzaji huu kazini ni halali?**

*14 Desemba 2009*

Ajira ya mtu haiwezi kusitishwa tu kwa misingi ya hali yake ya maambukizi ya VVU/UKIMWI. Mfanyakazi mwenye VVU/UKIMWI, ni kama wafanyakazi wengine anaruhusiwa kufanya kazi chini ya masharti ya kawaida, ilimradi tu yupo sawa kiafya kufanya kazi. Kama hali ya mfanyakazi ni mbaya na mfanyakazi hawezi kuendelea na kazi, kuna mambo ambayo mwajiri anapaswa kuzingatia kabla ya kuamua hatma ya mfanyakazi. Kumuachisha mtu kazi kienyeji kwa misingi ya hali yake ya VVU/UKIMWI ni ubaguzi dhidi ya mwajiriwa na ni kinyume cha sheria na kosa la jinai chini ya sheria.

Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini namba 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya VVU na UKIMWI (Kinga na Udhibiti), Namba. 28 ya 2008 zinazuia vitendo, sera au tabia yoyote ya mwajiri ambayo inanyanyapaa au kubagua kwa njia yoyote ile mwajiriwa kwa kuwa na, kudhaniwa au kuhisiwa kuwa ana VVU/UKIMWI.

Kwa mfano, chini ya Sheria ya VVU na UKIMWI (Kinga na Udhibiti), imetamkwa kuwa mtu yeyote ambaye anamnyanyapaa au kumbagua kwa namna yoyote mtu mwenye VVU/UKIMWI anatenda kosa na anawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili au kifungo kisichozidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

Katika kesi uliyosema, ikiwa waajiriwa wenzako watafukuzwa kazi kwa sababu ya hali zao za VVU/UKIMWI, wanaweza kutoa taarifa polisi na kwenye kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa msaada na mwongozo zaidi. Kama ilivyoelezwa katika sheria, ni kosa ambalo mwajiri wako anaweza kufungwa.

## Kuajiri Msichana mwenye Umri wa miaka 14 kama Mfanyakazi wa ndani

**Nina msichana wa kazi ambaye ana umri wa miaka 14. Mmoja wa marafiki zangu alikuja nyumbani kwangu na kuniambia kwamba ni kinyume cha sheria kumwajiri mtoto wa umri huo. Ninafahamu watu wengine wengi ambao wana wasichana wa kazi wenye umri mdogo kuliko hata wangu. Je, ninavunja sheria?**

*19 Octoba 2009*

Ajira za utotoni ni suala la haki za binadamu na lenye unyeti mkubwa. Ajira za utotoni ni kitendo cha kumwajiri mtoto chini ya umri fulani uliowekwa kisheria. Kitendo hicho huchukuliwa kama unyonyaji na Umoja wa Mataifa na mashirika mengine ya kimataifa, pia ni kinyume cha sheria katika nchi nyingi ikiwemo Tanzania.

Mfuko/Shirika la Watoto Duniani (UNICEF) linakadiria kwamba takribani watoto milioni 158 wenye umri wa miaka 5-14 wapo katika ajira za utotoni – hii ni sawa na mtoto mmoja katika kila watoto sita duniani. Mamilioni ya watoto wameajiriwa katika shughuli hatarishi kama vile kwenye migodi, viwanda vya kutengeneza kemikali na madawa ya kuulia wadudu mashambani (kilimo) au wanasimamia mitambo hatari. Wapo kila mahali wakitumika kama wafanyakazi wa majumbani, wamefichwa ndani ya kuta za karakana na mashambani lakini hawaonekani. Kusini mwa Jangwa la Sahara karibu kila watoto watatu, mmoja wao yuko katika ajira za watoto, na kuwakilisha watoto milioni sitini na tisa.

Umri wa chini ambao binadamu anaweza kufanya kazi hutofautiana kutoka nchi moja kwenda nyingine. Hapa Tanzania chini ya sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004, mtoto ni mtu aliye chini ya umri wa miaka 14 na kwa madhumuni ya ajira kwenye sekta hatarishi, mtoto maana yake ni mtu aliye chini ya umri wa miaka 18. Chini ya sheria hii, ni marufuku kwa mtu kuajiri mtoto chini ya umri wa miaka 14 isipokuwa anaweza tu kuajiriwa kufanya kazi nyepesi ambazo hazina uwezekano wa kudhohofisha afya na maendeleo yake; na haziathiri mahudhurio yake shuleni, kushiriki katika programu ya ufundi au mafunzo yaliyothibitishwa na mamlaka mahsusi. Kuajiri mtoto kwa kukiuka sheria iliyotajwa hapo juu ni kosa.

Kwa hiyo, kama mfanyakazi wako wa ndani haudhurii shule, kumwajiri ni kinyume cha sheria.

## Umri wa kustaafu Sekta binafsi

**Kampuni yangu inataka kumstaafisha afisa mwandamizi ambaye amekuwa akifanya kazi nasi kwa kipindi cha miaka ishirini na tano sasa. Je, kuna umri wa kustaafu ambao ninatakiwa kufuata? Nimeambiwa kwamba siwezi kumwondoa kwenye ajira kwa sababu ya umri.**

*5 Octoba 2009*

Ni wazi mnataka kumuachisha kazi kwa sababu ya umri. Tunachukulia kwamba mpo kwenye sekta binafsi ambayo haina umri wa kisheria kustaafu. Pia hakuna sheria ambayo inasema kwamba huwezi kumstaafisha mfanyakazi – kwa hiyo taarifa uliyonayo si sahihi.

Kama mkataba wenu una umri wa kustaafu, huo unakuwa umri wa kustaafu kwa mfanyakazi husika. Kwa kuchukulia kwamba hakuna umri wa kustaafu uliowekwa katika mkataba wenu wa ajira, ungetumia umri wa kawaida wa kustaafu au sera ya kustaafu ya kampuni yenu. Kwa mfano, kama zamani umri wa kustaafu kwenye kampuni yenu ni miaka 65, moja kwa moja, huo ndio utakuwa umri wa kustaafu kwa mfanyakazi. Kama kampuni yenu haina umri wa kustaafia, basi kanuni za kustaafia za sekta husika zinaweza kutumika. Hii itategemea na sekta mliyopo.

## Kufukuzwa Kazi kwa Kunyonyesha

**Nilijifungua mtoto miezi sita iliyopita na kurejea kazini baada ya wiki kumi baada ya kujifungua. Nahitaji kumnyonyesha mtoto wangu kila saa moja na kwenda nyumbani kwa muda wa dakika kumi na tano kila saa. Awali mwajiri wangu hakukataa lakini wiki nne zilizopita, nilipewa taarifa kwamba hii haitaruhusiwa tena na kwamba kama siwezi kuacha kunyonyesha, ninaweza kuachishwa kazi. Tafadhali nishauri?**

*27 Julai 2009*

Ratiba ya kunyonyesha kila saa ni ngumu sana kuelewa na kuamini, labda kama unamaanisha kila baada ya masaa machache. Hata hivyo, kwa lengo la kujibu swali lako, tutachukulia kuwa unamaanisha kunyonyesha kila saa moja.

Mwajiri wako hawezi kukuzuia kunyonyesha. Hata hivyo, kwa kuangalia hali yako, labda mwajiri wako anamaanisha kwamba unyonyeshaji wa kila saa moja haukubaliki. Hili linaweza kuwa si jibu unalolitaka, lakini tunashindwa kuelewa kivipi unaweza kwenda nyumbani kumnyonyesha mwanao kila saa na bado ufanye kazi. Unaweza kuwa unafanya kazi masaa matatu mpaka manne kwa siku na hakuna mwajiri anayeweza kukubaliana na hilo. Jaribu kufikiria jambo hili kwa kujiweka katika nafasi ya mwajiri pia.

Wakati tukisikitika pamoja, tungependa kukukumbusha juu ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, ambayo inasema kwamba iwapo mfanyakazi ananyonyesha, mwajiri atapaswa kumruhusu mfanyakazi kumnyonyesha mtoto kwa muda usiozidi masaa mawili tu kwa siku. Katika hali yako, unatumia zaidi ya masaa mawili kumnyonyesha mtoto na kama hautabadilika, hii inaweza kuwa sababu nzuri ya kuachishwa kazi.

## Kulazimishwa Kupima VVU / UKIMWI

**Nimeomba kazi ya Katibu Muhtasi kwenye kampuni ya usafirishaji na nimelazimishwa kupima VVU/ UKIMWI. Je, hii inaruhusiwa? Matokeo ya vipimo yatafanywaje? Je, daktari wangu anaweza kutuma matokeo ya vipimo kwa mwajiri wangu mtarajiwa?**

*6 Julai 2009*

Sheria ya VVU na UKIMWI (Kinga na Udhibiti) ya mwaka 2008 iko wazi sana juu ya hili. Hakuna mtu anaweza kulazimishwa kupima VVU isipokuwa kama kuna amri ya mahakama au kama mtu ni mchangiaji wa viungo vya binadamu au damu. Hakuna ridhaa inayohitajika juu ya kupima VVU/ UKIMWI kwa watu wanaotuhumiwa kufanya makosa ya kujamiiana/ngono.

Sheria pia inaruhusu daktari kufanya vipimo vya VVU bila ridhaa ya mhusika, kama mtu huyo hajitambui na hawezi kutoa ridhaa na iwapo daktari anaamini kuwa kipimo hicho ni muhimu kitabibu na kinafanywa kwa maslahi ya mgonjwa.

Katika hali yako, hakuna lolote kati ya hayo hapo juu linahusika, hivyo huwezi kulazimishwa kufanya vipimo.

Kuhusu kutolewa kwa matokeo ya VVU, sheria pia inasema kwamba matokeo yote ya vipimo vya VVU yatakuwa ya siri na yatatolewa tu kwa mtu aliyepima. Hata hivyo, matokeo hayo pia yanaweza kutolewa kwa mlezi wa mtoto kama aliyepimwa ni mtoto, mwenzi, mpenzi wa mtu aliyepimwa au mahakama. Daktari hawezi kutuma majibu kwa mwajiri wako bila idhini yako na kuvujisha siri za mgonjwa ni kosa la jinai.

## Kuiba ili kufidia Mshahara

**Nilikuwa na msichana wa kazi ambaye alifanya kazi kwangu kwa muda wa miaka mitatu. Kwa bahati mbaya, sijamlipa mshahara wake kwa miezi saba iliyopita.**

**Aliamua kuiba radio yangu na kutoroka. Je, anawajibika kwa kitendo hicho?**

*6 Aprili 2009*

Msichana wa kazi anaweza kushtakiwa kwa wizi chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu. Chini ya sheria, kujitwalia mali kwa hila/nia mbaya inayomilikiwa na mtu mwingine kwa nia ya kutokumrudishia tena mwenye mali ni kosa la kuiba na linaadhibiwa kisheria kwa kifungo cha miaka mitatu jela.

Kwa upande wako, hujamlipa mshahara wake kwa miezi saba, msichana huyo anaweza kudai kwamba hakufanya kitendo hicho kwa hila/nia mbaya kwa kuwa aliamini kwamba alichukua redio kufidia mishahara yake ambayo haijalipwa.

Ipo kanuni inayosema kwamba mtu hatakutwa na kosa la jinai kuhusu mali/kitu kama kitendo alichofanya, alikifanya kama mkakati wa kudai haki zake na hakuwa na nia ya kufanya udaganyifu.

Kwa kuzingatia mishahara ambayo hakulipwa, msichana wako wa kazi, kama atapelekwa mahakamani, kuna uwezekano mkubwa kuwa ataachiwa huru ikiwa atathibitisha kwamba alikuwa anadai haki na kwamba hajalipwa mshahara wake. Ni utetezi mzuri kwake. Kuepusha hayo kutokea siku za usoni, unapaswa kuwalipa watu wako kwa muda muafaka.

## Mshahara sio ule Ulioahidiwa

**Nimeajiriwa na shirika fulani na niliahidiwa mshahara kama ulivyoonekana kwenye tangazo la kazi gazetini. Kwa bahati mbaya, wakati nilipoajiriwa, walinipa mshahara mdogo kuliko ule uliotangazwa. Wanadai kwamba nitalipwa mshahara uliotangazwa ikiwa nitafanya vizuri. Ninawezaje kupata haki zangu?**

*2 Machi 2009*

Kwa kawaida tangazo la gazetini ni mwaliko wa kuitikia/kufanya makubaliano na sio tamko kamili, labda kama tangazo linaweza kutafsiriwa vinginevyo, ambapo kwako sivyo. Masharti ya mkataba wa ajira kama yalivyoainishwa kwenye tangazo hayakuwa tamko kamili, ndio maana wakati ulipoitikia wito/tangazo, kulikuwa na usaili ambao ulifanyiwa na kisha kupewa tamko la mshahara.

Nchini Tanzania, kuna kanuni maalum zinazosimamia mikataba ya ajira ili kulinda wafanyakazi. Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini inasema kwamba mfanyakazi anapoajiriwa tu anatakiwa kujua malipo na namna ya kukokotoa malipo hayo na maelezo ya malupulupu yoyote au malipo ya mali /vitu (payments in kind).

Kama ulisaini mkataba na mwajiri wako, basi masharti ya mkataba ni yale ambayo yanaonekana kwenye nyaraka ulizosaini na si kile kilichoonekana kwenye tangazo. Ulikuwa huru kuchagua kutokusaini; kwa kuwa ulisaini mkataba, huwezi kukataa kwamba hukufahamu mshahara uliotolewa. Kama mshahara upo chini ya kile kilichopo kwenye mkataba, una kesi nzuri dhidi ya mwajiri wako na unapaswa kufuatilia.

Tumejibu swali hili kwa kudhania tu na bila kuona tangazo husika. Pia, tunapendekeza upate ushauri kutoka kwa mshauri wa masuala ya ajira.

## Vyama vya Wafanyakazi Mahali pa Kazi

**Chama cha wafanyakazi kinataka kuwasajili wafanyakazi wetu kuwa wanachama wao. Sitaki chama cha wafanyakazi. Je, nifanye nini?**

*9 Februari 2009*

Sheria inatoa haki kwa chama chochote cha wafanyakazi kilichosajiliwa na kuidhinishwa kutembelea mahali pa kazi/majengo ya mwajiri kwa lengo la kusajili na kuongea na wanachama, kukutana na kuwasiliana nao na kuona namna wanavyohusiana na mwajiri, kufanya mikutano ya wafanyakazi

kwenye majengo ya mwajiri na kupiga kura katika uchaguzi wowote chini ya katiba ya chama cha wafanyakazi. Kwa hiyo, chama cha wafanyakazi kina haki ya kuwasajili wafanyakazi wako na pia unatakiwa na sheria kutoa kwa chama cha wafanyakazi vifaa vyovyote muhimu vinavyohitajika kuendesha shughuli zake sehemu ya kazi. Mbali na hivyo, sheria pia inaruhusu chama cha wafanyakazi kuanzisha tawi katika sehemu yoyote ya kazi ambapo wanachama wake kumi au zaidi wameajiriwa.

Hii ina maana kuwa chama cha wafanyakazi kina haki ya kufungua tawi katika kampuni yako ikiwa tu wafanyakazi wako kumi ni wanachama wa chama hicho. Ikiwa masharti kama hayo yametimizwa huwezi kuzuia kuanzisha chama cha wafanyakazi katika eneo lako la kazi kwa kuwa ni haki iliyotolewa kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, chama cha wafanyakazi hakiwezi kusajili wanachama kwa nguvu katika majengo yako. Kama wafanyakazi wako hawataki kujiunga, basi chama hakiwezi kuwalazimisha.

## Kuachishwa Kazi

**Nimeachishwa kazi baada ya kufanya kazi kwa kipindi cha miaka saba. Nililipwa mshahara wa mwezi mmoja kwa kuwa sikupewa notisi. Je, kuna stahiki gani nyingine na jinsi gani ninaweza kuzipata?**

*2 Februari 2009*

Tuchukulie haupingi kuachishwa kazi, stahiki zako zitategemea mkataba wa ajira kati yako na mwajiri. Haki zako kisheria za kuachishwa kazi, ukiachilia mbali mshahara wa mwezi mmoja kwa kutokupewa notisi, ni pamoja na: mshahara/malipo kwa ajili ya kazi iliyokwishafanya kabla ya kuachishwa, malipo ya likizo kama hazikuchukuliwa, mkono wa kwaheri/kiinua mgongo, posho ya usafiri (ambayo itajumuisha posho ya kujikimu) kama umefukuzwa kazi sehemu tofauti na ulipoajiriwa. Unastahili pia kupata cheti cha kazi. Ikiwa mwajiri wako atapuuza haki zako, unashauriwa kupeleka jambo hilo kwenye Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kuachishwa kazi.

# Haki za Mteja na Mdai

**Sheria inatambua kwamba wateja hawasomi mikataba. Sheria inabadilika kuhakikisha kwamba wateja wanalindwa moja kwa moja.**

Makubaliano mengi ya biashara huambatana na mikataba rasmi iliyokwishaandaliwa kabla na hivi ndivyo inavyo paswa kuwa. Hata hivyo, mikataba ni mirefu na inachosha kusoma hivyo wengi wetu huipitia juu juu na kuisaini. Je, wangapi kati yetu husoma mkataba mzima? Sura hii inaelezea nini kitatokea iwapo hautasoma mkataba wote. Sura hii pia inaelezea migogoro mbalimbali kati ya wateja na watoa huduma ambao wanaweza kuwa: kampuni ya bima, kampuni ya simu, taasisi ya fedha au mtoa huduma za afya na pia migogoro ya mikataba ya upangaji. Una haki ya kutafuta ufafanuzi - hivyo ushauri wetu kwako ni kusoma, uliza maswali na soma tena. Kabla ya kusaini nyaraka rasmi au kuingia katika makubaliano uliza maswali kama hujaelewa au kama kuna kitu kinakutatiza. Huna cha kupoteza kwa kuuliza maswali, lakini unaweza kupoteza vingi/mengi kwa kutokuuliza.

## Kuchukuliwa Ardhi Bagamoyo

**Mwaka 2006, nilinunua ardhi kwa jirani yangu ambaye anapakana na shamba langu maeneo ya Bagamoyo. Hakukuwa na mkataba rasmi wa mauzo, isipokuwa barua ambayo niliandika kwa mnunuzi ambapo muuzaji alikiri kupokea fedha ya manunuzi ya ardhi. Baadaye, muuzaji aliuza ardhi yangu kwa mtu mwingine bila ya mimi kujua wala ridhaa yangu. Nilishauriwa kuwafungulia mashtaka muuzaji na mnunuzi kwa pamoja ili kurudisha ardhi yangu, cha kushangaza Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi ametoa hukumu dhidi yangu. Je, ninaweza kufanya nini? Vipi kuhusu fedha nilizomlipa muuzaji?**

*25 Aprili 2011*

Hatuna nakala ya mwenendo wa mashtaka kutoka Baraza la Ardhi ambao ungetuwezesha kujua sababu ya wewe kushindwa kesi, na wala hatuna nakala ya barua ya makubaliano kati yako na muuzaji juu ya mauzo ya ardhi. Hiyo ingetusaidia sana kama tungejua aina ya utetezi uliotolewa kwenye Baraza la Ardhi na upande mwingine. Kutokana na uzoefu wetu, tunahisi kwamba unaweza kuwa ulishindwa kesi kwa sababu barua yenu ya mauziano ya ardhi haikukidhi masharti muhimu ya sheria yaliyohusiana na mikataba ya mauziano ya ardhi. Sheria ya Ardhi inataka mkataba wa mauzo ya ardhi; ufanywe kwa maandishi, ambao unaweza kuwa ni mkataba, hati ya makubaliano, muhtasari, ilimradi tu inagusia masharti muhimu kama vile wahusika, bei na maelezo ya utambuzi wa ardhi inayouzwa.

Kuhusu pesa zako, inategemea na madai yaliyowasilishwa na wakili wako kwenye Baraza la Ardhi na sababu za maamuzi ya Baraza. Kama bado unaamini kuwa maamuzi ya Baraza hayakuwa sawa, tunakushauri ukate rufaa Mahakama Kuu kwa hatua zaidi. Wakili wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Wamiliki wa Viwanda wanakula Njama kuhusu Bei

**Kuna viwanda fulani vinavyomilikiwa na baadhi ya wazalishaji wakubwa/matajiri ambao wametengeneza tabia ya kuhodhi soko. Wamekula njama na kupandisha bei ya bidhaa na kutengeneza uhaba bandia wa bidhaa. Hiki ni kitendo ambacho kinapingana na kanuni za ushindani. Je, kuna sheria ambayo inaweza kuwalinda walaji katika mazingira kama haya?**

*25 Aprili 2011*

Sheria ya Ushindani itakulinda. Sheria hii ilianzisha Baraza la/Tume ya Ushindani (FCC) ambayo husimamia shughuli hizo na kulinda maslahi ya walaji. Sheria ya Ushindani inajumuisha Kanuni za Ushindani, na katika kanuni hizo kuna utaratibu wa kushughulikia malalamiko ya walaji. Kama mlaji, unaweza kulalamika kwa kuwasilisha taarifa husika kwa Tume kwa namna yoyote, au kwa kutumia fomu maalum ambayo imetolewa katika kanuni za Tume. Baada ya hapo, idara ya uchunguzi ya Tume itapitia malalamiko yako na kuamua kama wale uliowalalamikia wana kesi ya kujibu au la. Tume inaweza kutumia utashi wake kushughulikia malalamiko yako au la na kama hawatayashughulikia malalamiko yako watatoa sababu ya kutokufanya hivyo. Tunashauri kwamba utumie njia hizo kupigania haki yako kupitia Tume.

## Majeraha kutokana na Masumbwi

**Nilipigana na mwana masumbwi wa Tanzania ambaye aliniumiza vibaya chini ya taya. Niliumia vibaya na polisi wamekataa kupokea malalamiko yangu. Je, ninaweza kumshitaki na kudai fidia?**

*18 Aprili 2011*

Kwenye sheria kuna msemo maarufu unaosema 'huwezi kumshtaki mtu kwa

maumivu uliyoyaridhia mwenyewe kwa hiari yako.' Kwenye sheria ya madhara hakuna kesi inayoweza kufunguliwa na mtu yeyote na hakuna mtu anayeweza kusimamia haki ambayo ameitelekeza au ameipuuza kwa hiari yake.

Kanuni hii inatumika kwa vitendo vya makusudi ambavyo vinginevyo vinaweza kuwa ni vya madhara. Inaonesha wazi kuwa majeraha yako yametokana na shindano la masumbwi/ngumi na ndiyo maana polisi wamekataa kupokea malalamiko yako.

Kwa maarifa tuliyo nayo kuhusu mchezo wa ndondi, kupigwa ngumi chini ya taya ni halali, hivyo kwa maoni yetu, kuna uwezekano mdogo sana wa wewe kufanikiwa iwapo utaamua kuwasilisha shauri lako mahakamani. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kudaganywa na Wahalifu wa Mtandaoni

**Ninatafuta kazi, na wakati nikitafuta kazi, niliona tangazo kwenye tovuti. Moja ya mahitaji ilikuwa kufanya mtihani wa kupima kiwango cha uelewa wa Kiingereza inayotolewa na taasisi moja ng'ambo. Nilikuwa na chaguzi mbili - kulipa kwa kutumia kadi ya malipo, ambayo sina, ama kuweka fedha kwenye akaunti fulani ya benki, ambapo nilichagua njia hii ya pili. Kwa bahati mbaya, hadi sasa sijaambiwa mahali pa kufanyia mtihani huo. Nilifanya uchunguzi na kugundua tovuti hiyo haifanyi kazi tena. Nikituma barua pepe kwenye anuani niliyokuwa nawasiliana nayo hazijibiwi. Simu zangu zote nikipiga huingia katika mfumo wa ujumbe wa sauti, na hakuna mtu anayejibu. Nilienda polisi ambako niliambiwa mimi ni mmoja wa mamia ya watu waliotolea taarifa jambo hili, na kwamba hawana mbinu wala ujuzi kuwafuatilia hawa matapeli. Je, mnafikiri kuwa ninaweza kufanikiwa kupata fedha yangu?**

*4 Aprili 2011*

Ni vigumu kufuatilia na kufanikiwa kuwapata matapeli hawa. Tovuti, iwe ya kitanzania au ya kigeni, inaweza kuendeshwa ikiwa mbali kutoka sehemu yoyote ya dunia na ni vigumu kujua nani ni mwendeshaji na ni vigumu kujua kama tovuti ni ya kweli au la. Tunasikitika na wewe na polisi ambao pia hawajui nini cha kufanya na hawana vifaa vya kushughulikia suala hilo. Ni lazima kuweka wazi kuwa, kwa mujibu wa waandishi/wachambuzi mbalimbali wa sheria ya jinai, mojawapo ya tishio kubwa kwa usalama wetu ni wahalifu wa mtandaoni ambao hawajulikani na wanaweza kufanya shughuli zao bila kuonekana. Ulaghai mwingine unaojulikana kwenye mtandao ni pamoja na wahalifu hawa kukutumia ujumbe kwenye barua pepe yako wakitaka uwape neno la siri ili wakutunzie kwa ajili ya kumbukumbu au kurudisha taarifa zako zikipotea - mara nyingi ujumbe huo hudai umetoka kwa mtoa huduma wako. Mara tu utakapotoa neno la siri, matapeli hawa hutuma barua pepe kwa watu wako wa karibu ambao wapo kwenye orodha ya barua pepe zako wakidai kwamba umekwama na unahitaji pesa kidogo. Pia, wanatoa akaunti ya benki ili watu wako wa karibu waweke pesa, na kuendelea kupokea pesa kwa yeyote anayetuma.

Tukirudi kwenye swali lako, ni kweli umetapeliwa, ni kosa la jinai, na umefanya jambo sahihi kuwapa taarifa polisi. Kuhusu kurudisha pesa zako, unatakiwa kuwaona wataalamu wa masuala ya teknolojia ya habari na mawasiliano ambao wanaweza kufuatilia kujua tovuti hiyo iko wapi. Unayo nafasi pia ya kufuatilia mmiliki wa tovuti kupitia akaunti ya benki waliyoitumia. Benki wana wajibu wa kujiridhisha kwa kina kabla ya kumfungulia mteja wao akaunti.

## Masharti ya Kudumu ya Kampuni ya Usafirishaji Vifurushi

**Nilitumia kampuni ya usafirishaji vifurushi**

**kutuma hati yangu ya kusafiria (pasipoti) kwenye ubalozi nje ya Tanzania. Kifurushi kilipotea na kusababisha nichelewe kutuma maombi ya viza ya mwanafunzi, matokeo yake nilipoteza mwaka mzima wa masomo. Baadaye nilituma upya maombi ya hati mpya ya kusafiria, na kutuma maombi pia kwa ajili ya viza. Meneja wa kampuni ya usafirishaji vifurushi ameniambia kwamba masharti yao ya kudumu ya usafirishaji yanaweka ukomo wa kufidia pesa niliyotumia. Alinionyesha nyaraka husika ambayo ina maandishi madogo madogo yaliyobanana. Je, ninaweza kufanya nini?**

*28 Machi 2011*

Kampuni ya usafirishaji vifurushi haiwezi kuweka kikomo cha kuwajibika kwa namna inavyoonesha. Uliingia nao mkataba wa kupeleka hati yako ya kusafiria kwenye ubalozi. Makubaliano yalikuwa ni kufikisha kifurushi, na wewe kulipa kiasi fulani. Kwa kuwa hawakufikisha kifurushi, kampuni ya usafirishaji imekiuka wajibu wake. Inaonesha hukuona masharti ya ubebaji vifurushi wakati uliposafirisha kifurushi chako; na hata kama uliona, kuna ukiukwaji na unayo sababu nzuri ya kufungua mashtaka dhidi ya kampuni ya kusafirisha vifurushi. Kwa bahati mbaya, watu wengi wanadhani kuwa kitu chochote kilichoandikwa vizuri 'hakina makosa' na kinaweka utaratibu wa kudumu. Hiyo si kweli. Hupaswi kukata tamaa; wakili wako anaweza kukuongoza zaidi baada ya kusoma masharti ya kudumu ya kufanya biashara na kuelewa jambo zima.

## Kushindwa kulipia Tozo/Ada ya Bima

**Bima ya gari langu ilifutwa moja kwa moja na wakala wa bima. Hata hivyo, sikujulishwa kuwa ada za bima hazijalipiwa. Kwa kuwa sasa nina madai, kampuni ya bima inakataa kulipa, kwa kuwa sijalipa ada za bima, ingawa nina stika ya bima. Kiasi cha ada ya bima ninayodaiwa ni chini ya shilingi milioni 1, na madai yangu yanakaribia milioni 20. Nilikubaliana na kampuni ya bima kwamba wanilipie hiyo tofauti, lakini kwa mshangao mkubwa wamekataa. Je, nifanye nini?**

*28 Mai 2011*

Jibu rahisi kwa swali lako ni kuwa daima hakikisha unalipa ada ya bima yako kwa wakati. Kanuni za bima za kidunia, na sheria zipo wazi - kutokulipa ada ya bima hupelekea bima kubatilishwa. Haijalishi kuwa una stika. Kuwa na stika haimaanishi moja kwa moja kuwa una mkataba halali wa bima. Hivyo, tunakubaliana na kampuni ya bima kuwa hupaswi kulipwa. Kwa upande mwingine, iwapo kampuni ya bima ingefidia ada ya bima kwa kutumia madai yako kama ulivyopendekeza, ingekiuka kanuni za bima. Kwa kifupi, makampuni ya bima hukusanya ada za bima mapema, na hutarajia kulipa kidogo kuliko kiwango cha ada kilichokusanywa. Utaratibu huu unaitwa, 'kubali jukumu kwa kutumia mabaki/ziada'. Njia nyingine makampuni ya bima yanayotumia kutengeneza pesa ni kwa kuwekeza ada za bima katika biashara mbalimbali, hii inaitwa 'mapato ya uwekezaji'. Pendekezo lako la kulipwa linaziba moja ya vyanzo vikuu vya mapato ya makampuni ya bima. Labda kama kampuni ya bima ikulipe kwa hiari/huruma tu, vinginevyo madai haya hayalipiki.

## Daktari kuzuia Taarifa

**Kama wiki ishirini zilizopita, mjamzito mmoja aliletwa kwangu na mmoja wa madaktari wa ngazi ya chini. Baada ya kumchunguza na kuagiza kufanyika baadhi ya vipimo, niligundua kitu kibaya sana kwa mtoto aliyeko tumboni. Kadi ya taarifa ya mwanamke huyo ilikuwa na namba za simu za mumewe ambaye alitupa ridhaa ya kuwasiliana naye ikiwa kuna jambo lolote. Niliona huyo mjamzito asingeweza kuhimili kupokea taarifa zile. Baada ya kutafakari**

**kwa siku mbili, nilimwomba mwanamke huyo aje kuniona. Wakati huo, nilimpigia mume wake ambaye kwa bahati mbaya alikuwa amesafiri. Iliniwia vigumu kujadili jambo hilo kwenye simu na nilisisitiza anione haraka. Alikuja siku iliyofuata na nilimweleza jambo hilo. Wanandoa hao walipotea kwa muda mrefu bila taarifa, hadi hivi karibuni baada ya mwanasheria wao kunitumia notisi iliyodai wanandoa hao wana nia ya kunishitaki kwa kutompa taarifa mwanamke huyo papo hapo. Inaonekana mwanamke huyo alienda kutibiwa Nairobi, na kijusi/mtoto alifariki. Madaktari wa Nairobi wameandika katika taarifa yao kwamba, kama angetibiwa mapema maisha ya mtoto yangeokolewa. Je, nifanye nini?**

*21 Machi 2011*

Upendeleo wa kitabibu ni haki ya daktari kutotoa taarifa kwa mgonjwa pale anapoona kwamba kutoa taarifa kunaweza kusababisha madhara makubwa na ya ghafla kwa mgonjwa, kwa mfano, pale mgonjwa anaposumbuliwa na msongo wa mawazo. Katika mazingira ya kipekee, haja ya kuficha taarifa inaweza kupuuzwa ili kupata ruhusa mapema kutoka kwa wahusika ili kuendelea na matibabu. Katika hali yako, hatuna maelezo kamili. Hata hivyo, unaonekana una hoja/utetezi unaokubalika na unaweza kuwasiliana na mwanasheria wako.

## Warithi kulipa Madeni

**Mimi ni Mtanzania ninayeishi Ulaya na ninafanya kazi kwenye Ubalozi wa Tanzania. Wakati wa likizo takribani miaka mitano iliyopita, niliingia mkataba wa ununuzi wa ardhi iliyoko Dar es Salaam. Kutokana na kuwa na kazi nyingi, sikuweza kushughulikia uhamisho wa ardhi iliyonunuliwa kwa jina langu. Mwaka 2008, nilianza mchakato wa kuhamisha umiliki wa ardhi lakini haukufanikiwa kutokana na kukosa ridhaa ya Kamishna wa Ardhi. Baada ya Kamishna kukataa, mwanasheria aliyeshughulikia alinipa taarifa kwamba mchakato mzima wa mauzo haukuwa umekidhi vigezo na kwamba ninatakiwa kudai fedha yangu. Baada ya kwenda kwa muuzaji, nilipewa taarifa na mkewe kwamba alifariki kwa ajali mwaka uliopita na kwamba mali zote za marehemu zilifunguliwa mirathi na msimamizi na kugawanywa kwa warithi wake. Kiwango nilicholipia kama malipo ya awali ni kikubwa. Je, nifanye nini?**

*28 Mei 2011*

Bado hujatueleza sababu ya Kamishna wa Ardhi kukataa kuridhia. Kama tungejua hilo, tungeweza kukushauri uendelee kufuatilia ridhaa husika. Suala la ridhaa ni utaratibu wa kawaida na si rasmi sana na halibatilishi mkataba kati yako na muuzaji. Swali la msingi ni – je, unaweza kurejesha fedha yako iliyolipwa kama kianzio? Ukweli kwamba muuzaji amefariki na mali zake zimegawanya kwa warithi wake haliwezi kubadilisha jibu. Kama umechagua kuacha kufuatilia ridhaa ya Kamishna, tunakushauri umwone msimamizi wa mirathi ambaye atapitia nyaraka, na kumtaka kila mrithi kurejesha kiasi fulani cha pesa kwa kadili ya urithi wake ili ulipwe madai yako. Kama msimamizi hatoi ushirikiano, sheria inakuruhusu kufungua kesi ya fidia dhidi ya msimamizi na wanufaikaji wote. Tunakushauri umuone mwanasheria wako kwa msaada zaidi.

## Vipodozi vilivyotengenezwa chini ya Kiwango vimeharibu Ngozi

**Nilinunua losheni Kariakoo ili kung'arisha ngozi yangu. Losheni hiyo ilitengenezwa Afrika Kusini na imesababisha ngozi yangu kubanduka. Hivyo, imenisababishia matatizo makubwa ya ngozi. Je, nani anadhibiti uagizaji wa losheni hizo? Je, nifanye nini?**

*21 Februari 2011*

Nchini Tanzania kuna chombo kinachoitwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA). Chombo hiki kina mamlaka ya kudhibiti dawa zote na vipodozi vinavyoingizwa kutoka nje ya Tanzania, na kina mamlaka ya kutembelea duka lolote au kwenda kwenye maghala na kukagua madawa na vipodozi vinavyouzwa au kuhifadhiwa. Mamlaka ina uwezo wa kutangaza vipodozi au dawa kuwa na madhara na kupiga marufuku uagizaji au kuuza bidhaa hizo. Kama mfanyabiashara anakaidi kuacha kuuza bidhaa zilizopigwa marufuku, anaweza kutozwa faini au kufungwa.

Hatua ya kwanza ni wewe kuwajulisha TFDA kuhusu bidhaa, ulikonunua, na nini kilichotokea. TFDA inajulikana sana nchini Tanzania kwa kuchukua hatua stahiki na hivyo tunashauri uwaone mara moja.

Kuhusu kumshtaki mfanyabiashara, una sababu ya kuchukua hatua dhidi yake na unaweza kumshtaki. Njia nyingine ni ya kumuunganisha muuzaji na mtengenezaji na kuwashtaki pamoja kama ilivyoamuliwa kwenye kesi moja maarufu ya Kiingereza inayoitwa *Donoghue dhidi ya Stevenson*. Kesi hii yenye umri wa miaka themanini ilianzisha kanuni ya kupanua wajibu/uwajibikaji. Kesi hii ilianzisha kanuni moja ambayo Majaji waliita kanuni ya 'jirani', ambayo waliitoa kwenye Biblia Takatifu, yaani 'mpende jirani yako', inayopatikana kwenye hadithi ya Msamaria Mwema. Tunapendekeza kuwa umshtaki mtengenezaji kwa kuwa ana mengi ya kupoteza. Si tu kwamba losheni anazosambaza zitapigwa marufuku kuingia sokoni, lakini pia mtengenezaji anaweza kujikuta bidhaa zake zote zinapigwa marufuku.

Ni lazima ieleweke kwamba kuwajibika kwa mtengenezaji kutategemea kama au la bidhaa halisi ilibadilishwa au kuingiliwa baada ya bidhaa husika kutoka kwa mtengenezaji. Kuna watu wengi wa kati ambao wanahusika: msambazaji, muagizaji, na mfanyabiashara/muuzaji wa mwisho. Marekebisho yoyote yaliyofanywa na mmoja wa watu hao yatamuengua mtengenezaji kwenye wajibu/makosa.

Mwisho, tusingependa kuchukuliwa kama madaktari, kwani sisi siyo, lakini ni ukweli unaojulikana kuwa vipodozi vya kung'arisha ngozi/kujichubua/mkorogo huwa na kemikali kali kama risasi na zebaki ambayo huua seli fulani za rangi ya asili katika ngozi na kufanya uonekane laini/mng'aavu, lakini si mtoto. Kemikali kama hizo zinahusishwa na saratani ya ngozi, na inapendekezwa kwamba usitumie bidhaa hizo. Kuwa mweupe hakukufanyi kuwa mrembo, ukizingatia kwamba uzuri wa mtu uko machoni pa mtazamaji. "Kipenda roho hula nyama mbichi", Waswahili husema.

## Uvutaji Sigara na Kondakta wa Daladala

**Huwa ninatembelea Dar es Salaam na kutumia mabasi yanayojulikana kama daladala. Katika safari ya hivi karibuni kutoka mjini kwenda Gongo la Mboto kondakta alianza kuvuta sigara, ambayo iliibua mabishano makali kati ya abiria na kondakta, ambaye alisema yeye ni bosi na basi hilo ni mali yake. Kondakta pia alitumia lugha ya matusi dhidi ya abiria. Je, uvutaji sigara katika mabasi unaruhusiwa kisheria? Je, ni hatua gani sahihi za kisheria tungeweza kuchukua dhidi ya kondakta?**

*31 Januari 2011*

Maadili ya makondakta wa mabasi yanasimamiwa na Kanuni za Usalama Barabarani kuhusu Maadili ya Madereva, Makondakta na Abiria. Katika kanuni hizo, ni marufuku kwa kondakta kuvuta sigara katika chombo cha usafiri wakati wa safari au wakati wowote ikiwa kuna abiria ndani ya gari. Kondakta ana wajibu wa kuchukua tahadhari zote kuhakikisha usalama wa abiria wakati wa kuingia, au kushuka kwenye mabasi. Kondakta pia haruhusiwi kutumia lugha mbaya au ya

kukera, pia anapaswa kujiheshimu na kuwa muungwana.

Hatua ya haraka ya kuchukua ni kutoa taarifa ya tukio hilo kwa afisa wa polisi, ambaye baada ya uchunguzi anaweza kupeleka suala hilo mahakamani. Baada ya kutiwa hatiani, mtuhumiwa anaweza kulipa faini au kufungwa jela kwa kipindi kisichozidi mwezi mmoja au vyote kwa pamoja.

## Kampuni za Simu za Mkononi zinaiba Muda wa Maongezi

**Nina uhakika kuwa kampuni yangu ya simu ya mkononi inakata senti chache kila siku kwenye akaunti yangu ya malipo ya baadaye. Pia, wanakata mawasiliano makusudi ili upige tena simu, wapate fedha zaidi. Je, nifanye?**

*24 Januari 2011*

Kama mteja wa simu ya mkononi, una mahusiano ya kimkataba na kampuni husika. Madai yako dhidi ya kampuni ya simu za mkononi yanaweza kuwa ya kweli na unaweza kuwashtaki, lakini ugumu unakuja katika kuthibitisha madai haya.

Tulifanya utafiti juu ya suala hili na kugundua kuwa baadhi ya watoa huduma za simu katika sehemu nyingine duniani wamewahi kukutwa na hatia ya makosa tofauti tofauti ya namna hii. Kwa ujumla, mtoa huduma wako hawezi kuwa ni mtakatifu muda wote, na kama una ushahidi dhidi yake, una kesi nzuri dhidi yake. Pia, unaweza kupelekea taarifa hizo kwa mamlaka husika ili kampuni hiyo ichunguzwe, kwani ikiwa wanakata salio kwenye akaunti yako, wanaweza kuwa wanafanya vivyo hivyo kwa wateja wao wengine.

Tunakushauri ukusanye ushahidi na kuwaona wanasheria wako.

## Kupasuka kwa Tairi ya Gari na kusababisha Ajali

**Nikiwa naendesha gari kutoka Morogoro kwenda Mbeya moja ya tairi ya gari yangu ilipasuka, na kusababisha nigongane uso kwa uso na basi. Watu kadhaa walijeruhiwa vibaya, na polisi waliripoti kuwa ajali imesababishwa na kupasuka kwa tairi. Je, ninaweza kumshtaki mtengeneza tairi? Ni nani mwingine naweza kumshtaki?**

*10 Januari 2011*

Unaweza kumshtaki mtu yeyote, ambaye, kwa maoni yako alisababisha ajali. Anaweza kuwa mwenda kwa miguu, au gari jingine, anaweza kuwa abiria kwenye gari lako ambaye alikuchanganya, anaweza kuwa mtengeneza gari. Inawezekana kabisa kuwa mtu yoyote ambaye unaweza kumfikiria kuwa amesababisha ajali hiyo. Hata hivyo, lazima ushtaki upande ambao unaweza kuthibitisha tuhuma dhidi yake. Hakuna sheria ambayo inakuzuia kumshtaki mtu yeyote; hata hivyo, kumbuka kwamba upande ulioushtaki na kukushinda kesi, unaweza kudai gharama/fidia kutoka kwako baada ya kesi kumalizika, ikiwa umeshindwa.

Unadai kwamba polisi ilithibitisha kuwa ajali hiyo ilisababishwa na tairi kupasuka. Kutokana na tunachokisoma hapa, polisi haijathibitisha kwamba ajali hiyo ilitokana na ubovu/dosari ya tairi kutoka kwa mtengenezaji, bali tairi ilipasuka tu. Kupasuka kwa tairi kunaweza kusiwe kumesababishwa na makosa ya mtengenezaji, japo hatuondoi uhusika wake. Lakini inaweza kuwa imesababishwa na tairi kujazwa upepo mwingi au kidogo, ukosefu wa matengenezo ya mara kwa mara ya tairi, au sababu nyingine zozote zile. Katika kesi hii, ni vigumu sana kwetu kukushauri kuwa umshtaki mtengeneza tairi au la. Unapaswa kuchunguza na kuelewa sababu halisi ambayo imesababisha ajali hii, kisha ufanye uamuzi sahihi. Polisi si wataalamu katika kubaini ubora wa tairi, na kama utashtaki mtengeneza tairi, atawaleta wataalamu wake ili kupinga chochote unachojaribu kuthibitisha. Unahitaji

kupata ushauri wa wataalamu wa tairi kabla ya kufungua kesi.

## Wizi wa Utambulisho kwenye Google.com

**Nimegundua kuwa picha yangu, jina langu kamili na maelezo binafsi, ikiwa ni pamoja na eneo ninaloishi na kufanyia kazi, vyote viko kwenye mtandao wa Facebook. Cha kushangaza ni kwamba habari ni sahihi, lakini mhusika sio mimi, ni mtu fulani anayejifanya kuwa mimi. Mtu huyo ameomba urafiki kwa marafiki zangu na anazungumza kila aina ya upuuzi. Sina akaunti Facebook na nina tabia nzuri. Ukurasa huo wa Facebook unaonesha kuwa mimi ni mwanamke ambaye natafuta kwa nguvu zote uhusiano wa muda mfupi wa kingono. Nimejua haya wiki chache zilizopita. Nimekuwa nikipigiwa simu na wanaume nisiowajua wakionesha kunitaka kimapenzi. Mwanzoni niliona sifa, baadaye nikagundua kuwa wanaume hao wanadhani mimi ni changudoa/najiuza. Jambo hili limenisababishia aibu kubwa. Pia, mchumba wangu anaelekea kuamini haya na anataka kuniacha. Je, nifanye nini? Marafiki zangu wameniambia haiwezekani kuishtaki kampuni ya Facebook kwani ni mtandao mkubwa mno.**

*27 Desemba 2010*

Teknolojia inakuja na manufaa mengi, lakini ni wazi umekumbana na ubaya wake. Wizi wa utambulisho ni changamoto kubwa ijayo katika ulimwengu wa mtandao. Inasemekana kwamba baadhi ya tovuti zina nguvu zaidi ya Serikali, kwa kuwa zinaweza kueneza habari kwa ufanisi, kwa nguvu, na kwa kasi ya mwanga/ajabu. Ndiyo, hili ni tatizo kubwa, si kwako tu, bali hata kwa raia wa nchi yoyote ile. Uhalifu wa kimtandao unaongezeka na umekuta watu wengi hawajajiandaa.

Kwa kujibu swali lako, unaweza kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mtandao wa Facebook, mtu anayejifanya ni wewe, na mtoa huduma mwingine yeyote anayesaidia kusambaza taarifa hizo duniani kote.

Japo unaweza kufungua kesi juu ya kuchafuliwa jina, njia ya haraka ya kutatua changamoto hii ni kuwaandikia Facebook ili waweze kuchunguza jambo hilo. Tuna taarifa kuwa Facebook huchukulia suala la wizi wa utambulisho kwa uzito mkubwa, na baada ya kufanya uchunguzi wa haraka, watamfungia mtumiaji huyo anayejifanya kuwa ni wewe. Wewe sio wa kwanza kukumbwa na suala kama hili katika Facebook.

Kuhusu uwezekano wa kuwapata au kuwashtaki Facebook, tafadhali tambua kuwa Facebook ni kampuni inayojulikana sana nchini Marekani, na wanaweza kupelekewa wito/samansi kutoka Tanzania. Ukweli kwamba ni kampuni kubwa haimaanishi kuwa huwezi kuwashtaki - hakuna sheria ambayo inakuzuia kuwashtaki.

Kwa uzoefu wetu, tunapenda kukujulisha kuwa mara nyingi marafiki zetu, au marafiki wa zamani, ndio hufanya wizi wa utambulisho, kwani wana taarifa zako zote. Hatutaki kuamini ushauri wa 'huwezi kushtaki' kutoka kwa 'marafiki' zako. Kinyume chake, ungetilia shaka marafiki zako na kuchunguza ni nani kati yao anaweza kuwa amefanya wizi huu wa utambulisho. Ikithibitika, unaweza kumshtaki pia.

Mwisho, Facebook wamewahi kushtakiwa mara nyingi kwa sababu mbalimbali. Tuna taarifa kuwa wamewahi kushtakiwa kwa ukiukwaji wa haki ya faragha, utoaji siri, kuchafua jina na kuhamisha taarifa kinyume cha sheria. Inawezekana kabisa kuchukua hatua kwa kilichokutokea, unapaswa kuwasiliana na wanasheria wako kwa msaada zaidi.

## Uvundo wa Kuku, sina Furaha ya Maisha

**Mimi ni mstaafu ninaishi peke yangu katika nyumba ya vyumba viwili jijini Dar es Saalam. Nimekuwa nikiishi kwa amani katika nyumba**

**yangu kwa kipindi cha miaka thelathini hadi mgahawa ulipofunguliwa karibu na nyumba yangu miezi michache iliyopita. Mgahawani hapo wanachoma/kukaanga kuku usiku. Japo sijali kero zitokanazo na magari kupaki mgahawani, uchomaji wa kuku hufanya nyumba yangu kujaa harufu ya viungo wanavyotumia. Hali hii imefanya nikose raha kabisa. Nilipowasiliana na mamlaka ya jiji, walikuja, na kula kuku na mmiliki wa mgahawa na kuondoka bila kuchukua hatua zozote. Nimeandika barua kwa kila mtu niliyefikiri anaweza kutatua tatizo hili, hadi Meya wa jiji, lakini hadi sasa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Nimeshuhudia watu maarufu, na hata Mawaziri wakija kula kuku, ambao ninakubali ni watamu na safi sana, lakini kunusa harufu yake kila siku nyumbani kwangu kunanipa msongo wa mawazo. Je, nifanye nini? Nimeambiwa, kwa kuwa sina mkataba na mmiliki wa mgahawa siwezi kumshtaki.**

*20 Desemba 2010*

Kwa sababu Mawaziri wanakuja kula kuku hapo haiwezi kubadili jambo baya kuwa zuri. Kwa hali yoyote ile, tuna uhakika kuwa Waziri au wateja wengine wa mgahawa huo hawawezi kufurahishwa na usumbufu unaoupata. Katika kesi moja maarufu sana ya Kiingereza mmoja wa Majaji alipata kusema kwamba 'kila mtu ... ana haki ya asili kufurahia hewa safi isiyokuwa na harufu mbaya, na mtu yeyote ambaye huchafua hali ya hewa ana hatia ya kusababisha usumbufu/kero/adha.'

Kitendo cha mmiliki wa mgahawa kinakupa haki wewe ya kufungua kesi ya madai na hauna haja ya kuwa na mkataba nae ili umshtaki. Una kesi nzuri sana na inawezekana kabisa kupata amri ya zuio kama utafuata taratibu sahihi za kimahakama. Hupaswi kusitasita ikiwa hali hii inakusababishia usumbufu mwingi - wasiliana na wakili wako.

## Kila kitu Wanapotaka

**Niliingia mkataba wa mkopo na benki. Kila kitu hufanyika wao wanapotaka. Mkopo nalipa wanapotaka, riba nalipa wanapotaka, na kama kuna kuweka dhamana zaidi naweka wanapotaka. Hii ni kama hukumu yangu ya maisha. Je, ninawezaje kujinasua kwenye hili?**

*13 Desemba 2010*

Kwa namna ulivyouliza swali lako, inaonekana umesaini nyaraka za mkopo na kisha ukaanza kuzisoma. Kwa uzoefu wetu wa miaka mingi, tumegundua kwamba wakopaji hufanya hivi - kwanza kupata pesa kutoka benki, na baadaye kuanza kusoma nyaraka pale wanapokiuka mkataba au wanapopata tatizo!

Mapatano ya kulipa kwa hati za dhamana benki hufanyika pale tu benki inapotaka/dai. Ulipaji wa namna hii una faida kwa benki kwa sababu benki haitabanwa na Sheria ya Ukomo wa Mashtaka kwani ni mpaka inapodai. Hata hivyo, uhalali wa ulipaji wa namna hii hutokea tu pale ambapo muda wa kulipa deni umeshafika na deni/mkopo kuwa umeiva. Hii haimaanishi kwamba mkopo wa muda maalum unabadilika na kuwa mkopo wa kulipa benki inapotaka. Ikiwa hicho ndicho kinachokutatiza, basi hicho ni kifungu cha kawaida kwenye mikataba ya namna hiyo.

Ni lazima tueleze kwamba kipengele cha kuongeza dhamana benki 'inapotaka' si cha kawaida. Kama tungesoma hati ya mkopo yote kwa ujumla wake tungejua kipengele hicho kinatakiwa kitafsiriwe namna gani, lakini kwa kusoma kipengele hicho peke yake kinaonekana ni sharti gumu sana na kinaonekana kweli kama kifungo cha maisha. Kwa kuwa hatukuona hati nzima, tunakushauri kuwasiliana na mwanasheria wako kwa mwongozo zaidi.

## Umiliki Wenza na Umiliki wa Pamoja

**Mimi na mke wangu tumeishi maisha yetu yote katika ghorofa ya Shirika la Nyumba**

**ya Taifa. Hatimaye tumenunua nyumba yetu na tumepewa uchaguzi wa kumiliki kama wamiliki wenza au, wa pamoja. Je, kuna tofauti gani kati ya aina hizi mbili, na unapendekeza tufanye nini?**

*13 Desemba 2010*

'Umiliki wa pamoja' na 'umiliki wenza" zote ni aina za umiliki. Kwenye umiliki wa pamoja, wamiliki wote wanamiliki mali yote kwa pamoja na hakuna mmiliki mwenye sehemu ya peke yake kwenye mali hiyo. Ikiwa mmoja wa wamiliki akifa moja kwa moja mali inamilikiwa na mmiliki aliye baki hata kama mmiliki aliyekufa angeacha wosia kwamba sehemu yake ya umiliki igawiwe kwa mtu mwingine zaidi ya yule mmiliki mwenza.

Kwa upande mwingine 'umiliki wenza' ni kinyume cha umiliki wa pamoja. Katika umiliki wa pamoja, kila mmiliki ana sehemu yake inayojulikana kwenye mali. Kwa mfano, mtu na mkewe wanaweza kumiliki mali sawa kwa sawa. Aina hii ya umiliki inafaa zaidi pale wamiliki wanapotaka kumiliki mali katika mgawanyo uliobainishwa kabla. Kwenye 'umiliki wenza' ikiwa mmoja wa wamiliki amefariki, sehemu yake ya mali itaenda kwa mtu yeyote aliye tajwa kwenye wosia au kama marehemu hakuandika wosia basi mali yake itagawanywa kwa mujibu wa kanuni zinazosimamia mali ya watu waliokufa bila kuacha wosia.

Kwa kawaida tunawashauri wanandoa ambapo wanaishi vizuri kufuata mfumo wa umiliki wa pamoja kwakuwa inaaminika hakuna faida ya kufanya mgawanyo wa mali hiyo. Hii itasaidia kama mmoja wao akifa mali itaenda moja kwa moja kwa mwanandoa aliyebakia/hai.

## Kubadilika kwa Viwango vya Riba

**Nilikopa shilingi milioni 550 benki na hivi sasa nina mgogoro nao kwa namna walivyokokotoa riba kwenye akaunti yangu ya mkopo. Nimeshtushwa na benki ilivyobadilisha mno riba sambamba na mabadiliko ya hawala za Serikali kwa miaka mingi. Je, hii inaweza kufanyika? Je, nini dawa yake?**

*29 Novemba 2010*

Sheria inayotumika ni Sheria ya Fedha ya Mikopo, ambayo iko wazi katika kifungu cha 10 kuwa kiwango cha riba kinaweza kubadilika kutoka kipindi kimoja hadi kingine kulingana na kanuni zilizowekwa kwenye mkataba wa mkopo. Kama, kwa mujibu wa mkataba wa mkopo, kiwango cha riba kinaweza kubadilishwa kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mkopaji, basi benki inaweza kubadili kiwango cha riba. Kwa ujumla, kama kuna riba inayobadilika, lazima ielezwe wazi kwenye mkataba kuwa, benki itamweleza mkopaji katika namna ambayo anaweza kuelewa kirahisi, kiwango kipya cha riba, muda wa kuanza kutumika, mabadiliko yoyote juu ya kiasi kinachopaswa kulipwa, na tarehe ya kuanza kulipa na mbadala wowote wa viwango vipya, kama mkataba wa mkopo unataka hivyo.

Hivyo, sheria inaruhusu mabadiliko ya kiwango cha riba kama mlikubaliana hivyo. Hata hivyo, kwa kuwa unasema ulishtuka kuona viwango vya riba vikibadilika, tunachukulia kuwa haukupewa taarifa za mabadiliko hayo. Kama hivyo ndivyo, una nafasi nzuri ya kupinga ongezeko la viwango vya riba.

Kwa tahadhari, angalia vizuri taarifa zako za kibenki, ingawaje tunaamini mabadiliko ya viwango vya riba yanaweza kuwa kwa faida yako. Kama hivyo ndivyo benki inaweza kukubishia juu ya makato hayo!

## Hati/Notisi ya Madai kutoka Benki

**Nilikopa benki na kuweka mali yangu kama dhamana ambayo ina hati ya rehani/poni iliyosajiliwa. Biashara yangu haifanyi vizuri**

**na niko nyuma katika kufanya marejesho kwa miezi sita tu. Benki imeniletea hati/ notisi ya madai yenye maneno makali/ vitisho kwa kutorejesha fedha hizo kwa wakati, ikisema kwamba watachukua hatua zaidi ikiwa sitalipa. Je, kisheria barua hiyo ina madhara gani? Je, nina kesi yoyote dhidi ya benki? Nifanyeje?**

*29 Novemba 2010*

Kuna ukweli usiopingika hapa. Umekopa pesa na haujalipa. Una mkopo na benki ina dhamana yako ikiwa utashindwa kulipa. Kwa mtazamo wa benki si 'miezi sita tu'. Miezi sita kwa benki ni muda mrefu sana kwa kuwa watu wanaoweka fedha benki hawawezi kusubiri kipindi chote hicho wala hawawezi kukubali sababu zako.

Umuhimu wa barua hiyo kisheria ni kwamba inaweza kufuatiwa na notisi ya kisheria chini ya kifungu cha 127 cha Sheria ya Ardhi ambacho kinakupa siku sitini tu kulipa mkopo au wauze dhamana/poni husika. Hatuna uhakika ni sababu gani utazitoa mahakamani ili itoe amri ya kuzuia uuzaji wa mali yako, kwani umeshakiri kuwa haujalipa. Kulipa deni kwa wakati ni kitu muhimu sana kwenye mkataba wa mkopo, na umeshakiuka.

Ushauri wetu ni ama ulipe kiasi kilichobaki au jaribu kuweka mikakati mipya ya ulipaji wa mkopo au vinginevyo zungumza na benki nyingine ambayo itakuwa tayari kuchukua mkopo wako kwa dhamana ile ile uliyoweka. Kushindwa kufanya chochote kati ya hayo yaliyoelezwa hapo juu kutapelekea dhamana husika kuuzwa. Kwa bahati mbaya, hakuna pesa za bure hasa kutoka benki.

## Kunichungulia Nyumbani kwangu

**Nimekuwa nikiishi katikati ya Jiji kwenye nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa kipindi cha miaka kumi na tano. Hivi karibuni hoteli ya ghorofa kumi imejengwa karibu na jengo letu. Kuna chumba kimoja katika hoteli ambacho kinakaliwa na meneja wa hoteli na familia yake, na madirisha yake daima yako wazi. Wanaweza kuniona kupitia dirisha langu wakati ninabadili nguo. Je, hii si kinyume cha sheria? Ninawezaje kuwazuia kufanya hivyo? Haki zangu ni zipi?**

*15 Novemba 2010*

Kwanza kabisa hakuna sheria ambayo inaweza kuzuia meneja wa hoteli kufungua na kuacha dirisha lake wazi. Hatuna uhakika ikiwa unauliza kuhusu uhalali wa familia ya meneja wa hoteli kukuchungulia kupitia dirisha lako au hoteli kujengwa karibu na jengo lenu. Kwa vyovyote vile, ni vigumu mahakama kukubali maombi yako kumzuia meneja kuacha dirisha lake wazi. Jengo hilo limejengwa kwa kibali halali cha ujenzi, na mambo yote, ikiwa ni pamoja na umbali kati ya majengo, huzingatiwa wakati wa kutoa kibali cha ujenzi. Unahitaji kushauriana na mwanasheria wako ili kuona kama kuna sababu nyingine yoyote ambayo haujaeleza ambayo unaweza kuitumia dhidi ya mmiliki wa hoteli au msimamizi wa hoteli.

Tunashauri pia kwamba kawaida wakati wa kubadilisha nguo, mapazia huwa yanafungwa. Unaweza kufanya hivyo pia.

## Benki inadai kupitia Hati ya Udhamini binafsi

**Miaka michache iliyopita rafiki yangu alikuwa akikamilisha taratibu za kuchukua mkopo benki mkoani Mwanza. Meneja wa benki ambaye tulikuwa tukifahamiana wakati huo alimwambia akope chini ya udhamini wangu binafsi kwa kuwa benki ilikuwa inanifahamu vizuri. Nilisaini dhamana bila kujiridhisha. Rafiki yangu amekiuka masharti ya mkopo, na benki inanidai. Hata sauti ya meneja wa benki imebadilika wakati akizungumza na mimi. Sikukopa fedha, wala sikuzitumia. Rafiki yangu alipoteza fedha kihalali kwenye biashara ya dhahabu, na benki inanifuatilia. Kwa kweli, wiki chache zilizopita, benki hiyo**

**ilijaribu kunizuia kuchukua fedha kwenye akaunti yangu ya kampuni, ingawa baadaye waliniruhusu. Hali hii inaniogopesha sana. Je, nifanye nini? Je, wanaweza kuuza nyumba yangu ya ndoa/familia?**

*8 Novemba 2010*

Ni ukweli usiopingika kuwa mara zote sauti za mameneja wa benki hubadilika wakati mteja anaposhindwa kulipa! Tunahitaji kusoma masharti ya dhamana ili kuelewa ulichodhamini na kwa kiasi gani. Hata hivyo, jambo moja liko wazi, kuwa chini ya hati yako ya udhamini binafsi, benki haiwezi na haipaswi kutumia pesa zilizo kwenye akaunti ya kampuni kulipia deni/mkopo, ambayo tunaamini ni kampuni yenye dhima ya kikomo. Kisheria, kampuni yako na wewe ni watu wawili tofauti. Kama watajaribu kufanya hivyo tena, unaweza kuishtaki benki na kudai fidia.

Dhamana nyingi binafsi zinakuwajibisha wewe binafsi kulipa kiasi ambacho hakijalipwa na mkopaji. Wakati wa kusaini, ulipaswa kusoma hati ya dhamana. Ni vigumu sana kukataa dhamana hiyo wakati huu.

Kuhusu benki kutaka kuchukua nyumba yako ya ndoa/familia, itategemea na maneno yaliyotumika kwenye mkataba wa udhamini. Nyumba ya ndoa ni mali nyeti sana na uuzwaji wake huathiri watu wengi, ikiwa ni pamoja na watoto wako. Wakati benki inaweza kuchukua mali zako muhimu, nyumba yako, haitakuwa rahisi kwake kufanya hivyo, kwa kuwa mke anaweza kuwa hakuwahi kutoa idhini ya kuwekwa rehani. Kwa vyovyote vile, unahitaji kuwasiliana na mwanasheria wako.

## Benki inadai Bima ya Maisha

**Ninakaribia kukopa Dola za Marekani milioni 8 kwenye benki moja hivi Dar es Salaam. Benki inataka pia niwape bima yangu ya maisha kwa thamani hiyo hiyo. Ninashindwa kuelewa kwa nini wanataka hivyo, kwa kuwa mkopo tuliokubaliana ni zaidi ya Dola za Marekani milioni 11. Je, bima yangu ya maisha ni muhimu? Je, nifanye nini?**

*8 Novemba 2010*

Benki inajaribu kulinda maslahi yake. Kampuni yako inaweza kuwa ni ya mtu mmoja au wewe ni mtu muhimu sana kwenye hiyo kampuni, na ikiwa utafariki, benki inahisi kwamba haitalipwa deni lake lote.

Kuna vitu tunahitaji kukuelewesha. Kwanza, thamani ya bima si lazima iwe kiasi kamili cha mkopo. Dhamana uliyoweka benki inatosha kwa benki kulinda mkopo wake, na hivyo basi unaweza kujadiliana na benki juu ya kiwango cha chini cha bima ya maisha.

Pili, unaweza kujadiliana na benki juu ya anayelipa tozo/ada ya bima. Ikiwa benki iko tayari kuchangia, kitu ambacho baadhi ya benki zinakubali, inaweza kukupa unafuu. Kuweka bima ya maisha sio wazo baya - unachohitaji kuangalia ni jinsi unavyoweza kupunguza tozo/ada unayolipa kwenye bima. Mwisho, inategemea na jinsi ambavyo utazungumza na benki. Utaratibu huu ni wa kawaida kwenye soko, hasa kwa mikopo mikubwa na ndiyo maana hatushangazwi kuona benki inahitaji bima hiyo.

## Upasuaji umecheleweshwa, Mtoto amekufa

**Mke wangu alikuwa katika chumba cha kujifungulia katika hospitali kubwa na mpya jijini Dar es Salaam. Tuliingia kwenye wodi ya wazazi saa 12:25 jioni siku ya Jumamosi na tulihudumiwa na mkunga. Mke wangu alipelekwa mara moja kwenye chumba cha kujifungulia. Mnamo saa 3 usiku mapigo ya moyo ya kijusi yalianza kushuka na muuguzi wa zamu alitumia simu yake kumbipu daktari kwa sababu hakuwa na salio. Daktari hakumpigia. Saa 3:05 usiku, muuguzi alitumia simu yangu kumpigia daktari, ambaye alijibu kwamba alikuwa**

**mbali sana na kwamba muuguzi anapaswa kumwita daktari mwingine, ambaye hakuwa zamu. Daktari mwingine hakupokea simu ingawa iliita sana. Hivyo tukajaribu kumpigia tena simu daktari aliyekuwa zamu, simu yake ilikuwa imezimwa. Muda wote huo mke wangu alikuwa kwenye chumba maalum akisubiri daktari wa upasuaji. Wakati huo huo mapigo ya moyo wa kijusi yaliendelea kushuka. Kama saa 3:45 usiku, muuguzi aliamua kumwita mpasuaji mkuu wa zamu ambaye alielekeza kuwa mke wangu ahamishiwe haraka kwenye chumba cha upasuaji na kwamba atafika ndani ya dakika ishirini. Kwa sababu ilikuwa ni siku ya Jumamosi usiku, hakukuwa na wauguzi na wahudumu wengi zamu, hivyo tulimsaidia muuguzi kusukuma kitanda kwenda chumba cha upasuaji. Baada tu ya kufika saa 4 usiku, mpasuaji mkuu alifika, alikimbilia chumba cha upasuaji na akamfanyia upasuaji (wa kujifungua) mke wangu. Mtoto wa kike mzuri alizaliwa. Baada ya muda Daktari wa upasuaji alitoka na kutueleza kwamba mtoto hakuwa wa kawaida na kwamba anatakiwa kuwekewa oksijeni usiku huo. Mtoto huyo alikufa saa 10:45 alfajiri siku iliyofuata. Nilifanya utafiti kwenye mtandao na kupata ukweli fulani. Kwanza, dharura ilikuwa kwa sababu kitovu kilichomoza, kama daktari wa zamu angefika kwa wakati, ingeokoa maisha ya binti yangu. Pili, mke wangu alikuwa amelazwa chali, kichwa chini kidogo na miguu juu wakati akisubiri daktari, hivyo kuthibitisha kuwa kitovu kilichomoza. Muuguzi na madaktari walijaribu kutushawishi kuwa yalikuwa ni mapenzi ya Mungu na kwamba inawezekana mtoto angekufa tu, lakini ninaamini kwamba hospitali inawajibika kwa hili. Pia inaonesha kwamba daktari ambaye alikataa kuja haishi mbali na hospitali na alikuwa anapaswa kuwa zamu siku hiyo. Nimepoteza binti yangu kwa sababu ya uzembe wa hospitali – hawezi kuwa nasi tena. Ninataka kuchukua hatua dhidi ya hospitali hii ili kuhakikisha kuwa hili halitokei kwa mtu mwingine tena. Je, nifanye nini?**

*25 octoba 2010*

Tunafurahi kusikia kwamba hukubaliani na kauli isiyo na msingi ya wafanyakazi wa hospitali kwamba kifo cha mwanao kingeweza kutokea kwa vyovyote vile. Muuguzi na daktari ambaye alikuambia hilo labda angesomea utabiri na si utabibu.

Ni dhahiri kwamba hospitali na/au wataalamu wa afya walikuwa wazembe kwa jinsi walivyoshughulikia zoezi zima la kujifungua. Kujifungua ni kitendo cha hatari kwa mama na mtoto, ndio maana watu huenda kujifungulia hospitali na si nyumbani.

Katika kesi yako, na kutokana na maelezo uliyotupa katika swali lako, ni dhahiri kwamba hospitali na ma/daktari wanawajibika kwa kifo cha mtoto wako. Lazima ujiulize maswali matatu: Je, hospitali ilikuwa na wajibu wowote kwa mkeo? Jibu ni ndiyo. Pili, Je, madaktari na/hospitali wamevunja wajibu huo? Jibu ni ndiyo – kwa kuwa ni hospitali inayohudumia wajawazito ilipaswa kuwa na daktari wa upasuaji ambaye yuko zamu, na daktari huyo wa upasuaji lazima aitikie wito husika kwa wakati. Mwisho, je, uzembe huo ulipelekea kifo cha kichanga? Jibu ni ndiyo.

Tunaamini una nafasi nzuri ya kufanikiwa na hupaswi kushtaki tu hospitali bali pia daktari ambaye hakuonekana. Unapaswa pia kuwajumuisha watu wengine ambao unafikiri walikuwa na wajibu.

## Muuzaji alibadilisha Sampuli

**Mimi ni meneja ununuzi wa shule, nimekuja Dar kununua vifaa mbalimbali kwa ajili ya maabara yetu ya sayansi. Moja ya vitu nilivyopaswa kununua ilikuwa ni dazani moja ya mizani, ambayo sampuli zake niliziona na kuzikubali. Muuzaji aliahidi kuniletea vitu hivyo shuleni huko Lushoto. Siku kumi baadaye, bidhaa ilipoletwa, mizani**

**ilikuwa tofauti kabisa na ile aliyonionesha. Je, hili si kosa?**

*13 Desemba 2010*

Sheria ya Ushindani inatamka wazi kwamba kama kuna mkataba wa kusambaza bidhaa kwenda kwa mnunuzi/mteja, pia kuna kipengele kwenye mkataba, kilicho wazi au fiche, chenye kutamka kuwa bidhaa husika zinauzwa kwa kuzingatia sampuli iliyooneshwa. Zaidi, kuna masharti fiche kuwa, mzigo ni lazima uendane na ubora uliooneshwa kwenye sampuli, na mnunuzi atakuwa na nafasi ya kulinganisha kama mzigo alionunua unaendana na sampuli na kwamba mzigo haupaswi kuwa na kasoro zozote ambazo zitafanya bidhaa husika kutokuwa na ubora wa kuuzika, na ambazo zinaweza kuwa hazionekani baada ya kufanya ukaguzi wa kawaida wa sampuli.

Kwa hiyo unaweza kumchukulia hatua muuzaji chini ya kifungu hiki cha sheria.

## Kinyozi amenyoa Nywele zangu zote

**Je, ninaweza kumfanya nini kinyozi ambaye amenyoa kwa makusudi masharubu yangu niliyoyafuga kwa kipindi cha miaka kumi? Na vipi kama ameweka bango linalosema kinyozi hawajibiki kwa madhara au kasoro zozote zitakazotokea? Je, hiyo inabadili msimamo wenu?**

*25 Octoba 2010*

Hatuna uhakika kama ni kweli kinyozi amenyoa masharubu yako au unauliza tu swali kupata ufahamu wa kawaida. Sisi sote tumewahi kwenda kwa vinyozi nchini Tanzania na hatujawahi kuona bango linalosema 'kinyozi hawajibiki kwa madhara au kasoro zozote zitakazotokea'!

Kukiwa na mkataba wa kutoa huduma, kuna vipengele huchukuliwa kama ni sehemu ya mkataba hata kama havijawekwa. Na kipengele cha namna hiyo kwenye mkataba wenu wa kunyoa nywele au masharubu, ni kutumia ujuzi kutoa huduma nzuri na kwa uangalifu. Kila mtoa huduma awapo kwenye shughuli zake za kila siku anawajibu fiche kuwa atatumia ujuzi kutoa huduma nzuri na kwa uangalifu.

Katika kesi yako, kinyozi hajatumia ujuzi wala hakuwa makini na unaweza kumshtaki. Hii inatuleta kwenye sehemu ya pili ya swali - je, bango/taarifa hiyo inamwondolea kinyozi wajibu kutumia ujuzi na kuwa mwangalifu? Jibu letu ni hapana.

## Dawa isiyofaa kutoka kwa Mfamasia

**Niliandikiwa dawa na daktari wangu, na kisha kupewa dawa tofauti na mfamasia. Ikapelekea kiwango cha sukari kuwa juu, sikuweza kwenda kazini kwa muda mrefu na kuteseka sana. Mmiliki wa famasi aliniomba msamaha. Je, nimsamehe?**

*18 Octoba 2010*

Hatuna uelewa juu ya 'kutoa' msamaha na hatujui kama tuna sifa ya kukushauri katika hili. Kama wanasheria, tuna hakika juu ya jambo moja tu - una kesi nzuri dhidi ya mfamasia na famasi. Unaweza kuwashtaki pamoja. Unaweza kudai fidia japo nchini Tanzania hatuna mifano mingi kama nchi nyingine zilizoendelea kuhusu suala lako, lakini kesi yako ni nzuri na una nafasi ya kushinda. Usiogope kuwashtaki wataalamu kwa kuwa inasaidia kuufanya mfumo ufanye kazi vizuri.

## Ukomo wa kupanga baada ya Kifo cha Mume wangu

**Mimi ni mjane mwenye watoto watatu. Mume wangu amefariki hivi karibuni na kutuacha katika nyumba ya kupanga inayomilikiwa na shirika fulani la umma. Tumeishi kwenye nyumba hii kwa takribani miaka ishirini na daima tulikuwa tukilipa kodi kwa wakati. Cha kushangaza, mume**

**wangu alivyofariki, mwenye nyumba ametutaka tuhame, akidai kuwa aliyesaini mkataba wa kupanga ameshafariki, hivyo mkataba umekoma. Je, madai haya yana maana kisheria? Je, nifanye nini?**

*18 Octoba 2010*

Kutokana na maelezo yako, na kwa kuangalia sheria, labda kama muda wa kodi umeisha au hamkulipa kodi, kitendo cha mwenye nyumba ni kinyume cha sheria. Kifo hakiwezi kusitisha makubaliano ya upangaji - hatudhani kama mkataba wa upangaji ulikuwa na kipengele hicho na hata kama kingekuwepo, mngeweza kukipinga. Kwa kawaida kama mume amefariki, mke anaweza kuendelea na mkataba ikiwa mke alikuwa akiishi kwenye nyumba hiyo hiyo kabla ya kifo cha mumewe ilimradi tu baada ya kifo cha mume unaendelea kufuata vigezo na masharti ya upangaji ikiwemo kulipa kodi kwa wakati. Kitendo cha mwenye nyumba kinapaswa kulaaniwa. Hata hivyo unatakiwa kusoma mkataba huo kwa ukamilifu ili kuhakikisha kuwa hakuna vikwazo vingine ambavyo vingeweza kusababisha mkataba kusitishwa. Ikiwa mwenye nyumba haelewi unaweza kufungua shauri mahakamani. Tunakushauri kuwasiliana na mwanasheria wako.

## Mmiliki mpya hataki kuendelea na Mkataba

**Nimekuwa nikiishi kwenye nyumba kubwa na ya kisasa eneo la Oysterbay kwa muda wa miaka mitatu. Mwenye nyumba aliuza nyumba hiyo kwa mtu mwingine ambaye hayuko tayari kuongeza muda wa mkataba kwani anataka kuibomoa na kujenga mpya. Je, mkataba wangu wa upangaji unamhusu mmiliki mpya? Kwa nini asingenipa nafasi ya kununua nyumba hiyo kabla ya kumuuzia mtu mwingine? Je, nifanye nini? Je, hii si kinyume na sera za nchi?**

*18 Octoba 2010*

Jibu letu kwa swali hili haliwezi kukufurahisha.

Kulingana na barua yako, mnunuzi alinunua nyumba wakati wewe umepanga na kwa hiyo anafungwa na mkataba wa upangaji, na yeye ni mwenye nyumba wako mpya. Kama mkataba umefika ukomo na hataki kuongeza muda mkataba, huwezi kufanya chochote.

Pia hakuna sheria inayomlazimisha mwenye nyumba kumuuzia nyumba mpangaji wake isipokuwa labda kama kulikuwa na kipengele maalum cha namna hiyo kwenye mkataba kinachosema hivyo, kitu ambacho hatukioni kwenye mkataba wako.

Vile vile hakuna sera ya nchi inayokulinda. Sheria inapenda kuwepo na majengo mapya ili kuondoa changamoto ya makazi. Kinyume chake ni sahihi - kuzuia ujenzi ni kwenda kinyume na sera ya nchi.

Tunakushauri kuonana na mwanasheria wako ili kuona kama kuna njia mbadala.

## Mkopo kulipwa Wanapotaka

**Niko kwenye hatua za mwisho za kukopa dola milioni 2 kwenye benki kubwa nchini Tanzania. Nyaraka moja inasema kwa uwazi kwamba ikiwa ombi langu litakubaliwa, nitalazimika kulipa mkopo wanapohitaji. Nilizungumza na benki, wakadai huu ni utaratibu wa kawaida na kwamba kila mtu hapa mjini ambaye amewahi kukopa amesaini waraka kama huo, hata wale ambao wamekopeshwa makumi ya mamilioni, na kwamba mimi, kama 'mkopaji mdogo/samaki mdogo' siwezi kuishawishi benki kuandaa upya nyaraka hizo. Je, hii ni kawaida?**

*11 Octoba 2010*

Aina hii ya mkopo mnaojadiliana na benki unaonesha ni mkopo unaolipwa kila inapohitajika. Nyaraka za dhamana za benki, makubaliano ya kulipa, mara nyingi huwa ni 'lipa inapohitajika'. Hii ina faida kwa benki

kwani Sheria ya Ukomo wa Mashtaka haiwezi kuwabana hadi wahitaji kulipwa. Vinginevyo mkopo wa muda maalum usingekuwa na maana kama wakiondoa kipengele hiki kwa kuwa uwekezaji wako ni wa muda mrefu. Kitu pekee ambacho unatakiwa kusisitiza ni kwamba madai ya pesa yote yafanywe muda wa kulipa mkopo ukifika.

Maoni ya benki kwamba wengine wamesaini nyaraka kama hizo hayana msingi wowote. Jambo la kushangaza ni benki kutumia maneno 'samaki wakubwa/matajiri na samaki wadogo/kipato cha kawaida'. Nyaraka zote za mkopo zinapaswa kusomwa, kueleweka, na kujadiliwa na kisha kusainiwa na kugongwa mhuri na wewe mwenyewe. Hamu yako ya kutaka kuanza mradi haraka haraka kwa mkopo, isikushawishi kusaini chochote unacholetewa - unaweza baadaye kujutia.

## Kamari 'Karata Tatu/Kekundu'

**Kituo cha Polisi kilikataa kupokea na kuyafanyia kazi malalamiko yangu dhidi ya mcheza kamari ' karata tatu ' ambaye alinilaghai na kuchukua shilingi 10,000 wakati wa mchezo. Polisi walikataa kuchukua hatua hata baada ya kusisitiza kwamba mtuhumiwa bado alikuwa sehemu ya tukio, wanasema nimepoteza fedha kwa upumbavu wangu. Je, jibu la polisi linakubaliwa? Je, mchezo huu ni halali kisheria?**

*11 October 2010*

Labda ulikuwa ukicheza mchezo huu sehemu ambayo haina kibali, hivyo kufanya aina hii ya kamari/bahati nasibu kuwa kinyume cha sheria. Polisi walipaswa kuchukua hatua dhidi ya 'mkosaji', lakini pia wangeweza kuchukua hatua dhidi yako. Una bahati sana kwa kuwa wote wawili mlipaswa kukamatwa. Wakati mwingine watu ambao wanaenda polisi kulalamika huishia Kukamatwa wenyewe - polisi wana uwezo wa kufanya hivyo. Kuwa wa kwanza kulalamika polisi hakukuondolei hatia.

## Utaratibu wa Kujitetea kwenye Shauri la Haraka

**Nilinunua gari shilingi milioni 20 na kutoa hundi yenye tarehe ya mbele. Baada ya kutoa hundi, nilipewa gari, ambalo nilianza kulitumia. Muuzaji aliwasilisha hundi benki lakini haikulipwa kwa sababu benki hawakuwa na fedha ya kulipa. Muuzaji hakuridhika na kunifungulia shauri la haraka akidai, miongoni mwa mambo mengine, arudishiwe fedha yake ya manunuzi pamoja na fidia. Sina utaalamu wa sheria na wala sijui kama hili ni kosa. Tafadhali naomba ushauri mzuri.**

*4 Oktoba 2010*

Katika kujibu swali hili, tunadhani kwamba si kweli kuwa benki haikuwa na hela bali akaunti yako ndiyo haikuwa na hela ya kulipa.

Shauri la haraka (summary proceedings) kwa kawaida linahusu kesi ambazo zinahitaji hatua za haraka kuchuliwa na kwa ujumla uhusisha masuala madogo madogo yaliyo wazi kama vile: kutolipa bili za huduma za umma, mkopo wa benki na hundi zilizokataliwa, kama ilivyo hapa.

Utaratibu wa kujitetea kwenye aina hii ya shauri si wa moja kwa moja - mlalamikiwa lazima aombe kibali mahakama husika ndani ya muda uliobainishwa kwenye wito wa mahakama/samansi, ili aweze kupata haki ya kujitetea. Maombi ya kibali cha kujitetea lazima yaambatane na kiapo ambacho kinaonesha ni mambo gani mlalamikiwa anamtaka mlalamikaji kuthibitisha kabla ya kupata maamuzi ya haraka.

Kwa ufupi, kiapo chako ni lazima kioneshe hoja za msingi ambazo zinahitaji utatuzi wa kisheria na kuiridhisha mahakama.

Katika swali lako, hujasema kwa nini hundi

ilikataliwa. Kama huna sababu za msingi za zinazohitaji utatuzi wa kisheria ni ngumu kufanikiwa, na mahakama inaweza kukataa maombi yako. Kama maombi yako ya kupata kibali cha kujitetea yakikataliwa, hukumu inaweza kutolewa dhidi yako.

Ushauri wetu kwako, ambao labda usingependa kuusikia – mlipe muuzaji haraka sana na uombe kuondolewa madai ya fidia.

Huhitaji kuwa mtaalamu wa sheria kujua matokeo ya kutoa hundi wakati ukijua kuwa akaunti yako haina fedha ya kutosha - hili ni kosa la jinai lijulikanalo kama 'kurusha tiara' (kite flying)na unaweza kufungwa.

## Kutolewa kwenye Mashindano ya Urembo Tanzania

**Nina umri wa miaka 23 na nimeolewa nilitaka kushiriki katika mashindano ya urembo Tanzania mwaka jana, lakini ombi langu lilikataliwa kuwa nimeolewa. Nina sifa zote kuwa mrembo wa Tanzania na sitaiangusha nchi yangu kama wawakilishi waliokwisha tangulia katika mashindano ya urembo Tanzania. Je, kanuni inayozuia wanawake walioolewa kushiriki mashindani ya urembo si ya kibaguzi? Nataka kushiriki katika mashindano hayo – mnanishaurije?**

*20 Septemba 2010*

Ingawa tunasikitika kukataliwa kwako kushiriki, lakini hatuoni ubaguzi wowote hapo. Ni kweli kwamba kutokuwachukulia watu wote kwa usawa wakati hakuna tofauti zozote baina ya wale waliopendelewa na wale wasiopendelewa ni kinyume cha sheria, kwenye suala lako hatuoni kuwepo kwa ubaguzi huo.

Kama yalivyo mashindano mengine, waandaaji wa mashindano ya urembo wa Tanzania wana uhuru wa kuandaa kanuni zao na kubainisha sifa za washiriki kwenye mashindano. Ni kweli, unaweza kuwa mzuri na unaweza kufanya vizuri kuliko warembo waliotangulia, lakini waandaaji hawawezi kupindisha taratibu zao ili kukupa upendeleo wewe. Kukataliwa kwako kushiriki kungeoneonekana tofauti kama kanuni zingeruhusu wanawake walioolewa, na wewe ukakataliwa.

Kama bado una wito wa kushiriki kwenye mashindano ya urembo, unaweza kutafuta mashindano mengine yanayoruhusu wanawake walioolewa kushiriki, labda Bi. Tanzania. Kwa jibu letu hili kwako, hatumaanishi kuwa wanawake walioolewa si wazuri kama wanawake ambao hawajaolewa. Yote kwa yote, kama msemo wa Kigiriki wa karne ya 3 usemavyo, uzuri upo machoni pa mtazamaji.

## Masharti ya Mkataba nyuma ya Risiti

**Nilipanda basi kutoka Morogoro kwenda Mwanza. Nilipofika mwisho wa safari yangu, niliona moja ya vitu muhimu kwenye moja ya mabegi yangu matano vimeharibiwa kabisa na maji. Baadhi ya vitu vilikuwa vya kielektroniki na vya thamani kubwa. Nilitoa taarifa kwenye ofisi ya kampuni ya mabasi lakini niliambiwa kuwa kulikuwa na taarifa/notisi nyuma ya risiti kuwa kampuni ya basi ilikuwa haina dhamana kwa uharibifu wowote au hasara ya mizigo. Hata hivyo, mimi sikupewa risiti, nimepewa tu tiketi ya safari. Je, kampuni ya mabasi inaweza kujiwekea ukomo wa kuwajibika kwake kwa kuweka sentensi moja tu kwenye risiti namna hii? Sikuweza hata kuona/kusoma nyuma ya risiti hiyo? Je, kuna kitu naweza kufanya?**

*9 Agosti 2010*

Sheria inasema wazi kwamba kama mtu au kampuni inataka kujiondoa kwenye wajibu, inatakiwa kumtaarifu kwa uwazi kabisa mtu inayeingia naye mkataba kuhusu kujiondoa huko. Kwa suala lako haiwezi kuchukuliwa kama ulipewa hiyo taarifa ya kujiondoa

kwenye wajibu kwa kuwa hukutaarifiwa kabla ya kuanza safari. Zaidi ya hilo, masharti yalikuwa kwenye risiti, sio tiketi na kwa mazingira hayo kuna uwezekano mkubwa kwamba ulikuwa tayari umeshaingia mkataba wa usafiri. Tumeshawishika kuwa unaweza kufungua shauri dhidi ya kampuni na kudai fidia kutokana na uharibifu wa mali zako.

## Ununuzi wa Gari kwenye Mtandao

**Nataka kununua gari kupitia mtandaoni (internet) kwa sababu ni bei nafuu. Nilipata tovuti ambayo inauza magari, lakini wanataka malipo yote kabla ya kukupa gari. Je, kuna njia nyingine yoyote ya kulipa? Je, ninunue gari?**

*26 Julai 2010*

Kununua gari au la si suala la kisheria. Pengine jambo unalotaka kujua ni kama ni salama kununua gari kupitia mtandao.

Jibu la haraka ni hapana. Mambo mengi yanaweza kwenda vibaya/mrama - maelezo ya gari kwenye mtandao yanaweza kutofautiana na gari unayoletewa, au unaweza usipate gari kabisa. Tunajua kuna watu wachache ambao walipata magari bora kupitia mtandao; pia tumekutana na watu ambao walilipa kwenye mtandao na hawajawahi kupokea bidhaa hizo. Ni vigumu sana kuthibitisha uhalali/uwepo wa kampuni unayofanya nayo mawasiliano kwenye mtandao. Hata hivyo, haya ni maamuzi yako ya kibiashara. Tukutahadharishe kuwa mchakato wa kurudisha fedha iliyolipwa kupitia mtandao ni ngumu sana hasa pale ambapo haujui anwani ya mahali au utambulisho wa yule ambaye umefanya naye biashara.

Njia salama ya malipo ambayo inatoa ulinzi zaidi ni barua ya mikopo/dhamana ya biashara (letter of credit). Ikiwa bado una shauku ya kununua gari kupitia mtandao, tunapendekeza kuwasiliana na mabenki na kufanya mchakato wa kupata barua ya mkopo.

Kabla ya kufungua barua ya mkopo, unapaswa kuchunguza kama tovuti hiyo inapokea aina hiyo ya malipo au la.

## Uzembe wa Kitabibu na kusababisha Kifo

**Baba yangu alipelekwa kwenye chumba cha dharura cha hospitali ili kufanyiwa upasuaji. Aina ya damu yake ilikuwa kundi A na kwa makosa ya wahudumu wa afya walimpa kundi B. Wakati tukiwa kwenye chumba cha kutunzia damu/benki ya damu, niliendelea kusisitiza kwa muuguzi kuwa hospitali hiyo inafanya makosa, lakini muuguzi alikuwa na uhakika wa matokeo ya damu na kundi husika kutoka maabara. Baadaye waligundua kwamba maabara walitumia vitendanishi ambavyo havikuhifadhiwa vizuri. Kutokana na uzembe wa hospitali baba yangu alifariki saa chache baada ya upasuaji. Je, naweza kushtaki na kuidai hospitali?**

*19 Julai 2010*

Mwenendo mbaya katika utoaji tiba unahusisha mambo mengi zaidi ya matibabu kwenda vibaya. Kama unataka kushtaki na kushinda juu ya madai ya utendaji mbaya, unahitaji kuthibitisha mambo kadhaa ili kufaulu.

Mtoa huduma wako wa afya ana wajibu wa kisheria kwako kutokana na uhusiano wa daktari na mgonjwa. Sehemu ya wajibu huu ni kutoa huduma ambayo inalingana na viwango vya taaluma husika. Kushinda madai ya utendaji mbovu wa kitabibu, unahitaji kuthibitisha kwamba daktari hakutoa huduma kwa kiwango cha ubora kinachotakiwa

Ingawa si rahisi kuthibitisha utendaji mbovu wa kitabibu, inaonekana kama una ushahidi wa kutosha ili kuchukua hatua dhidi ya hospitali, madaktari na wauguzi. Kesi yako dhidi ya hospitali au daktari aliyeshughulikia matibabu, haiwezi kumfufua baba yako, lakini

hakika itasaidia kuboresha ufanisi katika hospitali hiyo.

## Kukataliwa kwa Madai ya Bima ya Maisha

**Miaka saba iliyopita, mume wangu alikuwa amekata bima ya maisha kutoka kwa kampuni binafsi. Alikufa mwezi Septemba mwaka jana baada ya kuruka kutoka kwenye gari iliyokuwa katika mwendo kasi. Awali kampuni ya bima ililipa gharama za mazishi na kuonesha dalili zote kwamba wangeweza kulipa madai mengine ndani ya siku tisini. Nimepewa taarifa kwamba hawatalipa. Je, nifanye nini? Je, naweza kuishtaki kampuni ya bima?**

*28 Juni 2010*

Haujatoa sababu za kukataliwa madai hayo, lakini kuna kitu tumegundua katika swali lako. Kwa nini mume wako aliruka kutoka katika gari linalotembea? Nini kilisababisha hatua hiyo? Kama alijiua, madai hayatalipwa. Katika kila bima ya maisha, kuna kifungu kinachoondoa 'kujiua' kwenye ulinzi wa bima, au kuweka ukomo wa uwajibikaji wa kampuni, kwa kiwango sawa na tozo/ada zilizokwishalipwa. Ukweli kwamba kampuni ya bima ililipa gharama za mazishi, hakuwezi kutafsiriwa kuwa imekubali madai husika. Tunapendekeza kuwa ukutane na wakili wako ambaye atakuongoza hatua kwa hatua kabla ya kukimbilia mahakamani.

## Nahitaji kurudishiwa Fedha yangu

**Nililipia chumba mapema katika moja ya hoteli mjini Mbeya ambapo nilitakiwa kuhudhuria semina ya siku saba. Hata hivyo, kutokana na sababu ambazo hazikuelezwa mratibu wa semina aliahirisha semina husika, na hivyo sikuweza kwenda Mbeya. Mmiliki wa hoteli hataki kunirejeshea fedha nilizolipia. Je, nifanye nini ili kurejesha fedha yangu, kwa kuwa sikutumia huduma?**

*14 Juni 2010*

Mkataba wako ulikuwa ni wa kununua huduma ya chumba. Kwa kawaida, mteja anaponunua huduma anawajibu wa kulipia mkataba wa huduma. Kwa hiyo kama ulikodi chumba huwezi tu kirahisi na ghafla kuamua kusitisha, na kisheria, mmiliki ana haki ya kutokurudishia fedha yako na anaweza hata kukushtaki kwa kumtia hasara kama anaweza kuthibitisha kwamba alipata hasara zaidi kutokana na kutofika kwako. Katika kesi yako, inategemea namna gani ulitoa taarifa mapema juu ya kusitisha kwako kwa mmiliki wa hoteli na masharti husika. Kutokana na maelezo yako, hakuna uwezekano kwamba unaweza kufanikiwa katika shauri lako dhidi ya mmiliki wa hoteli. Unaweza pia kufikiria kumshtaki mratibu wa semina, lakini hiyo itategemea na vigezo na masharti ya semina/mwaliko husika.

## Waranti ya Bidhaa haikutiliwa maanani

**Mimi ni fundi cherehani kwenye kiwanda cha ushonaji Manispaa ya Tabora. Mnamo Septemba 2009, nilinunua cherehani nne kwenye mojawapo ya maduka jijini Dar es Salaam, nilipewa risiti halali na waranti ya miezi sita. Mwezi mmoja baadaye niligundua kwamba baadhi ya cherehani zilikuwa mbovu. Kwa sababu ya muda uliokuwa umebaki kwenye waranti, niliwasiliana na muuzaji kwa ajili ya matengenezo au kupewa cherehani nyingine. Lakini muuzaji alijibu kuwa wamesitisha uuzaji wa aina hiyo ya cherehani! Je, hii si uvunjaji wa mkataba? Je, kwa mujibu wa waranti, ninaweza kurudishiwa gharama ya usafiri kama nitarudisha cherehani Dar? Je, ninaweza kulipwa fidia kutokana na hasara niliyopata?**

*21 Juni 2010*

Kamusi ya Kiingereza neno "Warranty" inaielezea kama ni hakikisho la kisheria kwamba huduma au bidhaa pamoja na mambo mengine inafaa kwa matumizi, haina kasoro yoyote kutoka kwa mtengenezaji na

inakidhi vigezo vya kisheria. Kwa kawaida, waranti inaeleza hali na muda muuzaji anaweza kakarabati/kurekebisha, kubadilisha au kufidia ununuzi wa bidhaa mbovu pasipo mnunuzi kuingia gharama yoyote.

Katika suala lako, ni dhahiri uko ndani ya muda wa ukomo wa waranti. Unahitaji kusoma zaidi masharti ya udhamini kuona ni vitu gani vinavyozungumziwa kwenye waranti. Kimsingi, sababu uliyopewa na muuzaji wa cherehani juu ya kusitisha uuzaji wa cherehani husika haina msingi wowote na inaweza kupingwa kirahisi tu. Una kesi nzuri juu ya hili.

Kama waranti inatoa fidia kwa ajili ya usafiri wa kurudisha mzigo kwa muuzaji itategemea na maneno/masharti ya waranti. Kwa kawaida hasara ya biashara huwa si sehemu ya waranti, lakini inaweza kudaiwa, itategemea na jinsi ambavyo wakili wako ataelewa/atalichukulia jambo hili.

## Makubaliano ya Kukodi na Kununua

**Januari 2009, nilikodi pikipiki ya magurudumu matatu ijulikanayo kama bajaji kutoka kampuni moja jijini Dar es Salaam, kwa makubaliano kwamba nitalipa kwa awamu sita zilizo sawa, baada ya malipo ya awamu ya mwisho bajaji itakuwa ya kwangu. Nililipa awamu tano na awamu ya mwisho ilitakiwa kulipwa mwishoni mwa mwezi Novemba 2009. Hata hivyo, nimegundua kwamba bajaji ni mbovu. Kampuni hiyo imepuuza madai ya ubovu wa bajaji, wanasema kuwa madai ni ya kutunga kwa maana nilikuwa na nafasi ya kukagua bajaji kabla sijaichukua. Kampuni inasisitiza kuwa ni lazima nilipe kiasi kilichobaki mara moja vinginevyo watanishtaki. Je, haki zangu ni zipi katika mazingira hayo? Nategemea kurudisha bajaji kwa kampuni hiyo na kudai fedha yangu.**

*7 Juni 2010*

Mkataba wako ulikuwa ni wa kukodi ambao una kipengele cha kununua ndani yake ambapo kampuni inakukodisha na baadaye kukumilikisha baada ya kuwalipa kiasi fulani cha fedha. Sheria inaipa kampuni wajibu wa kujua kwamba bajaji iko imara na madhubuti kwa ajili ya lengo lililokusudiwa. Kama uharibifu au hasara itatokana na baadhi ya kasoro katika uimara au umadhubuti wa bajaji kampuni itawajibika si tu kwa matokeo yaliyotokea bali pia kwa kukosa umakini. Kampuni pia itawajibika kulipa fidia kutokana hasara iliyotokana na kasoro za bajaji hiyo.

Kwa bahati mbaya, hatuwezi kujibu swali lako kwa usahihi sana kwani hatujui ni aina gani ya kasoro umezibaini. Kama ni kuharibika kwa kawaida au la, ikiwa ni uzembe wako, basi itakuwa vigumu sana kushinda kesi. Kwa upande mwingine, kama bajaji haikuwa na ubora sahihi kutoka kwa mtengenezaji, utetezi wa kampuni kwamba ulipewa nafasi ya kufanya ukaguzi wa awali wa bajaji kabla hujainunua, hautakuwa na maana kisheria. Kwa kuwa unajua ukweli halisi kuliko sisi, unaweza kuamua ni maelezo yapi hapo juu yanaendana na kesi yako.

## Kusitisha Bima

**Napenda kusitisha bima yangu, lakini wakala wa bima anasisitiza kwamba haitawezekana, lazima nisubiri mpaka bima itakapofikia kikomo. Je, huu ndio utaratibu Tanzania?**

*14 Juni 2010*

Bima yako ni sawa na mkataba mwingine wowote, ambapo kwa kawaida kuna kipengele cha kusitisha mkataba. Kwa uzoefu wetu wa soko la bima, mkataba wa bima unaweza kusitishwa, na mara nyingi hakuna kizuizi. Kwa upande wako, itategemea na masharti ya bima husika, ambayo tunakushauri ukayasome vizuri.

Pindi mteja anapojitoa katika bima, hawezi

tena kupata malipo ya bima na hata mwisho wa bima pia huwezi kurudishiwa ada zako na ndiyo maana huenda wakala wako amekuwa akisita kutokana na sababu hii, lakini jaribu kumdodosa/kuwasiliana naye tena.

## Mifugo kuharibu Uwanja wangu

**Jirani yangu hafungii mifugo yake (mbuzi) kwenye zizi lake. Matokeo yake, mbuzi wake hutoroka na kuingia kwenye bustani yangu na kuharibu mboga na kunisababishia hasara. Nilishalalamika kwake, lakini haoneshi ushirikiano. Pia nilishatoa taarifa kwa mamlaka husika (polisi na Serikali za mitaa), lakini inaonekana kuwa jirani anafahamika sana, hivyo anahurumiwa na polisi. Je, nina haki yoyote dhidi ya jirani yangu? Tafadhali nishaurini.**

*21 Juni 2010*

Kwa ujumla sheria inawataka wamiliki wa mifugo kuifungia katika eneo sahihi, ili mifugo yao isilete uharibifu au kuharibu mali za watu wengine au kuwajeruhi majirani. Kushindwa au kutotimiza wajibu huo, hufanya mmiliki wa mifugo kuwajibika, na bila kujali kama kutoroka huko kwa mifugo kumetokea kwa makusudi au kwa uzembe.

Katika hili, una kesi nzuri dhidi ya jirani yako kwa uharibifu wa bustani yako na mali nyinginezo. Unaweza pia kuwakamata na kuwahifadhi mbuzi hao, lakini kama utaamua kufanya hivyo, lazima uhakikishe kwamba unawahudumia vizuri kwa kuwapa chakula cha kutosha na maji. Ikiwa utaendelea kuwatunza na mmiliki hakuchukua hatua yoyote ya kuwakomboa unaweza kuwauza mbuzi na kuchukua baadhi ya mapato ya mauzo ili kufidia thamani ya bustani yako iliyoharibiwa na gharama nyinginezo, ikiwa ni pamoja na gharama zilizotumika kuwatunza mbuzi hao.

## Bei na Uhalali wa Mkataba

**Mwaka 2003, nilinunulia lori kwa bei ya shilingi milioni 5.6 kutoka kwa mwajiri wangu ambaye nilifanya kazi kwake kwa miaka kumi na tano kama dereva. Mwajiri wangu alifariki mwaka 2009, kwa sasa familia ya marehemu inajaribu kuvunja mkataba wa kuuziana lori kwa madai kuwa thamani ya lori ni kubwa kuliko bei niliyonunulia. Familia ameripoti suala hili polisi, ambao pia wanadai kuwa nimegushi sahihi ya marehemu. Je, nifanye nini?**

*24 Mei 2010*

Kwa kuwa mauzo yalikuwa kwa mkataba, tudhani kwamba ninyi nyote mlipata kile mlichokubaliana. Mahakama haiwezi kuingilia makubaliano ya kibiashara kati ya watu wanaotaka kuuziana mali zao, vinginevyo tungekuwa na misururu mirefu mahakamani! Jambo muhimu ni kwamba lori ni la marehemu, na ulilinunua kihalali kwa bei aliyoridhia. Kwa mtazamo wetu, bei ni thamani (ujira/malipo) ya lori, ambayo inatosha kisheria. Katika mikataba ya mauziano ya bidhaa, ujira si lazima utosheleze, isipokuwa unapaswa kutolewa kwa maridhiano ya pande zote mbili. Labda kama kuna jambo unatuficha, hatuoni namna ambayo familia inaweza kuvunja makubaliano hayo.

Kuhusu suala la kwenda polisi, sheria haimzuii mtu yeyote kutoa taarifa polisi kwa suala ambalo, kwa maoni yake, anaona kuna viashiria vya uhalifu. Waache polisi wafanye uchunguzi wao.

## Wafamasia ambao Hawajasajiliwa

**Mkoani Morogoro nusu ya wafanyakazi wa maduka ya dawa hawana sifa za kuwa wafamasia, lakini wanajifanya wafamasia. Je, hii si hatari? Je, hakuna sheria ambayo inaweza kuwazuia kujifanya wafamasia? Je, sio kwamba wanawadanganya watu?**

*10 Mei 2010*

Sheria ya Famasi imeweka Baraza la Famasi ambalo ni chombo pekee ambacho husajili

wafamasia nchini Tanzania. Baraza hili pia linasimamia mwenendo na kuweka viwango kwa wafamasia, linayo orodha ya wafamasia nchini kote na hutathmini viwango vya elimu ya wauza madawa. Hivyo sheria ipo.

Sheria ya Famasi inasema kwamba hakuna mtu mwingine yeyote zaidi ya wafamasia wenye sifa anaweza kutumia jina hili, au nembo yoyote au maelezo kuonesha kwamba yeye ni mfamasia. Aidha, sheria inasema kwamba, mtu yeyote ambaye anajifanya kuwa ni mfamasia, wakati sio, anafanya makosa na anaweza kutozwa faini ya shilingi milioni 2 au kifungo kisichozidi miaka miwili, au adhabu zote mbili pamoja.

Unaweza kuripoti suala hili kwenye Baraza la Famasi. Sheria inawataka wataalamu wote wa dawa za binadamu kujisajili kwenye Bodi ya Wafamasia.

## Kucheza Kamari Tanzania

**Mimi ni mtaalamu wa kigeni na nilikuwa nikiishi Mwanza mwaka uliopita. Miezi michache iliyopita, kwa mara ya kwanza kabisa, nilisafiri kwenda Mwanza kutoka Dar kwa njia ya barabara, nilikerwa sana kuona jinsi watu maskini wanavyocheza kamari maeneo mbalimbali kando ya barabara kuu. Kulikuwa na mashine nyingi za kamari na watu walikuwa wamejipanga kucheza. Je, sheria inaruhusu shughuli hii? Je, hakuna kizuizi cha umri, maana niliona hata watoto wadogo wakicheza kamari? Pia niliona kijana mdogo akizozana na mmiliki juu ya kiasi alichopaswa kulipwa. Pia ninaamini kwamba wamiliki wanawadhulumu washindi. Kwa kutilia maanani kuwa Tanzania ni moja ya nchi maskini zaidi duniani, huoni kwamba kamari inapaswa kupigwa marufuku?**

*10 Mei 2010*

Kamari ipo chini ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, ambayo huratibu mashine hizo. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, kucheza kamari nchini Tanzania si kinyume cha sheria. Mashine zote lazima zipate leseni kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, ambayo ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria hiyo. Pia Bodi hutoa leseni mbalimbali kwa kuzingatia aina ya mchezo wa kubahatisha.

Kuhusu watoto kucheza kamari, Sheria ya mchezo huo iko wazi sana kuhusu umri wa washiriki - umri wa chini ni miaka 18. Sheria inaweka kosa kwa mmiliki kuwaruhusu watu chini ya umri huu kukusanyika katika maeneo ya michezo ya kubahatisha, kuwepo wakati wa mchezo au kucheza mchezo wowote kati ya michezo hiyo. Sheria inasema wazi kwamba mtu yeyote ambaye atakiuka katazo hili anaweza kutozwa faini ya shilingi 500,000 au kifungo cha miezi mitatu, au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Sheria pia inakataza udanganyifu dhidi ya mshindi na imetoa faini ya shilingi milioni moja au kifungo cha mwaka mmoja au vyote viwili kwa pamoja. Masharti mengine ya Sheria hiyo ni pamoja na kunyang'anywa leseni na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha pale ambapo umekiuka Sheria, faini na adhabu ya kifungo kwa washiriki ambao wamefanya jaribio la kudanganya. Sheria pia inatoa misamaha kwa taasisi za kutoa msaada ambazo huendesha bahati nasibu ili kuchangisha fedha, lakini wanapaswa kutumia au kutoa kiasi cha fedha zote zilizochangishwa katika kutoa msaada.

Kwa bahati mbaya hatuwezi kujibu sehemu ya mwisho ya swali lako kuhusu pendekezo la kupiga marufuku kamari.

## Wajibu wa Wamiliki wa Akaunti ya pamoja Benki

**Mume wangu alifungua akaunti kwenye mojawapo ya benki jijini Dar es Salaam mwaka 1998. Ilikuwa akaunti ya pamoja ambapo mimi nilikuwa mmoja wa waweka saini. Ingawa sijawahi kwenda benki, mume wangu alikuwa akiweka fedha katika akaunti hii kwa ajili ya matumizi yetu ya pamoja.**

**Mume wangu alifariki miezi nane iliyopita na benki wamekataa kutoa fedha kwangu kwa misingi kwamba baadhi ya hatua katika fomu ya ufunguzi wa akaunti hii zilikuwa zimekiukwa, ingawa taarifa fupi ya benki imekuwa ikitoka ikiwa na majina yetu wote wawili mpaka sasa. Benki haitoi ushirikiano/majibu mazuri, imekuwa ikionesha dalili zote za kujaribu kunizuia kuchukua fedha hizi. Tafadhali nisaidieni.**

*3 Mei 2010*

Iko wazi kwenye fomu ya masharti ya benki kuwa benki ina makubaliano na kila mmoja wa wamiliki wa akaunti ya pamoja. Unasema kuwa ni mmoja wa watia saini wa akaunti. Hii inamaanisha kuwa benki inakufahamu, tunashindwa kuelewa kwa nini benki hawatoi fedha husika kwako. Labda kama kuna taarifa ambazo unaficha, tunajibu swali kama ifuatavyo.

Katika kesi sawa na yako ndani ya Jumuiya ya Madola, iliwahi kuamuliwa kwamba kutokuchangia au kutoa pesa kwa mmiliki mmojawapo kwenye akaunti ya pamoja hakumzuii mtu huyo kunufaika. Hata kama hajui kabisa kama akaunti hiyo ya pamoja ipo. Zaidi ya hayo, ukweli kwamba mmoja wa wamiliki wa akaunti hiyo hakutarajia kuitumia kabisa hiyo wakati mwenzake yuko hai, haimzuii mmiliki aliyehai kuirithi akaunti yote. Kisheria, akaunti ya pamoja ni deni la pamoja la wamiliki wa akaunti hiyo.

Kulingana na Sheria hapo juu na ukweli kama ulivyowasilishwa kwetu, tunaamini kwamba benki inazuia fedha yako kinyume na sheria na una kesi nzuri dhidi ya benki. Tunashauri uwasiliane na wanasheria wako.

## Mke wa mwenye Nyumba ni Kero

**Mwenye nyumba wangu (hasa mke wake) mara nyingi hutembelea nyumba niliyopanga licha ya kwamba nazingatia masharti yote ya upangaji. Mwenye nyumba huja kwangu wakati wowote. Hatujulishi kwa simu - anakuja siku na muda/saa yoyote anayotaka. Hali hii inasumbua sana familia yetu. Nimemwambia zaidi ya mara moja kwamba anapaswa kupiga simu kabla ya kututembelea. Je, sina haki zozote? Anadai kwamba sheria inaruhusu mwenye nyumba kutembelea nyumba aliyokodisha. Pia ana mwanasheria mzuri sana anayemuunga mkono. Je, nifanye nini?**

*26 Aprili 2010*

Mwenye nyumba yuko sahihi kwamba ana haki ya kuja na kukagua nyumba aliyopangisha. Kama mpangaji wa nyumba, pamoja na kwamba una haki ya kutumia na kufurahia nyumba uliyopanga, bado mwenye nyumba ana haki ya umiliki wa nyumba husika. Kwa suala lako, hujatuambia vigezo na masharti ya upangaji wako, lakini kwa ujumla mwenye nyumba anaruhusiwa kuja na kukagua nyumba aliyopangisha.

Hata hivyo, ukweli kwamba anakuja wakati wowote bila taarifa kama anavyofanya anavunja sheria. Sheria inakulinda kuwa, wakati mmiliki ana haki ya kuja na kukagua nyumba aliyoipangisha, anatakiwa kukupa taarifa mapema kabla ya kufanya hivyo. Kutokana na swali lako na unavyoonesha kukerwa, tunahisi kwamba mwenye nyumba anakuja kila siku au kila wiki bila taarifa. Labda hana kazi nyingine ya kufanya na hivyo 'amejishikiza' kwenye mali yake!

Kwa hali yoyote, ikiwa hali hii itaendelea, unaweza kumzuia asiingie bila taarifa na kumshtaki kwa usumbufu/kero. Mwenye nyumba anatakiwa kuwa na busara juu ya wakati gani anaweza kuja na kwa malengo gani. Wakati umepanga una haki ya faragha, kuishi kwa amani na kufurahia mali husika.

Ukweli kwamba ana timu nzuri ya wanasheria hauna maana - wanasheria hawawezi kubadilisha sheria. Sote tunaishi chini ya sheria. Unaweza pia kushauriana na wakili wako.

## Daktari anaficha Taarifa zangu

**Nimekuwa nikitembelea hospitali moja jijini Dar es Saalam kwa miezi mitatu iliyopita na kwa kuepuka usumbufu nimekuwa nikiambatana na mama yangu. Chanzo cha ugonjwa wangu kilikuwa hakijulikani na madaktari waliendelea kufanya vipimo mbalimbali. Miezi michache iliyopita nilienda kumuona daktari na kuniambia kuwa alihitaji kuzungumza na mama yangu, ambaye alikuwa hajaambatana nami siku hiyo. Je, daktari ana haki ya kunificha taarifa kama hii? Kwa nini mama yangu apewe taarifa na si mimi?**

*19 Aprili 2010*

Kwa kawaida, daktari hawezi kuficha/ kuzuia taarifa za mgonjwa. Hata hivyo, kuna hali ambayo daktari ana haki ya kuzuia taarifa, na ana kinga kisheria iwapo atashtakiwa kwa kuzuia taarifa.

Upendeleo wa kitabibu ni haki ya daktari kutotoa taarifa kwa mgonjwa pale anapoona kwamba kutoa taarifa hizo kunaweza kusababisha madhara ya ghafla na makubwa kwa mgonjwa. Upendeleo wa kitabibu ni kanuni ndogo inayolegeza masharti ya kanuni kuu, ambayo kwa kawaida humkataza daktari kutoa taarifa za mgonjwa kwa mtu mwingine. Kanuni hii ndogo inatumika ikiwa kutoa taarifa husika kwa mgonjwa kunaweza kusababisha madhara makubwa na ya ghafla kwa mgonjwa, kama vile tabia ya kujiua. Kanuni ya upendeleo wa kitabibu haitakubalika kama daktari ataona kwamba mgonjwa anaweza kukosa huduma muhimu.

Unatakiwa kuelewa kwa nini daktari alikataa kutoa taarifa kwako. Kama inaangukia kwenye hayo tuliyoeleza hapo juu basi huwezi kumshtaki daktari. Kama haiangukii humo, basi unaweza kumshtaki daktari kwa kufichua taarifa za matibabu kwa mtu mwingine.

## Mpangaji na Haki ya Kwanza ya Kukataa

**Nimekuwa mpangaji kwa miaka mingi. Miezi mitatu iliyopita nilipewa taarifa ya kuhama kwa misingi kwamba mali husika ilikuwa imeuzwa. Je, hakuna sheria ambayo inamtaka mwenye nyumba kutoa nafasi ya kwanza kwa mpangaji kununua kabla ya kutafuta soko?**

*19 Aprili 2010*

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Tanzania, hakuna kifungu cha sheria ambacho kinampa mwenye nyumba wajibu wa kuuza mali yake kwa mpangaji wake wa sasa isipokuwa kama imeelezwa kwenye mkataba wa upangaji, kitu ambacho ni nadra sana kutokea. Kama mkataba wa upangaji wako una kipengele cha kununua, au haki ya kukataa kwanza, basi kulingana na maneno ya kifungu hicho, unaweza kuwa na uwezo wa kupinga uuzaji wa mali husika na si vinginevyo.

Kama mwenye nyumba yako ni taasisi ya umma, masharti ya matangazo na zabuni lazima yatimizwe. Ikiwa masharti hayo hayakutimizwa, unaweza kupinga uuzaji huo. Zaidi ya hayo, ingawa mali imeuzwa, haki yako ya kukaa kama mpangaji bado inabaki kama ilivyo, kutegemeana na masharti yaliyopo katika mkataba wa upangaji. Unapaswa kusoma kifungu cha kuvunja mkataba wa upangaji kwa mwongozo zaidi.

## Nimeathirika lakini si Mhusika kwenye Mkataba

**Mwenye nyumba yangu ameingia mkataba na watu ambao wanaleta usumbufu kwenye eneo tunaloishi. Alitutaarifu juu ya mkataba huu lakini hatujakubaliana naye. Mwanasheria wetu anasema kwa kuwa sisi si wahusika kwenye mkataba, hatuwezi kufanya chochote. Je, unapendekeza nini? Usumbufu huu unaathiri afya zetu.**

*26 Aprili 2010*

Kwa bahati mbaya, umeelekezwa vibaya. Kwa maelezo uliyotupa, una kesi nzuri dhidi ya mwenye nyumba wako. Ili mradi tu

ukiwa umetekeleza vigezo na masharti ya upangaji, una haki ya kuishi mazingira tulivu na kufurahia bila bughudha/usumbufu. Hili ndilo agano la lazima lililowekwa na sheria ili kusimamia uhusiano wa mwenye nyumba na mpangaji.

Ingawaje hujasema maudhui ya mkataba ambao mwenye nyumba wenu ameingia wala aina ya usumbufu mnaoupata, maoni yetu ni kwamba kama usumbufu unaathiri afya yako unaweza kuwasilisha mashtaka dhidi ya wote wawili, mwenye nyumba na upande unaosababisha tatizo katika mahakama yoyote yenye mamlaka husika na kupata zuio dhidi ya kero ambayo inaathiri afya yako. Unahitaji kuwasiliana na wakili wako akuongoze zaidi.

## Kununua Bidhaa zilizoibiwa

**Mvulana aliyeajiriwa na duka kubwa huko Mbeya alikutwa na hatia ya kuiba mabati elfu moja kutoka kwa mwajiri wake. Bila kufahamu nilinunua Mabati husika kutoka kwa mvulana huyo kwa bei ya soko. Si tu kuwa Hakimu alimhukumu mvulana huyo, bali pia aliamuru mabati mia saba yaliyohifadhiwa kituo cha polisi yarejeshwe kwa mmiliki. Sijaridhishwa na amri ya mahakama kwani nilinunua bidhaa hizo kwa nia njema bila kujua kwamba zilikuwa zimeibiwa. Je, amri ya mahakama ni sahihi?**

*29 Machi 2010*

Hatuna uhakika na unachomaanisha unaposema 'kununua bidhaa bila kufahamu' kwa bei ya soko. Tunaamini kuna baadhi ya mambo/maelezo ambayo utakuwa hujaweka wazi wakati unatuandikia! Kwa mfano, Mbeya ni mji mdogo na mvulana kujitokeza 'tu' kukuuzia mabati inatia shaka sana. Huenda haujawahi kufanya biashara na 'mvulana' huyu kabla, lakini bado unadai kwamba umenunua bidhaa husika kwa nia njema.

Kutokana na maelezo uliyotupa, haiwezekani kuwa bidhaa zilikuwa za kijana huyo, na bila ruhusa (kibali) ya/cha mmiliki hauwezi na hautaweza kutambuliwa kisheria kama mmiliki halali wa bidhaa husika. Sheria iko wazi kuwa, iwapo bidhaa zitauzwa na mtuhumiwa wa wizi kushtakiwa na kukutwa na hatia, umiliki wa mali husika unarudi kwa mtu ambaye alikuwa mmiliki wa bidhaa na mahakama inaweza kutoa amri ya kurejeshewa bidhaa/mali. Kwa upande wako, bidhaa zinatambulika na hatuoni chochote kibaya juu ya amri ya mahakama. Tuna shauku ya kujua kwa nini mahakama iliamuru kuwa bidhaa zinazopaswa kurejeshwa kwa mmiliki wa awali ni zile zilizopo kwenye kituo cha polisi tu, wakati mabati mia tatu bado yako chini ya himaya yako.

Kuhusu hatima ya fedha ulizolipa kununua mabati, unaweza kufungua kesi ya madai dhidi ya kijana aliyekuuzia. Kabla ya kufungua kesi husika, wanasheria wako wanapaswa kufanya uchambuzi wa kina na haraka kuhusu gharama husika dhidi ya faida itakayopatikana, vinginevyo utaishia 'kupata hasara zaidi'.

## Hundi kupotea Benki

**Niliweka benki hundi ya Dola 220,000. Kiasi hiki cha pesa kiliingizwa kwenye akaunti yangu na kutumika. Miezi sita baada ya amana hiyo, benki, bila ya kunijulisha, ilipunguza kiasi hicho hicho cha fedha kutoka kwenye akaunti yangu 'baada tu' ya kuweka hundi nyingine yenye thamani kubwa. Niliwasiliana na benki yangu, na meneja wa benki (wa kigeni) alinijibu kwa ukali kwamba hundi ya awali imepotea na kwamba niandikiwe hundi nyingine na kuiwasilisha tena. Sikutaka kuingia kwenye mgogoro na benki yangu kuhusu suala hili na nikaamua kuwasiliana na mteja wangu, kampuni ambayo hutoa huduma kwa makampuni ya madini. Waliniambia kinagaubaga kuwa, uongozi wote wa kampuni umebadilika hivyo itakuwa**

**vigumu sana kutoa hundi nyingine. Je, benki inaweza kutoa fedha kutoka kwenye akaunti pasipo ridhaa yangu? Nina shida sana na fedha, lakini benki haitaki kunielewa.**

*15 Machi 2010*

Kuna kesi nchini Tanzania inafanana sana na tatizo lako, ambapo Mahakama ya Rufaa ya Tanzania iliamua kuwa, ikiwa mteja atapeleka hundi benki-wakala na hundi husika kupotea, benki yake inawajibu wa kutoa taarifa husika mapema ili mteja aweze kuchukua hatua stahiki ambazo zinaweza kumuwezesha kuepuka hasara zaidi kutokana na upotevu huo; iliamuliwa pia benki ina wajibu huo pasipo kujali kuwa hundi ilipotezwa na benki yenyewe au wakala wa benki hiyo (mhusika/mtu wa tatu).

Kutokana na hali tajwa hapo juu, Mahakama ya Rufaa ilikubaliana na uamuzi wa Mahakama Kuu iliyotoa tuzo kwa mteja kiasi alichokuwa anadai pamoja na fidia. Katika madai yako, muda ambao benki ilikutaarifu haukuwa mwafaka. Una nafasi nzuri sana ya kufanikiwa kurejesha fedha ambazo zilichukuliwa na pia kudai fidia kwa upotevu huo.

## Madai ya Bidhaa chini ya Kiwango

**Kwa zaidi ya miaka hamsini kampuni yetu imekuwa kwenye biashara ya kutengeneza peremende/biskuti. Viwanda vyetu vimekuwa vikitumia teknolojia ya daraja la juu duniani ili kuhakikisha kwamba tunazalisha bidhaa bora na safi kwa viwango vya kimataifa. Miezi sita iliyopita, mteja tunayemfahamu alitutumia notisi/hati ya madai kwamba mtoto wake aliugua baada ya kutumia moja ya bidhaa zetu. Sasa mtu huyo ametufungulia kesi na kudai malipo ya shilingi milioni 400. Je, huu si uonevu uliopitiliza? Jinsi gani sheria inaruhusu watu kufungua kesi zisizo na msingi kama hii? Je, bima inaweza kubeba jukumu hili?**

*1 Machi 2010*

Hakuna uonevu katika madai haya. Mdai wako anaamini kampuni yako imemkosea kwa kupeleka sokoni bidhaa ambazo ziko chini ya kiwango. Hata kama umekuwa katika biashara hiyo kwa miongo mitano, upo uwezekano wa kutengeneza bidhaa zisizo na ubora. Imetokea hivi karibuni kwa kampuni kubwa kama Toyota, inaweza pia kutokea kwa mtu yeyote ikiwa ni pamoja na kampuni yako.

Unachohitaji kuelewa ni kwamba mdai wako anatakiwa kuthibitisha kesi hii mahakamani. Anapaswa kuthibitisha jinsi mtoto wake alivyoathirika, na jinsi alivyofikia madai ya shilingi milioni 400. Hiki kinaweza kuwa kiasi kikubwa kwa Tanzania, lakini kimataifa, kwenye kesi kama hizo wadai hudai mabilioni ya fedha.

Sheria haiwazuii watu kufungua madai ambayo wanaamini kwa dhati kabisa kuwa kweli. Itakuwa ni kinyume na sera za nchi na itasababisha ukosefu wa haki. Ni juu ya mahakama kuamua kama kuna kesi ya msingi au la, na kiasi gani, kama kipo, kinapaswa kutolewa.

Kwa upande wa bima, bima ya kawaida mara nyingi haiusiki katika hili. Kama una bima ya bidhaa au bima ya kiwanda, inaweza kulipa. Bima kama hii pia hutumika kulipia ada za wakili.

## Kampuni za Simu kudanganya Watumiaji

**Nimekuwa Tanzania kwa miaka mingi sasa na nimeshuhudia sekta ya mawasiliano ya simu za mkononi ikikua. Ushindani umeongezeka na udanganyifu umeongezeka pia. Kwa mfano, kila siku wanakijiji wengi maskini wanajiunga na vifurushi vya kuongea bila kikomo kwa siku, lakini baada tu ya kukatwa tozo husika huunganishwa na huduma ya kuongea bure mchana tu! Hii hutokea kila siku. Hivi karibuni mteja ambaye alijaribu kujiunga na huduma hii ya bure alikatwa salio lake lote, kiasi cha shilingi 5,000. Asasi**

**yetu inawahudumia baadhi ya watu maskini zaidi duniani, ni aibu kuona kwamba makampuni haya ya simu yanaiba kutoka kwa watu kama hao. Kama makampuni haya ya simu yanataka kuiba, wanapaswa kuiba kutoka kwa watu matajiri mijini na si wakulima maskini. Je, tufanye nini juu ya udhalimu huu?**

*8 Machi 2010*

Maoni yako juu ya nani anapaswa kuibiwa na kampuni za simu yanatukumbusha kisa cha Robin Hood. Sheria za Tanzania hazibagui kati ya tajiri na maskini, hivyo kama utamuibia tajiri, sheria haiwezi kukuangalia kwa namna tofauti. Pendekezo lako halina msingi kwa kuwa ni kinyume cha sheria. Pia unadhani kwamba matukio kama hayo yanatokea katika eneo ulilopo tu. Kama kweli yapo, na watu wengi wanadai yapo, kuna uwezekano matukio kama hayo yakawa yanatokea pia maeneo mengine ya Tanzania, kwa matajiri na maskini.

Njia bora ni kuitumia kampuni ya simu notisi/hati ya madai ukielezea kilichokea na lini kimetokea. Kwa bahati mbaya, wateja wa malipo ya kabla hawapewi taarifa fupi ya juu ya matumizi yao kila mwezi, hivyo itakuwa busara kwa mdai kuomba taarifa yake fupi kabla ya kutuma taarifa ya kukusudia kushtaki.

Ikiwa barua haijajibiwa, au majibu hayamridhishi mlalamikaji, anaweza kuendelea na kufungua shauri dhidi ya kampuni ya simu. Kumbuka kwamba mlalamikaji anatakiwa kuthibitisha kesi yake. Mdai anapaswa kuwa tayari kutoa ushahidi sahihi ili kuthibitisha madai yake, ambayo inaweza kuwa ngumu. Hata hivyo, kama kampuni za simu zinaiba kwa makusudi au mitambo yake imeshindwa kuhimili na kuleta hasara kwa watumiaji ni jambo ambalo mahakama itapaswa kutolea maamuzi.

## Benki imevujisha Siri kwa Mke wangu

**Nina akaunti katika benki moja jijini Dar es Salaam. Hii ni akaunti yangu binafsi na sijawahi kumshirikisha mtu yoyote ikiwa ni pamoja na mke wangu. Miezi michache iliyopita wakati nikiwa ng'ambo kikazi, mke wangu aliona taarifa za benki za zamani kwenye moja ya droo yangu. Kwa kuwa anajuana na baadhi ya wafanyakazi wa benki, aliweza kuwashawishi wakampa taarifa ya kibenki kuhusu akaunti yangu bila idhini yangu. Kinachonisikitisha zaidi ni kwamba mimi na mke wangu tulikuwa tunakaribia kutengana, hivyo jambo hili lilifanya hali kuwa mbaya zaidi. Mke wangu sasa amekuja na madai ambayo kamwe asingeweza/kuota kuyafanya kama asingeona taarifa hiyo ya benki. Je, nifanyeje?**

*22 Februari 2010*

Unapouliza 'nifanye nini', tunadhani kwamba unataka tukushauri juu ya benki kuvunja haki ya usiri na si nini unapaswa kufanya juu ya madai ya mkeo.

Benki ina wajibu wa kisheria na kimaadili kutokutoa taarifa za akaunti yako kwa mtu mwingine, labda kama sheria imewalazimisha benki kufanya hivyo au ambapo maslahi ya benki yanahitaji kuweka taarifa hizo wazi au mwenye akaunti ameridhia kutoa taarifa hizo. Ingawa ni mkeo wa ndoa, katika sheria, nyinyi ni watu wawili tofauti. Kwa sababu tu mwanamke ni mkeo, hiyo haimpi haki ya kufahamu akaunti yako ya benki.

Benki imekiuka wajibu wake na unaweza kuishtaki benki na kudai fidia. Tafadhali tambua kwamba, pia una uwezo wa kumshtaki mkeo kutegemea na mazingira ambayo aliweza kupata taarifa hizo.

## Tairi la Ndege kwenye Gari langu

**Mimi ni dereva teksi katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Mwalimu JK Nyerere. Hivi karibuni, wakati gari langu likiwa limeegeshwa kwenye uwanja wa ndege, kitu kutoka kwenye ndege ambacho kinaonekana kama tairi, kilishuka na**

**kuharibu kioo cha mbele cha gari langu. Sikufanya biashara kwa muda wa wiki mbili kwani nilikuwa nikifanya matengenezo. Je, ni jinsi gani ninaweza kupata fidia ya hasara hii? Tafadhali naomba ushauri.**

*8 Februari 2010*

Hili ni tukio la ajabu sana. Kama lilikuwa gurudumu, tunashangaa jinsi gani ndege ilitua! Hatuna taarifa ya ajali ya ndege ikitua iliyotokea hivi karibuni kwenye ukanda huu, tunashangaa kilikuwa 'kitu' gani. Kwa vyovyote vile, tutajibu swali lako bila kujali ni kitu gani.

Sheria za Tanzania zinatoa fidia kwa madhara yaliyosababishwa na chombo cha angani. Mtu aliyepata hasara anaweza kufidiwa kama anaweza kuthibitisha kwamba hasara hiyo imesababishwa na chombo cha angani. Sheria ya Usafiri wa Anga inaeleza kuwa endapo mtu au mali (mfano gari lako) iliyo ardhini au majini atasababishiwa/itasababishiwa hasara au uharibifu mkubwa na mtu aliye ndani ya ndege, au kitu kilichodondoka kutoka katika ndege iliyo angani, inayotaka kuruka au kutua, hasara hiyo au uharibifu huo utafidiwa pasipokuthibitisha nia ovu (mens rea) ya mmiliki wa ndege hiyo; labda tu akithibitisha kuwa hasara au uharibifu huo ulisababishwa au kuchangiwa na uzembe au kutojali kwa muathirika au sababu nyingineyo iliyo nje ya uwezo wa mmiliki wa ndege.

Sheria iko upande wako lakini unatakiwa kuthibitisha kuwa gurudumu au kitu hicho kilianguka kutoka kwenye ndege. Unaweza pia kupata fidia kutoka kwenye mfuko wako wa bima, ingawa unatakiwa kuangalia kama bima yako inafidia uharibifu wa kioo cha mbele ya gari. Bima nyingi hazifanyi hivyo, na utahitaji bima nyingine ambayo pia utatakiwa kuilipia tozo/ada tofauti.

## Kughushi kwenye Akaunti yangu

**Nina akaunti binafsi katika moja ya benki mjini Musoma. Siku niliyotakiwa kusafiri kwenda Dar, niliangalia taarifa yangu fupi ya benki nikagundua kwamba kuna kiasi kikubwa cha fedha kilichukuliwa kinyemela kutoka kwenye akaunti yangu. Baada ya kurejea kutoka Dar, nilikwenda kuwaona benki, na kuambiwa kuwa nimechelewa kutoa taarifa ya jambo hili hivyo sitaweza kufidiwa. Nilidai nakala ya hundi iliyotumika kuchukua pesa niligundua saini kwenye hundi hiyo ilikuwa tofauti na saini yangu kwa 100%. Hata kipofu angeweza kuona tofauti hiyo. Benki haitoi ushirikiano. Je, kuna chochote ninaweza kufanya?**

*4 Januari 2010*

Kinachotushangaza ni kwamba kumekuwa na tukio la kughushi na haujatoa taarifa benki mpaka ulipotoka Dar. Ikiwa kiasi ni kikubwa kama unavyodai, tumeshtushwa kabisa na jinsi ulivyoshughulikia suala hili.

Katika taratibu za kibenki, mteja ana wajibu wa kuijulisha benki yake juu ya malipo yoyote ya kughushi haraka iwezekanavyo mara anapofahamu kutokea kwake. Hii mara zote hujulikana kama wajibu wa Greenwood, kutoka kwenye kesi maarufu ya Kiingereza. Kama hakufanya hivyo, benki itakubali hundi, na hivyo atazuiliwa kudai kwamba akaunti yake imegushiwa.

Wajibu na jukumu husika linamtaka mhusika kuhakikisha kwamba mtu yeyote asimruhusu mtu mwingine kuathirika na matumizi ya hundi ya kugushi, ambayo ameiona au anaonekana hakuwa ameiona.

Mwisho, tunahisi unaweza kufanya kitu katika hili, lakini uwezekano wa wewe kupata fidia yote ni mdogo kwa kiasi fulani, kwa sababu ya kanuni ya Greenwood. Tunapendekeza ukutane na wanasheria wako na kuwaelezea vizuri kabla ya kuishtaki benki.

## Benki haikunipa Taarifa

**Kwa kipindi cha miaka kumi na tano iliyopita, nimekuwa mteja wa benki fulani**

**nchini Tanzania. Pia nimekuwa mmoja wa wakopaji wao wakubwa baada ya kuwa nimewekeza katika sekta mbalimbali nchini. Zaidi ya miaka miwili iliyopita, nimekuwa nikisafiri na kutumia zaidi ya muda wangu nje ya nchi kwa matibabu na nimerudi hivi karibuni. Niliporudi, niligundua kwamba benki hawakunifahamisha juu ya uzinduzi au uwepo wa bidhaa/huduma mbalimbali mpya na zenye ofa ambazo zingeokoa mamilioni ya riba na ada nyingine za kibenki. Washindani wangu walitumia mwanya huo wa ofa na wamefanikiwa sana. Je, benki haikuwa na wajibu wa kunijulisha? Je, benki hawana wajibu wa kuwajali wateja wake?**

*28 Desemba 2009*

Kuna majukumu mengi ambayo benki inatakiwa kufanya kwa wateja wake ikiwa ni pamoja na kulinda wateja dhidi ya udanganyifu wa mawakala wake (ikiwa ni pamoja na wakurugenzi), ulinzi wa kisheria na wakati fulani kutoa ushauri wa kifedha na uwekezaji. Haiwezekani kutoa orodha kamili ya wajibu wa benki kumlinda mteja, kwa sababu katika hali yoyote mahakama inaangalia mkataba, au katika shauri la madhara, ukaribu wa wahusika, busara na haki katika mazingira husika.

Swali lako ni kama benki ilitakiwa kukupa taarifa ya ofa nzuri ilizotoa ambazo zingekupa faida na kuokoa mamilioni ya pesa.

Hii itategemea na aina ya mkataba ulioingia na benki. Kwa uzoefu wetu, ni vigumu sana kwa benki kuweka kipengele kwenye mkataba wowote, chenye masharti yanayohitaji benki kutoa taarifa ya bidhaa/huduma hizo. Mwisho, kama utachagua bidhaa husika au la ni uamuzi wako. Ni sawa na kisa ambapo ulienda dukani, ukanunua runinga kwa bei fulani, halafu kesho yake duka linatoa punguzo la asilimia hamsini; hauna haki ya kudai punguzo hilo.

Katika kesi maarufu ya kiingereza ya Suriya & Douglas dhidi ya Midland Benk, Mahakama ya Rufaa ilikataa hoja ya wakili wa mlalamikaji kuwa kuna haja ya benki kuwataarifu wateja wake juu ya uwepo wa bidhaa mpya na zenye faida.

Kesi yako inafanana sana na kesi ya Midland, hivyo ni vigumu kushinda kesi yako dhidi ya benki husika. Tunakushauri uwasiliane na wanasheria wako kwa ushauri zaidi.

## Mgeni anayelipia

**Mimi ni mwanafunzi kutoka Singida kwa sasa nasoma masomo ya kidato cha tano huko Dodoma. Ninakaa na familia kama mgeni ninayelipia. Nilipewa chumba nilichokuwa naishi na wanafunzi wengine wawili. Wiki chache nyuma, familia hiyo iliongeza wanafunzi wanne kwenye chumba hicho kimoja, hivyo tukawa watu saba katika chumba kimoja. Ukubwa wa chumba si zaidi ya mita za mraba kumi na tano. Hakuna hata nafasi ya kupumua tunapojikuta wote tuko chumbani kwa wakati mmoja. Tumebanana zaidi ya gerezani. Je, nifanye nini?**

*21 Desemba 2009*

Familia unayokaa imevunja mkataba ulioingia nayo. Hata hivyo, kwa suala kama hili, kweli ni haki kushtaki kwa uvunjaji wa mkataba tu? La hasha! Familia hiyo pia imekiuka kifungu cha 63 cha Sheria ya Afya ya Umma ya mwaka 2008 ambayo inasema: mtu yoyote hataweza kwa wakati wowote kupokea na kutoa malazi kwenye nyumba ya kulala wageni, chumba, nyumba ya kuishi, shule, taasisi, hosteli, gari, chombo cha moto, treni au chombo chochote idadi zaidi ya watu kuliko uwezo wake na kusababisha msongamano. Mtu yeyote anayekiuka maelekezo haya anatenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi 200,000 au kifungo kwa muda wa miezi mitatu au vyote viwili kwa pamoja.

Kwa upande wako, wanafunzi saba kutumia chumba cha ukubwa wa mita

za mraba kumi na tano kuna uwezekano mkubwa ni msongamano. Unahitaji kutoa taarifa hii kwa familia unayokaa nayo, maana wanaweza kufungwa gerezani kwa kukiuka Sheria ya Afya ya Umma.

## Kampuni ya Bima hovyo

**Miezi michache iliyopita kiwanda changu kiliungua moto. Nilifanya kilichowezekana kuokoa vitu vilivyokuwa ndani ikiwa ni pamoja na mali za thamani kubwa - zaidi ya yote, mashine yangu. Wafanyakazi wangu walihatarisha maisha yao kwa kunisaidia kuokoa mashine hiyo ghali ikiwa ni pamoja na vitu vingine. Hata hivyo, katika kuokoa mashine, kwa sababu ya kasi ambayo tulikuwa nayo katika uokozi, mashine iliharibika ambapo gharama ya kuikarabati ni 30% tu ya gharama ya kununua mashine mpya kama ingeungua. Kampuni ya bima inadai kuwa bima yangu ni ya moto, lakini kwa sababu niliokoa mashine, haitafidiwa kwa sababu haikuungua. Natamani ningeacha mashine yangu iungue ili nifidiwe. Nimechanganyikiwa, tafadhali nisaidieni.**

*23 November 2009*

Tunaweza kuhisi kuchanganyikiwa kwako. Kitendo chako cha usamaria wema kimekuweka katika matatizo na pengine unatamani mashine yako ingeungua.

Hatua yako ya kupunguza hasara ni matakwa katika bima yoyote. Pia si jambo la ajabu kwa mnufaika wa bima kuchukua hatua kwa lengo la kupunguza hasara, lakini ikapelekea kusababisha uharibifu zaidi. Hii haivunji mlolongo wa kisababishi. Vinginevyo, atakayeathirika ni kampuni ya bima, kwani kwa kufanya hivyo, kutakatisha tamaa vitendo vya kupunguza hasara za majanga husika.

Kitu muhimu katika swali lako ni kama uharibifu wa mashine yako utafidiwa na bima ya moto. Kama tukichukua tafsiri kali, kama inavyofanya kampuni ya bima, mashine haitakuwa mnufaika wa bima.

Hata hivyo, kwa kuwa 'juhudi za kuokoa' mashine zilipelekea kuharibika kwake ni wazi uharibifu huo unafidiwa na bima. Zaidi, unaweza kuomba kurudishiwa gharama ulizotumia katika kukabiliana na moto.

Mwisho, wapelekee notisi/hati ya madai na uwaeleze kuwa kwa kadiri wanavyochelewa kukulipa, ndivyo unavyopoteza biashara yako. Kama watagoma kulipa, washtaki, una kesi nzuri sana.

## Kujenga katika Eneo la Wazi

**Kuna wamiliki sita tofauti na kuna njia moja inayotumiwa na wamiliki wote sita kwenye jengo ninaloishi. Mmoja wa wakazi nyuma ya jengo ameanza ujenzi kwenye njia hii na hivyo kuziba njia ya wapangaji wengine kwenda kwenye matanki yao, ikiwa ni pamoja na kuvunja haki yao ya kutembea kwa uhuru. Je, wapangaji wana haki zipi?**

*19 Octoba 2009*

Kutokana na swali lako inaonekana kama eneo alilojenga jirani yako ni eneo la wazi ambalo linatakiwa kutumiwa na wamiliki wote sita katika eneo la nyumba unazozisema.

Hakuna shaka kuwa wapangaji katika ghorofa ya juu wanahitaji kufikia eneo lenye matanki, kutokana na ukweli ulioutoa kwetu, ujenzi huo au kuziba huko ni kinyume cha sheria. Pia, ni kero. Unaweza kulalamika mahakamani ili kero hiyo iondolewe au kupata amri ya kuingia au kubomoa, kutegemea na hali husika.

Unaweza pia kuwasiliana na manispaa kuangalia kama ujenzi huo ni halali na kama walitoa kibali. Kama hakuna kibali kilichotolewa, manispaa ina haki ya kuingilia kati na kubomoa ujenzi huo uliofanywa kinyume cha sheria.

## Benki haikuingiza Hundi yangu

**Nilifungua akaunti katika benki moja na nimekuwa nikiitumia mara kwa mara.**

**Niliingiza hundi yenye kiasi kikubwa cha fedha miezi tisa nyuma, mpaka leo hundi hiyo haijawekwa kwenye akaunti yangu. Meneja anaendelea kunipa sababu zisizoeleweka kuwa hundi hiyo inafanyiwa uthibitisho wa kimataifa. Hivi karibuni aliniambia kuwa akaunti yangu haiwezi kubeba kiasi hicho cha fedha kwa vile thamani ya hundi ni mara tano zaidi ya pato langu la mwaka. Biashara yangu inazorota kwa sababu hii. Je, benki inaweza kukaa na fedha yangu namna hii?**

*12 Octoba 2009*

Kama yote unayotuambia ni kweli, basi una kesi nzuri sana, vinginevyo labda kama hundi ni ya kughushi, au imekataliwa kitu ambacho hujatuambia. Kwa vyovyote vile, benki inapaswa kukupa sababu za kuchelewa. Ili uwe na kesi nzuri dhidi ya benki unahitaji kuthibitisha yafuatayo: kwamba wewe ni mteja wa benki na uhusiano upo katika misingi ifuatayo: lazima uwe na akaunti katika benki – ambayo unayo; uhusiano wa benki na mteja huanza mara tu fedha au hundi inapolipwa na benki kukubali - hii pia inaonekana kwenye kesi yako; muda si kigezo muhimu kwenye suala la mahusiano kati ya benki na mteja, tukimaanisha kuwa si muhimu akaunti kuwa imefunguliwa na kuendeshwa kwa muda fulani ili kupata sifa ya mteja wa benki. Kwa kuwa tumejibu kwa kukubali, una uhusiano wa mteja na benki.

Vivyo hivyo, benki ina wajibu wa kutumia ujuzi na uwezo wake katika kushughulikia na kuwasilisha malipo ya hundi kwenye akaunti yako. Haichukui muda wa miezi tisa katika kupitisha hundi inayotoka nje ya nchi/hundi ya kimataifa, hii kweli ni sababu dhaifu sana. Katika benki nyingi, mchakato hauzidi wiki nne hadi sita.

Meneja amekwambia kwamba kiasi ni kikubwa na kwamba hakiwezi 'kuingia' katika akaunti yako. Tafadhali kumbuka kuwa benki ina maelfu ya akaunti na kila akaunti haina kasiki/sefu yake yenyewe ambapo pesa huingizwa au kuondolewa! Labda alikuwa akimaanisha kwamba kwa kuangalia hali ya kawaida ya akaunti yako, kiasi kilichoingia ni kikubwa kiasi kwamba 'inatia shaka' uhalali wa fedha hiyo. Kwa kawaida, benki itawasilisha muamala huo Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya uchunguzi, hata hivyo haiwezi kuchukua miezi tisa.

Unazungushwa bila kupewa sababu. Una haki ya kudai kupewa sababu na unapaswa kufanya hivyo kwa maandishi. Benki haiwezi kuifanya hivyo hundi yako. Unaweza kuiandikia benki juu ya hali hii na usumbufu wanaokusababishia na kama wanaendelea kutoa sababu zisizo na maana unaweza kuishtaki benki. Katika kesi yako, unapaswa pia kuomba fidia.

Tafadhali kumbuka kuwa ushauri wetu unatokana na maelezo uliyotupatia. Benki kutokuingiza kiasi cha fedha katika akaunti yako, bila kutoa sababu kwa zaidi ya miezi tisa inaibua maswali mengi sana. Kama kuna kitu chochote umetuficha ni vyema kupuuza ushauri wetu, na kuomba ushauri kutoka kwa wanasheria wako.

## Upande wa Tatu unadai kutokana na Ajali

**Gari langu lilihusika katika ajali na mpanda baiskeli mjini Dodoma. Mpanda baiskeli alijeruhiwa na kupelekwa hospitali kwa matibabu. Nililipia matibabu. Nimekuwa nikishikiliwa kwa kusababisha ajali kwani sikujua kama mtaa ulikuwa na njia ya kwenda tu. Mpanda baiskeli alikuwa na madai mengine kadhaa dhidi yangu. Niliyapeleka madai hayo kwenye kampuni yangu ya bima jijini Dar es Salaam. Mpanda baiskeli alisafiri kwenda Dar es Salaam na kampuni ya bima ilitaka kumlipa kiasi kidogo sana cha shilingi 50,000 ili kumaliza jambo hili. Kiasi hicho hakiwezi hata kufidia gharama za usafiri wa huyu mtu maskini**

**kwenda Dar, hivyo alikataa. Sasa mpanda baiskeli kafungua mashtaka dhidi yangu. Je, nifanye nini?**

*28 Septemba 2009*

Makampuni ya bima yana sifa mbaya duniani kote kwa kuchelewesha au kukataa kulipa madai ya wateja, hasa yanayohusisha madai ya mtu/mhusika wa tatu. Kesi yako haina tofauti. Pia tumesikitishwa na kiasi ambacho kampuni ya bima ilitaka kumlipa – inaonyesha 'roho mbaya' waliyonayo kama ulivyosema. Kuna utani wa kawaida dhidi ya kampuni za bima, kwamba hawawezi kutambua kiasi wanachopaswa kulipa kwa waathirika wa upande wa tatu mpaka siku meneja wa bima atakapoathirika na kudai kulipwa kama mtu/mhusika wa tatu. Katika hali kama hii, hakuna haja ya kusubiri sana!

Tunashauri kwamba katika utetezi wako, ilete kampuni ya bima kuwa sehemu ya mashtaka kwa kufuata utaratibu wa kuongeza mtu wa tatu (third party) katika shauri. Ukishtakiwa (wewe) na mtu uliyemsababishia ajali (mpanda baiskeli), omba kibali cha mahakama cha kumleta mtu/mhusika wa tatu (kampuni ya bima) kwa kufuata utaratibu husika kwa kuwa una haki ya kuchangiwa au kufidiwa na kampuni ya bima. Mahakama ikikubali ombi hilo, kampuni itakuwa imeingizwa kwenye kesi husika, na kisheria itatakiwa kujitetea yenyewe.

Mbali na haya, ni lazima pia upeleke mahakamani waraka/taarifa ya utetezi kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja mara baada ya kupokea notisi/hati ya madai.

## Kuondolewa Makaburi ili Kuchimba Madini

**Wazazi wangu hivi karibuni walinijuza kuwa eneo ambalo hutumiwa kama makaburi katika kijiji chetu linataka kuchukuliwa na kupewa mwekezaji wa kigeni, ambaye anataka kuanzisha mgodi. Inaaminika kuwa eneo hili ni tajiri sana kwa almasi. Tunapaswa kufanya nini?**

*21 Septemba 2009*

Suala hili ni nyeti sana. Kwa upande mmoja kuna makaburi ya wanakijiji ambayo hayaingizi mapato yoyote serikalini bali ni kumbukumbu tu kwa wanakijiji. Kwa upande mwingine kuna Serikali mbayo inajaribu kumruhusu mwekezaji ili kuanzisha mgodi ambao utaweza kuwanufaisha wanakijiji na watanzania wote kwa ujumla.

Mtazamo wa mchumi ungekuwa, mgodi una manufaa zaidi kuliko eneo la makaburi. Viongozi wa dini wanaweza kusema kuwa tunahitaji kuheshimu wafu na hatupaswi kuthamini sana mali kuliko mambo ya kiroho.

Sheria inayosimamia suala hilo - Sheria ya Kuondosha Makaburi- inasema kwamba Waziri mwenye dhamana ya ardhi anaweza kuruhusu kaburi au maiti zilizofukiwa humo kuondolewa kutoka kwenye ardhi kama kaburi hilo liko kwenye ardhi ambayo inahitajika kwa manufaa ya umma. Maana ya neno 'kwa manufaa ya umma' imeelezwa kwenye Sheria ya Utwaaji wa Ardhi, ambayo pamoja na mambo mengine, inasema kuwa ardhi itasemekana imechukuliwa kwa manufaa ya umma kama itakuwa ni kwa ajili ya au kuhusu uchimbaji madini au mafuta.

Taratibu za kufuata ni kwa waziri kutoa taarifa ya siku ishirini na moja kwa ajili ya kuondoa makaburi. Katika muda huu wa siku ishirini na moja unaweza kupinga mpango huo huku ukitoa sababu zako. Ukweli kwamba kuna almasi zenye faida kubwa katika eneo hili, kunapunguza nafasi yako ya kufanikiwa.

## Fidia kutokana na Vifo kwenye Ndege ya Yemeni

**Miezi michache iliyopita ndege ya Yemeni ilianguka pwani ya Komoro na kuua abiria wote isipokuwa abiria mmoja. Mume wangu alikuwa kwenye ndege hiyo. Mwili wake**

**ulipatikana katika pwani ya Tanzania na nilisafirishwa na shirika la ndege la Yemeni kuja kutambua maiti. Shirika hilo la ndege linataka kunipatia Dola za Kimarekani 20,000 kama fidia ya kifo walichosababisha. Nimepewa nyaraka fulani nisaini kabla ya kupewa malipo. Japo nina shida ya fedha, lakini ninasita kukubali ukarimu wao. Hata sikuwa nazitarajia. Je, wanajaribu kunitega? Je, nichukue fedha hizo?**

*14 Septemba 2009*

Huo si ukarimu. Kama mjane wa marehemu, una haki ya kulidai shirika hilo la ndege. Kumbuka kwamba umepoteza mpendwa wako, na hakuna kiasi chochote cha pesa kinaweza kumrudisha.

Kiasi ambacho shirika la ndege linatakiwa kukulipa kinasimamiwa na makubaliano mbalimbali ya kimataifa ambayo baadhi yake ni Mikataba ya Vienna na Montreal. Mikataba hii ya kimataifa inasimamia uwajibikaji wa wasafirishaji kwa watu, mizigo au bidhaa kimataifa.

Tutajibu maswali yako moja baada ya jingine: Je, usaini nyaraka husika? Kuna uwezekano mkubwa kwamba nyaraka hizo zitawezesha shirika kuweka kikomo juu ya wajibu wake na kiasi wanachotaka kukulipa, hivyo huwezi kupata zaidi ya Dola za Kimarekani 20,000 ambazo wanataka kukupatia. Je, Dola 20,000 zinatosha? Kiasi hiki ni kidogo ukilinganisha na kiwango kilichotajwa katika mikataba ya kimataifa. Kiasi kinatofautiana kulingana na mahali ulipo, makazi yako na mambo mengine kama hayo, lakini kiasi hicho kiko juu kuliko wanachotaka kukupa. Umeonesha kuwa na uhitaji mkubwa wa pesa, ndiyo maana wamekupa kiwango kidogo.

Je, wanakudanganya? Ndege au kampuni ya bima wanajaribu kupunguza hasara. Unaweza kuita udanganyifu au vinginevyo, inategemea na unavyolitazama suala hilo. Kwa maoni yetu, shirika la ndege au bima wanajaribu kunufaika kupitia kwenu kwa kulipa kiasi kidogo. Kama utachukua fedha au la ni uamuzi wako lakini tunapendekeza utafute msaada wa kisheria kutoka kwa wanasheria wa masuala ya anga mara moja.

Pia tunapenda kukwambia kwamba familia za wahanga wa ajali ya Shirika la Ndege la Ufaransa (Air France) walipewa fidia ya Sarafu ya Umoja wa Ulaya Euro 17,500 kama malipo ya awali tu. Malipo haya yalitolewa na bima ya shirika la ndege bila masharti yoyote. Malipo ya mwisho kwa wahanga hao yanategemea kuwa malaki ya dola kwa kila abiria.

## Bima kwa ajili ya Dhamana/Rehani

**Kwa mara ya kwanza nimechukua mkopo wa shilingi milioni 800 kutoka benki moja jijini Dar es Salaam nikiwa nimeweka nyumba yangu kama dhamana. Benki ilisisitiza kuwa nibadilishe bima yangu ioneshe kuwa benki ndio wafidiwa. Sielewi kwa nini nibadilishe bima yangu kuendana na matakwa yao? Je, wanataka kunilaghai? Kwa nini benki inataka bima? Nani anapaswa kulipia ada ya bima husika?**

*31 Agosti 2009*

Suala la kuchukua mkopo kwa mara ya kwanza halina uhusiano wowote na sheria, na hasa kuhusu bima. Tunavyoongea, nyumba ni mali yako. Hata hivyo, kama utashindwa kurejesha mkopo wako kwa wakati, benki itachukua nyumba yako ili kufidia mkopo.

Hatuna uhakika kama benki inakuomba kubadilisha bima kabisa ili kuonesha jina lake au wanataka na wao waonekane kama wafaidikaji pamoja na wewe. Kama wanataka kuchukua bima hiyo kuwa yao, inaweza kukusababishia madhara/matatizo, kitu ambacho kwa maoni yetu hakikubaliki. Lakini kama benki wanataka kuwa wafaidikaji sambamba na wewe, hicho ni kitu cha kawaida na hatudhani kuwa unadanganywa.

Benki inajali na kufuatilia bima yako kwa sababu ina maslahi ya kulinda kwenye mali iliyowekwa dhamana.

Katika Sheria za Bima, mnufaika lazima awe na maslahi kwenye mali anayoikatia bima, vinginevyo bima hiyo itaonekana batili kwa kuwa itaonekana kama mchezo wa kamari/bahati nasibu.

Mtu ataonekana kama ana maslahi na mali anayoikatia bima kama itaonekana kuwa anapata faida kwa kumiliki mali hiyo au atapata hasara kama mali hiyo itapotea au kuharibika kama janga litatokea.

Kwa mfano, kama jengo unalowekea dhamana litaungua moto, benki haitaambulia chochote kama benki si mmoja wa wafaidikaji wa bima.

Pia unataka kujua nani analipia ada ya bima. Taratibu za soko la Tanzania linamtaka mkopaji kulipia ada ya bima. Unaweza ukazungumza na benki juu ya hilo, kwa kuwa tumeona katika baadhi ya makubaliano benki zikichangia ada ya bima.

## Kushtaki Mgahawa kutokana na Sumu ya Chakula

**Familia yetu ilitoka kwa ajili ya chakula cha jioni katika mgahawa maarufu sana jijini Dar na wote wanne tulipata maumivu makali ya tumbo masaa mawili baada ya mlo huo. Chakula kilikuwa kitamu sana, lakini daktari alituambia kuwa kuna uwezekano mkubwa chakula kilikuwa na bakteria ambao walisababisha maumivu. Je, tunaweza kushtaki mgahawa?**

*24 Agosti 2009*

Unaweza kumshtaki mtu yeyote kwa kitu chochote. Kama ni muhimu kutumia muda au rasilimali zako ni suala jingine - hata hivyo ni uamuzi wako binafsi.

Ingawa huenda ikawa vigumu kuthibitisha kuwa ni mgahawa huu ndio uliosababisha tatizo, unaweza kufungua shauri mahakamani. Hata hivyo, unaweza kwanza kujaribu kumalizana nao nje ya mahakama, na ili kuanza mchakato husika, unapaswa kuutumia mgahawa notisi/taarifa ya madai.

Kama hilo litashindikana, unaweza kumshtaki mmiliki wa mgahawa kwa tendo la uzembe, kwa kuandaa chakula kisichofaa kwa matumizi ya binadamu. Lakini kutokana na kukosekana kwa ushahidi wa wazi, unaweza kumshtaki mmiliki wa mgahawa kwa kushindwa kuwachagua wasambazaji wazuri wa chakula na usimamizi mbovu kwa wafanyakazi ambao wanaweza kuwa wamesababisha maambukizi kwa kushindwa kuosha mikono yao vizuri kwa sabuni.

Kufanikiwa kwa shauri lako kutategemea ushahidi utakaoutoa. Huenda wewe si mgeni pekee uliyepata matatizo hayo - tafuta watu wengine ambao wamekumbwa na tatizo kama hilo. Unaweza pia kushangazwa na taarifa walizonazo wahudumu juu ya hali ya usafi wa mgahawa. Kusanya taarifa nyingi kadiri uwezavyo ili kuthibitisha kesi yako. Jua kwamba mmiliki wa mgahawa pia atapambana na wewe - jitayarishe.

## Majeraha makubwa katika Ukumbi wa Mazoezi ya Viungo/Jimu

**Nilikuwa nikifanya mazoezi kwenye jimu moja jijini Dar, lakini moja ya mashine ilishindwa kufanya kazi na kunisababishia majeraha makubwa sana begani. Waya ulikatika na uzito wote ulinielemea. Kwa bahati nilikuwa kwenye uzito wa kati na kunusurika, lakini majeraha yangekuwa mabaya sana. Jimu hii wana tabia ya kutofanya matengenezo/kukarabati mashine zao. Nilipomwambia meneja, kwa ukali alinionesha maandishi ukutani yaliyosomeka – "Kila mteja anafanya mazoezi kwa madhara yake mwenyewe". Je, hiyo inawaondoa kwenye hatia? Wamehusisha pia mwanasheria wao. Sina**

**imani na wanasheria kwani mara zote uharibu mambo.**

*17 Agosti 2009*

Kwa sababu jimu ina ilani, haina maana huwezi kuwashtaki. Jimu ina wajibu wa kujali wateja wao na kilichotokea ni ushahidi tosha wa kuvunja wajibu huo, ili mradi haukushiriki kwa njia yoyote katika kukata waya. Ukubwa wa majeraha unatufanya tuamini kuwa unaweza kumshtaki mmiliki na meneja wake kwa kushindwa kutekeleza wajibu wao.

Kwa bahati mbaya, hatujaona kesi za aina hii nchini Tanzania lakini mahali pengine kumshtaki mmiliki wa jimu au mkufunzi wako ni jambo la kawaida sana.

Kushirikisha mwanasheria wao ni ishara tosha kuwa wana wasiwasi juu ya hatua unazoweza kuchukua. Suala la kutokuamini wanasheria halina maana. Uwepo wa wanasheria na jinsi wanavyofikiri, kumefanya dunia kuwa mahali pa ufanisi zaidi. Wanasheria wote si malaika , lakini wote si wabaya kama unavyotaka kutuaminisha. Usifikirie mara mbili - ishtaki jimu.

## Kampuni ya Bima inanifuatilia

**Lori langu lilihusika katika ajali kwa kugongana uso kwa uso na basi na gari la abiria kwa wakati mmoja. Dereva wangu amekutwa na hatia na mahakama na kutozwa faini. Kampuni ya bima ambayo basi na gari la abiria walikata bima imeanza kunifuatilia. Wananidai zaidi ya shilingi milioni 200 kwa hasara waliyoipata. Nashindwa kuelewa hili linawezekanaje? Je, hii si kinyume cha sheria?**

*6 Julai 2009*

Hii katika kanuni za bima inaitwa “subrogation” , yaani kuvaa uhusika wa mpokea bima, na ni halali. Kanuni hii inatokana na kanuni ya ulipaji fidia na ni haki ya kampuni ya bima iliyolipa hasara, kumshtaki mtu aliyesababisha ajali kwa kutumia jina la mpokea bima. Ni kanuni inayomwajibisha aliyesababisha ajali na kumzuia mpokea bima kunufaika mara mbili, kwa kudai fidia kutoka kwa kampuni ya bima na mtu aliyesababisha ajali, kitendo ambacho kinaweza kuathiri kanuni za ulipaji fidia.

Ulipaswa kuwa na bima ya mtu wa tatu (third party) ambayo ni lazima. Kama huna, hilo ni kosa la jinai. Kama ungekuwa na bima ya third party, kampuni ya bima ingeweza kuishtaki kampuni nyingine ya bima ambayo ingemlipa mtu wa tatu. Hii ni hali ya kawaida.

Kinachotushangaza ni kwa nini kampuni ya bima ikudai wewe fidia. Inawezekana kwamba hukuwa na bima au bima yako ilikuwa imeisha muda wake au stika ya bima ya mtu wa tatu iliibiwa. Unahitaji kuwasiliana na wakala wa bima yako au wakili kwa mwongozo zaidi.

## Madai ya Bima yamekataliwa

**Julai mwaka jana, nilikata bima kwa ajili ya duka langu dhidi ya wizi katika moja ya makampuni ya bima ya ndani. Walinipa hati ya fidia na hatimaye bima. Hivi karibuni duka langu liliibiwa na kampuni ya bima imekataa kushughulikia madai yangu kwa sababu sikuwa nimelipa ada ya bima. Pesa ya kulipia ilikuwepo lakini kampuni haikuja kuchukua ada yake ya bima. Kwa nini nihangaike? Je, kampuni imekula njama dhidi yangu? Hata hivyo nimewatumia hundi posta kwa njia ya rejista.**

*15 Juni 2009*

Mkataba wa bima ni ule ambao upande mmoja unalipa ada/ujira ili kufidiwa siku za usoni ikiwa hasara au janga lililokatiwa bima litatokea. Tunasikitika na wewe, labda kama sera ya bima husika ilikuwa wazi kuwa kampuni yako ya bima itakuja kuchukua ada ya bima, hatuoni kama kuna uwezekano wa kulipwa. Kwa kawaida ni wewe ndiye unayetakiwa kupeleka ada ya bima kwenye kampuni yako.

Katika madai yako haukulipa ada ambayo

ndio ujira/malipo, na bila kuwa na malipo hakuna mkataba na kwa hiyo hakuna bima. Labda kama kuna mambo mengine ambayo hatujui, hatuoni namna ambayo kampuni ya bima inaweza kukulipa. Wewe utarejeshewa tu malipo ya ada uliyotuma posta kwa njia ya rejista. Pia hatuoni ulaji njama wowote dhidi yako.

Pia tunapenda kukueleza wazi kwamba hii ni mara ya pili au ya tatu kupokea maswali ambapo ada ya bima haikuwa imelipwa!

## Kuumia Kiwandani

**Mjomba wangu anafanya kazi kama mhandisi kwenye kiwanda fulani. Anatumia ngazi katika kazi yake ambayo anapewa na mtunza stoo. Hivi karibuni alianguka kutoka kwenye ngazi kwa kukanyaga sehemu mbovu ya ngazi. Alijeruhiwa vibaya na kupelekwa hospitali. Mwajiri alikataa kuwajibika kwa madai kuwa mjomba wangu alikuwa mzembe katika matumizi ya ngazi. Je, mwajiri ana hatia? Tafadhali nishauri.**

*8 Juni 2009*

Mwajiri ana wajibu wa kuhakikisha usalama kwa wafanyakazi wake. Hasa mwajiri wa kiwandani ana wajibu wa kuhakikisha kuwa kiwanda chake ni salama na vifaa vyake vinatunzwa/kukarabatiwa vizuri. Kwa mfano, kwa mujibu wa Sheria ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi ya 2004, mwajiri ana wajibu wa kuhakikisha kwamba hakuna mfanyakazi wake yeyote ataendesha mashine isipokuwa kama mfanyakazi huyo ana mafunzo ya kutosha ya kutumia mashine, pia awe na ufahamu juu ya hatari zitokanazo na matumizi ya mashine husika. Wamiliki wengi wa viwanda ama hawafahamu sheria hii au hawaifuati.

Kutokana na maelezo uliyotoa hapo juu, inaonekana kama ngazi ilikuwa mbovu na labda ilikuwa haifanyiwi matengenezo, hasa kama sehemu ya ngazi iliporomoka. Ukweli kwamba mjomba wako alipewa ngazi na mtunza stoo hauiondolei wajibu kampuni. Na hata kama mtunza stoo angekuwa amekagua ngazi kuhakikisha usalama wake (kitu ambacho hakufanya), bado kampuni itawajibika kwa uzembe wa mtunza stoo. Labda Kama kuna kitu chochote cha ziada zaidi ya hiki, hatuoni jinsi gani mwajiri wa mjomba wako anaweza kukwepa hili.

Ikiwa hakuna uthibitisho kuwa majeraha yalisababishwa na uzembe wa mjomba wako, basi anayo haki kudai fidia chini ya sheria husika bali pia kudai fidia itokanayo na, au ambayo ni matokeo ya, tukio hilo.

## Kampuni ya Bima ilinidanganya

**Ghala langu liliteketea lote kwa moto. Nilikuwa na bima kutoka kampuni ya ndani ambayo ilinikata 5% ya kiasi cha madai ambacho tulikubaliana. Najihisi kudanganywa. Nimesoma mtandaoni kwamba makampuni ya bima yana tabia za kudanganya wateja wake. Je, nifanye nini?**

*23 Machi 2009*

Kitu ambacho kampuni ilikata kwenye madai yako kwa kanuni za bima kinaitwa "policy excess" yaani kiasi ambacho mteja anawajibika kuchangia katika madai. Ni kifungu cha kawaida/lazima katika mikataba ya bima. Malipo ya ziada huwa ni sehemu ya ada ya bima unayolipa, kwa lengo la kupunguza madai yako madogo madogo ambayo unaweza kuyadai. Kuandaa malipo ya bima ni ghali. Wakati mwingine gharama zinazotumika kushughulikia madai ya bima ni kubwa sana kuliko hata madai yenyewe na ndiyo maana wanaweka "policy excess" kwenye mkataba wa bima.

Kwa kujibu swali lako, hatuna uhakika kuhusu kifungu cha "policy excess" kilichowekwa kwenye bima yako. Ikiwa policy excess ni 5% ya madai ya yako, kampuni ya bima haijakulaghai. Kifungu cha kawaida

ni 5% ya kiwango kinacholipwa au kiasi kilichokubaliwa, kinatumika kiasi cha chini kati ya hivyo. Kama kuna kipengele hicho, basi fanya hesabu kidogo ili kuona ikiwa kampuni imetoza kiwango cha chini kati ya hivyo viwili. Kuhusu ulichosoma kwenye mtandao, zingatia kuwa makampuni ya bima duniani kote yako makini sana kwenye suala la kulipa fidia. Hatuyatetei makampuni ya bima, ila wakati mwingine wanufaikaji wa bima wanalalamika bila sababu za msingi kwa kukosa uelewa juu ya mikataba ya bima waliyoingia.

## Tofauti kati ya Fidia za Jumla na Maalum

**Mmoja wa wateja wetu ameishtaki kampuni yetu si tu kwa uvunjaji wa mkataba ambao niliingia nao, lakini pia kwa kusababisha hasara ya jumla na maalumu. Amekuja na njia za kijanja kuongeza kiasi husika. Nini maana ya fidia za jumla na maalum? Je, naweza kumzuia kudai kiasi chote hiki?**

*30 Machi 2009*

Kwa ufafanuzi, fidia za jumla ni mambo yale ya hasara au uharibifu ambayo hayahitaji kudaiwa au kutajwa kwenye hati yako ya malalamiko ili kuunda ushahidi wa kesi yako. Fidia maalum ni ile ambayo lazima kudaiwa au kufafanuliwa kwa uwazi kabisa ili kushinda. Tofauti hizi mbili zinawachanganya wengi. Namna nyingine ya kuzielezea, fidia za jumla ni zile ambazo sheria inazichukulia kama stahiki unazozistahili kulingana na aina ya shauri, wakati fidia maalum ni zile zimetokana na mazingira fulani kwa kosa fulani, na ni lazima zidaiwe kwa uwazi na zithibitishwe ili kushinda.

Fidia za jumla pia ni aina ya fidia ambazo hutolewa kwa hasara ambazo haziwezi kukadiriwa, kwa mfano, maumivu au kudhalilishwa, kuchafuliwa jina, n.k. Wakati huo huo, fidia maalum ni fidia ambazo hasara zake zinaweza kukadiriwa kama vile matumizi au mapato yaliyopotea.

Huwezi kumzuia kudai kiasi hicho cha 'madai bunifu'. Unachoweza kufanya ni kuandaa utetezi madhubuti dhidi ya madai. Mdai ana jukumu la kuthibitisha madai hayo ili apate fidia.

## Abiria anadai Fidia kutokana na Ajali

**Gari langu lilipata ajali jijini Tanga na mmoja wa abiria alikuwa amejeruhiwa vibaya sana na hivyo dereva wangu alishtakiwa na kutozwa faini kwa kusababisha ajali. Kwa sasa nimeshtakiwa na abiria huyo akidai fidia. Je, nifanye nini?**

*9 Machi 2009*

Hatusemi kuwa tayari una wajibu wa kulipa, kushtakiwa kwa namna ulivyoelezea kunawezekana. Umeshtakiwa kwa kanuni ya kuwajibika kwa niaba (vicarious liability). Kanuni hii inamwajibisha mtu kwa makosa yaliyofanywa na mtu mwingine kwa mfano, bosi kushtakiwa kwa makosa ya mtumishi wake. Kanuni hii hutumika kwa kesi zinazotokana na uzembe. Sheria inatutaka kuwa makini kwa wenzetu katika shughuli zetu za kila siku. Kwa mfano, mmiliki wa daladala anapaswa kumwajiri dereva aliyepitia mafunzo na mwenye leseni. Kama ajali itatokana na uzembe wa dereva kutegemea na maelezo, mmiliki pia anaweza kuwajibika. Kwa kawaida, mmiliki hawezi kujitetea kwamba hakumruhusu dereva kuendesha hivyo.

Kwa upande wako, abiria aliyejeruhiwa anaweza kukushtaki wewe, dereva wako ama kampuni yako ya bima kama akipenda.

Tunakushauri umweke mwanasheria. Kama kesi imefunguliwa dhidi yako, mwanasheria wako anaweza kuiunganisha kampuni ya bima kwenye kesi. Wakili wako atatakiwa kuomba ridhaa ya/kibali cha mahakama ili kuiunganisha kampuni ya bima kwenye shauri, chini ya utaratibu uitwao 'notisi ya mtu

wa tatu' (kuongeza mtu mwingine kwenye shauri). Kutegemea na sera ya bima yako, unaweza au usiweze kufidiwa.

## Kampuni ya Bima kukataa Kulipa Dai langu

**Jengo langu limeungua na kampuni yangu ya bima inasema sitaweza kulipwa kwa kuwa sijalipa ada ya bima. Niliiambia kampuni hiyo kuwa wanaweza kukata ada husika kutoka kwenye madai au ninaweza kulipa ada ya bima sasa hivi, lakini wamekataa. Je, naweza kuwashitaki?**

*23 Februari 2009*

Bima ni mkataba ambao kampuni ya bima inachukua ada kutoka kwa mtoa bima ili kuweza kumfidia wakati wa janga alilolikatia bima. Kwa kawaida ili mkataba huo uwe na nguvu kisheria ni lazima kuwe na janga ambalo halikukusudiwa/halikutegemewa, na mmiliki wa mali iliyokatiwa bima awe na maslahi kwenye mali husika.

Tuchukulie mali ni yako na una maslahi nayo, ada ya bima kwa mujibu wa sera ya bima ni kitu muhimu sana kwenye mkataba wa bima. Labda kama umekubaliana na kampuni yako ya bima juu ya muda tofauti wa kulipia ada ya bima, na uko ndani ya muda huo, ni ngumu sana kushinda.

Makampuni ya bima yanaishi kwa malipo/ ada ya bima inayolipwa kabla ya janga/ hasara kutokea, kwa kawaida kwa mwaka, na kuwekezwa na kampuni ili kuweza kulipa madai yajayo. Kama wabima wote wasingelipa ada za bima kama unavyofanya wewe basi kampuni za bima zisingekuwepo. Kesi yako ni ngumu sana, kama msingekuwa mmekubaliana masharti ya malipo na kampuni yako ya bima, uwezekano wa wewe kulipwa ni mdogo sana kwa kuwa huna mkataba na kampuni yako ya bima.

## Jela kwa kuvuta Sigara hadharani

**Naona watu wakivuta sigara katika maeneo ya umma bila kujali wengine. Je, hii inaruhusiwa?**

*9 Februari 2009*

Kuvuta sigara katika maeneo ya umma imepigwa marufuku na sheria. Sheria ya Bidhaa za Tumbaku ya 2003, ambayo lengo lake kuu ni kupunguza matumizi ya tumbaku na madhara yake kwa watu, kuzuia utengenezaji, usambazaji na matumizi ya bidhaa za tumbaku ambayo ni pamoja na uvutaji sigara katika sehemu za umma. Eneo la umma/wazi ni pamoja na huduma ya afya, maktaba, mahali pa ibada, majengo yaliyoambatanishwa kwa lengo la mikutano ya jamii na kitamaduni, michezo au burudani, maeneo ya chakula ya umma, majengo ya ofisi, usafiri wa umma wa angani, ardhini au majini, mabandani, mazingira yaliyoambatana kama vile masoko, maduka makubwa, na mengine yoyote yaliyozuiliwa mahali ambapo umma unakusanyika. Ni kosa la jinai kuvuta sigara katika maeneo ya umma na yeyote ambaye atatenda kosa hili adhabu yake ni faini isiyozidi shilingi 500,000 au kufungwa kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja. Kama raia mwema unahimizwa kuripoti matukio yoyote ya mtu anayevuta sigara katika maeneo ya umma, katika kituo cha polisi kilicho karibu. Watu wengi hawana ufahamu wa sheria hii.

## Benki inamnyanyasa Mke

**Mimi ni mwanamke niliye katika ndoa. Ndoa yetu imedumu kwa kipindi cha miaka mitatu. Mume wangu ameweka dhamana nyumba yetu ya ndoa bila kunishirikisha na kupata fedha kutoka benki. Ameshindwa kulipa mkopo, na benki imetoa notisi ya kufanya mnada wa nyumba yetu. Je, nifanyeje?**

*2 Februari 2009*

Rehani/poni ni hati ya nyumba au mkataba wa upangaji au kitu chochote kinachotumika kupata mkopo ili kutimiza masharti ya

mkopo. Mtu anayeweka nyumba yake kama dhamana ili kupata mkopo anaitwa mkopaji na mtu anayekopesha anaitwa mkopeshaji na mkataba wa ukopeshaji unaitwa hati ya mkopo/waraka wa rehani.

Nyumba ambayo mmekuwa mkiishi na mumeo ni nyumba ya ndoa/familia. Nyumba ya familia ni jengo/nyumba au sehemu ya jengo ambamo mume na mke kwa kawaida huishi pamoja. Sheria inayoshughulika mikopo nchini Tanzania inatambua haki za mke au mume pale linapokuja suala la nyumba ya familia. Hati ya mkopo haina nguvu kisheria kama haikusainiwa na mkopaji na mke wake anayeishi kwenye nyumba hiyo. Kwa hiyo, dhamana yoyote inayohusu nyumba ya familia ni lazima mke wa mkopaji asaini hati ya mkopo. Sheria inamtaka mkopeshaji kujiridhisha kama mkopaji ana mke au la.

Kama tulivyoeleza hapo juu, hati ya mkopo aliyoisaini mumeo na benki ni batili kwa kushindwa kuzingatia masharti ya hapo juu. Kwa kuwa tayari wamekupa taarifa/notisi ya kupiga nyumba mnada, wahi Mahakama ya Ardhi ukafungue shauri kupinga uuzwaji huo. Kwa maelezo yako, una kesi nzuri na unaweza kushinda.

## Mziki mkubwa, Siwezi kulala

**Je, kuna sheria yoyote ambayo inakataza mziki mkubwa kuchezwa katika maeneo ya makazi ya watu? Kinondoni kuna klabu, na mara nyingi huandaa matamasha ya wazi/hadhara, pati na sherehe, na kupiga mziki kwa sauti ya juu sana na hivyo kuwasumbua wakazi wa eneo hilo. Tafadhali tushauri.**

*9 Februari 2009*

Kitendo cha kufanya matamasha ya umma na kupiga mziki kwa sauti ya juu sana na kusumbua wakazi ndani ya eneo husika ni kosa. Ni kosa ambalo kisheria linajulikana kama kero/adha (nuisance). Adha ni kitendo au hali inayoingilia uhuru wa watu kutumia ardhi yao, afya, usalama, starehe, au mali ya umma.

Mtu atakuwa na hatia ya kusababisha adha kwa umma kama atafanya kitu kinachosababisha majeraha, hatari au kero kwa umma au watu ambao huishi maeneo hayo. Adha ni kitendo kinachoathiri umma mzima au sehemu yake na kinaingilia haki ya utulivu wa watu au jamii kwa ujumla, kwa mfano, kubeba vitu vinavyotoa harufu mbaya au kelele zinazosababisha kero zisizovumilika kama ilivyo kwenye kesi yako.

## Jela kwa kuvuta Sigara

**Nimegundua kuwa mtoto wangu wa kiume mwenye umri wa miaka 16 anavuta sigara. Nimeshtushwa na idadi ya matangazo ya sigara nchini Tanzania. Je, kufanya hivyo si kinyume cha sheria? Nchini Uingereza ambapo nimeishi, kuna udhibiti wa hali ya juu. Kwa nini Tanzania hakuna udhibiti kama huo? Nimegundua pia, hapa migahawa haina sehemu maalum ya kuvutia sigara.**

*12 Januari 2009*

Uvutaji sigara na uuzaji bidhaa za tumbaku nchini Tanzania unaratibiwa na Sheria ya Viwanda vya Tumbaku ya mwaka 2001 na Sheria ya Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku ya mwaka 2003 (TPRA 2003). Ni watu wachache sana wanajua uwepo wa Sheria hii au hata kuizingatia. Kwa kuanzia ni haramu kwa kijana wako wa umri wa miaka 16 kuvuta sigara kulingana na kifungu cha 7 (1) cha TPRA 2003 ambacho kiko wazi sana, na kinasema 'hakuna mtu aliye chini ya umri wa miaka 18 ataruhusiwa kuvuta sigara au kuuza bidhaa za tumbaku.' Sigara ni bidhaa itokanayo na tumbaku. Kama mtu atapatikana na hatia kwa kikiuka kifungu hiki, kama mtoto wako alivyofanya, kwa mujibu wa kifungu cha 33 (2) cha Sheria hiyo, anaweza kufungwa kifungo cha miaka miwili au kutozwa faini ya shilingi milioni 2. Kuna adhabu sawa kwa wale wanaopatikana na hatia ya kuuza bidhaa hizo

kwa watoto walio chini ya miaka kumi na nane. Kujibu sehemu ya pili ya swali lako, matangazo ya sigara nchini Tanzania yana utaratibu wake kulingana na kifungu cha 26 cha TPRA 2003. Moja ya mambo muhimu katika kifungu hiki ni kwamba ni marufuku kwa mtu kutangaza bidhaa za tumbaku akijaribu kuonesha kama bidhaa za tumbaku zina tija/faida kwenye michezo au mafanikio ya riadha, mafanikio ya kitaaluma, ngono, kwamba watu wengi ni wavuta sigara na kwamba kwa ujumla sigara huleta mafanikio katika maisha. Hivyo, kama utaona matangazo yanayoonesha jambo lolote kati ya yaliyotajwa hapo juu, kampuni au mtengenezaji anayetangaza bidhaa anatenda kosa ambalo lina adhabu ya kifungo. Pia si haramu kwa makampuni ya sigara kujitangaza ili mradi wanafuata miongozo ya matangazo. Jibu la sehemu ya mwisho ya swali lako ni kuwa, kulingana na kifungu cha 13 cha TPRA 2003, imeelezwa wazi kuwa 'mtu yeyote ambaye ni msimamizi wa taasisi ya elimu ya juu, jengo la ofisi, hoteli, baa au mgahawa, na sehemu nyingine za starehe, anapaswa kutenganisha vyumba vya wavutaji sigara na wasiovuta sigara.' Mmiliki anatakiwa pia kuhakikisha kuwa kuna chumba tofauti kwa ajili ya kuvutia sigara na kina mfumo mzuri wa kuingiza hewa na kwamba vyumba husika vinatoa ulinzi wa kutosha dhidi ya wasiovuta sigara, pamoja na alama sahihi zinazoelekeza sehemu zinazoruhusiwa na zisizoruhusiwa kuvuta sigara. Wamiliki wa migahawa wanaokiuka utaratibu huo hapo juu, watatozwa faini ya kati ya shilingi milioni 5 na 20, au kwenda jela kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu, au adhabu zote mbil kwa pamoja.

# Migogoro ya Biashara na Malalamiko

**Kutia sahihi kwenye mkataba ni sawa na kupigilia msumari wa mwisho kwenye jeneza lako. Usome kabla ya kuusaini.**

Sura hii inazungumzia maswali yahusuyo walaji/wateja na masuala ya mikataba. Sura hii inajikita katika mikataba ya kibiashara, mikataba kwa ajili ya utoaji wa huduma na bidhaa katika biashara, mikataba ya ushirikiano (ubia), mikataba ya kukodisha na mambo mengine ya namna hiyo. Pia inaelekeza/inaelezea kwa kina juu ya kuandaa mikataba mbalimbali, kutoa mbinu juu ya kusaini mikataba, vipengele vya adhabu, maneno yanayotumika katika mikataba na mengineyo mengi. Kuandaa mikataba na kupata maneno sahihi ni vigumu lakini ni rahisi kufanya - umakini unatakiwa. Kutumia muda wa kutosha katika upembuzi kabla ya kuingia mkataba ni jambo linaloshauriwa.

## Duka la Jirani linashindana na langu

**Nina duka pembezoni mwa barabara kuu huko Arusha. Kwa miaka ishirini iliyopita, mimi na jirani yangu tumeheshimu makubaliano yetu kuwa hatauza bidhaa zinazofanana na zangu. Hivi karibuni alihama na kuuza duka lake. Mmiliki mpya alisaini mkataba kama huo lakini ameanza kuuza bidhaa zinazofanana na zangu. Nina mpango wa kumchukulia hatua - tafadhali nishauri.**

*28 Mechi 2011*

Ingawa tungependa sana kuwa upande wako, tunadhani kuwa mkataba kati yako na jirani yako mpya unazuia ustawi wa biashara. Mikataba inayozuia ustawi wa biashara ni mikataba ambayo mtu hubinya uhuru wake wa sasa au baadaye kuhusu namna ya kufanya biashara yake au biashara na wengine, mara nyingi kwa njia ya agano. Makubaliano haya yanaweza kuchukuliwa kuwa yanazuia ushindani wa kibiashara na hivyo kukiuka Sheria ya Ushindani wa Kibiashara nchini Tanzania. Mikataba mingine kama hiyo tumeiona katika sekta ya ajira, kati ya waajiri na wafanyakazi, hasa wataalamu wa kigeni, ambapo mfanyakazi husaini mkataba na mwajiri kuwa hawezi kufanya kazi kwa mshindani wake yoyote wa kibiashara ikiwa mwajiri wake wa sasa ataendelea kufanya biashara hiyo. Hii pia inachukuliwa kama zuio la biashara. Kwa bahati mbaya, hatuoni namna yoyote ya kutekeleza makubaliano haya kisheria. Kuna uwezekano mkubwa kuwa mkataba wako ni batili. Bila shaka, unaweza kutafuta ushauri zaidi wa kisheria.

## Benki kupelekwa Mahakamani

**Benki yetu imekopesha fedha kwa kampuni iliyowekewa dhamana ya mkopo husika na mtu mwingine. Tumetuma hati ya madai kwa mdeni, ameshindwa kulipa, hivyo ameshindwa kutekeleza wajibu. Tukiwa katika maandalizi ya kudai haki yetu kwenye mkopo na dhamana husika, mkopaji alitushtaki kwa misingi kuwa tunadai kiasi kisicho sahihi. Japo ni kweli kuwa kiasi tunachodai kimezidishwa, kiasi kilichozidi ni chini ya shilingi milioni 1. Je, tufanyeje?**

*21 Machi 2011*

Kuna maamuzi yanayokinzana kutoka mahakama mbalimbali kuhusu uhalali na ufanisi wa hati ya madai iliyokosewa kwenye kiasi cha fedha kinachodaiwa. Katika kesi yenu, inaonekana kama mkopaji amekiri kwamba alikopa na kuna kiasi cha fedha anapaswa kuwalipa. Jambo linalobishaniwa hapa ni tofauti kati ya kiasi anachoamini anapaswa kulipa na kiasi mnachomtaka alipe kwenye hati ya madai. Inaonekana kwetu pia mmekubali kwamba kulikuwa na makosa kwenye kiasi mnachokidai. Kama hivyo ndivyo, yuko sahihi lakini hiyo haimaanishi kuwa hapaswi kulipa! Kukiri kwake kuwa alikopa na hajalipa ni jambo jema kwenu – tumieni mwanya huo kumaliza kesi kwa kukubali kiasi alichokiri.

## Kukosekana kwa Azimio la Bodi

**Mimi ni mbia mkuu na mmoja wa wakurugenzi watatu wa kampuni mashuhuri ya kuzalisha mali jijijni Dar es Salaam. Nilivyosafiri kwenda nje ya nchi majukumu yangu yalibebwa na mmoja wa wakurugenzi. Nimegundua kuwa mkurugenzi huyo alighushi sahihi na azimio la bodi na kukopa shilingi bilioni moja kutoka benki ya kimataifa. Mkurugenzi huyo aliweka rehani moja ya yadi muhimu za kampuni na sasa benki inatushinikiza kulipa mkopo. Je, benki inaweza kutulazimisha kulipa?**

*21 Mei 2011*

Benki inaweza kabisa kutoa shinikizo kwenu, kwani inaamini kuwa imeikopesha fedha kampuni yenu. Swali la msingi ni je

benki itakuwa na haki zipi ikiwa mtashindwa au kukataa kulipa deni hilo. Kuna mambo mengi ya kuzingatia katika jambo hili. Kwa mfano, je, benki ilichunguza na kujiridhisha juu ya uhalali wa sahihi husika? Je, benki ilijua kuhusu mchezo huo mchafu? Je, kuna mali imewekwa rehani? Je, kulikuwa na ishara yoyote ya kuwepo mchezo mchafu ambao ungeishtua benki? Kwa kawaida, ni nani katika kampuni yenu huwa anashughulika na mabenki? Je, unatilia shaka muda na kasi iliyotumika katika kupitisha mkopo? Unapaswa kufanya tathmini ya haya yote na kuamua kama una kesi dhidi ya benki au la. Hoja yako ya msingi inaweza kuwa benki haikufuata utaratibu sahihi wakati wa kutoa mkopo. Huenda ikawa ni safari ngumu, tunakushauri utoe maelezo yote sahihi kwa mwanasheria wako ili akuongoze zaidi.

## Kuuzwa kwa Madini ya Tanzanite kimakosa

**Kwa miaka ishirini iliyopita nimekuwa nikijihusisha na biashara ya mawe ya thamani hapa Arusha. Kama wiki kumi na mbili zilizopita, niliuza mawe nikiamini kabisa kuwa ni madini ya tanzanite. Mnunuzi aliyachunguza mawe hayo na kuyanunua kwa Dola 22,000. Sasa imethibitika kuwa mawe hayo si tanzanite. Nimefanya biashara na mnunuzi huyu kwa muda wa miaka kumi na tukio hili limenisababishia matatizo makubwa. Anataka kusitisha mauzo. Je, nifanyeje?**

*7 Aprili 2011*

Katika swali lako refu pamoja na maelezo yote uliyoyatoa (tumejikita kwenye swali la msingi tu) ukielezea uhusiano kati yako na mnunuzi. Umedokeza kuwa unataka kumrudishia pesa aliyolipia vito. Kwa vyovyote vile huo ni uamuzi wako. Hata hivyo, wewe au mtu mwingine yeyote anaetuandikia, humpatia mtazamo wa kisheria, na sheria ilivyoshughulikia tatizo kama lako. Kisha, utafanya uamuzi wa kibiashara. Kabla ya kuendelea kusoma, tunakutahadharisha kuwa maoni yetu ni tofauti kabisa na kile ambacho unataka kufanya.

Sheria iko wazi tangu mwanzoni mwa karne ya 19 kuwa, kama mkataba haujaweka wazi, muuzaji hubeba hasara itokanayo na kuuza bidhaa kwa bei ya chini, na mnunuzi hubeba hasara itokanayo na kuzidisha malipo. Swali la msingi hapa ni kama mnunuzi anaweza kubatilisha uuzaji wa bidhaa kwa kutokujua 'kisio la thamani halisi' ya vito husika sokoni.

Majibu yetu ni kuwa kama hakuna udanganyifu au ahadi/dhamana ya ubora, kisio la thamani halisi ya mali iliyouzwa, ikilinganishwa na bei iliyolipwa, si kigezo cha kubatilisha mauzo. Hakuna kati yenu aliyejua kuwa hayo mawe si tanzanite, hivyo hakuna udanganyifu. Aidha, kulikuwa hakuna makubaliano kuhusu dhamana ya ubora, ama kwa kusema wazi au kificho. Kwa hiyo, wote wawili mmepata hasara sawa, na mnunuzi hawezi 'kusitisha' mauziano.

Jambo la msingi ambalo hatuna budi kusema – pendekezo lako la jinsi ya kutatua changamoto hii ni la kipekee na linapatikana katika maandiko matakatifu tu. Kama ulivyodokeza katika barua yako kwetu, uhusiano wako na mnunuzi ni muhimu zaidi kuliko Dola 22,000, kwa maana hiyo unaweza kurejesha kwake kiasi alichokulipa.

## Kwa nini niwe na Udhamini binafsi?

**Kuna tofauti gani kati ya udhamini wa kampuni na binafsi, na je benki inaweza kuhitaji zote mbili? Je, kuomba udhamini binafsi ni kinyume na dhana ya kisheria kwamba kampuni hubeba majukumu yake yenyewe nje ya wamiliki wake? Mimi ni mkurugenzi wa kampuni lakini sio mwanahisa. Kwa nini nisaini dhamana ya namna hiyo wakati sipokei gawio lolote au marupurupu mengine ya kifedha kutoka**

**kwenye kampuni?**

*28 Februari 2011*

Kuweka dhamana katika mambo ya mikopo ina maana kuwa unatoa ahadi kuhusu jambo fulani na uthibitisho kuwa deni litalipwa. Kisheria kuna aina kadhaa za udhamini, pamoja na ambazo umetaja - udhamini wa kampuni na binafsi.

Udhamini wa kampuni ni pale ambapo kampuni moja inadhamini kampuni nyingine juu ya malipo yote au sehemu ya mkopo ambao bado haujalipwa na kuahidi kulipa ikiwa mdeni atashindwa kulipa mkopo huo. Nchini Tanzania, mara nyingi udhamini wa kampuni hutokea pale ambapo kampuni mama inadhamini kampuni tanzu, au kampuni ndugu ambayo inamiliki hisa katika kampuni inayokopa. Udhamini huo wa kampuni una nguvu kisheria ikiwa tu umepitishwa na Bodi ya Wakurugenzi, na Kanuni na Mwongozo wa Kampuni husika zinaruhusu kampuni kutoa udhamini huo. Kwa uzoefu wetu, mara nyingi benki katika kutoa mikopo huwa hazipewi maazimio sahihi ya bodi kutoka kwenye kampuni ili kudhamini mkopo, au huwa hazijihangaishi kusoma Kanuni na Mwongozo wa Kampuni kujiridhisha kama bodi ilikuwa na mamlaka ya kufanya hivyo. Hii ina madhara makubwa kwa mkopeshaji anapoamua kuchukua dhamana. Mabenki huishia kulaumu mahakama wanaposhindwa kesi!

Kwa upande mwingine, udhamini binafsi ni dhamana anayoweka mtu binafsi na kuahidi kulipa mkopo wote au sehemu ya mkopo ikiwa kampuni iliyokopa inashindwa kulipa.

Tofauti kubwa kati ya dhamana hizi mbili ni kuwa udhamini wa kampuni unatolewa na kampuni, wakati udhamini binafsi unatolewa na mtu binafsi.

Tukirejea kwenye swali lako kuhusu dhana ya kisheria kwamba kampuni hubeba majukumu yake yenyewe nje ya wamiliki wake, hili ni swali muhimu sana ambalo wakurugenzi wengi na wanahisa ulipuuza. Dhana ya kisheria kwamba kampuni hubeba majukumu yake yenyewe nje ya wamiliki wake ni kanuni muhimu sana katika Sheria za Kampuni ambazo zinatambua kampuni kama mtu kisheria anayejitegemea na ni tofauti na wakurugenzi na wanahisa, na hivyo kulinda mali binafsi za wamiliki na wawekezaji dhidi ya kesi za kampuni. Mkurugenzi au mwanahisa akisaini dhamana binafsi, anajiingiza katika hatari ya yeye binafsi kuwajibika kwa ajili ya madeni ya kampuni. Hiki ni kitu cha kawaida katika baadhi ya nchi, kwani mabenki wanataka kupunguza hasara. Hata hivyo, katika baadhi ya nchi, benki hutoza riba kubwa kama hakuna udhamini binafsi. Kwa bahati mbaya, hili jambo haliwezekani hapa nchini.

Swali lako ni kwa nini uhatarishe mali zako binafsi kwa ajili ya kampuni wakati wewe ni mkurugenzi tu na si mwanahisa? Tunakubaliana na wewe. Kwa nini? Kwa sababu hizi, unaweza kukataa kuhatarisha mali zako binafsi kwa ajili ya mkopo wa kampuni, na hupaswi kuweka dhamana binafsi.

## Kushirikiana na Sekta ya Umma

**Sisi ni kampuni kutoka Australia, kwa sasa tuko kwenye mazungumzo ya kuwa na ubia na Wizara mojawapo Serikalini ili kufanya mapinduzi ya kilimo nchini. Mradi huu utachukua takribani miongo mitatu, na tunataka kuhakikisha kuwa nyaraka ziko sahihi. Tunatambua kuwa mradi huu ni muhimu sana hapa nchini lakini tunataka kujiridhisha na mkataba kabla ya kuwekeza Dola milioni 300 katika mradi huo. Tufuate taratibu zipi? Tunataka kuepuka matatizo yoyote baadaye.**

*14 Februari 2011*

Mradi wako unasimamiwa na Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi,

ambayo ni sheria mpya iliyoanza kufanya kazi hivi karibuni. Chini ya sheria hii, kuna Kitengo cha Uratibu ambacho kiko chini ya Mratibu Mkuu. Kitengo cha Uratibu kinaratibu miradi yote inayoshirikisha sekta ya umma na binafsi, kufanya tathmini, kuchunguza iwapo inatoa thamani ya fedha, kukuza ubia wa sekta binafsi na umma, na muhimu zaidi, kuamua kama mradi huo ni nafuu kwa wizara husika.

Tukirejea barua yako, haiko wazi kama mratibu ameajiriwa au la, na kama kitengo cha uratibu kinafanya kazi - ingawa tuna mashaka, tunakushauri uwasiliane na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), ambapo kitengo hicho kilianzishwa.

Pia kwa mujibu wa sheria, kutakuwa na kitengo cha fedha kwa ajili ya kupitia uwezekano wa kufanyika miradi yenye ubia kati ya sekta ya umma na binafsi na kuhakikisha kwamba ni yenye tija kiuchumi. Ni jukumu la Waziri wa Fedha kuidhinisha. Kumbuka pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni lazima atoe maoni yake ya kisheria kabla ya mkataba husika kusainiwa.

Baada ya kusoma swali lako, inaonekana kana kwamba unafanya majadiliano na Wizara husika bila kufuata utaratibu tuliotaja hapo juu. Pia, tungependa kuongeza kuwa kama umewasilisha pendekezo lako litachukuliwa kama zabuni isiyo rasmi, kwa mujibu wa sheria na kanuni zake zabuni isiyo rasmi, na kwa uelewa wetu, ni zabuni ambazo zinakuwa hazijatangazwa. Kwa ujumla, kwa kuwa huu ni mradi muhimu na unaohitajika Tanzania, unapaswa kuwasiliana na Kituo cha Uwekezaji ambacho kitakusaidia kwa uharaka zaidi. Ni muhimu kuwa, katika mchakato huu, nyinyi au Wizara, hamtavunja sheria.

## Je, Raia wa Kigeni anaweza Kumiliki Ardhi?

**Sisi ni kampuni ya kigeni na tunataka kumiliki ardhi nchini Tanzania. Mhasibu wangu ananiambia kuwa tunaweza kufanya hivyo, lakini mwanasheria anadai haiwezekani. Nimechanganyikiwa kabisa – je, tuendelee na ununuzi wa ardhi? Tutasononeka sana kama haturuhusiwi kumiliki ardhi. Katika enzi hizi ni kitu cha ajabu sana kuwa na sheria ya namna hiyo. Tafadhali tushauri.**

*7 Februari 2011*

Tungependa sana kukufurahisha katika majibu yetu, lakini hatuna jinsi zaidi ya kukuhuzunisha. Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 inatamka wazi katika kifungu cha 20 (1) kuwa hairuhusiwi kabisa raia wa kigeni kugawiwa au kupewa ardhi, isipokuwa tu kwa madhumuni ya uwekezaji chini ya Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997. Kifungu cha 20 (4) kinaongeza zaidi kuwa kwa madhumuni ya sheria hii, kampuni yoyote ambayo hisa zake nyingi zinamilikiwa na wageni itachukuliwa kuwa ni kampuni ya kigeni/ si raia.

Mhasibu wenu anazungumzia kuhusu kifungu cha 435 (2) cha Sheria ya Makampuni ya 2002, ambacho kinasema kuwa kuanzia tarehe ya usajili na kama itaendelea kuwa na usajili, kampuni ya kigeni itakuwa na haki ya kushikilia ardhi nchini Tanzania kama kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria hii.

Utata unasababishwa na Sheria ya Makampuni ambayo inaruhusu makampuni ya kigeni kumiliki ardhi wakati Sheria ya Ardhi inakataza umiliki huo. Hata hivyo, Sheria ya Ardhi inatamka wazi kuwa, bila kujali masharti yaliyowekwa katika Sheria nyingine yoyote, Sheria hii itasimamia ardhi yote au jambo lolote linalohusika ardhi ya Tanzania Bara, na sheria nyingine yoyote inayokinzana au yenye masharti yanayokinzana na Sheria hii, itakuwa batili kwa kadri ya ukinzani/ubatili huo.

Kama umevumilia na kuweza kusoma maelezo yote hapo juu, utagundua kuwa Sheria ya Ardhi ina nguvu zaidi ya Sheria ya Makampuni, na huwezi kumiliki ardhi kama kampuni ya kigeni nchini Tanzania isipokuwa tu kama una usajili chini ya Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997.

Kuhusu kile unachoita 'maajabu' ya sheria, kila nchi ina sera zake, na sera ya sasa ya ardhi nchini Tanzania hairuhusu makampuni ya kigeni yanayokuja Tanzania kuhodhi ardhi kwa lengo la kujinufaisha bila utaratibu. Hakuna kitu cha kushangaza hapo. Kama unahitaji ardhi kwa ajili ya mradi wenu, unaweza kwenda Kituo cha Uwekezaji (TIC) jijini Dar es Salaam na kupata cheti cha motisha (certificate of incentives). Kuna taratibu za kufuata ambazo zimerahisishwa. Kituo hicho kinajulikana kwa ufanisi wake, usisite kuwasiliana nao.

## TRA hawaheshimu Sheria

**Nimeingia mkataba na wakala wa Serikali juu ya mradi wenye umuhimu wa kitaifa na unaofanyika Tanzania yote. Nilipewa misamaha fulani kwa ajili ya mradi ambayo siwezi weka wazi hapa kwani ni siri chini ya mkataba. Kwa miaka miwili ya mwanzo, Mamlaka ya Mapato (TRA) ilikubali misamaha na kutokudai kodi. Tangu Julai 2010, TRA wamekataa kutambua makubaliano hayo, na kudai kuwa misamaha hiyo si halali tena, ingawa mkataba husika haujaisha. TRA wanadai kuwa kuna sheria mpya ambayo inabatilisha makubaliano hayo. Inawezekana vipi idara mbili za Serikali kutoafikiana? Je, nifanyeje? Kampuni yetu ni kubwa na tulikuja Tanzania kwa sababu ya motisha husika. Kwa nini wanatuondolea? Imefanya mradi nzima ukose maana tena.**

*17 Januari 2011*

Kwa kawaida misamaha inayotolewa na Serikali si ya siri, kipengele cha mkataba kinachofanya misamaha hiyo kuwa ya siri kinashangaza sana. Kama tungejua msamaha husika, tungeweza kukuongoza katika hili, kwani nyie si wa kwanza kuathirika na kukosekana kwa mawasiliano kati ya TRA na idara nyingine za Serikali.

Kwanza kabisa, sheria ina nguvu zaidi ya mkataba wowote. Sheria ipo juu ya mkataba, bila kujali mkataba umetayarishwa vizuri kiasi gani hauwezi kubadili sheria. Kisheria, kinachotokea ni kuwa kilichopo kwenye mkataba kinapingana na sheria. Kwa mujibu wa TRA, sheria inachukua mkondo wake na ni kanuni ya kawaida ambayo ni sahihi. Huwezi kusimamisha sheria kwa kuwa hubadilika mara kwa mara.

Iwapo mradi wenu ulitegemea misamaha husika, na mlifanya kwa kuzingatia makubaliano hayo, mna kesi nzuri na mnaweza kuishtaki idara ya Serikali iliyosaini mkataba huo. Hata hivyo, hii inaweza kuchukua muda mwingi na gharama kubwa.

Katika uzoefu wetu, kama mradi una umuhimu kitaifa kama mnavyodai, ni vyema kuitisha kikao cha haraka kitakachohusisha TRA, Idara na Wizara husika. Kama mlipitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kupata misamaha/motisha, basi mnaweza pia kuihusisha TIC. Bila shaka, kama kuna tofauti kati ya sheria na mkataba, TRA hawawezi kulaumiwa moja kwa moja, kwani wao wanatekeleza sheria.

Ngoja tukupe muhtasari kuhusu matumizi mabaya ya misamaha ya kodi, kuna taarifa kuwa sehemu kubwa ya misamaha inatumiwa vibaya, Serikali na TRA wanakabiliwa na shinikizo kubwa kutatua tatizo hili. Pia inadaiwa kuwa Tanzania inatoa idadi kubwa ya misamaha isiyo ya lazima na ambayo kwa ujumla haina tija kiuchumi, na kwa kweli hukwamisha ukusanyaji kodi. Ni wazi kuwa uwepo wa wawekezaji wasio waaminifu kunaumiza utendaji wa wawekezaji wenye nia njema kama nyie.

Yote kwa yote, kama kikao hicho hakitafanikiwa, una kesi nzuri dhidi ya Idara uliyofunganayo mkataba, na unaweza kuwashtaki. Tunapendekeza uwashtaki katika Mahakama Kuu, Kitengo cha Biashara.

## Nani anaidhinisha Rufaa ya Kodi?

**Inasikitisha kuwa TRA wametoa tathmini**

**mbovu ya kodi na ikanibidi niipinge kwenye Bodi ya Rufaa ya Kodi. Nilishangazwa nilipotaarifiwa na mshauri wangu wa kodi kuwa tunapaswa kuwasilisha hesabu zetu kwenye bodi kupinga makadirio ya TRA, hii ni tofauti na sehemu nyingine duniani ambapo mamlaka ya kodi inakuwa ya kwanza kuthibitisha madai yake dhidi ya mlipa kodi. Je, hii ni kweli au ni njama ya mshauri wangu kutaka kujipatia pesa ya haraka haraka kutoka kwangu?**

*17 Januari 2011*

Sheria ya Rufaa ya Kodi ya Mapato iko wazi sana kuwa ni wajibu wa mrufani kuthibitisha kwamba tathmini au uamuzi ulifanyika kimakosa au umepita kiasi. Kwa kuwa wewe ni mrufani, mshauri wako wa kodi yuko sahihi. Hatujawahi kusikia kuhusu mfumo wa mahakama, hata katika 'nchi nyingine', ambapo mrufaniwa anawasilisha kesi yake kwanza. Ni muhimu tukuonye kuwa haya ni mambo yanayogusa mapato ya Serikali na Bodi ya Rufaa ya Kodi haitaki mchezo, kesi hizi husikilizwa na kumalizwa haraka sana.

## Siamini Sahihi

**Ninaingia katika mkataba japo nina wasiwasi kuwa mwenzangu anaweza kuikana sahihi yake. Huwa siamini sahihi. Vipi akiparura tu sahihi yake? Je, ninawezaje kujilinda?**

*10 Januari 2011*

Hili ni swali zuri sana. Njia rahisi ya kujilinda na udanganyifu wowote ni kuwashawishi waweke alama ya dole gumba. Labda waamue kukata vidole gumba vyao, utakuwa umetatua tatizo. Tuna uhakika kuwa wahusika katika mkataba wanathamini vidole gumba vyao zaidi ya mkataba husika.

Uko sahihi kabisa, sahihi inaweza kusababisha matatizo - watia sahihi wanaweza kuzikana. Hata hivyo, kuna njia nyingine za kuthibitisha kuwa kulikuwa na mkataba halali. Kwa mfano, mkataba unapaswa kugongwa muhuri wa kampuni. Vilevile, unaweza kusema kuwa muhuri wa kampuni unaweza kughushiwa. Vigezo vingine vinaweza kuwa malipo yaliyofanyika na utekelezaji wa baadhi ya majukumu katika mkataba. Vigezo vyote hivi vinaweza kutumika dhidi ya upande unaoikana sahihi yake katika mkataba. Unaweza pia kuthibitisha sahihi zao kwa kulinganisha na sahihi zilizopo kwenye hati zao za kusafiria/pasipoti na kutunza nakala ya pasipoti hizo. Kama bado una wasiwasi, wasiliana na mwanasheria wako, ambaye anaweza kuandaa viapo juu ya mkataba husika.

## Kesi iliyofunguliwa Kimakosa

**Niliishtaki kampuni jijini Dar es Salaam kwa ukiukwaji wa mkataba, niligundua, baada ya kufungua kesi, kuwa ukiukwaji haukusababishwa na yule niliyemshtaki. Kilichotokea ni kuwa mmoja wa wakurugenzi wenzangu, ambaye alikua ng'ambo kwa mwaka mzima kwa ajili ya matibabu, aliidhinisha ucheleshwaji mizigo katika mkataba, ambacho ndo kiini cha kesi husika. Sikufahamu kama kulikuwa makubaliano hayo nikaishtaki kampuni husika. Je, mnashauri nifanye nini? Je, mkurugenzi mwenzangu alipitiliza mamlaka yake?**

*3 Januari 2011*

Chini ya sheria zetu, baada ya kesi kuwa imefunguliwa, mdai anaweza, wakati wowote, kuiondoa kesi hiyo mahakamani. Kwenye suala hili, una uhuru wa kufanya hivyo, ingawa mshtakiwa anaweza kudai kurudishiwa gharama. Pia lazima uwe na uhakika kuwa unataka kuiondoa kesi, kwa sababu mara tu ukifanya hivyo, sheria hiyo itakuzuia kuifungua kesi hiyo kwa mara nyingine. Katika kujibu swali hili, tumechukulia kuwa wewe ndio mdai pekee kwenye shauri.

Kwa bahati mbaya hatupo kwenye nafasi

nzuri ya kujibu sehemu ya pili ya swali lako, kwa kuwa hatuna taarifa za kutosha. Ingawa, lazima tukwambie kuwa inashangaza kuona ni kwa vipi, nyie wakurugenzi wawili hamuwasiliani, inaweza kuwagharimu kwenye kampuni yenu siku za usoni, sio tu kwenye kesi hii ila hata mambo mengine ya kibiashara. Mnapaswa kurekebisha mapungufu kwenye mawasiliano haraka iwezekanavyo.

## Mmiliki wa Zamani anaitaka Ardhi yangu

**Nilihama na familia yangu kutoka kijijini kwangu kuja Dar es Salaam miaka kumi na sita iliyopita, na kupata makazi katika eneo liitwalo Tegeta. Wakati nahamia hapa, kulikuwa na watu wachache sana katika eneo hili. Kama miaka miwili iliyopita, mtu anayeonekana kuwa tajiri, alikuja kwenye eneo langu na kuniambia napaswa kuondoka, kwa kuwa lile eneo ni mali yake. Alinionesha mkataba wa zamani na Hati Miliki ya Ardhi kuonesha kwamba ni mmiliki halali na aliuziwa kabla sijahamia eneo husika. Miezi michache iliyopita, mtu huyo alikuja na polisi kujaribu kuniondoa kwa lazima. Je, sheria ya ardhi inasemaje? Je, anaweza kuingilia haki zangu namna hii?**

*27 Desemba 2010*

Sheria ya Tanzania iko wazi kuwa mtu yeyote mwenye hati miliki ya ardhi, alimaarufu kama '*title deed*', anapaswa kuendeleza ardhi ndani ya muda muafaka au kwa mujibu wa maelekezo/masharti yaliyotolewa katika hati miliki husika. Hatuna uhakika mtu huyo alikuwa wapi kwa zaidi ya miaka kumi na sita. Ni wazi kuna kitu hakipo sawa hapa.

Sheria ya Ardhi inatambua umiliki wa ardhi baada ya kutelekezwa na mmiliki wa awali, hasa baada ya mgeni kuikalia na kuindeleza kama yake kwa kipindi cha muda usiopungua miaka kumi na mbili au zaidi, hivyo basi mtu aliyekalia eneo kwa kipindi cha miaka kumi na miwili au zaidi atajitwalia eneo kwa njia ya umiliki baada ya kutelekezwa na mmiliki wa awali. Mtu aliyejitwalia au kujimilikisha ardhi baada ya kutelekezwa na mmiliki wa awali ana haki sawa na mmiliki wa awali mwenye hati miliki.

Zaidi ya hayo, sheria inaruhusu mmliki aliyejitwalia ardhi baada ya kutelekezwa na mmiliki wa awali kuomba na kupewa hati miliki ya eneo husika. Kwa hiyo, kama kila ulichosema hapo ni kweli, na haujaficha taarifa yoyote, basi wewe ni mmiliki halali wa eneo husika na kufukuzwa kwako hakukuwa halali.

Kuhusu polisi kuingilia, ni mpaka kuwe na amri ya mahakama ya kukuondoa, bila hivyo polisi hawawezi kukuondoa.

## Rehani/Poni dhidi ya Kukodisha/ Kupangisha

**Tulikopesha kampuni fedha na wakaweka jengo lao rehani. Mahusiano yetu yamekuwa mazuri kwa miaka mitatu. Mapema mwaka huu kampuni imeanza kushindwa kulipa mkopo kwa wakati na tukawapa notisi ya kuuza dhamana yao. Inaonekana mkopaji amemtaarifu mpangaji, ambao wanalindwa sana na sheria za Tanzania, ambaye alipata hati ya zuio kutoka mahakamani, akisema wameshalipa kodi ya nyumba ya miaka mitatu ijayo. Kwa sasa hatuwezi kuipata tena hela tunayoidai, wala kuuza mali zao, na mkopaji anaendelea kukiuka mkataba. Je, tufanyeje?**

*22 Novemba 2010*

Ni vigumu sana kukupa ushauri juu ya hili bila kusoma nyaraka zote. Hata hivyo, kwa kawaida, mlipaswa kuwa na kipengele kwenye mkataba ambacho kinakataza kupokea kodi ya jengo lililowekwa rehani kwa muda unaozidi mwaka mmoja. Inawezekana hamkuwa na kifungu cha namna hiyo.

Kama mkopaji amekiuka masharti ya

mkopo, na wewe hutaki kujiingiza kwenye mgogoro wa kimahakama na mpangaji wa sasa, tunaamini kwamba endapo zuio litaondolewa, unaweza ukaendelea na uuzaji wa jengo lililowekwa rehani, na mnunuzi kulinunua kwa sharti la kuheshimu mkataba wa upangaji. Pia, tungependa kupitia mkataba wa upangaji – inawezekana mkopaji amekula njama na mpangaji, ambapo ni vigumu kuthibitisha. Ukweli kuwa kuna mpangaji wa muda mrefu kutaathiri bei ya kuuzia, na kuna mambo unayopaswa kuzingatia kabla hujafanya jambo lolote. Ni busara kuwasiliana na wakili wako kupata suluhisho sahihi ambalo litazingatia muda na fedha zinazohitajika kutatua tatizo hili.

## Usajili wa Stakabadhi ya Mkopo/ Karadha

**Tulimkopesha fedha mtu binafsi na akaweka dhamana ya nyumba ya mtu mwingine. Karadha ambazo zimesainiwa hazijasajiliwa kwa kipindi cha miezi sita kutokana na kutoonekana kwa faili kwenye Mamlaka ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Baada ya kupatikana kwa faili hivi karibuni, BRELA wamekataa kusajili karadha husika. Je, unashauri tufanyeje?**

*22 Novemba 2010*

Sheria iko wazi kuwa kila mali ya kampuni inayowekwa rehani na kampuni ni batili dhidi ya mfilisi, msimamizi, au mkopeshaji wa kampuni kama maelezo ya rehani/ dhamana (yaani stakabadhi ya mkopo) hayatawasilishwa kwa Msajili kwa ajili ya usajili ndani ya siku arobaini na mbili kutoka siku yalipoandaliwa. Karadha inaangukia kwenye kundi hili na hivyo ilipaswa kusajiliwa ndani ya siku arobaini na mbili.

Una njia kadhaa za kufuata. Kwanza unaweza ukaweka tarehe nyingine kwenye stakabadhi ya mkopo na kumpata mkopaji na kumsihi asaini upya kwa tarehe ya sasa na kuhakikisha kumbukumbu zimewekwa sawa. Wakopaji wengi hawataki kufanya hivi wakiwa wamekiuka masharti ya mkopo. Tunatumaini hivi sivyo.

Njia nyingine ni kuomba muda wa nyongeza mahakamani ili kusajili dhamana husika kwa kutumia kifungu cha 105 cha Sheria ya Makampuni 2002 (Sura ya 212) ambacho kinasema, kwa maneno mengi, kwamba ikiwa kampuni inashindwa kusajili dhamana ndani ya muda, basi inaweza kukata rufaa mahakamani ili kuongezewa muda wa kufanya usajili, ikiwa tu kushindwa huko kufanya usajili ndani ya muda kulitokea kwa bahati mbaya au kulisababishwa na sababu nyingine za msingi.

Sababu zako ni za msingi kwani ulishindwa kusajili dhamana husika kutokana na kutoonekana kwa faili la kampuni, kwa bahati mbaya hili sio jambo linalotokea mara kwa mara. Tafadhali zingatia ushauri.

## Kuhifadhi jina la Kampuni

**Sisi ni kampuni ya kigeni tunaotaka kujisajili nchini Tanzania. Jina la kampuni yetu linajulikana vizuri sana kote Ulaya Mashariki na Asia. Nimesikia baadhi ya watu wakiongea sokoni kuhusu wizi wa majina, kuwa mara tu tutakapoanza mchakato wa usajili, jina letu litasajiliwa haraka haraka na mtu mwingine kabla ya kukamilika usajili wetu, na kisha tutatakiwa kununua jina hilo kutoka kwa watu hao. Je, tunawezaje kujilinda? Tumelitafuta jina tunalokusudia kusajili kwa njia ya kawaida, bado halijasajiliwa.**

*22 Novemba 2010*

Hatujawahi kusikia au kukutana na madai kama hayo, hata hivyo tutajibu swali lako. Baada ya kuwasilisha maombi ya jina fulani, unaweza kumwomba Msajili kuhifadhi jina hilo. Sheria ya Makampuni ipo wazi kuhusu jambo hili, kuwa Msajili anaweza, kwa maombi ya maandishi, kuhifadhi jina wakati taratibu za

usajili wa kampuni au kubadili jina la kampuni ukiendelea. Utunzaji wa jina wa namna hiyo utakuwa na nguvu kisheria kwa kipindi cha siku thelathini, au kwa sababu maalum msajili anaweza kuongeza muda kwa kipindi kingine kisichozidi siku sitini, katika kipindi hicho hakuna mtu au kampuni nyingine itaruhusiwa kusajili jina hilo.

Tambua kwamba hakuna jina lilonaweza kuhifadhiwa, na hakuna kampuni inaweza kusajiliwa kwa jina ambalo, kwa maoni ya Msajili, ni sawa au linafanana na majina ya yanayoonekana katika orodha ya majina ya makampuni au vinginevyo si zuri.

Sheria inakulinda, na tunapendekeza uteue wakala mzuri wa usajili au kampuni ya kisheria ili kuendelea na mchakato husika.

## Mahusiano kati ya Mhusika Mkuu na Wakala wake

**Niliteua wakala mjini Mbeya kusimamia bidhaa za plastiki kwa ajili ya kampuni yetu. Katika mwaka wa kwanza kwa kushirikiana uhusiano wetu ulikuwa mzuri. Lakini mwaka wa pili, wakala huyu alianza kuchelewesha malipo, kushindwa kutunza mahesabu vizuri, na hivi karibuni amekuwa akidai kwamba mfumo mzima wa mahesabu hautoi uhakika wa kutulipa. Je, tunalishughulikiaje jambo hili, la yeye kushindwa kuweka mahesabu vizuri ya bidhaa tulizomletea? Je, tufanyeje?**

*15 Novemba 2010*

Ni wajibu wa wakala kuweka hesabu sahihi za mauzo yake yote na kuwa tayari wakati wote kuziwasilisha kwako, mhusika mkuu. Kama atashindwa kuweka hesabu sahihi, kuna dhana kuwa kila kitu kitapimwa na kuamuliwa kwa faida ya mhusika mkuu. Hivyo, kama wakala amechanganya mali zake na zako, vitu vyote ambavyo atashindwa kuvibainisha kuwa ni vyake vitachukuliwa kuwa ni vyako. Aidha, mara nyingi mikataba ya kawaida ya uwakala husema kuwa vitabu na nyaraka zote zinazohusiana na biashara ya mhusika mkuu ni lazima, zikihitajika, zikabidhiwe kwake mara moja.

Katika shauri lako, unaweza kusitisha mkataba wa uwakala kwa kuzingatia kipengele husika cha mkataba. Hata hivyo, unapaswa kuzingatia madhara ya kufanya hivyo kisheria na kibiashara.

## Kushikilia Mali kinyume cha Sheria

**Agosti mwaka 2009, rafiki yangu aliniomba kutumia gari langu aina ya Toyota kwenda kutalii mbuga za Serengeti. Gari langu lilipaswa kurudishwa mwezi Oktoba, mpaka sasa gari langu halijarudishwa. Nimeshuhudia gari hilo likiendeshwa Dar es Salaam na watu wengine nisiowafahamu. Je, ninawezaje kuirejesha Toyota yangu? Ninapoteza mapato ya kukodisha.**

*8 Novemba 2010*

Ni wazi kuwa rafiki yako alipata gari hiyo kwa ridhaa yako kwa kipindi cha miezi miwili. Baada ya miezi miwili iliyotajwa inaonekana rafiki yako aliendelea kulitumia gari lako kimakosa, hivyo una haki ya kurejeshewa umiliki. Umeomba akurudishie gari lako, lakini rafiki yako amegoma kulirudisha. Kisheria hii inajulikana kama kubadilisha matumizi (conversion) na unaweza kufungua mashtaka na kudai fidia. Ikithibitika mahakamani, suluhisho litakuwa kurejeshewa gari au kulipwa thamani ya gari. Aidha, fidia pia inaweza kutolewa. Hata hivyo, ili kufanikiwa katika kesi ya kubadili matumizi, lazima uthibitishe kwamba ulidai kurudishiwa gari hiyo ya Toyota na rafiki yako alikataa. Tunakushauri kuwaona wanasheria wako ili kumwandikia hati/notisi ya madai ambayo itatumika kama ushahidi wakati wa kesi kwamba ulitumia njia rasmi kudai kurudishiwa gari lako.

## TRA inatunyanyasa

**Kampuni yetu imefanya uwekezaji mkubwa sana nchini Tanzania, na tunatarajia kunufaika ndani ya muda mrefu. Zaidi ya miaka miwili iliyopita tumeshuhudia unyanyasaji mkubwa unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Meneja katika mkoa wetu huniambia hadharani kwamba wamewekeana malengo ya kukusanya mapato na hivyo hawataki mchezo. Kwa mfano, tunapigiwa simu kuelekea mwisho wa mwezi ili kujua ni kiasi gani cha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) tutalipa. Inaonekana TRA wamenuia kutoza makampuni makubwa tu ambayo tayari yanalipa kodi nyingi. Inaonekana kuna watu wengi ambao hawalipi kodi na TRA haiwakagui. Swali langu linafuatia. Tumekuwa tukiletewa makadirio ya kulipa kodi ambazo hazina uhalisia wowote. Ni makadirio tu na hakuna ukaguzi wa mahesabu. Meneja wa kodi ananiambia kwamba tunaweza kuzungumza kuhusu kupunguza kiasi hicho. Kwa maoni yetu hatuna deni. Kwa maoni ya TRA, wanatudai kodi zaidi ya shilingi bilioni mbili. Upande wa pili ni kwamba TRA hawajaturudishia malipo yetu ya VAT licha ya kuomba kulipwa miezi tisa iliyopita. Je, tufanye nini, TRA ni kama wanalipiza kisasi? Ni kwa namna gani kampuni za kigeni zinaweza kudumu Tanzania kwa matumizi haya mabaya ya mamlaka/madaraka?**

*20 Septemba 2010*

TRA inaendeshwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zingine. Hata kama Serikali inataka kuongeza kiasi cha mapato inachokusanya kupitia kodi, TRA inapaswa kufuata taratibu zilizopo. Pia tumeshtushwa na jinsi tathmini hiyo ilivyotolewa bila kufanya ukaguzi, labda kama kampuni yenu haikutoa ushirikiano kwa TRA wakati au baada ya ukaguzi.

Kwa mujibu wa Sheria ya Rufaa ya Kodi ya Mapato, mtu yeyote ambaye hakubaliani na makadirio yaliyofanyika anaweza kuwasilisha taarifa ya pingamizi kwa Kamishna Mkuu. Taarifa hiyo ya pingamizi lazima ieleze sababu za kupinga na kupelekwa kwa Kamishna Mkuu ndani ya siku thelathini kutoka siku ya makadirio. Kwa bahati mbaya, wakati tunajibu swali hili, siku thelathini zimekwisha na tunaamini kwamba tayari umefanya hivyo.

Jambo pekee katika pingamizi hili kuhusu makadirio ni kwamba wakati utakapoliwasilisha, mtu anayeishughulikia ni lazima alipie Bodi na kuna nafasi ya kukata rufaa zaidi kwenye Baraza la Rufaa za Kodi ya Mapato. Na kama hukuridhika, rufaa ya mwisho inaweza kufanywa kwenye Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ambayo ni nafasi ya mwisho. Tunapendekeza kwamba ufuate utaratibu huo hapo juu.

Wakati unapozungumza na wafanyakazi wa TRA, tafadhali tambua kwamba ni sehemu ya utaratibu wao wa msingi wanapotoa huduma, kuwajali wateja, kwa ukarimu na kiurafiki. Kama una tatizo kuhusu hili, tafathali mwandikie Kamishna Mkuu ambaye ataweza kushughulikia tatizo lako.

## Dalali wa Mahakama anazuia Mauzo kuendelea

**Miaka miwili iliyopita nilimshtaki mtu kwa kuvunja mkataba wa kibiashara. Mali ya mdaiwa ilibainishwa, kushikiliwa na kuuzwa. Dalali wa mahakama aliyetekeleza amri ya mahakama alinipa 1/3 ya mauzo na kuchukua kiasi kilichosalia. Nadhani hii haikuwa sawa - alisema tu kwamba hiki ndicho kiasi nilichopaswa kulipwa. Je, hii ni sawa kisheria?**

*13 Septemba 2010*

Hakuna sababu ya msingi yeye kufanya hivyo, wala hatufahamu sheria yoyote inayoruhusu tabia hiyo ya Dalali wa Mahakama. Kisheria, ada zote, malipo na posho zingine

zinazolipwa kwa Dalali wa Mahakama au afisa anayetekeleza amri ya mahakama zinapaswa kuwasilishwa mahakamani. Si jukumu lao kuamua kiasi gani wachukue.

Dalali wa mahakama anatakiwa kuwasilisha madai yake ya gharama mahakamani ndani ya siku ishirini na moja na mahakama itaamua kiasi gani kilipwe baada ya kusikiliza pande zote. Ada, gharama na posho zinazotozwa zinajumuisha gharama za matangazo, kuandaa orodha ya mali husika, na gharama zote za kuhakikisha usalama wa mali zinazoshikiliwa. Dalali huyo wa mahakama anaweza kuwa amevunja sheria na una haki ya kuchukua hatua dhidi yake.

Katika kujibu swali hili, tunachukulia kwamba mapato ya mauzo hayakukidhi kikamilifu kiasi kilichoamuriwa. Ikiwa kiasi kilichopatikana ni kikubwa kuliko kilichoamuriwa, jibu letu linahusika zaidi. Tunapendekeza uwasiliane na wakili wako kwa mwongozo zaidi.

## Kuvunja Mkataba kwa Maridhiano

**Nimeingia katika mkataba wa kusambaza malighafi za kutengenezea vifaa vya umeme wa jua. Bidhaa zinatakiwa kusafirishwa kwenda China, na kampuni husika imenitumia mkataba wa miaka mitatu kwa lugha ya Kichina. Mimi sina haki ya kuvunja mkataba, bali muagizaji wa bidhaa. Nimetafsiriwa mkataba huo, na kugundua kwamba kuna kifungu cha kusitisha mkataba kwa maridhiano. Je, hiyo haikiuki madhumuni ya kuwa na mkataba huu? Pia kuna kifungu juu ya kufanya mazungumzo ikiwa bei ya malighafi itayumba kwa ongezeko au punguzo la 10%. Je hii ni sawa?**

*23 Agosti 2010*

Umetafsiri mkataba katika lugha ya Kiingereza/Kiswahili, lakini kwa uhakika utakwenda kusaini mkataba ulioandikwa kwa Kichina. Itakuwa hekima kwako kumwomba muagizaji akutumie mkataba ulio katika lugha ya Kiingereza/Kiswahili. Tafsiri ina changamoto zake na kuna kesi nyingi za namna hiyo ambapo neno moja au mawili katika lugha moja yanaweza yasiwe na tafsiri ileile kwenye lugha nyingine, na hivyo kusababisha migogoro ambayo huchukua miaka mingi kutatuliwa.

Kifungu kinachohusu kusitisha mkataba kwa maridhiano hakipingani na lengo la mkataba. Chini ya Sheria ya Mikataba, wahusika hawana tu uhuru wa kuingia katika mkataba bali pia wana uhuru wa kusitisha mkataba kwa makubaliano. Kifungu hiki kitatamka kuwa ikiwa pande zote zinataka kuvunja mkataba, zina haki ya kufanya hivyo. Hata hivyo, tunaona kipengele hicho kikikinzana na mtazamo wako wa kutokutaka kuvunjwa kwa mkataba. Ili tuwe na uhakika ni muhimu tusome mkataba wote.

Pia tungependa kusema kwamba kifungu cha kuvunja mkataba kwa ridhaa ya pamoja hutokea mara chache, na hakiongezi thamani yoyote ya mkataba unapoandaliwa. Ni muhimu kupata maoni ya wakili wako kabla ya kuingia mkataba huu.

Kama kifungu cha mapitio ya mkataba kinaleta mantiki katika biashara yako, hayo ni maamuzi binafsi ya kibiashara. Tuseme tu kuwa ni lazima kubainisha mambo muhimu wakati wa mapitio ya mkataba, mazungumzo hayo yatadumu kwa muda gani, na nini kitatokea ikiwa hayatafanikiwa. Kwa mfano, unaweza kuwa na kifungu ambacho kinasimamisha utekelezaji wa mkataba katika kipindi hicho cha majadiliano.

## Kutekeleza Wajibu dhidi ya Tarehe ya kuanza Mkataba

**Nilisaini mkataba Juni mwaka 2009 na kuanza kutekeleza wajibu wangu chini ya mkataba kama msambazaji. Nilihitimisha wajibu wangu mwezi Agosti 2009, na kisha kuambiwa kuwa tarehe ya kuanza mkataba**

**haikuwa mwezi Juni 2009. Kwa uzoefu mkubwa nilionao, nimelipokea suala hili kwa mshangao mkubwa, jinsi gani kampuni kubwa kama hii imeshindwa kufuata utaratibu. Je, kipengele hicho cha mkataba kinaleta maana yoyote kwenu?**

*2 Agosti 2010*

Ni bahati mbaya kwamba katika uzoefu wako wote, hujawahi kukutana na mkataba ambao una tarehe ya utekelezaji (tarehe ya kuanza) ambayo ni tofauti na tarehe ya kusaini mkataba. Tarehe ya kusaini haimaanishi moja kwa moja kwamba unapaswa kuanza utekelezaji siku hiyo hiyo. Tarehe ya utekelezaji au tarehe ya kuanza ndio ambayo inatumika kuonesha wakati gani utekelezaji wa mkataba unaweza kuanza.

Kwa upande wako, umetekeleza wajibu wako kabla ya tarehe sahihi ya kukamilisha, na hivyo kucheleweshewa malipo. Ni vigumu sana kukwambia nini cha kufanya pasipo kusoma mkataba mzima. Lakini jambo moja ni dhahiri - kampuni haiwezi kukataa kwamba umetekeleza wajibu wako, isipokuwa kama huduma zilizotolewa ni za kitaalamu sana au zinazingatia muda uliopangwa. Kampuni haitakuwa na haki ya kufanya ilivyofanya, kama wakati unatekeleza mkataba, kampuni hii iliona kwamba utendaji umeanza, na haikuchukua hatua zozote kukutaarifu tarehe ya utekelezaji. Suala hili linaweza kuwa gumu sana, itategemea na maneno yaliyotumika kwenye mkataba husika.

## Hundi yenye Tarehe ya mbele imetolewa kabla ya Muda

**Nilitoa hundi ya tarehe ya mbele na mhusika akaipeleka benki yake. Kabla ya siku ya kuiva kwa hundi, benki yangu ilitoa kiasi husika kwenye akaunti yangu na kuwapa. Imenibidi nisitishe malipo ya hundi husika, kwa kuwa muuzaji niliyemwandikia hundi hakuwahi kuleta bidhaa zangu kwa muda muafaka. Je, nifanyeje?**

*26 Julai 2010*

Kuna masuala mawili tofauti hapa. Kwanza, ni kutokuleta bidhaa kwa wakati, kitendo ambacho kinaweza kabisa kuvunja mkataba. Unaweza kumshtaki muuzaji kwa kukiuka mkataba na kurejesha fedha yako.

Suala la msingi zaidi tunaloliona hapa ni kitendo cha benki yako kushughulikia hundi kabla ya tarehe iliyoelekezwa na hundi. Hundi ya tarehe ya mbele ni hawala ambayo ina tarehe ya mbele ya tarehe ya kuidhinishwa kwake. Benki inayofanya malipo hairuhusiwi kulipa hundi ya tarehe ya mbele na kutoa fedha kwenye akaunti ya mteja wake kabla ya tarehe husika. Benki inayotoa malipo pia haipaswi kuichukulia hundi kama madai yaliyowasilishwa ili kupitishwa na kuchukua fedha ya mteja kulipa hundi husika. Una kesi nzuri dhidi ya benki kwa kufanya malipo kabla ya tarehe ya hundi kuiva. Kwa kuzingatia mambo mengine, unaweza pia kupata fidia kutoka benki.

## Kununua sehemu ya Kampuni

**Ninanunua 15% ya kampuni na sina uhakika jinsi biashara hii inafanyika. Katibu wa Kampuni kwa kipindi fulani alizungumzia kuhamisha hisa, na baadaye kugawanya hisa. Lengo langu ni kumiliki 15% ya hisa kwenye kampuni. Je, ninunue sehemu ya kampuni? Je, ni makubaliano gani muhimu ninatakiwa kufanya katika biashara hiyo?**

*12 Julai 2010*

Hatuwezi kukuamria kama ununue 15% ya hisa au la. Huo ni uamuzi wako na sio wetu na hivyo hatuwezi kujibu sehemu hiyo ya swali lako.

Wewe au Katibu wa Kampuni mnaonekana kuchanganya kuhamisha hisa na kugawanya hisa. Kuhamisha hisa ni pale ambapo mwanahisa anaweza kuhamisha hisa zake

kwako, kwa ujira fulani. Hiyo itaondoa umiliki au wanahisa wake na kukuwezesha wewe kuwa mwanahisa. Katika uhamisho huo, unapaswa kutoa ujira kwa mwanahisa ambaye anahamishia hisa kwako. Kuhamisha hisa ni mojawapo ya njia ambayo unaweza kumiliki kampuni hii.

Njia ya pili ya umiliki ni kampuni yenyewe kukupatia hisa za thamani fulani. Kiasi unacholipa kwa mgawo huo hulipwa kwa kampuni. Katika mgawo wa hisa, utahitaji mkataba wa kugawiwa hisa ambao utasimamia uhusiano wako na kampuni. Nyaraka nyingine muhimu katika manunuzi hayo ni mkataba wa wanahisa ambao utasimamia uhusiano wako na wanahisa waliopo/wengine. Mara nyingi, aina hii ya makubaliano hupuuzwa na wanachama, lakini ni nyaraka muhimu sana kwa wanahisa. Si jambo la busara kujadili makubaliano ya wanahisa bila kusoma na kuelewa mkataba wa wanahisa.

## Sahihi kughushiwa kwenye Hundi

**Mhasibu wetu msaidizi amekuwa akichukua fedha kutoka benki kwa niaba yetu kwa miaka mingi. Hivi karibuni alitumia moja ya nakala ya hundi, akaghushi sahihi za wakurugenzi wote, na kuchukua zaidi ya Dola 100,000. Sahihi zilizoghushiwa zinafafana sana na sahihi halisi, lakini ukizitazama kwa makini utagundua tofauti. Benki inadai tulifanya uzembe kumwamini mfanyakazi, na wamelipa pesa kwa nia njema. Benki pia inadai kwamba alikuwa wakala aliyeidhinishwa na kampuni, na hivyo hatuwezi kudai chochote kutoka benki. Je, tunapaswa kufanya nini?**

*19 Julai 2010*

Benki inayofanya malipo huwa ni wakala wa mteja wake. Kama wakala, benki inayofanya malipo ina haki ya kufidiwa kwa malipo yoyote iliyofanya ikiwa tu kama imefanya hivyo kwa idhini ya mteja wake. Katika kesi yenu, mhasibu msaidizi alikuwa hana mamlaka ya kusaini hundi, bali kuchukua fedha. Hivyo basi benki haikufanya hivyo kwa maelekezo yenu na kupelekea hasara hii.

Mabenki hayakiri makosa kirahisi! Hatushangazwi wao kukataa kuwajibika. Kwa maelezo hayo ya benki, labda kama kuna jambo mnalificha kwetu, hayawezi kutumika kwenye utetezi mahakamani. Hatuoni uhusiano wa moja kwa moja kati ya kipengele cha kuamini mlichosema na hundi iliyoghushiwa, labda kama mmemtumia mhasibu msaidizi kutumia udhaifu katika utaratibu wa benki kuiba pesa.

Tunashauri upate mtaalamu wa sahihi ili kuangalia sahihi ambazo unadai zimeghushiwa. Mara tu utakapohakikisha kuwa hundi zimeghushiwa, wapelekee benki hati ya madai. Ikiwa hilo litashindikana unaweza kuishitaki benki na kudai kurejeshewa kiasi kilichotajwa. Kutokana na maelezo hapo juu, tunaamini una kesi nzuri dhidi ya benki. Kwa uzoefu wetu, baada ya kupata ripoti ya uchunguzi juu ya sahihi ambayo inathibitisha kuwa sahihi zilighushiwa, kwa kawaida benki hukubali kosa na kulipa.

## Kifungu cha Bei nzuri kwenye Mkataba

**Ingawa mimi si mwanasheria, huwa nafanya majadiliano ya mikataba kwa niaba ya mashirika ya Serikali na taasisi nyingine nchini Tanzania. Ningependa kujua kama katika mkataba ninaweza kuingiza kifungu ambapo muuzaji anathibitisha kwamba bei ambayo ameiandika ndiyo bei ya chini kabisa ambayo hajawahi kumpatia mteja wake yeyote nchini Tanzania. Kimsingi, ninataka kuwa na uwezo wa kuchukua hatua kwa malipo ya juu katika mikataba. Ni jinsi gani ninaweza kufanya hivyo na je, hili ni jambo la kawaida?**

*19 Julai 2010*

Ajira yako ni kujadili mikataba kwa niaba ya wahusika. Huoni kwamba, kama wauzaji wote watakubali kipengele hicho, itafanya ukose kazi? Katika uchumi wa soko huria, mambo mengi huchangia katika kuamua bei ya bidhaa au huduma, kubwa zaidi likiwa ni mahitaji na ugavi. Bei ya bidhaa fulani inaweza kupanda au kushuka kulingana na siku uliyonunua. Mambo mengine mengi huamua bei pia. Ingawa wazo ni zuri, hatudhani kama wauzaji watakubaliana na kifungu kama hicho.

Mojawapo ya kifungu tunachokifahamu ni kile kifungu kinachopendwa zaidi, ambacho kinampa mnunuzi kupata sifa za mteja mzuri zaidi. Kifungu kama hiki kwa kawaida kinasomeka hivi: 'muuzaji anatamka kuwa gharama, kiwango cha bei, ada, malipo mengine na punguzo la bei katika makubaliano hayamkandamizi mnunuzi kuliko masharti au upendeleo uliotolewa au kupewa mteja mwingine yeyote wakati makubaliano haya yanatiwa sahihi na muuzaji.' Kipindi chote cha makubaliano haya, ikiwa muuzaji atafanya makubaliano mengine juu ya bidhaa husika yenye gharama, bei, ada, malipo mengine na punguzo la bei ambayo ni nafuu kwa mteja mwingine, vipengele hivyo vitaongezwa mara moja kwa muuzaji.

## Kubadili Jina kwa lazima

**Msajili wa Makampuni alisajili jina la kampuni yangu miaka ishirini iliyopita. Cha kushangaza, Msajili amenitaarifu kuwa jina la kampuni yangu linachanganya. Sielewi ni kwa nini imemchukua Msajili miaka ishirini kugundua hili. Nimegundua kwamba jina la kampuni yangu linafanana na jina la benki moja huko Afrika Magharibi, ambayo imemtaka Msajili aniandikie. Baada ya kufanya utafiti kwenye mtandao, nimegundua kwamba benki hiyo imeanzishwa baada ya kampuni yangu kuwa imesajiliwa. Je, barua hii kutoka kwa Msajili ni ya haki/sahihi?**

*5 Julai 2010*

Sheria ya Makampuni iko wazi kwamba kama, kwa maoni ya Waziri, jina ambalo kampuni imesajiliwa linapotosha kulingana na asili ya shughuli zake na kuna uwezekano wa kusababisha madhara kwa umma, anaweza kuielekeza kubadili jina lake.

Unaweza kupinga maelekezo hayo kwa kupeleka maombi maalum mahakamani. Maombi hayo yanapaswa kufanyika ndani ya wiki tatu toka tarehe uliyopokea maelekezo. Maelekezo hayo lazima, kama si msingi wa maombi husika mahakamani, yazingatiwe ndani ya kipindi cha wiki sita tangu tarehe ya kutolewa maelekezo au kwa muda mrefu zaidi kama ambavyo Msajili atafikiri inafaa kuruhusu.

Inaonekana jina hilo lina thamani kubwa, itakuwa ni vyema zaidi ukiwasiliana na wakili wako.

## Uhusiano kati ya Mkandarasi na Mkandarasi Mdogo

**Nimepewa mkataba wa mabilioni ya fedha ya kitanzania kwa ajili ya mradi wa ujenzi huko Dodoma. Nitatakiwa kugawa sehemu kubwa ya kazi kwa mkandarasi mdogo (sub-contractor), lakini sina fedha ya kutosha kumlipa mkandarasi mdogo, na nitategemea fedha kutoka kwa mteja kukidhi mahitaji ya mkandarasi mdogo. Ni mambo gani ya muhimu ninapaswa kujua?**

*28 Juni 2010*

Mkataba kati yako na mkandarasi mdogo itabidi uwe na masharti sawa na mkataba kati yako na mteja wako. Muda wa kukamilisha mradi, wigo wa kazi, ubora wa malighafi, n.k.

Moja ya kifungu ambacho unapaswa ukiweke kwenye mkataba wako ni 'utalipwa nikilipwa'. Hiki ni kipengele ambacho kinamtaka mkandarasi mkuu kumlipa mkandarasi mdogo kwa kazi iliyofanyika kwa kutegemea kama mteja amemlipa mkandarasi mkuu kwa kazi iliyofanyika. Katika

kifungu kama hicho mkandarasi mdogo hujikuta katika hatari ya kutokulipwa kama mteja atashindwa kumlipa mkandarasi mkuu. Kama kampuni yako ya ujenzi ni ndogo, hatuna uhakika kama mkandarasi mdogo, hasa kama ni kampuni kubwa kuliko kampuni yako, atakubaliana na masharti kama hayo. Njia nyingine, mkandarasi mdogo atakuomba dhamana ya benki, ambayo ni gharama kubwa na vigumu kuipata kama huna mali yoyote ya kuweka rehani.

## Dhamana binafsi na Mkopo Benki

**Mimi ni mkurugenzi katika biashara ya familia lakini sina hisa. Malipo yangu pekee ni ada ya ukurugenzi kwa mwaka. Tumekuwa tukikopa sana kutoka kwenye baadhi ya benki kubwa sana nchini Tanzania. Kwa miaka mingi, mauzo yetu yamekuwa yanapungua na kupoteza soko, na kampuni kuwa na matatizo ya kifedha. Katika nyaraka nyingi za benki, nimekuwa nikisaini dhamana binafsi kama sehemu ya nyaraka za mkopo. Kuna madhara gani kwenye dhamana ya namna hiyo ikiwa benki itachukua hatua zozote? Kampuni yetu ni yenye dhima ya kikomo. Je, hilo linaleta tofauti yoyote?**

*21 Juni 2010*

Kwa maana rahisi, dhamana binafsi ni dhamana ambayo wewe, kama mdhamini, utabeba jukumu binafsi kulipa mkopo husika, ikiwa kampuni itakiuka masharti.

Kwa uzoefu wetu katika soko ni kwamba mikataba ya dhamana binafsi hutayarishwa kiupana sana ili kulinda maslahi ya benki. Unaposaini dhamana binafsi, ambayo ni ukurusa mmoja au mbili za 'nyaraka inayovutia' inakuondolea ulinzi wa mali na uwajibikaji binafsi dhidi ya madeni ya kampuni, ambao uwepo kwa kusajili kampuni yenye dhima ya kikomo.

Kimsingi, kama kampuni itashindwa kulipa deni na benki kuingilia, benki ikishindwa kurudisha pesa zake kutoka kwenye mali zilizowekwa rehani na kampuni, benki italazimika, kutokana na makubaliano ya dhamana binafsi, kuchukua mali zako binafsi.

Unahitaji kujipanga jinsi ya kusimamia mambo yako binafsi ikiwa jambo hilo litatokea. Unahitaji kuonana na mtaalamu mzuri wa sheria za makampuni.

## Kuchoma Moto bidhaa zilizotaifishwa

**Nimekuwa nchini hapa kwa miaka kumi sasa na mara zote nimeguswa na umaskini uliokithiri. Kwa miaka kadhaa iliyopita, nimebaini kwamba Mamlaka ya Jiji hairuhusu wafanyabiashara ndogo ndogo (machinga) kuuza chochote kando kando ya barabara. Tanzania ni kati ya nchi maskini zaidi duniani, na inanishangaza kwa nini Mamlaka ya Jiji inaweka masharti kama hayo. Hata jimbo la New York linaruhusu, kwa kiwango fulani, wafanyabiashara kuuza bidhaa zao kando kando ya barabara. Swali langu lina sehemu mbili. Kwanza, je, ni halali kwa mgambo wa jiji kumpiga mfanyabiashara ndogo ndogo? Pili, je, ni halali kwao kutaifisha na kuchoma moto mali za maskini hawa?**

*21 Juni 2010*

Ni lazima tueleze kuwa sheria ndogo za jiji haziruhusu aina hii ya biashara na ni kosa linaloweza kupelekea kukamatwa. Kujibu swali lako, mgambo wa jiji hawaruhusiwi kuwapiga wafanyabiashara na wanaweza tu kutumia nguvu ya kadiri kuwakamata. Na kama bidhaa hizi zinaweza kutaifishwa au la, jibu letu ni hapana.

Kwa mujibu wa sheria, mgambo wa jiji wanatakiwa kupeleka bidhaa hizo kwenye Mahakama ya Jiji ambayo kwa Dar es Salaam ipo Barabara ya Sokoine ili kupata maelekezo sahihi juu ya bidhaa hizo, na kuendelea kulingana na walivyoagizwa kufanya. Ni

lazima kufuata utaratibu huu, hawawezi tu kutaifisha na kuchoma vitu. Ingawa umeibua hoja muhimu, umaskini si sababu ya kuvunja sheria. Sheria ni ileile kwa matajiri na maskini.

## Watoa huduma za Mtandao wameniibia

**Miaka kumi na miwili iliyopita nilikuwa Tanzania na wenzangu watatu ambao nilisoma nao nchini Marekani na kuamua kuanzisha huduma ya mtandao. Wakati huo hatukuwa na fedha. Nilikuwa mtu muhimu katika masuala ya kiufundi kwenye usimamizi wa mradi na kutumia mwaka mzima kufanya kazi zote kama sehemu ya mchango wangu. Marafiki zangu wawili walibeba jukumu la kutafuta fedha na ofisi inayofaa. Kwa masikitiko hawakufanikiwa, na mradi ukafa. Kisha nikaondoka nchini kuelekea ng'ambo kufanya kazi, bado niko huko. Nimefahamishwa kuwa marafiki zangu hao wawili walifanikiwa kupata ufadhili baada ya mimi kuondoka, na leo hii ni moja kati ya watoa huduma za mtandao wakubwa kabisa nchini Tanzania. Je, nina madai yoyote juu ya kampuni hiyo? Je, ninaweza kupata zuio la mahakama?**

*14 Juni 2010*

Hili ni swali zuri sana. Katika swali lako hujasema kama kampuni hiyo mliisajili kwa pamoja na marafiki zako wawili au la. Kama ilikuwa hivyo, ungekuwa na unaendelea kuwa mwanahisa. Lakini, kama hivyo sivyo, tunadhani kwamba usingeweza kutuandikia!

Kuna mifano kadhaa ambayo tunaweza kutoa hapa. Mojawapo ni kwamba mlisajili kwa pamoja kampuni ambayo ilishindwa kuanza kazi. Baada ya kuondoka, inawezekana wale marafiki zako wawili walifanikiwa kupata mtaji, na kusajili kampuni mpya ukiwa haupo. Katika hili, kwa kuwa hukupewa fidia kutokana na muda wako mwingi uliotumia kutayarisha nyaraka muhimu za biashara, unayo sababu ya msingi kuchukua hatua dhidi ya kampuni hiyo.

Mazingira mengine ni ambapo kampuni hiyo hiyo ambayo mlisajili inaendelea kufanya kazi na bila uwepo wako, ilitoa hisa zingine kwa wanahisa watarajiwa, na kufuta hisa zako. Hilo pia linaweza kuangaliwa katika mtazamo wa sheria za kampuni, na linaweza kuwa na suluhu baada ya mwanasheria wako kufanya utafiti wa kampuni katika ofisi ya Msajili wa Makapuni.

Mazingira ya tatu ni pale ambapo huduma zao za sasa za mtandao ni tofauti kabisa zile za awali mlizojaribu kuianzisha. Kama ni hivyo, tunapendekeza kwamba ushauriane na wanasheria wako na kuangalia muda uliopita tangu kuanzishwa kwa kampuni tajwa. Kuna Sheria ya Ukomo wa Mashtaka ambayo inaweka kikomo cha muda wa kufungua kesi kwa baadhi ya mashauri.

## Mshirika wa zamani anatumia Nembo ya Ubia

**Mwaka 1998, mimi pamoja na rafiki zangu watatu tulianzisha ubia. Tulisajili jina la biashara, ambalo pia tulilisajili kama nembo yetu. Biashara yetu ilikua kwa kasi sana kwa miaka kadhaa. Kwa bahati mbaya, kulikuwa na kutokuelewana kati yetu, na mwaka 2003 mmoja wa wabia alijiondoa kwenye ubia. Mwaka 2005, mbia ambaye alijiondoa alianzisha biashara yake mwenyewe, ambayo inafanana na biashara ambayo tulikuwa tunafanya pamoja. Pia anatumia nembo ya utambulisho wa biashara ambayo tulisajili chini ya ubia. Tunapoteza wateja, na jina letu limechafuliwa, kwani bidhaa zake ni duni ukilinganisha na zetu. Je, ni jinsi gani tunaweza kumzuia asifanye biashara kwa kutumia jina hili lililosajiliwa? Tafadhali tushauri.**

*24 Mei 2010*

Kwa mujibu wa sheria, jina la biashara ambalo mlisajili kwa ajili ya ubia wenu - lilimilikiwa kwa pamoja na nyie wote

wanne. Kunapotokea mabadiliko ya idadi au utambulisho wa wabia, jina la biashara na nembo ya utambulisho wa biashara vitabakia kuwa chini ya ubia, bila kujali utambulisho wa wabia waliobakia. Mbia ambaye anajiondoa kwenye ubia hana haki tena kisheria kuendelea kutumia nembo ya biashara ya ubia kwa sababu si mali yake binafsi, bali mali ya ubia. Kitendo chake cha kutumia nembo husika ni ukiukwaji wa sheria. Mnaweza kufungua kesi dhidi ya mbia mwezenu wa zamani na kuomba zuio la kudumu la mahakama kutokana na yeye kutumia nembo ambayo inamilikiwa na ubia wa sasa.

Kutokana na swali lako, inaonekana kwamba mbia mwenzenu wa zamani pia alisajili kampuni yenye jina linalofanana (au jina hilo hilo) mnalotumia. Hii ni ajabu, kwa kuwa Msajili wa Majina ya Biashara kwa kawaida huwa haruhusu hilo. Pia, hii inaweza kuhojiwa, na tunawashauri kumwandikia Msajili wa Makampuni na kumuomba afanye marekebisho.

Hata hivyo, kesi yako ni dhaifu juu ya kumzuia mbia mwezenu wa zamani kufanya biashara sawa na yenu. Kwa kawaida mahakama huikataa hoja za namna hii, kwa kuwa huzuia biashara na ni kinyume na sera za nchi. Unatakiwa kumwona wakili wako kwa mwongozo zaidi.

## Nilisaini Mkataba kwa Kifaransa

**Mimi ni mkandarasi niliyejikita jijini Mwanza na nilisaini mkataba wa kufanya kazi fulani nchini Rwanda. Mkataba uliandaliwa katika lugha ya Kifaransa na nilisaini bila kuuelewa vizuri. Kumetoa matatizo fulani katika ujenzi na sijalipwa, kwa kuwa mteja anapinga baadhi ya ankara. Hivi karibuni nilipokea taarifa kutoka kwa wanasheria wa mteja wangu kuwa wanataka niwalipe fidia kwa mujibu wa mkataba. Sikumbuki chochote kuhusu kipengele cha kulipa fidia kwenye mkataba. Je, unanisaidiaje?**

*31 Mei 2010*

Kwanza, kamwe usisaini kitu chochote ambacho hukielewi. Pili, kutokana na swali lako, tumeelewa kuwa huwezi kuzungumza Kifaransa, na bado ulisaini mkataba kwa Kifaransa. Hili linatupa shida kidogo. Tatu, kwa kuanzia, hatuoni ni jinsi gani unaweza kukumbuka chochote, kwa kuwa ulisaini mkataba kwenye lugha ambayo huielewi.

Je, mkataba ni halali kwa kuzingatia kuwa ulisaini bila kujua maudhui ya kile ulichokuwa unasaini? Hii inaweza tu kujibiwa baada ya kuelewa historia nzima ya biashara husika. Je, kuna barua pepe zozote? Je, una hati halisi ya zabuni? Je, umewahi kumwandikia mteja? Kama utaratibu ulivyo, hupaswi kusaini chochote bila kufahamu maudhui yake. Kanuni ya pili ni kwamba hakuna kitu kama mkataba wenye masharti yasiyobadilika – siku zote hakikisha unasoma kila kitu kwenye mkataba. Kwa kuwa si kawaida kukataa uwepo wa baadhi ya vipengele katika mkataba kwa kudhania tu kwamba mkataba umeandikwa katika lugha tofauti, huenda kutakuwa na matumaini fulani baada ya wakili wako kuangalia historia ya biashara husika.

## Jina la Kampuni linapotosha

**Miaka michache iliyopita nilipokea barua kutoka kwa Msajili wa Makampuni, ambaye alipewa taarifa na Waziri kuwa jina la kampuni yangu linapotosha umma na ni lazima nilibadilishe. Sikufanya hivyo; kwa kuwa niliamini lilikuwa halipotoshi. Hivi karibuni nimepokea taarifa/notisi ikinijulisha kuwa hatua zitachukuliwa dhidi yangu kama sitabadilisha jina la kampuni yangu. Je, hii ni kinyume cha sheria? Nilidhani Tanzania inafuata misingi ya soko huria. Kama nikibadilisha jina la kampuni yangu, je bado nitapaswa kulipa kodi za zamani kwa TRA?**

*12 Aprili 2010*

Kweli Tanzania inajaribu kuiga kanuni za

soko huria, lakini hata katika uchumi kama huo kuna sheria, kanuni na taratibu za kufuata. Kuwa na soko huria haina maana kwamba sheria hazitumiki au kwamba unaweza kufanya vyovyote unavyotaka.

Waziri, kwa mujibu kwa Sheria ya Makampuni, anaweza kutoa amri ya kubadili jina kama jina lililosajiliwa linapotosha. Utaratibu ni ama kutii amri kutoka kwa Waziri na kubadilisha jina la kampuni, au kupeleka maombi mahakamani kupinga utaratibu huo. Uamuzi wa kukaa kimya unaweza kupelekea kupigwa faini au faini ya kukaidi.

Pia tambua kuwa mabadiliko ya jina la kampuni hayaathiri haki yoyote au majukumu ya kampuni, chini ya jina la zamani. Hivyo, wajibu wako kwa TRA uko pale pale. Vinginevyo kila mmoja angebadili jina la kampuni yake ili kukwepa madai/malimbikizo ya kodi ya zamani!

## Kuhamisha Majukumu katika Mikataba

**Nimeingia mkataba na mnunuzi wa magogo kutoka China. Nipo pia katika mazungumzo na kampuni fulani ambayo inataka/inaweza kununua mali zangu na hadhi yangu (good will). Nifanye nini kumbana mnunuzi wa magogo ikiwa biashara hii itafanyika. Napendelea zaidi kuuza biashara yangu yote na si sehemu tu. Je, kuna faida yoyote atakayopata kwa kununua hadhi na mali zangu na si jina la biashara?**

*12 Aprili 2010*

Unahitaji kuwa na uwezo kuhamishia majukumu yako katika mkataba kwa kampuni ambayo ina nia ya kuwanunua. Kifungu kinachohamisha majukumu kitahamishia mkataba kwa kampuni hii mpya. Unapoandaa mkataba, hakikisha kwamba majukumu yatahamishwa papo hapo, baada ya biashara yako kuuzwa, mkataba utahamishiwa kwa kampuni mpya moja kwa moja. Baadhi ya vifungu vinavyohamisha majukumu/mkataba huhitaji ridhaa ya mnunuzi, na hivyo kufanya iwe vigumu sana.

Kujibu sehemu ya pili ya swali lako, faida anayopata mnunuzi kufanya biashara kwa njia hii, mara nyingi ni kumlinda mnunuzi dhidi ya madeni yoyote ya kodi kutoka kampuni inayouzwa.

## Sipati Ushirikiano kutoka kwa Mmiliki mwenza

**Kama miezi kumi na mbili iliyopita nilinunua eneo la makazi ambalo lipo kwenye ghorofa ya tano ya jengo fulani hapa jijini Dar es Salaam. Jengo hili lina ghorofa kumi na kuna geti linalotumiwa na wote. Hivi karibuni tulipata mmiliki mwenza mpya ambaye ni mzee na anakera sana. Anakataa kuchangia gharama za kawaida kwa ajili ya usafi wa mazingira. Hivi karibuni kibaraza cha ghorofa lake (roshani) kilianza kupasuka na kila mtu alikubali kuchangia fedha kwa ajili ya kukarabati lakini yeye alikataa. Je, sheria inatulindaje dhidi yake? Anasema yeye ni mzee sana hivyo hawezi kufanya chochote!**

*19 Aprili 2010*

Hakuna sheria tofauti kwa ajili ya wazee tu. Sheria ni sheria - inatumika kwa wote, ikiwa ni pamoja na huyo mmiliki-mwenza.

Kwa mujibu wa Sheria ya Umiliki wa Pamoja/Ubia ya mwaka 2008, haki na wajibu wa wakazi wanaomiliki jengo kwa pamoja, kama nyie, ni kwamba mnapaswa kuchangia gharama za pamoja; pia hakuna mmiliki-mwenza anaruhusiwa kuingilia, hata kwenye eneo lake mwenyewe, kunapofanyika matengenezo yaliyokubaliwa na wamiliki wote, ikijumuisha na kazi yoyote ya dharura.

Huyu mmiliki-mwenza anavunja sheria, japo kimaadili mnatakiwa kuheshimu wazee, lakini mnazo haki zenu pia kisheria.

Unaweza kufungua shauri dhidi ya huyu mmiliki-mwenza na uwezekano wa kushinda, kwa mujibu wa maelezo yenu, ni mkubwa.

Mmiliki-mwenza anaweza kuwajibika kulipa faini isiyozidi pesa za kitanzania million 5 au kupewa kifungo kisichozidi miaka miwili.

## Siwezi kuwajibika kama Mkurugenzi

**Niliteuliwa kama mkurugenzi katika kampuni mwaka mmoja uliopita. Inavyoonekana, nilitakiwa kumiliki hisa kwenye kampuni kwa mujibu wa kanuni za kampuni. Nilitaarifiwa, lakini nilikuwa nimesafiri na niliporudi nilikuta nimeondolewa kama mkurugenzi wa kampuni. Je, kampuni inaweza kufanya jambo kama hilo?**

*29 Machi 2010*

Tuweke wazi kuwa, kampuni ina haki ya kufanya hicho ilichofanya. Sheria ya Makampuni iko wazi kabisa kwamba itakuwa ni jukumu la kila mkurugenzi ambaye kwa kanuni za kampuni anatakiwa kumiliki kiwango fulani cha hisa, na ambaye hana sifa hizo, apate sifa hizo ndani ya miezi miwili baada ya kuteuliwa, au muda mfupi zaidi kama ambavyo itaelekezwa na kanuni za kampuni. Inaongeza zaidi kuwa atapaswa kuachia ofisi ya mkurugenzi wa kampuni kama mkurugenzi huyo hawezi, ndani ya miezi miwili toka siku ya uteuzi, kupata sifa husika na mtu anayeondolewa ofisini chini ya kifungu hiki hataweza kuchaguliwa tena kuwa mkurugenzi wa kampuni mpaka apate sifa tajwa.

Kwa kifupi utapaswa kuanza upya mchakato wa kuteuliwa tena, na kwa sasa, tafadhali tambua wewe sio mkurugenzi tena na hupaswi kujifanya mkurugenzi.

## Kufariki kwa mmoja wa Wahusika kwenye Mkataba Tegemezi

**Mnamo Julai 2009, niliingia mkataba wa kununua kipande cha ardhi na jirani yangu huko Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam. Ilikubaliwa kuwa mkataba utaanza kufanya kazi baada ya kupata idhini na ridhaa ya kaka wa muuzaji aliyeko London ambaye alitarajiwa kuja Dar es Salaam mwishoni wa mwaka 2009. Kwa bahati mbaya, muuzaji alifariki mwezi Januari katika ajali ya barabarani na sasa kaka wa marehemu, ameamua kutokuidhinisha mauzo. Haki zangu ni zipi? Je, mkataba una nguvu kisheria kwani tulikuwa tumeshausaini?**

*22 Machi 2010*

Mkataba wowote ambao uhalali wake unategemea kutokea au kutotokea kwa tukio fulani ambalo ni muhimu kwenye mkataba, unaitwa 'mkataba tegemezi' (contingent contract). Mkataba wako ni mkataba tegemezi kwa kuwa unategemea kutokea kwa tukio fulani, ambalo ni idhini ya kaka wa muuzaji. Kwa upande wako, na kwa bahati mbaya kabla ya kibali kupatikana muuzaji alifariki. Katika sheria, kifo cha mmoja wa upande katika mkataba tegemezi kuna athari ya kuvunja mkataba kati ya pande zote.

Kama umelipa bei ya manunuzi (ujira) ya ardhi husika, kulingana na masharti ya mkataba, kuna uwezekano mkubwa kurejeshewa fedha yako. Tunakushauri kudai fedha yako kutoka kwenye mali ya marehemu au kwa warithi wake.

## Taratibu za kuitisha Kikao cha Bodi ya Kampuni

**Mimi ni mkurugenzi wa kampuni nchini Tanzania. Hivi karibuni, nimegundua kwamba sijaalikwa kwenye vikao kadhaa vya bodi kwa sababu ninaishi mkoani. Je, sheria inaruhusu hili? Wiki chache zilizopita nilipewa taarifa ya kikao cha bodi siku mbili kabla ya kikao. Je, kuna sheria ambayo inanilinda?**

*15 Machi 2010*

Ukweli kwamba unaishi mkoani na unaweza usiwe na uwezo wa kuhudhuria

vikao, haina maana kwamba usipewe taarifa. Sheria ya Makampuni inasema kwamba kikao chochote cha bodi kifanyike baada ya kutoa taarifa ndani ya siku zisizo pungua ishirini na moja kwa wakurugenzi. Kama kampuni imekiuka sheria hii, maamuzi au maazimio yoyote yanayopitishwa katika kikao kama hicho yanaweza kupingwa.

## Kupanga bei ya Soko

**Mimi ni mshauri katika sekta ya mawasiliano ya simu na nimegundua kuwa kampuni mbili kati ya kampuni kubwa za mawasiliano nchini, mara kwa mara ,hujadili bidhaa zao na kupanga bei na hivyo kuwaumiza watumiaji wa simu za mkononi. Tanzania bado ina gharama za juu duniani kwenye baadhi ya huduma za simu za mkononi. Je, hakuna sheria ambayo inaweza kuwazuia kufanya hivyo?**

*8 Machi 2010*

Sheria ya Ushindani hairuhusu jambo hili. Kifungu cha 9 cha Sheria kiko wazi kuwa hairuhusiwi kufanya au kutekeleza makubaliano hayo kama lengo lake, na athari zake au mwelekeo wa athari za makubaliano hayo ni kupanga bei miongoni wa washindani. Sheria inaeleza maana ya kupanga bei kati ya washindani kuwa ni kupanga, kuzuia au kudhibiti bei, ushuru, gharama za ziada au gharama nyingine kwa ajili ya, au masharti au taratibu ambazo, upande mmoja katika makubaliano unauza au unajipatia, unaomba kuuza au kupata, bidhaa au huduma, katika ushindani na upande mwingine kwenye makubaliano hayo.

Unaweza kuona wazi kwamba matendo ya kampuni hizo za simu ni kinyume cha sheria. Hata hivyo, changamoto ni kuthibitisha kwamba wanakula njama na kupanga bei. Kuwa na bei sawa sokoni haimaanishi kuwa wanakula njama. Unaweza, kutoa taarifa kwa Tume ya Ushindani ambao wanaweza kuchunguza.

## Mkataba wenye Kipengele cha Kununua

**Niliingia mkataba wa kununua mgahawa, ikiwa kuna siku mmiliki wa mgahawa huo ataamua kuuza. Tulikubaliana kuwa angeweza kunipa nafasi ya kwanza kuchukua/kununua biashara nzima kwa bei ambayo itaamuliwa kwa wakati huo. Mmiliki amenigeuka na kusema kuwa hayuko tayari kuniuzia biashara hiyo kwa kuwa anaye mnunuzi mwingine. Mwanasheria wangu anataka nilipeleke jambo hili mahakamani. Je, kuna hatua nyingine ambazo naweza kuchukua?**

*22 Februari 2010*

Aina hii ya kifungu katika mkataba wakati mwingine hujulikana kama ‘haki ya kukataa kwanza au haki ya kushtuliwa kwanza’, ambapo upande mmoja unakubali kutoa kwa upande mwingine nafasi ya kufanya nao biashara fulani kabla ya kushirikisha mtu mwingine.

Njia bora ni kuteua mpatanishi na kuona kama anaweza kuwafanya mtatue mgogoro wenu kwa amani. Bila hivyo, mnapaswa kufungua kesi. Lazima pia uombe amri ya mahakama kuzuia huyo mmiliki kuuza mgahawa kwa mtu mwingine wakati unasubiri uamuzi wa kesi ya msingi. Hii itazuia malumbano na mmiliki mpya.

Tulichokibaini, katika jambo hili, ni kama mkataba mlioingia ni halali kisheria au la. Mkataba lazima uwe na malipo/ujira ambao unafafanuliwa kama kitendo, kutokufanya au ahadi kutoka upande mmoja kwenye mkataba ambao huwa ni bei ambayo upande huo hununua ahadi ya mwingine. Mkataba bila ya ujira ni makubaliano yaliyo uchi (makubaliano tupu) ambayo huongozwa na msemo kuwa, haki ya kuchukua hatua haipatikani kwenye makubaliano yasiyo na malipo (mkono mtupu haulambwi). Kutoka kwenye swali lako, hatuna uhakika kama makubaliano hayo yana

ujira wowote. Je, ulilipa kiasi chochote kidogo au kinachofanana na hicho kulinda haki ya kushtuliwa kwanza? Kama sivyo, mkataba ni batili na hutaweza kuchukua hatua zozote. Baada ya kusoma mkataba wote, wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kuuziwa Bidhaa Mbovu

**Mimi ni mfanyabiashara wa tairi mjini Mbeya. Katikati ya mwezi Desemba 2008, niliagiza matairi mia mbili kutoka kwa msambazaji wangu jijini Dar es Salaam, ambaye aliomba kulipwa kwanza. Baada ya kumlipa, niliambiwa nichukue matairi kutoka kwenye kituo kimojawapo cha mabasi mjini Mbeya. Wiki mbili baadaye niligundua matairi arobaini, kati ya yote, yalikuwa mabovu. Nilimjuza msambazaji wangu ambaye amenionesha ankara ambayo kwa uwazi inaeleza kuwa mara tu bidhaa inapouzwa, haiwezi kubadilishwa au kurudishwa. Msambazaji anadai kwamba nilipaswa kuwa nimeyakagua matairi kabla ya kuyanunua. Ni zaidi ya miezi miwili sasa jambo hilo halijapatiwa ufumbuzi. Je, nifanyeje?**

*1 Februari 2010*

Sheria ya Mauzo ya Bidhaa kwa ujumla inampa mnunuzi wajibu wa kukagua ubora wa bidhaa ambazo anazinunua, hasa kama mnunuzi ana nafasi ya kufanya hivyo. Tumezingatia kwa uangalifu mazingira yanayozunguka suala lako na kugundua kwamba mambo yalivyokuwa, wakati wa kununua na kupokea, hukupewa muda wa kukagua bidhaa. Kanuni ya 'mnunuzi chukua tahadhari' yaani mnunuzi kuwa makini, haiwezi kutumika dhidi yako. Hata kama kanuni hii ingetumika hapa, msambazaji wako, kama muuzaji, asingeweza kufutiwa wajibu wa kusambaza bidhaa zenye ubora. Kwa kukuletea au kukuuzia matairi mabovu, msambazaji wako alifanya kitendo cha kuvunja waranti iliyotumika.

Utetezi wake kuwa 'mara tu bidhaa inapouzwa haiwezi kurudishwa' hauwezi kuzingatiwa kiujumla na kutumika hata katika hali ambayo bidhaa zinaonekana dhairi ni duni/chini ya kiwango cha ubora.

Inaonekana kama una kesi nzuri dhidi muuzaji wako, labda kama kuna maelezo ya ziada ambayo hukutueleza. Kwa kuwa mna mkataba, inamaanisha kwamba unaweza kuchukua hatua dhidi ya msambazaji ndani ya miaka sita toka siku ulipofahamu tatizo hili. Ikiwa kumfuatilia tu hakusaidii kupata pesa zako, unaweza kumshitaki msambazaji na si tu unaweza kuomba kurudishiwa malipo ya matairi mabovu bali pia kudai fidia.

## Kushindwa kulipa Mkopo Benki

**Niliingia katika makubaliano ya mkopo ambapo kampuni yangu ilikopa zaidi ya shilingi bilioni 2.5 kutoka benki mojawapo nchini Tanzania. Benki hiyo imekuwa ikinunua vifaa kutoka kwangu na haijanilipa kwa kiasi sawa na hicho. Benki imenipeleka mahakamani na mimi nimepeleka madai kinzani (counter claim) ya kiasi sawa na chao. Kesi imeanza kusikilizwa Mahakama ya Biashara. Je, nina nafasi gani ya kufanikiwa? Je, kitu gani kingine ninaweza kufanya ili kujikwamua na deni hili? Je, nini kitatokea kama nitashindwa kesi?**

*25 Januari 2010*

Tunashangaa kwamba benki husika imekuwa ikinunua pia 'vifaa' kutoka kwako. Wakati tulipokuwa tunajibu swali hili, tulikuwa tunatafakari juu ya benki gani nchini Tanzania ambayo inanunua vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 2.5! Na ikawa bahati kwamba unaidai benki hiyo kwa kiasi hicho hicho. Suala hili zima lina harufu ya ufisadi, lakini wajibu wetu ni kujibu swali lako, kama tunavyofanya hapa chini.

Unapaswa kufahamu kwamba kuna

biashara mbili tofauti katika swali lako. Kwanza ni mkataba wa mkopo ambapo umekopa fedha na hukurejesha. Kwa upande mwingine, inaonekana kuwa kuna mkataba wa usambazaji ambapo benki imekuwa ikinunua vifaa fulani kutoka kwako.

Unajaribu kulinda maslahi yako katika mkataba wa kuuziana vifaa kwa kutokulipa mkopo na umeibua madai kinzani.

Mara nyingi, kama si zote, makubaliano ya mkopo huwa na masharti yaliyo wazi kuwa kiasi cha mkopo kinalipwa bila makato, au madai kinzani. Hatujasoma mkataba wenu wa mkopo lakini kuna uwezekano mkubwa kuwa masharti haya yatakuwepo. Kama hivi ndivyo, basi madai yako kinzani yatashindwa. Unachokifanya ni kuchelewesha muda na kujiongezea kiasi utakachopaswa kulipa hapo baadaye. Kwa msisitizo, kama makubaliano yalifanyika kwa kutumia mkataba wa mkopo usiobadilika masharti, una nafasi ndogo sana ya kushinda.

Swali lako la pili juu ya nini unaweza kufanya ili kuepuka deni hilo ni swali ambalo tumechagua kutokulijibu. Kama ukikopa fedha kutoka benki, una wajibu wa kulipa labda kama kweli kampuni yako imefilisika na huna jinsi (hakuna namna ya kulipa).

Kama ukishindwa kesi, si tu kwamba benki itauza dhamana kurudisha fedha yake bali pia itachukua mali zako kufidia deni kwani inawezekana kabisa ulisaini dhamana binafsi. Mahakama ya Biashara Tanzania ni kati ya mahakama zenye kasi na ufanisi mkubwa nchini, hivyo kuchelewa kwako hakutodumu muda mrefu. Unaweza kujikuta kwenye matatizo/shimoni zaidi.

## Petroli kumwagika Kibaha

**Nilikodisha lori kusafirisha mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha. Njiani, kutokana na uendeshaji mbaya, baadhi ya mapipa (SimTanks) kwenye gari yalitoboka na nilipoteza zaidi ya lita 1000 za petroli. Je, ninawezaje kupata fidia kutoka kwa mmiliki wa gari?**

*18 Januari 2010*

Majibu yetu hayatokufurahisha kabisa. Chini ya sheria mpya iliyotungwa ya Petroli ya mwaka 2008, hauruhusiwi kusafirisha bidhaa ya petroli kwenye mapipa ya kawaida kama ulivyofanya. Wewe, mmiliki wa lori, dereva na mkurugenzi mwingine yeyote kwenye kampuni yako, mnaweza kufungwa na au kulipa faini ikiwa mtakutwa na hatia ya kosa hili. Sheria inataja magari yenye matenki maalum ambayo yanaweza kubeba bidhaa kama hizo.

Pia, jua kwamba kumwagika petroli, kwa mujibu wa sheria, inahesabika kama umwagikaji mkubwa. Na endapo taasisi ya Serikali au Serikali ya mtaa itaingia gharama au matumizi kwa sababu ya tukio hilo, gharama hizo zinapaswa kufidiwa na waliohusika kufanya kitendo hicho. Katika kesi hii, kuna uwezekano mkubwa kwamba wewe na mmiliki wa lori mnapaswa kulipa gharama za kusafisha mafuta yaliyovuja.

Kuhusu madai yako kwa mmiliki wa lori, tambua kwamba kwa kuwa kitendo cha kubeba mafuta ya petroli kilikuwa kinyume cha sheria, hakukuwa na mkataba, na kama hakuna mkataba, huwezi kudai fidia ya hasara yoyote.

## Bidhaa Halali sasa imekuwa Haramu

**Niliagiza mzigo wa vifaa vya plastiki vilivyokuwa halali kisheria wakati nilipoviagiza, lakini kutokana na kanuni mpya zilizotungwa, kwa sasa ni haramu kuviagiza bidhaa hizo. Masharti ya mkataba yalikuwa ni kuwa ninalipa 50% wakati wa kusaini mkataba, na iliyobaki wakati bidhaa zitakapowasili. Kwa mtazamo wa kanuni mpya, siwezi kuondoa mzigo bandarini, ninaangalia namna ya kuzirudisha bidhaa hizo nje ya nchi au kuzirudisha kwa**

**muuzaji. Muuzaji ananiwekea shinikizo kukamilisha malipo yaliyobaki na anatishia kuchukua dhamana niliyowekewa na benki ili kumalizia malipo. Je, kuna chochote ninaweza kufanya?**

*11 Januari 2010*

Mkataba wako 'hauwezi kutekelezeka'. Dhana ya mkataba kutokutekelezeka baada ya kutokea jambo ambalo halikutazamiwa na wahusika imefafanuliwa kwa njia mbalimbali - wakati mwingine ni kutoweka kwa kitu ambacho wahusika walifikiria ndio msingi wa mkataba wao, muda mwingine inaamuliwa kwa kuangalia ugumu wa kutekeleza masharti, na muda mwingine mahakama inaongezea mambo ambayo inadhani yalikusudiwa kuwa sehemu ya mkataba. Haijalishi, ni jinsi utakavyoiweka, matokeo ya kisheria ni yale yale. Ufafanuzi huu ni kwa mujibu wa kesi maaarufu ya Uingereza, *Joseph Steam Line dhidi ya Imperial Smelting Corporation.*

Iliamuliwa kuwa pale ambapo dhana ya mkataba kutokutekelezeka inapotumika, hakuna ukiukwaji wa mkataba. Kinachotokea ni kwamba masharti ya mkataba yanakosa nguvu tena tokea muda ambao hali iliyopelekea kutokutekelezeka kwa mkataba itokee.

Kwa urahisi, mkataba kutokutekelezeka ni kuvunjika kwa mkataba bila kutarajia kwa sababu ya tukio/mazingira ambayo hufanya utekelezeji wake kushindikana au kuwa kinyume cha sheria au kuzuia dhumuni lake kuu kufikiwa.

Labda kama kuna kifungu maalum katika mkataba kuhusu mazingara yanayoweka kufanya mkataba kutokutekelezeka, mkataba usiotekelezeka hufikia kikomo mara moja.

Katika kesi yako, kwa kuchukulia kuwa ulichotueleza ni kweli, kuna uwezekano mkubwa kuwa mkataba wako hautekelezeki na hupaswi kulipa kiasi kilichobaki. Pia, kwa mujibu wa masharti ya malipo kwenye mkataba, utawajibika kulipa ikiwa bidhaa ilipokelewa. Hujatufafanulia unamaanisha nini unaposema kupokelewa, tunachukulia kuwa unamaanisha bidhaa kufika kwenye ghala lako. Hilo pia halikutokea.

Kuhusu dhamana ya benki, wanasheria wako wanapaswa kuangalia maandishi ya makubaliano ya dhamana ili wakuongoze zaidi. Dhana ya mkataba kutokutekelezeka inaweza isitumike huko.

## Kifungu cha Marekebisho ya Bei

**Nimeingia katika mkataba wa usambazaji wa vifaa kwa kiwango fulani cha bei. Hata hivyo, nilipotuma ankara kwa mnunuzi, alipunguza kiasi akidai kwamba bei yake sokoni imeshuka. Aliniomba nirejee kifungu cha marekebisho ya bei mwishoni mwa mkataba ambacho kinasomeka kuwa bei yangu itakuwa 12.5% zaidi ya bei ya soko wakati wa kuwasilisha bidhaa au Dola za Kimarekani 1,000, au yoyote itakayokuwa chini kati ya hizo. Hesabu zangu zote zilijikita kwenye Dola 1,000 na hicho ndicho kiwango nilichoandika kwenye ankara. Mikataba haipaswi kuwa na utata. Je, hiki si kifungu haramu? Nimedanganywa, nahitaji msaada wenu.**

*4 Januari 2010*

Kutokana na maelezo yako, haujadanganywa. Inaonekana kama kutokana na furaha ya kusaini mkataba huu hukusoma maudhui yake vizuri. Haijalishi kuwa kifungu hicho kipo mwishoni mwa mkataba.

Kifungu cha marekebisho ya bei ni cha kawaida katika mikataba, hasa kwenye bidhaa ambayo bei yake inategemea mahitaji na ugavi kimataifa ambako bei ya soko inapatikana kwenye masoko ya kimataifa.

Unapaswa kuwaona wanasheria wako na kuwapa ukweli wote labda wanaweza kugundua kitu fulani ambacho kinaweza kusaidia. Kama suala hili litaangaliwa

kama lilivyo, hatuoni ni jinsi gani unaweza kufanikiwa.

## Uhamishaji Haramu wa Fedha

**Moja ya washindani wangu anafahamika kwa kuhamishia fedha yake katika akaunti ya benki ng'ambo, kutoka kwenye vyanzo haramu vya mapato hapa nchini Kongo. Je, kuhamisha huko kunaruhusiwa? Je, hakuna udhibiti wowote juu ya fedha haramu kama hizo? Nini kitatokea ikiwa kampuni yenye ukomo katika uwajibikaji wa wamiliki wake inajihusisha katika tabia hiyo? Je, wakurugenzi watawajibika vipi?**

*11 Januari 2010*

Suala hili lipo chini ya Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha, ambayo ilianza kutumika kuanzia Januari 2007. Sheria hii imefafanua utakatishaji fedha kuwa ni kitendo cha mtu au watu kujihusisha, moja kwa moja au kwa njia nyingine katika kubadili, kuhamisha, kuficha, kutumia au kujipatia, fedha au mali inayojulikana kuwa imepatikana kinyume cha sheria na kwamba tendo hilo lina lengo la kukwepa mkono wa sheria.

Kifungu cha 12 cha Sheria kinasomeka kuwa, mtu ambaye anajihusisha moja kwa moja au vinginevyo, katika biashara ambayo inahusisha mali inayotokana na makosa sababishi (predicate offences) wakati akijua au alipaswa kujua au alipaswa kuwa anajua kwamba mali hiyo inatokana na kufanya kosa sababishi atakuwa ametenda kosa la utakatishaji fedha.

Sheria inatafsiri pana sana ya makosa shirikishi ambayo inagusa pia suala ambalo umeongelea kwenye swali lako.

Sheria inasema zaidi kwamba mtu yeyote aliyeshiriki katika kutakatisha fedha atatozwa faini ya kiwango cha chini cha shilingi milioni 100 na cha juu ni shilingi milioni 500 au kwenda jela miaka isiyozidi kumi. Adhabu ya kifedha ni kali sana ikiwa kosa limetendwa na kampuni au taasisi/asasi kubwa ambapo faini ya kiwango cha chini ni shilingi milioni 500 na cha juu ni shilingi bilioni 1.

Sheria inaeleza wazi kabisa kuwa kama kosa limefanywa na kampuni, mkurugenzi, meneja, mwendeshaji, mshirika/mbia au mtu yeyote anayehusika katika usimamizi na uendeshaji wa kampuni, wote hawa wanawajibika binafsi.

## Madai ya Wasambazaji bidhaa kuhusiana na Bima

**Mimi ni msambazaji wa bidhaa za chuma kutoka Ulaya Mashariki na India na nafanyia shughuli zangu Dubai. Niliingia makubaliano ya kuuza bidhaa na kampuni ya Tanzania na nililipa bima yote kwa niaba ya mteja kwa asilimia 105%. Baada ya kulipwa, nilihamisha haki zilizoko katika bima kwenda kwenye jina la mnunuzi. Bidhaa zilipata hasara kwa ujumla na mnunuzi alifanikiwa kulipwa kiasi chote nilichokuwa nimekatia bima. Nia yangu ni kufungua shauri la madai kwa mnunuzi kudai sehemu ya asilimia ya ziada niliyokatia bima yaani 5%. Natakiwa kufungua kesi Tanzania au Dubai?**

*28 Desemba 2009*

Ingawa si sehemu ya ombi lako, lakini tunapaswa kujadili kwanza msingi wa kesi hii kabla ya jambo lako husika.

Suala la bima ya ziada, dhidi ya mtoa bima, lishaamuliwa kwa muda mrefu kuwa mnunuzi anapata faida kamili iliyopo kwenye bima, hata kama soko limeanguka tangu tarehe ya mkataba. Muuzaji, baada ya kuhamisha kabisa maslahi yake chini ya sera ya bima, hatakuwa na nafasi ya kudai kuwa mnunuzi arejeshe kiasi kinachoonyesha kushuka/kuanguka kwa soko. Tuchukulie sasa kwamba muuzaji amekatia bima bidhaa ya zaidi ya kile kinachohitajika chini ya mkataba wa usafirishaji. Kwenye kesi ya *Strass dhidi ya Spillers na Bakers Ltd,* muuzaji alikatia bima bidhaa kwa thamani ya

juu kuliko ilivyohitajika chini ya mkataba wa usafirishaji. Iliamuliwa na mahakama kwamba muuzaji hakuwa na haja ya kuwajibika kwa mnunuzi kwa kiasi cha ziada kilichopokelewa kutokana na malipo. Ilionekana na mahakama kuwa kitendo hicho kiliruhusu wauzaji kujilinda wenyewe dhidi ya ongezeka la soko lisilotarajiwa. Aidha, ilieleweka katika sekta ya bima kwamba vitendo hivi vilikuwa ni vya ziada kwenye biashara ya nafaka na kwamba sera hiyo ilikuwa imara na yenye ufanisi. Hata hivyo, imeshawahi amuliwa kwenye kesi nyingine kuwa kama muuzaji amechukua bima zaidi ya thamani ya mkataba na akampa bima mnunuzi kwa kubadilishana nyaraka, mnunuzi hana jukumu la kuwajibika kwa muuzaji kwa kiasi cha ziada cha fedha iliyopokelewa kutoka kwenye bima.

Kesi yako inawiana kwa ukaribu na maoni ya mwisho - haujaelezea nani aliyelipa kwa malipo ya ziada. Ikiwa ni mnunuzi, hakika hautakuwa na na nguvu ya kisheria ya kufungua kesi. Hata hivyo, ikiwa malipo ya ziada yalilipwa na wewe mwenyewe, unahitaji kupata mwanasheria ili aweze kupitia maelezo kwa kina. Hata hivyo, sisi tunaona nafasi ndogo ya mafanikio kama bima imehamishiwa kwa mnunuzi.

Kuhusu sehemu muafaka ya kufungua shauri/kesi, mwanasheria wako anaweza kukuongoza baada ya kupitia maelezo ya kesi kwa kina.

## Ukosefu wa Usawa kwenye Majadiliano

**Mimi ni mmiliki wa kampuni ndogo ya uwakala ambayo huandaa muziki nchini Tanzania. Ninafanya kazi na makampuni mengi na hivi karibuni kampuni kubwa sana ya kuzalisha pombe ilinipatia kazi. Kampuni hiyo ina mkataba usiobadilika masharti kwa wasambazaji wake wote hivyo nilisaini bila majadiliano. Nimeshakamilisha jukumu langu na kwa sababu ya tatizo dogo sana la kiufundi katika huo mkataba, malipo yangu yamesitishwa. Kila wakati nikiulizia, wananiambia kuwa nimevunja mkataba. Hata hivyo, muziki ambao nilioandaa unatumiwa na kampuni husika na unapendwa na kila mtu anayeusikia. Wanasheria wangu wananiambia kuwa nimefungwa kabisa na mkataba na kwamba ni vigumu sana kupata kiasi cha fedha kilichobakia. Ninahisi kwamba kampuni hii kubwa inanifanyia vitendo ambavyo sio sahihi. Nifanye nini?**

*14 Desemba 2009*

Kwa kifupi, kutoka kwenye swali lako refu uliloandika (hadi ikatupasa kulipunguza ili kupata nafasi ya kuliweka kwenye safu hii), unafanyiwa vitendo visivyo sahihi na mzalishaji bia. Umeeleza kwamba umesaini mkataba ambao masharti yake kwa jinsi ulivyoandaliwa hukuwa na uwezo wa kuyabadilisha, lakini ukweli unabakia kuwa kwa muonekano wake na kwa maoni ya mwanasheria wako, ulisaini na hivyo kukubaliana na masharti ya mkataba.

Kwenye sheria ya mkataba ya zamani, nguvu ya mazungumzo baina ya pande mbili katika mkataba sio suala la uchunguzi wa mahakama. Mahakama inaingilia pale tu itakapodhihirika kuna mchezo mchafu unatendeka, na mahakama haina shughuli kubwa zaidi ya hapo kwa kuwa sio jukumu lake kuhakikisha kwamba majadiliano yanakuwa sawa, au kuona kwamba upande mmoja haupati faida isiyofaa dhidi ya mwingine au kuweka masharti yasiyofaa kwa sababu ya uwezo wake mkubwa katika majadiliano.

Hata hivyo, mtazamo wa kisasa katika Sheria ya Mkataba, ni tofauti kabisa. Ingawa mafundisho ya usawa wa nguvu za majadiliano haitambuliki kihivyo, mahusiano ya nguvu za majadiliano ya pande mbili katika mkataba mara nyingi huzingatiwa, hasa ambapo suala linalohusu uhalali wa vifungu vya msamaha katika mikataba ambayo upande mmoja hauna nafasi ya kubadilisha masharti yake.

Unaweza kujaribu kuangalia tatizo kutoka pembe kama ilivyoshauriwa na mtazamo wa kisasa wa sheria ya mkataba, ukizingatia mkataba uliosaini. Kwa siku zijazo usisaini mkataba bila kuupitia kwa umakini.

## Dhamana kwenye Bidhaa zilizouzwa

**Mimi ni kampuni kutoka Uganda inayoanza shughuli zake nchini Tanzania. Nimegundua kwamba mara nyingi wakati bidhaa zinafikishwa, mnunuzi halipi malipo ya bidhaa kwa wakati. Je, kuna njia yeyote ambayo ninaweza kuitumia kujilinda kwa kuweza angalau kuzichukua bidhaa ikiwa sijalipwa?**

*16 Novemba 2009*

Mbali na tahadhari za kawaida ambazo unapaswa kuzichukua kwa kuhakikisha kuna mkataba umesainiwa, unaweza kuingiza kifungu cha "muendelezo wa umiliki wa bidhaa".

Chini ya kifungu cha muendelezo wa umiliki wa bidhaa, muuzaji wa bidhaa anataka muendelezo wa umiliki wa bidhaa, hata baada ya bidhaa kufikishwa kwa mnunuzi, hadi atakapopokea malipo kamili.

Kutoka kwenye mtazamo wa wauzaji, ni muhimu sana kubakiza umiliki wa bidhaa hasa pale mnunuzi anapokuwa amefilisika au ameingia katika utaratibu wa kufilisika kabla ya kulipa. Uwekaji wa kifungu cha muendelezo wa umiliki wa bidhaa unapaswa kufanywa kwa uangalifu kwa bidhaa zitakazokuwa katika miliki ya mnunuzi ambaye anaweza kuzihifadhi mahali ambapo hapajulikani na wewe, au mnunuzi anaweza kuchanganya bidhaa na bidhaa zingine zinazofanana na zake.

Vipengele vingine muhimu vya kuzingatia wakati wa kuandaa kifungu hiki ni pamoja na kuweka wazi kile mnunuzi anachoweza na asichoweza kufanya kwenye hizo bidhaa na kama bidhaa zinaweza kuuzwa na mnunuzi hadi malipo ya mwisho.

## Barua ya Faraja toka Kampuni Hodhi

**Kampuni yangu inajishughulisha na sekta ya madini. Tuko katika hatua za mwisho za kununua mashine kutoka kwa mtengenezaji ambaye kampuni hodhi yake ipo Mashariki ya Mbali. Muuzaji hajulikani kwetu na tumeomba dhamana ya utendaji kutoka kampuni hodhi. Kampuni hodhi imetutumia barua ya faraja (letter of comfort) ya ukurasa mmoja - tunaweza kuendelea na biashara?**

*23 November 2009*

Hiyo barua sio dhamana labda kama inalenga kuwafunga kisheria. Barua ya faraja - kwa mfano, ni barua ya kuthibitisha kuwa ni sera ya mtoaji ili kuhakikisha kuwa matawi yake yanaweza kwa wakati wote kutimiza wajibu wao - inaweza kutengenezwa ili kuonesha dhana ya uwajibikaji lakini mara nyingi hutengenezwa ili kukupa imani tu na si zaidi ya hapo. Hii hutokea hasa pale upande unaotoa hiyo barua umekataa kutoa dhamana. Kuna dhana kwamba ahadi iliyotolewa katika mazingira ya kibiashara inalenga kubana kisheria lakini hii inapingwa na ushahidi unaoonesha kuwa hii haikuwa nia ya kila upande/wahusika, na ni jukumu la mahakama kuhakikisha uwepo wa hiyo nia.

Ni vigumu kukupa mwongozo bila kusoma kilichoandikwa kwenye barua ya faraja, lakini kuna uwezekano mkubwa kuwa hii sio dhamana na ikiwa sharti lako la awali la kuingia katika biashara hii ni dhamana, hupaswi kuendelea.

## Muda ni wa Kuzingatiwa katika Mikataba

**Ninaingia mkataba wa kurekebisha programu ya kompyuta kwenye benki iliyopo Dar. Mkataba ambao ninaingia umetilia mkazo sana na unataja mara kadhaa kwamba "muda ni wa kuzingatiwa" kwenye makubaliano. Je! Kuna kitu ambacho benki inajaribu kunitega kwa kutaja muda mara**

**kwa mara? Unashauri nifanye nini?**

*16 Novemba 2009*

Ushauri wa kwanza ni wewe kuhakikisha unasoma mkataba kwa umakini. Huyu si mteja wa kawaida - hii ni benki unayojihusisha nayo na programu na vifaa vingine katika mabenki ndivyo vinavyoifanya benki kufanya shughuli zake siku hizi. Pia kuna kanuni za Benki Kuu ya Tanzania inayotoa muongozo wa aina ya mikataba ambayo mabenki yanaweza kuingia.

Uvunjaji wa kipengele cha "kuzingatia muda" kinawapa upande mwingine haki ya kuvunja mkataba. Ikiwa yote, au masharti fulani ya makubaliano yanapaswa kuwa chini ya masharti ya kuzingatia muda itategemea na nafasi ya majadiliano ya kila upande. Mara nyingi, kama ilivyo katika mkataba huu, kifungu cha jumla huwekwa kikisisitiza kuzingatia muda kuhusiana na masharti yote ya mkataba; katika mazingira hayo unapaswa kuyaangalia masharti haya kwa umakini ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa kila jambo kwa kuzingatia muda uliopangwa unawezekana.

Hupaswi kuwa na mihemko ya furaha na kuamua tu kusaini mkataba. Lazima uwe na uhakika katika kile unachoweza na usichoweza kufanya, ndani ya muda uliotolewa. Pia unatakiwa uangalie madhara ya kushindwa kutimiza jukumu kulingana na muda uliotajwa katika kila suala na ikiwa na tarehe zote na kama muda na tarehe za kutimiza hilo jukumu zimetajwa.

Benki haikutegi - benki ina imani kwa kile kinachotarajiwa kufanywa na wewe. Kama unataka kutimiza matarajio yao, maadam yanawezekana, unaweza kuendelea kusaini mkataba. Kama hauwezi, hupaswi kusaini mkataba huu - utakutana na matatizo baadaye.

## Haki katika Ubia

**Mnamo Oktoba 2007, niliingia katika ubia wa mdomo na rafiki ili kuanza biashara ya kununua na kuuza mazao mbalimbali. Tulikubaliana kuwa sitahusika na lolote na rafiki yangu ndiye alipaswa kutunza vitabu vyote vya mahesabu ya biashara hii. Tangu biashara imeanza rafiki yangu hataki kunionesha vitabu vya kutunzia mahesabu. Hapingi ubia uliopo ila daima huchelewa au hughairi kunipa taarifa yoyote. Kuna kitu ambacho sio sahihi kinaendelea. Nifanye nini?**

*9 Novemba 2009*

Kama tusemavyo mara nyingi, mikataba ya mdomo inatambuliwa kisheria lakini ni vigumu kuithibitisha. Pia huleta utata mwingi. Inashauriwa daima kuwa, mikataba inapaswa kuandikwa na kusainiwa na pande zote husika. Kesi yako ni mfano wa kesi za kumuamini mtu na fedha sababu tu ni rafiki yako, jamaa au mpenzi.

Kwa bahati mbaya, sheria inatambua kila mtu tofauti na mtu mwingine na kwa hiyo kwa shughuli yoyote unayofanya, lazima uhakikishe kwamba kila kitu kinaandikwa na mashaka yeyote yanashughulikiwa mwanzoni na si pale wahusika kwenye mkataba wana mgogoro.

Una bahati kwamba rafiki yako hapingi uwepo wa huo ubia, ingawa umeshindwa kutuambia jinsi gani amekubaliana na jambo hili. Kama ni kwa mdomo, basi utakuwa na wajibu ya kuthibitisha kwamba upo huo ubia, ikiwa atakataa baadaye.

Nia yako kwa sasa ni kujua biashara inaendeleaje. Kama mbia, una haki ya kupata taarifa za fedha ya kampuni yako. Tuchukulie kuwa umejaribu njia nyingine zote za kumshawishi mbia mwenzako kukupatia nyaraka, tunakushauri kafungue mashtaka kwenye mahakama yenye mamlaka ili kupata amri ya kumtaka mbia mwenzako aonyeshe nyaraka ili uzikague na kujiridhisha na usahihi wake.

## Utekelezwaji wa Mkataba binafsi

**Sisi wawili tuliingia kwenye mkataba binafsi wa kufanya shughuli fulani. Mkataba ulifanyika kwa maandishi ukiwa na kanuni na masharti yote. Upande mwingine kwenye mkataba umeshindwa kutimiza ahadi zake na nimeshalipa malipo ya awali kulingana na mkataba. Nilienda kwa mwanasheria akaniambia kuwa itakuwa vigumu kusimimamia utelekezaji wake. Naweza kuteua mkusanya madeni?**

*23 Novemba 2009*

Kutokana na swali lako, inaonekana kuna taarifa fulani unazoficha. Hatuna uhakika unamaanisha nini hasa unaposema mkataba binafsi? Inavyoonekana ni kama mkataba huo ni haramu.

Mkataba haramu ni mkataba ambao uundwaji wake, lengo lake, au utendaji wake upo katika uovu, kinyume na sheria ya nchi, au kinyume na sera za nchi, hakuna mahakama itakayousimamia au kuutekeleza. Kwa ufupi, 'hakuna mkataba.' Katika hali ambapo watenda maovu wawili wanaingia mkataba usio halali na mmoja wapo kunufaika dhidi ya mwingine, sheria haiwezi ingilia kurekebisha hali hiyo.

Ikiwa mkataba wako ni kinyume cha sheria huwezi kuutekeleza. Mifano ya mikataba haramu ni pamoja na usambazaji wa madawa yaliyozuiwa, kununua na kushiriki katika ukahaba, upelekaji wa fedha nje ya nchi kinyume na sheria na kadhalika. Mkataba pia unaweza kuamuliwa ni batili ikiwa uko kinyume na sera ya nchi. Mkusanya madeni hawezi kutekeleza mkataba haramu.

## Makosa ya Mkandarasi, Muendelezaji ameshtakiwa

**Mimi ni muendelezaji wa eneo kubwa la ardhi lililopo Dar. Hivi karibuni winchi (mashine) iliyokuwa inatumika kufanya kazi kwenye eneo langu ilisababisha uharibifu kwenye kiwanja cha jirani. Sasa nimepelekwa mahakamani kama muendelezaji. Ninawezaje kuingizwa kwenye tatizo kwa makosa ya mkandarasi? Pia nina cheti cha motisha kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na niliambiwa kuwa ninalindwa kikamilifu. Inawezekanaje mwekezaji mkubwa anakatishwa tamaa kiasi hiki?**

*30 Novemba 2009*

Umeibua hoja zenye msingi sana hapa. Kabla ya kujibu maswali yako ya iwapo unawajibika kwa matendo ya mkandarasi wako au la, tungependa kujibu maswali yako mengine na kauli zako.

Kwa kuanzia, kwa sababu tu una hati ya motisha ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) haimaanishi kwamba huwezi kushtakiwa. Haijalishi una cheti cha TIC au la, bado unatakiwa kufuata utawala wa sheria nchini Tanzania, kama vile ungekuwa mahali pengine popote duniani. Cheti hiki kinalinda uwekezaji wako na si matendo yako.

Hatuna uhakika kuhusu kukatishwa tamaa; umeshtakiwa katika mahakama ni lazima ujitetee. Ni sehemu ya ulimwengu wa biashara. Bila kuficha maneno, cheti cha TIC hupunguza vikwazo vingi lakini hakitaweza, na hakiwezi, kukupa ulinzi kutokana na matukio kama hilo ulilotaja. Unachoweza kufanya ni kuwajulisha TIC kuhusu hili kwa madhumuni ya kuweka kumbukumbu ikiwa kama kuna mtu kwa makusudi anajaribu kuharibu malengo yako kwenye mradi huo.

Je, unawajibika kwa vitendo vya mkandarasi wako? Kuna kesi maarufu sana ya Kiingereza - *Rylands dhidi ya Fletcher* ambayo iliamuliwa kwamba uwajibikaji kwenye kesi za namna hiyo ni mkali na sio utetezi kusema kuwa tukio limetokea pasipo ruhusa yako, au kushindwa kutekeleza wajibu wako au kupuuza au hata kwamba ulikuwa hujui kuwepo kwa tukio husika. Ufafanuzi

wake ni kuwa, unaweza kuwajibishwa lakini pia una mkataba na mkandarasi ambaye anaweza kukufidia kutokana na madhara aliyosababisha. Mkandarasi anapaswa kuwa na bima ya madhara yote ambayo inapaswa kujumuisha uharibifu uliofanywa na winchi (mashine). Kama huna bima ya namna hii, utaishia kulipa gharama za uharibifu uliofanywa.

## Ulinzi wa Taarifa za Siri

**Kampuni yangu inafanya mazungumzo na kampuni kutoka Kenya kuhusu kuinunua. Ninatoa taarifa fulani kwao ambazo wanaweza kuzitumia kwa faida, baadaye. Ninawezaje kujilinda kwa 100% dhidi ya upande huu, ambao unaweza kuishia kushindana dhidi yangu, ikiwa makubaliano hayatafikiwa?**

*9 Novemba 2009*

Hili ni swali zuri sana. Tunashauri kwamba uhakikishe upande unaopokea wanasaini mkataba wa kutotoa siri ambao utatoa ulinzi mzuri.

Usiri au mkataba wa kutotoa siri ni muhimu kwa upande wowote ambao utahitaji kulinda taarifa za siri. Jinsi umuhimu wa taarifa za siri unavyongezeka, ndivyo pia ugumu kwenye makubaliano unavyokuwa.

Kwenye mkataba wako, kutotoa siri ni muhimu kuwa na ufafanuzi wa neno 'taarifa za siri', ambayo ni moja ya sehemu muhimu zaidi katika makubaliano hayo. Kiuhalisia, mkataba unapaswa kuweka wazi, kadiri iwezekanavyo, wigo wa taarifa zitakazozingatiwa kwenye makubaliano labda kama, taarifa hiyo ya siri inategemewa kufichuliwa kwenye mkataba wa kutotoa siri wenyewe. Japokuwa mkataba utatoa ulinzi mzuri, ni vigumu sana kuhakikisha utakuwa kwa asilimia mia moja.

## Udanganyifu kwenye Benki

**Kiasi ambacho kampuni yangu ilidhamiria kuilipa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) kilitolewa kutoka kwenye akaunti yangu lakini hakijalipwa TRA. TRA sasa wananidai mimi na benki inadai kwamba nilipaswa kuangalia taarifa za akaunti yangu ya benki. Ni dhahiri kabisa kwamba udanganyifu ulifanyika kwenye benki. Benki haitaki kukubali kuwajibika kwa lolote. Nifanye nini?**

*2 Novemba 2009*

Kwa ujumla, mteja ana wajibu wa kuchukua tahadhari sahihi na za msingi kudhibiti udanganyifu. Uamuzi mmoja kwenye mahakama ulisema (tunanukuu) 'Kimsingi, mahusiano kati ya benki na mteja ni yale ya mkopaji na mkopeshwaji. Na uandaaji na ulipaji wa hundi dhidi ya fedha ya mteja iliyopo kwenye mikono ya benki ni ule wa wakala na mhusika mkuu.

Benki pia ina jukumu la kimaadili kwako kama mteja wake na imeamuliwa katika kesi mbalimbali kwamba kwa kuwa wakala ananufaika basi yampasa kutekeleza kwa ujuzi na weledi maelezo ya mkuu wake.

Inaonekana kwamba kiasi fulani kilichotakiwa kipelekwe TRA kilitolewa kwenye akaunti yako na kupelekwa kwa mtu mwingine tofauti. Kuna njama kati ya mtu mwingine na maafisa wa benki. Kama hilo linaweza kuthibitishwa, una kesi nzuri sana dhidi ya benki. Kitendo cha kutogundua tatizo kupitia taarifa za benki hakuiondoi benki kwenye uwajibikaji. Ikiwa benki haitaki kutoa ushirikiano na kurudisha pesa katika akaunti yako au kupeleka fedha TRA, unapaswa kufikiria kuipeleka benki mahakamani. Kutokana na maelezo, labda kama kuna maelezo umetuficha, una kesi nzuri sana.

## Ghala limekatiwa Bima mara mbili

**Kaka yangu alikatia bima ghala letu na bila dhamira mbaya, nami nikafanya hivyo pia. Hivi karibuni, kulitokea moto na ghala lote**

**likateketea kabisa. Tulidai malipo dhidi ya moja ya makampuni, ambayo kwa namna fulani waligundua kuwa tuna bima mbili. Kampuni ya bima inajaribu kupata 50% ya kiasi cha madai kutoka kwa kampuni nyingine ya bima. Tumekwama katikati. Je, hii ni haki?**

*26 Oktoba 2009*

Watoa bima na sisi, kama wanasheria, tunaona jambo hili linaleta mashaka sana. Mna bima mbili na neno 'bila dhamira mbaya' ni muhimu sana kwako kufanikiwa. Iwapo makampuni haya mawili ya bima yakijua kuwa 'ulificha kutoa taarifa za msingi', madai yako hayawezi kulipwa. Unaonekana una matumaini sana kwamba kiasi hicho kitalipwa tu, ukisubiria nusu ya mchango kutoka kampuni nyingine kwa kiasi kinachodaiwa - hatuna uhakika hayo matumaini yako yanatoka wapi. Makampuni ya bima pia yataangalia miaka iliyopita ili kuona kama umekuwa unakatia bima mbili kwa miaka yote au ni mwaka huu tu, mliopata hasara. Tunajua kwamba makampuni ya bima duniani kote yanachukiwa, lakini lazima ujue kwamba kuna udanganyifu mwingi kwenye bima nchini Tanzania. Kama ilivyo kwa taasisi nyingine yoyote ya biashara, makampuni ya bima pia yanapaswa kulinda maslahi yao.

Kwa kawaida bima nyingi huweka kifungu cha uwiano sawa. Lengo kuu la hiki kifungu ni kuzuia mtu, ambaye ana bima mbili, kudai hasara nzima kwenye bima zote mbili. Kifungu hiki huifanya bima kuwajibika kulipa kiasi kile tu kulingana na uwiano uliowekwa na humtaka mwenye bima kudai kiasi kilichobaki kutoka kwenye bima nyingine. Kwa upande wako, kampuni yako ya bima, inafanya jambo jema, kujaribu kupata fedha kutoka kwenye kampuni nyingine ya bima ili iweze kukulipa dai lako. Unatakiwa utambue kwamba kifungu cha namna hiyo huwekwa makusudi kwa lengo la kuzuia udanganyifu.

Je, hii ni haki? Jibu ni ndiyo. Ikiwa ni kweli ulifanya bila dhamira mbaya, unapaswa kulipwa, isipokuwa tu kama kuna taarifa za ziada ambazo haziko katika ufahamu wetu.

## Masharti mengi katika Kifungu cha Kuhamisha Majukumu

**Nimesaini mkataba wa muda mrefu na kampuni miaka kadhaa iliyopita. Mkataba ni wa usambazaji malighafi fulani. Ningependa kuhamisha mkataba kwenda kampuni nyingine kwa kuwa nina nia ya kufunga shughuli zangu nchini Tanzania. Upande mwingine umenitaarifu kwamba kuna utaratibu wa kufuata na kwamba jukumu haliwezi fanyika bila kupitia huo utaratibu. Walinionesha kifungu cha kuhamisha majukumu kilichopo kwenye mkataba. Je, kifungu cha kuhamisha majukumu hakipaswi kuruhusu uhamishwaji wa majukumu moja kwa moja?**

*12 Oktoba 2009*

Mkataba uliosaini unazuia badala ya kukataza uhamishwaji wa majukumu. Vifungu vya namna hiyo wakati mwingine hujulikana kama vifungu vya kuzuia uhamishwaji wa majukumu. Zina faida ya kutobadilika kuliko kifungu cha kawaida cha kuhamisha majukumu, lakini ni rahisi kubadilika kuliko kutoruhusu uhamishwaji wa majukumu.

Hujaeleza taratibu ni zipi katika kuhamisha majukumu. Mara nyingi vifungu vya namna hii huhitaji ombi rasmi ili ruhusa itolewe na hasa kwa kuzingatia mahitaji ya masharti ya awali ya majukumu ya mkataba. Vifungu hivi pia hutoa vigezo mbalimbali ambavyo msingi wake ni kuzuia kuhamishwa kwa majukumu bila ruhusa.

Umeuliza iwapo kifungu cha kuhamisha majukumu kinapaswa kuwepo bila masharti yeyote. Yote yatategemea lengo la kifungu hicho. Kifungu chako kinazuia na inaonekana utahitaji kutimiza masharti hayo kabla ya

kuhamisha majukumu. Vinginevyo utakuwa umevunja mkataba.

Jambo moja la ziada ambalo unatakiwa kuzingatia ni kuona kama kuna mahitaji yoyote rasmi chini ya mkataba kwa wewe kuwajulisha upande mwingine kuhusu mabadiliko ya wanahisa au wakurugenzi. Ikiwa sio, unaweza kuuza kampuni nzima kwa mtu unayetarajia kumhamishia mkataba, isipokuwa tu kama kutakuwa na sababu (sababu za kodi) zinazozuia wewe kufanya hivyo.

## Fidia kwa Vipodozi vilivyoteketezwa

**Ninamiliki duka la kuuza vipodozi katikati ya Jiji. Wiki iliyopita mtu aliyejitambulisha kama Mkaguzi kutoka Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Tanzania alikamata baadhi ya vipodozi vilivyokuwepo dukani na kuviteketeza kwa moto akidai kwamba ni hatari kwa matumizi ya binadamu na Serikali imepiga marufuku kuuza. Naweza kudai fidia kwa kuwa nilikuwa nafanya biashara nikiwa na leseni halali ya kuuza vipodozi?**

*5 Oktoba 2009*

Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003 inakataza wazi uuzaji wa aina yeyote ya vipodozi; isipokuwa kama bidhaa hiyo ya vipodozi inaendana na masharti yaliyowekwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Tanzania (TFDA). Waziri wa Afya pia, anaweza, kupitia gazeti la Serikali, kutangaza kukataza bidhaa yoyote ya vipodozi kutumiwa au kuuzwa.

Kama vipodozi ulivyokuwa unauza vilikuwa vimetangazwa kupigwa marufuku kwa ajili ya kuuzwa, basi kilichofanywa na Mkaguzi kilikuwa ndani ya sheria. Nia ya TFDA ni kulinda wananchi kutotumia madawa na vipodozi hatarishi.

Kama una sababu yoyote ya kuamini kwamba vipodozi havikuwa sehemu ya orodha iliyopigwa marufuku, basi unaweza kukata rufaa kwa Waziri dhidi ya kitendo hicho, ingawa hakutokuwa na uwajibikaji binafsi wa Mkaguzi, ikiwa alikuwa anafanya au kutekeleza majukumu chini ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, kwa nia njema.

Kuhusu suala la fidia, ikiwa bidhaa zilizoteketezwa hazikupigwa marufuku, una kesi nzuri na unaweza kuendelea kudai fidia kwa ajili ya bidhaa hizo na hasara zingine.

Tungependa kusema kwamba kwa kuwa tu una leseni haimaanishi kwamba unaweza kuuza bidhaa za vipodozi zilizopigwa marufuku.

## Makubaliano ya Awali

**Nilikuja Dar es Salaam kujadili mpango fulani kwenye sekta ya madini. Baada ya wiki kadhaa za majadiliano, makubaliano ya awali ya kina yalisainiwa na upande mwingine ambaye ni mwenyeji, na nilitimiza masharti yote kwa mujibu wa makubaliano ya awali na kulipa kiasi kilichokubaliwa. Upande mwingine umekataa kutekeleza misingi iliyopo kwenye makubaliano ya awali ukidai kuwa hauwabani. Tafadhali naomba ushauri.**

*28 Septemba 2009*

Kuelezea maana ya "makubaliano ya awali" inategemea imetumika katika muktadha upi. Hata hivyo, kwa kawaida makubaliano ya awali huandaa aina ya nyaraka zitakazotumika kwenye mkataba ambazo upande mmoja au pande mbili zinakusudia kuanzisha majadiliano na kutekeleza masharti ya mkataba. Inaonekana hatua uliyoifikia ilikuwa zaidi ya hii na huenda ukawa umeshasaini mkataba, ambao unaweza ukawa na msaada mkubwa kwako.

Ingawa hatuna maelezo yote na hata nakala ya makubaliano ya awali, inaonekana kama makubaliano yako ya awali yameandaliwa kama vile ulikuwa mkataba na kwa sababu tu unasoma makubaliano ya awali, haimaanishi

kwamba hauwezi kutafsiriwa kama mkataba. Tunashauri kuwasilisha makubaliano yako ya awali kwa mwanasheria wako kwa ajili ya kutafsiri maudhui yake.

## Deni la Familia kwenye Mkataba

**Nimekuwa najishughulisha na biashara ya mbao na baba yangu hadi hivi karibuni nilipoamua kuanzisha kampuni yangu mwenyewe. Baada ya kutapeliwa na muuzaji, niliingia kwenye deni kubwa ambalo baba yangu aliamua kulichukua ili kulilipa. Hayo yote yalifanywa kwa kusaini barua. Baba yangu bado hajalipa hilo deni na tarehe iliyotakiwa kulipa hilo deni imeshapita. Mfanyabiashara ametishia kufungua mashtaka ya madai dhidi yangu. Je, nina wajibika kwa lolote? Tafadhali niongoze.**

*28 Septemba 2009*

Kwenye Sheria ya Mikataba, kuna kanuni ya "kuhuisha" inayotambua kuwa upande mmoja kwenye mkataba unaweza kumuondoa upande mwingine na kumbadilisha na mtu mwingine ambaye atachukua majukumu ya mtu aliyetolewa. Kutokana na maelezo uliyotupa, ni dhahiri kwamba deni lako limeshachukuliwa rasmi na baba yako chini ya kanuni ya kuhuisha. Kwa mujibu wa barua ambayo baba yako amesaini, mkataba mpya ulitengenezwa kati ya mkopeshaji wako na baba yako.

Kwa mujibu wa kifungu cha 62 cha Sheria ya Mikataba, iwapo wahusika kwenye mkataba wamekubaliana kuingia mkataba mpya kwa lengo kufuta mkataba wa mwanzo au kubadilisha mkataba huo, mkataba wa awali hauwezi kutekelezwa. Kwa hiyo, hata kama hapo awali hakukuwa na mahusiano ya kimkataba kati ya mkopeshaji wako na baba yako, kwa kutumia kanuni ya kuhuisha, mkataba mpya kati yao uliundwa wakati baba yako amesaini kwenye ile barua.

Ni baba yako ambaye anapaswa kulipa deni. Ikiwa mfanyabiashara huyo ataamua kuanzisha shtaka kwa ajili ya kulipwa deni lake, basi anatakiwa afanye hivyo dhidi ya baba yako. Huwezi kuwekwa sehemu ya shauri hilo na itakuwa ni kosa kisheria kushtaki upande usiohusika iwapo ataamua kukushtaki. Kwa uhakika, baba yako ndiye anayetakiwa kuwa na wasiwasi na sio wewe.

## Tishio la Kubomolewa na Amri ya Zuio

**Mamlaka ya Kinondoni ilinipa kibali cha kuendeleza ofisi katika eneo fulani lililopo Toure Drive, Dar es Salaam. Sasa tuko kwenye ghorofa ya tatu na tumepewa taarifa ya kubomoa ndani ya siku thelathini. Mwanasheria wetu anatushauri kwenda mahakamani na kufungua kesi na kupata amri ya zuio. Sijawahi kuhusika katika kesi yoyote na nisingependa kupambana mahakamani. Nifanye nini? Je, amri ya zuio ni nini na masharti yake ni yapi? Je, Jaji atakuwa tayari kutoa amri hiyo dhidi ya mamlaka iliyomteua?**

*21 September 2009*

Mwanasheria wenu yupo sahihi. Unapaswa kuwasilisha maombi mahakamani ili kupata zuio. Tunatambua kuwa hujawahi kuwa mahakamani - hata hivyo, unakwenda mahakamani ili kupigania haki zako, ukiamini kuwa una vibali halali labda kama hauna tatizo ukibomolewa.

Una mambo mawili ya kuchagua, chaguo la mahakama ni la kwanza. Chaguo la pili ni kujaribu kutatua hili kwa njia ya majadiliano nje ya mahakama na mamlaka ya Kinondoni lakini hakikisha kuwa unapata baraka zao kwa maandishi.

Zuio ni suluhisho la kisheria ambalo mtu huelekezwa kutofanya au kufanya jambo fulani au kitu fulani, na kwa upande wako zuio hilo litaelekezwa kwa mamlaka ya Kinondoni, watumishi wake na mawakala wake. Ni zuio

ambalo lengo lake ni kuhakikisha jambo linagombaniwa linabaki kama lilivyo kusubiria maamuzi ya kesi ya msingi.

Kanuni zinazoongoza busara ya mahakama wakati wa kutoa zuio la muda ambazo unapaswa kuzizingatia ni kwamba unapaswa kuithibitishia mahakama kwamba kuna kesi ya msingi, ikimaanisha kuwa kuna mgogoro mkubwa wa kutolewa maamuzi kwenye hiyo kesi na kwa muonekano wa kesi ulivyo kuna uwezekano wa wewe kuwa na haki, kwamba kuna hasara isiyoweza kufidiwa ambayo inaweza kutokea na kwamba uingiliaji wa mahakama ni muhimu ili kukulinda wewe kutokana na hasara hiyo ambayo ni ngumu kuifidia kwa pesa na kwamba kwa manufaa ya pande zote, hasara ambayo inaweza kusababishwa iwapo mahakama itagoma kuruhusu ombi la zuio hilo ni kubwa kwako kuliko hasara atakayoipata mpinzani wako (Manispaa) mahakama ikitoa zuio. Kwa kifupi eleza kuwa una kikubwa cha kupoteza kuliko Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

Swali lako la mwisho ni kama Majaji watakuwa huru katika kutoa amri ya zuio dhidi ya taasisi iliyowateua. Ieleweke kuwa Majaji wanateuliwa moja kwa moja na Rais bila kuingiliwa na mtu yeyote ikiwemo halmashauri za manispaa ambazo ni mamlaka za chini. Na kama ilivyo kwenye nchi nyingine nyingi, majaji wa Tanzania wanasimamia utawala wa sheria. Haijalishi ni nani anashindana dhidi ya nani. Tunaamini mfumo wa mahakama utaweza kukulinda, iwapo kama hujahusika na uovu wowote.

Kama utapitia kanuni moja baada ya nyingine za hapo juu, utaona kwamba una nafasi nzuri sana za kupata zuio. Sikitiko letu - kwa sababu ya mlundikano wa maswali, tumeweza kujibu swali lako baada ya miezi mitatu tangu ulitume. Tunaamini kwamba ulifuata ushauri wa mwanasheria wako, ulifungua shtaka na kupata amri ya zuio!

## Uvunjaji wa Taratibu za Zabuni

**Niliomba zabuni ya usambazaji magari makubwa kwenye idara ya Serikali. Kutokana na vikwazo vya muda, niliambiwa kwa mdomo kwamba niendelee na utaratibu wa kuyaagiza hayo magari. Baada ya kufanya mpango wa uagizaji na baada ya mara kadhaa kufuatilia mkataba, niliambiwa kuwa kila mtu ambaye aliomba zabuni, nikiwemo mimi, amekataliwa. Niko kwenye mshtuko. Tafadhali naomba ushauri.**

*7 Septemba 2009*

Manunuzi nchini Tanzania yapo chini ya Sheria ya Manunuzi ya Umma. Chini ya Sheria hiyo, Bodi ya Zabuni ina haki ya kukataa zabuni nzima. Hii uhalalishwa tu ikiwa kuna ukosefu wa ushidani katika zabuni. Zabuni kwa kiasi kikubwa hukataliwa kwa nyaraka za zabuni, kiuchumi au data za kiufundi za mradi zimebadilishwa au kiasi cha fedha kilichowekwa kwenye zabuni ni cha juu kuliko kiasi kilichopangwa. Kama zabuni ilikataliwa kutokana na ukosefu wa ushindani, basi Bodi ya Zabuni inaweza kutangaza tena zabuni.

Kwa upande wako, hatujui kwa nini zabuni imekataliwa. Inaweza kuwa imetokana na mojawapo ya sababu hapo juu na hivyo ni halali. Hakuna la ziada ambalo unaweza kufanya katika hatua hii.

Kuhusu uagizaji wa magari, hujataja ni nani aliyekupa ruhusa ya kuagiza. Inashangaza kuona kwamba uliandaa utaratibu wa kuagiza magari bila ya kuwa na mkataba wa maandishi. Kwa hali yoyote, ikiwa ndivyo ulivyokuwa ukifanya kazi na idara hiyo kwa miaka kadhaa, unaweza kuwa na nafasi ndogo sana ya kudai kuwa kulikuwa na mkataba. Hata hivyo, nafasi yako ya kufanikiwa katika utekelezaji wa huo mkataba au kulipwa fidia ni ndogo sana. Unahitaji kuonana na mwanasheria wako kwa mwongozo zaidi.

## Ndege kukaguliwa kabla ya Kuondoka

**Mimi ni mfanyakazi katika kampuni ndogo**

**ya kukodisha ndege kutoka Kenya. Hivi karibuni, nilikuwa nasafiri kutoka Mombasa kwenda Pemba ikanilazimu kwa dharura nitue Dar. Nilikuwa nimebeba raia wawili wa Yemeni na mwingine kutoka Somalia, wote wanafanya kazi kampuni hiyo hiyo. Wakati wa kutua, nilizingirwa na kundi la polisi ambao walidai kwamba wanahisi ninajihusisha na shughuli za kigaidi, hivyo wanahitaji kuikagua ndege na abiria. Tulibaki Dar zaidi ya masaa manne na kupoteza kazi ya kurudi na abiria kwa sababu ya jambo hili. Je, ukaguzi ulifanyika kihalali? Inakuwaje sisi nchini kwetu hatuna utaratibu kama huo? Je, ninaweza kudai fidia kwa kupoteza biashara?**

*14 Septemba 2009*

Haijalishi kama wewe ni kampuni ndogo au kubwa, sheria yetu inamchukulia kila mtu sawa. Chini ya Sheria ya Kuzuia Ugaidi, polisi anaruhusiwa kusimamisha, kuingia na kukagua ndege, chombo cha usafiri au gari yoyote ikiwa ana sababu ya kusadiki kuwa ndani yake kuna ushahidi wa kufanyika au uwezekano wa kufanyika kosa, kwa hiyo ukaguzi ulifanyika kisheria. Kuhusu kuwa hamna "tabia hiyo" huko kwenu, hatujakuelewa unamaanisha nini. Tanzania ni nchi huru ambayo ina sheria zake ambazo ni lazima zizingatiwe. Haijalishi kama wewe ni jirani yetu – ukiwa kwenye anga ya Tanzania au juu ya ardhi, sheria ya Tanzania itatumika. Na kulingana na maoni yetu ukaguzi ulifanyika kisheria, hakuna uwezekano wa wewe kudai fidia.

## Kudai upya Zawadi

**Nimekuwa katika mawasiliano na rafiki yangu wa utotoni kwa miaka mingi. Katika kipindi cha urafiki wetu tumepeana zawadi mbalimbali. Siku kadhaa zilizopita, rafiki yangu, ambaye kwa sasa anaishi Dubai, alisafirisha gari kwa jina langu kama zawadi. Nilitumia gharama kulitoa gari na sasa wakati naendesha hilo gari, rafiki yangu anataka nimrudishie hilo gari. Nifanye nini? Je, anaweza kudai kurudishiwa gari kwa namna hii?**

*17 Agosti 2009*

Zawadi ni uhamisho wa hiari wa mali kutoka kwa mtu mmoja au taasisi kwenda kwa mtu mwingine unaofanyika bila madai au malipo, kwa nia thabiti kwamba mali hiyo haitorudi kwa mtoaji na kwa nia thabiti kwa upande wa mpokeaji kubaki na mali hiyo kama yake mwenyewe bila kurejesha kwa mtoaji. Kwa zawadi kuwa halali, hata hivyo, lazima kuwe na tendo la kutoa kwa upande wa mtoaji/mfadhili na tendo la kupokea kwa upande wa mpokeaji/mfadhiliwa, nia ya kutoa na nia ya kupokea, ufikaji wa mali kwa mpokeaji na zawadi lazima ukamilike. Kinyume cha hapo, utoaji wa zawadi unaweza ukasitishwa muda wowote kabla haijafika kwa mpokeaji.

Kwa mazingira yako, kulikuwa na nia ya wazi ya kutoa gari na wewe ulikuwa na nia ya kukubaliana na hilo. Kwa kuwa ulilitoa, ukalisajili kwa jina lako na liko katika miliki yako, labda kama umeridhia kulirudisha, kisheria gari ni mali yako. Kama hakuna kitu chochote ulichotuficha, unaweza kuendelea kufurahia kulitumia gari lako.

## Muda ni Muhimu katika Mkataba

**Mimi ni mnunuzi wa samaki niliyeko Ulaya na sasa niko kwenye mazungumzo ya mkataba na kampuni ya kusindika samaki iliyopo Mwanza. Nawezaje kukabiliana na suala la usafirishaji kwa wakati kitu ambacho ni muhimu katika mikataba ya namna hii?**

*24 Agosti 2009*

Kipengele hiki lazima kielezwe wazi katika mkataba. Kwa kuwa upo katika biashara ya chakula ambacho ni rahisi kuharibika, ni

muhimu mno kwa wewe kuweka kifungu kihusucho umuhimu wa kuzingatia muda. Endapo tu kifungu hicho kitajumuishwa kwenye mkataba wako, muda wa kuridhisha wakati wa kuteleza mkataba utatumika kama kutatokea tatizo lolote kuhusu suala la muda. Kwa njia hii, utakuwa umeweka muda sahihi wa utekelezaji kuwa muhimu, na kama halitafanyika kwa wakati uliopangwa, unaweza kudai fidia kwa uvunjifu wa mkataba. Kifungu hiki kinatakiwa kitengenezwe kutatua masuala yahusuyo muda katika mkataba wako.

Mfano wa kifungu tunachoweza kupendekeza: 'Muda ni wa kuzingatia kulingana na vipengele vyote vya mkataba huu ambavyo vinabainisha muda kwenye utendaji; ikizingatiwa, hata hivyo, kuwa yaliyotangulia yasifafanuliwe kuzuia au kuunyima upande mmoja faida ya uhuru wowote au kutumia muda ulioruhusiwa kwenye mkataba huu'.

Kipengele kingine ambacho unatakiwa kukizingatia ni masharti ya malipo - shauriana na mwanasheria wako kwa mwongozo zaidi.

## Maana ya Vifupisho vya maneno katika Mikataba ya Kibiashara Kimataifa (Incoterms)

**Nimeingia mkataba na msambazaji wa kigeni. Cha kushangaza mkataba una kurasa chache ingawa bidhaa zina thamani ya mamilioni ya Dola. Mkataba unataja neno Incoterms. Ni nini hiki na mimi nalindwaje?**

*10 Agosti 2009*

Ulitakiwa uulize hili swali kabla ya kusaini mkataba! Misemo ya kizamani ya kwamba biashara kubwa huwa na mikataba mirefu, haina maana tena. Kwa sababu tu wewe unanunua bidhaa zenye thamani ya mamilioni ya Dola haina maana kwamba mkataba lazima uwe mrefu. Mkataba mzuri ni ule unaozingatia pande zote katika mazingira yote. Kwa sababu tu mkataba wako ni mfupi haina maana kwamba haujaandaliwa vizuri - unahitaji kuangalia maudhui ya mkataba kutambua kama umelindwa au la.

Nikija kwenye swali lako, Incoterms ni mkusanyiko wa maana ya maneno ya biashara za kimataifa yanayotambuliwa kimataifa, kama vile kujua ni wakati gani nani (muuzaji au mnunuzi) atawajibika na bidhaa zinazosafirishwa (Free on Board - FOB), jukumu la usafirishaji mizigo baada ya bidhaa kulipiwa na ukomo wa jukumu hilo (Cost and Freight - CFR) na gharama zinazohusiana na bima na usafirishaji (Cost, Insurance and Freight - CIF), iliyoandaliwa na Baraza la Biashara la Kimataifa (ICC) mjini Paris, Ufaransa. Inafafanua majukumu katika mikataba ya biashara na wajibu kati ya mnunuzi na muuzaji. Ni muhimu sana na husaidia kuokoa gharama. Msafirishaji bidhaa na muagizaji bidhaa hawana haja ya kufanya majadiliano marefu kuhusu masharti ya kila manunuzi. Wakishakubaliana tu kwenye neno la kibiashara kama FOB, wanaweza kuuza na kununua kwa kwa kutumia FOB bila kujadili nani atakuwa na jukumu la usafirishaji, bima ya mizigo, na gharama nyingine na hatari. Incoterms katika matumizi ya sasa ni toleo la mwaka 2000.

Incoterms huleta umakini na hutoa majukumu ya wazi kwa pande zote mbili. Iwapo haya yalijadiliwa haijulikani lakini kwa kawaida Incoterms hutoa ulinzi bora kwa wote, mnunuzi na muuzaji. Kwa mazingira yako, unahitaji kusoma mkataba ili uwe na uhakika kama unalindwa vya kutosha.

## Taarifa ya Kubomoa kutoka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)

**Mimi ni 'mmiliki mwenza' wa jengo na Shirika la Nyumba Tanzania (NHC) na nimepewa notisi ya miezi mitatu ya kubomoa. Mimi sio mpangaji wa NHC na nina hati miliki ingawa ghorofa nyingine mbili katika jengo**

**hili zinamilikiwa na NHC. Silipi kodi kwa NHC na nimeshtushwa na taarifa hii ambayo inashangaza. Sitakiwi kufidiwa? Haki zangu ni zipi? Inawezekanaje NHC kuuza kiwanja bila ruhusa yangu? Nifanye nini?**

*17 Agosti 2009*

Hili ni suala ambalo wengi linawakabili. Taarifa za uvunjwaji wa mali ambazo zinamilikiwa kwa pamoja na NHC kwa maoni yetu, lina changamoto, ikizingatiwa kwamba hukushirikishwa wala kufikiriwa kuingia kwenye ubia. Mazingira yako ni tofauti na yale ya mpangaji na hivyo una kesi nzuri.

Kihistoria, majengo yaliyotwaliwa na Serikali kipindi cha utaifishaji yaliwekwa chini ya NHC ya sasa. Wale wamiliki wa nyumba wakawa wapangaji lakini baadaye, Serikali iliamua, kwa mamlaka iliyokuwa nayo, kurudisha ghorofa zile ambazo mmiliki husika alikuwa akiishi. Mkataba wa muda mrefu wa kupangisha ulikubaliwa na ndicho hicho unachokiita 'hati miliki' kilitolewa.

Hujashirikishwa katika mchakato wowote bali umepewa taarifa ya kuvunja. Swali lako ni muhimu – unawezaje kupata fidia au tuseme unawezaje kuondokana na hii hali?.

Tutakushauri mbinu mbili. Maoni yetu ni kwamba una kesi nzuri dhidi NHC na pia dhidi ya mbia wao atakayeendeleza, na hivyo tunapendekeza ukutane na NHC kuona uwezekano wa kulitatua suala hili kwa amani.

Ukiona hujaridhika na mazungumzo au fidia iliyotolewa na NHC, kama ipo, unaweza kuwasilisha kesi katika Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi. Inashauriwa pia ni vyema kupata amri ya zuio la muda dhidi ya ubomoaji.

## Ni lazima Mkataba wangu uwe kwa Maandishi?

**Kwa nini watu wananishauri kuwa na mikataba ya maandishi wakati sheria inatambua mikataba ya mdomo? Nimekuwa katika biashara kwa zaidi ya miaka sitini na nimeamini kwamba neno hutawala dunia. Mikataba huleta kutoaminiana. Maoni yako ni yapi?**

*10 Agosti 2009*

Hatuna uhakika ulipoupata huu msemo 'neno hutawala dunia' ila kwa hakika ni jambo jema kujifunza hili.

Mkataba mzuri uliowekwa kwenye maandishi hupunguza utata katika kila kipengele au masharti. Ni muhimu pia kwa mwendelezo iwapo mikataba itaandikwa kwa uwazi. Mungu apishie mbali, kama mtu mmojawapo katika mkataba akafariki, warithi wanawezaje kuuendeleza? Mara zote tunawashauri wateja wetu kuwa wakati wa mikataba ya mdomo ushapita – zimeshapita siku zile ambazo unaweza tu kutegemea neno la mtu. Mikataba haileti kutoaminiana bali, huhakikisha kwamba mahusiano yanaimarishwa.

Hatukubaliani kabisa na wewe, isipokuwa, kama, unaendesha biashara ndogo sana, kiasi kwamba kiasi kinachotakiwa kuandikiwa mkataba hakina maana kwamba hata gharama ya karatasi ya kuchapisha huo mkataba itakuwa kubwa sana kuzidi gharama itakayohusika katika mkataba. Vinginevyo unapaswa kuweka mkataba wako kwenye maandishi. Unaweza ukaandika hata kwa mkono na katika lugha ya kawaida isiyokuwa ya kisheria, lakini unapaswa kuwa kwenye maandishi. Kwa hakika umekuwa ni mtu mwenye bahati sana kwa kipindi chote cha miaka sitini.

## Kubomoa kwa sababu ya Kutokulipwa

**Niliingia mkataba na kampuni ambayo iliahidi kunilipa ndani ya siku thelathini kuanzia siku ya kuwapa huduma nyeti. Ili kuufanya mkataba wa malipo uwe madhubuti, tulikubaliana kuwa kama haitonilipa ndani ya muda tuliokubaliana,**

**nitakuwa na haki ya kubomoa moja ya majengo yao. Sijalipwa na nimepewa amri kutoka Mahakama ya Ardhi kwamba siwezi kubomoa jengo hilo. Nifanye nini?**

*3 Agosti 2009*

Huu ni mkataba wa ajabu sana. Kwa nini unataka kubomoa jengo la mdeni wako kama hautolipwa? Utapata unafuu gani, labda kama ardhi ingekuja kwako baada ya kubomoa, kitu ambacho siyo. Hii inaonekana kama michezo ya kuigiza ya Shakespear au "Pwagu na Pwaguzi" na tunashangaa kama kweli mkataba huu upo. Katika hali yoyote, tutakujibu kama vile mkataba huo upo.

Kutokana na maelezo hapo juu, ni wazi kwamba kampuni uliyoipa huduma haijalipa. Lengo la msingi kwako ni kuokoa hizo fedha chini ya taratibu zetu za madai kulingana na mkataba mlioingia.

Kuhusu suala la kubomoa, hii ni kinyume cha sera za umma na pia inaashiria kuharibu mali ya mdaiwa na ni kinyume cha sheria. Hata kama kampuni ilisaini mkataba kuruhusu kufanyika kwa tendo hilo, mahakama itaisaidia kampuni. Mahakama iko sahihi kutoa amri ya zuio. Tunapendekeza kwamba tumia nguvu zako kurejesha fedha yako kuliko kubomoa hilo jengo.

## Mabadiliko ya Matumizi ya Hati Miliki ya Ardhi

**Nina eneo la ardhi karibu na Kibaha lenye hati ya umiliki wa miaka thelathini na tatu kuanzia 2002. Ardhi ni kwa ajili ya matumizi ya shule na ndivyo inavyoeleza kwenye hati. Hata hivyo, kwa sasa ningependa kujenga kituo cha mafuta badala ya shule. Je, ninahitaji idhini yoyote?**

*17 Agosti 2009*

Kulingana na Sheria ya Ardhi, unatakiwa kuomba kwa Kamishna wa Ardhi kubadilisha matumizi ili kutekeleza maendeleo haya mapya. Maombi yako lazima yaeleze pia kwa nini unakusudia kubadili matumizi ya ardhi.

Baada ya maombi, Kamishna atashauriana na kuzingatia maoni ya mamlaka inayosimamia huo mji, Serikali ya Mtaa na mamlaka nyingine yoyote ambayo idhini yake ni muhimu kwa ajili ya hayo mabadiliko.

Baada ya kupata idhini kutoka kwenye hizo mamlaka utatakiwa kupeleka hati yako ya umiliki wa ardhi kwa ajili ya kuidhinisha hayo matumizi. Hutakiwi kuanza maendelezo kabla idhini haijatolewa kwani maendeleo hayo yatakuwa ni haramu na kusababisha uvunjwaji wa majengo hayo au kufutwa kwa hati miliki ya ardhi. Unatakiwa ufahamu kwamba mabadiliko ya matumizi kwa mazingira yako yanaweza kukataliwa kwa kuzingatia sera za umma ikiwa ardhi ilikuwa na imelengwa mahsusi kwa ajili ya ujenzi wa shule.

## Kifungu kinachozuia Mabadiliko ya Mkataba

**Niliingia mkataba na kampuni iliyopo Dubai ambao ulisema kuwa mabadiliko yoyote katika mkataba yanapaswa kuwa katika maandishi. Je, hiki kifungu kinatenda haki? Nimezoea kufanya shughuli zangu kupitia simu ya mkononi na hata kwa mabadiliko kidogo tu, wanataka nifanye kwa maandishi. Inapoteza muda wangu. Nifanye nini?**

*27 Julai, 2009*

Muuzaji anajaribu kuwalinda ninyi nyote pamoja na kampuni yake. Kifungu hiki unachozungumzia ni "kifungu kinachozuia mabadiliko ya mdomo" na kinatumika zaidi katika mikataba ya kimataifa. Kifungu kinahitaji kwamba mabadiliko yoyote, hata kama ni madogo kiasi gani, yafanyike kwa maandishi. Ni kifungu kizuri na muhimu ambapo kwa bahati mbaya kinaonekana hakikusaidii.

Njia ya kulizunguka hili ni kuiomba kampuni ifanye marekebisho ya mkataba na kuweka kifungu kingine ambacho kitakuruhusu wewe kuomba kufanya mabadiliko kwa njia ya barua za kimtandao au ujumbe mfupi, ingawa upokelewaji wa ujumbe mfupi mahakamani bado una utata. Tunatambua unaweza ukawa kwenye mizunguko na huna nafasi ya kuweza kuiandikia kampuni kila wakati. Barua pepe na ujumbe mfupi unapatikana kwenye simu yako na zinaweza kutumika. Lazima kufahamu kwamba inakuwa vigumu sana kwa upande wowote kuthibitisha kesi yake wakati maelekezo ya mdomo yanapotolewa.

## Mgogoro wa Kimaslahi wa Mkurugenzi

**Mimi ni mkurugenzi wa kampuni ya madini ambapo nimegundua kwamba mkurugenzi mwenzangu pia ni mkurugenzi wa kampuni nyingine ambayo tumekuwa tukiipatia mikataba ya kutusambazia bidhaa. Ni hivi karibuni tu nimekuja kufahamu hilo. Mikataba yote ilifuata taratibu zote za zabuni na siwezi kusema kwamba mkurugenzi mwenzangu sio mwaminifu. Je sheria inasemaje?**

*20 Julai 2009*

Kwenye sekta ya madini, hakuna sheria ambayo hairuhusu mkurugenzi wa kampuni moja kuwa mkurugenzi wa kampuni nyingine. Isingekuwa kwa maslahi ya umma kwa kuwa na sheria kama hizo.

Hata hivyo, suala la kufichua taarifa limeelezwa wazi katika kipengele cha 209 cha Sheria ya Makampuni ambayo inaeleza wazi kwamba litakuwa jukumu la mkurugenzi wa kampuni pale ambapo yeye au mtu mwingine, kwa njia yoyote, moja kwa moja au sio moja kwa moja, ana maslahi kwenye mkataba au mkataba unaopendekezwa na kampuni kuweka wazi aina ya maslahi yake kwenye kikao na wakurugenzi wa kampuni.

Kwa hiyo, mkurugenzi mwenzako alilazimika aweke wazi maslahi aliyokuwa nayo kwenye kampuni iliyowasambazia vifaa. Hii inatumika hata kama yeye alipata hayo maslahi baada ya mkataba kufanyika.

Katika swali lako unaonekana kuondoa uwezekano wa udanganyifu au matumizi mabaya ya madaraka. Iwapo moja kati ya haya lilitumika, inaweza kumgharimu mkurugenzi mwenzio nafasi ya ukurugenzi wake.

Katika hali yoyote, kulingana na maelezo uliyotupatia na kulingana na Sheria ya Makampuni, mkurugenzi mwenzako atatakiwa kulipa faini kwa kutoweka wazi kuhusu ukurugenzi wake kwenye kampuni nyingine.

## Mkataba wa Usafirishaji umekuwa Mchungu

**Nilikodisha meli kubwa ya kubeba bidhaa za kwenda na kurudi Afrika Mashariki. Imeelezwa kwenye mkataba kuwa endapo kutatokea mgogoro tutapeleka mgogoro huo kwenye usuluhishi nchini Uingereza chini ya sheria ya Uingereza kabla ya kufungua kesi kwenye Mahakama ya Biashara Tanzania. Tuna matatizo kwenye mkataba na upande mwingine umepeleka suala hilo kwa msuluhishi ambaye ni ghali sana. Naweza kuhamishia huu mgogoro kwenye Mahakama ya Biashara?**

*20 Julai 2009*

Usuluhishi unatofautiana na uendeshaji kesi kwenye mahakama kwa kuwa utaratibu wake hauko rasmi hasa pale panapotokea mgogoro, bali hutegemea makubaliano ya awali kati ya pande husika, kama ilivyo katika mazingira yako. Pia ina vivutio vingi kwa wale wanaotarajia kufungua mashtaka kwani wakati mwingine huwa ni nafuu zaidi kuliko kwenda mahakamani, ni ya haraka zaidi na haiko kwenye mfumo rasmi. Wasuluhishi ambao huchaguliwa na wahusika kwenye mkataba kwa kawaida huwa ni wataalamu

kwenye eneo hilo ambao hawafikirii kujifunga na maamuzi ya kimahakama.

Katika hali hii, hakuna uwezekano wa wewe kuhamisha mgogoro huu kwenda Mahakama ya Biashara bila kwenda kwenye usuluhishi nchini Uingereza. Sheria itakayotumika wakati wa usuluhishi itakuwa ni sheria ya usuluhishi ya mwaka 1996 ya nchini Uingereza. Wakati mwingine unatakiwa kuwa makini zaidi na kipengele cha usuluhishi kabla ya kusaini. Tunakushauri kuteua wakili nchini Uingereza.

## Fidia kwa ajili ya Sarafu Bandia

**Mimi ni meneja benki hapa Dar. Katika mfululizo wa kupokea na kutoa sarafu, tulipokea sarafu kutoka kwa wateja ambazo ni bandia. Nimelazimika kuzipeleka Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kuziondoa kwenye mzunguko na kuziharibu. Je, benki kuu haiwajibiki kutufidia?**

*13 Julai 2009*

Kughushi ni kufanya nakala halisi ya kitu fulani kwa lengo la kuwadanganya watu kufikiri kwamba ni kitu halisi. Ikumbukwe kwamba kutoa sarafu ambayo ni bandia ni kosa la jinai na unaweza adhibiwa chini ya sheria.

Sheria yetu ya makosa ya jinai iko wazi kwenye hili kuwa afisa yeyote wa Serikali au meneja wa benki ambaye anapokea, wakati wa kutimiza majukumu yake ya kazi, sarafu yeyote, ambayo yeye ana kila sababu ya kuamini kuwa ni bandia anatakiwa aizuie na aipeleke kwa afisa wa Benki Kuu ya Tanzania ambaye atatakiwa kuikata, kuifuta au kuiharibu kwa fidia au bila fidia, kadiri atakavyoona inafaa. Maamuzi ya afisa wa Benki Kuu ya Tanzania kuhusu fidia itolewe au isitolewe yatakuwa ni ya mwisho, na hakuna mtu yeyote atakayestahili kudai, na hakuna shauri au hatua itachukuliwa dhidi ya Benki Kuu ya Tanzania au Serikali kuhusiana na hasara yoyote au madhara yaliyopatikana kwa sababu za kuiondoa na kuikata, kuifuta au kuiharibu.

Kwa hiyo, Benki Kuu ya Tanzania ina mamlaka ya hiari linapokuja suala la kuifidia benki yako. Kwa mwenendo wa soko ulivyo, hakuna uwezekano wa benki kulipwa fidia ila Benki Kuu ya Tanzania ndiyo yenye uamuzi wa mwisho.

## Hela imehamishiwa Kimakosa kwenye Akaunti yangu

**Benki yangu kimakosa iliingiza kwenye akaunti yangu kiasi kikubwa cha fedha. Sikujua kuhusu hili na kuishia kuzitumia fedha hizo. Benki sasa inanitafuta mimi. Ninawezaje kudai haki juu ya hizo fedha?**

*27 Julai 2009*

Benki zinaweza kufanya makosa kwa sababu zinaendeshwa na binadamu. Hii si mara ya kwanza sisi kusikia makosa kama hayo. Pia tunapata ugumu kuamini unaposema kuwa ulikuwa hufahamu kuhusu hela iliyoingia kwenye akaunti yako na ukaishia kuitumia .

Benki yako ina haki ya kukutafuta ili uweze kurudisha fedha yote iliyoingizwa kimakosa kwenye akaunti yako. Huna haki na hela ambayo ilitumwa kwenye akaunti yako isipokuwa tu kama utaweza kuthibitisha iliwekwa kwa ajili yako. Kwa sababu ulishaitumia hiyo hela na unahitaji muda wa kuilipa, unatakiwa kuwasiliana na meneja wa benki ambaye baada ya kufanya tathmini sahihi anaweza kukupa au kutokupa muda wa kuilipa hiyo hela.

## Kufunga Shughuli za Kampuni

**Kuna kampuni inayofanya shughuli zake hapa Dar haijalipa deni lake la muda mrefu kwenye kampuni ninayoimiliki. Nimeambiwa kwamba naweza kufunga shughuli za hii kampuni ikiwa watashindwa kunilipa. Je, hii inamaanisha nini?**

*13 Julai 2009*

Kufunga au kufilisi shughuli za kampuni ni utaratibu ambao kampuni inaweza kuvunjwa. Inaweza kuanzishwa na wanahisa au wakopeshaji wa kampuni au kwa amri ya mahakama. Inahusisha uteuzi wa mfilisi ili kuweza kuchukua udhibiti wa kampuni kutoka kwa wakurugenzi wake. Mfilisi hukusanya mali, hulipa madeni, na hugawanya ziada yoyote kwa wanahisa wa kampuni kwa mujibu wa haki zao.

Tishio la kufilisiwa ni kubwa, huchochea makampuni mengi kuchukua hatua. Kwa kawaida, kama deni lipo na halina ubishi, hatua sahihi kwa kampuni, ambayo ipo katika mchakato wa kufilisiwa au kufungiwa biashara zake, ni kulipa tu.

Kipengele cha 279 cha Sheria ya Makampuni kinakuruhusu wewe kufungua maombi ya kuifunga kampuni kama haina na uwezo wa kulipa deni lake, na imeshindwa kufanya hivyo, siku ishirini na moja tangu siku ulipowapa taarifa ya kutaka kulipwa deni hilo. Wakati wa kusikiliza maombi hayo mahakama inaweza ikayafuta, kuahirisha usikilizwaji wake, au kutoa amri nyingine ya mpito, au nyingine yoyote ambayo mahakama itaona inafaa.

## Taarifa za kila mwaka kwa Makampuni

**Kwa nini ninatakiwa kuwasilisha taarifa za kila mwaka kwa Msajili wa Makampuni? Je, ni lazima kwangu kufanya hivyo? Hii inaongeza urasimu Tanzania.**

*20 Julai 2009*

Uwasilishaji wa taarifa hufanyika ili kuhakikisha kwamba jalada lako la kampuni linakuwa na taarifa mpya kwa Msajili wa Makampuni. Haya ni mahitaji ya sheria na ni ya lazima. Taarifa za kila mwaka hufanywa wakati wa maadhimisho ya siku kampuni iliposajiliwa, au siku ambayo taarifa za miaka ya awali ziliwasilishwa.

Sheria ya Makampuni inaeleza wazi kuhusu matakwa ya marejesho hayo. Kama kampuni itashindwa kurejesha taarifa za mwaka ndani ya siku ishirini na moja, kampuni au maafisa wa kampuni iliyoshindwa kutimiza wajibu huo watatozwa fani.

Hatukubaliani na wewe juu ya maoni yako ya mwisho kuhusu kuongeza urasimu - nchi nyingi zina mfumo huo wa kurejesha taarifa za kila mwaka.

## Dhamana ya Kampuni Hodhi ni Batili

**Nilisaini mkataba na kampuni ya madini iliyopo Tanzania na wakati wa mazungumzo tulikubaliana kuwa ikitokea wameshindwa kutimiza wajibu wao, kampuni hodhi itawajibika. Kichwa cha habari cha kifungu hicho kwenye mkataba kinasomeka 'Dhamana ya Kampuni Hodhi' lakini wakati wa kusoma kifungu, inashangaza kuona inaiondoa kampuni hodhi kutoka kwenye udhamini wa utekelezaji wa kampuni tanzu. Kichwa cha habari cha kifungu na kifungu chenyewe vinatofautina. Nifanye nini?**

*29 Juni 2009*

Ni vigumu sana kwa sisi kukupa jibu la ndiyo au hapana bila kusoma mkataba mzima lakini kwa jinsi ulivyo, inaonekana itakuwa ni vigumu kwa wewe kutekeleza kifungu hicho kwa jinsi unavyotaka. Utafungwa na mkataba kama ulivyo.

Hata hivyo, unatakiwa kuangalia kama kuna kifungu kinachozungumzia mkataba mzima. Kifungu kama hicho huwekwa ili kuufanya mkataba kuwa kielelezo cha mwisho ambacho unaweza kukitegemea, bila kujali mlikubaliana nini kabla ya kusaini. Unapaswa pia kuangalia kama kuna kifungu kinachosema vichwa vya habari vitatumika kwa ajili kurahisisha usomaji au kurahisisha kumbukumbu tu, na haitoathiri muundo au tafsiri yoyote ya masharti ya mkataba. Kama vifungu hivyo viwili vinaonekana, hautokuwa na uwezo wa kuilazimisha kampuni hodhi

kwa utekelezaji. Unatakiwa kushauriana na wakili wako kwa maelekezo zaidi.

## Kukamata Bidhaa ambazo Hazijalipiwa

**Nimekuwa nikiuza bidhaa kwa wateja na ningependa kujua ni jinsi gani naweza kujilinda kipindi ambacho hawalipi na nataka kuzirejesha bidhaa zangu. Nifanye nini?**

*22 Juni 2009*

Iwapo unahitaji kuzirejesha bidhaa zako, unaweza kuingiza kwenye mkataba wako wa mauzo kifungu cha 'mwendelezo wa umiliki wa bidhaa'. Kifungu cha mwendelezo wa umiliki wa bidhaa kitasema, utaendelea kumiliki bidhaa zilizouzwa hadi pale utakapolipwa, na unaweza kuingia kwenye eneo la mteja, kwa taarifa au bila taarifa, kuzichukua bidhaa hizo kwa kuwa hazijalipiwa. Kutegemeana na bidhaa unazouza, utahitaji kifungu makini cha umiliki wa bidhaa, kwa mfano, mteja wako ameuza bidhaa zako kwa mtu mwingine au amechakata bidhaa zako na kuzalisha bidhaa nyingine.

Unatakiwa kuhakikisha kwamba urejeshaji wa mali zako ni jambo muhimu. Hakikisha pia unaweza kuonesha bidhaa zipi ni za kwako. Kama hutoweza kuonesha bidhaa zipi ni za kwako kutoka kwenye bidhaa zinazofanana na za kwako kwenye eneo la mteja, haitokuwa rahisi kuweza kuzirejesha. Masharti yako ya biashara lazima yamtake mteja wako kuhifadhi bidhaa zako tofauti mpaka unalipwa. Kwenye utendaji wa kawaida, ni mara chache sana wateja huzingatia hilo, hivyo weka alama bidhaa zako kwa namna fulani - kwa jina lako au nembo, au idadi au mfululizo wa namba - hivyo kuweza kuzitambua hata kama zitachanganywa na bidhaa nyingine.

## Uuzwaji wa Sehemu iliyopo kwenye Hati Miliki

**Nimeuza sehemu ya ardhi iliyosajiliwa na nataka kugawa ardhi hiyo ili kila mnunuzi awe na umiliki tofauti. Je, ni sheria zipi zinahusika na taratibu za kufuatwa ili kufanya huo mgawanyiko?**

*29 Juni 2009*

Masuala yote yanayohusiana na uhamishwaji wa ardhi iliyosajiliwa husimamiwa na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999. Chini ya sheria hiyo mmiliki wa ardhi mwenye hati miliki anayetaka kuuza ardhi yake anaweza kuomba kwa Kamishna wa Ardhi kwa ajili ya kupata kibali cha kuhamisha ardhi yote au sehemu ya ardhi hiyo, vyovyote itakavyokuwa.

Kwa kawaida, maombi ya kibali cha uuzaji wa ardhi kwa Kamishna wa Ardhi hufanyika kwa pamoja na fomu za uhamishaji haki miliki. Hizi ni pamoja na kuwasilisha fomu za taarifa ya uhamishaji wa hati miliki na fomu kwa ajili ya uhamisho wa hati miliki, zikiambatana na mkataba wa mauziano uliosainiwa na muuzaji na mnunuzi. Mkataba wa mauziano unatakiwa kuonesha kwa kina maelezo kuhusu vipimo na bei ya sehemu ya hati miliki iliyouzwa.

Mara baada ya mauzo kuthibitishwa, Msajili wa Hati ataingiza majina ya muuzaji na mnunuzi kwenye masjala na umiliki wa kiwanja sasa utazingatia hisa alizokuwa nazo kila mmoja kwenye kiwanja.

Kwa madhumuni ya kugawa kiwanja, sheria inakuhitaji wewe kuomba kwa Mkurugenzi wa Manispaa husika aweze kuidhinisha. Barua ya maombi iliyoambatana na hati ndogo, lazima ieleze sababu za ugawaji. Maombi yanaweza kuwa na mafanikio kama, kwa mfano, viwanja vyote vitakuwa tayari vimeendelezwa kwa kujengwa nyumba juu yake na kwamba nyumba hizo zimejengwa kwa vibali vya ujenzi vinavyotambuliwa.

Kibali cha kugawa kiwanja kinaweza, hata hivyo, kukataliwa kama ukubwa wa viwanja, baada ya kugawanywa, ni vidogo mno ikilinganishwa na viwanja vilivyopo jirani na eneo hilo.

## Kifungu cha Adhabu kwenye Mkataba

**Niliingia mkataba na kampuni ya ujenzi nchini Tanzania na kulikuwa na kifungu cha malipo ya fidia kwa ucheleweshaji wowote katika kukamilisha kazi. Palipotokea ucheleweshaji na nikadai malipo ya fidia, upande mwingine waliamua kwenda mahakamani na kulalamikia kifungu hicho wakidai kilikuwa ni kifungu cha adhabu. Tofauti ni nini? Sina haki ya kudai malipo ya fidia?**

*15 Juni 2009*

Mkataba unaweza kujumuisha kifungu cha 'malipo ya fidia' kitakachoelezea fidia gani italipwa kama upande mmoja utashindwa kutimiza wajibu wao katika mkataba. Lakini kama kitahusu 'kifungu cha adhabu', hakiwezi kutekelezeka.

Kifungu cha malipo ya fidia mara nyingi hutumika kwenye miradi ya ujenzi - kukubali kiwango cha fidia kama muda wa mradi utaongezeka.

Kujadili fidia mapema na kuijumuisha kwenye mkataba ina faida kadhaa ambazo huhusisha manufaa kwa wote mteja na muuzaji kutokana na ongezeko tarajiwa, fidia ambazo vinginevyo zingekuwa ngumu kuzipima, kama vile faida iliyopotea inaelezwa, uwezekano wa kufungua mashtaka ya madai kutokana na uvunjwaji wa mkataba hupungua na haja ya kutimiza masharti ya mkataba huzingatiwa, hupunguza athari za uvunjaji wa mkataba.

Kwa kawaida, masharti yaliyokubaliwa kwa uhuru na pande mbili katika mkataba yanatekelezeka. Hata hivyo, kifungu cha malipo ya fidia hakiwezi kutekelezeka kama kitahusu adhabu. Kifungu cha malipo ya fidia kilichokuwa na makisio ya kuridhisha ya hasara inayotarajiwa kinatekelezeka. Kifungu kinachojaribu kutishia muuzaji kutekeleza mkataba, badala ya kumfidia mteja kwa uvunjaji, ni adhabu. Pia makadirio yasiyo na uhalisia yanaweza kuchukuliwa kama adhabu na iwapo kitachukuliwa kama malipo ya fidia au adhabu sio muhimu.

Ni jinsi gani mtu anaweza kujua kama kifungu hicho ni kifungu cha malipo ya fidia au kifungu cha adhabu? Tabia za kifungu cha malipo ya fidia ni: makadirio yanayoridhisha kwenye hasara tarajiwa (bila kujali kiasi cha hasara halisi kitakachotokea), si lazima makadirio ya awali yawe sahihi bali yanapaswa kuwa halali, ya kuridhisha wakati wa kuingia mkataba badala ya wakati uvunjaji wa mkataba unapotokea na masharti yaliyojadiliwa kuna uwezekano mkubwa wa kuchukuliwa kuwa ni ya kuridhisha kuliko kifungu cha malipo ya fidia ambacho kimeibuliwa tu. Lengo ni kulinda maslahi ya wauzaji wadogo dhidi ya wale wakubwa.

Tabia ya kifungu cha adhabu ni: fidia huwa kubwa kuliko kiasi cha hasara kinachotarajiwa kutokea kutokana na uvunjwaji wa mkataba, na inapotokea tatizo, kiasi cha malipo ya fedha huwa ni kikubwa kuliko kiasi tarajiwa na kulipa fidia zaidi kwa matatizo madogo kwenye mkataba ukilinganisha na matatizo makubwa ambayo husababisha hasara kubwa.

Vifungu hivi vya malipo ya fidia vinatakiwa viandaliwe kwa umakini na umakini zaidi unatakiwa kuzingatiwa pale kifungu cha malipo ya fidia huwa suluhisho pekee pale inapokea mkataba umevunjwa. Kama kifungu hakitekelezeki, hakuna njia nyingine ya kudai fidia. Unapaswa kuweka ushahidi wa mazungumzo ya kukubali uwepo wa vifungu vya malipo ya fidia, na misingi ambayo kiasi hicho cha fidia kilikubaliwa.

Kwa mazingira yako, mkandarasi anajaribu 'kukimbia' hasara kwa kudai kuwa ni kifungu cha adhabu, hivyo kukifanya kisitekelezeke. Unahitaji kukiangalia kifungu katika muktadha wa tuliyoyaeleza hapo juu. Wakili wako atakuwa na uwezo wa kukuelekeza.

## Meli imetekwa Nyara na Maharamia

**Meli iliyokuwa imebeba shehena ya mizigo kuelekea Tanzania ilitangazwa kutekwa nyara. Wamiliki wa meli wametangaza kitu kinachoitwa 'hasara ya pamoja' na wanataka sisi tusaini nyaraka fulani. Nini maana ya hasara ya pamoja na tufanye nini?**

*8 Juni 2009*

Sheria ya hasara ya pamoja ni kanuni ya kisheria kwenye sheria za baharini ambayo pande zote kwenye safari hatarishi ya baharini, kwa usawa wanagawana hasara yoyote iliyojitokeza kutokana na kutolewa sadaka sehemu ya meli au shehena ya mizigo kuokoa meli nzima wakati wa dharura. Pale wanapokabiliwa na tukio la hatari baharini, wafanyakazi wa meli mara nyingi wanakosa muda sahihi wa kuchambua ni shehena ya mzigo wa nani unatupwa baharini. Hivyo, ili kuepuka mgogoro ambao unaweza kupoteza muda mwingi, kukatengenezwa utaratibu wa usawa ambapo wafanyabiashara wote ambao mizigo yao ipo melini wataitwa ili kuchangia sehemu, kulingana na hisa au asilimia, kwa mfanyabiashara au wafanyabiashara ambao bidhaa zao zilitupwa baharini kuondokana na hatari iliyokuwa mbele yao. Ingawa hasara ya pamoja asili yake ni kutokana sheria za kale za bahari, inaendelea kutumika kama sehemu ya sheria hadi sasa.

Ili hasara ya pamoja iwepo, mahakama wamekubali mambo haya matatu kuwepo. Kwanza, hatari iliyo wazi ambapo chombo, mizigo na watu wote kwenye meli walihusika, hatari iliyokuwa wazi na isiyoepukika, isipokuwa kwa kukubali kuingia kiasi fulani cha hasara ya mzigo kwa lengo la kuokoa kilichobaki.

Pili, lazima kuwe na utayari wa pamoja wa kutupa sehemu ya mizigo baharini, kwa lengo la kuepuka hatari iliyopo mbele yao, kwa maneno mengine, ni kuondoa hatari ambayo ingesababisha madhara makubwa na kuifanya iwe ndogo.

Mwisho, jaribio la kuepuka hatari ya pamoja lazima liwe la mafanikio.

Kutokana na yale uliyosema kuhusu maharamia, inaonekana kwamba tamko la hasara ya pamoja ni tamko sahihi. Hata hivyo, hatuwezi kukushauri iwapo unaweza kusaini nyaraka zote au baadhi hadi tutakapojua maudhui ya kile utakachosaini. Tunakushauri wasiliana na wakili wako ili aweze kutafsiri maudhui ya barua uliyotumiwa.

## Mahusiano ya Kiuwakala

**Mimi ni msambazaji wa bidhaa kwa muuzaji mkubwa wa bidhaa za rejareja na jumla Jijini Mwanza. Hivi karibuni nimemsikia akiwaambia wateja kwamba yeye ni wakala wetu. Nawezaje kujilinda dhidi yake ili asifanye kitu kwa niaba yangu?**

*1 Juni 2009*

Tunafurahi kuwa umeligundua hili. Watu wachache hugundua. Kwanza kabisa, je, una mkataba naye wa kumsambazia bidhaa? Kama huna, tunakushauri wasiliana na mwanasheria wako na hakikisha kwamba mkataba unatayarishwa ambao utaeleza wazi kabisa kwamba mnunuzi huyo wa jijini Mwanza sio wakala wako.

Kisheria, uwakala ni uhusiano ambao hujitokeza pale ambapo mtu mmoja (wakala) ana mamlaka, ambayo yameelezwa wazi au yamepatikana kutokana na mazingira yalivyo, kufanya kwa niaba ya mwingine (Mhusika mkuu) na amekubali kufanya hivyo. Kwa hiyo, wakala yuko katika nafasi ya kumuingiza mmiliki kwenye mkataba au mahusiano mengine na mtu mwingine. Mara nyingi, wahusika huwa wanataka kukana kuwepo kwa mahusiano ya kiuwakala kwa sababu ya matatizo ambayo yanaweza kutokea.

Kwenye mkataba utakaotengeneza, muelekeze wakili wako kuingiza, na kulingana na aina ya biashara kwa nia ya

kuboresha, kifungu kifuatacho: mkataba huu hautoanzisha au kuashiria ushirikiano wowote, ubia, uwakala, uhusiano wa kuaminiana au mahusiano mengine kati ya pande husika zaidi ya uhusiano wa kimkataba kama ulivyoelezwa wazi katika mkataba huu. Hakuna upande utakaokuwa na wala kuwakilisha kwamba una mamlaka yoyote ya kutoa ahadi zozote kwa niaba ya upande mwingine.

## Vidokezo muhimu wakati wa kusaini Mkataba

**Nategemea kuingia kwenye mkataba hivi karibuni. Ni mambo gani muhimu natakiwa kuzingatia kabla ya kusaini?**

*18 Mei 2009*

Kwanza kabisa, hakikisha unasoma na kuelewa kila neno lililopo kwenye mkataba. Epuka kusaini mkataba kwa mazoea, hivyo hakikisha unauliza maswali kama kuna kitu hukielewi. Pia hakikisha kwamba kiasi mnachokubalina kimetajwa vizuri ikiwa ni pamoja na masharti ya malipo yaani ni wakati gani kiasi hicho kinatakiwa kulipwa.

Tumebaini kwamba mikataba mingi haielezi wazi bidhaa au huduma zinazouzwa - sisitiza kwamba maelezo hayo yanakuwepo ndani ya mkataba. Angalia kama kiasi kilichopo kwenye mkataba kinahusisha kodi. Mambo mengine ambayo unapaswa kuangalia ni pamoja na: iwapo upande mwingine unaweza kuingia katika mkataba, je, mkataba ni halali kisheria? Je, una mamlaka ya kusaini mkataba huu kwa niaba ya kampuni yako? Fidia ya mkataba huu ni ipi pale utakapovunjika? Ni muda gani utatumika kutekeleza mkataba, kuna vibali vyovyote vitahitajika kutoka kwenye mamlaka ili kutekeleza mkataba huu?. Unatakiwa kuhakikisha kwamba yale yote ambayo yamekubaliwa yamewekwa kwenye mkataba – itakuwa haina maana kama utasaini mkataba na baadaye ukalalamika kwamba mkataba hauna kile kilichokubaliwa. Kumbuka kwamba mkataba mzuri ni ule usio na utata na rahisi kuuelewa. Wakili wako anaweza kukupa mwongozo zaidi kabla ya kusaini.

## Mkanganyiko wa Tarehe za Mkataba

**Nilisaini mkataba tarehe fulani na kudhani kuwa wajibu wangu ulianza siku niliyosaini, nikaja kugundua kuwa nilipaswa kuanza kutoa huduma yangu mwezi mmoja baadaye. Kwa nini kuna mkanganyiko wa terehe hivyo? Kwa nini mkataba haukupaswa kuanza siku ambayo ulisainiwa?**

*25 Mei 2009*

Inaonekana unachanganya tarehe ya kuanza kwa mkataba na tarehe ya kusaini mkataba. Tarehe hizi mbili si lazima ziwe moja. Huu ni mkanganyiko wa kawaida miongoni mwa watu wengi. Kwa mfano, unaweza kuingia mkataba leo na kukubali kuwa utaanza kutekeleza masharti ya mkataba wiki mbili baadaye.

Tarehe ya kuanza kwa mkataba kwa kawaida huonyeshwa kwenye mkataba. Kama hamna, unaweza kuchukulia siku ya kusaini mkataba ikawa ndiyo siku ya kuanza mkataba. Hujatueleza kama mkataba uliosaini kama una tarehe ya kuanza mkataba. Kama ipo hivyo basi mkataba utaanza kwenye siku hiyo tajwa/husika. Unahitaji kuangalia mkataba uliosaini.

Ni muhimu kusoma mkataba kwa umakini, kuelewa kanuni na masharti yake ni yapi kabla ya kusaini. Kama huelewi sehemu yoyote ya mkataba, unapaswa daima kutafuta ushauri wa kisheria. Inakuwa vigumu sana kupambana na kanuni na masharti ya mkataba baada ya kusaini. Tumegundua matukio mengi ambapo pande husika hawajasoma mkataba baada ya kuambiwa na upande mwingine kwamba hutoweza badilisha masharti ya mkataba! Hakuna ufafanuzi sahihi wa mkataba

usiobadilika masharti hivyo kuwa makini.

## Bila Leseni, bila Bima

**Nilisimamishwa na askari wa barabarani kwa kosa fulani. Je, unaweza kufungwa kwa kosa la barabarani? Kama ndivyo, kivipi na naweza kushtakiwa kwa lipi? Ni kosa kubwa kiasi gani kuendesha gari bila leseni na bila bima? Naweza kulalamika?**

*18 Mei 2009*

Ndiyo, unaweza kufungwa kwa kosa la barabarani. Sheria yetu ya makosa ya barabarani inatoa adhabu mbalimbali kwa makosa mbalimbali kuanzia faini, kufungwa au adhabu zote mbili. Hata hivyo, sheria iko wazi kwamba kwenye kosa lolote, kama sheria husika inatoa chaguzi tofauti za adhabu kuanzia na adhabu ya faini kama ilivyo kwenye makosa mengi chini ya sheria zetu, mahakama inayotia mtu hatiani lazima itoe hukumu ya faini isipokuwa kama kuna mazingira sahihi yanayohalalisha kutolewa hukumu nyingine tofauti. Mahakama inaweza kwa mfano, kuchagua kutoa adhabu ya kifungo kwa mtuhumiwa badala ya faini, kutokana na ushahidi wa hatia za awali na tabia za jumla za mtuhumiwa, kwa mfano, kama itathibitishwa kwamba mtuhumiwa ana mazoea ya kurudiarudia makosa ya barabarani. Hii ni bila kujali aina ya kosa.

Chini ya sheria, makosa yote ya barabarani ni makosa makubwa. Hata hivyo, kimazoea kuna aina mbili za makosa - makosa makubwa na madogo. Makosa makubwa yanahusisha makosa yale ambayo moja kwa moja yanasababisha hatari kwa watu. Haya yanahusiana na makosa ya kusababisha majeraha mwilini au kifo kutokana na uzembe au uendeshaji gari usiozingatia usalama barabarani na kuendesha gari bila leseni au bima. Makosa haya husikilizwa na mahakama na adhabu yake ni ama faini au kufungwa jela au vyote, kulingana na mazingira ya kila kesi husika.

Makosa madogo yanahusu makosa kama kuendesha gari barabarani likiwa na tairi chakavu, kushindwa kwa wamiliki kutoa vitambulisho kwa madereva au kuendesha baiskeli kwa utaratibu ambao ulishapigwa marufuku. Wahalifu wa makosa haya huadhibiwa papo hapo kwa kulipa faini elekezi kwenye kituo cha polisi kilicho karibu na eneo lilipofanyika kosa au moja kwa moja kwa afisa wa polisi wa barabarani aliyekukamata, na kupewa risiti rasmi.

Swali lako halibainishi kosa gani ulilokamatwa nalo na iwapo ulilipa faini au la. Hata hivyo, kutokana na swali ulilouliza, inaonekana hukuwa na leseni ya kuendesha gari au bima. Tafadhali, tambua kwamba makosa yote haya mawili adhabu yake ni kifungo kwa kuwa ni makosa makubwa.

Kuhusu kulalamika, hatuna uhakika unataka kulalamika kuhusu nini. Haina maana kulalamika kuhusu maafisa wa polisi wa barabarani wakati wewe ndo umevunja sheria. Ripoti kwenye makala za magazeti ya hivi karibuni inakadiriwa kuwa ajali za barabarani inaelekea kuwa moja ya chanzo kikuu cha vifo Kusini mwa Jangwa la Sahara barani Afrika kwa mwaka 2012.

## Mtoto amejeruhiwa kwenye Nyumba ya Rafiki

**Mtoto mwenye umri wa miaka 7 kutoka kitongoji cha jirani cha Msasani Peninsula alikuja kucheza na binti yangu katika nyumba yetu, ambayo tulipangishwa na kampuni. Wakati wakicheza mtoto wa jirani alipata majeraha wakati paa yetu ya nje ilipoporomoka. Mama wa mtoto ni kama anataka kujitengenezea faida kupitia hili tatizo na anakusudia kutufungulia mashtaka kwa ajili ya fidia na gharama za matibabu kwa majeraha aliyopata. Nawajibika kumlipa fidia?**

*11 Mei 2009*

Ni jambo lisilo la kawaida kwa paa kuporomoka. Kutokana na maelezo uliyoyatoa, nyumba yako inaonekana si sehemu salama ya kuishi. Sheria ya wajibu wa mmiliki wa makazi inakupa wewe wajibu wa kutunza maeneo unayoyamiliki na usalama kwa watu wote wanaopanga na kuingia maeneo hayo. Sio utetezi kusema kwamba wewe ni mpangaji tu na sio mmiliki wa nyumba.

Sheria inatoa wajibu wa kawaida wa kujali kwa mkazi wa jengo kama ilivyo kwa mmiliki. Sheria inatarajia kila mkazi, iwe ni mpangaji au mmiliki, kuchukua hatua muafaka za kuzuia maendeleo ya hali ya hatari katika majengo yao.

Kama mama wa mtoto ataweza kuthibitisha kwamba wewe au mmiliki wa jengo hamkuchukua hatua stahiki, utawajibika. Tofauti pekee hutokea pale mtu alijeruhiwa, alijua hiyo hatari, akaikubali na kisha akajeruhiwa. Hata hivyo, upekee huo hauwezi kutokea kwa mtoto mwenye umri wa miaka 7.

Kuhusu mama kutaka kujipatia faida, ni vigumu sana kwetu kutoa maoni. Kila mtu anataka kulinda mtoto wake; kudai haki yake kwa mujibu wa sheria haimaanishi kwamba yeye ni mpenda fedha.

## Kifungu kinachohusisha Makubaliano yote kwenye Mkataba

**Nilisaini mkataba ambao ulikuwa na kifungu kinachosema kuwa vipengele vyote vya makubaliano vimo ndani ya mkataba. Hata hivyo, mtu aliyeniuzia mashine aliniahidi zaidi ya kile kilichokuwemo kwenye mkataba. Mkataba ni wa mauziano ya mashine yenye thamani ya mabilioni. Je, nitalishughulikiaje hili? Nina bima - naweza kudai kupitia bima?**

*27 Aprili 2009*

Unapaswa kuwa makini kusoma nyaraka yoyote inayohusiana na mikataba kabla ya kusaini. Kifungu kinachotengeneza sehemu ya mkataba wako wakati mwingine hujulikana kama kifungu kinachokamilisha mkataba. Lengo la kifungu hicho ni kutamka kwamba vipengele vyote vya mkataba vinapatikana ndani ya mkataba ulioandikwa baina ya wahusika kwenye mkataba. Kwa sababu hii, kifungu hiki kinajaribu kuondoa nyaraka nyingine au kauli nyingine kuingia kama sehemu ya mkataba. Haya yanaweza kuhusisha kauli zilizotolewa na mwakilishi wa upande mmoja wa mkataba ili kuushawishi upande mwingine kuingia kwenye mkataba na / au nyaraka hizo ni kama vile vipeperushi vya matangazo au mawasiliano yeyote yaliyofanywa baina ya pande husika kabla ya mkataba.

Kabla ya kusaini mkataba, unatakiwa kusisitiza kujumuishwa kwa ahadi ambazo mtu wa masoko alitamka. Hujatueleza hizo ahadi zilikuwa ni zipi lakini kutokana na maelezo yaliyotolewa, inaonekana utakuwa na kesi ngumu sana ya kupambana nayo. Na ukweli kwamba mashine ina thamani ya mabilioni haikupi utetezi wa aina yoyote.

Kuhusu bima, mkataba wa bima ni ule ambao upande mmoja (mtoa bima) anakubali kwa malipo kuchukua jukumu la kulipa gharama ya fedha kwa ajili ya mtu mwingine (mpokea bima) pale panatokea tukio au tatizo fulani. Kwa mikataba kama hii kutekelezeka lazima kuwe na vipengele visivyotabirika kuhusu tukio lililokatiwa bima, kitu ambacho hatukioni kwenye tatizo lako. Hujatuleza ni aina gani ya bima uliyokuwa nayo lakini ni vigumu sana kwa bima kukupa ulinzi wa aina yoyote. Tunakushauri kumuhusisha wakili atakayesoma mkataba wote kuhusiana na hicho unachokisema na kuangalia kama kuna kingine chochote kwenye vifungu vingine vinavyoweza kukupa ulinzi.

## Utambulisho wa Benki umegeuka Mwiba

**Benki moja maarufu nchini Tanzania ilimtambulisha mteja fulani wa benki hiyo kwangu. Utambulisho huo ulikuwa ni wa jumla. Nilifanya biashara na mteja huyo na nimepata hasara ya shilingi ya kitanzania Milioni 285, kwenye malipo ya awali. Ninaweza kuishtaki benki?**

*13 Aprili 2009*

Unajaribu kuishtaki benki kwa kile tunachokiita uzembe katika kutoa taarifa sahihi ambazo huhusisha kauli zilizotolewa kwa uaminifu lakini bila kuwa na sababu za msingi za kuaminiwa.

Mara nyingi benki hutoa barua za utambulisho za jumla na zisizo wazi. Pia huweka vipengele vya kujiondoa kwenye lawama kwenye hizo barua. Lengo ni kuzuia au kuepuka uwajibikaji ambao unaweza kujitokeza, kwenye mazingira kama yako. Benki kwa kawaida sio mawakala wa kutoa utambulisho kwenye biashara na hii pia hutumika Tanzania.

Kama benki ilifanya kwa uaminifu wakati inatoa barua ya utambulisho, ni vigumu kufanikiwa kwenye shauri lako. Kwenye biashara ya namna hii baadaye, tunakushauri upate malipo ya awali ya hati fungani au dhamana ya benki kwa kiasi utakacholipa awali. Bado unahitaji kushauriana na mawakili wako kwa ajili ya kutafsiri barua ambayo benki wamekupa kuona kama unayo haki ya kufungua mashtaka.

## Mkataba wenye Tafsiri isiyo Rasmi

**Mimi ni mfanyabiashara wa Kitanzania niliyeingia mkataba na kampuni ya Uingereza kwa ajili ya usambazaji wa programu fulani. Baada ya kusaini mkataba, nilishangazwa na jinsi walivyotafsiri baadhi ya maneno. Neno la kawaida kwenye sekta hiyo lakini tafsiri yao kwenye mkataba ni tofauti na tafisri ya kawaida. Ningependa kutafsiri mkataba kulingana na tafsiri ya kawaida lakini wao hawataki, wakisema limetafsiriwa vizuri kwenye mkataba niliosaini. Nifanye nini?**

*6 Aprili 2009*

Kwa kuanzia, kabla ya kusaini nyaraka yoyote unatakiwa usome kila neno lilikuwepo kwenye mkataba. Kwa bahati mbaya umeshaingia mkataba na sasa umeamua kupingana na tafsiri ambayo ipo tayari kwenye mkataba. Kwenye swali lako hujataja hilo neno hasa ni lipi na limetafsiriwa vipi kwenye mkataba. Hata hivyo tutajibu swalli lako kwa ujumla.

Njia pekee ambayo upande kwenye mkataba unaweza kutoa tafsiri sahihi ya neno, ni kujumuisha tafsiri ya neno hilo kwenye mkataba, kama ilivyo kwenye mkataba wako. Kwa ujumla, mahakama itatumia tafsiri iliyotolewa na pande husika kwenye mkataba, haijalishi ni kiasi gani tofauti hiyo inaweza kuwa kwenye tafsiri ya kawaida ya neno hilo. Hata kama neno halijatafsiriwa bayana, mahakama inaweza kulitafsiri neno hilo kulingana na jinsi lilivyotumika na pande mbili kwenye mkataba na sio kulingana na tafsiri ya kawaida ya kamusi. Hata hivyo, ili kuweza kupata suluhisho, mahakama itaangalia ushahidi uliopo kwenye mkataba wenyewe yaani mazingira husika ya jinsi neno lilivyotumika.

Kwenye tatizo lako, hakuna uwezekano wa mahakama kukubaliana na maana ya kawaida ya neno, kwa kuwa neno hilo limetafsiriwa wazi kwenye mkataba uliosaini.

## Duka limeibiwa, Hakuna fidia

**Duka langu limeibiwa na walinzi walikutwa na hatia mahakamani. Sijapata chochote kutokana na bidhaa zilizoibiwa. Naweza kurejesha ghrama zangu kutoka kwenye kampuni ya ulinzi?**

*30 Machi 2009*

Kitendo cha walinzi kukutwa na hatia haimaanishi mahakama inaweza kutoa amri ya wewe kulipwa fidia dhidi ya kampuni ya ulinzi kwa bidhaa ambazo zimeibiwa. Hii ni kwa sababu jukumu la mahakama ya ni kubainisha jinai ya watuhumiwa.

Hata hivyo, kuna uwezekano una mkataba na kampuni ya ulinzi. Kwa kuwa wamepatikana na hatia ya kosa linalotokana na wizi uliotokea dukani kwako ni ushahidi tosha kwamba kampuni ya ulinzi imevunja mkataba. Una sababu nzuri ya kufungua mashtaka dhidi ya kampuni ya ulinzi kwa thamani ya bidhaa zilizoibiwa dukani kwako na gharama za usumbufu kwa kuvunja mkataba. Kutegemeana na kiasi husika, unaweza kufikiria kuishtaki kampuni yako ya ulinzi.

## Mkataba haupo kwenye Karatasi ya Kisheria

**Hivi karibuni nilitakiwa kusaini kwenye kila ukurasa wa mkataba. Je, sheria inanilazimisha kufanya hivyo? Nilibaini kuwa aliyetengeneza mkataba alitumia karatasi nyeupe badala ya karatasi za kawaida za kisheria. Je, hilo linaweza kubatilisha mkataba wangu?**

*2 Machi 2009*

Mkataba ni ushirikiano wa hiari kati ya watu wawili wenye uwezo wa kufanya au kuacha kufanya kitendo kwa malipo halali. Mkataba unaweza kuwa wa mdomo au wa maandishi na wahusika kwenye mkataba wa maandishi wanafungwa na maneno yaliyokuwa kwenye mkataba huo hivyo pale panatokea mgogoro, kuhusu kanuni na masharti ya mkataba, marejeo yatakuwa kwenye makubaliano na sio kwenye mambo mengine yaliyo nje ya mkataba.

Umeombwa kusaini kila ukurasa wa mkataba. Hakuna sheria inayokulazimisha wewe kufanya hivyo. Ni tahadhari tu ya muandaaji wa mkataba ili kuepukana na vitendo vya kughushi baadaye. Mara nyingi wahusika wasiyo waaminifu kwenye mkataba hubadilisha kurasa, ili kukidhi mahitaji yao, na kusababisha mivutano ya kisheria. Kusaini katika kila kurasa hupunguza uwezekano wa ukurasa kubadilishwa kinyume na sheria kwa siku zijazo na ni utaratibu wa kawaida.

Kuhusu matumizi ya karatasi nyeupe, hili ni suala la kitaalamu zaidi. Pia ni rahisi kuweza kutambua vitendo vya kughushi au udanganyifu kwenye karatasi ya kisheria kuliko kwenye karatasi za kawaida na ndiyo maana hutumika.

## Saini Mkataba au nenda Jela

**Mwanangu alikuwa akifanya kazi kwenye kampuni kubwa ya nje iliyopo nchini Tanzania. Mmoja wa wasaidizi wake alihusika katika kuiba mali za kampuni na mwanangu alihojiwa na polisi. Polisi waliendelea kumsumbua mwanangu. Nilimfuata mwajiri ambaye alinitishia kuwa mwanangu atafungwa, labda kama nitasaini mkataba wa kukubali kulipa. Natokea kwenye familia maskini na pia baada ya kutishiwa kuumizwa sikusoma mkataba na nikasaini, ili mradi niweze kuondoka kwenye eneo la mwajiri. Sina pesa za kulipa na mwajiri anataka kunipeleka mahakamani. Unanishauri nini?**

*16 Februari 2009*

Mkataba ni makubaliano ya kisheria na yanahusisha kutoa na kukubali ahadi kwa kila upande. Kuna masharti mengine ya mkataba lazima yazingatiwe ili makubalinao yaweze kukubalika kisheria. Lazima kuwe na malipo halali (labda kama mkataba huo ni wa hati rasmi ya makubaliano), wahusika wawe na nia ya kutengeneza mahusiano ya kisheria, wahusika lazima wawe na uwezo wa kuingia kwenye mkataba, mkataba lazima uzingatie masharti ya kisheria na lazima wakati wa

kuingia pande zote husika ziwe huru. Mkataba lazima uwe wa kisheria, mtu hawezi kuingia kwenye mkataba wa kuuza au kusafirisha, kwa mfano, madawa ya kulevya, vinginevyo mkataba utakuwa batili.

Kutokana na maelezo mafupi uliyotueleza, inaonyesha uliwekwa chini ya shinikizo ili usaini mkataba. Shinikizo humaanisha msukumo, hasa kuhusu tishio kuumiza mwili, linalowekwa kwa mtu, kufanya jambo kwa namna fulani. Shinikizo huhusisha vurugu au vitisho vya kufanyiwa vurugu kwenda kwa malamikaji au mtu yeyote wa familia yake. Vitisho hivyo sio lazima iwe sababu pekee ya kuingia mkataba. Inajitosheleza kusema kuwa vitisho ndiyo sababu iliyokushawishi kuingia kwenye mkataba.

Mikataba iliyoingiwa chini ya shinikizo inaweza ikaepukika na kuwekwa pembeni, kwa chaguo la muathirika. Una kesi nzuri kupinga uhalali wa mkataba na tunakushauri uwasiliane na wakili wako.

## Kwa nini nifanye Usuluhishi?

**Niliingia mkataba na upande ambao ulishindwa kunilipa. Suala hili limepelekwa kwa msuluhishi. Kwa nini nifanye usuluhishi? Tafadhali shauri.**

*19 Januari 2009*

Kuna uwezekano mkubwa kwamba mkataba wako una kifungu cha usuluhishi ambacho kinakutaka kupeleka suala hilo kwenye usuluhishi. Usuluhishi ni uamuzi wa mgogoro unaofanywa na mtu mmoja au zaidi ambao hawahusiki kwenye huo mkataba (wasuluhishi) badala ya mahakama. Wasuluhishi huteuliwa na wahusika kwenye mgogoro kulingana na masharti ya mkataba. Msuluhishi husikiliza pande zote mbili. Kulingana na kifungu cha usuluhishi na haki katika maamuzi, tuzo iliyotolewa na msuluhishi inaweza kupingwa mahakamani. Hujatueleza kama mkataba ulioingia una kipengele cha usuluhishi. Kama kipo unatakiwa kwenda kwenye usuluhishi kwa sababu ni sheria, kwa kuwa wahusika kwenye mkataba wenye kifungu cha usuluhishi hawawezi kwenda moja kwa moja mahakamani. Kama hakuna kifungu hicho, huna sababu ya kwenda kwenye usuluhishi na unaweza kwenda kufungua shauri mahakamani.

## Shauri lililo Nje ya Muda

**Mwaka 2001, niliingia kwenye mkataba na kampuni iliyopo Dar kusambaza bidhaa fulani, na kuzikabidhi mwishoni mwa mwaka huo. Hata hivyo, kampuni haikuheshimu mkataba. Nifanyeje ili kuweza kuokoa au kupata fedha yangu.**

*12 Januari 2009*

Kila tatizo lina ukomo wa muda wa kushtaki, kufungua mashtaka chini ya mkataba ni miaka 6 tangu tarehe ya tatizo lilipotokea. Kwa mantiki hii, uko nje ya muda. Hata hivyo, huu sio mwisho wa kufungua shauri ili uweze kupata haki yako. Unayo nafasi ya kupeleka maombi kwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kushtaki nje ya muda ukieleza sababu za kuchelewa na ukieleza nini unadai dhidi ya upande mwingine. Waziri baada ya kushauriana na Mwanasheria Mkuu anaweza kutoa amri ya kuongeza muda. Hii inapatikana chini ya kifungu cha 44(1) ya Sheria ya Ukomo wa Mashtaka, (Sura ya 89 Marejeo ya Mwaka 2002). Baadhi ya sababu ambazo hukubalika ili kuruhusu kufunguaa mashtaka nje ya muda ni ugonjwa, kupotea kwa nyaraka, kuwa gerezani na kutokuwa na uwezo wa kufungua shauri kwa sababu ulisafiri nje ya nchi. Kwenye tatizo lako, hauko wazi kwa kiasi kikubwa ni nini kilisababisha uchelewe kufungua shauri lako. Kama sababu zako zitakubaliwa, utapewa ruhusa ya kushtaki nje ya muda na unaweza kuendelea kufungua kesi mahakamani kwa uvunjaji wa mkataba.

## Kuvunjwa kwa Mkataba

**Niliingia mkataba na kampuni kwa ajili ya kusambaza bidhaa fulani na wakati nakabidhiwa baadhi ya hizo bidhaa, ubora wake haukuwa ule uliokubaliwa. Wameshindwa kuleta bidhaa zingine zilizobaki na wamekuwa wakinikwepa. Nifanyeje?**

*5 Januari 2009*

Muuzaji hajatimiza, kulingana na kanuni na masharti ya mkataba, kufikisha kile kilichokubaliwa kimkataba. Hatimaye, suluhisho la kurejeshwa pale ulipokuwa ni sahihi pale upande mmoja umetimiza wajibu wake kwenye mkataba lakini hajapata kile kilichokubaliwa kutoka upande mwingine. Unatakiwa utambue kuwa, suluhisho la msingi la uvunjaji mkataba ni fidia. Hili hutekelezwa kwa kuzingatia kuwa ingawa muathirika wa uvunjaji mkataba anaweza kuomba utekelezwaji wa mkataba au amri ya zuio, amri hizo ni za kisheria hivyo hutolewa kwa busara ya mahakama. Kwenye tatizo lako, maelezo ni machache sana. Hatuna uhakika ni kwa asilimia ngapi ya kiasi mlichokubaliana umelipwa, iwapo mkataba ulikuwa na uwazi wa kutosha kuhusu ubora na kwamba hakuna utata na sababu zipi za kuendelea kuchelewa. Tunashauri uwasiliane na wakili wako haraka.

## Kuagiza Mzigo kwa mara ya Kwanza

**Nataka kusafirisha bidhaa kwa njia ya bahari kutoka kwa muuzaji aliyepo Mashariki ya Mbali. Wamenipa mikataba ya aina mbili - FOB na CIF. Je, hii inamaanisha nini? Je, nitahakikisha vipi mizigo inafika Tanzania baada ya kufanya malipo? Muuzaji anataka malipo awali kwa 100%.**

*12 Januari 2009*

Maneno yaliyotajwa kwenye swali lako ni mikataba ya kawaida kwa ajili ya kuuza bidhaa kimataifa. Kwenye mkataba wa FOB, muuzaji huhakikisha sio tu kupeleka bidhaa kwenye meli bali kuona kuwa inapakiwa kwenye meli. Wajibu wa muuzaji unaendelea hadi kwenye gharama zote zilizotumika kabla ya usafirishaji, ikiwemo malipo ya upakiaji, ukiondoa usafirishaji na bima. Wewe kama mnunuzi utawajibika kulipia usafirshaji na bima. Kama hakuna makubaliano tofauti, mnunuzi ana haki na wajibu wa kuchagua bandari na tarehe, na kwa ujumla kufanya mipango kwa ajili ya, usafirishaji wa bidhaa. Mara baada ya bidhaa kufikishwa na kushushwa salama, muuzaji atakuwa amefikisha kwa mnunuzi na jukumu la hasara linahamia kwa mnunuzi. Ukiamua kutumia mkataba wa FOB, tungependa kukushauri kuzikatia bima bidhaa zako na kampuni ya bima iliyopo nchini. CIF husimama kwa ajili ya Gharama, Bima na Usafirishaji. Kwenye mikataba ya CIF, muuzaji si tu anakubali kuuza bidhaa bali pia kuingia mkataba wa usafirishaji (kulipia usafirishaji) ambao utahakikisha bidhaa zinafikishwa kwenye bandari iliyokusudiwa na mnunuzi, ili kulinda hasara zinazoweza kujitokeza wakati mizigo ikiwa safarini. Muuzaji atakuwa ametimiza wajibu wake kwenye mkataba pale atakapokabidhi nyaraka husika kwa mnunuzi, ankara zinazobainisha bidhaa na gharama zake, hati ya shehena kama ushahidi wa mkataba wa usafirishaji, bima na nyaraka zingine, kama ilivyoelezwa kwenye mkataba.

Tukija kwenye swali lako la pili, tungependa kukushauri, usilipe 100% kabla, au malipo yoyote ya awali. Utaratibu wa kawaida ni kwa wewe kupata barua ya dhamana kutoka kwenye benki yako. Hii ni nyaraka ambayo benki yako itawajibika kulipa fedha kwa muuzaji kupitia benki iliyochaguliwa na muuzaji wakati wa uwasilishaji wa nyaraka zilizoainishwa kwenye barua. Kwa mfano, kama mkataba wako ni CIF, basi benki yako itailipa benki ya muuzaji pale tu itakapopokea nyaraka za shehena na bima ikiwa na ankara.

# Mambo Yahusuyo Wanasheria, Taratibu za Mahakama na Maadili

“ **Wanasheria wanaweza wasikubali lakini ukweli ni kwamba haki ni zaidi ya maamuzi ya mahakama.**

Huna hatia mpaka ithibitishwe vinginevyo! Una hatia au la, kila mtu anastahili usawa na haki wakati wa kusikilizwa shauri lake . Sura hii inajibu maswali kuhusu masuala ya kimahakama, ukamataji haramu, wito/samansi, uendeshaji wa mashauri mahakamani, kutoa ushahidi, kuwasilisha utetezi, ukataji wa rufaa, kuita mashahidi na taratibu zinazohusiana na mahakama. Pia inajibu maswali kuhusu mahakama mbalimbali na udhibiti wa gharama zako za kisheria, ingawa sio mada itakayowavutia wanasheria! Njia sahihi ni kuyakwepa matatizo ili ukae mbali na mahakama.

## Tuzo kwa ajili ya Gharama ni Ndogo sana

**Mimi ni mfanyabiashara wa Tanzania na mkazi wa Sumbawanga. Mwaka 2009, nilifanikiwa kutetea mashtaka ambayo mteja wangu alifungua dhidi yangu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa madai ya uvunjaji wa mkataba. Nimekatishwa tamaa na kiasi kidogo cha gharama nilichopewa na Mahakama ukilinganisha na kiasi nilichotumia kuteteta shitaka hilo, ikijumuisha gharama za usafiri, teksi, chakula, takrima na malazi kwa mashahidi wangu. Nahisi kwamba mahakama haijatenda haki kwangu. Nifanye nini?**

*25 Aprili 2011*

Kodi ya mahakama (taxation) ni neno la kisheria linalotokana na mchakato wa mahakama kutathmini gharama ambazo upande ulioshinda kesi uliingia wakati wa kusimamia shauri hilo. Mtoza ushuru wa mahakama, ambaye kwa kawaida huwa Msajili, Naibu Msajili, au Hakimu Mfawidhi kwa mahakama za chini, ni Afisa wa Mahakama anayehusika na kutoza kodi hii. Mchakato huanza na upande wa mashtaka ulioshinda, kuwasilisha orodha ya gharama mahakamani, ambazo kwa kawaida hujulikana kama hati ya gharama. Hii inahusu kiasi ambacho mtu alitumia wakati wa kuendesha na anatakiwa kuwasilisha ndani ya siku sitini tangu tarehe ya hukumu. Gharama muhimu ndizo huzingatiwa na mahakama.

Gharama zilizotumika kukirimu wanasheria au mashahidi wako hazikubaliwi. Madai ya gharama lazima yathibitishwe na risiti na vocha kwa malipo yote, pamoja na nyaraka, rasimu, au nakala, na lazima ziwe na uhalisia. Uhalisia hutegema busara za kisheria za mtoza ushuru wa mahakama, ambaye huangalia ukweli wa mambo, ugumu, umuhimu kwa umma na mazingira mengine ya kesi na kuamua juu ya kiasi gani kuhusu madai ya gharama yalipwe. Kama mtoza ushuru wa mahakama alikosea kanuni hizi, upande usioridhishwa unaweza kupeleka suala hilo kwa Jaji wa Makakama Kuu. Uamuzi wa mtoza ushuru wa mahakama juu ya kiasi kinachotakiwa kulipwa ni wa mwisho. Kuhusu swali lako, hatuko kwenye nafasi ya kupingana na maamuzi ya mtoza ushuru wa mahakama, kwa kuwa hatuna taarifa za kutosha. Hatuna maelezo ya madai ya gharama uliyopeleka mahakamani, hatuna pia nakala ya maamuzi ya Mtoza Ushuru wa Mahakama. Hata hivyo, kama unadhani mtoza ushuru wa mahakama alikosea kwenye tathmini ya gharama, tunakushauri kupeleka suala hilo kwa Jaji.

Marejeo kwa Jaji hufanywa kwa “maombi maalum” yakiambatana na kiapo, yafanyike ndani ya siku ishirini na moja (21) baada ya nakala iliyothibitishwa ya maamuzi ya Mtoza Ushuru kutolewa. Pale ambapo tarehe ya mwisho imepita, unaweza kupeleka maombi kwa ajili ya kuongezewa muda ukionyesha sababu za msingi za kuchelewa.

## Kujitetea mwenyewe Mahakamani

**Nimeshtakiwa kwa kosa la wizi na nataka kujitetea mwenyewe. Inaruhusiwa? Unanishauri nifanye nini? Vitabu vyovyote ninavyoweza kusoma?**

*28 Februari 2011*

Kwenye sheria kuna kanuni za asili ambazo ni za msingi na takatifu ambazo lazima zizingatiwe. Mojawapo ni haki ya kusikilizwa. Hii ina maana kwamba yeyote aliyeshtakiwa na kosa lolote ana haki ya kujitetea. Utaratibu ni kama ufuatao: wakati wa kukamatwa ni lazima utaarifiwe haki yako ya kuwa na wakili, haki ya kukaa kimya, na kwa haraka kupelekwa kituo cha polisi. Mara unapofikishwa mahakamani, hati ya mashtaka itasomwa dhidi yako, utatakiwa kukiri hatia au la.

Wizi ni kosa lenye dhamana na dahamana

itakuwa wazi tu kama utatimiza masharti ya dhamana. Kuna uwezekano ukakataa kosa. Baada ya kukataa, maelezo ya wali yatasomwa ambapo upande wa mashtaka utataja orodha ya mashahidi na wewe utatakiwa kutoa orodha yako. Baada ya hapo shauri litaanza kusikilizwa, ambapo upande wa mashtaka utaleta mashahidi wake na unaweza kuwauliza maswali. Unahitaji kukabiliana na ushuhuda wa mashahidi ili kukanusha tuhuma dhidi yako.

Haya yote yanaweza kuonekana kama ya kuvutia kwa jinsi tunavyoandika, ila kumbuka kuwa taratibu za kimahakama zinaweza kuwa za kiufundi zaidi na tunakushauri kumwajiri wakili kukuwakilisha.

Baadhi ya watu maarufu, akiwemo Rais wa zamani wa Liberia, Bw. Charles Taylor na Rais wa zamani wa Yugoslavia, Bw. Slobodan Milosevic, walijitetea wenyewe waliposhtakiwa. Kwa vidokezo zaidi, tunapendekeza ukasome kitabu cha Jaji maarufu mstaafu B.D. Chipeta (marehemu kwa sasa) kinachoitwa "Kitabu kwa ajili ya Waendesha Mashtaka wa Serikali".

## Kosa la Uendeshaji na Jela

**Nilihusika katika ajali ya barabarani na sasa niko kwenye hatari ya kufungwa. Kosa langu ni kusababisha madhara kwa uendeshaji mbaya. Daima nilidhani makosa ya barabarani hutatuliwa kwa kulipa faini. Nifanye nini?**

*4 Aprili 2011*

Uendeshaji hatarishi wa gari ni moja ya makosa makubwa chini ya Sheria ya Usalama Barabarani. Ili kuthibitisha kosa hili, vipengele vifuatavyo lazima viwepo: (1) mtuhumiwa alikuwa anaendesha gari, (2) uendeshaji ulikuwa ni hatarishi au wa kizembe hivyo kusababisha majeruhi au kifo. Makosa mengi ya barabarani hutatuliwa kwa kulipa faini. Hata hivyo, kwa mtazamo wa uzito wa kosa hili, na kwa maslahi ya umma, ni kweli kwamba ukikutwa na hatia unaweza kufungwa. Hutoweza kukataa kwamba hukuendesha gari, ila iwapo ulikuwa unaendesha kwa mwendo hatarishi au la ni jambo la kidhahania na hutegemea na mazingira ya kila kesi. Mtafute wakili wako kwa msaada zaidi.

## Mabadiliko ya hati ya Mashtaka wakati wa Kesi

**Miaka miwili iliyopita mjomba wangu alishtakiwa kwa kujeruhi kinyume na sheria. Alikana mashtaka na waendesha mashtaka walileta mashahidi watatu. Cha kushangaza wakati shahidi wa tatu wa upande wa mashtaka amekuja, upande wa mashtaka walibadilisha hati ya mashtaka na kuweka kosa la kusababisha madhara makubwa ya mwili, na baada ya kusikilizwa kwa utetezi, alikutwa na hatia na kuhukumiwa kwenda jela miaka 3. Je, ilikuwa ni sahihi kubadilisha hati ya mashtaka?.**

*11 Aprili 2011*

Ubadilishwaji wa hati ya mashtaka husimamiwa na kifungu cha 234 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai ambacho kinaeleza kuwa upande wa mashtaka unaweza kurekebisha na/au kubadilisha hati ya mashtaka katika hatua yeyote ya kesi kwa sababu mbalimbali kama vile ubovu wa hati ya mashtaka kwenye kiini au muundo. Hata hivyo, baada ya mabadiliko, mtuhumiwa ana haki ya kukiri upya mabadiliko ya hati ya mashtaka. Mahakama inatakiwa kumfahamisha haki yake ya kuwaita upya mashahidi kuja kutoa ushahidi upya au kuhojiwa zaidi. Utaratibu wote huu lazima uonekane kwenye mwenendo wa mashtaka.

Upungufu wowote wa taratibu hizi husababisha makosa makubwa yanayoweza kisheria kuharibu maamuzi yatayofikiwa mwisho wa kesi. Kwa kuwa maelezo yako yapo kimya, iwapo taratibu hizi zlifuatwa au la, tuanakushauri wasiliana na wakili wako ukiwa

na mwenendo wa mashtaka kwa ushauri zaidi. Iwapo ilikuwa ni haki kubadilisha hati ya mastaka ni suala la dhahania. Kwenye macho ya mtuhumiwa inaweza kuonekana kuwa sio haki, na kwenye macho ya upande wa mashtaka inaweza kuwa ni haki. Hata hivyo, sheria inaeleza wazi kuwa upande wa mashtaka unaweza kubadilisha hati ya mashtaka.

## Madai baada ya Muda wa Ukomo kupita.

**Mwaka 1999, niliingia kwenye mkataba na rafiki yangu wa kulipa Milioni 50 ambazo zilitokana na biashara. Hata hivyo, kutokana na matatizo yangu ya kifedha, sikuweza kulipa kama ilivyoahidiwa. Miezi michache iliyopita nilipokea notisi ya madai ya siku 14 kutoka kwa mwanasheria wa rafiki yangu akidai kiasi hicho na gharama nyingine zinazohusiana. Nimejibu notisi ya madai na nimekubali deni, lakini mdai ana shauku ya kwenda mahakamani mara moja baada ya hizo siku 14 bila taarifa ya ziada. Tafadhali nishauri.**

*11 Aprili 2011*

Hakuna shaka kuwa uhusiano wako na rafiki yako uliratibiwa na mkataba wa maandishi wa mwaka 1999. Hata hivyo, kisheria, ukomo wa muda wa kufungua mashtaka inayohusu mikataba ya maandishi ni miaka sita. Kwenye tatizo lako, kuna tarehe mbili tofauti - tarehe ya mkataba wako wa mwaka 1999 na tarehe ya kukubali deni la mwaka 1999 ambalo umesema ni miezi michache iliyopita. Kwa mujibu wa Sheria ya Ukomo wa Mashtaka, huwezi kutekeleza deni lililokubaliwa baada ya muda wa ukomo.

Chini ya Sheria ya Ukomo wa Mashtaka, rafiki hawezi kuwa na madai dhidi yako kama yalifanyika zaidi ya miaka 6 tangu siku ulipovunja mkataba. Kwenye mazingira maalum waziri anyehusika na sheria anaweza kuongeza muda wa ziada wa miaka mitatu, ambao unaweza kusogeza muda wa ukomo hadi 2008. Baada ya 2008, rafiki yako hawezi kuwa na madai dhidi yako, hata kama ulilikubali deni hilo upya. Ingawa unaweza kuwa na wajibu wa kiamaadili wa kulipa, kisheria una utetezi mzuri pale utakapoamua kutokulipa. Hata hivyo, tunapendekeza uonane na wakili wako kwa ajili ya ushauri zaidi na mwongozo.

## Mahakama na Ushahidi wa Kielektroniki

**Katika benki ninapofanya kazi, katika hali isiyo ya kawaida, kuna mkopo ulitolewa ambapo nyaraka zote zilifanyika kwa njia ya barua pepe. Kwa kuwa mkopeshwaji alikuwa ni rafiki wa karibu wa Meneja, pia aliweza kupewa mkopo wa kiasi kikubwa zaidi kinyume na utaratibu. Mkopo huo haukuwa na dhamana, na mkopaji amegoma kulipa. Timu yetu ya wanasheria inasema hatuna kesi, kwa maana ya kwamba mahakama haitakubali ushahidi wa kielektroniki kwa kuwa itakuwa vigumu kuthibitisha deni husika. Je, hii ni kweli?**

*4 Aprili 2011*

Katika hali ya kawaida timu yenu ya kisheria ipo sahihi. Lakini kimantiki wanachosema kisheria hakiendani na uhalisia kwani mkopo ulifanyika na mkopeshwaji alipatiwa fedha husika. Kwa mujibu wa swali lako, tunaona kwamba inawezekana kuthibitisha hilo, na mkopeshwaji alikuwa akiwasiliana kwa barua pepe na meneja mikopo. Kwa nini basi mahakama isiweze kuunga mkono kesi yako? Kanuni kuu ni kwamba mdai anapaswa athibitishe madai yake.

Sheria ya Ushahidi ni ya zamani sana na haitoi fursa kwa ushahidi wa kielektroniki kwani ilipitishwa kwa mujibu wa mfumo wa Sheria za Makwabwela za Uingereza. Kanuni ya Ushahidi Bora inasema kwamba

nyaraka halisi pekee ndizo zinazokubalika mahakamani. Hauna nyaraka halisi – je, unapaswa kufanya nini? Katika shauri la kukumbukwa, Mahakama Kuu katika Kitengo cha Biashara imewahi kuruhusu ushahidi wa kielektroniki. Suala kuu mbele ya mahakama ilikuwa endapo ushahidi wa kielektroniki uliochapishwa kutoka katika kompyuta unakubalika chini ya Sheria ya Ushahidi. Jaji aliamua kuwa mahakama zinapaswa kuyakubali na kuyaelewa mapinduzi ya kiteknolojia ambayo yameikumba dunia. Kwa kumalizia, Jaji aliongeza kuwa sheria haiwezi kufumba macho yake kwa kinachotokea kote ulimwenguni na katika sekta ya kibenki. Ingawa ushahidi wa kielekroniki uliruhusiwa katika kesi tajwa hapo juu, kuna kesi nyingine nyingi ambapo mahakama hazikuruhusu ushahidi wa kielektroniki. Pamoja na kwamba jambo hili linaonekana kuangaliwa kiurahisi na mahakama, ukweli ni kwamba maelezo ya kesi husika ndiyo yatakayoamua kukubaliwa ama la kwa ushahidi wa kielektroniki. Kwa muktadha wa suala lako, kwa maana ya benki, kwa kiasi fulani inatoa picha ya namna ambavyo uhifadhi wa kumbukumbu katika mabenki kwa kiasi kikubwa ni wa kizamani.

Benki yako haina chaguo zaidi ya kufungua shauri na kupinga hoja za upande wa utetezi kwa kutumia kilichoamuliwa na mahakama hapo juu. Jambo la kujifunza kwako na kwa wadau wengine wa mabenki ni kwa njia mbili kama ifuatavyo; kujikosoa na kujitathmini kwa mameneja wakuu na kuhakikisha kwamba wanafuata miongozo katika kutoa mikopo (ni lazima ieleweke kwamba baadhi ya mabenki nchini Tanzania bado hayana miongozo sahihi) na pili, kila kitu ambacho benki inafanya lazima kiwekwe kumbukumbu na kisainiwe. Barua pepe ni rahisi, lakini zinaweza kuleta hasara kubwa.

## Kudharau Mahakama

**Niliitwa kama shahidi katika kesi ambayo wakati nikihojiwa ilikuwa dhahiri kabisa kwamba Jaji alikuwa upande wa mwanasheria wa mdai. Sikujisikia vizuri kabisa, na ilifikia hatua ambapo sikuweza kuvumilia tena na nilifanya fujo kidogo katika mahakama. Jaji alinikuta na hatia ya kutoheshimu mahakama na amepanga tarehe ya kunihukumu. Je, hii ni ya kawaida?**

*14 Machi 2011*

Kudharau mahakama kunafafanuliwa kama kutotii amri au utaratibu wa Mahakama, kama vile ukiukaji wa maagizo. Kwa mfano, kama zuio likipelekwa kwa mshtakiwa kwa pamoja na taarifa ya adhabu, kukiuka kunaweza kusababisha mshtakiwa kufungwa. Mifano mingine ya dharau kwa mahakama ni pamoja na kuingilia kwa makusudi maamuzi ya kimahakama, matumizi ya lugha za vitisho na kufanya fujo mahakamani na kutuhumu bila uthibitisho mamlaka na uadilifu wa mahakama. Pia kuna taarifa za watu waliopelekwa jela kwa simu zao kuita ndani ya mahakama. Dhana ya jumla ni kwamba majaji wanapaswa kutumia utashi wao kwa uangalifu sana. Kwa upande wako hatujui jinsi mwenendo wa hasira zako ulivyokuwa mahakamani. Fahamu kwamba kudharau mahakama inaweza kupelekea kifungo hadi cha miezi sita jela. Tunashauri uwasiliane na mwanasheria wako kwa mwongozo zaidi.

## Kukiri Hatia

**Nilikamatwa kwa kosa ambalo mwendesha mashtaka wa Serikali na Hakimu waliniambia kabla ya kesi kuanza, kwamba nikiri kosa na suala litaishia kwa mimi kulipa faini tu. Ilionekana kama njia sahihi na ya haraka na nilifanya kama nilivyoshauriwa. Kwa mshangao mkubwa nilipewa hukumu ya mwezi mmoja jela. Je, Hakimu na Mwendesha Mashtaka wanaweza kunidanganya kama hivyo?**

*14 Machi 2011*

Tunaanza kwa kusema kwamba si

Mwendesha Mashtaka wala Hakimu anayeruhusiwa kukuongoza katika masuala hayo. Hawapo upande wako, kwa hiyo mwongozo huo hautakiwi na pia sio halali. Kwa bahati mbaya hujatuambia kosa lilikuwa lipi, lakini makosa mengi yana nafasi ya faini au hukumu ya jela, na kanuni kuu ni kwamba faini inapaswa kuanza. Hadi kufikia tumejibu swali lako (kwa sababu ya maswali mengi tuliyonayo), tunaamini utakuwa umeshatoka jela. Tunakuhurumia lakini tunakukumbusha umuhimu wa kuwa na uwakilishi sahihi wa kisheria unapokuwa mahakamani.

## Polisi wa Usalama Barabarani kuomba Lifti

**Nilisimamishwa na afisa wa polisi wa usalama barabarani na kuniomba lifti. Kutokana na ugeni wangu, na kutojua mambo yanavyoenda hapa, nilikataa. Afisa huyo alimpigia afisa mwenzake katika kituo kinachofuata ambaye pia alinisimamisha. Nilipelekwa kituoni na kuhojiwa. Je, ni lazima kwa dereva kutoa lifti kwa polisi wa usalama wa barabarani?**

*28 Februari 2011*

Hatuna ufahamu na sheria yoyote ambayo inalazimisha kumbeba afisa wa polisi wa usalama barabarani. Kupelekwa kwenye kituo cha polisi kwa kutombeba afisa wa polisi ni matumizi mabaya ya madaraka na unaweza kuripoti hii kwa mkuu wa polisi wa wa usalama barabarani jijini Dar es Salaam. Hakikisha malalamiko yako ni ya maandishi na yamepolekewa. Kwa kuwa hautarajii barua yako ipotee, unapaswa ufuatilie na kudai majibu kwa maandishi. Tunaamini unafahamu namba za vitambulisho vya maafisa wa polisi husika.

## Mtoto kasababisha Moto

**Tunaishi kilomita 55 kutoka Mbeya Kusini mwa Tanzania, ambapo hali ya hewa ni baridi sana. Mtoto wetu mwenye umri wa miaka 9 alikuwa msituni. Katika hali ya kujipatia joto, aliwasha moto. Kwa bahati mbaya na bila kujua, aliwasha moto juu ya nyasi ngumu na kavu, na moto ukamzidi udhibiti na kuteketeza nyumba ndogo ya familia. Wakati wa moto, hapakuwa na mtu aliyepo kwenye nyumba hiyo. Suala hilo liliripotiwa polisi na mtoto wangu alipelekwa mahakamani. Mahakama iliamuru nimlipe fidia mmiliki wa kibanda kwa kiasi fulani. Je, hii ni haki? Sina uwezo wa kulipa fidia hiyo. Nifanye nini?**

*14 Februari 2011*

Sheria ya Kanuni za Adhabu inasema kwamba mtu aliye chini ya umri wa miaka 7 hawezi kutenda kosa la jinai, na kwamba mtu aliye chini ya umri wa miaka 12 hawajibiki kwa makosa ya jinai isipokuwa wakati wa kitendo husika, awe na uwezo wa kujua kwamba hakupaswa kufanya kitendo hicho. Ni jukumu la upande wa mashtaka kuthibitisha kuwa mtoto wako alikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu moto huo.

Mtoto akikutwa na hatia, na mahakama ikiwa na maoni kwamba kesi itakuwa bora zaidi kuisha kwa kulipa faini, kwa maslahi ya mtoto, sheria inaruhusu mzazi kulipa faini. Hata hivyo, mzazi ambaye amri hiyo inaelekezwa kwake anapaswa kupewa fursa ya kusikilizwa. Inaonekana kama haukupata nafasi hiyo na unaweza kukata rufaa.

## Rufaa kuanza baada ya Hukumu ya Jela

**Mwaka 2007, kaka yangu ambaye alikuwa mwajiriwa wa shirika fulani la umma alishtakiwa kwa kuiba fedha kutoka kwa mwajiri wake. Alishtakiwa, akakutwa na hatia na akahukumiwa kwenda jela kwa kipindi cha miaka mitatu. Licha ya kuwa na hatia na kuhukumiwa, Jamhuri ilikata rufaa Mahakama Kuu ili kupinga uamuzi wa Mahakama ya Wilaya, ikisema kuwa hukumu ya miaka mitatu jela ilikuwa ndogo sana. Hii ilitushtua sana. Mnamo Mei 2009,**

**ndugu yangu alikamilisha kifungo chake cha gerezani na akaachiliwa kutoka jela. Sasa ameletewa wito wa mahakama kumtaka kuhudhuria rufaa dhidi yake. Je, rufaa ya Jamhuri inaruhusiwa kisheria? Je, kwa kiasi gani rufaa hiyo itafanikiwa? Je, rufaa ni halali, hasa kuzingatia ukweli kwamba tayari ametumikia adhabu yake na kufunguliwa kutoka jela? Nini kitatokea endapo rufaa dhidi yake itafanikiwa? Tafadhali shauri, kwani wote huku tumechanganyikiwa.**

*24 Januari 2011*

Kiukweli jambo hili linachanganya. Inaonekana wazi kabisa kwamba Jamhuri haikuridhishwa na ukali wa hukumu ya miaka mitatu iliyotolewa kwa ndugu yako. Jamhuri inataka kuona hukumu inaongezwa, kitu ambacho kinaruhusiwa. Ni kama ambavyo kaka yako angeona adhabu hiyo ni kali pia angekata rufaa. Kwa kuzingatia kwamba kaka yako alishtakiwa kuiba mali ya shirika la umma, ambalo ni mamlaka maalum, chini ya Sheria ya Kiwango cha Chini cha Adhabu, adhabu sahihi kwa ajili ya kosa hilo ilipaswa kuwa kifungo cha miaka mitano na sio miaka mitatu. Huu ndio ukweli mchungu ambao unapaswa kuufahamu.

Kwa kuwa mahakama ilitoa adhabu ndogo, ambayo haiendani na masharti ya kisheria, Mahakama Kuu haitaweza kuwa na njia nyingine ya kuzuia mchakato wa kisheria kama unavyotakiwa kufanyika, na inaweza kutoa hukumu stahiki, hata kama hii itasababisha matokeo mabaya kwa kaka yako.

Kama kaka yako alitumikia adhabu yake tayari, muda wa adhabu hiyo utazingatiwa katika hesabu sahihi ya kifungo kipya. Labda kama kuna mambo mengine ambayo hukutuambia, katika hali ilivyo uwezekano wa rufaa kufanikiwa ni mkubwa sana na kaka yako atatumikia miaka mingine miwili jela.

## Ulinzi kwa Mashahidi Mahakamani

**Mnamo Novemba 2009, mke wangu alisimama mbele ya Mahakama ya Wilaya ambako alitoa ushahidi kwa niaba ya mtuhumiwa katika kesi inayomhusu jirani yangu, ambaye alishtakiwa kwa kosa la kushambulia mke wa mfanyabiashara tajiri, ambaye pia ni jirani yetu. Wakati wa kuhoji, Mwendesha Mashtaka wa Serikali alimchanganya mke wangu kwa maswali magumu na mwishowe akamtuhumu kuwa mwongo na aliyesaidia kosa hilo. Mke wangu sasa amekimbia kutoka nyumbani kwetu, akiogopa kuwa atakamatwa kwa ushahidi aliotoa. Je, kuna uwezekano wowote kwamba atashtakiwa? Tafadhali shauri.**

*24 Januari 2011*

Hatufahamu kuhusu maswali aliyohojiwa mke wako na jinsi alivyojibu maswali hayo. Kwa maelezo machache uliyotupatia, hatuamini kama kuna chochote mke wako anahitaji kuwa na wasiwasi nacho. Kanuni kuu ya sheria ni kwamba shahidi katika mahakama hawezi kukamatwa au kushtakiwa kwa sababu ya ushahidi wowote wa kibinafsi unaotolewa, wala ushahidi huo hauwezi kutumiwa kama ushahidi dhidi ya shahidi katika kesi yoyote inayofuata. Sheria inatoa kinga kwa mashahidi kuondokana na kushtakiwa kwa misingi ya ushahidi wanaoutoa katika mahakama, isipokuwa kama kwa makusudi wametoa ushahidi wa uongo, ambao sio jambo tunaloliona hapa. Kama hakuna sababu nyingine zilizopelekea mke wako kuondoka, tuna hakika anaweza kurudi bila kukamatwa.

## Kuita Mashahidi wakati wa Rufaa

**Mnamo mwaka wa 2000, watatu kati yetu tulishtakiwa katika Mahakama ya Wilaya kwa makosa mawili: kuiba kama mtumishi wa umma na kuwa na silaha kinyume na sheria. Baada ya kesi kusikilizwa mahakama ilinikuta sina kesi ya kujibu. Watuhumiwa wenzangu walikutwa na hatia. Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai alikata rufaa Mahakama Kuu, na Jaji aliwaita**

**tena mashahidi watatu na akaita shahidi mmoja mpya kutoa ushahidi dhidi yangu. Mahakama Kuu ilitengua uamuzi wa kuniachia na kusema nina kesi ya kujibu na kuamuru niunganishwe na watuhumiwa wenzangu kwa ajili ya utetezi kwenye mahakama inayosikiliza kesi. Je, Jaji alikuwa sawa na alitenda haki kusikiliza ushahidi mpya? Tafadhali nishauri.**

*24 Januari 2011*

Chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, sheria inaruhusu Mahakama Kuu kumuita mtu yeyote au kumuita tena shahidi yeyote ikiwa ushahidi wao unaonekana kuwa muhimu kwa uamuzi sahihi wa kesi husika. Mahakama Kuu pia ina mamlaka, wakati wa kupitia rufaa kutoka mahakama za chini, kuchukua ushahidi wa ziada (ikiwa ni lazima) yenyewe au kuagiza ushahidi huo uchukuliwe katika mahakama ya chini. Hata hivyo, Mahakama Kuu lazima irekodi sababu zake za kuchukua ushahidi wa ziada na haipaswi kutumia vibaya jambo hili na kulifanya kuwa shauri jipya, kuziba mapengo kwenye kesi ya upande wa mashtaka au kubadilisha hali ya kesi dhidi ya mtuhumiwa. Ushahidi ulioongezwa na Mahakama Kuu utachukuliwa kama ni ushahidi uliochukuliwa wakati kesi mbele ya mahakama ya chini. Kwa kuwa hatuna rekodi za mahakama ili tuziangalie, ambazo zingeweza kutusaidia kukushauri iwapo kama ushahidi wa ziada ulihitajika kwa uamuzi huo au la, tunakushauri wasiliana na wakili wako kwa ushauri zaidi.

## Ada ya 3% katika Mahakama ya Biashara

**Sisi ni kampuni iliyosajiliwa nchini Afrika Kusini ambayo inasambaza mizigo kwa kampuni iliyopo Tanzania. Uhusiano wetu na mnunuzi umeingia dosari na tunatarajia kuwapeleka mahakamani. Mawakili wetu wametujulisha kuhusu ada ya kusajili shauri Mahakama ya Biashara kuwa ni asilimia 3 ya madai ya shilingi ya Kitanzania bilioni 4 na wao wanataka malipo ya kisheria kwa kiasi sawa. Je, ada hii si nyingi? Nini wastani wa muda wa kukamilisha kesi katika Mahakama ya Biashara?**

*3 Januari 2011*

Mahakama ya Biashara ni mahakama inayopendwa na jamii ya wafanyabiashara nchini Tanzania. Malipo ya Mahakama ya Biashara ni 3% kwa Shilingi za Kitanzania Milioni 200 ya kwanza, na 1% kwa kiasi kitakachozidi shilingi ya kitanzania Milioni 200. Hivyo, kwa madai ya shilingi ya kitanzania bilioni 4, ada ya mahakama itakuwa shilingi ya kitanzania Milioni 6 ukijumlisha na shilingi ya kitanzania Milioni 38 jumla yake ni shilingi ya kitanzania Milioni 44. Kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 120 mlichoambiwa, ni dhahiri kina makosa. Hatutaki kutoa maoni juu ya ada za kisheria ambazo mmeambiwa, kwani huo ni uamuzi wa kibiashara.

Kwa sasa, Mahakama ya Biashara inachukua wastani wa miezi kumi na minne hadi kumi na sita ili kukamilisha kesi. Hata hivyo, inategemea utata wa jambo hilo na ikiwa linahusisha maombi yoyote. Mahakama ya Biashara inazingatia sana suala la muda katika kuhitimisha mashauri na haikubaliani sana na mbinu za ucheleweshaji kesi za mawakili.

Pia tunapenda kuwatahadharisha kwamba kwa kuwa nyie sio taasisi iliyosajiliwa Tanzania, kuna uwezekano kwamba mdaiwa, akaomba dhamana kwa ajili ya gharama za kesi. Mtapaswa kuandaa fedha kwa ajili ya maombi hayo ili kuepusha kuchelewesha kesi ya msingi.

## Hati ya Uwakilishi – Mtoaji Amekufa

**Ndugu yangu wa karibu alitoa hati ya uwakilishi (power of attorney) kwa wakili wake kufanya kwa niaba yake mauzo ya mali yake iliyopo Shinyanga. Kwa bahati mbaya**

**ndugu yangu amekufa na inavyoonesha wakili huyo anatumia hati ya uwakilishi vibaya. Mamlaka hiyo inatumikaje? Je, mamlaka hiyo hupewa mawakili tu? Je, hati ya uwakilishi inapotolewa, inamaanisha pia kwamba mapato ya mali inayouzwa inaenda kwa mtu mwenye hati ya uwakilishi tu?**

*3 Januari 2011*

Hati ya uwakilishi (power of attorney) ni mamlaka inayotolewa na mtu mmoja kwenda kwa mwingine ili kutenda kwa niaba yake. Hati ya uwakilishi hufa na mtoaji, kwa mazingira ya hapa, ni ndugu yako. Baada ya kifo, wosia wa mtoaji huanza kutumika, na wakili hana haki na hawezi kutenda kupitia mamlaka hiyo.

Kuhusiana na mapato ya mauzo ya mali, ni muhimu kwako kusoma mamlaka hayo yameandikwaje. Hati ya uwakilishi inamuwezesha wakili kutenda kwa niaba ya mhusika (mtoaji wa hati ya uwakilishi), lakini haimaanishi kwamba wakili atabaki na kiasi kilichopatikana baada ya mauzo husika. Katika shughuli uliyotaja, ikiwa mkataba ulifanyika baada ya kifo cha ndugu yako, basi hati ya uwakilishi ilikuwa imeisha muda na mtu aliyepewa mamlaka alifanya bila nguvu yoyote, na mkataba wowote alioingia ni batili.

Ingawa neno 'hati ya uwakilishi' kwa namna fulani inaashiria kwamba mwanasheria anahusika, mamlaka haipaswi kutolewa kwa wakili tu.

## Ufundi kisheria Mahakamani

**Nilifungua maombi katika Mahakama Kuu ya Iringa kupata usaidizi fulani kwenye jambo la msingi. Ilikuwa ni maombi ya kuzuia benki kutaka kuuza mali yangu kwa kutolipa mkopo. Kwa mshangao mkubwa maombi hayakuwahi kusikilizwa, na maombi yangu yalitupwa kwa sababu za kiufundi. Badala ya kufungua maombi chini ya kifungu cha sheria cha 68, wakili wangu alinukuu sehemu nyingine ambapo Jaji alisema sio kifungu sahihi. Kwa sababu tu ya makosa ya namba, shauri lilitupwa. Ni haki ya aina gani hii? Kwa nini mahakama ilitupa ombi langu kwa mambo haya madogo bila kushughulikia suala kuu lililopo?**

*20 Desemba 2010*

Kwa sasa inaeleweka wazi kwamba kutotaja ama kutaja kwa makosa kifungu cha sheria kinachowezesha kufungua maombi ni jambo linalopelekea ombi husika kutokuwa na uwezo wa kusikilizwa. Hiki inaonekana ndicho kilichotokea kwenye kesi yako ya pingamizi dhidi ya benki. Baadhi ya mawakili wamejenga hoja kwamba sababu za kiufundi zisifanye shauri la msingi kutosikilizwa, kama unavyodai. Lakini Mahakama ya Rufaa ya Tanzania imeweka wazi kwenye maamuzi kadhaa kwamba kutaja kifungu sahihi cha sheria ni jambo la msingi. Na kama kifungu kisicho sahihi kimetajwa, basi ombi hilo husika la kisheria lazima litupwe.

Katiba ya Tanzania katika Ibara ya 107 inaunga mkono mtazamo wako kwamba sababu zisizo za kiufundi hazipaswi kuzuia mahakama kuzingatia hoja za msingi, ambapo katika kesi yako haijaelezwa kabisa. Hata hivyo, kwa kukabiliana na hili, Mahakama ya Rufaa imesema kuwa ni sheria hizo hizo na taratibu ambazo hutumiwa kuwezesha utoaji haki; hivyo sio sababu za kiufundi tu.

Tunashauri uwasiliane na wakili wako na fikiria kuwasilisha tena maombi kwa ajili ya kuomba zuio la mahakama.

## Siku Ishirini na Moja kuwasilisha Utetezi.

**Nililetewa wito wa kutokea mahakamani. Hata hivyo, sikuweza kuwasilisha utetezi wa maandishi ndani ya muda wa siku 21 kama Karani wa Mahakama alivyoelekeza nifanye. Nifanye nini? Niongeze pia kwamba nimeshtakiwa kimakosa, kwani mimi ndiye nilipaswa kushtaki. Ninafanyaje ili niweze**

**kufungua shauri langu wakati mimi tayari mdaiwa?**

*20 Desemba 2010*

Kuna tofauti kati ya wito wa kufika mahakamani na wito wa kuwasilisha utetezi wa kimaandishi. Inaonekana ulipewa wito wa kufika mahakamani. Sheria inasema kwamba endapo utapokea wito wa kuitwa mahakamani na kama utaelekezwa na mahakama, unatakiwa kabla au wakati wa kusikiliza shauri kwa mara ya kwanza au kwa wakati ambao mahakama inaweza kuruhusu, uwasilishe utetezi wa kesi yako. Hatuna uhakika kuhusu wito wako ulivyosema, lakini ikiwa tu ni wito wa kutokea mahakamani, na ikiwa hakuna amri nyingine ya kuwasilisha utetezi imetolewa, basi bado upo ndani ya muda.

Kama wito ulikuwa ni kwa ajili kuwasilisha utetezi wa maandishi, sheria ipo wazi kwamba unapaswa kufanya hivyo ndani ya siku ishirini na moja kuanzia siku ya kupokea wito. Unahesabu siku ishirini na moja kuanzia siku uliyopokea wito, na endapo siku ishirini na moja zinaishia siku za mwishoni mwa juma, basi Jumatatu inayofuatia huchukuliwa kama siku ya ishirini na moja. Pia endapo siku ya ishirini na moja ni sikukuu ya kitaifa, basi siku inayofuata ya kazi itachukuliwa kama siku ya ishirini na moja.

Unapaswa kuelewa aina ya wito uliopokea na tafuta mwanasheria wa kukushauri. Kama muda umeisha, unapaswa kuwasilisha maombi mahakamani ili kuongezewa muda kwa kuelezea sababu zilizokufanya uchelewe. Na endapo una madai dhidi ya mleta maombi, unapaswa kuyajumlisha katika utetezi wako kama madai kinzani. Itakua vema kama utalishughulikia suala hili kwa haraka bila kupoteza muda zaidi.

## Mdhamini ameamuriwa kulipa Gharama

**Miaka miwili iliyopita, mjomba wangu alishtakiwa kwa kuiba gari na kesi ilifunguliwa mbele ya Mahakama ya Wilaya ya Mtwara. Mjomba wangu alikanusha mashtaka dhidi yake na dhamana ilitolewa. Nilikuwa mdhamini wake na nilisaini dhamana ya Shilingi za Kitanzania 500,000. Mojawapo ya siku ya shauri, mjomba wangu hakuweza kutokea, kwani alikuwa ameenda Mwanza kumuuguza mama yake aliyekuwa mgonjwa. Nilikwenda mahakamani na kumjulisha Hakimu lakini aliniamuru kulipa Shilingi za Kitanzania 150,000 kama gharama kwa shahidi kutoka Dar es Salaam na Shilingi za Kitanzania 40,000 kwa shahidi kutoka Masasi. Ili kuepuka kupelekwa jela, nililipa. Je, hii ilikuwa amri ya haki?**

*6 Desemba 2012*

Kama unachosema ni kweli na mjomba wako hajajihusisha na mbinu za kuchelewesha kesi kwa makusudi, na kwamba mama yake alikuwa mgonjwa sana siku ya kusikilizwa kesi, hatuoni sababu ya msingi kwenye amri hiyo iliyotolewa na Hakimu anayesikiliza kesi.

Kukosekana kwa mshtakiwa kulikuwa kunasababishwa na mambo nje ya uwezo wake, ambayo wewe pia usingeweza fanya lolote. Hivyo, si haki kwa wewe kulipia gharama za mashahidi wa upande wa mashtaka bila kujali walisafiri toka wapi. Una uhuru wa kukata rufaa Mahakama Kuu ili itengue maamuzi hayo. Mshauri wako wa kisheria anaweza kukuongoza zaidi.

## Hati ya Kukamatwa kwa suala la Kodi

**Kwa takribani zaidi miaka minne tumekuwa na changamoto na Bodi ya Rufaa ya Kodi ya Mapato inayohusiana na Kodi ya Ongezeko la Thamani ya kiasi kikubwa cha fedha. Kesi hiyo ilikuwa ikiendelea kwa muda mrefu hadi wiki chache zilizopita wakati Bodi ya Rufaa ya Kodi ya Mapato ilipotoa hati ya kukamatwa kwangu kama Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa kampuni ya warufani. Hili halikunishangaza tu, lakini pia**

**limeharibu sana sifa yangu. Je, Bodi ya Rufaa inaweza kuamuru kukamatwa kwangu, na kama ni hivyo, nifanye nini ili kuepuka? Kwa taarifa tu, mimi ni mwekezaji na nina uwekezaji katika nchi ishirini za Kiafrika ikiwa ni pamoja na Tanzania. Je, kunaweza kuwa na upendeleo kwa wawekezaji kama mimi?**

*29 Novemba 2010*

Kuwa mwekezaji katika nchi ishirini za Kiafrika hakukuondolei wajibu wa kulipa kodi. Hata makampuni yenye uwekezaji duniani kote hulipa kodi nchini Tanzania. Hiyo sio sababu ya msingi ya kushinda rufaa, na hakuna uwezekano wa wewe au kampuni yako kupata upendeleo.

Tunapenda kukujulisha kwamba sio kawaida kwa kesi kwenda kwa muda mrefu hivyo katika Bodi ya Rufaa ya Kodi ya Mapato, kwa kawaida hufanyika haraka sana. Tunataraji hujachanganya kati ya Bodi ya Rufaa ya Kodi ya Mapato na Baraza la Rufaa la Kodi ya Mapato, ambacho ni chombo cha rufaa kutoka kwenye Bodi ya Rufaa ya Kodi ya Mapato.

Kutokana na swali lako, hati hii ya kukamatwa inawezekana ilitolewa kwa sababu haukutokea kama shahidi kwenye Bodi ya Rufaa. Kanuni ya 13 ya Kanuni za Bodi ya Rufaa za Kodi ya Mapato inasema kwamba mtu ambaye amepewa wito wa kutokea mbele ya Bodi na akashindwa kuzingatia wito huo bila sababu za msingi anafanya kosa chini ya Kanuni hizo. Pia inaongezea kwamba wakati mtu ambaye amepewa wito wa kutokea mbele ya Bodi kama shahidi na hajazingatia wito huo, Bodi inaweza kutoa hati ya kukamatwa ili kuhakikisha uwepo wa mtu huyo kabla ya Bodi kukaa katika tarehe, wakati na mahali palipotajwa kwenye hati husika. Wanasheria wako wanapaswa kushughulikia suala hili mara moja kabla ya kukamatwa - unaweza ukawaeleza sababu kwa nini ulishindwa kuonekana mbele ya Bodi. Tafadhali tambua kwamba Serikali (Tanzania), kama serikali zingine, inachukulia kwa uzito sana kazi za Bodi ya Rufaa, kwa sababu ni mhimili huu ambao unashughulikia kipengele muhimu cha mapato ya Serikali kupitia ukusanyaji wa kodi.

## Kiziwi kama Shahidi (Shahidi Kiziwi)

**Mimi ni mwanafunzi wa sheria ambaye nimekuwa nahudhuria kesi mbalimbali jijini Arusha. Hivi karibuni kulikuwa na kesi ambayo upande wa mashtaka ulileta shahidi ambaye alikuwa kiziwi na bubu. Bila chembe ya shaka Jaji alikataa ushahidi. Kiuhalisia yule bubu na kiziwi alikuwa shahidi muhimu sana, kwani alikuwa katika eneo uhalifu ulipotokea. Je, unafikiri Jaji alikuwa sahihi? Je, huu sio ubaguzi?**

*15 Novemba 2010*

Sheria ipo wazi kwamba mtu asiyeweza kuzungumza anaweza kutoa ushahidi kwa namna nyingine yoyote ambayo anaweza kuifanya ambayo ni sahihi, kama kwa kuandika au lugha ya ishara, ikiwa inaweza kuandikwa au kufanywa mahakamani. Mtu ambaye ni bubu na kiziwi sio shahidi asiyetakiwa kama anao uwezo wa kuelewa maana ya kiapo, na kama uelewa wake unaweza kutafsiriwa na kupokekelewa kutoka kwake kwa njia ya lugha ya ishara. Anaweza kuchunguzwa kupitia kwa mkalimani aliyeapa ambaye anaelewa lugha ya ishara. Kwa maoni yetu, kama mkalimani alikuwepo, hatuoni mantiki ya Jaji kukataa ushahidi.

## Mahakama kuandaa Mikataba

**Mara kadhaa nimeshuhudia jinsi watu wanavyopambana mahakamani ili kupata tafsiri sahihi ya mikataba. Kwa nini twende mahakamani kunapokuwa na matatizo? Hatuwezi kuifanya mahakama iwe inaandaa mikataba ili kuondoa haja ya kwenda mahakamani? Uandaaji wa mikataba sio mbinu ya wanasheria kujipatia pesa?**

*1 Novemba 2010*

Mawazo yako ni mazuri kwa nadharia, lakini hayawezekani kivitendo. Mahakama inaongozwa na mtu aitwaye Jaji, ambaye pia ni mtaalamu katika sheria. Mahakama haziendeshwi na Mungu na wala kalamu ya jaji si kalamu ya Mungu. Kwa hiyo, kwa kuwa majaji ni watu kama walivyo mawakili, hata kama mahakama zikiandaa mikataba migogoro itabaki pale pale. Mtu hawezi kwenda mahakama ili kupata mikataba iliyoandaliwa kwani kazi ya mahakama ni kutafsiri sheria. Itakuwaje, ikiwa mkataba ulioandaliwa na Mahakama utakuwa na mgogoro? Nani atasimamia shauri? Kwa sababu tu mkataba umeandaliwa na mahakama haimaanishi kuwa hakutakuwa na mgogoro. Dunia nzima kuna kilio kwamba mahakama zimekuwa nyoronyoro katika uendeshaji kesi, jaribu kufikiria utendaji wa mahakama iwapo itakuwa ni lazima kwa mahakama kuandaa mikataba.

Kuandaa mkataba kunahusisha ujuzi mkubwa wa kitaalamu; wanasheria wanajitahidi kuzuia kutokea kwa mambo yasiyotarajiwa, hata hivyo bado kuna matukio ambayo wanasheria hawawezi kutarajia, wakati wa kuiandaa mikataba hiyo.

Maoni yako juu ya uandaaji wa mikataba kuwa ni njia ya wanasheria kujipatia pesa si sawa. Matatizo mengi hutokea kwa sababu watu wanasubiri muda mrefu kabla ya kushauriana na mawakili wao. Msemo mmoja wa Kiswahili unasema “usipoziba ufa utajenga ukuta”- unafunga mjadala wote.

## Kuhudhuria Kituo cha Polisi wakati wa kusubiri Kesi

**Mnamo Julai 2010, nilikamatwa na polisi kwa madai ya kwamba nilihusika katika kuvunja na kuingia katika nyumba ya mtu. Nilishtakiwa katika Mahakama ya Wilaya na nilipata dhamana. Wakati nasubiri kesi hiyo, niliitwa tena kwenye kituo cha polisi kwa ajili ya mahojiano zaidi. Je, hii ni sahihi kiutaratibu? Ninawezaje kuzuia hili?**

*1 Novemba 2010*

Labda kama umeitwa kwenda kituo cha polisi kwa ajili ya tukio tofauti, kitu ambacho kinaonekana siyo, hivyo kuna uwezekano kitendo cha kukuita tena polisi, wakati kesi inaendelea mahakamani, kilikuwa kinyume cha sheria. Kitendo cha polisi ni cha kutia shaka kwa sababu mara mtuhumiwa akipelekwa mahakamani, anakuwa chini ya mamlaka ya mahakama; mamlaka ya polisi kuwaita au kukamata watu chini ya sheria ina maana ya kukabiliana na wahalifu kabla ya kesi zao kupelekwa mahakamani. Katika hali kama yako, polisi inaweza tu kushughulika na mtuhumiwa kwa idhini ya mahakama, ambayo mara chache sana hutolewa. Kwa hali ilivyo, tunakushauri kutoa ripoti mahakamani haraka, kwa hatua stahiki. Vinginevyo, unaweza kulalamika moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai ili aingilie kati.

## Uendeshaji wa Kesi kwa Siri

**Mimi ni msichana wa miaka 21 ninasoma shule ya sekondari Dar es Salaam. Binti wa jirani yetu ambaye ni rafiki yangu na tunasoma wote darasa moja usiku mmoja alibakwa wakati ameenda kibandani kununua maji. Kwa bahati nzuri mtuhumiwa alikamatwa na kushtakiwa Mahakama ya Wilaya. Tulihudhuria mahakamani kila siku kesi ilipokuwa ikiitwa. Hata hivyo, mashahidi walipoanza kutoa ushahidi wao tuliamuriwa na mahakama kutoka nje ya chumba cha mahakama. Je hii ni haki? Tulitaka kushuhudia taratibu za uendeshaji wa mahakama toka mwanzo mpaka mwisho kuhakikisha kuwa haki inatendeka. Je, sio haki yetu kushuhudia mwenendo wa kesi mahakamani? Je, hudhani kuwa Hakimu alipanga kumpendelea mtuhumiwa, hivyo kutaka uendeshaji wa kesi uwe wa siri?**

*1 Novemba 2010*

Kimsingi, kila mtu ana haki ya kuwepo mahakamani kama kuna nafasi ya kutosha

kuweza kuwatosheleza wote na hakuna usumbufu wowote wakati wa uendeshaji kesi. Ni kawaida hata hivyo kama kesi inahusiana na mambo ya aibu inapoitwa, sheria inaelekeza wanawake na watoto kutoka nje ya mahakama, ila kama kuna mtu mzima wa kike atasisitiza kuwepo wakati kesi ikisikilizwa, hakuna nguvu itakayoweza kuzuia uwepo wake. Inaelezwa wazi kwenye sheria zetu, Sheria ya Makosa ya Kujamiiana na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kuwa kwenye kesi za ubakaji au shahidi mwenye umri chini ya miaka 16 ameitwa kwenye kesi inayohusiana na kosa la kiheshima au kimaadili, mahakama inaweza ikatoa amri ya kuwaondoa watu wote isipokuwa wajumbe au maafisa wa mahakama au wahusika kwenye kesi au wanasheria wao. Hata hivyo hii haiwezi kuzuia mashahidi kuitwa kutoa ushahidi. Tafadhali elewa kwamba hatua iliyochukuliwa na mahakama ni ya kawaida kwa kesi za aina hii kwa hiyo hakuna kitu cha kuhofia labda kama una ushahidi wa kutosha kuthibitisha tuhuma za upendeleo. Zaidi ya hayo ikiwa upo kwenye orodha ya mashahidi unaweza kuitwa kwenda kutoa ushahidi.

## Kuzuiwa kufanya Usuluhishi nje ya Tanzania

**Mmoja wa mbia wa ndani ninayeingia nae kwenye mkataba, ameniambia kuwa kutokana na sheria za ndani, usuluhishi wowote lazima ufanyike Tanzania. Hili halijanishangaza kwa sababu ya historia ya kijamaa ya nchi, lakini je, kuna uwezekano ukabadilika?**

*25 Oktoba 2010*

Tunashangaa kusikia hili. Hatuna uhakika wa sheria inayokuzuia wewe kuchagua jukwaa la usuluhishi nje ya nchi. Upande mwingine labda anataka kujaribu kupunguza gharama kwani kufanya usuluhishi nje ya nchi ni gharama sana. Kama upande mwingine unakudanganya kuhusu usuluhishi, unatakiwa kusoma mkataba wote na kujua ni kitu gani kingine hujakigundua.

## Kushindwa kuuliza kama Kaolewa

**Desemba mwaka 2008, nilishtakiwa Mahakama ya Mwanzo kwa ajili ya fidia kwa kosa la ugoni, ingawa nilitoa ushahidi wa kujitosheleza kuwa nilikuwa sifahamu kama mwanamke ambaye nimetuhumiwa naye kufanya mapenzi alikuwa ni mke halali wa mlalamikaji. Kiukweli kabla sijaanzisha mahusiano huyu mwanamke aliniambia kuwa hajafunga ndoa kitu ambacho niliamini ni kweli. Nauliza kama Hakimu aliyeendesha kesi ametenda haki kuamua kama alivyoamua, na ukizingatia matendo yake wakati wa kesi. Wakati kesi ikiendelea hakurekodi ushahidi wangu na muda mwingine aliniingilia wakati natoa ushahidi wangu. Je, kuna njia yoyote naweza kupinga kilichoamuriwa na mahakama, ukizingatia kwamba baada ya kutolewa hukumu niliamuriwa kulipa shilingi ya Kitanzania 150,000/= kwa mdai, ambapo nilitimiza mara moja?**

*11 Oktoba 2010*

Barua yako inasema kwamba unahisi kesi yako haikuendeshwa vizuri. Bila kupitia kumbukumbu za mahakama, hatuwezi kutoa maoni yetu kama tuhuma zako dhidi ya Hakimu ni za kweli au la. Hata hivyo mara nyingi ni vigumu kushutumu kumbukumbu za mahakama endapo mlalamikaji alikuwa na haki ya kumuuliza Hakimu au Jaji kumsomea ushahidi wake na akashindwa kuitumia haki yake. Inaonekana hukuitumia hii haki.

Kuhusu uzito wa ushahidi wako, vile vile hatuwezi kutoa maoni yetu kwa sababu hatuji ni ushahidi upi ulioutoa, wala uzito wa ushahidi wa mlalamikaji. Hii ikiwa ni kesi ya madai, ushahidi kwa mujibu wa sheria unapimwa kutokana na mizania ya uwezekano (balance of probabilities).

Inaonekana ushahidi wa mpinzani wako umeuzidi wa kwako. Tunakushauri uendelee na utaratibu wa kukata rufaa. Tunapendekeza utafute ushauri wa mwanasheria.

## Hakimu kuingilia mamlaka ya Mwendesha Mashtaka

**Kaka yangu alishtakiwa na baadae kutiwa hatiani kwa makosa ya kuvunja duka na kuiba. Sakata lilianza pale alipokutwa na bidhaa zilizoibiwa, na kuitwa kama shahidi upande wa Jamhuri. Wakati anatoa ushahidi wake dhidi ya mtuhumiwa, Hakimu alitoa amri kwamba na kaka yangu naye aongezwe kwenye hati ya mashtaka, sambamba na mtuhumiwa sababu Hakimu aliamini kabisa kuwa kaka yangu ana mchango kwenye uhalifu huo. Je hii ni haki? Je Hakimu ana mamlaka hayo?**

*4 Oktoba 2010*

Ikiwa kama usemayo ni kweli, kaka yako aliongezwa kimakosa kwenye hati ya mashtaka hivyo alitiwa hatiani kimakosa. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inaipa mamlaka mahakama kurekebisha hati ya mashtaka kama ina makosa kwenye muundo au maudhui. Sheria haiipi mahakama nguvu ya kuingilia mamlaka ya Mwendesha Mashtaka na kuamuru kwamba mtu ajumuishwe kwenye hati ya mashtaka. Kwenye kesi yako mahakama imejiongoza vibaya. Una haki zote za kukata rufaa, ni matumaini yetu kuwa upo ndani ya muda unaotakiwa na sheria wa kukata rufaa Mahakama Kuu ya Tanzania.

## Utekelezaji wa Amri ya kuachia Ardhi

**Mnamo mwaka 2005, nilishinda kesi dhidi ya mtu ambaye nilimshtaki Mahakama Kuu ya Tanzania kwa kigezo cha umiliki wa ardhi iliyotelekezwa kwenye kipande changu cha ardhi. Mtu huyo alifariki miaka michache iliyopita. Mazingira ya kesi yapo hivi, marehemu alijenga nyumba kwenye ardhi hiyo na kuipangisha kwa familia nyingine. Mwaka jana, baada ya kushinda kesi yangu, niliwasilisha maombi ya utekelezwaji wa hukumu kwa ajili ya kuchukua eneo langu, lakini ombi langu lilikwama kwa sababu waliokuwa wanaishi kwenye nyumba hiyo waliweka pingamizi, wakidai kuwa ni wamiliki, na walinunua eneo hilo kwa marehemu. Jaji alikubaliana na pingamizi hilo licha ya kuwa kuna hukumu dhidi ya marehemu. Je, maamuzi ya Jaji yapo sahihi? Jaji anawezaje kufanya makosa?**

*27 Septemba 2010*

Kwa maelezo uliyotupatia hayatoi ufafanuzi wa kina juu ya pingamizi lililowekwa na mpinzani wako, kutufanya sisi kuelewa kwa nini Jaji alifanya maamuzi hayo. Hata hivyo, kwa muonekano wa kisheria, tunaweza kusema kwamba, kuhusiana na wewe na hao walioweka pingamizi, hakuna sababu ya kulifanya ombi lako la kumiliki ardhi yako kuwa la kukazia hukumu uliyopata dhidi ya marehemu. Ushindi wako dhidi ya marehemu ulikuwa mzuri dhidi ya marehemu na mtu yoyote anayedai kupitia kwake. Kiukweli, waweka pingamizi hawadai kupitia marehemu. Wanadai kuwa ni wamiliki halali wa ardhi hiyo. Mahakama haiwezi kwa msingi wa hukumu pekee, kutoa amri ya kuachia eneo dhidi ya waweka pingamizi. Kutokana na maelezo, maoni yetu ni kwamba Jaji alikuwa sahihi kukubaliana na pingamizi. Ni bahati mbaya kwako, ila unapaswa kufungua kesi ya uvamizi dhidi ya waweka pingamizi.

Pia umeuliza, inawezekanaje Jaji kufanya makosa? Jaji sio malaika wala mtenda miujiza. Ni mtu wa kawaida kama wewe na sisi. Kuna kesi nyingi ambazo majaji wamekosea - baadhi ya makosa ni yamewaaibisha baadhi ya majaji wakongwe, sio tu kwa Tanzania, bali duniani kote. Hii ndo sababu ya kuwa na utaratibu wa kukataa rufaa kuhakikisha kuwa haki inapatikana.

## Thamani ya Ushahidi wa Ndugu wa Mlalamikaji

**Mwaka 2007, kaka yangu mkubwa alishutumiwa kwa shambulio la kutaka kusababisha majeraha makubwa ya mwili, na tukio hilo liliripotiwa kituo cha polisi na mama wa mlalamikaji. Kesi hiyo ililetwa mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Mbeya, ambapo kesi ilisikilizwa, na akatiwa hatiani na kupewa adhabu ya kifungo cha gerezani. Wakati wa usikilizaji wa kesi, upande wa mashtaka ulileta mashahidi watano kuthibitisha kesi yao. Hata hivyo, mashahidi wanne wa upande wa mashtaka ambapo ndimo hatia ilizingatiwa, walikuwa ni ndugu wa mlalamikaji. Kwa dhati kabisa nasema kuwa, kaka yangu hakufanya kosa analotuhumiwa nalo na mahakama haikutakiwa kummkuta na hatia, kama isingekubaliana na ushahidi wa ndugu wa mlalamikaji, ambao kwa hakika ulikuwa sio wa kweli. Je, ushahidi wa ndugu una thamani gani kisheria? Je mahakama inaweza kumtia hatiani mtuhumiwa kwa ushahidi wa ndugu pekee na nafasi ya mafanikio kwenye rufaa ikoje? Kaka yangu alikata rufaa Mahakama Kuu toka mwaka 2008 mpaka sasa rufaa yake haijasikilizwa. Karani wa mahakama ameshidwa kutoa majibu uhakika wa tarehe ya rufaa. Je, hakuna uwezekano kuwa ndugu wa mlalamikaji ndio wanaofanya michezo michafu dhidi ya kaka yangu? Tafadhali nishauri juu ya hatua sahihi za kuchukua.**

*13 Septemba 2010*

Kutokana na maelezo yako, hoja yako ya msingi ni iwapo ndugu wa mlalamikaji wanaweza kutoa ushahidi kwa niaba yake. Sheria ya Ushahidi ipo wazi kwamba kila mtu ana uwezo wa kutoa ushahidi labda kama mahakama imeona kuwa hana uwezo wa kuelewa maswali yaliyoelekezwa kwake au hawezi kutoa majibu sahihi ya maswali kutokana na sababu ya umri (miaka 14 au chini ya), ugonjwa (wa mwili au akili) au sababu nyingine. Hakuna kanuni za mazoea au sheria ambayo inataka ushahidi wa ndugu ukataliwe moja kwa moja. Kukosekana kwa vigezo tofauti na vilivyotajwa hapo juu, ushahidi wa ndugu ni bora kama ulivyo ushahidi wa mtu mwingine, na mahakama inaweza ikautegemea huo tu kumtia mtu hatiani. Hata hivyo, kama shahidi huyo akionekana anapendelea au haaminiki, mahakama itapokea ushahidi huo kwa tahadhari na itajipa onyo kabla ya kuzingatia ushahidi huo wakati wa kumtia mtu hatiani. Kwenye mazingira hayo, Mahakama itahitaji ushahidi mwingine kwa ajili ya kuthibitisha. Wakili wa utetezi nae huwa na jukumu la msingi katika kuisaidia mahakama kufikia uamuzi wa haki.

Kuhusiana na nafasi ya mafanikio ya rufaa ya kaka yako, itategemea zaidi na ushahidi uliopo kwenye kumbukumbu za mahakama. Mahakama ya Rufaa itachunguza ushahidi na kuamua kama kesi ilithibitishwa kwa viwango vinavyotakiwa na sheria, ambapo kwa mazingira ya hii kesi ni kuthibitisha pasipo na mashaka. Ni jukumu la upande wa mashtaka kuthibitisha kesi pasipo na mashaka, na endapo upande wa utetezi wakiweza hata kwa kiasi kidogo kuonesha mashaka kwenye mawazo ya Hakimu au Jaji kadri itakavyokuwa, Hakimu au Jaji atamuachia huru mtuhumiwa. Kuwa rufaa ipo Mahakama Kuu unashauriwa uwasiliane na Msajili wa Mahakama Kuu katika kanda husika ambaye atakutaarifu kwa nini rufaa ya kaka yako bado haijasikilizwa. Kunaweza kuwa na sababu mbalimbali za kuchelewa huko.

## Ushahidi mpya kwenye Mahakama ya Rufaa

**Nimekuwa nikiendesha kesi Mahakama Kuu kwa muda wa miaka nane. Kesi kwa sasa imeisha na nimekataa rufaa. Kuna sehemu ya ushahidi ambao haukutolewa kwenye Mahakama Kuu ambao nimemuomba mwanasheria wangu auwasilishe. Hata hivyo**

**amekataa kwa kusema kuwa Mahakama ya Rufaa haikubali kuongeza ushahidi wa ziada. Je hii ni sawa?**

*30 Agosti 2010*

Sheria na Kanuni za Mwenendo wa Madai (Sura ya 33 Marejeo ya Mwaka 2002) inasomeka kama ifuatavyo; 'wahusika katika rufaa hawaruhusiwi kutoa ushahidi wowote wa ziada kwa maneno au nyaraka, mahakamani. Lakini iwapo mahakama ambayo maamuzi yake yamekatiwa rufaa ilikataa kupokea ushahidi ambao ulitakiwa upokelewe; au mahakama ikitaka nyaraka yoyote kutolewa au shahidi yoyote kuhojiwa ili kuisaidia kutoa maamuzi, au sababu nyingine yoyote ya msingi, mahakama inaweza kuruhusu ushahidi huo au nyaraka kutolewa au shahidi kuhojiwa.'

Sio sahihi kwamba unakataliwa kutoa ushahidi wa ziada. Kwa bahati mbaya tunashindwa kukuongoza vizuri kwani hatuna uhakika ushahidi huo ni upi na kwa nini haukutolewa mahakamani. Wanasheria wako wanatakiwa kufanya maamuzi sahihi.

## Mahakama haijiheshimu

**Mimi ni mfanyakazi wa benki mwenye uzoefu wa miaka ishirini na tano na nimekuwa nikifanya kazi Tanzania kwa takribani mwaka mmoja na nusu sasa. Kwa uzoefu wangu nchini Tanzania nimegundua kwamba mahakama za Tanzania zina wahurumia wakopaji wanaoshindwa kurejesha mikopo. Mahakama hazionekani kutambua ukweli kwamba mkopaji amechukua fedha toka benki. Wanasheria wa Tanzania wanawatetea wakopaji utadhani hawakuchukua fedha hizo benki. Je, unawezaje kushtaki kwa ufanisi nchini Tanzania? Je, ni fidia zipi nyingine benki inazo?**

*30 Agosti 2010*

Kuna watu wengi wanakiuka masharti ya mikopo kwenye soko la sasa – maoni yako ni sahihi. Hata hivyo tukukumbushe kuwa katika miaka kumi na moja ya uwepo wa Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara, mabenki yamefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana kushinda kesi zao za madai. Ni mahakama sahihi kwa mabenki kwani imekuwa ikitoa matokeo mazuri.

Hata hivyo, wakati mwingine benki ni za kulaumiwa. Kwa mfano mikopo yenye dhamana iliyotolewa na asiye mkopaji (third party), benki nyingi kwa miaka kadhaa iliyopita zimeathirika kwa sababu walisahau kupata ridhaa ya mke, kwa kuruhusu mali, hasa mali ya ndoa, kuwekwa kama dhamana bila ridhaa hiyo. Benki pia zimeshidwa kufanya upembuzi yakinifu na nyingi hutoa fedha kabla ya kukamilika kwa dhamana.

Hatuamini kwamba mahakama ni ya kulaumiwa pekee. Benki zina mtindo wa kulaumu mahakama, labda kwa ajili ya kuzifurahisha bodi za wakurugenzi wake.

Tukirudi kwenye swali lako juu ya fidia zingine zilizopo; tafadhali tambua kuwa sheria ni kali sana kwa wakopaji. Sheria inaruhusu benki kuuza mali iliyowekwa rehani baada ya kutoa taarifa ya siku sitini bila ya kwenda mahakamani. Unatakiwa ufahamu kuwa hakuna sheria inaweza kuwa mbadala kwa benki katika kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kutoa mkopo. Soko lililopo lina changamoto lakini lina mwelekeo mzuri. Tuna imani kuwa benki yako sio moja kati ya zile zilizojiingiza kwenye kutoa mikopo bila ya kujihakikishia ukamilifu wa dhamana - benki mara nyingi hujitetea yenyewe kwa kudai wateja waliwapa shinikizo kubwa na hivyo wakaamua kutoa mkopo.

## Jaji alimkejeli Mwanasheria wangu

**Nilifungua shauri Mahakama Kuu mkoani Mwanza na nilipoteza kesi hiyo. Mwanasheria wangu aliniambia kuwa wakati hukumu ikitolewa Jaji alimkejeli,**

**ikionesha wazi upendeleo. Amefanya kejeli, kwa lengo la kumdhalilisha mwanasheria wangu, kitu ambacho kipo wazi kabisa kwenye hukumu. Nifanyeje?**

*23 Agosti 2010*

Pamoja na mambo mengine, hukumu hujumuisha maelezo ya pande zote kwenye kesi, muhtasari wa ushahidi uliotolewa na mashahidi, sababu za uamuzi na uamuzi wenyewe. Hatujasoma hukumu, lakini kwa sababu tu Jaji katumia vichekesho, kitu ambacho majaji hufanya wakati mwingine, haimaanishi kuwa alikuwa na upendeleo.

Kila Jaji ana aina yake ya uandishi – wengine wana uandishi wa moja kwa moja; na wengine huandika kwa dhihaka na ucheshi. Tumesoma hukumu za majaji kwenye nchi za Magharibi ambao huandika hukumu kwa mtindo wa mashairi. Kama Jaji ameamua hoja iliyopo mbele yake, hatuoni sababu ya msingi kwa mwanasheria wako kulalamika. Inawezekana analalamika kuhusu Jaji kwa kuwa ameshindwa kesi.

Badala ya kuangalia mambo yasiyo na maana, angalia makosa muhimu ya kimantiki au kisheria kwenye hukumu na ukate rufaa.

## Masuala ambayo yanaweza kupelekwa Mahakama ya Biashara

**Msingi wa suala langu unatokana na shughuli niliyojiingiza, ya kusambaza vipuri kwenye kampuni inayojishughulisha na kilimo. Sijalipwa kwa maelezo kuwa nilisambaza vipuri vilivyo chini ya viwango, madai ambayo naamini hayana msingi wowote. Nataka kufungua kesi katika Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara jijini Dar es Salaam, lakini nimepewa taarifa na wanasheria kuwa sitaweza kufungua kesi katika mahakama hii kwa sababu mgogoro huu si wa kibiashara, kwa kuwa mimi ni mtu binafsi. Ingawa nakiri kuwa sikuwahi kufanya biashara kama kampuni, lakini sielewi sababu ya msingi inayonifanya nisikubaliwe. Je, kuna fidia naweza pata?**

*23 Agosti 2010*

Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara imethibitisha kuwa na ufanisi wa hali ya juu na tunaelewa kwa nini unataka kufungua kesi huko.

Chini ya sheria, kesi ya biashara ni ile inayohusisha mambo muhimu ya biashara, ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa biashara au taasisi ya kibiashara, usimamizi wa biashara au taasisi ya kibiashara, uhusiano wa kimkataba wa biashara kati ya biashara au taasisi ya kibiashara na taasisi nyingine au watu wengine nje ya uhusiano huo, wajibu wa kibiashara au taasisi ya kibiashara au kazi zake zinatokana na biashara au shughuli za kibiashara, urekebishaji au malipo ya mkopo wa biashara au kwenye biashara au taasisi ya kibiashara au mtu, kuhuisha au kufilisika kwa biashara au taasisi ya kibiashara au watu, utekelezaji wa tuzo ya Mahakama ya Hakimu Mkazi au baraza lenye mamlaka iliyoanzishwa kutokana na mikataba au makubaliano ya pamoja kusaidiana ambayo Tanzania imeridhia na kuwa sehemu ya sheria ya Tanzania, utekelezaji wa tuzo ya usuluhishi, mashtaka yanayohusiana na sheria za baharini, na mashtaka ya usuluhishi.

Maana ya suala la kibiashara ni pana sana na tunashidwa kuelewa kwa nini suala lako, kwa mujibu wa wanasheria wako, lishindikane kuainishwa kwenye moja kati ya makundi hapo juu. Labda kama kiasi kinachodaiwa kipo chini ya kiwango cha kimamlaka ya Mahakama Kuu, Kitengo cha Biashara, tunashindwa kuelewa kwa nini ushidwe kufungua kesi yako hapo. Unaweza kutafuta msaada mwingine wa kisheria.

## Kutumia vibaya Madaraka ya Polisi

**Kwa miezi minne iliyopita nimekuwa nikikamatwa kwa kipindi cha zaidi ya mara**

**tano na afisa mmoja wa polisi wa kituo kimoja cha polisi jirani kwa madai dhaifu na ya usumbufu ya jirani yangu, ambaye hajaolewa na ni mfanyabiashara tajiri. Hakujawahi kuwa na mashtaka yoyote dhidi yangu baadala yake nimeishia kutumia muda wa usiku kituo cha polisi. Sasa nimegundua kuwa huyo mwanamke ana uhusiano wa karibu na afisa mmoja wa polisi hapo kituoni. Nawezaje kuzuia huu ukamataji? Je, naweza kupata amri ya mahakama kuzuia polisi kunikamata?**

*9 Agosti 2010*

Hujatuhabarisha kuhusu chanzo cha mgogoro kati yako na huyo mwanamke. Ni lazima kutakua na kitu kwenye malalamiko yake yanayoleta msuguano huu. Itakuwa ni wazo zuri kufahamu.

Umetamka kupata amri ya zuio la mahakama. Unaweza kuwasilisha malalamiko kwenye ofisi ya Mwendesha Mashtaka ya Jinai, ambayo atashughulikia matatizo yako.

Suala lako haliishii hapa. Ikiwa mamlaka ya juu ikisema kwamba afisa wa polisi amekuwa akikukamata bila sababu za msingi au kwa sababu ya uhusiano wake na yule mwanamke, utaweza kufungua mashtaka ya madai dhidi ya afisa wa polisi kwa kutumia mamlaka yake vibaya. Makosa hayo ya madai, yakithibitishwa mahakamani, anaweza kuchukuliwa hatua, na kuna fidia anazoweza kupata muhanga. Kwa mamlaka nyingine matumizi mabaya ya mamlaka ya polisi huitwa matumizi mabaya ya ofisi ya umma.

## Deni na Mfungwa wa Madai

**Nilishindwa kulipa deni kwa sababu pesa nilizoziazima zilitumika kwenye mradi mwingine. Mahakama iliniamuru kulipa kiasi ninachodaiwa pamoja na riba na fidia ya shilingi milioni 100. Mkopeshaji sasa ananitishia kunifunga kwa kushindwa kutimiza amri ya mahakama. Je, naweza nikapelekwa gerezani kwa kushidwa kulipa hicho kiasi? Kushidwa huku kulipa kwa uhakika hakulingani na kosa la jinai. Je, mkopeshaji anaweza kuninyanyasa kiasi hiki?**

*9 Agosti 2010*

Inatakiwa utambue kuwa ulichukuwa pesa na hukuzitumia kwa mujibu wa sababu ulizochukulia mkopo. Kama mkopeshaji ni benki unatakiwa uelewe kuwa hizo ni fedha zinazowekwa na watu na zimekopeshwa kwako. Labda kama kuna maelezo ambayo hujatupatia, hatuoni unyanyasaji wowote uliofanywa na mkopeshaji.

Linapokuja suala mfungwa wa madai, sheria ipo wazi kwamba kwa kila amri ya mahakama ya kulipa fedha inaweza kutekelezwa kwa kumuweka mdaiwa kizuizini kama mfungwa wa madai, au kukamata na kuuza mali za mdaiwa au vyote viwili.

Kabla ya kuchukuliwa kama mfungwa wa madai, mdai lazima aweke posho ya kujikimu mahakamani kwa ajili ya kumtunza mfungwa wa madai wakati anatumikia kifungu chake. Kifungo hicho cha madai adhabu yake haizidi miezi sita na bado hakiwezi kukuondoa kwenye deni unalodaiwa.

## Sijajua nani wa Kumshtaki

**Namiliki kipande cha ardhi ambacho hakijapimwa jijini Dar es Salaam. Hivi karibuni nimekuta mafundi wakijenga ukuta kwenye ardhi yangu chini ya maelekezo ya mtu mmoja wanayemtambua kama bosi wao. Jitihada zangu za kumtambua wanayemuita ni bosi wao na wapi alipo hazijazaa matunda. Je, naweza nikafanya nini kwa hii hali ambapo mafundi wameongeza kasi ya ujenzi na sjui ni nani wa kumwajibisha?**

*2 Agosti 2010*

Kutokuwa na uhakika wa nani wa kumshtaki haimaanishi kuwaruhusu mafundi

kuendelea kujenga ukuta. Fundi mwenyewe anaweza kuwa mvamizi! Kwenye hali kama hii, sheria inakuruhusu kuwashtaki kwa pamoja wote waliohusika na ujenzi wa ukuta huu. Unaweza ukaishtaki kampuni inayojenga, mafundi wa kampuni na mtu yeyote yule au kampuni unayoamini inajihusisha na kitendo hiki haramu. Wakati kesi inasubiriwa, unatakiwa uombe amri ya zuio la muda ili kuzuia ujenzi huo usiendelee.

## Kumshtaki Hakimu kwa kumtia Mtu Hatiani kimakosa

**Nilishtakiwa kwa kosa la wizi wa kutumia silaha mbele ya Mahakama ya Wilaya mkoani Morogoro na kutiwa hatiani na kutumikia kifungo cha miaka thelathini. Wakati kesi ikiendelea nilimwambia Hakimu kwamba sikutenda kosa hilo lakini akaamua kunifunga. Nilikata rufaa Mahakama Kuu na nikafanikiwa na kuachiwa huru kuhusiana na mashtaka dhidi yangu. Nimekuwa gerezani kwa muda wa miaka saba kimakosa na sasa nataka nimshtaki Hakimu aliyeendesha kesi yangu kwa kuniharibia maisha yangu pamoja na kunifunga kimakosa. Je, naweza kumshtaki Hakimu?**

*19 Julai 2010*

Katika utendaji wao wa kazi, Mahakimu na Majaji kazi zao ni kuendesha kesi kwa uaminifu bila kuogopa wala kuingiliwa na mtu yeyote yule. Ikitokea imethibitika kuwa kuna matumizi mabaya ya madaraka kwa upande wa Hakimu au Jaji, upande wowote ulioathirika kwenye kesi unaweza kuomba mahakamani kumtaka Hakimu huyo au Jaji huyo kujiondoa kwenye uendeshaji wa kesi hiyo. Mahakimu na majaji wanasikiliza na kuamua kesi kulingana na ushahidi ulio mbele yao na sheria zetu zinaeleza wazi kwamba hakuna Hakimu wala Jaji atawajibika kwa kosa alilofanya, ikiwa kitendo hicho kilifanyika wakati yupo kwenye utendaji wake wa kazi.

Kwa upande wako, hujataja ni kitendo kipi cha utovu wa nidhamu kilifanywa na Hakimu aliyesimamia kesi. Hakimu aliyesimamia kesi anaweza akawa amekosea katika kuchunguza na/au kutathmini ushahidi uliotolewa mbele yake, ila hicho pekee hakiwezi kuhalalisha uwajibikaji juu yake labda kama ikithibitika kuwa alifanya kwa makusudi au pasipo na uaminifu, kitu ambacho hatukioni.

## Haki ya Kusikilizwa

**Kesi yangu iliyopo Mahakama Kuu ilisikilizwa bila ya mimi kuwepo. Sikuwahi kupokea wito wa mahakama na wala sikujua kuwa kuna hukumu dhidi yangu. Nawezaje kupata haki kwa mfumo wetu ikiwa sikupewa taarifa? Inawezekana vipi wakala wa mahakama akaweza kujua sehemu ninapoishi ili kutekeleza hukumu, na karani wa mahakama anayewasilisha wito wa mahakama asijue naishi wapi?**

*12 Julai 2010*

Mahakama zinaongozwa na kanuni za asili za kutenda haki ambazo zinasema kwamba hakuna mtu atakutwa na hatia bila kusikilizwa. Kuna maamuzi mengi ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ambapo wameelezea juu ya haki ya kusikilizwa. Mahakama imesema kwamba uamuzi ukifikiwa bila ya kuruhusu upande mmoja kusikilizwa ni batili na inawezekana kufutwa. Unachotakiwa ufanye kwa haraka ni kufanya maombi ya kuweka kando uamuzi wa upande mmoja uliofikiwa na mahakama, kwa kutaja sababu za kutokuhudhuria kwako. Inatakiwa uwasiliane na mwanasheria wako kwa mwongozo zaidi.

## Ada ya Ofisi za Mawakili

**Mimi ni raia kutoka Ulaya Mashariki na nimewekeza Tanzania chini ya cheti cha motisha cha Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC). Mwaka 2008 nilipambana kwenye kesi**

**kubwa dhidi ya kampuni iliyopo hapa Dar Es Salaam na kutumia ofisi ya mawakili iliyopo hapa Dar Es Salaam. Nilitozwa ada ya 3% ya kiasi kilichokuwa kinadaiwa kwenye kesi. Je, hayo sio mambo ya ajabu? Je, TIC inaweza kusaidia kwenye hili, kwa kuwa mimi ni mwekezaji wa kigeni? Kwa nchi nyingine mawakala wa uwekezaji wanachukua jukumu la kuwajali wawekezaji, ikiwemo kinga ya uwekezaji. Tafadhali nishauri.**

*5 Julai 2010*

Kwanza kabisa, kituo cha uwekezaji Tanzania (TIC) hakiwezi kukusaidia makubaliano yako ya ada ya uwakili. TIC inachoangalia ni miundombinu ya uwekezaji kwa wawekezaji. Haifanyi wala haitakiwi kukuongoza katika mradi wako. Hatuna uhakika ni nchi zipi mawakala wa uwekezaji wanafanya makubaliano ya ada ya uwakili kwa wawekezaji wao.

Kwa Tanzania ilivyo, hakuna mtu ambaye yupo juu ya sheria hivyo hakuna kinga ya mwekezaji. Ingawa kunaweza kuwa na baadhi ya motisha kwa wawekezaji, haya yote yapo ndani ya mipaka fulani na hakuna kinga inayotolewa.

Kuhusu ada ya uwakili, Sheria ya Malipo ya Mawakili Pamoja na Gharama za Kodi ndiyo inayotaja 3% ambayo unaiongelea. Sheria ipo wazi kwamba wakili lazima atoze 3% kwa kinachodaiwa kama ada. Hatuna uhakika na maelezo yote wa kesi hiyo, lakini hatuoni chochote kibaya kilichofanyika kwenye kiasi cha asilimia ulichokitaja.

## Haki ya kukaa Kimya

**Nimesoma mara nyingi kuhusiana na haki ya mtu kukaa kimya akiwa amekamatwa. Hii inaweza kutumika dhidi yangu mahakamani nikiwa nimeshtakiwa? Kwa nini sheria inanitaka nikae kimya wakati sina hatia?**

*14 Juni 2010*

Tunalazimika kueleza mapema kabisa kuwa sheria haikutaki wewe ukae kimya. Ni wewe mwenyewe unayeamua kukaa kimya.

Haki ya kukaa kimya ni haki ya mtu anaeshtakiwa na kosa la jinai, hapaswi kutoa maelezo yoyote wala kutoa ushahidi. Mara nyingi huchukuliwa kama mfano mzuri wa mfumo wa utoaji haki kwenye jinai; hukusudiwa kuwalinda wasiyo na hatia. Ingawa mara nyingi haki ya kukaa kimya hupingwa kwa kuwa hukwamisha watu kukutwa na hatia.

Kwa kawaida haki ya kukaa kimya haiwezi kutumiwa dhidi yako mahakamani. Ukiwa umekamatwa, kwa sababu ya mkanganyiko unaoweza kusababishwa na kukamatwa kwako, huna haki tu ya kukaa kimya, bali pia una haki ya kuwa na rafiki, ndugu au wakili. Hii, hata hivyo, inategemea umekamatwa kwa kosa gani na la ukubwa gani.

## Mfungwa wa Madai

**Nimepoteza kesi Mahakama Kuu na nimeamuriwa kulipa Shilingi za Kitanzania milioni 118 pamoja na riba. Sipingani na kiasi hicho, ila sina uwezo wa kulipa. Nini madhara ya kutokulipa? Mwanasheria wangu ananitisha nikishindwa kulipa kiasi hicho, nitafungwa. Mtu anaweza kufungwa kwa ajili ya kesi ya madai? Kama ni hivyo, ni kwa muda gani?**

*21 Juni 2010*

Wewe unatambulika kama mdaiwa wa hukumu; katika hukumu, ni mtu ambaye hukumu imetolewa ikimuamuru kulipa kiasi fulani cha pesa na bado halipi. Sheria ipo wazi kuwa mdaiwa wa hukumu anaweza kukamatwa wakati wa kukazia hukumu muda wowote na katika siku yoyote, na haraka itakavyowezekana, ataletwa mahakamani, na mahakama itaamuru mtu huyo kuwekwa kizuizini. Sheria inaelekeza zaidi kuwa mdaiwa wa hukumu akikamatwa kwa utekelezwaji wa hukumu ya kulipa fedha na kuletwa

mahakamani, mahakama itamtaarifu kuwa anaweza kuomba kutangazwa kafilisika, na hapo ataachiwa huru kama hajafanya udanganyifu kuhusiana na maombi hayo, na kama atatimiza vinavyotakiwa na sheria ya mufilisi kwa wakati huo. Kama hautofungua maombi ya ufilisi, kipindi unachotarajiwa kufungwa ni miezi sita. Ndani ya kipindi hicho, mdai atapaswa kumlipa mdaiwa wa hukumu posho ya kujikimu. Swali lako la kuwa mtu anaweza kuwa mfungwa wa madai, jibu lake ni ndiyo.

## Kumshtaki Mfungwa

**Nimefungua shauri la madai dhidi ya rafiki yangu ambae anatumikia kifungo cha miaka mitatu gerezani kwa kosa la jinai. Hakimu hataki kutoa hati ya wito wa kuja mahakamani kwa mdaiwa, akisema kuwa tayari yupo gerezani. Kuna sheria inayonikataza mimi kumshtaki mfungwa? Nitaendeleaje? Mwanasheria wangu anasema tunapaswa kufungua maombi ya kuendelea na kesi upande mmoja.**

*21 Juni 2010*

Hakimu hayupo sahihi kukataa kuendelea na kesi. Hakuna sheria inayokataza mtu kumshtaki mtu aliye gerezani. Mamlaka za Magereza huwa zinaruhusu mfungwa kwenda mahakamani kutetea kesi yake, kama ameitwa kufanya hivyo. Hatuelewi kwa nini Hakimu anakuzuia usiendelee na kesi. Akiendelea hivyo, unaweza kumuomba Hakimu husika kujiondoa kwenye kesi ili apangiwe Hakimu mwingine.

Hatujafurahishwa na mikakati uliyoshauriwa na mwanasheria wako. Anachopendekeza ni usikilizwaji wa kesi unaofanywa bila kuwepo upande mwingine. Ni kinyume na kanuni za haki ya asili kuendelea na kesi kwa upande mmoja wakati mlalamikiwa akiwa hajapewa hati ya wito au tayari ameshindwa kutimiza wajibu. Katika hali isiyowezekana, ikitokea umepata amri hiyo, inaweza kupingwa kwenye hatua za baadae na kuchelewesha madai yako.

## Hati ya Kukamatwa kwa kutokutokea Mahakamani

**Hati ya kukamatwa imetolewa dhidi yangu kwa kosa la kutokuhudhuria wakati kesi yangu ya jinai ilipoitwa. Afisa wa polisi alisisitiza kunikamata, ingawa nilitoa maelezo mazuri kuwa nilikuwepo kwenye mazingira ya mahakama na sikusikia kesi yangu ikiitwa. Nifanyeje? Mahakama inaweza kunikuta na hatia kwa hili?**

*7 June 2010*

Kwenye kesi za namna hii, hati ya kukamata sio mwisho wa kesi. Amri ya kukamata mara zote humuhitaji mtu anayekamatwa kuonesha kwa nini hapaswi kuadhibiwa kwa kutoonekana kwake wakati kesi inaitwa. Kama mahakama itajiridhisha na maelezo yaliyotolewa, basi amri ya kukamata itabatilishwa. Kwenye kesi yako, hatuoni tatizo lolote kama ulichosema ni ukweli na ukaweza kutoa maelezo ya kutosha mahakamani, kuwa ulifika katika muda sahihi ila haukusikia kesi yako ilipoitwa.

Kuhusiana na afisa wa polisi aliyekataa kukubali maelezo yako, maoni yetu ni kuwa polisi alikuwa sahihi, kwa kuwa hati ya kukamata ni amri halali ya mahakama, isiyowezwa kubadilishwa na polisi. Wajibu wa afisa wa polisi si zaidi ya ile ya kumkamata mtu huyo na kumfikisha mahakamani kwa ajili ya amri zaidi au mwongozo. Kama utaendelea kuhofu, tunakushauri utafute msaada wa kisheria.

Kwa hilo unaloita kukutwa na hatia, tafadhali elewa kuwa hiyo si kukutwa na hatia ya kesi ya msingi uliyokuwa nayo. Kesi itaendelea kabla ya hukumu kusomwa.

## Kushtakiwa kwa Kosa la Barabarani

**Nimeshtakiwa kwa kosa la barabarani kwa kuendesha pembezoni mwa barabara,**

**ingawa huu ni utaratibu wa kawaida hapa Dar es Salaam. Afisa wa polisi walisisitiza kuwa nina hatia. Hii ni haki? Kwa nini peke yangu? Nikaamriiwa nitoe faini kwa muda huo, ila nikakataa kwa kuwa nilikuwa sipati risiti ya malipo.**

*7 Juni 2010*

Kutokana na maelezo uliyotupa haipingiki kuwa umetenda kosa ulilotuhumiwa nalo. Ingawa hii ni tabia ya madereva wengi wa Dar es Salaam kuendesha pembezoni mwa barabara, hii pekee haileti uhalali wa kitendo chako. Inaweza tu kupunguza uzito wa kesi na kupelekea kuchiwa huru kulingana na namna utakavyojitetea. Chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu ya nchini Tanzania, mtu anayetenda kosa kwa uaminifu na busara, ila kwa kutokujua, akiamini uhalali wake, hawezi kuwajibika kwa kosa hilo, kwa kiwango kikubwa kuliko vile hali ilivyotakiwa kuwa kama alivyoamini inapaswa kuwa. Kwenye suala lako, kukutwa na hatia kutategemea ushahidi wa upande wa mashtaka na namna utakavyojitetea.

Kwa malipo ya faini ya kutembea pembezoni mwa barabara, ni kama vile uliombwa kwa ajili ya rushwa. Unapolipa faini, unapaswa kudai risiti. Rushwa siku zote huombwa bila kutoa risiti.

## Polisi kanipiga Kofi

**Nilikuwa naendesha kwa amani tu siku moja ndipo afisa wa polisi aliyekuwa kwenye pikipiki aliponisimamisha. Akaniuliza leseni yangu ya udereva na kadi ya usajili, ambayo niliyatekeleza. Halafu akaangalia stika ya bima, mtungi wa kuzimia moto, taa na pembe tatu inayoakisi na hakuweza kukuta kosa lolote kwenye gari langu. Kisha, bila kuangalia kwenye matairi, akasema matairi yangu yalikuwa yamekwisha na ninapaswa kulipa faini kwa kuendesha gari lisilo salama barabarani. Nikaamua niangalie matairi mwenyewe, nilikuwa naendesha gari jipya aina ya Toyata Land Cruiser, na sikuwa na uhakika kama tuhuma zake zilikuwa sahihi. Matairi yalikuwa mapya, na nilimtaarifu polisi vilivyo. Hakufurahishwa na akaanza kunieleza ni jinsi gani sisi jamii ya wazungu tunaoishi Tanzania tulivyo na majivuno. Halafu akachukua leseni yangu na kutoa stika ya bima ambapo nilipinga na sikuwa nafahamu kwa nini alifanya kitendo kile. Nilikuwa na uhakika haikuwa haki na tukaanza kujibizana, na baada ya dakika chache wakati tunajibizana akanipiga kofi. Nimekuwa nchini kwa miezi isiyozidi sita. Je, sheria inaruhusu askari wa barabarani kutenda haya? Je, anaweza kuniita mimi Mzungu?**

*31 Mei 2010*

Labda kama polisi alikuwa anajihami (tuamini labda ulikuwa ukijaribu kumshambulia), hapaswi kumpiga kofi yoyote, ikiwemo mhalifu wa barabarani. Kutokana na maelezo, hatuoni dalili zozote za shambulizi kutoka kwako, kwa hiyo kofi ni shambulio na ni kosa la jinai. Unaweza kuwasilisha malalamiko yako dhidi ya polisi huyo katika kituo chochote cha polisi, na anaweza kushtakiwa kwa kufanya kazi kinyume na mamlaka yake. Tunakumbuka miaka michache iliyopita kulikuwa na tukio kama hilo, ilipelekea afisa wa polisi huyo kufukuzwa kazi. Tunakushauri pia upeleke malalamiko rasmi kwa mkuu wa askari wa barabarani Dar es salaam, ambaye atachunguza suala hili.

Kwa kukuita Mzungu (mtu mweupe), neno mzungu sio la kukashfu katika maana yake asilia kwa hiyo hatuoni kosa lolote kwenye hilo neno. Maneno mengine yanayotumika sana kwenye Kiswahili yanajumuisha Mhindi na Mwarabu. Kutokana na maelezo hapo juu, hatuamini kama una kesi ya msingi dhidi ya afisa wa polisi kwa kukuita Mzungu.

Pia fahamu kuwa afisa polisi hawezi kuchukua stika yako ya Bima na leseni ya

udereva. Akifanya hivyo, atakua amefanya kinyume na mamlaka aliyopewa kisheria.

## Kuachiwa kwa Wafungwa kwa muda wa Matazamio

**Mimi ni mfanyabiashara wa kike ninayemiliki mashamba ya kuku. Karibu na moja ya mashamba hayo kuna watoto wa mtaani ambao wanaiba kuku. Nilitoa taarifa polisi na wezi wawili walikamatwa na kukiri kutenda kosa. Walihukumiwa kifungo, ila Hakimu akawaachia kwa kipindi cha matazamio cha miezi sita. Nilitaka wafungwe. Ni sahihi kwa Hakimu kuwaachia waende kwenye kipindi cha matazamio? Nataka niwafundishe adabu hawa watoto. Nifanyeje?**

*24 Mei 2010*

Tunaanza kujibu swali lako kwa kuwahurumia pande zote mbili-wakati umepoteza baadhi ya kuku wako, lazima uweke akilini kuwa hawa ni watoto, labda ni yatima, bila makazi na chakula. Hawa pia ni watoto wasio na elimu na wamekosa matumaini ya kimaisha. Unatakiwa uangalie upya tabia zako za kikatili na ishi kama kibinadamu.

Tukirudi kwenye sheria, kwa mujibu wa Sheria ya Uangalizi ya watenda makosa, kama mahakama ikiona kwa kuzingatia umri, chanzo cha kosa lenyewe na utimamu wa mkosaji, ni afadhali kumuachia mkosaji kwa matazamio, mahakama ina mamlaka ya kumuachia mkosaji kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu, na mkosaji atakua chini ya uangalizi wa kudumu wa polisi. Kama mkosaji atafanya kosa lilelile ndani ya kipindi cha miaka mitatu, basi mkosaji huyo atakamatwa tena na atatumikia kifungo chake kilichobakia gerezani. Kusudio la hii ni kupunguza msongamano wa wafungwa. Ingawa ungependa wahalifu kwenda gerezani, Hakimu hajafanya kosa lolote na ni ngumu kushawishi maamuzi ya Hakimu.

## Kukiri Upotevu

**Mdogo wangu alikuwa anafanya kazi kwenye kampuni kama mtunza stoo. Kampuni inajihusisha na uuzaji wa vifaa vya umeme kwa jumla na rejareja. Wakati wa kupakia, ilibainika kuna upotevu. Mdogo wangu alikubaliana na huo upotevu na alipelekwa polisi, ambapo kwa sasa anachunguzwa. Tufanyaje?**

*8 Machi 2010*

Kesi nzima inategemea na uchunguzi wa polisi. Kwenye sheria za jinai, kukiri upotevu haimaanishi ni kukiri wizi. Ili kutenda jinai ya wizi, lazima kuwe na kitendo kisichokua cha uaminifu cha kuchukua mali ya mtu mwingine. Kwenye hili, itategemea na ushahidi utakaoletwa na upande wa mashtaka. Ni vigumu sana kwetu kukisia hatia yake au kutokuwa na hatia kwake bila kujua yaliyomo kwenye uchunguzi. Inawezekana pia upotevu ulisababishwa na makosa ya kimahesabu au kuchukuliwa na watu wengine, sio lazima awe mdogo wako. Hili swali limejibiwa kwa kuzingatia kuwa mdogo wako alikiri kuna upotevu. Laiti kama angekiri wizi, mtazamo wetu ungekuwa tofauti.

## Kuachiwa huru kwa Watuhumiwa wenza

**Ndugu yangu na watuhumiwa wengine wawili walikamatwa kwa kosa la jinai na kupelekwa mahakamani ambapo tulimtoa kwa dhamana. Kesi imekuwa ikiendelea mahakamani, wakati upande mashtaka unakamilisha kesi yao cha kushangaza Hakimu aliwaachia huru watuhumiwa wengine wawili lakini si ndugu yangu. Ilinishtua kwamba kesi imeisha lakini ndugu yangu bado yupo gerezani.**

*3 Mei 2010*

Kesi za jinai ni tofauti na kesi za madai. Kwa kawaida, upelelezi ukikamilika upande

wa mashtaka unaendelea na usikilizaji wa awali ili kuona ni mambo gani mtuhumiwa anakubali na yapi anayakataa. Baada ya hapo, upande wa mashtaka utaleta mashahidi wa kujenga kesi yao. Kama upande wa mashtaka wameshatoa ushahidi wao, lakini kabla mtuhumiwa hajaanza kujitetea ni lazima mahakama itoe uamuzi wa kama mtuhumiwa au watuhumiwa wana kesi ya kujibu au la. Mahakama inatoa uamuzi huu kwa kuangalia mambo mengi ikiwemo ushahidi uliotolewa na mashahidi dhidi ya mtuhumiwa katika kushiriki kosa.

Sheria ipo wazi sana, kama ushahidi hautoshelezi kumtaka mtuhumiwa kujitetea dhidi ya tuhuma zinazomkabili au makosa mengine yoyoye ambayo yanaweza kumtia hatiani, mahakama itamuachia huru mshtakiwa.

Inawezekana hiki ndicho kilichotokea kwenye kesi unayoizungumzia. Kwa picha inayoonekana, inawezekana washtakiwa wawili hawakuwa na kesi ya kujibu na Hakimu aliamini ndugu yako anayo kesi ya kujibu. Huu si mwisho wa kesi kwa ndugu yako kwa sasa anaweza kuanza utetezi wake. Lakini kuwa na kesi ya kujibu haimaanishi kwamba ndugu yako ana hatia. Kesi bado haijaisha kwa rafiki yako.

## Mwendesha Mashtaka anakubali Dhamana, Hakimu anakataa

**Mdogo wangu aliletwa mbele ya Mahakama ya Hakimu Mkazi ambapo alisomewa hati ya mashtaka. Mwendesha Mashtaka hakuweka pingamizi dhidi ya dhamana lakini Hakimu alikataa kutoa dhamana bila sababu yoyote. Je mwisho wa siku si atamtia hatiani mtuhumiwa? Je, nifanye nini?**

*26 Aprili 2012*

Kwanza kabisa nikutaarifu kwamba kupewa au kutopewa dhamana na mahakama inayosikiliza shauri lako haimaanishi kwamba mtuhumiwa atakuwa na hatia au kuachiliwa huru. Kukataliwa au kutolewa kwa dhamana katika kesi ya jinai haina uhusiano na matokeo ya kesi. Kama mtuhumiwa kuwa huru au kuwa na hatia katika kesi ya jinai inategemea na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka na utetezi.

Katika kesi yoyote ya jinai iwapo dhamana itakubaliwa au kukataliwa ni uamuzi wa mahakama yenyewe ambapo inategemea chanzo na mazingira ya kesi husika. Hata kama upande wa mashtaka haujaweka pingamizi juu ya dhamana, dhamana haitolewi moja kwa moja. Bado haujataja ndugu yako ameshtakiwa kwa kosa lipi; katika hali yoyote, Hakimu ana mamlaka ya kukataa kutoa dhamana kwa sababu mbalimbali. Kama unafikiri kwamba amri ya mahakama haikuwa sawa basi unaweza kukata rufaa dhidi ya amri hiyo katika Mahakama Kuu. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi kulingana na mashtaka dhidi ya mtuhumiwa.

## Vitisho vya kutenda Kosa

**Nyumba yangu ilichomwa moto wakati nimesafiri. Polisi bado hawajamkamata mtu ambaye hapo awali alitishia kuchoma nyumba yangu moto na ambaye ni dhahiri ana la kujibu kwa kitendo hicho mahakamani. Nifanye nini ili kuhakikisha mtu huyu anashtakiwa? Nimepewa taarifa kwamba kaka wa mtuhumiwa aliyechoma nyumba yangu ameshaongea na polisi ndiyo maana wanachelewa kumpeleka mahakamani.**

*12 Aprili 2010*

Kwanza kabisa tunataka kukueleza kuwa polisi hawachukui kila kesi inayo ripotiwa kwao na kupeleka mahakamani bali kwa kesi ambazo zina uthibitisho wa ushahidi. Pia madai ya kuwa ndugu wa mtuhumiwa ameongea na maofisa wa polisi ili kuepusha wasimpeleke mtuhumiwa mahakamani ni madai tu ambayo labda kama una uthibitisho

hayawezi kuwa na umuhimu wowote .

Nirudi tena katika suala lako, kama ilivyojionesha awali, vitisho pekee haviwezi kuwa ushahidi kwamba mtu ambaye alitamka vitisho katika siku za nyuma ametenda kosa. Huenda kuna uwezekano kuwa alitenda kosa lakini hiyo sio hitimisho la kusema alitenda kosa. Lazima kuwe kuna kitu dhahiri zaidi ya kitendo cha kutishiwa kuonesha kuwa mtuhumiwa ametekeleza tishio lake. Katika kesi yako, kwa mfano, bado haujatuambia kama kuna mashahidi ambao wanaweza kuthibitisha madai yako kuwa mtuhumiwa ndiye mtu aliyechoma moto nyumba yako. Sababu yawezekana mtuhumiwa hajapelekwa mahakamani labda kwa sababu ushahidi dhidi yake labda ni dhaifu. Kwa bahati mbaya hatuna taarifa za kutosha za ushahidi uliowasilisha polisi kuweza kutupa mwongozo zaidi. Katika hali yoyote unaweza kuwasilisha malalamiko yako kwa barua kwa Mwendesha Mashtaka Mkuu katika kanda yako aweze kuingilia kati au kushughulikia suala lako.

## Kushindwa kujibu Madai Kinzani

**Mahakama imetoa hukumu dhidi yangu kwa kisingizio kwamba sikujibu madai kinzani yaliyotolewa na mshtakiwa katika utetezi wake dhidi ya kesi yangu licha ya ukweli kwamba kesi yangu bado haijaamuliwa. Kwa nini niteseke wakati mimi ni mdai? Naweza kufanikiwa kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu wa upande mmoja?**

*15 Machi 2010*

Madai yaliyotolewa na mshtakiwa katika utetezi wake dhidi ya mdai katika lugha ya kisheria yanaitwa 'madai kinzani' (counter claim). Madai kinzani yana vigezo na mfanano kama wa hati ya madai. Madai kinzani ni taarifa ya madai inayotolewa na mdaiwa dhidi ya mdai kwenye kesi ya mdai. Madai ya mdaiwa sio lazima yawe sawa na ya mdai au yatokane na tukio hilohilo. Kwa kuwa madai kinzani ni shauri kinzani, sheria inamtaka mtu huyo (mdai) ambaye madai kinzani yameelekezwa dhidi yake kujibu ndani ya muda uliowekwa na sheria ambapo kwa kawaida ni siku ishirini na moja. Kushindwa kuwasilisha utetezi wa madai kinzani inaipa nguvu mahakama kutoa hukumu dhidi ya aliyeshindwa kujitetea ikiwemo hukumu ya upande mmoja kutegemea na aina ya madai ya wote wawili, yaani mdai na mdaiwa.

Iwapo unaweza kufanikiwa kukata rufaa dhidi ya hukumu ya upande mmoja iliyotolewa dhidi yako au la, itategemea pia na maelezo na hoja za kisheria zinazohusiana na madai kinzani yalivyo. Hata hivyo kiutaratibu unahitaji kufanya maombi mahakamani ili kuweka kando hukumu iliyotolewa upande mmoja. Uwezekano wa kufanikiwa katika maombi hayo itategemea na sababu utakazotoa kwa nini ulishindwa kujibu madai kinzani.

## Kunyang'anywa Pasipoti

**Nasafiri kwenda China kila baada ya wiki chache kununua nguo za kike. Katikati ya mwezi Septemba nilikamatwa kwa kutaja bidhaa kidogo wakati wa kuwasili na kughushi ankara ambapo ni kawaida nchini Tanzania. Sioni tatizo lolote katika hili kwa kuwa mabadiliko ya thamani ya ankara ni kawaida hapa. Baada ya kukamatwa nilipelekwa kituo cha polisi na nilikaa huko kwa siku zote za mwisho wa juma. Wiki iliyofuata nilishtakiwa katika Mahakama ya Kisutu na niliwekewa dhamana. Kama sharti la dhamana, Hakimu alidai niweke pasipoti yangu kwake kama amana. Hata hivyo, kutokana na hali ya biashara yangu nahitaji kusafiri sana. Je nifanye nini? Je mahakama haiwezi kunirudishia pasipoti yangu ili niweze kusafiri kwa muda? Napata hasara kwenye biashara zangu kutokana na hali hii. Tafadhali nisaidie.**

*5 Aprili 2010*

Mtu yeyote anayetuhumiwa kufanya uhalifu huchukuliwa hana hatia hadi hatia itakapothibitika katika mahakama yenye mamlaka. Mtu kama huyo anayeshtakiwa kwa uhalifu ana haki ya dhamana labda kama mtuhumiwa ameshtakiwa kwa makosa ambayo hayana dhamana kama vile mauaji, uhaini na wizi wa kutumia silaha.

Dhamana ni kumuweka huru mtu aliyekamatwa au kufungwa, kwa kuwekewa dhamana itakayomfanya kuhudhuria mahala na siku husika atakayohitajika. Katika kutoa dhamana kwa washtakiwa mbali na dhamana iliyowekwa kwa kuwa au kutokuwa na wadhamini kwa kuhakikisha usalama wa kutosha kwa ajili ya kuonekana kwake mahakamani, mahakama pia inaweza kuweka masharti ya lazima kwa mtuhumiwa kusalimisha pasipoti yake au hati yoyote ya kusafiria na kuamuru mtuhumiwa kusalia katika eneo fulani. Mbali na masharti hayo, mahakama pia inaweza kuhitaji mshtakiwa kuripoti katika kituo cha polisi au mamlaka nyingine katika eneo la makazi yake au kuacha kutembelea eneo fulani au majengo au kushirikiana na watu fulani na hali nyingine yoyote ambayo mahakama itaona sahihi kuweka kwa mtuhumiwa. Sharti la kusalimisha pasipoti na hati nyingine za kusafiri ni kuhakikisha kwamba mtuhumiwa anahudhuria mahakamani katika tarehe zilizopangwa. Tunashauri kwamba katika tarehe ya kusikiliza kesi wakili wako afanye maombi kwa ajili ya kuachiwa pasipoti na kutoa sababu za kumshawishi Hakimu kwamba utahudhuria siku zote zitakazopangwa kusikilizwa.

Tunapenda kuongezea kwamba kugushi ankara ni kosa la jinai na utetezi wako kuwa ni jambo la kawaida au ilikuwa ndio mazoea ya kibiashara hauna msingi kisheria. Tatizo ambalo linakukabili ni kutokana na matendo yako mwenyewe, tusionekane kama wahubiri, ila yafaa kusema unapaswa kuachana na tabia hiyo.

## Kunyimwa Dhamana kwa misingi ya Usalama

**Kaka yangu ameshtakiwa kwa kosa la jinai katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mara, mjini Musoma. Mwendesha Mashtaka amefanikiwa kuiomba Mahakama kusogeza tarehe iliyopagwa na mahakama ili kuepuka kutoa dhamana kwa mtuhumiwa kwa sababu usalama wa mtuhumiwa utakuwa hatarini kama atapatiwa dhamana. Je, hii ni sababu nzuri na ya msingi ya kunyimwa dhamana?**

*22 Machi 2010*

Dhamana ni haki ya mtuhumiwa. Hata hivyo mahakama imepewa nguvu ya kuwa na mamlaka ya kuamua kukataa au kukubali kutoa dhamana kwa mshtakiwa kulingana na aina ya kosa ambalo mtuhumiwa huyo anashitakiwa nalo. Chini ya kifungu cha 148 (5) (d) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai mahakama imepewa mamlaka ya kumweka mtuhumiwa kizuizini kwa ajili ya usalama wake kama ikionekana kuna ulazima wa kufanya hivyo. Kabla ya mahakama haijatumia mamlaka hayo ni wajibu wa upande wa mashtaka kuiridhisha mahakama kwa sababu za uhakika kwamba usalama wa mtuhumiwa utakuwa hatarini kama ataachiwa kwa dhamana. Hofu ambazo hazina mashiko au tuhuma za polisi kwamba usalama wa mtuhumiwa utakua hatarini hauwezi kuzingatiwa. Kipimo sio kama itakuwa bora zaidi kwa mtuhumiwa kuwekwa kizuizini kwa ajili ya usalama wake bali iwapo ni muhimu kwamba mtuhumiwa lazima awekwe kizuizini kwa ajili ya usalama wake. Upande wa mashtaka lazima watoe ushahidi madhubuti wa kuonesha wazi kuwa usalama wa mtuhumiwa upo hatarini na taarifa kama hizo lazima zithibitishwe.

Katika kesi yako hujatuambia kosa linalomkabili kaka yako wala maelezo ya upande wa mashtaka yaliyotolewa

mahakamani ili kutuwezesha kutoa maoni yetu. Hata hivyo kama unaona uamuzi wa mahakama haukuzingatia taarifa zilizothibitika unaweza kupeleka maombi Mahakama Kuu.

## Kufutwa kwa Shauri licha ya Barua za Mawakili za Kuahirishwa kwa Kesi

**Nimekuwa katika shauri la madai kwa miaka miwili sasa. Hivi karibuni Hakimu anayesikiliza kesi yangu ameifuta licha ya mawakili wote kwa pamoja kuiandikia barua mahakama ili kuahirisha kesi. Je hii ni haki? Naweza kufanikiwa kupinga amri ya kufutwa kwa kesi yangu?**

*29 Machi 2010*

Hatuwezi kukupa mwongozo wa kina kwa kuwa hatuna ukweli wa kwa nini mawakili walitaka kuahirisha kesi na kwa nini Hakimu alikataa kukubaliana na ombi lao.

Kwa vyovyote itakavyokuwa, tunapenda kukuonesha sheria. Sheria ya Mwenendo na Kanuni za Madai Sura ya 33 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002 imetoa mamlaka yenye nguvu kwa mahakama kujisimamia wakati kuendesha kesi, ikiwa ni pamoja na nguvu ya kuahirisha au kutokuhairisha kesi. Ingawa barua ya ridhaa ya mawakili inaweza kuwa sababu ya kuzingatiwa katika maombi ya kuahirisha kesi, ridhaa hiyo haiwezi moja kwa moja kusababisha kuahirishwa kwa kesi . Jaji wa Mahakama Kuu siku moja aliwahi kusema 'katika kesi, si jukumu la mahakama kuwa chini ya shughuli za mawakili wapambanao katika kesi'.

Unaweza kuamua kukata rufaa na mafanikio ya rufaa yako yatategemea mazingira ya kesi yako na hasa zaidi juu ya sababu zilizosemwa katika barua ya mawakili kwa umoja wao ya kuomba kuahirishwa kwa kesi. Pia nikufahamishe kuwa mahakamani kwa sasa wamekua wakali kuruhusu kuahirisha kesi kwa sababu kesi zinazidi kuchelewa na ni hasara kwa upande ambao unatafuta haki.

## Kupokea Wito wa Mahakama kwa njia ya Magazeti

**Hivi karibuni nilisoma kwenye gazeti kwamba shauri limefunguliwa dhidi yangu Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kwamba ninatakiwa kutokea na kutoa utetezi wangu. Kwa bahati mbaya nilikuwa nimetingwa na mambo ya ofisi na hivyo sikuweza kuonekana. La kushangaza nimepewa karatasi za mahakama kuonesha kwamba hukumu ya upande mmoja imepitishwa dhidi yangu licha ya mawasiliano yote niliyofanya na Hakimu Mfawidhi ambapo nilimueleza kwa uwazi kuwa nitaiambia mahakama ni muda gani naweza kufika mbele yake. Pamoja na uwazi wangu kwa mahakama hicho ndicho kilichotokea. Je hii ni haki?**

*22 Machi 2010*

Kuitwa na mahakama siyo makubaliano kama ya saluni ambayo unaweza kuamua kubadili ratiba. Mahakama inatoa haki na sio lazima ikubali kufuata ratiba yako hasa wakati huna sababu ya msingi unapoiambia mahakama kwamba utakuja bila kuwa na dhamira ya kufanya hivyo.

Kutokana na maelezo ya hapo juu ni wazi kwamba wito wa mahakama uliupata kwa usahihi na hivyo huwezi kudai kwamba ulikuwa hujui kama kulikuwa na kesi inaendelea mahakamani. Wakati kesi inapofunguliwa na wito unapopokelewa na mdaiwa utaratibu ni kwamba mdaiwa au wakili wa mdaiwa anatakiwa kuandika maelezo ya utetezi wake kama ilivyo ainishwa kwenye Sheria ya Mwenendo na Kanuni za Madai Sura ya 33 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002. Wewe ndiyo wa kulaumiwa kwa hali uliyonayo sasa. Unaweza tu kuokoa hali hii kwa kufanya maombi mahakamani ya kuweka kando hukumu ya upande mmoja kama unaweza kuonesha sababu nzuri za kwa nini haukuonekana mahakamani wakati

umeitwa. Maombi ya kuweka kando hukumu ya upande mmoja unatakiwa ufanye ndani ya siku thelathini kutoka siku ambayo umepata hiyo hukumu ya upande mmoja vinginevyo itatakiwa kuomba muda wa nyongeza ili kufanya maombi hayo. Tunapendekeza utafute ushauri wa kisheria.

## Usuluhishi katika Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi

**Niliingia mkataba na wasambazaji wa kigeni ambapo kifungu cha usuluhishi kinasomeka "Kanuni za ICC Paris". Nilisaini mkataba na kwa sasa tupo katika msuguano. Nawezaje kupeleka suala hili katika Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi na namna gani mchakato wake unafanya kazi? Je, gharama zake zikoje na inawezakana kwa mtanzania kupeleka suala hilo ICC? Je, siwezi kusuluhisha nikiwa hapa Tanzania?**

*29 Machi 2010*

ICC, ni Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi, iliundwa mwaka 1923. Mahakama hii inajumuisha wanachama kutoka nchi tisini tofauti. Yenyewe haiwezi kutatua migogoro lakini husimamia michakato ya usuluhishi kutoka mwanzo mpaka utoaji wa tuzo na utekelezaji wake. Tuzo zote za ICC zinakaguliwa na Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi (ICC).

ICC haihitaji au haina fomu maalum ya kupeleka maombi chini ya kanuni zake. Lengo ni kukidhi mabadiliko ya usuluhishi hasa ukizingatia kwamba ICC ina uwanda wa kimataifa. Ibara ya 4 ibara ndogo ya 3 ya sheria yake inaeleza kwamba: "Ombi la usuluhishi ICC pamoja na mambo mengine litakuwa na taarifa zifuatazo: majina ya pande zote mbili kwa ukamilifu, maelezo na anwani za pande zote mbili, maelezo ya chanzo na mazingira yaliyopelekea mgogoro; maelezo ya maombi yanayoombwa ikiwemo kiasi cha fedha kinachoombwa na mdai; mikataba husika na hasa makubaliano ya usuluhishi; kila maelezo muhimu kuhusu idadi ya wapatanishi na chaguo lao kwa mujibu wa masharti ya ibara za ICC na uteuzi wowote wa msuluhishi unaotakiwa na maoni yoyote kuhusu mahali pa usuluhishi, sheria itakayotumika na lugha itakayotumika.

Kwa mujibu wa ICC pande zinazokinzana zinapaswa kufahamu kwamba: mahala pa usuluhishi patapangwa na mahakama isipokuwa kama itakubalika vinginevyo na pande husika; sheria husika itakayotumika ni zile ambazo Mahakama ya Usuluhishi itaona zinafaa kutumika labda kuwe na makubaliano ya pande zote mbili; na kwamba lugha ya usuluhishi mahakama yenyewe itaamua ikionekana hakuna makubaliano ya pande zote mbili.

Msimamo na maoni ya hoja hizi ya kila upande yatawekwa kwenye Maombi na Majibu ambayo yanaweza kuwa sehemu ya makubaliano kwenye moja au zaidi. Kwa yale ambayo pande zote mbili hazikukubaliana yatazingatiwa na mahakama au baraza la usuluhishi wakati wa kufanya maamuzi ya hoja hizo.

Unatakiwa utambue kwamba kwa kila ombi la usuluhishi linatakiwa kuambatana na malipo ya awali ya Dola za Marekani 2,500 ambazo hazitarejeshwa. Uzoefu wetu ni kwamba ICC inafanya kazi kwa ufanisi lakini pia ni ghali sana. Kwa ujumla inategemea ni kiasi gani kinachogombaniwa ili uweze kuona kama inafaa kukifuatilia.

Kuhusu kama unaweza kufanya usululishi Tanzania au la jibu letu ni hapana. Ulikuwa na nafasi ya kusoma mkataba ambapo ulikubaliana na kipengele hiki cha ICC. Haiwezekani kwa ombi lako la kufanya usuluhishi nchini Tanzania kukubaliwa labda kama upande mwingine utaridhia ombi hilo.

## Mahakama kujiamulia yenyewe

**Je mahakama, kwa kujiamulia yenyewe inaweza kumwita shahidi ingawa pande zote**

**mbili hazijaomba shahidi kutoa ushahidi wake? Kwenye kesi niliyofungua, nilishtuka kuona kwamba Jaji alituma wito kwa baadhi ya watu waliotajwa wakati kesi ikiendelea kusikilizwa ambapo hakuna mwanasheria wa upande wa mdaiwa wala mdai aliyehitaji kumtumia. Je, huu ni utaratibu sahihi?**

*8 Machi 2010*

Kwa ujumla ni wajibu wa upande wa mdai kuthibitisha kesi yake. Kwa kawaida mahakama huita mashahidi kama ikiombwa na pande husika na mahakama haiwezi kulaumiwa kushindwa kumwita shahidi. Hata hivyo mahakama ikiona kuwa kumwita shahidi fulani kutapelekea kutendeka kwa haki, inaweza kumuita shahidi huyo ili kuthibitisha au kukanusha ukweli fulani yenyewe bila kuombwa na upande wowote, isipokuwa kila upande utakuwa na haki ya kuhoji shahidi huyo aliyeletwa na mahakama.

## Kukata Rufaa kwa kukubali Kosa

**Je, sheria inasemaje kuhusu mtu ambaye amekubali kosa mahakamani na kukata rufaa kwamba hakukubali kosa kwa madai kuwa hakuelewa hati ya mashtaka? Kumekuwa na matukio mawili ya kesi kama hizo katika mkoa wa Mbeya ambayo nimeyaona.**

*15 Machi 2010*

Mtu aliyekubali kosa ana haki ya kubadili kwa kukanusha kosa hilo kabla ya hukumu. Kwa ujumla, hati ya mashtaka ikisomwa, kuelezewa na kueleweka kwa mtuhumiwa, na akakiri kosa hawezi kukata rufaa dhidi ya hatia. Hatuna maelezo yote yanayohusu kesi hiyo na jinsi gani alikubali kosa. Mahakama nchini Tanzania imesema kwamba kama kuna uwezekano wa kumtia mtu hatiani kwa kukiri kosa, ni muhimu mshtakiwa aelezwe kwa uwazi kila kipengele kwenye hati ya mashtaka na aulizwe kama anakubali au la kwa kila kipengele. Kwa mfano kama mtu aliulizwa kama anakubali kosa au la na akasema 'ni kweli', hiyo haimaanishi, kisheria, kwamba mtuhumiwa amekiri kosa. Tunashauri kupata usaidizi wa wakili ili kukusaidia kuamua juu ya uwezekano wa kufanikiwa katika rufaa yako.

## Ushahidi wa Kimazingira wasababisha kuachiwa kwa Mtuhumiwa

**Ninamiliki baa ambayo inafanya kazi mpaka usiku wa manane. Mwaka jana mhasibu wangu ambaye alikuwa mtu pekee aliyebaki kwenye baa kufanya hesabu za mauzo na kufanya majumuisho ya fedha zote za mauzo, alitoa taarifa ya upotevu fedha shilingi milioni 2. Hakuna mtu mwingine yeyote zaidi ila ni yeye ndiye aliyechukua hizo fedha. Hakuna kufuli wala sefu/kasiki iliyovujwa. Funguo zote za chumba cha kutunzia fedha na funguo za chumba cha kutunzia fedha anazo yeye mhasibu. Nilitoa taarifa polisi na alishtakiwa kwa kosa la wizi. Kwa sasa mhasibu ameachiwa huru. Je hii ni haki? Bima yangu pia inasita kunilipa fidia? Je nifanye nini?**

*1 Machi 2010*

Kwenye kesi za jinai kiwango cha uthibitisho ni kuthibitisha pasipo kubakiza shaka. Kwa hiyo kama wanasheria wa utetezi wanaweza kuonesha shaka hata kidogo kwenye fikra ya Hakimu, kwamba kuna uwezekano, hata kama ni mdogo sana, kuwa mtuhumiwa sio aliyefanya kosa hilo, mahakama itamwachia huru.

Katika kesi yako inaonekana kwamba upande wa mashtaka ulikua unategemea ushahidi wa kimazingira ambao si ushahidi wa moja kwa moja, ambao haukuweza kumshawishi Hakimu kuwa mtuhumiwa alitenda kosa na hivyo ikamuachia huru.

Kuhusu bima ya wizi, ni taratibu za kibima kwamba lazima wizi utokee ndipo uweze kufidiwa. Kwa kawaida, kwenye bima ya wizi kama wizi umefanywa na mwajiriwa wako bima haiwezi kulipa. Wizi wa mfanyakazi

unafidiwa chini ya bima ya uaminifu (fidelity insurance). Katika mazingira yako kuthibitisha wizi itakuwa changamoto kwa vile hakuna uvunjifu uliofanyika. Sehemu zote za kutunzia fedha na milango imekutwa iko salama ikionyesha kuwa ni wizi wa ndani au mahesabu yamekosewa. Tunakushauri wasiliana na wakili wako kwa ushauri zaidi kuhusu aina ya bima uliyokuwa nayo.

## Wazee wa Baraza kwenye Kesi

**Mimi ni mwanafunzi wa sheria na nilihudhuria kesi ya jinai katika Mahakama Kuu mjini Dodoma. Wakati kesi inaendelea niligundua kuwa Jaji hakuwapa nafasi wazee wa baraza kuuliza maswali kwa mashahidi. Je, hii haiwezi kutishia utoaji haki?**

*22 Februari 2010*

Wajibu wa wazee wa baraza kwenye kesi ni kumsaidia Jaji kwa mujibu wa Sheria ya ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na kwa kufanya hivyo wanaweza kuuliza maswali. Wazee wa baraza hawawezi kuzuiliwa kuuliza maswali ingawa Jaji ana uwezo wa kuzuia uulizwaji wa maswali ambayo yataonekana ni ya upendeleo au yasiyofaa kutokana na mada husika.

Kutokupewa nafasi kwa wazee wa baraza kuuliza maswali kwa mashahidi inamaanisha kuwa wazee wa baraza walitengwa kushiriki kiufanisi kwenye kesi na kushindwa kumsaidia Jaji. Huu si utaratibu na katika rufaa inaweza kuamuliwa kesi ianze upya.

## Maswali yasiyohusika kwa Mashahidi

**Niliitwa kama shahidi katika kesi fulani. Kiukweli ilinisumbua kwa sababu upande wa wakili wa utetezi alikazania kuuliza maswali ambayo hayahusiki. Hakimu hakuonesha weledi wake na alisisitiza mimi kujibu baadhi ya maswali na kuongeza maswali zaidi mwenyewe. Tunawezaje kuhakikisha kuwa haki inatendeka?**

*15 Februari 2010*

Wakili wa utetezi hujulikana kwa kukuuliza mashahidi maswali magumu ili kupima uaminifu wa shahidi yeyote. Na hivyo ndivyo wakili wa upande wa utetezi amefundishwa kufanya. Bila kujua ni maswali gani yaliyokuwa yanaulizwa hatuwezi kusema kama yalikuwa sahihi au la.

Pia, hakuna ubaya kwa Hakimu kukuliza maswali labda kama alikuwa anakulazimisha kujibu kwa namna ambayo wewe hukuipenda.

## Mabadiliko ya kukiri Kosa kabla ya Hukumu

**Kijana wa miaka 17 mwenye ugonjwa wa akili alishtakiwa kwa kumbaka binti yangu mwenye umri wa miaka 15. Wakati alipofikishwa kwenye Mahakama ya Watoto alikiri kufanya kosa na Mahakama ya Watoto ilikubali kukiri kwake. Aliwekwa mahabusu wakati akisubiri ripoti ya matibabu. Siku iliyofuata aliomba kubadili kukiri kwake kosa na Hakimu anayeendesha kesi akakubali. Kisha akarekebisha kumbukumbu zake na kuwaamuru upande wa mashtaka kuleta mashahidi. Je, kiutaratibu hii ni sawa? Inawezekana vipi mtu akakiri kosa halafu tena akakana kosa?**

*8 Februari 2010*

Katika kesi za jinai tuhuma zinasemekana zimekamilika wakati mtuhumiwa anapokiri. Inaweza kuwa kwa kukubali kosa au kukana kosa. Kukiri kosa ni kukubali kwa mtuhumiwa kwa kosa analotuhumiwa nalo. Pale ambapo mtuhumiwa anakubali kosa mahakama itaendelea na utaratibu wa kumtia hatiani. Pia ileweke kuwa kumtia mtu hatiani sio mwisho wa kesi za jinai kwani kesi ya jinai zinaisha pale mahakama inapotoa hukumu. Hata hivyo, sheria haimzuii mtuhumiwa kabla ya hukumu kubadili ungamo lake la kukiri kosa na kukataa kosa. Wakati hili linatokea mahakama husika inatakiwa kukubali mtuhumiwa kukananusha kosa alilokubali, kutokufanya hivyo itapelekea

mwenendo wote wa kesi kuonekana ni batili. Wakati tunakuhurumia kwa kitendo kilichofanyika ambacho si cha kibinadamu kwa binti yako, hatukubaliani na wewe kwamba utaratibu uliotumiwa na mahakama kwenye kesi yako haukuwa sahihi. Hata hivyo, kubadili ungamo hakumuondolei hatia mtuhumiwa, sheria itachukua mkondo wake.

## Kutiwa Hatiani kwa kuzingatia Ushahidi wa Mtu mmoja

**Mwezi wa tatu mwaka 2009 nilishtakiwa kwa kosa la kujipatia kiasi kikubwa cha fedha kwa njia ya udanganyifu. Shauri liliendeshwa na kukutwa na hatia kwa kuzingatia ushahidi wa mtu mmoja na nilipelekwa jela kwa kifungo cha miaka mitatu. Je, inawezekana vipi mimi kutiwa hatiani kwa kuzingatia ushahidi wa mtu mmoja?**

*1 Januari 2010*

Kutokana na uzoefu wetu kama mawakili na wanasheria wenye mafunzo, tukupe pole kwa kukufahamisha kwamba hakuna namna yeyote mtu anaweza akafanikiwa kupinga uamuzi wa mahakama kwa sababu ilifanya uamuzi wake kwa kuzingatia ushahidi wa mtu mmoja, la sivyo aoneshe kwamba ushahidi wa upande wa mashtaka kwa ujumla wake haukutosheleza kumtia hatiani mtuhumiwa au katika kumtia hatiani mahakama ilitumia kanuni ambayo sio sahihi ya kisheria.

Kama ilivyo katika mamlaka nyingine nyingi, sheria yetu ya ushahidi ipo wazi, cha muhimu si idadi ya mashahidi bali ni uzito wa ushahidi.

Labda kama ushahidi wa shahidi pekee ni dhaifu au kama unahitaji ushahidi shirikishi, kitu ambacho hatukioni kwenye kesi yako, hakuna mahakama yoyote ya rufaa inaweza kutengua uamuzi wa mahakama ya chini.

Kama utaona suala lako ni tofauti na tulilozungumza hapa, tunakushauri kwa kuzingatia ukomo wa muda, ukate rufaa dhidi ya uamuzi wa mahakama iliyosikiliza kesi yako.

## Pingamizi la Awali kwenye Mkataba wa Pango

**Mwanasheria wangu aliweka pingamizi la awali juu ya mkataba wa pango kwa madai kuwa sijawahi kupanga na kama mpangaji, sikuwahi saini mkataba wa kupanga. Ananiambia kwamba hii itaiondoa kesi. Je, hii ni sahihi? Je, unadhani nalazimika kuendelea?**

*25 January 2010*

Umeeleza baadhi ya pointi za kuvutia sana. Kwanza, baada ya kukubali kwenye swali kuwa wewe ni mpangaji halafu unaeleza tena kwamba hakukuwa na mkataba wa pango. Huwezi kusema hakukuwa na mkataba kabisa kwa sababu ili kuwe na mpangaji ni lazima kuwe na mwenye nyumba. Hatuna uhakika na mawazo yako.

Kwa maoni yetu, pingamizi la awali halitafanikiwa kwa sababu kwa kawaida pingamizi huwekwa kutokana na sababu za kisheria ambapo inachukuliwa kwamba maelezo yote yaliyotolewa na upande wa pili ni sahihi. Haiwezekani kuweka pingamizi kama kuna maelezo yanatakiwa kuthibitishwa. Katika kesi yako maoni ya mwanasheria wako ni kwamba mkataba wa kupanga haupo. Upande wa pili unaamini kwamba mkataba upo. Kwa kuwa kuna haja kwa mahakama kuangalia kwa undani kama mkataba wa upangaji upo au la pingamizi la awali haliwezi kusimama.

## Athari ya kukiri Kosa kwenye Adhabu

**Mwezi Januari mwaka 2009, mimi na rafiki yangu tulishtakiwa kwa kosa la wizi wa kutumia silaha katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam. Wakati nimeitwa kukiri, nikakiri kosa na hapohapo nilitiwa hatiani na kuhukumiwa kwenda jela kwa kipindi cha miaka thelathini. Kisha kesi**

**iliendelea dhidi ya rafiki yangu na mwisho wa kesi pia alipatikana na hatia na kuhukumiwa jela kwa kipindi cha miaka thelathini. Je, adhabu ya kifungo cha miaka thelathini jela dhidi yangu ni haki? Je, sikuwa na haki ya kupunguziwa adhabu kutokana na kukubali kosa? Je, naweza kufanikiwa kukata rufaa dhidi ya adhabu hiyo?**

*18 Januari 2010*

Ni kanuni inayotambulika kwamba, mtuhumiwa anaeonesha kujutia kosa lake wazi kwa kukiri kufanya kosa anastahili kupunguziwa adhabu anayostahili kupata kulingana na kosa lake; mhalifu kuonesha msisitizo kuwa kesi iendelee kusikilizwa haimaanishi kwamba adhabu yake iwe kubwa kama inavyotakiwa. Hata hivyo, kuruhusu kupunguziwa adhabu kwa kujutia kosa ni uamuzi binafsi wa mahakama na hauji moja kwa moja baada ya kukiri kosa. Wakati mwingine mahakama inaweza kuzingatia kiwango cha majuto ya mhalifu na kufanya punguzo kubwa zaidi la adhabu. Kwa mfano, katika kesi ambapo mkosaji hana pingamizi kwenye kesi kwa upande wa mashtaka ambayo wana ushahidi wa kutosha au katika kesi ya kuua bila kukusudia ambapo mkosaji kwa undani anajutia mauaji kutokana na sababu za ulevi.

Katika hali yako mambo ni tofauti kidogo. Wizi wa kutumia silaha ni kosa lililopangwa yaani makosa ambayo adhabu yake imepangwa na sheria. Mahakama hawana hiari ya kutoa punguzo lolote la adhabu kwa makosa yaliyopangwa. Kwa kuwa ulikiri, hatuna ushauri wa kukupa ila kukuambia kutumikia adhabu yako ya kifungo.

Na kama unaweza kukata rufaa au la, Sheria, yaani Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inazuia rufaa dhidi ya kutiwa hatiani kwa mtu aliyekiri kosa isipokuwa kama kukiri kwake hakukuwa wazi na adhabu iliyotolewa ilikuwa kali. Labda kama unatuambia haukuelewa ulichokubali, tunasikitika kukwambia kuwa adhabu uliyopewa ni halali kisheria. Wizi wa kutumia silaha ni kosa kubwa na sheria inaichukulia kwa uzito sana.

## Ukomo cha Muda wa Kushtaki

**Mimi ni mfanyabiashara ambaye nilikuwa namiliki kampuni ya usafiri wa watalii nchini Tanzania. Kwa miaka kumi iliyopita nimekuwa nikiishi nchini Sweden. Mjomba wangu ambaye ni mbia mwenzangu alikuwa muangalizi wa biashara hii mpaka ilipokufa kwa sababu ya kupungua kwa idadi ya watalii. Kwa sasa nimerudi Tanzania na nimegundua kwamba kampuni imeshindwa kwa sababu ya udanganyifu mkubwa uliofanyika kwenye kampuni. Na sasa nataka kurudisha fedha ambazo mjomba wangu amehusika katika hili. Wanasheria wangu wamenitaarifu kuwa kwakuwa hili ni suala la kimkataba sitaweza kushtaki sababu muda wa kikomo cha kushtaki ulishapita. Ni sheria gani hii? Tafadhali naomba unishauri jinsi gani naweza kurudisha fedha.**

*18 Januari 2010*

Ni Sheria ya Ukomo wa Mashtaka Sura ya 89 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002 ndiyo inaeleza ni muda gani unaweza kufungua mashtaka kudai haki yako au ni muda gani unakuwa huwezi kudai kwa kupitwa na muda. Ni kweli kuwa Sheria ya Ukomo wa Mashtaka imeweka kizuizi kwa kipindi cha muda wa miaka sita kwa shauri la mikataba isipokuwa tu kama itaelekeza vinginevyo.

Hata hivyo katika kesi yako hili ni suala la udanganyifu hivyo kikomo cha kushtaki kwa kesi ya mkataba hakiwezi kuanza hadi muda umegundua udanganyifu. Hivyo upo ndani ya muda ambapo unaweza kushtaki kulingana na mkataba wako.

Pia kumbuka kwamba kwenye makosa ya jinai kama vile udanganyifu, hakuna kikomo cha muda ni kama mfumo wa kushughulikia

haki katika makosa ya jinai unavyotaka. Hatuoni kizuizi chochote cha kushindwa kushtaki ili urudishe fedha yako.

## Usuluhishi ni nafuu zaidi kuliko Mahakama

**Nipo kwenye mazungumzo ya mkataba na mwenza kwenye mkataba huo anataka kuingiza kifungu cha usuluhishi kwamba ikitokea mgogoro baina yetu utatuliwe kwa njia ya usuluhishi kwa kuwa ni njia nafuu. Nina wasiwasi kwa kuwa bado hatujasaini mkataba na mwenza katika mkataba haamini kuhusu hilo. Je, unafikiri kuna ulazima wa kuendelea nalo?**

*11 Januari 2010*

Mbadala sahihi wa mahakama ni kwenda kwenye usuluhishi. Usuluhishi unatoa fursa kwa pande mbili katika mkataba kuchagua jukwaa huru na baraza huru la usuluhishi. Aidha, tuzo inayotolewa na baraza la usuluhishi huweza kutekelezwa dhidi ya upande ulioshindwa sio tu mahala usuluhishi ulipofanyika lakini pia kimataifa chini ya vifungu vya mikataba kama vile mkataba wa New York. Ingawa usuluhishi kwa ujumla ni wa haraka zaidi kuliko utatuzi wa mahakamani, kwa maoni yetu usuluhishi ni gharama zaidi kuliko mahakamani. Kuna ada mbalimbali ambazo zinahitaji kulipwa - ada ya wasuluhishi, kodi ya ukumbi wa usuluhishi, gharama za usafiri kwa wanasheria wanao shughulikia kesi na ada ya mwanasheria. Kwa haya yote yanafanya usuluhishi kuwa ghali zaidi kuliko kwenda mahakamani. Faida kubwa ya usuluhishi ni kwamba mafanikio hupatikana kwa haraka. Hasara nyingine ya usuluhishi ni pamoja na mamlaka madogo ya wasuluhishi, tuzo zinazokinzana, na kukosa uwezo wa jumla wa kuleta migogoro ya pande zinazokinzana kwa wingi mbele yake. Ubunifu wa wanasheria wanaoufanya wakati wapo mahakamani unapungua kwa kiasi kikubwa ukiamua kufanya usuluhishi.

Mtu anayependekeza kipengele cha usuluhishi kwenye mkataba asitazamwe kwa wasiwasi, isipokuwa labda kama kuna sababu nyingine zinazokufanya kuwa na wasiwasi. Ni vyema kujadili mkataba vizuri mwanzoni badala ya kuanza kutafuta visingizio baadaye.

Hatuwezi kutoa maoni yetu kuwa unapaswa kuendelea na mkataba au la; hayo ni maamuzi ya kibiashara.

## Hukumu ya Kenya kwenye Mahakama ya Tanzania

**Nimeshindwa kesi Mahakama Kuu ya Kenya. Mtekeleza hukumu amesajili hukumu ya Kenya kwenye Mahakama ya Biashara ya Tanzania, ambapo umetolewa wito wa mahakama nioneshe sababu kwa nini mali zangu zisikamatwe ili kukidhi kiasi ninachodaiwa au kwa nini nisishikiliwe kama mfungwa wa madai kama nitashindwa kulipa kiasi ninachodaiwa. Wanasheria wangu wamekata rufaa katika Mahakama ya Rufaa nchini Kenya lakini rufaa yangu bado haijasikilizwa. Kwa kweli naogopa hadi naanza kuhisi nikimbie. Je, unanishauri nifanye nini?**

*4 Januari 2010*

Tunadhani unataka tukushauri juu ya nini cha kufanya mahakamani na sio kama ukimbie au la!

Jambo lako sio gumu kama linavyoonekana. Rufaa ya nchini Kenya inakusaidia. Hiyo ni sababu nzuri ya kuiomba mahakama kwamba usajili wa hukumu uwekwe kando kusubiria rufaa. Na hii inatokana na mantiki ndogo kwamba kesi ya rufaa bado inaendelea nchini Kenya. Tutashangaa sana kama ombi lako halitakubalika.

## Wito haujapokelewa

**Muungwana mmoja aliyedai ametoka Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara alikuja**

**ofisini kwangu miezi sita iliyopita. Alikuwa na baadhi ya karatasi kutoka mahakamani ambapo mimi nilimwambia katibu wangu asizipokee mpaka nitakaporudi. Wakati nafika, yule afisa alishaondoka ofisini kwangu. Je, kuna kitu naweza fanya? Hizo karatasi zitakuwa zinahusu nini?**

*28 Desemba 2009*

Kuna uwezekano mkubwa kwamba mtu huyo alikuwa amebeba wito wa mahakama. Hakuna sheria ambayo inamkataza katibu wako kupokea wito wa mahakama. Miezi sita ni muda mrefu inawezekana kesi iliendelea kusikilizwa upande mmoja dhidi yako.

Tunashauri kwenda mara moja kwenye Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara na ukaangalie masjala kama kuna kesi ilianzishwa dhidi yako, kwenye familia yako au kampuni yoyote ambayo unajihusisha nayo.

## Kuunganishwa kwenye Kesi

**Mimi ni mshtakiwa wa pili katika kesi na sielewi kwa nini nimeunganishwa kwenye kesi. Mimi sio mmiliki wa kipande cha ardhi ambacho ndo chanzo cha kuwepo kwa shauri hili na wala sio jirani na wala sina urafiki na mtu yeyote kwenye kesi hii. Simjui mhusika yeyote kwenye kesi na sina uhakika wa kipi kinaendelea. Je, nifanye nini?**

*14 Desemba 2009*

Hatuna uhakika wa kwa nini unasema hujui sababu za wewe kushtakiwa. Hati ya madai iliyowasilishwa mahakamani itakuwa na maelezo yote pamoja na kwa nini umeshtakiwa. Labda kama kuna kitu ambacho unakificha, inawezekana umeunganishwa kwenye kesi kimakosa.

Hapa kuna makosa ya kumuunganisha mtu kwenye kesi, yaani pale ambapo mtu anaunganishwa kimakosa kama mdai au mdaiwa ikimaanisha kwamba watu wanaunganishwa kama wahusika kwenye kesi ambao hawakupaswa kuunganishwa, ndicho tunachokiona kwenye kesi yako. Unaweza kufanya maombi rasmi mahakamani ya kusitishwa kuwa mdaiwa na kutegemea na sababu unazozitoa mahakama inaweza kutoa maagizo sahihi. Maoni haya hayatakuwa na maana kama kuna taarifa unaficha.

## Zuio linaendelea, Kesi imefutwa

**Nimefungua kesi Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi jijini Dar es Salaam na kupata amri ya zuio la mahakama la kumzuia mshtakiwa kubomoa jengo ambalo mimi ni mpangaji. Jengo linamilikiwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ambao ni wadaiwa katika kesi hii. NHC walikuja na sababu za kimakosa ya kiufundi na kesi ikafutwa. Je, hiyo ni haki? Mwanasheria wangu kanihakikishia kwamba amri ya zuio tuliyopata bado ni halali kwa kuwa imechapishwa na tulipewa kabla. Nifanyeje?**

*7 Desemba 2009*

Zuio ni nafuu inayotolewa na mahakama ambapo mtu anazuiliwa kufanya tendo au kitu fulani. Kuna uwezekano mkubwa amri ya zuio lako ni ya muda kiuhalisia. Kwa kawaida hakuna nafuu ya muda mfupi inaweza kutolewa zaidi ya muda wa nafuu iliyoombwa kwenye kesi ya msingi.

Kama ni haki au sio haki kwa kesi yako kufutwa kwa sababu za kiufundi inategemea na sababu zilizotolewa. Yawezekana hati ya madai ilikuwa na makosa ambayo hayarekebishiki na hivyo kupelekea kufutwa kwa kesi. Kwa vyovyote vile, amri ya zuio la mahakama inakoma pale ambapo kesi yako inapofutwa. Mwanasheria wako anakupotosha kuwa amri ya zuio la mahakama bado ipo. Haijalishi kama imechapishwa au la. Kwa kifupi kufutwa kwa kesi imeipa njia NHC kubomoa jengo lako ikiwa hautaanzisha upya kesi nakupata amri ya zuio lingine la mahakama.

## Mamlaka ya Kukamata unapotuhumiwa kwa Ugaidi

**Maafisa saba wa jeshi la polisi waliovalia mavazi ya kiraia walivamia duka langu na kuanza kupekua. Walidai kwamba wananituhumu kwa kujihusisha na vitendo vya kigaidi kwa sababu nafanya biashara ya uwindaji. Baada ya masaa matano ya kupekua hawakupata chochote. Je, haki zangu ni zipi kisheria? Je, hawakutakiwa kuja na hati ya kupekua au kukamata?**

*14 Desemba 2009*

Sheria ya Kuzuia Ugaidi inaipa mamlaka polisi kumkagua au kuzuia mtu yoyote au kitu chochote kama wana sababu za msingi kutuhumu mtu huyo au kitu hicho kitatumika kufanya kitendo cha ugaidi. Sheria inaruhusu maafisa wa polisi, si chini ya cheo cha Mrakibu Msaidizi, kufanya upekuzi kwa maslahi ya usalama wa umma bila kibali cha upekuzi. Hivyo katika kesi yako, maafisa wa polisi walikuwa na haki ya kufanya upekuzi kama ilivyoainishwa kwamba angalau mmoja wa maafisa wa polisi awe na cheo cha Mrakibu Msaidizi. Si lazima kuwa katika biashara ya uwindaji kwa wao kuhalalisha utafutaji. Inaweza ikamkuta mtu yeyote yule kwenye sekta yoyote ile.

## Matatizo ya Familia kama kigezo cha kutoa Adhabu

**Mwanangu alikutwa na hatia ya kumuibia mwajiri wake na kufungwa jela kwa kipindi cha muda wa miaka mitatu. Mimi ni mjane, mwanangu ni mtalaka na mke wake wa zamani hajulikani alipo. Mwanangu alikuwa mwangalizi wa watoto wawili ambao mimi kwa sasa naanza kuwatunza. Hayo yote alielezwa Hakimu lakini bado alipewa adhabu iliyopita kiasi. Je, kuna njia yoyote anaweza kutumia kupunguza adhabu yake? Tafadhali nisaidie.**

*21 Desemba 2009*

Kifungo cha miaka mitatu kwa maoni yako ni kikubwa sana. Hii ni hoja ya kibinafsi zaidi na pengine mtu ambaye mwanao alimuibia anatamani mwanao angefungwa kifungo kikubwa zaidi. Yote kwa yote hatuna uhakika mwanao amemuibia nani lakini tuseme kama ni benki mahakama ina mtazamo kuwa benki ipo pale kuhudumia umma kwa ujumla kwa hiyo haitapunguza adhabu. Haitatushangaza kuona Mahakama Kuu ikiongeza adhabu kutoka miaka mitatu hadi miaka mitano, hivyo kuwa mwangalifu sana na sababu utakazozitoa kwenye rufaa.

Kujibu swali lako, mahakama kwa kawaida haiwezi kupunguza adhabu kwa sababu eti ina athari mbaya kwa wategemezi wa mhalifu. Kila mtuhumiwa ana mtegemezi, iwe ni mzazi anayeumwa, mtoto au mke - lazima kutambua kwamba wananchi wanahitaji ulinzi na mahakama inachukulia kosa la wizi kwa uzito. Wahalifu wanapaswa kufikiria madhara ya uhalifu kwa familia zao pamoja na watu wanaowaibia kabla ya kufanya uhalifu. Katika hali yoyote ile, migogoro ya familia haiwezi kuwa sababu ya msingi ya kukata rufaa.

## Kufukuzwa Kazi baadaye Kushtakiwa kwa Kosa hilohilo

**Rafiki yangu aliajiriwa kama muuzaji kwenye duka kubwa jijini Dar es Salaam. Alifukuzwa kazi kwa sababu ya wizi wa fedha. Yeye alinifahamisha kwamba kulikuwa na kikao cha nidhamu ambapo alikiri mashtaka. Sasa tunashangaa kuona kuwa polisi wamemtia nguvuni wiki chache baadaye kwa kosa lile lile. Tuliweza kumdhamini mahakamani na kwa sasa yupo nje. Tumesikia kuwa hakuna mtu anatakiwa kuadhibiwa mara mbili kwa kosa lile lile. Hii sio haki kwake, si ndiyo? Tafadhali saidia.**

*28 Desemba 2009*

Ingawa ni kweli kwamba hakuna mtu anapaswa kuadhibiwa mara mbili kwa kosa

moja, lakini kwa mazingira ya kesi hii, hali ni tofauti. Kusitishwa kwa ajira hakumfanyi mtu kutokushtakiwa kwa wizi na mwajiri wake.

Kilichofanyika awali ni taratibu za kinidhamu kwa mwajiri kulinda maslahi yake na kinachofanyika sasa ni kwa manufaa ya umma ili kuzuia uhalifu katika jamii na kuhakikisha hakuna mhalifu ambaye haadhibiwi.

Hata hivyo,tunalazimika kusema kuwa, kwa uzuri au ubaya, tabia ya watu wa ulimwengu wa sasa ya kupenda pesa ya mtelemko imekuwa chanzo cha maovu yote duniani. Sheria haizuii mtu kushtakiwa eti kwa sababu ameachishwa kazi na mwajiri wake.

Kitu sahihi rafiki yako anaweza kufanya ni kutubu na kuomba kwa Hakimu apunguziwe adhabu. Kama hili ni kosa lake la kwanza, anatakiwa kusema kwa kuwa inaweza kusaidia kupunguza adhabu.

## Haki ya Raia kukamata Watuhumiwa

**Mimi ni mkulima niishiye Mikumi Mkoani Morogoro. Miezi sita iliyopita mara baada ya usiku wa manane tulimkuta mtu karuka ukuta wetu na kukimbilia uelekeo wa shamba letu la kuku. Mara tu baada ya kuambiwa hivyo watoto wangu na mimi tulianza kumfuatilia. Tulimfunga kamba na kumpeleka kituo cha polisi ambapo aliwekwa kizuizini. Na sasa tumepokea wito wa mahakama kuwa tunashtakiwa kwa kosa la kumfunga mtu kimakosa. Imenishtua kwa jinsi kibao kilivyotugeukia. Mfumo wa Tanzania hautendi haki kabisa. Tafadhali nishauri ni kitu gani naweza fanya?**

*30 Novemba 2009*

Kwa maelezo uliyotupatia, inaonesha pasi na shaka kuwa mtu huyo alitaka kufanya uhalifu. Sheria zetu haswa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inampa mtu yeyote, ikiwemo raia wa kawaida, mamlaka ya kukamata bila kibali mtu yoyote ayeonekana amelala au amezubaazubaa bila sababu za msingi kwenye bustani au maeneo mengine nyakati za usiku ilimradi tu awe na sababu za msingi za kuamini kwamba mtu huyo anafanya au anataka kufanya uhalifu.

Ingawa si afisa wa polisi, sheria inakuruhusu kukamata raia ambaye unaamini ametenda kosa. Hatuoni tatizo lolote kwa jinsi ulivyolishughulikia tatizo hilo, labda kama ulitumia nguvu kubwa sana

Hatutaki kutoa maoni yetu kama mfumo wa utoaji haki Tanzania unatenda haki au la, hilo ni suala linalohitaji mjadala.

## Kuhudhuria Mahakamani

**Nilishuhudia kupigwa mtu mmoja nyumbani mwaka 2007. Muda mfupi baada ya tukio hilo, polisi walichukua maelezo yangu na sasa nimepewa wito wa mahakama ya kuhudhuria na kutoa ushahidi katika kesi hiyo. Je, kuna njia yoyote naweza kuepuka kwenda huko? Hata hivyo mtu huyo alikuwa anatuhumiwa kwa uchawi.**

*23 Novemba 2009*

Kwanza kabisa, unapaswa kuelewa kwamba wito wa mahakama wa kuhudhuria ni amri halali ya mahakama na jaribio lolotete la kudharau wito huo litakufanya uadhibiwe. Kuhudhuria mahakamani kutoa ushahidi hakuepukiki kwa sababu ushahidi huo utaisaidia mahakama kutoa haki. Wajibu wa mtu kutoa ushahidi ni wa lazima labda kama mtu huyo hawezi au ushahidi wake sio wa lazima, ila ni mahakama ndio yenye kuamua siku utakayohudhuria.

Kwenye kesi za jinai, mahakama imepewa mamlaka ya kumuweka gerezani mtu yoyote aliyehudhuria mahakamani kwa mujibu wa wito aliopewa, au yupo mahakamani na kutakiwa kutoa ushahidi, amekataa kuapa ili atoe ushahidi, au hataki kujibu maswali anayoulizwa au hataki kutoa nyaraka yeyote au kitu chochote ambacho anatakiwa kukitoa.

Kwa kesi yako tunakushauri kutii wito wa mahakama na katoe ushahidi, isipokuwa kama umesamehewa na mahakama baada ya kuhudhuria mbele yake.

Mtu hana hatia hadi pale itakapothibitishwa vinginevyo. Kama unavyosema, mtu huyo, anatuhumiwa kwa vitendo vya kichawi. Na yeye ana haki ya kikatiba ya kujitetea katika mahakama yenye mamlaka na mahakama itaamua kama hana hatia au ana hatia na si wewe.

## Tofauti kati ya Masharti na Wajibu

**Ninasaini mkataba ambao umeandaliwa na upande mwingine. Baada ya kusoma mkataba, nimekuta kuna baadhi ya sehemu ya mkataba inasomeka 'masharti' (conditions) na sehemu nyingine inasomeka 'wajibu' (warranties). Nini tofauti kati ya hayo maneno mawili? Je, kuna mbinu zozote nahitaji kujua kabla ya kutia saini mkataba?**

*23 Novemba 2009*

Tutaanza na swali lako la 'mbinu'. 'Mbinu' si tu kusoma mkataba bali pia kuuelewa. Kama kilichoandikwa kimetumia Kingereza cha kizamani na wewe unaelewa maneno lakini sio sentensi ni bora kupata msaada kutoka kwa mtu mwenye utaalamu wa mikataba. Kwa kifupi hakikisha kuwa unaelewa mkataba mzima kabla ya kuusaini.

Vipengele vya mkataba kwa kawaida vimegawanywa katika masharti au majukumu. Sharti ni kipengele cha msingi, kutokutekelezwa kwake kunafanya utekelezaji wa vipengele vilivyobaki kuwa tofauti kabisa kulingana na makubaliano ya awali. Kwa hiyo, kuvunja kwa kipengele hicho kutapelekea upande mwingine kuufanya mkataba huo kama haupo na kujitoa kwenye mkataba na hivyo kutokutekeleza majukumu yaliyopo kwenye mkataba.

Kwa upande mwingine, wajibu ni kipengele kidogo na uvunjaji wake unaweza tu kufidiwa kwa malipo ya fidia. Kuvunja kwa kipengele cha wajibu hakupelekei upande mmoja kujitoa katika utekelezaji wa majukumu ya mkataba. Hakuna ujanja wa kutofautisha maneno haya mawili. Ni vitu vya kawaida tu kwenye uandishi wa mikataba na ni nzuri kiutendaji.

## Chuki dhidi ya Jaji

**Mwezi uliopita kwa mara ya kwanza nilienda Mahakama Kuu Mwanza na kuishia kumchukia Jaji. Alikuja amechelewa sana bila kuonesha ishara ya kuomba msamaha. Nilipomsalimia hakuitikia na mbaya zaidi aliahirisha usikilizaji wa kesi kwa kusema amepata wito wa kwenda Dar. Nifanyeje?**

*30 November 2009*

Hatuna uhakika na swali lako ni lipi. Inaonekana una tatizo binafsi na Jaji ambapo ni vigumu kwetu kulitatua. Eti tu kwa sababu Jaji hajakusalimia, na kuwa wewe ni mara yako ya kwanza kuwa mahakamani haimaanishi kuwa uanze kumchukia. Hatakuwa tofauti na hajawekwa kwenye nafasi ile kuwafurahisha watu wanaohudhuria kwake.

Jaji anatoa haki. Unapoenda mahakamani ni kwa ajili ya haki sio kwa mambo ya kijamii. Hatuna uhakika chuki yako imeanzia wapi. Ikiwa kuna mambo mengine yalitokea kati yako na Jaji hujatuambia. Kama hukuridhika na ambavyo ataendesha shauri lako, unaweza kuweka pingamizi la kumkataa. Hakuna uchawi zaidi ya hapo.

## Dhamana tarajiwa

**Nimekuwa nikichunguzwa kwa kosa la jinai na ningependa kujua kama naweza kuomba dhamana kabla ya kupelekwa mahakamani. Katika mamlaka nyingine hili linaruhusiwa kama mtuhumiwa asiposababisha usumbufu.**

*16 Novemba 2009*

Unachotaja ni dhamana tarajiwa ambayo inatoa maelekezo ya kuachiwa mtu kwa dhamana, na hutolewa hata kabla ya mtu kukamatwa. Kwa mamlaka kama za India, sheria inaruhusu mtuhumiwa kufanya maombi hayo mahakamani. Kwa mujibu wa sheria zao, kuna mambo manne ambayo huzingatiwa kabla ya kupewa hiyo dhamana. Hayo ni; chanzo na uzito au ukubwa wa tuhuma zinazomkabili mtuhumiwa, historia ya mwombaji ikiwemo taarifa kama mahakama ilishawahi kumkuta muombaji na hatia, kama alishawahi kutumikia kifungo kwa makosa yanayotambulika, uwezekano wa lengo la tuhuma ni kumfedhehesha au kumvunjia heshima mwombaji kwa kumfanya kuwa mbaroni, na uwezekano wa mwombaji, kama atapewa dhamana tarajia, kuikimbia mahakama.

Kwa bahati mbaya, nchini Tanzania hatuna kifungu hicho, hivyo hauwezi ukaomba dhamana tarajia.

## Mkataba mrefu, Ada kubwa kwa Wanasheria

**Nilimshirikisha mwanasheria kutengeneza makubaliano ya kuuza mashine nchi jirani ya Rwanda. Mauzo yalikuwa rahisi lakini ulitengenezwa mkataba wa zaidi ya kurasa hamsini na kujumuisha vipengele visivyo vya lazima kuelekea mwishoni. Je, hivi ndiyo namna wanasheria wanatoza kwa huduma zao? Je, ni lazima kusaini mkataba huo?**

*2 Novemba 2009*

Ni vigumu sana kukujibu bila kusoma mkataba huo wa kurasa zaidi ya hamsini. Hata hivyo, ni lazima kutambua kwamba kazi ya mwanasheria ni kulinda maslahi yako na hata kama kuna uwezekano mdogo wa kutokea chochote kitakachokuathiri kama sehemu ya mkataba, ni bora wakili wako akakitaja kwenye mkataba ili kuhakikisha hakuna utata.

Vipengele vingi unavyosoma kuelekea mwisho wa mkataba, huitwa 'vifungu vya tafsiri'. Kwa mfano; uwezekano wa kusema theluji kuanguka Mwanza ni karibu na sifuri lakini kama vile uwezekano upo hata ikiwa kidogo mwanasheria mzuri atatumia hilo.

Kwa jinsi gani mawakili hutoza gharama zao kuna utata. Wateja wengi hawana ufahamu kwamba kipato cha mwanasheria hutegemea muda anaopoteza kufanya kazi fulani. Ni busara kukubaliana na wakili wako jinsi gani ya kumlipa kama ni kwa kila saa au kwa mkupuo. Kama unalipa ada kwa mkupuo swali lako litakuwa halina mashiko kwani hakutaathiri kiasi ulicholipa iwapo utakuwa na mkataba wa kurasa hamsini au kurasa tano. Malipo ya mkupuo ni ya kawaida nchini Tanzania. Iwapo unalipa kwa kila saa na unadhani baadhi ya vipengele havina umuhimu na vimewekwa kuongeza masaa ya kulipia unapaswa kuzungumza na mwanasheria wako. Yote kwa yote wanasheria nchini Tanzania ni nafuu sana kufanya nao kazi kuliko katika nchi nyingine jirani.

Hatutatoa maoni ya kama ni lazima usaini mkataba huu au la.

## Marekebisho ya Hati ya Mashtaka

**Mimi ni mfungwa naandika kutoka gereza la Ukonga. Nilishtakiwa kwa kosa la shambulio dhidi ya jirani yangu ambaye nina mgogoro naye kwenye mipaka ya kiwanja. Kwa ujumla upande wa Jamhuri uliita mashahidi watano. Kwa mshtuko baada ya kufunga kesi yangu ya utetezi Hakimu aliruhusu maombi ya upande wa mashtaka ya kurekebisha hati ya mashtaka ya shambulio la kawaida na kuwa shambulio la kujeruhi vibaya mwili na ndilo mwishowe nikakutwa nalo na hatia. Je, Hakimu alikuwa sawa kukubali maombi ya upande wa mashtaka? Nahisi kuwa Hakimu hakuwa upande wangu. Je, kuna nafasi yoyote ya kufanikiwa kwenye rufaa? Tafadhali nishauri.**

*19 Octoba 2009*

Kutokana na maelezo uliyotupa ni vigumu kwa sisi kuamua iwapo Hakimu wa kesi yako alikuwa na upendeleo kwa upande wa pili au la. Hata hivyo Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inaruhusu mahakama katika hatua yoyote ya kesi ikiwa inaonekana kwamba hati ya mashtaka ina mapungufu katika muundo au maudhui kutoa amri ya kurekebisha au kubadilisha hati hiyo. Katika hatua yoyote ya kesi ina maana hatua ya tangu unaposhtakiwa hadi kabla ya hukumu kutolewa, ilimradi tu kama mahakama itampa mtuhumiwa haki ya kuwahoji tena mashahidi wa mashtaka ambao walikwisha toa ushahidi wao. Hatua hii ni ya lazima na kama haikufuatwa itapelekea mwenendo wa kesi nzima kuwa batili. Isipokuwa kama unaweza kujenga hoja ya kwamba utaratibu unaotakiwa haukufuatwa, hauwezi ukakosoa uamuzi wa Hakimu aliyeendesha kesi yako, labda kama una sababu zingine za msingi, ambazo utazitumia kukata rufaa.

## Kumalizana nje ya Mahakama kwenye Kesi ya Jinai

**Ninamiliki biashara ya kusafirisha magogo nje ya nchi. Moja ya watumishi wangu aliiba fedha kwenye kampuni yangu na alishtakiwa kwa 'kuiba akiwa mtumishi'. Wakati mashtaka bado yakiendelea mahakamani, niliandika barua kwa Hakimu kutoa taarifa yangu kuwa sina nia ya kuendelea na mashtaka kwa sababu nimepata fidia ya hasara kutoka kwa baba wa mtuhumiwa. Mashtaka hayo yaliondolewa. Nimefahamishwa hata hivyo kwamba jalada limeitishwa Mahakama Kuu. Je, hii ni sahihi? Kwa nini Mahakama Kuu wameitisha jalada wakati mimi nimeamua kutokuendelea na kesi ukizingatia mimi ndo mlalamikaji?**

*26 Oktoba 2009*

Hii ni mara ya kwanza kwa sisi kusikia Hakimu kufuta kesi ya jinai kwa misingi ya kwamba imemalizwa nje ya mahakama. Kuyamaliza nje ya mahakama ni utaratibu mgeni kwenye kesi za jinai kwa Tanzania na kwingineko. Ingawa wewe ni mlalamikaji, katika kesi za jinai wahusika wa kesi ni Jamhuri na mtuhumiwa, na wewe kwa kawaida huja kama shahidi.

Labda kilichotokea ni kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ametumia mamlaka yake chini ya kifungu cha 91 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya kusema kwa niaba ya Jamhuri kwamba hana nia ya kuendelea na kesi hiyo.

Kwa kuzingatia kwamba kesi imefutwa kimakosa kwa sababu ya barua yako kwa Hakimu, Mahakama Kuu ina mamlaka chini ya kifungu cha 372 ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya kuitisha jalada. Mahakama Kuu inaweza kufanya hivyo ili kujiridhisha juu ya uhalali au usahihi wa maamuzi, adhabu au amri iliyorekodiwa au iliyotolewa na uhalali wa mwenendo wa kesi uliofanywa na Mahakama ya Hakimu Mkazi.

Kwa kifupi, mara tu uanzishapo malalamiko ya suala la jinai, mashtaka ya mtuhumiwa hufanywa na mwendesha mashtaka na si timu yako ya wanasheria. Hii itakuwa tofauti na kesi ya madai ambapo wakili huchukua jukumu la kuongoza.

## Mdaiwa kwenye Kesi amefariki

**Miezi michache iliyopita nilifungua kesi dhidi ya mmoja wa washirika wangu wa biashara na kesi bado inaendelea Mahakama Kuu. Nimepewa taarifa kuwa mmoja wa washirika wangu ninayemdai amefariki katika ajali ya gari. Nini kitatokea? Ni jinsi gani nitapata haki zangu?**

*19 Oktoba 2009*

Kisheria, kifo cha mdai au mdaiwa hakiwezi kusababisha kesi ya madai kusitishwa kama haki ya kushtaki imesalia. Kwa sheria zetu ikiwa mdaiwa amefariki na haki ya kushtaki imesalia,

mahakama, kwa maombi maalum, inaweza kuamuru wawakilishi halali wa mdaiwa kuwa sehemu ya kesi na kesi ikaendelea. Wawakilishi kisheria wameelezewa katika Sheria ya Mwenendo na Kanuni za Madai kuwa ni wasimamizi wa mali za marehemu akiwemo mtu yeyote anayeingilia mali za marehemu, na ambapo upande unaoshtaki au kushtakiwa katika nafasi ya uwakilishi, mtu yule ambaye mali itaenda kwake pale kitakapotokea kifo kwa upande wa mshtaki au mshtakiwa.

Katika kesi yako na kutokana na maelezo uliyotoa, haijulikani kama marehemu mdaiwa aliacha wosia au la. Kama mtu akifa na kuacha wosia ambao umemteua msimamizi wa mirathi, mtu aliyeteuliwa kama msimamizi wa mirathi atakuwa msimamizi wa mali ya marehemu toka tarehe ambayo marehemu amefariki, isipokuwa kama atajitoa katika usimamizi wa mirathi. Msimamizi wa mirathi anaweza kuingizwa shaurini hata kama bado hajapewa idhini ya mahakama kusimamia mirathi na anaweza kuendelea na kesi bila kuidhinishwa na mahakama mpaka pale atakapoidhinishwa. Kwa kumalizia, ni kwamba haki yako kwenye kesi ya madai haiwezi kupotea pale mdaiwa anapofariki.

## Ndugu yangu katumia vibaya Madaraka ya kuniwakilisha

**Mimi na kaka yangu tulinunua mali kwa pamoja miaka mingi iliyopita. Hatimaye, ilibidi nisafiri nje ya nchi kwa ajili ya matibabu ya dharura ambapo hali yangu ilinizuia kurudi Tanzania kwa miaka mitano. Kabla ya kuondoka, nilimpa ndugu yangu mamlaka ya jumla ya kuniwakilisha kwa niaba yangu kwa jambo lolote litakalotokea. Baada ya kurejea nimegundua ndugu yangu ametumia mamlaka niliyompa kuhamisha sehemu ya mali yangu kwenda kwenye jina la mtoto wake wa kiume. Ananiambia kuwa mtoto wake atashikilia mali hiyo kwa uaminifu kwa niaba yangu. Miaka yote ndugu yangu hajawahi kunidanganya – nimepokea sehemu yangu ya mapato ya kodi kwa wakati na kiasi sahihi. Na bado naendelea kupokea mapato ya kodi. Je, kuna sababu yoyote ya mimi kushtuka?**

*26 Oktoba 2009*

Kama kweli unamuamini kaka yako kiasi hicho, usingetuandikia swali hili. Kuna baadhi ya viashiria vya kutoaminiana vimetokea, ambavyo vimeleta wasiwasi katika akili yako na unashangaa 'kwa nini ndugu yako kahamisha mali kwa kutumia mamlaka ya uwakilishi?' Na hiyo ndiyo hofu yetu.

Hati ya uwakilishi kwa lugha rahisi ni nguvu anayopewa mtu na mtu mwingine kumwakilisha mtu aliyetoa nguvu hiyo. Uhamisho wa hati uliyofanywa na mfadhiliwa wa hati ya uwakilishi bila ufahamu au ridhaa ya mfadhili ni batili. Kuna kesi nyingi za namna hii ambapo mahakama ilitolea ufafanuzi suala hili. Zaidi, hata kama ilikuwa ya mapenzi tu, zingatio hilo haliwezi kuwa na nguvu kwa mfadhili wa hati ya uwakilishi bila ufahamu na ridhaa yake.

Jibu letu kwa swali lako kama kuna sababu ya kushtuka ni ndiyo. Hata hivyo, jaribu kutatua kirafiki na kama ikishidikana una kesi nzuri na unatakiwa kutafuta haki zako. Neno la tahadhari - mali hii mpaka tunapoongea mmiliki wake si wewe. Kama ukifa italeta mgogoro mkubwa kwa warithi kugombania. Inaonekana kuna mengi zaidi ya tunachokiona.

## Mahakama ya Biashara husikiliza Mashauri haraka sana

**Nilifungua kesi dhidi ya kampuni ya kimataifa kwenye Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara jijini Dar es Salaam. Nilifungua kesi mwezi wa saba mwaka 2009 baada ya hapo nilisafiri kwenda Ulaya kwa wiki nane. Niliporudi nilishtuka kuona kuwa kesi yangu imeshaamuliwa na sio tu kwamba**

**nilishindwa kesi, lakini pia nilitakiwa kulipa gharama za kesi za upande wa pili. Mwanasheria wangu ameniambia hatukufika hata kwenye msingi wa kesi sababu upande wa pili waliweka pingamizi. Ni kwa namna gani upande wa pili wanaweza kuweka pingamizi na shauri kuisha kwa uharaka hivyo?**

*12 Oktoba 2009*

Watu wengi wanalalamika kwamba mahakama zetu zipo polepole katika kusikiliza na kumaliza kesi! Hii ni mara ya kwanza kwetu kusikia malalamiko kuwa kesi imeendeshwa kwa uharaka mno.

Mahakama ya Biashara ni moja ya mahakama za haraka inayofaa kuitumia. Ina ufanisi, ina uelewa mzuri sana wa masuala ya kibiashara na labda ni moja ya mahakama bora za biashara kwenye ukanda huu. Moja ya sababu watu kushidwa kwenda Mahakama ya Biashara ni kwamba ina gharama kubwa.

Inaonekana upande wa utetezi ulifanikiwa katika pingamizi la awali na kupelekea kutupiliwa mbali shauri lako kabla hata ya kesi ya msingi. Bado una haki ya kukata rufaa katika Mahakama ya Rufaa. Moja ya sababu za rufaa ambayo huwezi kuitumia (kutokana na sauti ya swali lako), ni kwamba mahakama iliendesha kesi kwa haraka mno. Tunapendekeza uwasiliane na mwanasheria wako na kuangalia kama kuna uwezekano wa kufanikiwa rufaa yako kabla ya kukataa rufaa.

## Uraia wa Nchi mbili nchini Tanzania

**Mimi ni raia wa China kwa kuzaliwa. Naishi na kufanya biashara jijini Dar. Nimekuwa hapa kwa miaka sita sasa, na kwa sasa naielewa vizuri lugha ya Kiswahili na nimeoa mwanamke wa kitanzania. Ningependa kuomba uraia wa Tanzania lakini nataka kuendelea kuwa na pasipoti yangu ya China. Naweza kuwa na uraia wa nchi zote mbili? Ni jinsi gani naweza kuomba?**

*5 Oktoba 2009*

Nchi nyingi ikiwemo Marekani na nchi nyingine za Ulaya wanaruhusu uraia wa nchi mbili lakini Tanzania hairuhusu suala hili.

Kama unataka kuomba uraia wa Tanzania ni lazima kwanza kuukana uraia wako wa China kama utafanikiwa.

Ili kuomba uraia, sheria inataka kwamba maombi lazima kupelekwa kwa Waziri husika na uamuzi wa Waziri huwezi kuukatia rufaa wala kuufanyia marejeo kwenye mahakama yoyote na hivyo maamuzi yake ni ya mwisho.

## Kupekuliwa na Polisi

**Mimi ni mfanyabiashara wa kike, raia wa kikongo ninayeishi Dar es Salaam. Natuhumiwa kwa kukutwa na simu iliyoibiwa, pamoja na vitu vingine, nilipekuliwa na polisi wa kiume. Kisha nilipelekwa kituo cha polisi ambapo nilishikiliwa kwa masaa kumi na mbili. Sikupewa maji ya kunywa na pia nilinyimwa fursa ya kumeza dawa zangu za kisukari. Je, tabia ya aina hii inaruhusiwa nchini Tanzania?**

*28 Septemba 2009*

Kitendo cha kumpekua mtu kinasimamiwa na sheria. Maafisa wa polisi wana mamlaka ya kuingia katika chombo, makazi, boti, ndege n.k kufanya upekuzi ikionekana kuna ulazima wa kutuhumu kuwa kuna kitu cha wizi, au kimetumika au kimepangwa kutumika kufanyia uhalifu au silaha yoyote ya uhalifu au kitu chochote kilichofichwa au kinachokatazwa na sharia.

Kwa kuzingatia kanuni, polisi pia anaruhusiwa kumpekua mtu binafsi. Hata hivyo, sheria inahitaji kwamba wakati wowote ikionekana kuna ulazima wa kumpekua mwanamke upekuzi huo ufanywe na askari wa kike kwa sababu ya heshima. Kwa hiyo, upande wako kwa kuwa utaratibu huo haukufuatwa upekuzi huo ulifanyika kinyume cha sheria.

Kunyimwa maji na kutopewa muda

kutumia dawa zako, kifungu cha 55 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinasema kuwa wakati mtu yupo chini ya ulinzi, anatakiwa kutendewa kiubinadamu na utu wake ni lazima uheshimiwe. Kifungu hicho pia kinasema, kama mtuhumiwa ataomba kupatiwa matibabu, afisa wa polisi anatakiwa kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa mtuhumiwa anapatiwa matibabu au msaada. Hivyo, kukataliwa kutumia dawa zako za kisukari pia ni kinyume na sheria.

## Mipaka iliyopo kwenye Hati ya Uwakilishi

**Mwaka 2007 nilinunua kipande cha ardhi kisichopimwa jijini Dare es Salaam. Miezi michache baadae, nilisafiri kwenda Malaysia kwa masomo ya uzamili. Kabla ya kuondoka nchini nilimteua rafiki yangu chini ya hati maalum ya uwakilishi kushughulikia mchakato wa utafiti na kukamilisha usajili wa mali hiyo kwa jina langu, na alifanya hivyo. Mwaka 2008, rafiki yangu kwa kupitia mamlaka niliyompa aliweka dhamana ardhi yangu ili kupata mkopo benki. Rafiki yangu alishindwa marejesho ya mkopo benki na sasa benki iko katika mchakato wa kuchukua mali yangu. Je, nina sababu za kuanzisha kesi dhidi ya rafiki yangu? Vipi kuhusu benki? Naona hii kama fursa ya kutengeneza pesa zaidi.**

*14 Septemba 2009*

Kama kila kitu unachotuambia ni kweli, kuna uwezekano kwamba hoja ya benki ya kuchukua mali yako haiwezi kufanikiwa. Kitu muhimu ni je mamlaka uliyompa rafiki yako ni kufanya utafiti na hatimaye kusajili nyumba tu au kuiweka rehani kama alivyofanya? Wanasheria wako wanatakiwa kusoma hati ya uwakilishi kwa umakini na kuelewa neno kwa neno kwa sababu kiuhalisia benki haiwezi kutoa mkopo kwa sababu ulizozitaja. Kuna uwezakano kwamba kitu furani kinakosekana ingawa benki zinajulikana kwa kufanya makosa ya namna hiyo.

Kwa kuchukulia kuwa hati ya uwakilishi ilikuwa maalum kama unavyodai, kitendo cha rafiki yako cha kuweka rehani mali yako bila wewe kujua au kuridhia ni batili kwa hiyo dhamana hiyo haina ufanisi. Benki haiwezi kutekeleza hilo. Unaweza kushtaki benki na rafiki yako na unahitaji kupata amri ya zuio kutoka mahakamani kabla ya benki au mawakala kuchukua hatua yoyote zaidi.

Hatuna uhakika ni jinsi gani unaona kama ni fursa ya kupata pesa zaidi. Unaweza kudai fidia za aina mbalimbali lakini tambua kuwa benki nao watapambana kwa muda mrefu mahakamani. Benki ipo katika biashara ya kukopesha kwa kuweka dhamana na kushidwa kulipa mkopo haileti picha nzuri katika vitabu vya benki hiyo. Kuwa tayari kwa ajili ya mapambano ambayo yanaweza kuchukua muda mrefu mpaka kuisha.

## Nimeshitakiwa wakati napaswa kuwa Mshtaki/Mlalamikaji

**Nimepelekwa mahakamani na wakala wakati napaswa kumdai pesa zangu. mahakama inawezaje kukubaliana na kesi hizo? Nimekuwa nikiishi nchini Australia kwa muda mrefu na sijapata ona kitu kama hicho. Ninawezaje kushitakiwa ilihali mimi ndiyo napaswa kupewa pesa? Nifanyeje?**

*21 Septemba 2009*

Wakala wako labda anajaribu kudhoofisha nguvu yako za ukusanyaji madeni kwa kufungua kesi. Ameamua kuja na madai na kukushtaki. Hatakiwi kukushitaki wewe ili kurejesha fedha yako. Hujaeleza kwa nini amekushitaki, ila inawezekana, ni kutokana na uvunjwaji wa mkataba.

Kwa sababu tu kesi imefunguliwa mahakamani, haimaanishi kuwa imeshaamuliwa. Ni wajibu wa mahakama kuangalia pande zote na kuamua. Kwenye

kesi hii yeye ni mdai na wewe ni mdaiwa. Mahakama inaongozwa kwa kanuni na unayo nafasi ya kuweka madai kinzani kwenye utetezi wako.

Madai kinzani ni madai yanayoambatana na utetezi ambayo huletwa na mdaiwa kwenye kesi za madai ambayo huleta madai yanayojitegemea lakini madai hayo sio kinga dhidi ya madai yaliyoletwa na mdai. Unaweza kuunganisha madai yako kwenye kesi hiyohiyo ya madai lakini unatakiwa kujibu madai aliyotoa dhidi yako. Kwa sababu tu unadhani madai yake sio ya msingi, haimanishi kuwa mahakama itafikiria vivyo hivyo. Unatakiwa kuishawishi mahakama kuwa hakuna madai dhidi yako. Huo ni utaratibu wa kawaida wa kisheria duniani kote ikiwemo Australia.

## Upimaji wa VVU kwa Lazima

**Mimi ni mwanamume mwenye umri wa miaka 29 ninayeishi Lindi. Nimekuwa nikilazimishwa kupima VVU kitu ambacho napingana nacho kutokana na imani ya dini yangu. Tofauti na watu wengine ambao wanahofia kupima, mimi siogopi kwa sababu najua majibu yangu yatakuwa salama. Haki zangu ni zipi?**

*24 Agosti 2009*

Mtu anapaswa kuheshimu imani yako lakini mara nyingi inashauriwa kuwa kupima VVU/UKIMWI kuna faida zaidi kuliko hasara.

Swali lako ni iwapo unaweza kulazimishwa kupima au la. Sheria inakulinda - Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti VVU na UKIMWI imeeleza wazi kuwa mtu hawezi kulazimishwa kupima VVU isipokuwa kwa hiari yake, amekubali kupima au kuna amri ya mahakama imeamuru mtu huyo kupima. Sheria pia inaeleza kuwa haihitajiki ridhaa kwa mtu anayechangia kiungo chochote cha mwili au chembechembe hai au aliyetenda makosa ya kujamiiana. Sheria inapendekeza zaidi kuwa watu wa fani ya udaktari na mama wajawazito wafanye vipimo ingawa sio lazima.

Kutokana na maelezo yako, hakuna kati ya hayo yaliyotakiwa hapo juu kinahusiana na wewe, hivyo haulazimishwi kupima. Uhalali wa kupima haujalishi una umri gani, unatoka wapi au dini gani unaamini. Ni kosa kwa mtu yeyote kukulazimisha kupima.

## Uwepo wa Shauri baada ya Kifo

**Baba yangu alifariki mwaka jana kwa ajali ya gari. Wakati wa uhai wake alilishtaki gazeti kwa udhalilishaji. Sisi, kama watoto wake tunaweza kuendelea na shauri hilo? Tumefikia hatua nzuri sana kwenye shauri hilo na tumehakikishiwa ushindi kwa asilimia mia moja.**

*17 Agosti 2009*

Inashangaza sana kuona kuwa kuna mtu amewahakikishia ushindi. Hatuna hakika mtu huyo ni nani na kama ni wakili wenu anayewahakikishia ushindi kwa kiasi hiki basi anawapotosha. Tunajua kuwa hili si jibu unalolitafuta.

Swali lako linatutaka kueleza kwa ufupi madhara ya kifo kwenye mashtaka mbalimbali ya madai. Tofauti na sheria ya makosa ya jinai ambapo mashtaka hukoma mara baada ya kifo cha mtuhumiwa, hali ni tofauti kwenye mashtaka ya madai. Kwenye sheria ya madai kuna baadhi ya madai ambayo huendelea hata baada ya mtu aliyeshtaki au kushtakiwa kufariki na baadhi ambayo hayako hivyo. Chini ya Sheria ya Majanga na Mambo Mengineyo, panapotokea kifo cha mtu madai yote yataendelea dhidi yake au dhidi ya anaowadai isipokuwa kwenye madai ya kashfa, upotoshwaji, madai yatokanayo na ugoni na kushawishi mwenzi kuondoka au kutengana na mwenzi wake na madhara yote binafsi yasiyosababisha kifo cha mhusika kwenye kesi.

Madai hayaendelei kwenye makosa yanayohusiana na kashfa kwa sababu

madhara aliyoyapata mtu aliyekashifiwa sio lazima yaathiri mali zake.

Hivyo basi, kwa swali lako, haki ya baba kulishtaki gazeti kwa ajili ya fidia itokanayo na kukashfiwa ilikuwa ni haki yake binafsi na haki hiyo amekufa nayo. Kwa hiyo, shauri lililofunguliwa na baba yako limekoma baada ya kifo chake na wewe kama mwakilishi wake kisheria katika mali zake huwezi kuendelea na kesi hiyo (Mtu hufa na haki yake binafsi ya kushtaki).

## Meli kwenye Ukanda wa Bahari ya Tanzania

**Nilikuwa ndani ya meli yangu binafsi nikipita takribani umbali wa mita nne toka pwani ya Tanzania kuelekea Durban wakati mlinzi wa pwani yenu aliponisimamisha na kuikamata meli yangu na kukataa kutuachia. Sheria inasemaje kuhusu kupita kwenye ukanda wa bahari ya Tanzania?**

*17 Agosti 2009*

Mstari wa bahari unaotenganisha ukanda wa bahari ya nchi na ukanda wa bahari ulio nje ya nchi ni ukanda wa bahari ulio ndani ya mamlaka ya nchi ambayo hutekeleza mamlaka yake yanayohusiana na haki ya kipekee ya kuvua samaki na kutumia mazao yaliyo juu ya udongo wa bahari na udongo wa chini ya bahari na matumizi ya kipekee ya anga lililopo juu ya uso wa ukanda wa bahari wa nchi hiyo. Sheria inaruhusu meli zote za kigeni kuwa na haki kupita bila kuwa na hatia katika ukanda wa bahari ya Tanzania, ili mradi meli hiyo haihatarishi amani, usalama au utulivu kwenye nchi.

Unadai kuwa ulikuwa umbali wa mita nne kutoka pwani na hivyo ulikuwa ndani ya mipaka ya ukanda wa bahari ya Tanzania. Hujasema kwa nini meli yako ilikamatwa lakini kama ulikuwa unapita tu na hukusababisha tishio lolote kwa usalama na kwamba umemtaarifu ipasavyo mlinzi wa pwani ya Tanzania, hakukuwa na sababu ya kukamatwa.

## Mwanasheria wangu Ananichanganya

**Hivi karibuni nimemwajiri mwanasheria ili aweze kupinga mkataba niliouingia. Maneno anayoyatumia yananichanganya kwani wakati mwingine naambiwa mkataba ni batili na wakati mwingine husema unaepukika. Mwanzoni nilifikiri maneno yote ni sawa, na kugundua kumbe hayafanani. Nini tofauti kati ya mkataba batili na mkataba unaoepukika?**

*24 Agosti 2009*

Hatuwezi kukulaumu - maneno batili na kuepukika huonekana kama yanafanana lakini ni tofauti. Mkataba unaoepukika, ingawa ni halali wakati unafanyika, unaweza baadaye kuwekwa kando kwa sababu ya upotoshwaji, baadhi ya matukio ya kimakosa, ufichaji wa taarifa za msingi na/au ushawishi usio halali.

Kwa upande mwingine, mkataba batili ni ule ambao hauna nguvu ya kisheria toka siku ulipofanyika. Mkataba batili hutokea ikiwa mshiriki mmoja au washiriki wote hawana uwezo wa kisheria kuingia mkataba na wakati mwingine kama kuna makosa kiutendaji. Mkataba ulio kinyume na sheria ni batili lakini sio lazima mikataba yote batili iwe kinyume na sheria.

## Kushtakiwa Muuza Dawa za Kulevya nchini Marekani

**Mtanzania ambaye kwenye miaka ya 1980 alituhumiwa kuwa amehusika katika mauaji jijini Dar es Salaam, hivi karibuni amekamatwa nchini Marekani kwa tuhuma za uuzaji na usambazaji wa dawa za kulevya. Je, anaweza kushtakiwa hapa nchini ili aweze kutiwa hatiani na kupata adhabu ya kifo?**

*3 Agosti 2009*

Tunachoweza kukipata kwenye swali

lako, unataka mhalifu ashtakiwe nchini Tanzania, kwa kosa la mauaji na kuhukumiwa adhabu ya kifo na sio kushtakiwa kwa makosa yanayohusiana na dawa za kulevya nchini Marekani ambayo yana dhamana na kupelekea kifungo gerezani.

Kitu ambacho hasa unakitaka ni kukabidhiwa kwa mtuhumiwa nchini Tanzania. Kukabidhi mtuhumiwa ni kitendo cha nchi moja kukabidhi kwa nyingine mtu anayetuhumiwa kufanya makosa ya jinai kwenye nchi anayokabidhiwa. Kwa bahati mbaya nchi ya Tanzania na Marekani hazina mkataba wa kubadilishana wahalifu hivyo hakuna uwezekano wa moja kwa moja kwa mashtaka kuhamishwa toka nchini Marekani kuja nchini Tanzania. Kwa ajili ya kumbukumbu zako, baadhi ya nchi ambazo nchi ya Tanzania imeingia nazo mikataba hiyo ya kubalishana wahalifu ni kama Zambia, Kenya, Uganda, Australia, Mauritius, Malta na Singapore.

## Begi limechukuliwa Kimakosa

**Wiki iliyopita nilikuwa kwenye basi nikitoka Mwanza kuelekea Dar es Salaam. Nilipofika Dar, nilichukua begi la mtu mwingine kimakosa. Sikuweza kumtambua mmiliki wa begi. Baadaye kidogo watu wawili walikuja kwangu na kila mmoja kudai kuwa ni mmiliki wa begi hilo. Sijakabidhi begi kwa yeyote kwa kuwa sijui ni nani mmiliki halali kati yao. Begi lina vitu vya thamani. Nifanyeje?**

*27 Julai 2009*

Swali lako ni zuri sana. Sheria ya Mwenendo na Kanuni za Madai ina suluhisho kwenye tatizo hilo, kwa wewe kufungua shauri ambalo wewe huna maslahi nalo (interpleader proceedings). Shauri hilo hufunguliwa na mtu ambaye hana maslahi kwenye mali fulani lakini kuna watu wawili au zaidi wana maslahi. Kwa bahati mbaya unatakiwa ufungue shauri lakini kwa mazingira yalivyo ni vyema kufanya hivyo. Unatakiwa uwasilishe hati ya mashtaka ya madai mahakamani na ueleze kuwa huna maslahi kwenye mali iliyopo kwenye mgogoro zaidi ya gharama ulizotumia katika kutunza begi hilo na gharama za kufungua shauri hilo. Gharama hizo kwa kawaida hurudishwa mwishoni mwa shauri.

## Wagonjwa wa Akili Mitaani

**Nimerudi hivi karibuni toka Marekani na kuona watu wengi wanaosumbuliwa na ugonjwa akili mitaani. Baadhi ya watu hao wanaweza kuwa hatari. Hakuna kitu chochote kinachoweza kufanyika?**

*20 Julai 2009*

Katika kulinda na kusimamia haki za watu wenye ugonjwa wa akili, sheria yetu inataka watu wenye matatizo ya akili kupelekwa kwenye vituo vya kusimamia afya ya akili au kutoa taarifa katika mamlaka za ustawi wa jamii. Ni wajibu wa mkuu wa Kituo cha Polisi, mlinzi wa amani, Afisa Ustawi wa Jamii, kiongozi wa dini, Afisa Mtendaji Kata au Afisa Mtendaji Kijiji ambao wana sababu ya kuamini kuwa mtu yeyote katika eneo alipo ana tatizo la akili na hana usimamizi, kuhakikisha kwa haraka anapelekwa kituo cha kusimamia afya ya akili. Tunashauri uwasiliane na mmoja kati ya wahusika waliotajwa hapo juu.

## Kuua Mgonjwa kwa Huruma (Kifo cha Hiari)

**Baba yangu ni mgonjwa sana na madaktari hawana matumaini tena juu yake. Amekuwa kwenye hali ya umahututi kwa zaidi ya miezi sita na mmoja wa shangazi zetu ambaye ni muuguzi ameshauri tumsadie baba aweze kufa kwa kumchoma sindano yenye sumu na kupunguza mateso yake. Je, hii ipo kisheria?**

*20 Julai 2009*

Kuna msemo usemao huwezi kuchukua kile ambacho hujakitoa. Kuua kwa huruma ni kitendo ambacho humaliza uhai kwa namna

isiyo na maumivu, hufanywa na mtu mwingine tofauti na mgonjwa mwenyewe. Hii inaweza kuhusisha kuacha kutoa matibabu ya msingi ambayo husababisha kifo, kuondoa mashine zinazomsaidia kupumua, kutumia sumu kali au nguvu kuondoa uhai wa mgonjwa, kama shangazi yako anavyoshauri.

Kundoa uhai wa mtu kwa makusudi hakuruhusiwi kwenye sheria zetu. Ukimsaidia baba yako kufa, utakuwa umefanya mauaji hata kama ulitaka kumuondolea maumivu. Kitendo hicho ni kosa la kuua kwa makusudi kinyume na sheria na inaweza kupelekea adhabu ya kifo.

Kuna baadhi ya nchi duniani ambazo uuaji wa namna hiyo unaruhusiwa kisheria. Nchi hizo ni pamoja na jimbo la Oregon lililopo nchini Marekani, nchi ya Uswisi, nchi ya Ubelgiji na nchi ya Uholanzi. Sheria nyingi zilizopo kwenye nchi hizo zinamtaka daktari anayesaidia kuua, kutumia mbinu ya haraka yenye maumivu kidogo ya kumfanya mgonjwa afe. Wakati unaweza kujua ni kwa muda gani itasababisha kifo, ni vigumu kuamua ni njia ipi sahihi ya kufa isiyo ya maumivu na hii ndiyo imesababisha utata mwingi.

Suala hilo huleta utata zaidi juu ya nani anatakiwa kuamua kama mgonjwa anatakiwa afe hasa pale mgonjwa anapokuwa mahututi. Tunahuzunika pamoja nawe lakini tunasisitiza kuwa kitendo cha kusaidia au kuharakisha kifo cha baba yako ni kinyume na sheria.

## Kutembea Hadharani na Bastola

**Nilisimamishwa jioni moja na polisi ambao walinikuta na bastola yangu. Ninamiliki kihalali na nina leseni ya bastola hiyo. Hata hivyo, nimeshtakiwa kwa kosa la kutembea na silaha hatari maeneo ya hadhara. Je, nifanye nini?**

*6 Julai 2009*

Kwa kuwa una leseni na unamiliki kisheria bastola hiyo, kutembea maeneo ya hadhara na bastola sio kosa kwenye sheria zetu. Maeneo ya hadhara humaanisha pia nyumba za umma kama vile kumbi za sinema na maduka makubwa. Kutembea na bastola hadharani inakuwa ni kosa, kwa mfano, pale tu mmliki wa silaha hiyo ataanza, bila sababu ya msingi, kutoa vitisho kwa wale wanaomzunguka au kuitumia vibaya silaha hiyo. Hili likitokea, ndipo umiliki wa bunduki au bastola unakuwa sio halali na mmiliki anakuwa anamiliki silaha hatari kwenye eneo la hadhara. Hili halionekani hapa labda kama umesahau kulipia upya leseni ya bunduki yako (tafadhali angalia hilo). Labda kama kuna taarifa umezificha, mashtaka yanayokukabili ni batili na hayapo sawa. Unatakiwa utafute msaada wa kisheria.

## Kuendesha bila kuwa na Sifa

**Mimi ni fundi wa magari ninayefanya mafunzo ya vitendo kwenye karakana. Sina leseni ya udereva na nimekamatwa na askari wa usalama barabarani kwa kuendesha gari la mteja ambalo nilikuwa namsaidia kulikokota. Kiukweli nilikuwa ndani ya gari ambalo lilikuwa likikokotwa, nikishika tu usukani kwa kuwa injini ilikuwa haifanyi kazi. Nimeshtakiwa kwa kosa la kuendesha gari bila leseni. Ilikuwa kwa umbali mfupi tu na sio kwenye barabara kuu. Nilipaswa kuwa na leseni?**

*13 Julai 2009*

Jibu la swali lako ni ndiyo, ulipaswa kuwa na leseni. Chini ya Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 kama ilivyorejewa mwaka 2002 kuendesha gari bila ya kuwa na leseni halali au leseni ya mtu anayejifunza ni kinyume na sheria. Tafsiri ya neno dereva ni pana sana hujumuisha kuzungusha usukani wa gari ambalo linasukumwa au linakokotwa. Kitu cha msingi ni nani anayeongoza mwenendo wa gari. Ulikuwa unaliongoza gari hilo kwa kutumia breki na usukani na kulifanya gari

litembee. Haijalishi kama umeendesha umbali mfupi na umeendeshea mtaa wa nyuma au la. Ulitakiwa kuwa na leseni ya udereva na umeshitakiwa kihalali.

## Vigezo vya kupata Dhamana ya Polisi.

**Nilikamatwa na askari polisi kwa kosa dogo na nilisumbuliwa sana wakati nilipokuwa nahitaji dhamana. Ni vigezo gani askari polisi hutumia kutoa dhamana?**

*20 Julai 2009*

Dhamana ni kitendo cha jeshi la polisi au mahakama kumwachia mtu aliyekuwa kizuizini wakati akisubiri mashtaka yake. Jeshi la polisi huitaji wadhamini ambao watamleta mhalifu/ mtuhumiwa wakati wakitakiwa kufanya hivyo. Ni mkataba kati ya mdhamini na mahakama/ jeshi la polisi kuwa mtuhumiwa atapatikana wakati akihitajika.

Dhamana ni haki ya kila mtu. Hata hivyo, askari polisi ambaye ni mkuu wa kituo cha polisi husika au Hakimu wana mamlaka ya kutoa au kuzuia kutoa dhamana kutokana na sababu mbalimbali. Sababu hizi ni kama historia ya mtuhumiwa, kazi yake, hali yake ya kifamilia ikiwa pamoja na taarifa zake za siku za nyuma, mazingira ambayo kosa limefanywa, asili na uzito wa kosa lililofanywa na kama mtuhumiwa ataweza kutoroka.

Hatuna uhakika unaposema kosa jepesi unamaanisha nini. Kwa hali yoyote, unastahili kupata dhamana isipokuwa labda uwe unashitakiwa na kosa la kuua, umefanya kosa la uhaini au unyang'anyi kwa kutumia silaha ambapo dhamana imekatazwa.

## Zuio la Muda Mfupi limekataliwa.

**Kwenye kesi, niliomba zuio la muda (temporary injunction) na mahakama imekataa kutoa. Sababu iliyotolewa na mahakama ni kuwa nimechelewa kuomba zuio. Kukataa huko hakupo kisheria?**

*22 Juni 2009*

Zuio ni nafuu ya kisheria ambapo mtu huelekezwa kutofanya kitu au kufanya kitu fulani. Aina ya kwanza ya zuio pia hujulikana kama katazo/marufuku, na nyingine ni ile inayomlazimisha mtu kufanya jambo. Zuio la muda mara nyingi ni lile linatolewa kwa muda fulani kwa kutoa unafuu wa kulinda kitu kilichopo kwenye mgogoro kuwa katika hali kama kilivyo. Zuio la muda linaweza kutolewa mara moja, hadi pale maombi ya zuio la muda yatakapoamuliwa. Kuna uwezekano uliomba amri ya katazo

Pamoja na sababu zingine, mahakama huangalia muda ambao umetumia kuomba amri hizo. Kama muda mwingi umepita toka pale tatizo lilipotokea hadi muda ulioomba zuio, mahakama inaweza kuyakataa maombi yako ya zuio la muda na hakuna kitu kilichokosewa kwenyo hili.

## Haki ya kuita Mashahidi

**Mimi ni mfungwa ninayetumikia kifungo cha miaka thelathini katika gereza la Ukonga. Nilishtakiwa kwa kosa la unyang'anyi wa kutumia silaha na nilikuwa mahabusu toka siku niliyoletwa mahakamani mpaka siku ya mwisho wa kesi. Wakati wa kujitetea kwangu ulipofika, Hakimu aliyekuwa anaendesha kesi alikataa kutoa wito wa kuwaita mashahidi wangu. Ninaweza kukata rufaa dhidi ya hatia?**

*8 Juni 2009*

Haki ya mtuhumiwa kuita mashahidi ni haki ya kisheria. Sheria inayosimamia mwenendo wa makosa ya jinai kwenye mfumo wetu wa sheria ni Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Jedwali la Tatu la Sheria ya Mahakimu.

Kwa mfano, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inamtaka Hakimu kumweleza mtuhumiwa haki ya kuleta mashahidi wakati wa utetezi wa kesi yake.

Kawaida sheria ipo wazi kuwa pale tu mtuhumiwa atakapoonesha kuwa ana nia ya

kuita mashahidi, mahakama ina wajibu wa kuhakikisha kuwa mashahidi wanapatikana ili kutoa ushahidi kwa wakati muafaka kwa kutoa wito wa mahakama hasa pale mtuhumiwa akiwa hana wakili.

Hata hivyo, Hakimu ana mamlaka ya kukataa haki ya mtuhumiwa kuleta mashahidi akitoa sababu za kukataa, kwa mfano, ikiwa tu ushahidi wa mashahidi hao hauna uhusiano na kesi au mtuhumiwa akisema ana mashahidi lakini mashahidi hao hawapo mahakamani kutokana na makosa au uzembe wa mtuhumiwa. Kwa sababu yoyote ile, kila jambo lazima liwekwe kwenye kumbukumbu za mahakama.

Kwenye kesi yako, hujatueleza mazingira yaliyosababisha Hakimu kukataa kukupa haki yako ya kuita mashahidi wala uhusiano wa ushahidi ambao ungeletwa na mashahidi wako. Hata hivyo, kama unadhani ushahidi uliokusudiwa kuletwa na mashahidi wako ulikuwa muhimu kwenye kesi yako na kukosekana kwa mashahidi wako mahakamani lilikuwa sio kosa lako au uzembe wako na kwamba Hakimu alipaswa kuhairisha shauri, basi una sababu za msingi za rufaa. Nafasi yako ya kushinda rufaa hiyo inategemea na kumbukumbu za mahakama.

## Amekubali Kosa la Mauaji bado amehukumiwa Kunyongwa

**Rafiki yangu alihusika kwenye wizi ambapo mtu aliyeibiwa ameuawa. Rafiki yangu alikiri kosa la mauaji na amehukumiwa adhabu ya kifo. Ni lini atanyongwa? Nilifikiri kwamba kwa kuwa alikuwa mwaminifu kusema ukweli, angepewa adhabu ya kifungo. Rais anaweza kupunguza adhabu ya kifo?**

*25 Mei 2009*

Rafiki yako mwaminifu ameisaidia mahakama kutopoteza muda na rasilimali kwa kusema ukweli. Kwenye makosa ya jinai, kukubali kufanya kosa, pamoja na sababu zingine, huweza kupunguza uzito wa adhabu.

Bahati mbaya kwa rafiki yako, kosa la kuua chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu, lina adhabu moja tu – nayo ni kunyongwa hadi kufa. Hakuna nafasi ya kupunguziwa adhabu kwa mtu aliyeshtakiwa kwa kuua. Licha ya ukweli kwamba rafiki yako alikuwa mwaminifu haibadilishi ukweli kuwa alimuua mtu. Kuua ni kosa kubwa sana na sheria yetu huliangalia kwa umakini sana.

Rafiki yako atakuwa kwenye foleni ya kifo kusubiri saini ya Rais kuidhinisha kifo. Idhini hiyo hueleza wapi unyongaji utafanyika pamoja na sehemu ya mazishi. Hata hivyo, Rais ana mamlaka ya kubadilisha adhabu hiyo kwa kutoa adhabu nyingine tofauti na kifo au kusamehe mfungwa kabisa au kwa masharti.

## Ada ya Mahakama ya Biashara ziko juu

**Kwa nini nifungue kesi ya madai yenye thamani kubwa Mahakama ya Biashara? Mwanasheria wangu anajaribu kunitoza fedha nyingi zaidi?**

*18 Mei 2009*

Una mashaka yasiyo ya lazima kwa mwanasheria wako. Mahakama ya Biashara imewekwa kwa ajili ya kuendesha mashauri kwa haraka na kwa umakini zaidi. Migogoro hiyo ya kibiashara imefafanuliwa chini ya sheria zetu na mahakama nyingine, kama vile Mahakama Kuu, hazikatazwi kusikiliza migogoro hiyo. Kwa kuzingatia tathmini ya mwanasheria wako kwenye shauri hili inaonekanani kama ni vema mgogoro huo ukasikilizwa Mahakama ya Biashara.

Kutokana na muundo wake maalum, kufungua shauri Mahakama ya Biashara kwa kawaida ni gharama zaidi. Kwa kawaida ada ya mahakama ni asilimia 3% ya kiasi unachokidai. Hii ni ada ya mahakama na sio gharama ya mwanasheria. Kama utaona gharama ya kufungua shauri Mahakama ya Biashara ni ghali unaweza kufungua shauri Mahakama

Kuu. Hakuna hitaji la kilazima la kisheria kwa wewe kufungua kesi Mahakama ya Biashara.

## Shauri lililopita Muda wake

**Nimefungua shauri kwa kuvunja mkataba na mdaiwa ameweka pingamizi kuwa shauri lipo nje muda. Kwa mshangao Jaji amekubali maombi hayo. Naweza kukata rufaa?**

*11 Mei 2009*

Migogoro tofauti ina muda tofauti wa kikomo cha muda wa kufungua kesi ya madai. Katika mashtaka ya migogoro ya mikataba, kwa mujibu wa Sheria ya Ukomo cha Mashtaka, shtaka hilo linatakiwa lifunguliwe ndani ya miaka sita kuanzia siku ya uvunjifu. Hivyo, shauri lolote lililofunguliwa nje ya muda husika, mahakama haitokuwa na nguvu ya kulisikiliza.

Kwa maelezo yako hapo juu, inaonekana kuwa shauri lako halijafunguliwa ndani ya miaka sita hivyo mwanasheria wa upande wa utetetezi amefanikiwa kwenye pingamizi la awali ambalo limemaliza kesi yako. Kama una sababu nzuri za kuonesha kwa nini umechelewa kufungua shauri, unaweza kuomba kwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kuongezewa muda wa kufungua shitaka nje ya muda. Kama waziri atashawishika na sababu ulizotoa anaweza kuruhusu muda wa nyongeza wa kufungua shitaka lako. Muda huo wa nyongeza utakuwa ni nusu ya muda ambao upo kisheria. Kwenye kesi yako, Waziri anaweza kuongeza tena miaka mitatu ya nyongeza na kama uvunjifu huo wa mkataba umetokea ndani ya muda wa nyongeza shitaka lako halitakuwa nje ya ukomo wa muda wa kushitaki.

Kwa njia nyingine, kama unafikiri kuwa mahakama imekosea kukokotoa muda waweza kukata rufaa Mahakama ya Rufaa. Unatakiwa kutoa notisi ya kukata rufaa na kuomba mwenendo wa kesi, uamuzi mdogo na amri ya kutupilia mbali ili uweze kukata rufaa.

## Mtuhumiwa wa Mauaji kaachiwa huru.

**Nimesoma gazetini kuwa watuhumiwa wachache wa mashtaka ya mauaji wameachiwa huru wakati mashtaka ya mauaji yakiendelea, wakati wengine wakiendelea kujitetea mahakamani. Ni jinsi gani mahakama inaweza kuruhusu wengine waachiwe wakiwa katikati ya mashtaka? Kuna kitu sio sahihi.**

*18 Mei 2009*

Mara mtu anaposhtakiwa kwa kosa la jinai, ni jukumu la waendesha mashtaka kutoa ushahidi utakaoonesha kosa ambalo mtu ameshtakiwa nalo. Ni jukumu la kisheria kwa upande wa uendeshaji mashtaka, kwa kupitia ushahidi wa mashahidi na ushahidi mwingine, kuthibitisha pasipo na mashaka kuwa mtuhumiwa ana hatia. Kama wakati wa kufunga ushahidi wa kuthibitisha mashtaka, ikaonekana mbele ya mahakama kwa kwa jinsi ilivyo, shauri halijathibitishwa vya kutosha dhidi ya mtuhumiwa kumfanya aje kujitetea, mahakama itafutilia mbali mashtaka na kumuachia huru.

Jukumu la kuleta ushahidi wa kutosha ili kuweza kumtia mtu hatiani kabla ya mtuhumiwa kujitetea kisheria hujulikana kama uthibishaji wa kesi ya msingi. Kwa hiyo, kwenye mwenendo wa mashtaka ya jinai mahakama inaweza kumuachia mtu huru kwenye shauri kama ushahidi ulioletwa na upande wa mashtaka haujitoshelezi vya kutosha kumfanya mtuhumiwa ajiteteee. Ni utaratibu wa kisheria kwa mahakama kupima na kutathmini ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka na kuamua kuwa mtuhumiwa ana shitaka la kujibu au la. Kwa kujibu swali lako, watuhumiwa walioachiwa huru wakati kesi ikiendelea ni wale ambao mahakama imeona kwamba hawana kesi ya kujibu.

Wengine wana kesi ya kujibu na upande wa utetezi utaanza au kuendelea na kesi. Hakuna udanganyifu katika taratibu.

## Mikataba mirefu, Malipo zaidi kwa Wanasheria

**Nimeingia mkataba na kampuni ya kigeni na nimeshangazwa nimesaini mkataba wenye ukubwa kama kitabu. Maelezo yalikuwa ni mafupi lakini yana aina zote za vifungu. Kwa nini nilitakiwa nisaini mkataba mrefu kama ule? Wanasheria labda hutengeneza mikataba mirefu kwa ajili ya kutoza fedha nyingi zaidi.**

*4 Mei 2009*

Ungejiuliza wewe mwenyewe swali hilo kabla hujasaini mkataba huo na sio baada ya kusaini. Tumegundua kuwa makampuni mengi husaini nyaraka bila kujua halafu huja kulaumu baadaye - suala lako halina tofauti na hili. Urefu wa mkataba hauna maana yoyote. Unaweza kuwa na mkataba wenye ukubwa wa kitabu ukawa una makosa na unaweza kuwa na mkataba wenye nakala chache ukawa ni sahihi na wenye uzito/ wenye mashiko.

Lengo kuu la mkataba ni kuweka kumbukumbu ya mambo ambayo pande mbili zimekubaliana, ili kuepuka utata na migogoro itakayojitokeza hapo baadaye. Mkataba mrefu sio lazima uwe na makosa – inaweza ikawa kuwa mtu aliyeutengeneza amejumuisha “vifungu vya tafsiri” ili kuhakikisha kila kitu kinakuwepo, hata vile ambavyo havitarajiwi.

Ni vigumu kwetu kusema kuhusu kusudio la wanasheria kuandaa mikataba mirefu ni kutoza tozo kubwa. Wakati vifungu vingi vya tafsiri ni vifungu vya kunakiri na kuweka. Wakati mwingine uandishi wa mikataba mifupi yenye kila kitu huchukua muda mrefu na kuwagharimu wateja kuliko mikataba mirefu iliyo na vifungu vya kawaida.

## Gari kama Kizibiti cha Polisi

**Polisi wametaifisha gari langu na hawataki kulirudisha kwangu. Wanadai kuwa gari hilo litatumika kama kielelezo cha shitaka mahakamani. Tafadhali nishauri.**

*13 Aprili 2009*

Kisheria, jeshi la polisi linaruhusiwa kushikilia mali iliyokutwa wakati wa upelelezi wa mashtaka ya jinai mpaka pale maamuzi ya mwisho ya kesi yatakapotolewa, ili mradi umakini katika utunzaji wa mali hiyo unafanyika. Sababu za kushikilia mali hizo hutofautiana kulingana kesi yenyewe katika muda husika. Kwa mfano, hapawezi kuwa na uhalali kwa polisi kushikilia gari la mtu lililohusika kwenye makosa ya barabarani, haswa baada ya uchunguzi wa awali kukamilika. Kuna mazingira utekelezaji wa mamlaka ya kuchukua na kushikilia ni ya lazima na ni halali kama vile panapokuwa na sababu za msingi za kuamini kuwa gari tajwa lilitumika kufanyia kosa na kama litatolewa mahakamani, litathibitisha ushahidi kuhusu kufanyika kwa kosa hilo la jinai. Moja kati ya mazingira hayo ni pale inapodaiwa kuwa gari tajwa lilitumika katika ufanyaji wa kosa hilo la jinai.

Kama gari lako limetaifishwa kwa sababu ya kuhusika kwenye ufanyaji wa kosa la jinai, polisi wanaweza shikilia gari lako. Hujataja kosa hilo ni lipi kwa hiyo inatuwia vigumu kukupa jibu. Kumbuka katika utelekezaji wa haki, polisi wana haki ya kushikilia mali yoyote yakiwemo magari, ili kutolewa kama ushahidi.

## Madai juu ya Madai (Madai Kinzani)

**Nimefungua shauri la madai mahakamani lenye thamani ya shilingi ya kitanzania Milioni 150 kwa uvunjifu wa mkataba. Nimeshtushwa baada kusikia kutoka kwa mwanasheria kuwa mdaiwa kwenye kesi hiyo hiyo anadai shilingi ya kitanzania bilioni 1 kutoka kwangu. Sielewi hili linakujaje na nipo kwenye hali ya mshtuko. Mahakama inawezaje kuruhusu madai hayo**

**ambayo yametolewa mara tu baada ya mimi kupeleka shauri mahakamani? Nishauri tafadhali.**

*20 Aprili 2009*

Madai ya mdaiwa dhidi yako kwenye shauri ulilofungua yanaitwa madai kinzani. Madai kinzani ni madai yanayoletwa na mdaiwa kwenye shauri la madai ambayo huwa ni madai huru. Kwa kawaida sio utetezi kwenye madai unayoomba.

Sheria inaruhusu mdaiwa kuleta madai kinzani. Ni kazi ya mwanasheria wako kuhakikisha kuwa kesi inakuwa kwenye mwelekeo sahihi kama madai hayo ni ya uongo na yanakusudia kupoteza muda. Madai kinzani huweza pia kuletwa na mdaiwa dhidi ya mtu yeyote ambaye hayupo kwenye shauri na madai hayo sio lazima yawe yametokana na jambo hilo hilo. Ni hitaji la kisheria kuwa mahakama lazima isikilize pande zote mbili hivyo huwezi kuizuia mahakama kusikiliza dai hilo kinzani lililoletwa mbele yake.

## Baba kushikiliwa kwa Makosa ya Kijana wake

**Wakati wakiwa kwenye baa, kijana wangu mwenye umri wa miaka 21 akiwa na rafiki yake walipigania mwanamke. Kwa kutumia chupa ya bia, kijana wangu alimpiga rafiki yake kichwani na kusababisha madhara makubwa kichwani. Mwanangu sasa ametoroka. Jitihada zote za polisi kumkamata zimeshindikana. Polisi kama mbadala wamemkamata mume wangu na wanasema hawatamuachia mume wangu mpaka kijana wangu atakapoonekana. Hii ni haki?**

*27 April 2009*

Polisi hawawezi kumkamata mumeo isipokuwa kama askari huyo ana ushahidi kuwa mumeo alihusika kwa njia moja au nyingine na tukio au amemficha kijana wako yaani kuwazuia polisi kufanya kazi zao. Kitendo cha kumkamata mumeo kinakiuka haki yake ya kikatiba ya kwenda sehemu yoyote. Kijana wako ni mtu mzima kwa hiyo anawajibika kwa matendo yake. Kisheria mzazi hawezi kuwajibishwa kwa makosa ya kijana au binti yake. Tunakushauri uonane na kikundi kinachotetea haki za binadamu au mshirikishe wakili kwa msaada.

## Dereva aliyelewa anaendesha Gari

**Majuma machache yaliyopita mimi na marafiki zangu tulienda uwanja wa taifa kuangalia pambano la mpira. Baada ya pambano, rafiki yangu aliyekuwa akiendesha gari alikuwa ametumia kilevi sana na tukapata ajali. Niliumia vibaya kwenye ajali hiyo. Naweza kumshtaki rafiki yangu?**

*27 Aprili, 2009*

Ndiyo, unaweza kumshtaki. Hata hivyo, hujasema kama wote mlikuwa mmelewa au ni rafiki yako peke yake. Inawezekana wote mlikuwa mmelewa lakini hata kama hukulewa, kitendo cha wewe kupanda gari ukiwa unajua rafiki yako amelewa, itapunguza kiwango utakachodai.

Japokuwa rafiki yako alikuwa mzembe kuendesha gari akiwa amelewa, hakuna mashaka kuwa kwa kukubali kuendeshwa na dereva mlevi umechangia kupatikana kwa majeraha yako. Ungeweza kuepuka kwa kutopanda gari hilo. Kwa hiyo, ingawa una madai ya msingi dhidi ya rafiki yako kwa kuendesha gari akiwa amelewa, kuna uwezekano akaja na utetezi wa wewe kuchangia uzembe huo. Hivyo, kama utafanikiwa, nafuu utakayopewa itapungua kwa jinsi mahakama itakavyoona inafaa, kwa mujibu ya uchangiaji wako wa madhara uliyoyapata.

## Ninalazimika kutoa Ushahidi?

**Mume wangu ni mshukiwa wa uhalifu.**

**Wakati wa upekuzi nyumbani walikuta mifuko miwili ya bangi. Sasa nimepokea wito wa mahakama ukinihitaji nitokee mahakamani na kutoa ushahidi dhidi ya mume wangu. Sijisikii kwenda mahakamani. Nifanyeje?**

*20 Aprili 2009*

Kama ilivyo kwenye mashauri ya madai, kila mtu katika mashauri ya jinai ni shahidi timilifu, kama atakuwa na uelewa wa kutosha wa kutoa ushahidi na kuelewa maana ya kiapo. Shahidi timilifu wakati wote analazimika kutoa ushahidi. Wahusika kwenye kesi kwa kawaida hupima kesi zao na kuwasilisha mahakamani majina ya mshahidi kwa ajili ya kupata wito wa mahakama. Wito wa mahakama ukitolewa, walioitwa wanalazimika kuitikia wito. Ni wazi jina lako limewasilishwa na upande wa mashtaka kwa sababu wanadhani wewe una msaada mzuri katika kujenga kesi yao. Hata hivyo, kwa kuwa wewe ni mke wa mtuhumiwa unaweza kuchagua ama utoe au usitoe ushahidi dhidi ya mume wako. Utahitajika, hata hivyo, kwenda mahakamani kwa kuwa wito wa mahakama umeshatolewa na ieleze mahakama msimamo wako.

## Sifurahishwi na Hakimu

**Nina madai dhidi mdeni wangu kiasi cha Dola za Kimarekani 50,000, na nimempeleka mahakamani. Sifurahishwi na namna shauri linavyoendeshwa. Naona Hakimu akipendelea upande mmoja. Nimeshauriwa nifungue shauri hili Mahakama Kuu. Naomba ushauri tafadhali.**

*13 Aprili 2009*

Jaji au Hakimu ana jukumu la kutokuendesha shauri ambalo yeye binafsi ana maslahi nalo iwe kifedha, rangi yake, jinsia au tofauti za kisiasa. Kutokufanya hivyo ni sawa na kuendesha kesi yako mwenyewe, ambayo ni kinyume na msingi wa mafundisho ya haki ya asili kama vile hustahili kuwa jaji/mwamuzi wa kesi yako mwenyewe, kwa kilatini *nemo judex in causa sua*.

Kama unachosema ni sahihi, Hakimu anayehusika na kesi yako analazimika kujiondoa mwenyewe kwenye kesi. Utaratibu ni kwa wewe kumfahamisha Hakimu matakwa yako na ukiweza kuthibitisha tuhuma zako, Hakimu atajiondoa kwenye kuendesha kesi yako. Kwa hiyo unashauriwa kufanya maombi rasmi kwa njia ya maombi maalum yakiamabatana na hati ya kiapo ambapo utaeleza malalamiko yako dhidi ya Hakimu husika. Ni muhimu kwamba, haki haitakiwi tu kufanyika bali ionekane imefanyika. Tafadhali tambua kuwa huwezi peleka shauri Mahakama Kuu. Unatakiwa ufuate utaratibu ulioanishwa hapo juu.

## Kutembea na Kitambulisho

**Sheria inasemaje kuhusu kutembea na kitambulisho? Je, ni lazima? Miezi michache iliyopita, karibu na Las Vegas Casino, nilisimamishwa na polisi usiku na kughasiwa kwa sababu sikuwa nimetembea na kitambulisho. Tafadhali nishauri.**

*23 Machi 2009*

Kwa Tanzania, walau, hakuna sheria inayosimamia mambo yanayohusiana na vitambulisho. Mwaka 1986, kulikua na sheria iliyotungwa na bunge kwa ajili hiyo ila mpaka sasa haijaanza kufanya kazi. Hakuna mfumo rasmi ulioanzishwa kwa ajili ya utoaji wa vitambulisho Tanzania. Hii haimaanishi watu hawana vitambulisho. Watanzania wengi wanatembea na vitambulisho vya kazini au hata vya kupigia kura.

Kwa msisitizo, sio lazima kwa watanzania kutembea na vitambulisho vyao. Hata hivyo, inashauriwa kutembea na aina yoyote ya utambulisho kwa kuwa tumeona watu wasio na vitambulisho wakinyimwa dhamana na kukataliwa kupatiwa vifurushi vyao posta.

Katika nchi nyingine kama Afrika Kusini

au Kenya, ambapo wana mfumo rasmi wa vitambulisho vya utaifa, kutembea na vitambulisho ni lazima. Huko, polisi anaweza kusimamisha mtu yoyote, katika muda wowote na kumuamuru atoe kitambulisho chake. Hizi ni nchi zenye vitambulisho vya utaifa. Serikali inatumia vitambulisho hivyo kuwatambua walipa kodi na watu wanaweza kuzifikia huduma za kiafya na huduma nyingine za kijamii kwa kupitia vitambulisho vyao.

## Wito wa kutokea kama Shahidi

**Mtu aliniletea karatasi kutoka Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu nikitakiwa kutokea kwa Hakimu kama shahidi kwenye shauri. Sitaki kwenda. Nifanyeje?**

*30 Machi 2009*

Mashahidi ni muhimu sana kwa ajili ya kusimamia haki mahakamani. Kwenye mfumo wowote wa kimahakama, mashauri huamuliwa kwa kuangalia vielelezo vya kesi husika. Hata hivyo, mahakama hazijui ukweli wa kesi wanazofanyia maamuzi, isipokuwa kupitia mashahidi. Kwa kawaida, mashahidi huudhuria kesi kwa kupitia wito wa mahakama. Wito wa mahakama unaomtaka mtu aende na kutoa ushahidi ni amri halali ya mahakama husika na ina madhara kisheria kama amri itakaidiwa.

Ni kosa la jinai linaloadhibiwa kwa kifungo, kwa mtu kutokuheshimu wito wa mahakama, isipokuwa kama kuna sababu za msingi. Kwenye kesi yako haujaeleza sababu ya kutoenda mahakamani.

Tambua kuwa kwa lengo ya kusimamia haki, mahakama zimepewa nguvu ya kumlazimisha mtu yeyote mwenye uwezo wa kuwa shahidi kutokea mbele yake na kutoa ushahidi.

Unatakiwa utambue pia kuwa, wakati shahidi yupo mahakamani na akakataa kuapa au kujibu swali lolote, mtu huyo anaweza kupelekwa gerezani kwa muda wa miezi minane. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai. Kwenye kesi yako, tunakushauri utii matakwa ya wito wa mahakama. Hakuna njia nyingine. Ni amri halali. Unapaswa kutoa ushahidi ili kupelekea upatikanaji wa haki.

## Kukamatwa kwa kutokutaja Jina

**Nilisimamishwa na askari ambaye aliniuliza jina langu na ninapoishi. Nikakataa kumpa taarifa zangu kwa kuwa sikufahamu alikuwa anazihitaji kwa sababu gani. Nikakamatwa na kisha kupelekwa kituo cha polisi. Hii ni sawa kisheria?**

*23 Machi 2009*

Sheria yetu inasema afisa polisi akikuhisi umefanya au unaelekea kufanya kosa, na mtu aliehisiswa akakataa maombi ya askari kutaja jina lake au anapoishi, au kama akitaja jina na kusema anapoishi na askari akaamini ni vya uongo, mtu huyo atakamatwa na askari huyo ili majina yake au makazi yake vihakikiwe kwa ajili ya mahojiano ya awali.

Kwenye suala lako, kama kwa mtazamo wa askari ulifanya kosa, basi alikuwa na haki ya kukusimamisha na kukuuliza jina na makazi yako. Kutoka kwenye maelezo uliyoyatoa, kuna uwezekano kukamatwa kwako kulikuwa halali.

Pia utambue kuwa unayo haki ya kumuuliza askari yoyote anayekusimamisha, jina lake, cheo, na kituo cha kazi. Fahamu pia kuwa ni kosa linalostahili kufungwa kwa polisi kukataa kutaja jina, cheo au kituo chake cha kazi au kudanganya kuhusu taarifa zake.

## Kukataliwa kupewa Kibali/Hati ya Makazi Tanzania

**Mimi ni mwananchi wa Sudani na nimeomba hati ya makazi Tanzania. Idara ya Uhamiaji imekataa kuitoa. Nifanyeje?**

*30 Machi 2009*

Chini ya sheria yetu, mamlaka ya kutoa hati yoyote ya makazi ipo chini ya Mkurugenzi wa Huduma za Uhamiaji. Chini ya Sheria ya Uhamiaji, kila mtu anastahili, baada ya kufanya maombi na kukidhi vigezo fulani, kupatiwa hati ya makazi labda kama ni mhamiaji haramu. Mhamiaji haramu ni pamoja na watu wasioweza kujikimu, mtu anaejihusisha na biashara haramu ya madawa, mtu ambae kuna hati ya kuondolewa Tanzania imetolewa dhidi yake. Tanzania kuna hati za madaraja matatu za makazi. Nazo ni A, B na C.

Daraja A ni hati ambazo ni kwa ajili ya wanaokusudia kuingia na kubakia Tanzania na kujishughulisha na biashara yoyote. Daraja B ni hati ambazo zinatolewa kwa watu ambao wamepewa ajira ndani ya Tanzania kwa mujibu wa vigezo na ujuzi ambao haupatikani nchini au ni adimu. Daraja C hutolewa kwa watu ambao hawapati daraja A au B. Mkurugenzi wa huduma za uhamiaji ataweka wazi masharti ya kutimizwa ili mtu awezekupata hati ya daraja C.

Katika swali lako, haujatuambia chini ya daraja lipi unahitaji hati ya makazi wala sababu za kukataliwa maombi yako na Mkurugenzi wa Huduma za Uhamiaji. Lakini, uamuzi wa mkurugenzi wa huduma za uhamiaji kutokutoa hati yako ya makazi sio wa mwisho. Unaweza kukata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana kwenye mambo yanayohusiana na mambo ya uhamiaji ili kutathmini zaidi maombi yako.

## Askari kukamata kinyume cha Sheria

**Nilikuwa nyumbani usiku mmoja na familia yangu ambapo walikuja wanaume wawili wakidai wao ni maafisa wa polisi na kunitaka niende kituo cha polisi. Nikakataa, baadaye wakanilazimisha niende kituo cha polisi. Hii ni sawa kisheria?**

*9 Machi 2009*

Kiujumla polisi wamepewa mamlaka kisheria kukamata mtu yeyote ambaye wana sababu ya kuamini kuwa ametishia kusababisha uvunjifu wa amani mbele yao au hati ya kukamata imetolewa dhidi ya mtu huyo. Kwenye hili, suala lako haujatueleza kama askari waliokuja kukukamata walikuwa na hati ya kukukamata au amri yoyote inayowaamrisha kukukamata. Tuchukulie hawakuwa na chochote katika haya.

Hata hivyo, ni sheria kuwa, pale ambapo kosa linalodhaniwa kuwa ukamataji unatakiwa ufanyike ni kubwa kumfanya polisi kukamata bila hati na kwa kutumia nguvu za ziada, polisi mkamataji lazima amueleze mtu anayetakiwa kukamatwa sababu inayosababishwa akamatwe. Kwenye suala lako, maelezo ya kesi hii yanajieleza yenyewe, kuwa kilichofanywa na maafisa wa polisi sio utaratibu wa kisheria.

## Mahabusu kwa Siku Kumi na Nne

**Mtoto wangu wa kiume amewekwa mahabusu katika kituo cha polisi kwa takribani siku kumi na nne sasa. Maafisa wa polisi hawamruhusu kuwasiliana na ndugu zake wala mimi. Nifanyeje?**

*2 Machi 2009*

Kwenye Sheria za Makosa ya Jinai, mtuhumiwa anaonekana kuwa hana hatia mpaka itkapothibitika vinginevyo. Huu ndiyo ukweli bila kujali aina ya kosa mtu huyo anashtakiwa nalo. Ingawa kumshikilia mtu mahabusu ni muhimu katika mazingira fulani kwa ajili ya kurahisiha upelelezi wa polisi, sheria inaruhusu kila mtu aliye mahabusu kupata huduma za msingi. Hii inajumuisha haki ya kuwasiliana na mwanasheria, ndugu au rafiki anayemtaka na haki ya kupata dhamana ya polisi kama kosa linadhaminika.

Sheria inataka mtu asibakie chini ya mahabusu ya polisi kwa zaidi ya masaa arobaini na nane kabla ya kupelekwa mahamakani. Kwenye hili, mtoto wako alikuwa chini ya mahabusu ya polisi kwa siku kumi na

nne na hiyo ni kinyume na sheria. Alipaswa kupelekwa mahakamani au awe ameachiwa huru. Kutokuruhusiwa kuwasiliana na mtoto wako pia ni kinyume na sheria.

Tunakushauri kuweka mwanasheria au wasiliana na taasisi za kijamii kwa msaada wa kisheria.

## Miaka Miwili bila kusomwa Hukumu

**Tumekuwa tukisubiri hukumu kutolewa kwenye shauri la madai Mahakama Kuu kwa miaka miwili. Wakili wetu amekataa kufuatilia akidai kuwa inaweza kumuudhi jaji. Tafadhali shauri, tuchukue hatua gani?**

*9 Machi 2009*

Ni haki ya pande husika kwenda mahakamani pale ambapo mgogoro unapotokea na kushindwa kuhusuluhisha. Mahakama ndiyo sehemu ya mwisho kwa mtu anayehisi kuwa haki zake zimevunjwa. Mahakama ni mhifadhi na mwamuzi wa haki za watu. Pia sera ya sheria kuwa kesi ziishe mapema iwezekanavyo. Pale shauri inapokwisha, ni jukumu la jaji/hakimu kutoa hukumu ndani ya muda muafaka. Kushindwa kwa jaji/hakimu kutoa hukumu ndani ya muda muafaka sio haki.

Wakili wako hayuko sahihi anaposema Jaji atakasirika. Jaji anatoa haki, kwa hiyo hakuna hasira yoyote itakayosababishwa na kitendo cha wewe au wakili wako kufuatilia hukumu na wala hakuna hukumu itakayosomwa dhidi yako kwa kuwa ulikuwa unafatilia haki yako.

Hili ni shauri lako, hivyo unaweza kufatilia kwenye masjala ya Mahakama Kuu. Haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyonyimwa na kwa kitendo cha Mahakama Kuu kuchelewesha hukumu kwa zaidi ya miaka miwili ni kukunyima haki yako. Hata hivyo, uchelewaji huo sio wa kawaida, na kuna uwezekano mkubwa kuna kitu kwenye jalada ambacho wewe hukifahamu.

Tunashauri utafute mwanasheria mwingine au uandike barua kwa Msajili wa Mahakama kujua hukumu ya shauri lako imefikia katika hatua gani.

## Kesi imefutwa na Hakimu

**Ni sahihi kwa Hakimu kufuta kesi, mbele ya mlalamikaji, kwenye siku ya kusikilizwa, baada ya kutotokea siku za awali za kusikiliza kesi?**

*12 Januari 2009*

Kwa usimamizi sahihi wa haki, shauri likipangwa kwa ajili ya kusikilizwa, wahusika yaani, mlalamikaji na mlalamikiwa lazima wahakikishe shauri linaendelea katika siku iliyopangwa. Kwa mantiki hii hata Mwendesha Mashtaka ni mlalamikaji. Chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, (Sura 20, Marejeo ya Mwaka 2002) Hakimu amepewa mamlaka ya kufuta shauri na kumuachia huru mtuhumiwa kama upande wa mashtaka haujtokea kwenye siku ya kusikilizwa kwa kesi. Kwenye kesi yako, inaonekana mlalamikaji/ mwendesha mashtaka hakutokea katika siku za mwanzo za kusikilizwa na kesi ikafutwa katika tarehe iliyofuata, mbele yake.

Kama siku hiyo, Mwendesha Mashtaka hakuwa tayari kuita mashahidi na amekuja bila kujiandaa kuthibitisha madai yake dhidi ya mtuhumiwa, shauri linaweza kufutwa. Kufika tu mahakamani hakutoshi.

Kiujumla, hakimu ana mamlaka ya kufuta shauri kama mlalamikaji hatohudhuria au akihudhuria bila maandalizi ya kina na hasa kama uendeshaji wa shauri kwa upande mashtaka umekuwa wa kiubabaishaji au wa kizembe kupindukia.

## Rufaa ya Kesi ya Madai

**Nilikuwa na shauri la madai katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala na hukumu ikatoka dhidi yangu. Sijaridhishwa na maamuzi. Unanishauri nini?**

*19 Januari, 2009*

Awali ya yote, unapaswa mara moja kupeleka maombi kwenye mahakama iliyotoa hukumu kwa ajili ya kupata nakala ya hukumu na amri ya hukumu iliyothibitishwa. Baada ya kupata nakala hizo unatakiwa kuwasilisha sababu rufaa Mahakama Kuu ukiambatanisha na Agizo la Mahakama. Rufaa inatakiwa iwasilishwe Mahakama Kuu ndani ya siku thelathini tangu siku ya hukumu.

Umuhimu wa barua ya kuomba nakala za hukumu na kikazia hukumu mahakamani ni kwa ajili ya kuhesabu siku thelathini ambazo mtu ulipaswa kuwasilisha rufaa yako. Ina maana kuwa siku ambazo ulikuwa unasubiria hizo nakala za hukumu na kikazia hukumu kupatikana, hazitohusika wakati kuhesabu siku thelathini.

## Haki ya Dhamana

**Nani ana haki ya kupewa dhamana ya mahakama? Kwa nini baadhi ya watu wanapata dhamana na wengine hawapati?**

*19 Januari 2009*

Dhamana ya mahakama ni kuachiwa na mahakama, ikiwa na masharti au bila ya masharti, kwa mtu anaeshikiliwa mahabusu akisubiri shauri lake kusikilizwa. Ni mkataba kati ya mtuhumiwa na mahakama ya kuwa mtuhumiwa akihitajika atatokea mahakamani. Haki ya dhamana ni ya moja kwa moja isipokuwa kwa makosa yasiyodhaminika. Makosa yasiyodhaminika ni kuua, uhaini, wizi wa kutumia silaha, kunajisi na usafirishaji wa madawa haramu ya kulevya. Hata kwenye makosa yanayodhaminika, mahakama ina mamlaka ya kutoa au kutokutoa dhamana kwa mtuhumiwa kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo pale ikionekana kuwa mtuhumiwa alishawahi kupewa dhamana na akashindwa kutimiza masharti yake, au kutoroka na pengina kama mahakama itaona kuna umuhimu wa kumshikilia mtuhumiwa kwa ajili ya usalama wake binafsi.

Unapaswa kuelewa kuwa kwa makosa yanayodhaminika, mahakama inaweka masharti fulani, ambapo yakitekelezwa mtuhumiwa ataachiwa kwa dhamana. Mifano ya baadhi ya masharti ambayo mahakama inatoa ni wadhamini wawili watakao saini hati ya dhamana, kuweka hati ya mali isiyohamishika au kutoa fedha taslimu na kutoa hati ya kusafiria. Kama masharti haya hayajatimizwa, hata kama kosa linadhaminika, mtuhumiwa hatoachiwa kutoka mahabusu.

## Rufaa juu ya Kifungo

**Mdogo wangu alihukumiwa kifungo cha miaka mitatu na Mahakama ya Wilaya ya Kibaha. Hajaridhishwa na maamuzi hayo. Afanyaje?**

*12 Januari 2009*

Mtu ambaye hajaridhishwa na hukumu anayo haki ya kukata rufaa. Mdogo wako anapaswa kutoa notisi ya kukata rufaa ndani ya siku kumi tangu tarehe ya hukumu. Baadaye anaweza akakata rufaa Mahakama Kuu ndani ya siku arobaini na tano kutoka siku ambayo hukumu ilitolewa. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 361 (1)(a) na (b) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Sura ya 20 marejeo ya mwaka 2002).

Pia unapaswa kufahamu kuwa, unatakiwa upate nakala ya hukumu itakayo ambatanishwa kwenye hati ya rufaa. Inashauriwa awakilishwe na wakili Mahakamani.

## Mdaiwa hafiki mahakamani (Shauri la Madai)

**Nimefungua kesi ya madai dhidi ya mtu fulani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu. Mdaiwa hafiki mahakamani na hajapatiwa wito wa kuja mahakamani. Nimekuwa nikitokea mahakamani peke yangu, na kesi kila mara inakuja kwa ajili ya kutajwa. Nimedhulumiwa haki yangu. Tafadhali nishauri.**

*19 Januari 2009*

Kuna uwezekano kesi yako haiendelei kwa sababu upande wa pili haujapatiwa hati ya wito. Sheria iko wazi chini Amri ya V Kanuni ya 20 na ya 21 (Order V, Rules 20 and 21) ya Sheria na Kanuni za Mwenendo wa Madai (Sura 33 Marejeo ya Mwaka 2002) kwamba ukifungua kesi dhidi ya mtu ambaye hapatikani kwa urahisi kwa ajili ya kumpatia hati ya wito, unafanya maombi mahakamani kwa ajili ya kumpatia wito kwa njia mbadala. Hii inamaanisha kuwa wito utawekwa kwenye sehemu yake ya makazi au ya biashara au kutumwa kupitia kampuni maalum za kutuma na kupokea vifurushi kama mdaiwa yupo nje ya nchi. Baada ya hapo wito utazingatiwa kama umemfikia. Mahakama pia inakubali njia mbadala za kutoa wito kwa kuchapisha katika gazeti linalosomwa na watu wengi. Kama hatofika baada ya njia hizo mbadala, mahakama itaendelea kusikiliza kesi upande mmoja yaani bila kuwepo upande wa pili na unaweza kuthibitisha kesi na mahakama itafanya maamuzi itakavyoona inafaa.

## Kushtaki Gazeti la Udaku

**Mimi ni mtaalamu na nilihudhuria hafla katika moja ya hoteli Dar es Salaam. Wakati tupo sehemu ya kucheza mziki, nilikuwa nacheza na rafiki wa mke wangu, mbele ya mke wangu na ndipo nilipokuja kusoma moja ya magazeti ya udaku ya Kiswahili kuwa nina uhusiano wa kimapenzi na huyo rafiki wa mke wangu. Mke wangu alishtushwa ila bahati nzuri hakuamini kilichoandikwa. Gazeti hilo pia lilichapisha picha yetu wawili tukicheza na kukiwa na maelezo mabaya sana. Nifanyeje?**

*5 Januari 2009*

Unaweza kulishtaki gazeti kwa kukukashfu. Kashfa ni uchapishaji wa taarifa kuhusu mtu iliyolenga kumshushia hadhi yake mbele ya jamii ya watu wenye uelewa. Kashfa huwa katika njia ya maneno, picha, ishara au vitendo. Ili kufanikiwa kwenye kesi ya kukashifiwa, kigezo cha kwanza ni kama ililenga kupunguza imani ya watu wenye uelewa katika jamii juu yako. Kutokana na ulichosema, inawezekana ndivyo ilivyo kwenye kesi hii. Kigezo cha pili ni kama kashfa hizo zimeelekezwa kwako. Hili liko wazi kwa kuwa gazeti lilichapisha picha yako na pengine kutaja jina lako sehemu fulani. Mwisho, utapaswa kuthibitisha kuwa lilichapishwa na kuwafikia watu wengine. Hii ni dhahiri pia kwa kuwa gazeti linasambazwa nchi nzima. Una kesi nzuri dhidi ya gazeti hilo. Wakati tunazungumza kuhusu udhalilishwaji, baadhi ya utetezi uliopo kwa Gazeti ni ukweli na maoni ya sahihi – ya kwamba kauli ilikuwa ni maoni ya haki inapaswa kuwa ni ya ukweli na iwe imetolewa kwa nia njema kwenye jambo lenye tija kwa jamii. Kutokana na maelezo tuliyopata, una kesi nzuri.

# Jinai/Uhalifu

**Kwa sasa uhalifu mkubwa umekuwa ukifanyika kwa njia za kieletroniki na kimitandao. Ni ngumu kutambua, inasababisha matatizo ya kudumu na ngumu kwa mamlaka za kisheria kupambana nao. Hizi ni zama mpya za uhalifu usioweza kuonekana.**

Msingi wa kanuni za sheria ya Makosa ya Jinai ni kwamba jinai inajumuisha vitu viwili, kipengle cha utashi na kipengele cha kitendo. Ufahamu wa mtu kuwa matendo yake ni ya jinai ni sehemu ya utashi, na matendo yenyewe ndo sehemu ya kitendo. Jinai nyingi za sasa, pamoja na makosa ya jinai yaliyoibuliwa na mahakama, yametafsiriwa kwenye sheria ambazo hubeba neno au misemo ikionesha kuhitajika vipengele vya kiutashi na kimatendo. Vitendo vya jinai vinawagusa watu wote? Nini kinazingatiwa kama kosa la jinai? Kama ukimtusi mwajiriwa wako hiyo ni jinai? Au kama ukimpiga mtu kofi? Sura hii inafafanua ni vitendo gani vinazingatiwa kama jinai mbele ya sheria. Wizi, iwapo ni mkubwa au mdogo, iwapo ni kwa mumeo au mkeo, hata kama lengo lako ni kurudisha bado ni wizi na unaadhibiwa kisheria. Mtu anayetenda jinai ana hatia bila kujali kama hakuwa na ufahamu kuwa analofanya ni kosa na hakuwa na nia ya kufanya kosa la jinai. Kama kukosa uelewa wa kawaida wa kutambua yaliyo sahihi na yasiyo sahihi, lipi ni kosa la jinai na lipi sio, ndio kisingizio chako, basi sheria haitokua upande wako. Ni rahisi sana, kama ukitenda kosa la jinai basi utawajibishwa ambapo inaweza kuwa kulipa faini hadi kifungo. Na ndio, hata vyote viwili, faini na kifungo.

## Kupokelewa kwa Hukumu kwenye Kesi ya Jinai

**Mwanzoni mwa mwaka 2009, gari langu liliharibiwa vibaya kwenye ajali ya barabarani. Dereva aliyesababisha ajali alishtakiwa Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni. Mwanzo wa shauri, dereva alikana tuhuma zote dhidi yake. Baada ya mashahidi kutoa ushahidi, dereva alikubali na kukiri makosa. Baada ya kukiri makosa, alitiwa hatiani na kuamuriwa kulipa faini. Baada ya hapo, nilifungua kesi ya madai Mahakama ya Kisutu dhidi ya dereva kwa ajili fidia kwa gari langu lililoharibika. Kwa bahati mbaya, mashahidi wangu hawapatikani – mmoja amefariki mwaka uliopita na mwingine hapatikani kabisa na jitihada zote za kumpata zimeshindikana. Nimeomba mahakama kupokea na kuzingatia ushahidi wao walioutoa kwenye kesi ya makosa ya barabarani ila Hakimu aliyekuwa anaendesha kesi alikataa ombi langu. Nifanyeje? Naomba nisaidie, kwani nimepata hasara kubwa sana.**

*18 Aprili 2011*

Kukataa kwa Hakimu kuna mashiko. Hukumu kwenye kesi za jinai inahusika pale tu inapotamka mtu yeyote kuwa ana hatia kwa kosa aliloshtakiwa nalo kwa wakati huo. Ushahidi unaotolewa kwenye kesi za jinai hauwezi kutumika kwenye kesi za madai. Maswali yote kwenye kesi za madai, hata kama chanzo cha shauri hili lina uhusiano na makosa ya jinai, lazima liamuliwe peke yake. Kwa mujibu wa suala lako, Hakimu kwenye kesi ya madai ana wajibu wa kuamua madai ya fidia. Hajui lolote kuhusu ushahidi uliotolewa katika mahakama ya jinai, kwa sababu mambo ya kwenye kesi za jinai yanatofautiana na madai ya fidia kwenye kesi za madai. Vivyo hivyo, ushahidi wa kwenye shauri la jinai hauwezi kukubalika kwenye shauri la madai. Hii ndiyo sheria ya nchi kwa sasa. Maelezo uliyotoa hayatuelezi mashahidi wako wawili walishuhudia nini. Unapaswa kuendelea na kesi yako, kwa sababu kuthibitishwa kwa kesi hakutegemei idadi ya mashahidi, badala yake ni uzito wa ushahidi uliotolewa. Kwa ushauri zaidi unapaswa kuwasiliana na mwanasheria wako.

## Kupigana Hadharani

**Afisa polisi alikuta umati wa watu ukitazama mwanangu akipigana mtaani na kijana mwingine. Mwanangu aliweza kutoa wembe ambao ulitumiwa na kijana mwingine kumshambulia yeye. Vijana wote wawili wamekamatwa na polisi. Mwanangu anasema alishambuliwa kwanza na alikuwa anajihami. Tafadhali shauri.**

*11 Aprili 2011*

Kitendo kilichofanywa na mwanao na huyo kijana mwingine ni cha jinai kinatambulika kama kupigana mbele ya hadhara kinyume na sheria. Chini ya Kanuni ya Makosa ya Jinai, kosa hilo linaadhibiwa kwa kifungo cha miezi sita au faini ya isiyozidi Shilingi za Kitanzania 500.

Kwenye sheria, kujihami kumekuwa ni utetezi mzuri kuthibitisha nia ya kudhuru mwili au hata kifo kwa kuzingatia hakukuwa na nguvu ya ziada iliyotumika. Ili kushinda katika utetezi dhidi ya kesi ya kupigana hadharani, lazima uweze kuonesha haukuwa unapigana bali kujihami kwani mtu anayejihami hataki kupigana na hujitetea kuepuka kupigana. Kwa kuzingatia uliyoyasema, mtoto wako atapaswa kutoa ushahidi kuwa alishambuliwa na alikuwa anajihami na kwamba hakukua na mapigano na hivyo hakukutokea vurugu. Akishindwa kuthibitisha hayo, kosa hilo haliepukiki.

## Mauaji ya Jessica Lal

**Mimi ni mwanafunzi wa mwaka wa pili wa sheria katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.**

**Nimeangalia sinema na kusoma kuhusu Jessica Lal, mhudumu wa Kihindi aliyeuawa na mtoto wa mwanasiasa katika ukumbi wa starehe za usiku. Nimejifunza namna gani Mahakama Kuu ilivyoita mwenendo wa kesi wa mahakama iliyokuwa inaendesha kesi na kuisikiliza kesi ya mauaji. Je Mahakama Kuu ya Tanzania inaweza kufanya hivyo?**

*11 Aprili 2011*

Kesi uliyoitaja ni kesi ya kihistoria ya mauaji nchini India ambapo mtoto wa mwanansiasa maarufu alimuua kwa risasi mhudumu, Jessica Lal, mwaka 1999, kwenye tafrija ambapo kulikuwa na mwanga mdogo na sauti ya juu ya mziki. Mtuhumiwa aliachiwa huru na mahakama kwa sababu, pamoja na sababu nyingine upande wa mashtaka haukuweza kuthibitisha kesi pasi na chembe ya shaka ya kuwa mshitakiwa alikuwepo mahali ambapo mauaji yalitokea.

Baada ya kuachiwa, kesi ilishikiliwa na chombo maarufu cha habari ambacho kilianza kuchunguza mauaji hayo. Uchunguzi ulibaini kutokutendeka kwa haki na kupelekea kilio nchi nzima iliyopeleka Mahakama Kuu ya India, kwa maamuzi yake yenyewe (*sua motu*), kuitisha jalada kutoka mahakama iliyotoa hukumu.

Mahakama Kuu ikabatilisha maamuzi ya kuachiwa huru ya mahakama ya chini na kumkuta mtuhumiwa na hatia na kumhukumu kifungo cha maisha gerezani. Mtuhumiwa akakata rufaa katika Mahakama ya Juu ya India ambayo ni sawa na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ambapo Mahakama ya Juu nchini India ilikubaliana na maamuzi ya Mahakama Kuu ya India ya kumkuta na hatia na adhabu ya kifungo cha maisha iliyotolewa kwa mtoto wa mwanasiasa, kwa kusema kuwa upande wa mashtaka umethibitisha bila shaka uwepo wa mtuhumiwa katika eneo la tukio. Mahakama ya Juu iliongeza kuwa uwepo wa mtuhumiwa ulithibitishwa na ushahidi wa kuona kwa macho kwa mashahidi wa upande wa mashtaka. Mahakama ya Juu pia ilitanabaisha kuwa mwenendo wa mtuhumiwa baada ya mauaji unathibitisha uhalifu na iliwahukumu baadhi ya marafiki wa mtuhumiwa kwenda jela baada ya kuwakuta na hatia kwa kuharibu ushahidi na kuzuia kupatikana kwa haki.

Wakati mahakama ilikosoa chombo cha habari kile kwa namna kilivyoripoti, lakini ilisema kitendo hicho hakikuwa na athari kwa mtuhumiwa.

Tukirudi kwenye swali lako, kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Tanzania, Mahakama Kuu ya Tanzania ina haki sawa na Mahakama Kuu ya India. Mahakama Kuu siyo lazima iombwe na mtu-inaweza kuingilia kesi na kutoa maamuzi yenyewe.

Kesi ya Jessica Lal ni jambo linalothibitisha umuhimu wa vyombo vya habari katika upatikanaji wa haki na kumkumbusha kila mmoja kuwa hakuna aliye juu ya sheria. Lazima ifahamike kuwa hakuna ukomo wa muda kwenye mashauri ya jinai na kuachiwa huru na mahakama moja haimaanishi kuwa kesi haiwezi kufunguliwa tena kwenye mahakama nyingine, hata hivyo, itategemea uwepo wa taarifa mpya.

## Kunyanyasa Wanyama

**Ninamiliki mbwa kadhaa na ninawaweka katika kibanda cha mbao. Kama sehemu ya biashara yangu, huwa ninawachochea kwa njia isiyo ya asili ili wapandane na kuzaliana, kisha nawauza kwa watu au naajiri watoto waniuzie kwa watu mitaani. Siko vizuri sana kifedha na muda mwingine nakosa fedha ya kuwanunulia chakula. Siku moja watoto wanaoniuzia mbwa hao waliniletea wageni nyumbani kwangu ambao walitaka kuona namna ninavyowatunza mbwa wangu. Niliwaruhusu, baadaye nikaambiwa nilikuwa nimevunja matakwa ya viwango vya kufuga na kuuza wanyama**

**na kwa sababu hiyo nikakamatwa na sasa nashtakiwa kwa kosa la jinai. Sijapata kusikia jambo hili – hawa ni mbwa na sio binadamu. Upande wa mashtaka unapaswa kuwashtaki wahalifu sugu na sio wafuga mbwa. Hawana vitu vya msingi vya kufanya? Hakuna sheria inayowataka waendesha mashtaka kuweka vipaumbele nani wa kumpeleka mahakamani? Nifanyeje?**

*14 Februari 2011*

Kuna sheria inaitwa Sheria ya Haki za Wanyama ya mwaka 2008. Sheria hii ilianzisha taasisi inayohusika na udhibiti na kuzuia kutendewa vibaya au kuteswa kwa wanyama. Afisa wa taasisi hii, akijiridhisha kuwa kuna mtu anawatesa wanyama au kuwafuga kwenye mazingira yaliyo chini ya kiwango kilichoainishwa na Waziri mwenye dhamana, anaweza akamchunguza mtu huyo. Kama afisa huyo akigundua wanyama wanateswa au wanalazimishwa kuishi katika mazingira yasiyofaa, anaweza akamripoti mtu huyo kwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai naye atashitaki. Zaidi ya hapo, Sheria iko wazi kuwa hakuna mbwa wala paka atakae uzwa hadharani, isipokuwa katika maduka ya wanyama na sehemu zilizoidhinishwa. Pia fahamu kama unazalishaji wanyama kwa sababu za biashara, unapaswa kupata kibali cha biashara hiyo. Barua yako haielezi kama unamiliki kibali hicho. Kutokuwapa mbwa chakula mara kwa mara inachukuliwa kama unyanyasaji na hatuoni kwa nini usishitakiwe. Ingawa, lazima tueleze kuwa hii ni mara ya kwanza tunasikia shitaka la namna hii. Mwisho, hakuna sheria inayoelekeza waendesha mashtaka waweke vipaumbele nani wakumshtaki.

## Kugoma kwenda Kituo cha Polisi

**Nilikuwa natembea mtaani na nikagongana na mzee. Alikuwa ameshika begi kutokana na ule mgongano begi likaibiwa. Ndani ya muda mchache wa lile tukio nilizungukwa na polisi wawili wakiwa katika sare na wawili wakiwa na nguo za kawaida. Wakaanza kunihoji na kunitaka twende kituoni. Nikakataaa, nikapigwa kofi na mmoja wa hao polisi. Haki zangu ni zipi kwenye hali kama hii? Nilipaswa nifanyeje? Ilikuwa ni lazima kwangu kwenda polisi?**

*10 Januari 2011*

Inastaajabisha kwa polisi wanne kutokea ndani ya muda mfupi kama huo. Wananchi nchini kote siku zote huwa wanalalamika kuwa polisi huchelewa kufika kwenye maeneo uhalifu unapotokea. Katika kujibu swali hili, tuamini kuwa hao wanne walikuwa kweli ni polisi na sio matapeli, ambao ni wengi mjini.

Kwa kuanzia, hupaswi kupigwa kibao au kupigwa kwa namna yoyote na askari labda kama umejaribu kutoroka au kuwadhuru, kitu ambacho hakionekani kwenye hili suala lako. Hata ingekuwa hivyo, askari hapaswi kutumia nguvu iliyopitiliza kuliko inayodhaniwa. Kama ni mwanamke unapaswa kupekuliwa na askari wa jinsia ya kike. Ukiwa chini ya uangalizi wa polisi unapaswa kuwa kimya, una haki ya kuwa na wakili wako, na haki ya kuwajulisha marafiki au watu wa familia yako kuwa unashikiliwa na polisi, isipokua afisa wa polisi akiona ni muhimu kukuzuia wewe kuwajulisha kwenu kwa sababu itazuia taratibu za kiupelelezi. Una haki ya kuuliza kwa nini umekamatwa, ikijumuisha haki ya kujua jina la afisa aliekuweka chini ya ulinzi, namba ya beji yake, na ni kituo gani cha polisi wanakupeleka.

## Utambuzi wa Wezi

**Usiku tulishambuliwa na kundi la watu wanne, ambao waliingia ndani ya nyumba yetu wakiwa na bunduki. Tuliamuriwa tulale chini huku wakitafuta fedha kwenye nyumba na kiasi kikubwa cha fedha kiliibiwa. Nilitoa taarifa ya tukio hili kwa**

**afisa wa polisi ambaye mwanzoni alikataa kulisajili, akisema hajafurahishwa kwa kuwa tuliweka kiasi kikubwa cha fedha nyumbani. Baada ya masaa kadhaa ya majadiliano kwenye kituo cha polisi, tukio lilirekodiwa. Siku nne baadaye, mmoja wa watuhumiwa alikamatwa na nilimtambua akiwa kituo cha polisi. Suala lilienda mahakamani na cha kushangza aliachiwa huru kwa kigezo kwamba gwaride la utambuzi lilifanyika vibaya na kwamba kuna uwezekano akawa sio yeye. Hili kwa kweli limenishtua sana. Kwa nini mtu aachiwe huru baada ya kutambuliwa?**

*6 Desemba 2010*

Kwenye Sheria ya Jinai, mahakama hukabiliwa na kuamua hatima ya mshtakiwa ambayo hupelekea adhabu ya kifungo. Hivyo, mahakama lazima ziwe makini zaidi kuhakikisha kuwa mtu inayemtia hatiani ndiye mkosaji. Ni kanuni inayotambulika kisheria kuwa ushahidi wa utambuzi wa sura lazima ufanyiwe tathmini ya kina, kabla haujatumiwa kutoa hukumu, isipokuwa kama umethibitishwa na ushahidi mwingine tofauti, kitu ambacho hakionekani kuwepo kwenye hii kesi.

Zaidi ya hayo, kuna sheria na taratibu ambazo ni lazima zifuatwe ili utambuzi ufanyike kwa usahihi, kushindwa kufanya hivyo inamaanisha kuwa utambuzi hautafaa kwa ushahidi. Baadhi ya mambo ya msingi ya kuzingatia ni kuwa mtuhumiwa ana haki, na anatakiwa atambue haki zake, ya kuwa na rafiki, mmoja wa familia au mwanasheria na kwamba afisa anayehusika na upelelezi hasimamii zoezi la utambuzi. Zaidi ya hayo, mashahidi hawatakiwi kumuona mtuhumiwa kabla ya zoezi la utambuzi, mtuhumiwa anatakiwa awekwe na watu wengine wasiopungua wanane wenye kimo kinacholingana, umri na muonekano wa jumla, na kwamba mtuhumiwa anaweza kukaa sehemu yoyote anayoona inafaa na anaweza kubadilisha sehemu ya kukaa baada ya kila shahidi kuja kufanya utambuzi. Tahadhari lazima ichukuliwe kuwa mashahidi hawaruhusiwi kuwasiliana na wenzao baada ya kutoka kwenye mchakato wa utambuzi, na shahidi anatakiwa amguse yule anayemtambua (kuonesha kwa kidole tu haitoshi). Wakati wote, mtu anayesimamia gwaride la utambuzi lazima afanye kwa uadilifu mkubwa, vinginevyo umuhimu wa utambuzi kama ushahidi utashuka thamani kwa kiasi kikubwa.

Katika tukio hili, inaonekana polisi walishindwa kuhakikisha utambuzi wa haki unafanyika, hivyo kusababisha kesi kutofanikiwa, na mtuhumiwa kuachiwa huru. Suala limekuwa dhaifu zaidi kwa sababu umeeleza kwenye swali lako kwamba mliambiwa mlale chini wakati mnavamiwa. Kwa ujumla, wakati wa uvamizi ni ngumu sana kukumbuka nyuso za watu, mtu hupamabana na kujinasua kutoka kwenye hiyo hali akiwa hai kuliko kumtambua nani anafanya kosa la jinai.

Kuhusu afisa wa polisi aliyehoji kwa nini mnahifadhi fedha nyumbani, hatujui sheria yoyote inayozuia raia kuweka fedha kwenye nyumba zao. Inashauriwa ni vyema kuepuka kuweka kiasi kikubwa, lakini si kinyume cha sheria. Tumeshangazwa na tabia ya polisi. Jambo hili linatakiwa litaarifiwe kwa wakubwa wake kwa hatua muafaka.

## Kukamatwa Baa baada ya Usiku wa Manane

**Mara tu baada ya usiku wa manane Septemba mwaka jana, mimi na wapangaji wenzangu wawili tulikamatwa tukiwa baa iliyopo pembezoni mwa mtaa wetu Wilayani Mkuranga. Polisi walidai kuwa ni kosa kuwepo baa kwa wakati huo. Hawakutuachia hadi siku iliyofuata baada ya kuwekewa dhamana na ndugu zetu. Hata hivyo, polisi wametufungulia mashtaka**

**kwenye Mahakama ya Mwanzo. Afisa mmoja wa polisi, ambaye ni ndugu wa mtuhumiwa mwenzangu, ametushauri tukiri kosa, akidai kwamba kosa hilo huadhibiwa kwa faini ndogo tu. Hata hivyo, sikubaliani na ushauri wa afisa wa polisi, nadhani tunapaswa kukataa kosa, kwa kuwa tulikamatwa kwenye mazingira ya nyumbani ambapo tulikuwa tunakunywa bila kufanya fujo. Hivi huyu afisa hatupotoshi? Kwa miaka mingi, nimekuwa nakunywa hadi wakati huo bila tatizo lolote. Tafadhali tunaomba ushauri.**

*11 Oktoba 2010*

Sheria ya Vinywaji vya Kulevya inazuia mtu yeyote, awe mmiliki wa baa, mfanyakazi au mtu yeyote kubakia kwenye baa akinywa bia au kinywaji kingine baada ya saa tano usiku kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa au baada ya usiku wa manane kwa siku za Jumamosi, Jumapili na sikukuu za umma.

Maelezo ya kesi yanajumuisha vipengele vyote vya msingi vya kosa chini ya sheria na maelezo ya kwamba ulikuwa unakunywa zaidi ya muda huo kwa miaka kadhaa bila tatizo lolote sio utetezi mzuri. Kama unavyoweza kuona, watu wanaendelea kunywa au kuuza pombe zaidi ya masaa yaliyoelekezwa – hii ni kinyume na sheria. Watu hawatakiwi kujificha chini ya kivuli cha mamlaka zetu kushindwa kutekeleza majukumu yao kama sababu ya kuvunja sheria. Hata kama tungependa kwa kiasi gani kuwa upande wako, tunakubaliana na ushauri wa afisa wa polisi.

## Kushtakiwa kwa Shambulio

**Nimeshtakiwa kwa shambulio baada ya kumpiga mmoja wa marafiki zangu kwenye masaa ya baadaye sana ya usiku tukiwa baa kipindi cha mwisho wa juma la Pasaka mwaka jana. Kesi yangu haijaanza, lakini nimekuwa sitendewi haki tangu siku ya tukio, rafiki yangu mwingine alichanganya Redbull na pombe ambayo ilisababisha kufanya hiki kitendo. Inajulikana miongoni mwa marafiki zangu kuwa sinywi pombe. Nifanyeje?**

*13 Septemba 2010*

Tunaamini haujaribu kutupotosha; kwa upande mmoja hunywi, kwa upande mwingine ulikuwa baa hadi masaa ya baadaye sana usiku. Tukiwa tunawafahamu watu wachache sana ambao hawanywi ila wanaenda baa, tunawafahamu watu wachache ambao hawanyi na wako baa mpaka masaa ya usiku sana! Kwa hali yoyote, tutajibu swali lako tukiamni kuwa hunywi pombe.

Sheria iko wazi kabisa kwamba ulevi hauwezi kuwa sababu ya utetezi kwa kosa la lolote la jinai. Hata hivyo, sheria yetu inaeleza kuwa ulevi unaweza kuwa utetezi kwenye kosa lolote la jinai kama mtu aliyeshtakiwa, ataeleza kuwa alikuwa hajui nini alichokuwa anakifanya wakati wa kutenda kosa hilo, na hali ya ulevi ilisababishwa bila ridhaa yake kwa makusudi au kwa uzembe wa mtu mwingine, na mtu aliyeshtakiwa kwa sababu ya ulevi alikuwa hajitambui, kwa muda au vinginevyo wakati wa kutenda kosa hilo.

Kwenye kesi hii, una utetezi mzuri sana kwa kuwa kitendo cha uhalifu kilikuwa ni matokeo ya unywaji wa pombe. Kuna kesi ambazo zimezungumzia utetezi huo hatuoni sababu kwanini ushindwe kujitetea mwenyewe kwa mafanikio. Unahitaji kuanza kuandaa mashahidi ambao watakuja kutoa ushahidi kwa upande wako.

## Mapatano kwenye Masuala ya Jinai

**Mwanangu ameshtakiwa kwa kubaka binti ya jirani yangu. Wakati kesi ikiendelea kwenye Mahakama ya Wilaya familia ilikutana, ikajadili tatizo, na kuhitimisha kuwa suala hilo ni vizuri zaidi kutatuliwa nje ya mahakama ili kukuza maelewano na ujirani mwema. Jirani ni mtu niliyekua naye na ni rafiki yangu wa karibu. Wazee**

**walifanikiwa kumshawishi amuelekeze binti yake kuyaondoa mashtaka. Cha kushangaza, Hakimu anayesimamia kesi amekataa kukubaliana na ombi letu bila kutoa sababu yoyote. Je, hilo sio kosa kisheria? Kwanini mtoto wangu ashtakiwe wakati pande mbili husika wamekubali kusameheana?**

*6 Septemba 2010*

Sheria ya jinai hutafuta kudumisha amani na utulivu katika jamii na mamlaka zinazohusika kwa ajili ya kusimamia haki za jinai wana wajibu wa kuyamaliza masuala hayo kirafiki na kwa haraka. Hata hivyo, maridhiano ya makosa ya jinai hayahusu makosa yote. Inatumika tu kwa makosa madogomadogo kama vile shambulio la kawaida au makosa ya binafsi. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inaipa nguvu mahakama kusimamisha usikilizwaji wa shauri kwenye kesi inayostahili, kusubiria matokeo ya maridhiano nje ya mahakama.

Aina ya kosa mtoto anashtakiwa nalo sio kosa linaloweza kumalizwa kwa maridhiano kisheria. Ubakaji sio kosa binafsi, ni kosa kubwa ambalo mahakama haiwezi kuhamasisha maridhiano, maelezo ya kwamba ninyi ni majirani na mnafahamiana tangu utotoni hayana maana. Hiyo haimpi mtoto wako haki ya kumbaka mtoto wa rafiki yako. Jiweke kwenye nafasi ya jirani yako na liangalie hilo kwa mtazamo huo – ungekuwa wewe kama baba, ungemsamehe mtoto wa jirani yako kwa kumbaka binti yako? Hoja ya jirani yako ni ya hatari, haieleweki, ni ya kijinga na haina msingi.

Tunafurahi kusikia kwamba Hakimu hajaamua kwa hisia na kuruhusu hii aina ya maridhiano nje ya mahakama kwenye kosa kubwa kama la ubakaji. Hakuna mahali popote kwenye swali umekanusha kwa kile kilichofanywa na mtoto wako, itakuwa jambo la busara ukimshauri.

## Kutaifisha Dhamana ya Mdhamini

**Nilisimama kama mdhamini ili kuhakikisha kaka yangu anaachiwa kwa dhamana kwenye kesi ya jinai inayomkabili iliyopo Mahakama ya Wilaya. Wakati yupo nje kwa dhamana, mtuhumiwa alishindwa kutokea mahakamani. Nilitokea na kuitarifu mahakama kuwa asingeweza kuhudhuria kwa sababu ya ugonjwa. Hakimu anayesimamia kesi hakukubalina na maelezo yangu na badala yake akaniamrisha nilipe shilingi ya kitanzania 500,000/= ambayo niliahidi kama dhamana. Je, hii ilikuwa sahihi na haki? Kuna chochote ninachoweza kufanya ili kupata fedha yangu?**

*6 Septemba 2010*

Hatuna uhakika kama umetueleza taarifa nzima. Ingawa katika kujibu hili swali tutachukulia kuwa umeweka wazi taarifa zote za muhimu.

Kwa maoni yetu Hakimu anayesimamia kesi hakuwajibika vile inavyopaswa alifanya kwa namna isiyostahili dhidi yako. Kwa ujumla, mahakama ina nguvu ya kuwachukuliwa wadhamini hatua pindi mshtakiwa wanayemdhamini anapovunja masharti ya dhamana kama ilivyo hapa. Kama hakuna cha kulipa, mahakama inaweza kumpeleka mtu aliyesimama kama mdhamini, jela. Hata hivyo, kabla ya kutumia nguvu hizo, ambazo kwa kawaida ni za hiari, mahakama inatakiwa kwanza kujua iwapo sababu ziliotolewa kwa mshtakiwa kutotokea ni za kwelli au la. Katika hali kama yako, mahakama ilitakiwa kuahirisha kesi na kumtaka mtuhumiwa kuleta ushahidi kama kweli alikuwa mgonjwa. Amri hiyo ilitolewa mapema.

Amri kama hizi, zinaweza kukatiwa rufaa, na kama utatoa maelezo yako vizuri, rufaa yako lazima ifanikiwe na unaweza kurejesha fedha yako.

## Nguvu za Mahakama za Jinai kuamuru kulipa Fidia

**Mnamo januari 2009, mjomba wangu alishtakiwa kwa kukutwa na hatia ya kuiba ng'ombe. Ushahidi ambao ulimkuta na hatia ni kukutwa na ngozi ambayo mlalamikaji alisema ni ya ng'ombe wake. Baada ya kukutwa na hatia aliamuriwa kumfidia shilingi za Kitanzania 700,000/= mlalamikaji, hii ikiwa ni thamani ya ng'ombe aliyeibiwa na gharama alizotumia mlalamikaji. Je, ushahidi huu unatosha kukumkuta na hatia? Je, ilikuwa ni sahihi na haki kwa mahakama kutoa amri ya fidia dhidi ya mjomba wangu? Tafadhali tushauri juu ya nafasi ya kufanikiwa kama mjomba wangu atakata rufaa kupinga kukutwa kwake na hatia.**

*6 Septemba 2010*

Hatuwezi kukupa jibu kwa swali lako bila kupitia mwenendo wa mashtaka na kuelewa jinsi kesi ilivyoendeshwa. Kwa mfano, hatufahamu ushahidi upi ulitolewa na mlalamikaji katika kutambua ngozi ya ng'ombe wake, au iwapo ushahidi uliotolewa ulimuhusisha mjomba wako kama ndiye mwizi, au ni yule aliyepokea ng'ombe anayedhaniwa kuibiwa na ngozi au aliiba ngozi peke yake. Ni jambo la kushangaza pia kuona jinsi mlalamikaji alivyoweza kutambua ngozi – tunastaajabu ni kipi kilikuwa cha upekee zaidi kuhusu ngozi hiyo.

Kuhusu amri ya fidia, tambua kuwa mahakama za jinai zina nguvu za kuamrisha fidia kutegemea na aina ya kosa ambalo mshtakiwa ameshtakiwa nalo na mazingira ya kesi husika. Hata hivyo, kwenye kesi yako mahakama ilienda kinyume na mamlaka yake kwa kuamuru fidia. Katika tukio hili, mamlaka ya mahakama ya jinai yalikomea kubainisha ujinai wa mshtakiwa. Masuala kama vile thamani ya ng'ombe aliyeibiwa na gharama alizotumia mlalamikaji kumtafuta ng'ombe wake ni masuala ambayo yanahitaji kuthibitshwa kwenye kesi ya madai. Kwa jinsi ilivyo, angalau tuna uhakika rufaa ya mjomba wako itafanikiwa, ingawa alitakiwa akate rufaa ndani ya siku thelathini tokea tarehe ya hukumu. Iwapo hakukata rufaa, anatakiwa apeleleke maombi ya kukata rufaa nje ya muda na ataje sababu za kuchelewa. Mahakama inaweza kukubaliana na hizo sababu au la.

## Kesi ya Jinai wakati Shauri la Ardhi likiendelea

**Ninamiliki eneo la ardhi jijini Mwanza. Hivi karibuni jirani yangu ambaye mara nyingi alikuwa anatamani sehemu ya eneo la ardhi hiyo, alianza ujenzi kwenye eneo langu. Nikaamua kufungua kesi dhidi yake kwenye Mahakama Kuu ya Mwanza. Wakati shauri likiwa linaendela kwenye Mahakama Kuu, alilalamika polisi kwamba nimevamia eneo lake. Nikakamatwa na sasa kuna kesi ya jinai inaendelea katika Mahakama ya Wilaya dhidi yangu. Nina wasiwasi kuwa ninaweza kukutwa na hatia na iwapo hatia hiyo itaathiri kesi yangu iliyopo Mahakama Kuu. Tafadhali shauri.**

*16 Agosti 2010*

Kuna maamuzi mengi ya Mahakama Kuu ambayo yameshaamua kuwa hakuna mtu anayeweza kukutwa na hatia kwa kosa la uvamizi kama kuna shauri linaendelea kwenye mahakama yoyote kubaini juu ya nani ni mmiliki halali wa hiyo ardhi. Kwenye kesi yako, kuna nafasi kubwa kuwa kesi ya jinai dhidi yako haitoweza kuendelea ili kusubiria maamuzi ya shauri lililopo Mahakama Kuu.

## Nilichukuliwa kwa Mauaji

**Mimi na rafiki yangu tulikuwa tunakunywa wakati nilipomtania kuhusu kitu fulani ambacho huwa hakipendi. Alinipiga ngumi ya uso nami katika kujitetea nilimpiga. Akaishiwa fahamu, na tukamkimbiza**

**hospitali ambako alifariki siku iliyofuata. Nilichukuliwa na polisi na nimewekwa rumande kwa takribani miezi kumi na tano sasa. Marafiki zangu wengi walionitembelea nikiwa mahabusu wananishauri kuwa niko gerezani kimakosa, na kwamba ninatakiwa kushtakiwa kwa kosa la mauaji ya bila kukusudia, na sio kwa mauaji ya kukusudia. Nifanyeje? Natarajia kupelekwa Mahakama Kuu ya Dar es Salaam, kwa kuwa Mahakama ya Kisutu haina mamlaka ya kusikiliza suala hili. Tafadhali shauri.**

*16 Agosti 2010*

Mahakama ya Kisutu haiwezi kusikiliza mashauri ya namna hii, wala uwezo kutoa dhamana. Mahakama Kuu tu ndiyo yenye mamlaka ya kusikiliza kesi hii. Hati ya mashtaka huandaliwa na Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai, na itasomwa kwako ukiwa Mahakama Kuu.

Unatakiwa ufahamu kuwa bado hujashtakiwa, kwa kuwa Mahakama ya Kisutu inashughulika na maandalizi ambayo yatapelekea kuanza kwa shauri Mahakama Kuu, kama Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai ataamua hivyo. Pia tambua ni Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai pekee anayeweza kuamua iwapo ushtakiwe kwa kwa mauaji ya kukusudia au bila kukusudia.

Kutokana na maelezo, tukiamini kuwa hujatuficha chochote, tunakubaliana na rafiki zako kuwa unatakiwa ushtakiwe kwa kosa la kuua bila kukusudia na sio kuua kwa kukusudia. Na usiposhtakiwa kwa kosa la kuua bila kukusudia, hutokuwa na haki ya kupata dhamana.

## Kuuza Mapanga, Visu Mitaani

**Nimewaona mara nyingi watu wakimiliki, na wakati mwingine kuuza, mikuki, pinde, mishale, visu na mapanga kwenye mitaa ya Dar es Salaam. Je shughuli hizi ni halali?**

*9 Agosti 2010*

Barabara na mitaa ndani ya jiji ni maeneo ya umma. Tungependa kukutaarifu kuwa uuzwaji na umiliki wa bidhaa hizo ulizozitaja barabarani ni haramu na ni kinyume na sheria. Na sio tu kwa sababu wauzaji hawana leseni halali kuuza bidhaa hizo, ila pia kwa sababu bidhaa hizo ni silaha za hatari. Chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), uuzwaji wa bidhaa tajwa umeainishwa kama biashara hatarishi au ya mashambulizi. Pia ni kosa kumiliki bidhaa yoyote ya namna hii kwenye eneo la umma, labda kama bidhaa hizo zinahitajika kwa madhumuni yanayotambulika kisheria.

## Haki ya kukata Rufaa kwenye Kesi za Jinai

**Baada ya kutoa taarifa ya wizi nyumbani kwangu, kesi ya jinai ilifunguliwa dhidi ya mtoto wa jirani yangu, na kesi ilitajwa katika Mahakama ya Wilaya ambapo Mwendesha Mashtaka wa Serikali alisimamia hiyo kesi. Kwa bahati mbaya, mtuhumiwa (jirani) alishinda kesi. Nataka kukata rufaa Mahakama Kuu, lakini nimetaarifiwa kuwa kwa sababu ni kesi ya jinai, siwezi kukata rufaa. Ni Mwendesha Mashtaka wa Mahakama ya Wilaya pekee anayeweza kukata rufaa. Nimefuatilia kwenye ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Mahakama ya Wilaya, nikataarifiwa kuwa hana nia ya kukata rufaa. Je, ni kweli kwamba siwezi kukata rufaa Mahakama Kuu kwenye kesi kama hizo?**

*12 Julai 2010*

Kuna aina mbili za kesi kwenye sheria, jinai na madai. Kwenye kesi ya jinai kama yako, Mwendesha Mashtaka wa Mahakama ya Wilaya anawakilisha maslahi yako mahakamani, na wewe unabakia kama mlalamikaji. Pale hukumu inapotolewa dhidi ya upande wa mashtaka, Mwendesha Mashtaka ndiye mwenye mamlaka ya kuamua

iwapo atakata rufaa au la, kutegemea na uzito wa kesi iliyopo. Kwenye kesi yako, inaonekana kuwa hakuna ushahidi wa kutosha kumtia hatiani mtuhumiwa huyo, na Mwendesha Mashtaka ameamua kutokata rufaa.

## Kusubiria Kunyongwa kwa miaka Kumi na Nne

**Baada ya kukaa miaka saba mahabusu, kaka yangu alikutwa na hatia ya mauaji na amekuwa akisubiria kunyongwa kwa muda miaka kumi na nne. Nani anayeamua lini adhabu yake ya kunyongwa ifanyike? Utekelezaji wa adhabu hiyo hufanyika wapi? Anaweza kubadilishiwa adhabu yake ya kifo kwenda kwenye kifungo cha maisha?**

*16 Agosti 2010*

Orodha ya wanaosubiria kunyongwa hupelekwa kwa Rais kwa ajili ya idhini. Tumetaarifiwa kuwa ndani ya miaka kumi iliyopita, hakuna Rais aliyeidhinisha orodha ya watu wanaotakiwa kunyongwa, na hivyo hakuna utekelezaji wa adhabu hiyo umefanyika.

Utekelezaji hufanyika kwenye magereza kwa kunyongwa mpaka kufa, mbele ya afisa wa mahakama na daktari. Daktari huthibitisha kuwa kifo kilitokea kabla ya mazishi. Kuhusu kubadilishwa kwa hukumu, ni Rais tu mwenye uwezo huo.

## Utetezi wa kutokuwepo Sehemu ya tukio la Mauaji

**Nilimtembelea rafiki yangu aliye jirani na Mwanza na karibu na nyumba ya wageni niliyokuwa naishi, kuna mtu alikuwa amenyongwa hadi kufa. Chumba changu kilikuwa milango miwili tokea tukio lilipotokea. Nimechukuliwa na polisi kwa mauaji ingawa sikuwepo siku hiyo ya mauaji. Hata hivyo, polisi wanadai kuwa kuna mashahidi ambao wamenitaja. Nifanyeje?**

*22 Februari 2010*

Kutokuwepo eneo la tukio ni utetezi kwenye makosa ya jinai ukidai kuwa mtu hakuwepo kwenye eneo tukio wakati linafanyika na hivyo hawezi kuhusika na tukio hilo. Jukumu la kuthibitisha kutokuwepo kwako sio lako – ni upande wa mashtaka utakaokuwa na jukumu la kuthibitisha kuwa ulikuwepo. Hatia haiwezi kupatikana, kama ushahidi uliotolewa kuthibitisha kutokuwepo kwa mtuhumiwa kwenye eneo la tukio utaleta mashaka kuhusu hatia ya mtuhumiwa. Kwa maneno mengine, kama kutakuwepo na mashaka hata kidogo kuwa inawezekana ikawa sio wewe, utaachiwa huru.

Kwenye suala lako, ikiwa ni kweli hukuwepo kwenye eneo la tukio, una utetezi mzuri. Changamoto kubwa unayokabiliwa nayo kwa wakati huu ni muda utakaokuwa mahabusu wakati unashtakiwa na mauaji, ni kutopata dhamana. Kosa la mauaji nchini Tanzania, kama ilivyo katika nchi nyingine za Afrika na kwingineko, huvutia hukumu ya kifo. Lazima uhakikishe unaandaa utetezi mzuri.

## Kumiliki Bunduki kinyume cha Sheria

**Miaka kumi iliyopita, ili kukabiliana na ongezeko la ujambazi wa kutumia silaha Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kilimanjaro alitangaza hadharani kwamba wale wote wanaomiliki silaha kinyume na sheria wanatakiwa wazisalimishe kwa polisi na hakutakuwa na maswali au kesi ya jinai itakayofunguliwa dhidi ya watu hao. Kinyume na ahadi yake, wakati nasalimisha silaha yangu, Kamanda wa Polisi wa Mkoa aliamuru nikamatwe. Nilifunguliwa mashtaka, nikatiwa hatiani na kuhukumiwa. Wakati wa kesi nilijitetea kwa kutoa sababu kwamba umiliki wangu wa silaha ulikuwa halali kwa sababu nilizisalimisha silaha hizo baada ya tamko. Mahakama iliyokuwa inasikiliza kesi hiyo ilikataa utetezi wangu na ikandelea kunitia hatiani. Ilikuwa sahihi kisheria?**

*15 Februari 2010*

Ni Jambo lisilobishaniwa kuwa umiliki wako wa bunduki kabla, wakati na baada ya tamko uliendelea kuwa kinyume na sheria. Kwamba Serikali (kupitia polisi) wamekualika kujisalimisha, kwa faida yoyote, haibadilishi sheria au kutoa msamaha wa kisheria kwa umiliki wako.

Kwa kukufahamisha zaidi, si kila tendo la kuzingatia maelekezo ya Serikali litatoa msamaha wa kisheria. Maelekezo yenyewe pia yanaweza kuwa kinyume na sheria. Huwezi kukubaliana na hili lakini kwa kifupi kilichofanyika na mahakama kilikuwa sahihi kwenye mazingira hayo.

## Mume kumuibia Mke

**Nimekuwa kwenye ndoa kwa miaka mitatu na tumebarikiwa kupata mtoto. Namtunza mtoto na kuhakikisha kuwa nyumba iko vizuri. Mke wangu ana kipato kikubwa kuliko mimi pamoja na kazi nzuri kwenye benki moja maarufu nchini Tanzania. Hivi karibuni, nilikuwa na shida na hela na nikachukua hela kwenye mkoba wa mke wangu bila kumtaarifu. Mwanzoni alidhani kuwa ni msichana wa ndani ndiye aliyechukua na akaamua kuripoti suala hilo polisi. Msichana alihojiwa na alitoa kauli kwamba ananituhumu mimi kuchukua fedha hizo. Nilikamatwa na nimeshtakiwa kwa wizi. Mke wangu hakufurahishwa na kitendo nilichokifanya na aliwaacha polisi kufanya kazi yao. Ingawa niliwapa polisi cheti changu cha ndoa, cha ajabu wamekataa kuniachia niondoke. Nifanye nini?**

*18 Januari 2010*

Kwa mujibu Sheria yetu ya Kanuni za Adhabu, mume na mke ni watu wawili tofauti. Mume anaweza kuiba kwa mke wake na kinyume chake. Kwa kuwa ulichukua fedha kutoka kwa mkeo bila idhini yake basi umetenda kosa la jinai na utashtakiwa kwa wizi na kama kuna ushahidi wa kutosha kukutia hatiani, utafungwa.

Chini ya Sheria ya Ndoa, mume na mke pia huchukuliwa kama watu wawili tofauti na kila mmoja anaweza kumiliki mali yake wenyewe. Kwa bahati mbaya kwako, hata kama mke wako ana kipato kikubwa kuliko wewe, au ulikuwa unatunza watoto wakati yeye anafanya kazi, haimaanishi kwamba mali yake ni yako. Huu ndio msimamo wa kisheria.

## Kueneza UKIMWI kwa Makusudi

**Mimi ni mwanamume wa miaka 32 na nimekuwa katika mahusiano na mjane kwa takribani miaka kadhaa. Kabla ya kuwa wapenzi, nilisisitiza kuwa twende kupima VVU / UKIMWI. Kwa kuwa tulikuwa tunafanya kazi kwenye miji tofauti, kila mtu alienda peke yake. Vipimo vilionesha wote tuko salama. Hivi karibuni, nilienda kwa ajili ya kipimo cha VVU / UKIMWI kwa sababu nilitaka nimuoe. Cha kushangaza, matokeo yalionesha nimeathirika ingawa nimekuwa mwaminifu sana. Kingine nilichogundua zaidi ni kuwa mume wake alikufa kwa VVU na si kwa mshtuko wa moyo kama alivyodai. Alijua chanzo cha kifo kwani muda wote ambao mumewe alikuwa anaumwa, yeye ndiye alikuwa anamhudumia. Baada ya kupata taarifa hizi, nilimkabili mpenzi wangu ambaye alikiri kwamba yeye alighushi matokeo yake ya VVU. Tangu wakati huo tumetengana ila nimesikia kwa sasa ana mahusiano na mwanamume mwingine. Inaonekana kwa makusudi anaeneza ugonjwa huo. Je, hii ni sawa kisheria? Nifanye nini?**

*14 Desemba 2009*

Kwa mujibu wa kanuni zetu za adhabu, ni kosa la jinai kwa mtu kwa kujua au kwa uzembe kueneza ugonjwa wowote ambao ni wa kuambukiza na ni tishio kwa maisha ya binadamu mwingine. Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti VVU na UKIMWI inasema kuwa ni kosa kwa mtu yeyote, kwa makusudi, kueneza

VVU / UKIMWI kwa watu wengine na mtu yeyote ambaye anatenda kosa kama hilo atahukumiwa kifungo cha miaka si chini ya mitano lakini kisichozidi miaka kumi. Suala hili linaweza kuripotiwa polisi ili mtuhumiwa achukuliwe hatua stahiki.

## Uwindaji Tanzania

**Nimekuwa mwindaji Tanzania kwa takribani miaka saba. Kati ya mara saba nilizotembelea, nimewaona maafisa wa jeshi wakiwinda na silaha za kivita. Kwa kiasi kikubwa wanamimina risasi kwa wanyama na mara nyingine hukosa hata nafasi ya kuwabeba wanyama wote kwenye magari yao na kuwaacha wengi wakiwa wamekufa. Wanajeshi hao pia huwinda usiku wakiwa na taa zenye mwanga mkali. Je, sheria za uwindaji nchini zinaruhusu tabia kama hii? Sheria hizi zinawasamehe wanajeshi ambao mara nyingi huwazidi nguvu maafisa wanyama pori? Je, sheria inatoa ulinzi wowote kwa wanyama wenye mimba ili wasiwindwe?**

*21 Desemba 2009*

Shughuli za uwindaji zinasimamiwa na Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009 ambayo iko wazi katika yote yaliyoelezwa hapo juu. Sheria hairuhusu uwindaji wa kutumia silaha ya aina yoyote ya kivita yenye uwezo kupiga zaidi ya kibweta kimoja cha risasi unaotokana na msukumo mmoja wa kifyatulio cha bunduki au kujipakia yenyewe risasi zaidi ya mara moja bila ya kufyatuliwa na mpigaji/mtumiaji husika.

Sheria inasema kwamba mtu yeyote atakayekwenda kinyume na hili anatenda kosa na akikutwa na hatia atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua Shilingi Milioni moja na kisichozidi Shilingi milioni mbili au kifungo kwa muda usiopungua mwaka mmoja na usiozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili kwa pamoja. Hiyo hutumika pia katika uwindaji wa usiku ambao hukatazwa na ni kosa kisheria.

Sheria haimsamehi mtu yeyote wakiwemo maafisa wa vikosi vya jeshi .

Kwa wanyama wenye mimba, sheria iko wazi na ianaeleza kuwa mtu yeyote mwenye leseni, kibali, au ruhusa ya kimaandishi kuwinda mnyama wa aina yeyote, kuwinda mnyama mdogo wa aina hiyo au mnyama wa kike wa aina hiyo ambaye anaonekana **dhahiri** ana mimba au ameambatana na watoto wake, isipokuwa uwindaji wa watoto hao au wanawake hao umeruhusiwa rasmi na leseni, kibali au ruhusa ya kimaandishi, anatenda kosa na atawajibika atakapokutwa na hatia kulipa faini si chini ya mara mbili ya thamani ya mnyama huyo au kifungo cha muda usiopungua miaka mitatu au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Sheria inawalinda wanyama wenye mimba kwa maslahi ya kudumisha uwepo wa wanyama wengi. Neno "dhahiri" linaloonekana kabla ya neno mjamzito ni muhimu kulizingatia na lina tafsiri ya kipekee.

## Kuiba kutoka kwa Mwizi

**Miezi kumi na mbili iliyopita, nilikamatwa nikiiba ng'ombe kutoka kwa mchungaji wa ng'ombe Kaskazini mwa Tanzania. Tangu wakati huo nimeshtakiwa mahakamani na nategemea utetezi wa kwamba mtu niliyemwibia naye ni mwizi mzoefu. Nafasi yangu ya mafanikio ikoje?**

*2 Novemba 2009*

Maelezo yako yanaonekana kama hadithi za Robin Hood - shujaa wa kiingereza na mwizi aliyekuwa anaiba kutoka kwa matajiri na kuwapa maskini. Kuna methali nyingi ambazo zitaunga mkono madai yako. Moja ya methali maarufu inasema (tunanukuu) "sio kosa kuiba kutoka kwa mwizi". Kwa bahati mbaya sheria haimuungi mkono Robin Hood, methali au utetezi wako.

Wizi ni uchukuaji usio wa haki wa mali inayomilikiwa na mtu fulani kwa nia ya kuibakiza moja kwa moja. Unyang'anyi ni utwaaji wa haki ya mmiliki wa mali na inajumuisha kitendo chochote kinachoonesha kuwa mtu huyo anaifanya mali hiyo kama ya kwake.

Kosa la jinai huhusisha vipengele viwili: kitendo kikiambatana na nia ovu. Kitendo huhusisha ufanyaji kitu fulani kibaya. Nia ni hali ya akili. Mambo haya mawili ni lazima yawepo kwa wewe kupatikana na hatia.

Kwenye kesi yako, umekubali kwamba umeiba na ulifahamu nini ulikuwa unafanya, hivyo vyote viwili, kitendo na nia vinapatikana. Na kwa kuwa utetezi wako ni wa aina ya "Robin Hood" hauwezi kukubaliwa, kuna uwezekano wa kukutwa na hatia. Kosa la wizi adhabu yake ni kifungo na kuna uwezekano mkubwa kuwa utahukumiwa kifungo.

## Ukatili wa Mume umepelekea Kifo cha Mkewe

**Kaka yangu ameshtakiwa kwa mauaji kwa kusabisha kifo cha mke wake. Ni kweli alizoea kumtendea vibaya mke wake kwa kumfanyia ukatili wa kutisha. Siku ya tukio, marehemu alimfungia mumewe nje ya nyumba kwenye ghorofa la pili la jengo. Kaka yangu alitishia kumuua na akaanza kupiga dirisha la kioo ambalo hatimaye lilivunjika. Baada ya kusikia kuvunjika kwa kioo, marehemu aliogopa na aliamua kujirusha nje ya dirisha na kuvunja uti wake wa mgongo. Alipooza kwa miaka miwili na hivi karibuni alifariki kwa sababu ya ajali hiyo. Kaka yangu hivi sasa ameshtakiwa kwa mauaji na ameshindwa kupata dhamana. Je kaka yangu anaweza kushtakiwa kwa mauaji? Sio marehemu ndiye wa kulaumiwa kwa kifo chake mwenyewe?**

*5 Oktoba 2009*

Kimsingi kama mtu anatengeneza katika akili ya mwingine hisia za hatari ambazo husababisha mtu huyo kujaribu kukimbia, na kwa kufanywa hivyo mtu huyo akajijeruhi mwenyewe, mtu ambaye alitengeneza hali hiyo atawajibika kwa majeruhi hayo. Kanuni hii itatumika kwenye hii kesi.

Chini ya kanuni zetu za adhabu, mtu ataonekana kusababisha kifo cha mtu mwingine ingawa kitendo chake sio hasa au sababisho pekee la kifo, kama kwa uhalisia au kwa tishio la kikatili akasababisha mtu mwingine kufanya kitendo ambacho kimesababisha kifo cha mtu mwingine.

Hatujaelezwa kama kaka yako alibeba silaha yoyote, na kwa kiasi gani alikuwa karibu na dirisha wakati anajaribu kuvunja ili kwenda kule ambako marehemu alikuwepo.

Yote hayo yangetusaidia kuamua iwapo kwenye mazingira hayo, yalisababisha hofu ya kufanyiwa ukatili kwenye akili ya marehemu au la. Kuna uwezekano yalisababisha.

Maelezo ya kwamba alifariki miaka miwili baadaye ni muhimu sana kwenye mashtaka ya mauaji, kwani chini ya sheria zetu mtu hawezi kuonekana ameua mtu mwingine kama kifo cha mtu huyo hakijatokea ndani ya mwaka mmoja na siku moja. Hiyo pekee inamuondoa kaka yako kutoka kwenye kesi ya mauaji.

Kujibu swali lako, kwa mtazamo wa muda ulivyopita kati ya kuanguka na kifo, kaka yako hawezi kushtakiwa kwa mauaji. Hata hivyo, kulingana na tabia zake za awali anaweza kushtakiwa kwa kuua bila kukusudia. Swali lako la pili unaweza ukajijibu mwenyewe - kuwa na busara wakati unafikiri kuhusu hilo na sahau kwamba mtuhumiwa ni kaka yako. Hudhani kwamba kifo kilisababishwa na tishio la kikatili ambalo marehemu alitazamia? Maoni yetu ni kwamba, mtu yeyote mwenye busara jibu lake litakuwa ni ndiyo. Unaweza pia kufikiria matibabu kwa ajili ya kaka yako kuzuia tabia zake za vurugu.

## Tohara kwa Wanawake

**Shangazi yangu ambaye anaamini kwenye tamaduni za kale alimlazimisha dada yangu kuketetwa bila matibabu yoyote au ganzi. Dada yangu alipata matatizo ya mfadhaiko tangu wakati huo. Shangazi yangu ndiye anayetutunza kwa kuwa wazazi wetu wamefariki miaka kadhaa iliyopita kwa VVU/UKIMWI. Unanishauri nifanye nini?**

*7 Septemba 2009*

Haijalishi kama shangazi yako anaamini katika tamaduni za kale au ndiye anayewatunza au la. Amevunja sheria. Chini ya Sheria ya Makosa ya Kujamiiana, mtu yeyote ambaye, ana usimamizi, ameaminiwa au anamtunza mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18, anamtendea vibaya, anamkataa au anamtelekeza mtu huyo au kusababisha kufanyiwa tohara au kusaidia mtu huyo kudhalilishwa, kutendewa ukatili, kukataliwa au kutelekezwa kwa namna ambayo inaweza kusababisha mateso au madhara kwa afya, ikiwemo madhara kwenye, au kupoteza uwezo wa kuona au kusikia, au mguu au kiungo cha mwili au kuathirika kiakili, anatenda kosa kwa watoto. Na mtu yeyote anayetenda kosa la ukatili kwa watoto atahusika akipatikana na hatia atastahili kifungo kwa muda usiopungua miaka mitano lakini usiozidi miaka kumi na tano.

Unatakiwa kulitolea taarifa tukio hili polisi au taasisi yeyote inayosimamia haki za wanawake kwenye eneo lako. Tunatambua kuwa shangazi yako ni mtu pekee ambaye anawalea, kwa hiyo kumripoti inaweza kuwa ngumu, lakini sheria iko upande wako, iwapo utaamua kuchukua hatua.

## Kushtakiwa kwa Mauaji Mara Mbili

**Jaji hivi karibuni amewaachia huru watuhumiwa wote kwenye kesi ya Zombe na kuamuru polisi wawatafute watu waliohusika na mauaji. Kama watu wanaotafutwa wanakamatwa na kufunguliwa mashtaka, wale watu walioachiwa huru wanaweza kushtakiwa upya pamoja nao kwenye shtaka moja la mauaji?**

*31 Agosti 2009*

Kimsingi, hakuna utata chini ya sheria zetu juu ya swali ulilouliza. Watu walioachiwa walihukumiwa baada ya kutolewa ushahidi na mwisho wa siku wakaachiwa huru, ina maana kuwa kesi ya msingi iliamuliwa. Hawawezi tena kushtakiwa kwenye kosa lile lile. Mfumo wetu wa sheria unazuia watu kushtakiwa mara mbili kwa kosa lile lile. Sheria pia huenda mbali zaidi kwa kuzuia watu kuhukumiwa mara mbili kwa kosa lilelile.

Sheria yetu ya mwenendo wa makosa ya jinai inafanya hilo kama utetezi kamili, kwa kuzuia mashtaka yoyote ya jinai kwa kosa lilelile, dhidi ya mtu yeyote ambaye ameshtakiwa na kuachiwa na mahakama yenye mamlaka.

Mambo yangekuwa tofauti, ikiwa mtuhumiwa angeachiwa kabla ya kutoa ushahidi. Katika hali hiyo, hakuna kizuizi kwa mashtaka ya baadae juu ya kosa hilo lakini hili halipo kwenye kesi ya Zombe. Katika kesi hii suluhisho pekee Jamhuri ililonalo ni kukata rufaa Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Kinyume na hapo, suala kuhusiana na watuhumiwa walioachiwa huru limekwisha.

## Mbaroni akijiandaa Kuiba

**Mwanangu alionekana akifanya kitu cha kutiliwa mashaka kwenye eneo la makazi. Alikuwa na tochi, glavu na bisibisi mbili ambazo alizitupa alipowaona maafisa wa polisi. Hatimaye alikamatwa na kushtakiwa kwa kosa la kujaribu kuvunja nyumba usiku. Nifanye nini?**

*17 Agosti 2009*

Iwapo kutakuwa na nafasi ya mafanikio au la itategemea na ushahidi utakaotolewa na

upande wa mashtaka kuthibisha mashtaka dhidi ya mtoto wako. Tochi, glavu na bisibisi sio vifaa vilivyotengenezwa au kuandaliwa kwa matumizi ya kufanyia wizi au uvunjaji wa nyumba usiku ila mahakama wanayo haki ya kufanya makisio kutokana na tabia na mazingira ambayo mtuhumiwa alikutwa na vifaa hivyo kwa lengo la kubainisha dhamira.

Maelezo ya kesi yanaonesha kumuingiza hatiani mwanao – unahitaji kutafuta ushauri wa kisheria haraka iwezekanavyo. Hili ni kosa la jinai ambalo linaweza kumsababishia adhabu ya kifungo.

## Ujumbe Mfupi unaotishia Kuua

**Mtu nisiyemfahamu amenitumia ujumbe mfupi usiyo na jina kwenye simu yangu ya mkononi kwamba wataniua kama nisipowalipa kiasi cha pesa. Nifanyeje?**

*13 Julai 2009*

Kosa la kudai kwa vitisho wakati mwingine hujulikana kama kudai fedha kwa vitisho. Kwenye mamlaka nyingine ya kisheria hujulikana kama ulaghai. Inaweza ikawa tishio la kujeruhi mtu au kupata mali. Linaweza kuwa tishio la kusabisha madhara kwa mtu mwingine anayekusudiwa kujeruhiwa au kumshawishi mtu huyo ambaye vitisho vinaelekezwa kutoa hela au mali yenye thamani. Kitendo kinaweza kikaonekana kama kitisho kama kipo katika hali au kiwango ambacho kwa akili ya mtu wa kawaida yenye utulivu na ujasiri wa kawaida angeshawishika au kufanywa awe na wasiwasi hivyo kukubali madai hayo bila matakwa yake. Maana ya kitisho hutofautiana kutokana na mazingira ya kila kesi, ikiwa na maana kwamba kinachoweza kuwa kitisho kwa mtu wa kawaida hakiwezi kuwa kitisho kwa mtu yule kilipoelekezwa na kinyume chake.

Kabla ya mahakama kuamua kuwa kitendo hicho ni kitisho, itazingatia mazingira yote yakiwemo ufahamu wa mtuhumiwa kuhusu uwezo wa akili wa muathirika kujua iwapo muathirika alitishiwa na mtuhumiwa wakati madai yasiyokubalika yalipofanywa. Kudai fedha kwa lengo la kujipatia kipato huhusisha kudai hela kihalali ikiwa ni deni la mtu anayedai.

Kudai fedha au mali nyingine yoyote kwa kutishia ni kosa na adhabu yake ni kifungo kinachofikia miaka kumi na nne. Kwenye kesi yako, inaonekana hujui nani aliyekutumia ujumbe wa kukutishia. Tunakushauri ukatoe taarifa haraka kituo cha polisi kilichopo jirani. Kumbuka kwamba kama simu ya mkononi haijasajiliwa, itakuwa ngumu kwa polisi kujua mhalifu ni nani. Sio kawaida kwa mtu kupokea ujumbe kama huo. Kunaweza kuwa na taarifa za ziada ambazo hujatueleza, ambazo unaweza ukawambia polisi ili kuwawezesha kufanya upelelezi wa kina.

## Tabia ya Wizi

**Dada yangu ana tabia ya kuchukua vitu kwenye maduka makubwa na kuweka kwenye mfuko wake. Hawezi kabisa kuacha kufanya hivyo. Nimejaribu kumzuia bila mafanikio. Tunawezaje kumlinda?**

*6 Julai 2009*

Uchukuaji wa vitu wa namna hiyo ni sawa na kuiba. Hata hivyo, kuna uwezekano mkubwa dada yako ana hulka ya wizi, ni tabia inayotambulika kisheria. Huu ni ugonjwa wa akili ambao hupelekea kichocheo cha mvuto wa kuiba. Kichocheo cha mvuto ni haja isiyozuilika kufanya kitu na kwa kawaida sio utetezi kisheria labda kama umetokana na ugonjwa wa akili. Tunashauri kwamba dada yako akaonane na daktari na achunguzwe tabia hii isiyo ya kawaida.

## Shambulio la Aibu kwa Mwanamke

**Kaka yangu alikuwa anatembea kwenye barabara nyembamba na akamuona mwanamke mzuri anatembea mbele yake.**

**Alimfuata na kumpapasa kwenye kiuno chake na mapaja yake, na kumchombeza kwa maneno. Mwanamke mwenyewe kumbe ni binti wa waziri. Kaka yangu ameshtakiwa kwa kosa la shambulio la aibu. Unatushauri nini?**

*29 Juni 2009*

Hili ni tukio halisi la mtaani. Ngoja tuanze na mambo ambayo hayana msingi uliyoyataja. Haijalishi kama mwanakee anavutia au la. Pia haijalishi iwapo kama alikuwa ni binti wa waziri au la. Sheria inaangalia yeye kama mkazi au raia wa Tanzania na kumlinda ipasavyo.

Shambulio la aibu ni kosa la kufanya shambulio au kugusana kimwili na mtu ikihusisha vipengele vya kutoheshimu jinsia au madhara ya mwili bila idhini ya upande mwingine na kinyume na matakwa ya upande mwingine. Chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu (Sura ya 16 marejeo ya mwaka 2002), kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana Namba 4 ya mwaka 1998, kosa la shambulio la aibu adhabu yake ni kifungo kwa muda usiozidi miaka mitano au faini isiyozidi Shilingi za Kitanzania 300,000/= au adhabu zote mbili. Sheria inakataza wote wanaume na wanawake kufanya vitendo vya udhalilishaji, kama vile kutamka maneno au sauti au kufanya ishara kwa dhamira ya kusababisha usumbufu wa kijinsia kwa mtu mwingine. Maneno, sauti au ishara huwa za kukera kisheria, ikiwa mfanyaji amekusudia yasikilizwe au yaonekane na yule mtu mwingine. Shambulio linakuwa la aibu kama litaambatana na hali isiyo ya heshima kuelekea kwa mtu aliyeshambuliwa na sio utetezi kuwa hakukuwa na lengo la kuaibisha kwenye mawazo ya mfanyaji (mtuhumiwa).

Kwa upande wa kaka yako, pale tu mwanamke ameridhia au anamfahamu kwa namna ya ukaribu, kitu ambacho hakionekani kwa kesi hii, kumshika kwa namna ulivyoelezea, hata kwa "kumpapasa" (vyovyote imaanishavyo) ni sawa na shambulio la aibu. Maoni yetu ni kwamba kaka yako ana nafasi kubwa ya kupatikana na hatia. Unatakiwa, hata hivyo, kutafuta ushauri zaidi wa kisheria.

## Kuharibu Vizibiti

**Mimi ni mfanyabiashara katika shughuli za usafirishaji. Lori langu lilikamatwa kwa madai kuwa limebeba bidhaa zinazosadikika zimeibiwa na baadaye kutolewa mahakamani kama kizibiti. Mashtaka ya jinai yalifanyika na mshtakiwa alikutwa na hatia lakini polisi wamekataa kuliachia lori langu. Nifanyeje?**

*22 Juni 2009*

Kizibiti ni nyaraka au kitu chochote kilichotolewa kwa ajili ya ukaguzi/uchunguzi wa mahakama au kuonyeshwa kwa shahidi wakati wa kutoa ushahidi au kutumika wakati wa kumuandaa shahidi. Utolewaji wa kizibiti mahakamani utategemea mazingira ya kila kesi. Labda kama umetuficha taarifa fulani, maoni yetu ni kwamba kulikuwa hakuna sababu ya kulishikilia gari hilo. Hoja kuu mbele ya mahakama ni ile ya bidhaa zilizosadikiwa kuibiwa.

Vyovyote ingeweza kuwa, baada ya kesi kumalizika ulistahili kurudishiwa lori lako labda kama amri ya mahakama ya kulishikilia au madai kutoka kwa mtu mwingine kuwa lori hilo ni lake. Chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Sura ya 20 marejeo ya mwaka 2002), mahakama katika hatua yoyote ya mashtaka, ina mamlaka ya kuamuru kurudishwa kwa kizibiti kama itajiridhisha kuwa ni haki na sawa kufanya hivyo.

Kwenye kesi yako, kukosekana kwa amri yoyote ya mahakama ya kunyang'anywa, kuendelea kulishikilia lori lako ni kinyume na sheria. Unaweza kupeleka maombi mahakamani kuamuru kuachiliwa kwa gari.

## Ujumbe mbaya wa Maandishi

**Mimi ni mfanyabiashara mwanamke, kwa sasa ninaishi Shinyanga. Kabla ya hapo nilikuwa naishi jijini Dar es Salaam na ikatokea tukachangia mpenzi na mwanamke fulani ambaye pia anaishi Dar es Salaam. Kwa sasa nimekuwa napokea ujumbe wa maandishi wenye matusi kutoka kwake na nimetoa taarifa polisi kuhusu suala hili lakini hakuna hatua iliyochukuliwa. Nifanye nini?**

*1 Juni 2009*

Ni jambo la kushangaza kujua kwamba ulikuwa unachangia mpenzi na mwanamke mwingine. Hata hivyo swali lako ni kuhusu ujumbe wa maandishi wenye matusi ambao umekuwa ukipokea, pengine kutoka kwa mwanamke mwenye wivu hivyo hatutatoa maoni kuhusu kuchangia mpenzi.

Matumizi ya lugha ya matusi dhidi ya mwingine ni kosa la jinai dhidi ya uvunjifu wa amani katika jamii. Chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu kosa la namna hii huadhibwa kwa kifungo cha miezi sita. Sheria huangalia lugha za matusi za namna hii kwa mtazamo wa uvunjifu wa amani unaoweza kusababishwa. Kama lugha za matusi zitasababisha au zinaweza kusababisha uvunjifu wa amani, kwa mfano pande pande mbili au upande mwingine wa tatu wakiingia kwenye ugomvi, linakuwa ni kosa la jinai. Lengo la sheria kwa wakati wote ni kulinda amani na utulivu miongoni mwa jamii.

Kwenye suala lako, kwa bahati mbaya uko Shinyanga na hakuna uwezekano, kutokana na umbali kutokea kwa uvunjifu wa amani. Tunavyoona, hivi ndivyo polisi wanavyolichukulia hili tatizo. Hii ndiyo njia ya jumla ya kuliangalia swali lako. Kwa muongozo zaidi tunakushauri uonane na wakili wako huko Shinyanga.

## Ukatili kwa Wanyama

**Ninamiliki mbwa wa ulinzi kwa ajili ya usalama, kwa kuwa tunaishi shambani na hivi karibuni tumehamia Tanzania kutoka nje ya nchi. Mara zote mbwa huwa ndani ya eneo letu. Hata hivyo, jirani yangu amekuwa hampendi mbwa wetu. Miezi michache iliyopita, jirani aliruka juu ya uzio na kumpiga mbwa wangu, inawezekana na gongo na sasa mbwa huyo hawezi kutembea vizuri. Nifanye nini?**

*18 Mei 2009*

Kutokana na maelezo yako, inaonekana jirani yako ana chuki dhidi ya mbwa wako na pengine hata wewe. Kwa sheria ilivyo, kitendo cha jirani yako cha kumpiga na kumjeruhi mbwa wako hakikubaliki. Chini ya Sheria ya Kulinda Wanyama, kitendo cha jirani yako ni kosa la jinai na adhabu yake ni faini isiyodhidi Shilingi za Kitanzania 500,000/= au kifungo kwa muda usiozidi miezi 6 au adhabu zote mbili. Tunakushauri ukaripoti suala hili kwenye kituo cha polisi kwa hatua stahiki. Sheria nchini Tanzania, kama ilivyo nchi nyingine, hutoa ulinzi kwa wanyama dhidi ya ukatili. Jirani yako pia anawajibika kwa kosa la madai. Mbwa ni mali. Kwa kumpiga mbwa wako, jirani yako amefanya kosa la kuvamia kwenye mali yako. Unaweza kumshtaki kwa kudai hasara za jumla na mahsusi.

## Risasi zimefyatuliwa, Jirani ameuawa

**Miezi michache nyuma nyumba yetu iliporwa na majambazi wenye silaha. Katika kupambana na majambazi, baba yangu alifyatua risasi na jirani, aliyekuwa anakuja kutusaidia, aliuwawa. Baba yangu ameshtakiwa isivyo haki kwa mauaji. Tafadhali nishauri.**

*11 Mei 2009*

Tunasononeka pamoja nawe na baba yako - kutokana na maelezo, baba yako

hakudhamiria kumuua jirani yenu. Ilikuwa ni bahati mbaya. Kwenye Sheria ya Jinai, kusudio la mtuhumiwa ni muhimu sana katika kuamua hatia. Kwenye mauaji, kusudio humaanisha nia ya kuua mtu.

Kuna aina tatu za kusudio; maalum, jumla na lililohamishwa. Kwenye kusudio maalum, yule aliyedhamiriwa ndiye aliyeathiriwa. Kwenye kusudio la jumla, hakuna muathirika maalum aliyedhamiriwa. Na pale mtu amedhamiria kumuua Y na badala yake akamuua X, ndicho tunaita kusudio lililohamishwa. Maelezo ya kuwa baba yako alimuua jirani badala ya jambazi, hayaleti tofauti yoyote, kisheria ameua.

Baba yako anaweza kutumia utetezi wa kulinda mali. Hata hivyo analazimika kuthibitisha kuwa kitendo cha kufyatua risasi, hata kama angemuua jambazi kilikuwa sahihi. Kwa mazingira hayo, anaweza kushtakiwa kwa kosa dogo la kuua bila kukusudia. Adhabu ya kuua bila kukusudia ni kifungo cha maisha au chini ya hapo, na wakati mwingine kifungo cha nje chenye masharti, kutegemea na mazingira ya jinsi kosa lilivyofanyika. Ukweli ambao unabakia - ni kuwa kulikuwa na mtu aliyeuawa na sheria ni kali sana kuhusu hili. Baba yako hatoweza kupata dhamana kwenye kosa la mauaji na ni jukumu lako kuhakikisha kwamba upelelezi na mashtaka yanaharakishwa.

## Wajibu wa Mdhamini

**Binamu yangu alikamatwa kwa kosa la jinai na kupelekwa mahakamani. Nilimdhamini ili apate dhamana na tangu wakati huo nimekuwa nikihudhuria mahakamani. Sifurahishwi na tabia yake ndani na nje ya mahakama. Nifanyeje?**

*4 Mei 2009*

Mdhamini ni mtu ambaye hujifunga mwenyewe kukidhi wajibu wa mwingine. Kuhusiana na kesi za jinai, kabla ya mahakama haijatoa dhamana kwa mtuhumiwa, itahitaji mdhamini atayehakikisha mtuhumiwa anatokea tarehe na muda atakaohitajika. Hivyo mdhamini atahakikisha mtuhumiwa anatokea. Mahakama lazima ijiridhishe kwamba mdhamini ni wa kuaminika na mwenye tabia nzuri. Hakuna kifungu cha sheria kinachoeleza bayana vigezo ambavyo hutumika kutathmini kufaa kwa mdhamini. Sababu ambazo mara nyingi hutumika ni pamoja na uwezo wa kifedha wa mdhamini, historia yake na hata wakati mwingine uhusiano wa mtuhumiwa kwa mdhamini.

Lazima utambue kwamba kama mtuhumiwa asipotokea mahakamani kwa tarehe na muda uliopangwa, mahakama inaweza kukukamata wewe kama mdhamini. Umesema kwenye swali lako hufurahishwi na tabia ya mtuhumiwa. Hatuna uhakika ni nini usichokipenda, ila kama kuna chochote kile, na kama kitu hicho usichokipenda ni juu ya mashaka ya kuwa mtuhumiwa anaweza kukimbia au kujihusisha na kosa jingine la jinai, tunakushauri uende mahakamani na uombe kujitoa kwenye majukumu ya kuwa mdhamini. Hili ndilo suluhisho sahihi ulilonalo. Kama mazingira yataruhusu, unaweza ukamtaarifu mtuhumiwa juu ya nia yako ili aweze kuandaa mbadala wa mdhamini la sivyo atakamatwa tena.

## Kutoa Mimba ili kwenda Shule

**Binti yangu alifanikiwa kumaliza darasa la saba na amechaguliwa kujiunga shule ya sekondari iliyopo jijini Dar es Salaam. Hata hivyo, kabla ya kujiunga na shule niligundua alikuwa mjamzito. Alitoa mimba ili aweze kuendelea na masomo. Mimi na binti yangu tumeshtakiwa kwa kosa hilo. Utetezi tulionao ni upi?**

*27 Aprili 2009*

Chini ya Sheria yetu ya Kanuni za Adhabu utoaji mimba ni kosa linalostahili kifungo

kwa kipindi hadi miaka kumi na nne. Kwa kuwa wewe na binti yako mlifahamu kuwa ni mjamzito na mkatoa mimba ni kinyume na sheria. Kama upande wa mashtaka utaweza kuthibitisha kesi hii dhidi yenu, mnaweza kukutwa na hatia na kufungwa.

Kutokana na maelezo hapo juu, utetezi mnaoweza kuwa nao ni ule wa ulazima. Ulazima ni msukumo wa hali inayomlamizisha mtu kufanya kitendo kinyume na sheria. Kwenye kesi yenu, mnaweza kujaribu kuishawishi mahakama kuwa mlitoa mimba ili binti yako aweze kuendelea na masomo yake. Ukizingatia na msimamo wa sheria ulivyo sasa, hakuna uwezekano wa nyinyi kufanikiwa kwani ulazima wenu ni wa kibinafsi, ambao kisheria hauwezi halalisha kosa la jinai. Utetezi mwingine kama kutojua kama alikuwa mjamzito na utoaji mimba kwa sababu za kitabibu haziwahusu. Kunaweza kuwa na maelezo mengine ambayo ni muhimu kwenye kesi ambayo kuna uwezekano hujatuambia. Tunakushauri utafute mwanasheria na umueleze taarifa zote muhimu.

## Wanasheria wanaoendesha Kesi za Jinai

**Miezi michache iliyopita, niliibiwa na mwizi alipelekwa mahakamani. Nimekuwa nikifuatilia mwenendo wa mashtaka mahakamani na ninaona kuwa Mwendesha Mashtaka wa Serikali hafanyi jitihada za ziada katika kuiendesha kesi. Inaniuma kuona jinsi kesi inavyoendeshwa. Ni vigumu sana kwa jambazi huyo sugu kwenda jela. Kwa nini waendesha mashtaka binafsi hawaruhusiwi kuendesha kesi za watu wa namna hii? Naweza kuajiri mwanasheria kuisimamia hii kesi kwa niaba yangu?**

*6 Aprili 2009*

Hujatueleza ni kwa muda gani kesi yako ipo mahakamani na hatua iliyofikia, ili kutusaidia kutathmini iwapo Mwendesha Mashtaka anachangia kuichelewesha kesi. Hata hivyo, kuna sababu mbalimbali zinazoifanya kesi kuchukua muda mrefu kumalizika. Hizi ni pamoja uahirishaji kutokana na kutokamilka kwa upelelezi, kushindwa kwa mashahidi kuja mahakamani wanapoitwa kutoa ushahidi na sababu nyingine zilizo nje ya uwezo wa Mwendesha Mashtaka, kama kuumwa kwa Hakimu.

Kama unafikiri kuchelewa kwa kesi kunatokana na uzembe wa Mwendesha Mashtaka, tunakushauri ukalalamike kwenye ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai ili achukue hatua . Chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Sheria ya Usimamizi wa Mashtaka ya Taifa, Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai ana mamlaka juu ya uendeshaji wa kesi zote za jinai nchini. Anaweza kwa wakati wowote na hatua yoyote kuingilia au kuchukua uendeshaji wa kesi ya jinai na kumteua Mwendesha Mashtaka maalum (wakili wa Serikali) kusimamia uendeshaji wa kesi kwa manufaa ya umma.

Kama utashindwa kupata majibu sahihi kwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai unaweza kungalia jinsi ya kufungua mashtaka binafsi. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inaruhusu mtu binafsi, baada ya kuomba na kupata ruhusa ya mahakama kufungua mashtaka binafsi dhidi ya mtu aliyefanya kosa la jinai linaloadhibiwa chini ya sheria. Wizi ni kosa linaloadhibiwa chini ya sheria.

Taratibu za kufungua mashtaka binafsi ni kuwasilisha maombi mahakamani kwa njia ya maombi maalum yakiambatana na kiapo, ambayo utaeleza ikiwemo na mambo mengine kuwa umeiomba mamlaka ya uendeshaji mashtaka kumshtaki mtuhumiwa kwa kosa la jinai alilolifanya bila mafanikio.

Itakuwa ni busara ukimshirikisha mwanasheria binafsi akuelezee ni hatua gani kesi ilipo kwa sasa kabla ya kuanza kufanya maombi yoyote mahakamani.

## Rumande kwa Miaka Minne

**Kaka yangu ameshtakiwa kwa kosa la mauaji na yuko rumande kwa takribani miaka minne sasa. Kila wakati kesi inapokuja mbele ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Mwendesha Mashtaka anasema kuwa upelelezi bado haujakamilika. Kaka yangu hajafanya mauaji. Nifanye nini kuharakisha upelelezi?**

*30 Machi 2009*

Mauaji ni kosa kubwa ambalo adhabu yake ni moja tu, kifo, pale utakapokutwa na hatia. Inahusisha, kupoteza maisha ya mtu asiye na hatia. Ili kutenda haki kwa pande zote mbili, yaani mtuhumiwa na marehemu, upelelezi wa kina hufanyika. Hata hivyo, kwenye mazingira ya kawaida, kuchukua miaka minne bila kukamilisha upelelezi , pasipo shaka yoyote, ni muda mrefu sana.

Unatakiwa utambue kuwa Mahakama ya Hakimu Mkazi haina mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji. Kesi za mauaji husikilizwa na Mahakama Kuu tu. Hivyo basi, shauri la kesi la kaka yako halijaanza.

Mtu pekee anayeweza kuingilia uchelewaji wa upelelezi wa kesi ya kaka yako ni Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai. Kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ni Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai pekee mwenye nguvu ya kuingilia kati. Ana uwezo wa kuharakisha mchakato au kuliita na kulipitia faili lililopo polisi kwa ajili ya upelelezi na kama kwa maoni yake, hakuna ushahidi wowote kwenye faili unaojitosheleza kufungua kesi ya mauaji, anaweza kuamuru kutokuendelea kwa upelelezi na kumwachia huru kaka yako. Na kama, kwa maoni yake, faili lina ushahidi wa kutosha wa kushtaki, anaweza kuharakisha tarehe ya kusikiliza kesi.

Kwa hiyo, tunakushauri kuwasilisha malalamiko yako kwenye ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai kwenye ofisi ya kanda ya Mwanza au makao makuu jijini Dar es salaam na uelezee ucheleweshaji huo.

## Kofi la Uso

**Mimi ni mtu mwenye hasira sana na hivi karibuni nimewapiga makofi watu kadhaa ofisini kwangu baada ya kuniudhi. Niliwaomba msamaha. Hata hivyo hivi karibuni nilimpiga tena kofi mmoja wa wafanyakazi, ambaye anataka kuniripoti (polisi). Wakati nampiga kofi kiukweli sikuweza kujizuia. Kama nitashtakiwa ninao utetezi gani? Tafadhali shauri.**

*23 Februari 2009*

Kumpiga mtu kofi ni kosa, na kosa hilo huitwa shambulio la kawaida kwenye sheria zetu. Adhabu yake ni kifungo. Kwenye Sheria ya Jinai, makosa mengi yana utetezi kutegemeana na mazingira ambayo kosa husika lilitendeka.

Kwenye suala lako, hujatueleza kinagaubaga ni mazingira gani yaliyokupelekea umpige kofi mfanyakazi. Hasira pekee sio utetezi. Utetezi peke unaoweza kuwa nao ni kama kuchokozwa na kujitetea. Utetezi wa namna hii utategemea vitendo vilivyofanywa na mfanyakazi dhidi yako na kusababisha umpige kofi.

Uchokozi ni kitendo au maneno yanayosabisha mtu kupoteza uwezo wake wa kujizuia. Kwa ujumla, uchokozi sio utetezi unaotambulika kwenye sheria za jinai bali hupunguza ukubwa wa kosa kwa mfano; mauaji kwenda kwenye mauaji ya bila kukusudia.

Kutokana na maelezo uliyotupatia, inaonekana una hulka isiyozuilika ya kupiga makofi watu. Hulka isiyozuilika ni hali ya kushindwa kujizuia kufanya jambo fulani. Mara nyingi sio utetezi kisheria na hutoweza kutumia utetezi wa uwendawazimu labda kama tatizo lako lilitokana na ugonjwa wa akili. Tunakushauri utafute msaada wa kidaktari na uache kupiga watu makofi.

## Mauaji na Adhabu ya Kifo

**Je bado tuna hukumu ya kifo katika sheria zetu? Je, inaweza kukatiwa rufaa? Je adhabu hiyo ni ya haki?**

*9 Februari 2009*

Ndiyo, ni kweli kwamba bado tuna hukumu ya kifo chini ya Sheria zetu za adhabu. Chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu, (Sura ya 16 Marejeo ya Mwaka 2002), pale itakapothibitishwa kwamba mtu amesababisha kifo cha mtu mwingine, adhabu pekee iliyopo ni hukumu ya kifo kwa kunyongwa. Kusababisha kifo kunaweza, kisheria, kumaanisha, mtu anaweza kusababisha kifo kupitia uendeshaji mbaya au wakati wa kutimiza amri halali. Katika muktadha huu, hili sio sababisho la kifo.

Chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu, kwa mtu kuthibitisha kosa la mauaji, anatakiwa kuthibitisha pasipo shaka kwamba mtu anayesemekana kuuawa, amekufa kifo kisicho cha asili, kwamba kifo kilitokana na kitendo ambacho ni kinyume na sheria na kwa nia ovu. Kosa la mauaji husikilizwa na Mahakama Kuu tu au mahakama za chini zilizopewa mamlaka ya kusikiliza kesi hizo.

Hukumu ya kifo inaweza kukatiwa rufaa, mtu aliyekutwa na hatia na kuhukumiwa kifo anaweza kukata rufaa kwenye Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ndani ya siku sitini kuanzia siku ya hukumu. Utaratibu wa rufaa hutanguliwa na taarifa ya nia ya kukata rufaa, ambayo inatakiwa iwasilishwe siku kumi na nne kuanzia siku hukumu. Pale utakapochelewa kutoa taarifa ya nia ya kukata rufaa, mahakama inaweza kukuongezea muda kufanya hivyo. Hata hivyo, hakuna maombi ya kuongezewa muda wa kuwasilisha taarifa ya nia ya kukata rufaa au rufaa yatakayoruhusiwa baada ya Rais kusaini utekelezaji wa adhabu hiyo. Unatakiwa utambue kwamba baada ya Mahakama Kuu kutoa hukumu, utekelezwaji utafanyika pale tu Rais atakaposaini. Kuna wafungwa wengi wapo gerezani ambao wanasubiria kifo kwa kuwa Rais hajasaini ili utekelezaji ufanyike. Hata hivyo, kuna mazingira ambayo hata kama umekutwa na hatia ya kuua, mahakama haitoi adhabu ya kifo kwa kunyongwa. Mazingira hayo ni kama, wakati mfungwa anatenda kosa hilo alikuwa chini ya umri wa miaka 18 au pale mfungwa ni mwanamke ambaye wakati anakutwa na hatia alikuwa mjamzito. Kwenye mazingira hayo, mahakama mara nyingi hutoa adhabu ya kifungo cha maisha.

Swali lako la kama hukumu ya kifo ni ya haki au la, ni la kidhahania/kibinafsi. Watu wa familia ya marehemu kwa kawaida watasema ni haki - dhana ya jicho kwa jicho. Amnesty International inadhani hukumu ya kifo ni ya ukomo kabisa, inalenga kunyima haki za binadamu na inafanya kazi kukomesha adhabu ya kifo duniani kote. Kutokana na ripoti ya Amnesty International, tuna taarifa kwamba takribani nchi 137 duniani zimefuta adhabu ya kifo. Nchi kama China, Marekani na Tanzania hazijafanya hivyo.

# Kuhusu kitabu

Maswali & Majibu na FB Attorneys ni mkusanyiko wa majibu ya maswali ya kisheria kutoka kwa wananchi. Toleo hili la Kwanza linajumuisha maswali kutoka mwanzoni mwa mwaka 2009 hadi 2011. Maswali huchaguliwa kila wiki na kupitiwa kwa umakini. Kitabu kinajumuisha maswali ya kipekee kuanzia mambo ya mahusiano hadi misamaha ya kodi, masuala ya mikataba, migogoro ya ajira, masuala ya jinai na mengine mengi. Majibu yametayarishwa kwa umakini na waandishi kwa mtazamo wa kitaalamu na kisheria.

Safu ya Maswali & Majibu huchapishwa kila Jumatatu katika gazeti la Daily News, mojawapo ya magazeti maarufu ya Kiingereza nchini Tanzania.

ISBN 978-9976-5241-0-9

fbattorneys.co.tz



ISBN 978-9976-5241-0-9

FB ATTORNEYS